

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Nane

Al-Ahzab mpaka Al-Dukhân

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya <i>Suratu Al-Ahzaab</i>	1
Mtume ﷺ ana Khiyari, ya Kumkubali au Kumkataa Mwanamke.....	2
Malipo ya Wake Zake kwa Kuchagua Kubaki Pamoja na Mtume.....	5
Adabu za Kuingia Katika Nyumba za Mtume ﷺ na Amri ya Hijabu.....	8
Kukatazwa Kumuudhi Mtume ﷺ.....	12
Watu ambao Mwanamke Halazimiki kuwa na Hijabu.....	14
Amri ya Kumsalia Mtume ﷺ.....	16
Uwajibu wa Kumsalia Mtume ﷺ katika Sala Kabla ya Dua.....	20
Fadhila za Kumsalia Mtume ﷺ.....	20
Uwajibu wa Kumsalia Mtume ﷺ Kila Anapotajwa.....	23
Matukio ambamo Mtume ﷺ Husaliwa.....	25
Mwenye Kumuudhi Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ Amelaaniwa Duniani.....	30
Kemeo kwa Wazushi.....	31
Amri ya Hijabu.....	33
Angalizo na Onyo Kali kwa Wanafiki Waovu.....	34
Hapana Yeyote Aijuaye Siku ya Kiyama Isipokuwa Allah تعالى.....	37
Kulaaniwa Makafiri Kuka Kwao Motoni Milele na Kujuta Kwao.....	38
Uzushi wa Wayahudi dhidi ya Nabii Musa عليه السلام.....	40
Waumini Waamrisha Uchamungu na Ukweli.....	42
Namna Mwanaadamu Alivyochukua Amana.....	43
Matokeo ya Kuichukua Amana.....	46
Tafsiri ya <i>Suratu Saba'</i>	49
Shukrani na Elimu ya Ghaibu ni vya Allah تعالى Peke Yake.....	50
Saa Itakuja Ili Kila Mtu Alipwe Kulingana na Amali Zake.....	52
Ukanaji Akhera wa Makafiri na Kujibiwa kwao.....	57
Maelezo Juu ya Fadhila za Allah تعالى kwa Dawud عليه السلام.....	60
Fadhila za Allah تعالى juu ya Sulayman عليه السلام.....	62
Kufariki kwa Sulayman عليه السلام.....	65
Ukafiri wa Sheba (Sabai) na Kuadhibiwa Kwao.....	68
Bwawa la Ma'arib na Mafuriko.....	70
Biashara ya Sabaa na Kuangamizwa Kwao.....	74
Namna Dhana ya Ibilisi Inasadikishwa na Makafiri.....	78
Kushindwa kwa Miungu ya Washirikina.....	80

Allah تعالى Hana Mshiriki Katika Jambo Lolote.....	86
Muhammad ﷺ Ametumwa kwa Watu Wote.....	89
Makafiri Walivyouliza Kuhusu Lini Kiyama Kitatukia.....	91
Kuafikiana Makafiri Duniani juu ya Kuukataa Ukweli	93
Walioishi Maisha ya Anasa Walivyowakataa Mitume.....	98
Malaika Watawakataa Wenye Kuwaabudu Wao Katika Siku ya Kiyama.....	105
Kauli za Makafiri Juu ya Mtume ﷺ na Majibu yao.....	109
Kukanushwa kwa Madai Yao.....	111
Siombi Kwenu Malipo Yoyote kwa Kuufikisha Ujumbe.....	114
Tafsiri ya Suratul Fatir.....	121
Kutajwa Uwezo wa Allah تعالى	121
Hapana wa Kuzuia Rehema ya Allah تعالى	123
Ushahidi Mbalimbali wa Tawhid.....	125
Mtume Muhammad ﷺ Alipata Upinzani kama Mitume Waliopita.....	126
Adhabu kwa Kafiri na Zawadi ya Malipo kwa Muumini Siku ya Marejeo.....	129
Ushahidi wa Maisha baada ya Mauti.....	131
Utukufu Duniani na Akhera Unapatikana kwa Kumtii Allah تعالى	132
Amali Njema Hupanda kwa Allah تعالى	133
Allah تعالى Ndiye Muumbaji na Mjuzi wa Ghaibu.....	135
Miongoni mwa Neema na Ishara za Allah تعالى	139
Miungu ya Washirikina Haimiliki Hata ugozi wa tende (<i>Qitmir</i>).....	142
Watu ni mafukara kwa Allah تعالى na Kila Mtu Atabeba Mzigo Wake.....	144
Muumini na Kafiri Hawalingani.....	147
Kudura Timilifu ya Allah تعالى	151
Waislamu Ndio Watakaokuwa na Faida Akhera.....	154
Qur'an ni Kitabu cha Kweli cha Allah تعالى	155
Kama Makafiri wa Makka Wangelipigana Hudaybiyah	156
Fadhila za Maulamaa.....	157
Malipo ya Makafiri na Hali yao Itakavyokuwa Ndani ya Jahanamu.....	162
Maelezo Juu ya Kushindwa Miungu ya Washirikina.....	169
Makafiri Walitamani Mwonyaji Aje, Alipokuja, Walimkataa.....	172
Mwisho Mbaya wa Waliowapinga Mitume.....	175
Hekima ya kucheleweshwa Adhabu.....	175
Tafsiri ya Suratul Yasin.....	177
Fadhila za Surat Yasin.....	177

Mtume ﷺ Aliletwa kuwa Mwonyaji.....	179
Hali ya Wale Ambao Uovu umeshathibishwa juu yao.....	181
Kisa cha Watu wa Mjini na Mitume.....	189
Ole Wao Makafiri.....	204
Makafiri Wanakataa Kuwa Kuna Kufufuka.....	205
Hoja ya Kuwepo Muumba wa Mbingu na Kuwepo Uhai Baada ya Mauti.....	208
Miongoni mwa Alama za Uweza Mkubwa wa Allah تعالی.....	210
Miongoni mwa Dalili za Allah تعالی ni Kuwa Aliwabeba Katika Merikebu.....	217
Ubainifu wa Kupotoka Washirikina.....	220
Makafiri Wanapinga Uwepo wa Siku ya Ufufuo.....	222
Parapanda la Ufufuo.....	224
Ubainifu wa Maisha ya Watu wa Peponi.....	226
Kutenganishwa kwa Washirikina na Makemeo Watakayopata.....	229
Midomo ya Washirikina Itafungwa Siku ya Kiyama.....	232
Allah تعالی Hakumfundisha Mtume Wake ﷺ Mashairi.....	236
Kuna Alama za Utukufu wa Allah تعالی na Rahmah katika Wanyama.....	239
Miungu ya Washirikina Haina Msaada Wowote.....	241
Faraja ya Allah تعالی na Rahma Zake kwa Mtume ﷺ.....	242
Kukataa Kufufuliwa Baada ya Mauti na Kujibiwa kwao.....	243
Tafsiri ya <i>Suratu As-Saffat</i>.....	253
Malaika Wanashuhudia Tawhid ya Allah تعالی.....	254
Allah تعالی Ndiye Pekee Anayestahiki Kuabudiwa kwa Haki.....	256
Upambaji wa Mbingu na Kuzihifadhi Kwake Hutoka kwa Allah تعالی.....	257
Uhakika wa Uhai baada ya Umuti.....	260
Vitisho vya Siku ya Malipo.....	264
Mabishano ya Washirikina Siku ya Kiama.....	267
Adhabu ya Washirikina na Malipo ya Waumini Wakweli.....	272
Kukusanyika Watu wa Peponi, na Mazungumzo.....	278
Kisa cha Waisraeli Wawili.....	281
Mti Aina ya Zaqqum na Watu Wake.....	283
Utajo wa Nuhu عليه السلام na Watu Wake.....	290
Kisa cha Ibrahim عليه السلام na Watu Wake.....	293
Kuhama kwa Ibrahim عليه السلام Kupewa kwake Mtihani.....	301
Masimulizi Yenye Kueleza kuwa, Ismail عليه السلام ndiye Aliyetakiwa Achinjwe.....	306

Utajo wa Musa عليه السلام na Harun عليه السلام.....	309
Utajo wa Ilyasi عليه السلام.....	312
Utajo wa Kuangamizwa Watu wa Lut عليه السلام.....	315
Utajo wa Kisa cha Yunus عليه السلام.....	316
Kujibiwa Wenye Kumnasibishia Allah تعالى Watoto.....	323
Hakuna Anayeamini Maneno ya Washirikina.....	327
Hadhi ya Malaika na Kumtukuza Kwao Allah تعالى katika Safu.....	328
Quraysh Walitamani Wangukuwa na Utajo.....	330
Ahadi ya Ushindi na Amri ya Kujitenga na Washirikina.....	332
Tafsiri ya Surat Sad.....	337
Washirikina Walistaajabishwa na Ujumbe, Tauhidi na Qur'an.....	341
Kutajwa Sababu za Kushushwa Aya Hizi.....	343
Ukumbusho Juu ya Walioangamizwa katika Umma Zilizotangulia.....	350
Utajo wa Dawud عليه السلام.....	352
Kisa cha Mahasimu Wawili (Mbele ya Daudi عليه السلام).....	356
Sijida Iliyomo Katika Surat Swad.....	357
Daudi عليه السلام ni miongoni mwa Mitume Mtume ﷺ aliyoamrisha.....	358
Nasaha kwa Watawala na Viongozi.....	360
Hekima ya Kuumbwa Ulimwengu huu.....	362
Utajo wa Sulayman عليه السلام, Mtoto wa Dawud عليه السلام.....	364
Jinsi Allah تعالى Alivyomtahini Sulayman عليه السلام Kisha Akamfadhilisha.....	368
Utajo wa Ayyub عليه السلام.....	373
Utajo wa Mitume Wateule Bora Zaidi.....	378
Ubainisho wa Marejeo ya Waliobarikiwa.....	380
Ubainisho wa Mwisho wa Waovu.....	384
Kugombana Watu wa Motoni.....	385
Ujumbe wa Mtume Muhammad ﷺ ni Habari Kubwa.....	389
Kisa cha Adam عليه السلام na Ibilisi.....	392
Tafsiri ya Surat Az-Zumar.....	397
Fadhila za Surat Az-Zumar.....	397
Amri ya Tauhidi na Kukatazwa Ushirikina.....	399
Ushahidi Juu ya Nguvu na Uweza wa Allah تعالى na Kuwa Yeye Yuko Pekee.....	404
Allah تعالى Anachukia Ukafiri na Anaridhia Shukurani.....	409
Ukorofi wa Binadamu na Kumkumbuka Allah تعالى.....	410
Mchamungu Halingani na Muasi (Mtenda Dhambi).....	412

Amri ya Kumcha Allah تعالی, Kuhama na Kumuabudu Allah تعالی.....	414
Kuhofisha Adhabu ya Allah تعالی	416
Habari Njema kwa Watu Wema.....	419
Kitendawili cha Maisha ya Hapa Duniani.....	424
Watu wa Haki Hawalingani na Watu Waliopotea.....	425
Wasifu wa Qur'an.....	427
Mwisho wa Makafiri.....	431
Mfano wa Ushirikina.....	435
Mauti ya Mtume na Makureishi.....	437
Adhabu ya Makafiri na Waongo na Malipo Mema kwa Wachamungu.....	440
Allah تعالی Anawatosheleza Waja Wake.....	443
Wshirikina Wanaungana kuwa Allah تعالی Ndiye Muombaji.....	444
Allah تعالی Pekee Ndiye Ambaye Hufisha na Kuhuisha.....	449
Hakuna Maombezi Isipokuwa kwa Idhini ya Allah تعالی.....	451
Kuegemezwa Mambo ya Washirikina kwa Allah تعالی.....	453
Fidia Haitakubaliwa Siku ya Kiama.....	454
Mtu Anavyobadilika Anapopata Faraja baada ya Madhara.....	457
Wito wa Kutubu Kabla Haijafika Adhabu.....	460
Utajo wa Hadithi Zinakataza Kukata Tamaa.....	466
Mwisho wa Waliosema Uongo Dhidi ya Allah تعالی.....	472
Allah تعالی ni Muombaji na Mmiliki, na Kumshirikisha Hufuta Amali Njema.....	474
Washirikina Hawakumheshimu Allah تعالی Anavyostahiki.....	476
Kupulizwa Parapanda, Hukumu na Jaza.....	481
Makafiri Wataswagwa Kuelekea Jahanamu.....	486
Waumini Watapelekwa Peponi.....	489
Upana wa Milango ya Peponi.....	495
Tafsiri ya Suratu Ghafir.....	501
Fadhila za Surah Zenye Kuanza na <i>Ha Mim</i>	501
Sifa Mojawapo ya Makafiri ni Kupinga Aya za Allah تعالی.....	505
Wanaobeba Arshi Wanamsifu Allah تعالی na Wanawaombea Msamaha.....	507
Majuto ya Makafiri Baada ya Kuingia Jahanamu.....	512
Waumini Wanaamrisha Kumuabudu Allah تعالی Peke yake.....	516
Wahyi wa Allah تعالی kwa Kuwaonya Waja Wake.....	518
Onyo la Siku ya Kiama na Hukumu ya Allah تعالی katika Siku Hiyo.....	522
Mwisho Mbaya kwa Makafiri.....	527

Kisa cha Musa عليه السلام na Firauni	529
Musa عليه السلام Alisaidiwa na Muumini kutoka Katika Familia ya Firauni.....	533
Jinsi Firauni Alivyomfanyia Kejeli Mola Mlezi wa Musa عليه السلام.....	543
Mwendelezo wa Maneno ya Aliyemuamini Mussa عليه السلام.....	545
Hitimisho la Maneno ya Muumini, na Mwisho wa Makundi Yote.....	548
Kuthibitika Adhabu ya Kaburini.....	551
Mabishano ya Watu wa Jahanamu.....	555
Ushindi wa Mitume na Waumini.....	558
Ishara Kuwa Mtume na Waumini Watapata Ushindi.....	560
Uhai baada ya Mauti.....	562
Amri ya Kumuomba Allah تعالى kwa Rehema Zake na Wema.....	564
Dalili za Allah تعالى Juu ya Uwezo Wake na Tawhid Yake.....	568
Kuharamishwa Ushirikina, Kuamrisha Tawhid, na Ushahidi.....	572
Mwisho wa Matokeo ya Waliopinga na Kukataa Ishara za Allah تعالى.....	575
Amri ya kuwa na Subira na Habari Njema za Ushindi.....	579
Mifugo pia ni Neema kutoka kwa Allah تعالى na Ishara zake.....	581
Mazingatio kwa Hali za Waliotangulia.....	583
Tafsiri ya Suratu Fussilat.....	587
Sifa ya Qur'an, na Kauli za Wapingaji.....	588
Wito wa Tawhid.....	590
Baadhi ya Fafanuzi kuhusu Kuumbwa Ulimwengu huu.....	595
Onyo kwa Makafiri na Ukumbusho wa Kisa cha 'Ad na Thamud.....	603
Siku ya Kukusanywa Viungo vya Wakosaji.....	608
Marafiki wa Washirikina Wanawapambia Vitendo Viovu.....	613
Makafiri Walikatazana Kusikiliza Qur'an.....	614
Bishara kwa Waliomuamini Allah تعالى Peke Yake na Kuwa Imara.....	618
Fadhila za Kulingania kwa Allah تعالى.....	622
Katika Ishara za Allah تعالى.....	626
Adhabu ya Wakanushaji na Wasifu wa Qur'an.....	629
Washirikina na Athari ya Ulinganiaji Kwao	631
Kumfanya Mtume Musa عليه السلام kuwa Mfano Katika Kuwauliza.....	633
Kila Mmoja Atalipizwa Kisasi kwa Mujibu wa Amali Zake.....	635
Elimu ya Saa Iko kwa Allah تعالى.....	635
Mwanadamu Kubadilika Anapopata Raha Baada ya Shida.....	639
Qur'an na Dalili za Ukweli Wake.....	641

Tafsiri ya Surat Ash-Shura	645
Wahyi na Nguvu za Allah تعالى	646
Qur'an Iliteremshwa ili Kuonya	649
Allah تعالى ni Mlinzi, Mtawala na Muumbaji.....	655
Dini ya Mitume ni Moja.....	658
Onyo kwa Waliopinga Masuala ya Kidini.....	665
Riziki ya Allah تعالى na Ugawaji wake Duniani na Akhera.....	669
Kuwatungia Sheria Viumbe ni Katika Kumshirikisha Allah تعالى	671
Mfazaiko wa Washirikina katika Kiwanja cha Kukusanywa Watu.....	672
Habari njema za Neema za Peponi kwa Ajili ya Wenye Imani.....	675
Madai kuwa Mtume ﷺ Ameizua Qur'an - na Majibu ya Madai hayo.....	676
Allah تعالى Anakubali Toba na Anapokea Dua.....	678
Sababu ya Kutokuongezewa Kipato.....	681
Miongoni mwa Ishara za Allah تعالى ni Kuumbwa Mbingu na Ardhi.....	682
Mabalaa Huletwa na Dhambi.....	683
Meli pia ni Katika Ishara za Allah تعالى	686
Sifa za Wanaostahiki Yaliyoko kwa Allah تعالى	688
Fadhila ya Kusamehe na Ubora wa Kujinusuru.....	691
Hali ya Madhalimu katika Siku ya Kiama.....	696
Himizo la Kumtii Allah تعالى kabla ya Siku ya Kiama.....	698
Jinsi Wahyi Unavyoteremshwa.....	705
Tafsiri ya Surat Az-Zukhruf	709
Kuliwazwa Mtume ﷺ Juu ya Ukadhibishwaji wa Kikureishi.....	713
Kukiri kwa Washirikina Kwamba Allah تعالى Peke Yake Ndiye Muumba.....	716
Kukanushwa Washirikina Juu ya Kumjadili Allah تعالى	720
Ubainisho Kuwa Washirikina Hawana Hoja.....	726
Ibrahim عليه السلام Kutangaza Kujitenga na Shiriki na Watu Wake.....	730
Namna Watu wa Makka Walivyopinga.....	731
Mali Si Alama au Dalili ya Kuridhiwa.....	733
Shetani Ndiye Rafiki wa Mtu Anayempinga Allah تعالى	738
Lipizo la Allah تعالى kwa Maadui wa Mtume ni Lenye Kutokea.....	740
Kuhimizwa Kushikamana na Qur'an.....	741
Ishara ya Nabii Musa عليه السلام na Kuchekwa na Watu wa Firauni.....	744
Hotuba ya Firauni kwa Watu Wake	747
Dharau ya Makuraishi kwa Mwana wa Maryam.....	752

Kiyama Kitakuja Ghafla, na Kutatokea Uadui baina ya Marafiki.....	762
Bishara kwa Wachamungu Siku ya Kiyama, na Kuingia kwao Peponi.....	763
Mwisho Mbaya wa Waovu.....	766
Allah تعالى Hana Mtoto.....	770
Ubainifu wa Upekee wa Mola Mlezi.....	771
Masanamu Hayana Uwezo wa Nguvu ya Maombezi.....	772
Washirikina Wanakiri Upweke wa Allah تعالى katika Uumbaji.....	773
Malalamiko ya Mtume ﷺ kwa Allah تعالى	774
Tafsiri ya Suratu Ad-Dukhan.....	777
Fadhila za Suratu Ad-Dukhan.....	777
Qur'an Iliteremshwa katika Usiku Wenye Cheo.....	779
Kuwakhofisha Washirikina.....	782
Tafsiri ya "Batshah Kubwa".....	788
Kisa cha Nabii Musa عليه السلام na Firauni, na Kuokoka kwa Wana wa Israel.....	792
Majibu kwa Wanaopinga Kiyama.....	798
Dunia Imeumbwa kwa Hekima.....	802
Hali ya Washirikina na Adhabu yao Siku ya Kiyama.....	804
Hali ya Wachamungu na Neema Zao Peponi.....	806

Tafsiri ya Suratul Ahzaab

Sura ya 33

- Inaendelea -

* تَرْجِي مَنْ نَشَاءُ مِنْهُمْ وَتُؤَيِّ إِلَيْكَ مِنْ نَشَاءٍ ط وَمَنْ
 أَبْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ ءَ ذَلِكَ أَدَّتِي أَنْ
 تَقَرَّ أَعْيُنُهُنَّ وَلَا يَحْزَنَ وَيَرْضَيْنَ بِمَا ءَاتَيْتَهُنَّ كُلُّهُنَّ
 وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي قُلُوبِكُمْ ءَ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَلِيمًا ﴿٥١﴾
 لَا يَحِلُّ لَكَ الْبَسَاءُ مِنْ بَعْدِ وَلَا أَنْ تَبَدَّلَ مِنْ مِنْ أَزْوَاجٍ
 وَلَوْ أَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ إِلَّا مَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ ءَ وَكَانَ اللَّهُ
 عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ رَقِيبًا ﴿٥٢﴾ يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا
 تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَىٰ طَعَامٍ
 غَيْرَ نَظْرِينَ إِنَّهُ وَلَكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَادْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ
 فَانْتَشِرُوا وَلَا مُسْتَسْنَسِينَ لِحَدِيثٍ ءَ إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ يُؤْذَى
 النَّبِيَّ فَيَسْتَحْيِيءُ مِنْكُمْ ءَ وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيِيءُ مِنَ الْحَقِّ ءَ
 وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَءِ حِجَابٍ
 ذَٰلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ءَ وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ
 تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ وَلَا أَنْ تَنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ
 أَبَدًا ءَ إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٣﴾ إِنْ تَبَدُّوا
 شَيْئًا أَوْ خُفِّفُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٥٤﴾

* تَرْجِي مَنْ نَشَاءُ مِنْهُمْ وَتُؤَيِّ إِلَيْكَ
 مَنْ نَشَاءُ ط وَمَنْ أَبْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ
 فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ ءَ ذَلِكَ أَدَّتِي أَنْ
 تَقَرَّ أَعْيُنُهُنَّ وَلَا يَحْزَنَ وَيَرْضَيْنَ
 بِمَا ءَاتَيْتَهُنَّ كُلُّهُنَّ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا
 فِي قُلُوبِكُمْ ءَ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا
 حَلِيمًا ﴿٥١﴾

51. "Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao, na umsogeze umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliyemtenga, basi si vibaya kwako. Kufanya hivi kutapelekea yaburudike macho yao, wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unacho wapa wao wote. Na Mwenyezi Mungu Anajua yaliyomo nyoyoni mwenu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mpole."

Mtume ﷺ Ana Khiyari, ya Kumkubali au Kumkataa Mwanamke Anayejitolea Nafsi Yake Kwake

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa 'Aishah رضي الله عنها kwamba alikuwa anawaonea wivu wanawake ambao walijitolea nafsi zao kwa Mtume ﷺ. Aishah رضي الله عنها alisema: "Hivi mwanamke haoni aibu kujitoa nafsi yake pasi na mahari?" Allah تعالى Akateremsha,

تُرْجَىٰ مَن تَشَاءُ مِنْهُنَّ وَتُؤَيِّ إِلَيْكَ مَن تَشَاءُ^ط

"Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao, na umsogeze umtakaye."

'Aishah رضي الله عنها akasema: "Ninadhani, Mola Wako Anaharakisha Kuthibitisha matakwa yako."¹ Tulikwishaeleza kwamba Bukhari pia aliinukuu hadithi hii.² Hii imeonesha kwamba makusudio ya Kauli ya Allah تعالى:

تُرْجَىٰ

"Unaweza kuakhirisha zamu..."

Ni kuchelewesha, na,

مَن تَشَاءُ مِنْهُنَّ

"... kwa umtakaye katika wao..."

Yaani, wenye kujitoa zawadi nafsi zao,

وَتُؤَيِّ إِلَيْكَ مَن تَشَاءُ^ط

"...na umsogeze umtakaye."

Ukitaka mkubalie au mkatalie, na utakayemkataa utakuwa na khiyari baada ya hapo kwenda kumchukua. Kwa ajili hii, Amesema:

وَمَنْ أَبْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ^ع

"Na kama ukimtaka yule uliyemtenga, basi si vibaya kwako."

¹ Ahmad 6:158

² Fat'h Al-Bari 8:385

Wengine walisema: Makusudio ya Kauli ya Allah تعالى:

تُرْجَىٰ مَن تَشَاءُ مِنْهُنَّ

“Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao...”

Yaani, miongoni mwa wake zako, hakuna ubaya kwako kuacha kuwapangia zamu zao. Unaweza kumtanguliza umtakaye na kumuakhirishia umtakaye, na kumjamii umtakaye na kumuacha umtakaye. Haya yalisimuliwa kutoka kwa Ibn ‘Abbas, Mujahid, Hasan, Qatadah, Abu Razin, ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine.

Pamoja na haya, Mtume ﷺ alikuwa akiwapangia zamu. Kwa ajili hii, kundi la maulamaa wa kishafi na wengine wamesema kuwa upangaji zamu haukuwa wajibu kwa Mtume ﷺ wanatoa ushahidi wa Aya hii tukufu.

Al-Bukhari alinukuu kuwa ‘Aishah رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alikuwa akiomba idhini yetu (ili kubadili zamu) baada ya kushuka Aya hii:

تُرْجَىٰ مَن تَشَاءُ مِنْهُنَّ وَتُؤَيِّ إِلَيْكَ مَن تَشَاءُ^ط وَمَنْ أَيْتَعَيْتَ مِنْ عَزَلْتَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ^ع

“Unaweza kuakhirisha zamu kwa umtakaye katika wao, na umsogeze umtakaye. Na kama ukimtaka yule uliyemtenga, basi si vibaya kwako.”

Mimi (msimulizi) nilimuambia: “Umesemaje?” Akasema: “Nimesema, ‘Ningelikuwa mimi, nisingelimchagua yeyote juu yako, ewe Mtume wa Allah.’”¹ Hadithi hii ya ‘Aishah رضي الله عنها inajulisha juu ya kutokuwepo zamu. Hadithi yake ya kwanza inahukumu kwamba Aya iliteremshwa kuhusu wanawake waliojitolea nafsi zao kama zawadi, na kwa kuzingatia hilo, Bin Jarir رحمه الله تعالى ameridhia mtazamo huu, ya kuwa aya inajumuisha wanawake wenye kujitolea nafsi zao pamoja na wakeze alokuwa nao, akitaka humpangia zamu yeyote katika wao, na akitaka humpangii zamu.² Na rai hii aliyoichagua ni nzuri na ndio yenye nguvu na imewafikiana na Hadithi nyingi. Hivyo, Allah تعالى Akasema:

¹ Fat’h Al-Bari 8:385.

² At-Tabari 20:304.

ذَلِكَ أَذَىٰ أَنْ تَقْرَأَ عَيْنُهُنَّ وَلَا تَحْزَنَ ۗ وَيَرْضَيْنَ بِمَا آتَيْنَهُنَّ كُلُّهُنَّ

“Kufanya hivi kutapelekea yaburudike macho yao, wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unachowapa wao wote.”

Yaani, wakishajua kwamba Allah تعالى Amesema hakuna ubaya kwako kuondoa zamu. Ukitaka unaweza kuweka na usipotaka usifanye hivyo. Hakuna ubaya kwa chochote utakachokifanya katika hayo. Kisha, baada ya haya, una khiyari ya kuwapangia muda, hiyo si wajibu, watajisikia furaha na hayo na watapeana bishara na wataitambua fadhila yako kwao kwa kuwashirikisha, kuwafanyia usawa baina yao katika zamu, kuwatendea haki na uadilifu wako kwao.

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا فِي قُلُوبِكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Anajua yaliyomo nyoyoni mwenu...”

Yaani, dhidi ya kuwaendea baadhi yao kuliko wenzao, jambo ambalo haiyumkiniki kulikwepa. Ni sawa na alivyonukuu Imamu Ahmad kuwa 'Aishah رضي الله عنها amesema: “Mtume ﷺ alikuwa akigawa zamu za wake zake kwa uadilifu, kisha anasema,

«اللَّهُمَّ هَذَا فِغْلِي فِيمَا أَمْلِكُ، فَلَا تُلْمَنِي فِيمَا تَمْلِكُ وَلَا أَمْلِكُ»

“Ewe Allah! Hiki ni kitendo changu katika ninavyomiliki, basi usinilaumu katika Unayoyamiliki, wala mimi siyamiliki.”¹

Pia ilinukuliwa na wakusanyaji wa *Sunan* nne, na Abu Dawud akaongeza baada ya kauli yake,

«فَلَا تُلْمَنِي فِيمَا تَمْلِكُ وَلَا أَمْلِكُ»

“Basi usinilaumu katika Unayoyamiliki, wala mimi siyamiliki.”

Yaani, masuala ya moyoni.² Isnadi yake ni *Sahih*, na watu wote katika isnadi ni wa kuaminika. Baada ya maneno haya inafuata Kauli ya Allah تعالى:

¹ Ahmad 6:144.

² Abu Dawud 2:601, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:294, An-Nasai 7:63, Ibn Majah 1:633.

وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا

“...na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi...”

Yaani, siri za ndani kabisa, Kauli ya Allah تعالى:

حَلِيمًا

“...Mpole.”

Yaani, anasamehe na Kughufiri.

لَا تَحِلُّ لَكَ الْنِسَاءُ مِنْ بَعْدُ وَلَا أَنْ تَبَدَّلَ مِنْ مِمَّنْ أَرْوَجَ وَلَوْ أَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ إِلَّا مَا
مَلَكَتْ يَمِينُكَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ رَقِيبًا ﴿٥٢﴾

52. “Baada ya hawa hawakuhalikii wewe wanawake wengine, wala kuwabadilisha kwa wake wengine hata kama uzuri wao utakupendeza; isipokuwa yule uliyemiliki kwa mkono wako wa kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mchunguaji (Mtazamaji) wa kila kitu.”

Malipo ya Wake Zake kwa Kuchagua Kubaki Pamoja na Mtume ﷺ.

Maulamaa zaidi ya mmoja, kama vile Ibn ‘Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, Ibn Zayd, Ibn Jarir na wengine,¹ wametaja kwamba Aya hii iliteremshwa kama zawadi kwa wake wa Mtume ﷺ na Allah تعالى Kuwaridhia kwa uamuzi wao bora wa kumchagua Allah تعالى na Mtume Wake na Akhera, baada ya Mtume ﷺ kuwapa khiyari, kama ilivyotangulia kuelezwa katika Aya. Walipomchagua Mtume ﷺ, basi malipo yao kwa Allah تعالى ilikuwa ni kumuekea Mtume ﷺ ukomo abakie na wakeze hao tu, na Akamharamishia kuoa wengine au kuwabadilisha wengine wasiokuwa hao, hata kama atapendezwa na uzuri wao. Isipokuwa ‘inayowamiliki mikono yenu ya kuume,’ hakuna ubaya kwake. Kisha, Allah تعالى Aliviondoa vikwazo hivyo kwake, Akaifuta hukumu ya Aya hii, na Akamruhusu kuoa wanawake wengine zaidi,² lakini hakumuoa yeyote, ili fadhila za Mtume ﷺ kwao ziwe dhahiri.

¹ At-Tabari 20:297, 299.

² Ahmad 6:41.

Imamu Ahmad alinukuu kwamba 'Aishah رضي الله عنها alisema: "Mtume wa Allah hakufariki, hadi Allah تعالى Alipomruhusu (kuoa) wanawake wengine." Pia ilinukuliwa hilo na Tirmidhi na Nasai katika *Sunan* zao.¹

Wengine wamesema, maana ya Aya:

لَا تَحِلُّ لَكَ الْنِسَاءُ مِنْ بَعْدُ

"Baada ya hawa hawakuhalikii wewe wanawake wengine..."

Yaani, baada ya Sisi kukutajia baadhi ya sifa za wanawake halali katika wake zako ambao uliwapatia mahari zao na wale ambao mkono wako wa kuume uliwamiliki na mabinti wa ami, wa shangazi, wajomba, wa dada za mama, na wanaojitoa zawadi nafsi zao kwako. Wanawake wengine wasiokuwa hao si halali kwako. Hivi ndivyo ilivyosimuliwa na Ubayy bin Ka'b na Mujahid kutoka katika masimulizi yake na wengine.

Tirmidhi alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Mtume ﷺ alikatazwa kuwaoa wanawake wa namna fulani, isipokuwa waliokuwa miongoni mwa wanawake waliohama pamoja naye. Kwa kauli ya Allah تعالى:

لَا تَحِلُّ لَكَ الْنِسَاءُ مِنْ بَعْدُ وَلَا أَنْ تَبَدَّلَ بَيْنَ مِنْ أَزْوَاجٍ وَلَوْ أَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ إِلَّا مَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ⁴

"Baada ya hawa hawakuhalikii wewe wanawake wengine, wala kuwabadilisha kwa wake wengine hata kama uzuri wao utakupendeza; isipokuwa yule uliye mmiliki kwa mkono wako wa kulia."

Hivyo, Allah تعالى Aliwahalalisha wanawake Waumini, na wanawake waumini waliojitoa wenyewe kwa ajili ya Mtume ﷺ, na Aliharamisha kila aliyekuwa mfuasi wa dini isio Uislamu. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُ

"Na anayekataa kuamini bila shaka amali yake imepotea..." (5:153)

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:78, An-Nasai 6:56.

Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, alitoa rai kwamba Aya inaenea aina zote za wanawake waliotajwa, na kwa wanawake ambao aliokwishawaoa, ambao walikuwa tisa. Haya aliyoyasema ni mazuri, na huenda ndicho walichokimaanisha wengi katika *Salaf*, kwani wengi wao walizisimulia rai zote mbili kutoka kwake. Na wala hakuna kukinzana katika hilo. Allah Aalam.

Kauli ya Allah تَعَالَى:

وَلَا أَنْ تَبَدَّلَ بَيْنَ مِنْ أَزْوَاجٍ وَلَوْ أَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ

“...wala kuwabadilisha kwa wake wengine hata kama uzuri wao utakupendeza...”

Kwa hivyo, Alimkataza asiongeze zaidi yao iwapo atampa talaka mmoja wao na kutaka kumbadilisha mahali pake na mwingine, isipokuwa iliowamiliki mkono wake wa kuume.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَى طَعَامٍ غَيْرِ
نَظَرِينَ إِنَّهُ وَلَكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَادْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ فَانْتَشِرُوا وَلَا مُسْتَعْسَبِينَ لِخَدِيثِ إِنْ
ذَلِكَ كَانَ يُؤْذَى النَّبِيَّ فَيَسْتَحْيَ مِنْكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيَ مِنَ الْحَقِّ ۗ وَإِذَا
سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ۗ ذَلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ۗ وَمَا
كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ وَلَا أَنْ تَنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبْدَانًا ۗ إِنَّ
ذَلِكَ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٣﴾ إِنْ تَبَدُّوا شَيْئًا أَوْ خَفَوْهُ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ

شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٥٤﴾

53. “Enyi mlio amini! Msiingie nyumba za Nabii ila mpewe ruhusa kwenda kula, sio kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa basi ingieni, na mkisha kula tawanyikeni, wala msiweke mazungumzo. Hakika hayo yanamuudhi Nabii naye anakustahini, lakini Mwenyezi Mungu Hastahi kwa jambo la haki. Na mnapowauliza (wakeze) haja waulizeni nyuma ya mapazia. Hivyo ndio usafi zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao. Wala haitakiwi kumuudhi Mtume wa Mwenyezi

Mungu, wala kuwaoa wake zake baada yake kabisa. Hakika jambo hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

54. "Mkidhihirisha chochote kile, au mkikificha, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua kila kitu."

Adabu za Kuingia katika Nyumba za Mtume ﷺ na Amri ya Hijabu

Hii ni Aya ya Hijabu ambayo ndani yake kuna hukumu na taratibu za kisharia. Hii ni miongoni mwa Aya zilizoafikiana na rai ya 'Umar bin Khattwab رضي الله عنه ni kama ilivyothibiti ndani ya *Sahih* Mbili kwamba alisema: "Rai yangu iliwafikiana na ya Allah تعالى katika mambo matatu." Nilisema: 'Ewe Mtume wa Allah! ungelipafanya *Maqam Ibrahim* kuwa mahali pa kusali.'

Kisha Allah تعالى Aliteremsha,

وَأَتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلِّينَ

"Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia."
(2:125)

Pia nilisema: 'Ewe Mtume wa Allah! Wema na waovu huingia nyumbani kwa wake zako, hivyo, ungewawekea kizuizi.'

Allah تعالى Akateremsha Aya ya Hijabu. Tena baada ya wakeze Mtume ﷺ kula njama kuhusiana na wivu, niliwaambia

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّمَّنْ كُنَّ

"Asaa Mola Wake Mlezi, akikupeni talaka, akampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi..." (66:5)

Ikateremshwa.¹ Katika masimulizi aliyonukuu Muslim, mateka wa Badr wametajwa, na hili ni jambo la nne (kuhusu rai ya 'Umar رضي الله عنه kulingana na Mola Wake Mlezi).²

¹ Fat'h Al-Bari 1:601, Muslim 4:1865.

² Muslim 4:1765.

Bukhari alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه, kuwa alisema: ‘Umar bin Khattwab رضي الله عنه alisema, “Ewe Mtume wa Allah! Mwema na mwovu huingia kwako, ungeliswaamuru Mama wa Waislamu watumie hijabu. Allah تعالى Akateremsha Aya kuhusu Hijabu.”¹

Bukhari alimnukuu tena Anas bin Malik رضي الله عنه akisema: “Pindi Mtume ﷺ alipomuoa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها, aliwaalika watu, wakala chakula, kisha wakakaa kwa mazungumzo. Alipotaka kusimama, wao hawakusimama. Alipoona hivyo, alisimama. Baada ya kusimama, baadhi ya watu walisimama, wakasalia watu watatu wamekaa. Mtume ﷺ akaja ili aingie, lakini watu hao walikuwa bado wamekaa. Kisha wakasimama wakaondoka. Nikaja kwa Mtume ﷺ na kumjulisha kuwa wameshaondoka. Akaja na kuingia. Nikamfuata ili niingie, akaweka kizuizi baina yangu na yeye.”

Allah تعالى Akateremsha:

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لَا تَدْخُلُوْا بُيُوْتِ النَّبِيِّ اِلَّا اَنْ يُدْزَبَ لَكُمْ اِلَى طَعَامٍ غَيْرِ نٰظِرِيْنَ
اِنَّهٗ وَلٰيْكِنْ اِذَا دُعِيْتُمْ فَاَدْخُلُوْا فَاِذَا طَعِمْتُمْ فَانْتَشِرُوْا

“Enyi mlioamini! Msiingie nyumba za Nabii ila mpewe ruhusa kwenda kula, sio kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa basi ingieni, na mkisha kula tawanyikeni...”²

Vile vile Bukhari aliinukuu mahali pengine,³ na Muslim na Nasai.⁴ Bukhari alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه tena, kwamba: “Mtume ﷺ alimuoa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها kwa karamu ya nyama na mkate. Nikatumwa kuwaalika watu kwa ajili ya karamu. Watu wakawa wanakuja na kutoka. Nikawaalika, mpaka sikupata tena wa kumualika. Nikasema, ‘Ewe Mtume wa Allah! Sipati tena wa kumualika.’ Akasema:

«اَزْفَعُوا طَعَامَكُمْ»

“Kiondoeni chakula chenu.”

¹ Fat’h Al-Bari 8:387.

² Fat’h Al-Bari 8:387.

³ Fat’h Al-Bari 11:24.

⁴ Muslim 2:1050, An-Nasai katika Al-Kubra 6:435.

Wakabakia watu watatu wakizungumza katika nyumba. Mtume ﷺ akatoka na kuelekea katika chumba cha 'Aishah رضي الله عنها na kusema:

«السَّلَامُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ»

“Amani iwe juu yenu, watu wa nyumba hii, na rehema za Allah na baraka Zake.”

Akasema: 'Na juu yako pia iwe amani na rehema za Allah تعالى. umemkutaje mkeo (mpya) ewe Mtume wa Allah? Allah تعالى Akupe baraka.' Akazunguka kwa wakeze wote, akiwaambia kama alivyomuambia 'Aishah رضي الله عنها, na wao wanamuambia sawa na alivyosema 'Aishah رضي الله عنها. Kisha, Mtume ﷺ akarejea katika hiyo nyumba na kuwakuta watu watatu wakiongea. Mtume ﷺ alikuwa mwenye haya nyingi. Akatoka kuelekea kwa 'Aishah رضي الله عنها, sijui kwamba nilimjulisha au alijulishwa kwamba wale watu wameshaondoka. Akarejea, alipoweka mguu wake katika kizingiti cha mlango kwa ndani na mwingine ukiwa nje, aliweka pazia baina yangu na yeye. Kisha, Aya kuhusu Hijabu ilishushwa.¹ Hii ilinukuliwa na Bukhari peke yake kati ya Vitabu Sita, mbali ya Nasai katika *Al-Yawm wal-Laylah*.² Hivyo, Kauli ya Allah تعالى:

لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ

“Msiingie nyumba za Nabii...”

Ni kukatazwa kwa Waumini juu ya kuingia makazi ya Mtume ﷺ pasi na idhini, kama walivyokuwa wakifanya zama za ujahili na mwanzoni mwa Uislamu, mpaka Allah تعالى Akauneemesha umma huu na Akauamrisha hivyo. Hayo ni miongoni mwa Ukarimu wa Allah تعالى kwa umma huu. Kwa ajili hii, Mtume ﷺ amesema:

«إِيَّاكُمْ وَالذُّخُولَ عَلَى النِّسَاءِ»

“Nakutahadharisheni kuingia kwa wanawake.”³

Halafu Allah تعالى Akaweka ruhusa katika hilo, akasema:

¹ Fat'h Al-Bari 8:388.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:75.

³ Muslim 4:1711.

إِلَّا أَنْ يُؤَدَّبَ لَكُمْ إِلَى طَعَامٍ غَيْرَ نَبْطِينَ إِنَّهُ

“...ila mpewe ruhusa kwenda kula, sio kungojea kiive.”

Mujahid, Qatadah na wengine wamesema: “Maana yake, bila ya kungojea kuiva kwa chakula kitayarishwe.”² Yaani, bila ya kusubiria chakula ili kipikwe, hadi kitakapokaribia kutayarishwa, basi, mjidhihirishe kwa ajili ya kuingia. Jambo hili ni katika Anayoyakasirikia Allah تعالى na Kuyakemea. Huu ni ushahidi wa kuharamishwa uroho (mgeni asiyealikwa), na ndiyo Waarabu huita *Adh-Dhwayfain*. Khatwib Baghdadi aliandika kitabu juu ya mada hii kuwakemea wavamizi wa shughuli za watu bila ya kupewa mwaliko, pamoja na kutoa khabari zao nyingi ambazo ni ndefu sana kiasi cha kutokufaa kunukuliwa hapa. Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَلَكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَأَدْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ فَانْتَشِرُوا

“Lakini mtakapoitwa basi ingieni, na mkisha kula tawanyikeni...”

Ndani ya *Sahih Muslim* kuna Hadithi ya Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kwamba amesema, Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا دَعَا أَحَدُكُمْ أَخَاهُ فَلْيَجِبْ عُرْسًا كَانَ أَوْ غَيْرَهُ»

“Mmoja wenu anapomualika nduguye, basi amuitike, iwe kwa harusi au kwa jambo jingine.”³

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَلَا مُسْتَعْسِينَ لِحَدِيثٍ

“...wala msiweke mazungumzo.”

Yaani, kama ilivyotokea kwa wale watu watatu waliosalia nyuma na kufanya mazungumzo, wakajisahau mpaka kukawa na uzito kwa Mtume ﷺ. Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 20:306.

² Muslim 2:1053.

إِنَّ دَلِكُمْ كَانَ يُؤْذِي النَّبِيَّ فَيَسْتَحْيِيهِ مِنْكُمْ ۗ

“Hakika hayo yanamuudhi Nabii naye anakustahini...”

Ilisemekana kwamba maana yake ni kuwa, kuingia kwenu nyumbani kwake bila ya idhini yake kulikuwa kunampa uzito na kumsumbua. Lakini alikuwa hapendi kuwakataza kwa sababu ya haya zake nyingi, mpaka Allah تعالی Akateremsha Aya ya Kukataza. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيِيهِ مِنَ الْحَقِّ ۗ

“...lakini Mwenyezi Mungu Hastahi kwa jambo la haki.”

Yaani, kwa ajili hii, Allah تعالی Amekukatazeni kulifanya. Kisha Allah تعالی Amesema:

وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ۗ

“Na mnapowauliza wakeze haja waulizeni nyuma ya mapazia.”

Yaani, kama Nilivyokukatazeni kuingia kwao, basi nimekukatazeni kabisa kuwaangalia, hata kama mmoja wenu ana haja ya kuchukua kitu kutoka kwao, basi asiwaangalie, wala asiulize haja yoyote isipokuwa kutokea nyuma ya pazia.

Kukatazwa Kumuudhi Mtume ﷺ na Kubainishwa Utukufu wa Wakeze kwa Waislamu

Kauli ya Allah تعالی:

وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ وَلَا أَنْ تُنكِحُوا أَرْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَدًا ۗ إِنَّ

دَلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٤﴾

“Wala haitakiwi kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, wala kuwaoa wake zake baada yake kabisa. Hakika jambo hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Ibn Abu Hatim رضي الله عنهما alimnukuu Ibn ‘Abbas رحمه الله تعالی kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ

“Wala haitakiwi kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu...”

Kuwa alisema, “Hii iliteremshwa kuhusu mtu aliyetaka kumuoa mmoja wa wake wa Mtume ﷺ, baada ya kufariki kwake. Mtu mmoja alimuambia Sufyan, ‘Alikuwa ‘Aishah رضي الله عنها?’ Akasema: ‘Hivyo ndivyo walivyosema.’”¹

Haya kadhalika, yalisemwa na Muqatil bin Hayyan na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam.²

Alitaja katika isnadi yake, kutoka kwa Suddi kwamba, aliyedhamiria hayo ni Twalhah bin (‘Ubayd) رضي الله عنه mpaka ikateremshwa Aya hii ya kukataza. Hivyo, maulamaa wote wamekubaliana, kwamba baada ya kufariki Mtume ﷺ na kuwaacha wake zake, ni haramu kwa mtu mwingine kuwaoa baada yake, kwa sababu hao ni wakeze duniani na Akhera, tena ni Mama wa Waumini kama ilivyotangulia kuelezwa.

Allah تعالى Alifanya hilo kuwa ni jambo kubwa, Akalisitiza na Kulitolea maonyo kwa Kauli Yake,

إِنَّ ذَلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا

“Hakika jambo hilo ni kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Kisha, Allah تعالى Amesema:

إِنْ تَبَدُّوا شَيْئًا أَوْ تَخَفُوهُ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿١٩﴾

“Mkidhirisha chochote kile, au mkikificha, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua kila kitu.”

Yaani, chochote mnachoficha katika dhamira, hakijafichikana Kwake (Allah تعالى) hata chembe,

يَعْلَمُ خَائِنَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ

“(Mwenyezi Mungu) Anajua khiyana ya macho na yanayoficha vifua.” (40:19)

¹ Ad-Dur Al-Manthur 6:643. Hii ilinukuliwa na Ibn Abu Hatim bila ya isnadi.

² 164 At-Tabari 20:316

لَا جُنَاحَ عَلَيْهِنَّ فِي آبَائِهِنَّ وَلَا
 أَبْنَائِهِنَّ وَلَا إِخْوَانِهِنَّ وَلَا نِسَائِهِنَّ وَلَا
 مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ وَأَتَقِينَ اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ
 شَيْءٍ شَهِيدًا ﴿٥٥﴾ إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ ۚ
 يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾ إِنَّ
 الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ
 وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿٥٧﴾ وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ
 الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بِغَيْرِ مَا اكْتَسَبُوا فَقَدِ احْتَمَلُوا
 بُهْتَنًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٨﴾ يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لَأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ
 وَنِسَاءَ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلِيبِهِنَّ ۚ ذَلِكَ
 أَدَّىٰ أَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَنَ ۚ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٥٩﴾
 * لَيْسَ لَكَ يَنْتَهَى الْمُنْتَفِعُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ
 وَالْمُرْجِفُونَ فِي الْمَدِينَةِ لَنُغْرِبَنَّكَ بِهِمْ ثُمَّ لَا
 يُجَاوِزُونَكَ فِيهَا إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٠﴾ مَلْعُونِينَ أَيْنَمَا ثُقِفُوا
 أُخِذُوا وَقُتِلُوا تَقْتِيلًا ﴿٦١﴾ سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا
 مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَنْ نَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿٦٢﴾

لَا جُنَاحَ عَلَيْهِنَّ فِي آبَائِهِنَّ وَلَا
 أَبْنَائِهِنَّ وَلَا إِخْوَانِهِنَّ وَلَا نِسَائِهِنَّ وَلَا
 إِخْوَانِهِنَّ وَلَا أَبْنَاءَ أَخَوَاتِهِنَّ وَلَا
 نِسَائِهِنَّ وَلَا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ
 وَأَتَقِينَ اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ
 كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا ﴿٥٥﴾

55. "Hapana ubaya kwao (wake za Mtume) katika kuonana na baba zao, wala watoto wao, wala kaka zao, wala watoto wa kaka zao, wala watoto wa dada zao, wala wanawake wenzao, wala wale iliyowamiliki mikono yao ya kulia. (Na enyi wanawake), mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu."

Watu ambao Mwanamke halazimiki kuwa na Hijabu

Allah تعالی Alipowaamrisha

wanawake wajisitiri dhidi ya ajinabi, Alibainisha kwamba ndugu ambao hakuna wajibu wa kuwa na hijabu kwao.

Ni kama walioruhusiwa ambao wametajwa katika Surat An-Nur, katika Kauli ya Allah تعالی:

وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ آبَائِهِنَّ أَوْ أَبْنَائِهِنَّ
 أَوْ أَبْنَاءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَانِهِنَّ أَوْ بَنِي إِخْوَانِهِنَّ أَوْ نِسَائِهِنَّ أَوْ مَا
 مَلَكَتْ أَيْمَانُهُنَّ أَوْ التَّبِيعِينَ غَيْرِ أُولَى الْأَرْزَاقِ مِنَ الرِّجَالِ أَوْ الْوَالِدِ الَّذِينَ لَمْ
 يَظْهَرُوا عَلَى عَوْرَتِ النِّسَاءِ^ط

“...wala wasioneshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wanaume wasio na matamano, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyokhusu uke.” (24:31)

Aya hiyo ina maelezo zaidi ya haya, na Tafsihi na maelezo yake imeshatangulia kwa kiasi cha kutosha kwa kutokuwa na haja ya kuyarejea.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Sha'bi, 'Ikrimah waliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

لَا جُنَاحَ عَلَيْهِنَّ فِي آبَائِهِنَّ

“Hapana ubaya kwao (wake za Mtume) kuonana na baba zao...”

“Nilisema: ni vipi ami na mjomba, hawakutajwa?” Akasema: “Kwa sababu wao humsifia kwa ajili ya watoto wao, basi haipendezi kwa mwanamke kuondoa ushungi wake mbele ya mjomba wala ami yake.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا نِسَائِهِنَّ

“...wala wanawake wenzao...”

Yaani, kutojitia hijabu dhidi ya wanawake Waumini. Kauli ya Allah تعالى:

¹ At-Tabari 20:318.

وَلَا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ^١

“...wala wale iliyo wamiliki mikono yao ya kulia.”

Inamaanisha, wajakazi wao. Sa'id bin Musayyab alisema: “Inamaanisha wajakazi wa kike tu.” Hayo aliyankuu Ibn Abu Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Kauli ya Allah تَعَالَى:

وَأَتَقِينَ اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا

“...mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu.”

Yaani, mumkhofu faraghani na hadharani, Yeye Hushuhudia kila kitu, wala hakifichikani kitu kwake. Basi, mfikirieni Ambaye muda wote ni Mwenye kuchunga.

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٥٦﴾

56. “Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika Wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu.”

Amri ya Kumsalia Mtume ﷺ.

Bukhari alisema: “Abu Al-’Aliyah alisema: Sala ya Allah تَعَالَى ni Kumsifia yeye mbele ya Malaika, na Sala ya Malaika ni dua yao.” Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alisema: “Wanamtakia baraka.”¹ Abu ‘Isa At-Tirmidhi alisema: “Hii ilinukuliwa kutoka kwa Sufyan Ath-Thawri رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى na wanazuoni wengine ambao walisema, ‘Sala ya Allah تَعَالَى ni Rehema, na Sala ya Malaika ni kuomba kwao maghufira.”² Zilikuja Hadithi *Mutawatir* kutoka kwa Mtume ﷺ zikiamrisha jambo la kumsalia na namna ya kumswalia. Sisi tutazitaja, Inshaallah, kiasi tutakachoweza, na Allah تَعَالَى Ndiye tunayemuomba msaada.

Katika kuitafsiri Aya hii, Bukhari alinukuu kutoka kwa Ka’b bin ‘Ujrah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kwamba alisema: Kulisemwa, “Ewe Mtume wa Allah! Ama kuhusu kukutolea *Salam*, tayari tumeshajua. Lakini, vipi tukusalie?” Akasema:

¹ Fat’h Al-Bari 8:392.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 2:610.

«قُولُوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ،
إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ
إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ»

“Semeni: ‘Ewe Allah! Mrehemu Muhammad na familia ya Muhammad, kama ulivyomrehemu Ibrahim na familia ya Ibrahim. Kwa hakika! Wewe Ndiwe Mhimidiwa, Msifiwa. Ewe Allah! Mbariki Muhammad na familia ya Muhammad, kama Uliyombariki Ibrahim na familia ya Ibrahim. Kwa hakika! Wewe Ndiwe Mhimidiwa, Msifiwa.”¹

Na katika riwaya ya Tirmidhi na Abdurrahmani bin Abuu Laila alikuwa akisema, “Na Urehemu kwetu pamoja na wao.”

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn Abu Layla kuwa alisema: Ka’b bin ‘Ujrah رضي الله عنه alikutana nami, akasema, “Je nisikupatie zawadi?” Mtume ﷺ alitutokea, nasi tukasema: “Ewe Mtume wa Allah! Tunajua, au tunafahamu namna ya kukutolea Salam, basi, vipi tukusalie?”

«قُولُوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ،
إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ
إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ»

“Semeni: ‘Ewe Allah! Mrehemu Muhammad na familia ya Muhammad, kama Uliyomrehemu Ibrahim na familia ya Ibrahim. Kwa hakika! Wewe Ndiwe Mhimidiwa, Msifiwa. Ewe Allah! Mshushie baraka Muhammad na familia ya Muhammad, kama Uliyomshuhia baraka Ibrahim na familia ya Ibrahim. Kwa hakika! Wewe Ndiwe wa Kuhimidiwa, wa Kusifiwa.”

Hadithi hii imepokelewa na kundi la wakusanyaji wa hadithi ndani ya Vitabu vyao kupitia isnadi mbalimbali.

¹ Fat’h Al-Bari 8:392.

Hadithi Nyingine

Bukhari alimnukuu Sa'id Al-Khudri رضي الله عنه kuwa alisema: "Tulisema, 'Ewe Mtume ﷺ, hii ni Salam juu yako, basi ni vipi tukusalie?'" Akasema:

«قُولُوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ ،
وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ»

"Semeni: 'Ewe Allah! Mrehemu Muhammad, mja na Mjumbe Wako, kama Ulivyomrehemu Ibrahim. Na Ushushe baraka juu ya Muhammad na familia ya Muhammad kama ulivyoibariki familia ya Ibrahim."

Abu Swalih amesema, kutoka kwa Al-Laythi,

«عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ»

"Juu ya Muhammad na familia ya Muhammad kama Ulivyoibariki familia ya Ibrahim."

Ibrahim bin Hamzah alitusimulia, kuwa Ibn Abu Hazim na Ad-Daraawardi alitueleza, kuwa Yazid, yaani, Ibn Al-Had alisema:

«كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى
إِبْرَاهِيمَ وَآلِ إِبْرَاهِيمَ»

*"Kama Ulivyomrehemu Ibrahim. Na Um-bariki Muhammad na familia ya Muhammad kama Ulivyom-bariki Ibrahim na familia ya Ibrahim."*¹

Ilinukuliwa na An-Nasai na Ibn Majah pia.²

Hadithi Nyingine

Imamu Ahman alimnukuu Abu Humayd As-Sa'idi, kwamba wao walisema: "Ewe Mtume wa Allah! Ni namna gani tukusalie?" Akasema:

¹ Fat'h Al-Bari 8:392.

² An-Nasai 3:49, Ibn Majah 1:292.

«قُولُوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ»

“Semeni: ‘Ewe Allah! Mrehemu Muhammad, wakeze na watoto wake, kama Ulivyomrehemu Ibrahim. Na Um-bariki Muhammad, wakeze na watoto wake, kama Ulivyoibariki familia ya Ibrahim. Hakika Wewe Ndiwe Mhimidiwa, Msifiwa.”¹

Pia ilinukuliwa na kundi lililosalia, isipokuwa At-Tirmidhi.²

Hadithi Nyingine

Muslim alimnukuu Abu Sa’id Al-Answari رضي الله عنه, kuwa alisema: “Mtume ﷺ alitujia tukiwa katika kikao kwa Sa’d bin ‘Ubadah. Bashir bin Sa’d akamuambia: “Allah تعالى Ametuamrisha tukusalie, ewe Mtume wa Allah! Je, tukusalie vipi?” Mtume ﷺ akanyamaza, mpaka tukatamani kwamba asingelimuuliza. Kisha, Mtume ﷺ akasema:

«قُولُوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ فِي الْعَالَمِينَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ وَالسَّلَامُ كَمَا قَدْ عَلِمْتُمْ»

“Semeni: ‘Ewe Allah! Mrehemu Muhammad na kwa familia ya Muhammad, kama Ulivyoirehemu familia ya Ibrahim. Na mbariki Muhammad na ali ya Muhammad, kama Ulivyombariki Ibrahim na familia ya Ibrahim, ulimwenguni. Hakika Wewe Ndiwe Mhimidiwa, Msifiwa. Na Salam ni kama mnavyojua.”³

Hii pia ilinukuliwa na Abu Dawud, An-Nasai, At-Tirmidhi na Ibn Jarir. At-Tirmidhi alisema, “Ni Hasan Sahih.”⁴

¹ Ahmad 5:424.

² Fat’h Al-Bari 11:157, Muslim 1: 306, Abu Dawud 1:600, An-Nasai 3:49, Ibn Majah 1:293

³ Muslim 1:305

⁴ Abu Dawud 1:600 Tuhfat Al-Ahwadhi 9:84, An-Nasai katika Al-Kubra 6:436, At-Tabari

Uwajibu wa Kumsalia Mtume ﷺ Katika Sala Kabla ya Dua

Imamu Ahmad, Abu Dawud na At-Tirmidhi ambaye aliiweka katika daraja la *Sahih*. Pia, An-Nasai, Ibn Khuzaymah na Ibn Hibban, ndani ya *Sahih* zao, kutoka kwa Fadhwalah bin 'Ubayd رضي الله عنه, kuwa alisema: Mtume ﷺ alimsikia mtu mmoja akiomba dua katika Sala yake bila ya Kumsifu Allah تعالى wala kumswalia Mtume ﷺ. Akasema Mtume ﷺ:

«عَجَلٌ هَذَا»

“Amefanya haraka huyu.”

Kisha akamuita na kumuambia yeye na wengine.

«إِذَا صَلَّى أَحَدُكُمْ فَلْيَبْدَأْ بِتَسْبِيحِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ وَالشَّوْءِ عَلَيْهِ، ثُمَّ لِيُصَلِّ عَلَى النَّبِيِّ ثُمَّ لِيَبْدَعْ بِغَدُّ بِمَا شَاءَ»

“Mmoja wenu anapoomba dua, aanze kwa Kumsifu na Kumtukuza Allah, kisha amswalia Mtume, baada ya hapo aombe dua atakavyo.”¹

Fadhila za Kumsalia Mtume ﷺ

Imepokelewa kutoka kwa Abdurrahman bin Awf رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ alitoka akaelekea upande na kujikurubisha Kwake. Akaingia akaelekea Qibla akaenda chini hali ya kusujudu. Na sijida akairefusha sana hadi nikadhania ya kuwa Allah Amemfisha. Nikamsogelea akainua kichwa chake akasema: “Ni nani huyu?” Nikasema ni Abdurrahman. Mtume ﷺ akasema, “Unasemaje?” Nikasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! umesujudu sijida ndefu mno hadi nikadhani ya kuwa Allah labda Ameutoa uhai wako.” Mtume ﷺ akasema “Hakika Jibril amenijia akanipa habari nzuri ya kuwa Allah تعالى Anasema: “Yeyote yule atakayekutakia wewe rehema Nami Nitamtakia yeye rehema, na atakayekutakia amani Nami Nitamtakia yeye amani. Hivyo nikasujudu kwa ajili ya Allah kwa Kumshukuru.” Na Abdillah bin Masudi رضي الله عنه amesema:

¹ Ahmad 6:18, Abu Dawud 2:162, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:450, An-Nasai 3:44, Ibn Khuzaymah 1:351, Ibn Hibban 3:308.

“Hakika Mtume ﷺ amesema: “Mbora wa watu kwangu mimi siku ya kيامa ni yule anayekithirisha sana kuniswalia.”

Hadithi Nyingine

At-Tirmidhi alimnukuu Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه akisema: Mtume ﷺ baada ya kwisha kwa theluthi mbili za usiku, husimama na kusema,

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! اذْكُرُوا اللَّهَ، اذْكُرُوا اللَّهَ، جَاءَتِ الرَّاجِمَةُ تَبِعُهَا الرَّادِقَةُ، جَاءَ الْمَوْتُ بِمَا فِيهِ، جَاءَ الْمَوْتُ بِمَا فِيهِ»

“Enyi watu! Mkumbukeni Allah, mkumbukeni Allah, mpulizo wa kwanza wa parapanda umeshakuja, na utafuatiwa na mpulizo wa pili, mauti yamekuja na vihoro vyake pamwe, mauti yamekuja na vihoro vyake pamwe.”

Ubayy رضي الله عنه akasema: “Nilisema, ‘Ewe Mtume wa Allah! Mimi hukithirisha kukuswalia, je niweke kiasi gani cha kukuswalia?’ Akasema:

«مَا شِئْتُ»

“Upendavyo.”

Nikasema: “Robo.” Akasema:

«مَا شِئْتُ، فَإِنْ زِدْتَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكَ»

“Upendavyo, na ukizidisha, basi ni kheri kwako.”

Nikasema: “Nusu.” Akasema:

«مَا شِئْتُ، فَإِنْ زِدْتَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكَ»

“Upendavyo, na ukizidisha, basi ni kheri kwako.”

Nikasema: “Theluthi mbili.” Akasema:

«مَا شِئْتُ، فَإِنْ زِدْتَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكَ»

“Upendavyo, na ukizidisha, basi ni kheri kwako.”

Nikasema: "Sala yangu yote." Akasema:

«إِذْ نُنْفِئُكَ مِنْكَ، وَيُعْفِرُ لَكَ ذُنُوبَكَ»

*"Hiyo basi utatoshwa hamu yako na kughufiriwa madhambi yako."*¹

Kisha akasema: "Hadithi hii ni *Hasan*."

Hadithi Nyingine

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Twalhah kwamba siku moja, Mtume ﷺ alikuja akiwa mwenye furaha iliyoonekana usoni mwake. Wakasema: "Ewe Mtume wa Allah! Tunakuona usoni kwako kuwa una furaha." Akasema:

«إِنَّهُ أَتَانِي الْمَلَكُ فَقَالَ: يَا مُحَمَّدُ! أَمَا يُرْضِيكَ أَنَّ رَبَّكَ عَزَّ وَجَلَّ يَقُولُ: إِنَّهُ لَا يُصَلِّي عَلَيْكَ أَحَدٌ مِنْ أُمَّتِكَ إِلَّا صَلَّيْتُ عَلَيْهِ عَشْرًا، وَلَا يُسَلِّمُ عَلَيْكَ أَحَدٌ مِنْ أُمَّتِكَ إِلَّا سَلَّمْتُ عَلَيْهِ عَشْرًا، قُلْتُ: بَلَى»

*"Malaika amenijia, akasema: 'Ewe Muhammad! Inakuridhisha kwamba Allah Anasema, 'Hakuswali mmojawapo katika umma wako, isipokuwa Nitamswalia mara kumi. Wala hakusalimu yeyote katika umma wako, bali Mimi nitamsalimu mara kumi.' Nikasema: 'Khasa (kwanini nisiridhie).'"*²

Hii ilinukuliwa na An-Nasai pia.³

Isnadi Nyingine ya Usimulizi

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Twalhah Al-Answari akisema kuwa: Siku moja, Mtume ﷺ asubuhi moja alikuwa akionekana usoni kwake akiwa mwenye furaha. Wakasema: "Ewe Mtume wa Allah! Asubuhi hii umekuwa mwenye furaha ambapo furaha inaonekana usoni mwako." Akasema:

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:152.

² Ahmad 4:30.

³ An-Nasai 3:44.

«أَجَلُ أَتَانِي آتٍ مِنْ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ فَقَالَ: مَنْ صَلَّى عَلَيْكَ مِنْ أُمَّتِكَ صَلَاةً، كَتَبَ اللَّهُ لَهُ بِهَا عَشْرَ حَسَنَاتٍ وَمَحَا عَنْهُ عَشْرَ سَيِّئَاتٍ، وَرَفَعَ لَهُ عَشْرَ دَرَجَاتٍ، وَرَدَّ عَلَيْهِ مِنْهَا»

“Naam, hivi punde tu, alinjia mjaji (Malaika) kutoka kwa Mola Wangu, akasema: ‘Mmojawapo katika umma wako atakayekuswalia Sala moja, Allah Atamuandikia kwayo mema kumi kwa hilo na Atamfutia maovu kumi, Atampandisha daraja kumi na Atamrudishia maamkizi mfano wake.”¹

Hii nayo ina isnadi *jayyid* (nzuri), lakini hawakuiandika.

Hadithi Nyingine

Muslim, Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai walimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ صَلَّى عَلَيَّ وَاجِدَةً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا»

“Mwenye kuniswalia mimi mara moja, basi Allah Atamswalia mara kumi.”

At-Tirmidhi amesema: Hadithi hii ni *Hasan Sahih*. Katika mlango huo huo, kuna masimulizi kutoka kwa ‘Abdur-rahman bin ‘Awf, ‘Amir bin Rabi’ah, ‘Amaar, Abu Twalhah, Anas na Ubayy bin Ka’b رضي الله عنهم.¹

Uwajibu wa Kumswalia Mtume ﷺ Kila Anapotajwa.

Imamu Ahmad amenukuu kuwa Al-Husayn bin ‘Ali رضي الله عنهما amesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الْبَخِيلُ مَنْ ذُكِرَتْ عِنْدَهُ نَمٌّ لَمْ يُصَلِّ عَلَيَّ»

“Bakhili ni yule ambaye nimetajwa mbele yake kisha hakuniswalia.”

¹Ahmad 4:29.

²Muslim 1:306, Abu Dawud 2:184, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 2:608, An-Nasai 3:50.

Abu Sa'id رضي الله عنه alisema:

«فَلَمْ يُصَلِّ عَلَيَّ»

“...hakuniswalia.”¹

Hii pia ilinukuliwa na At-Tirmidhi, ambaye kisha alisema, “Hadithi hii ni *Hasan, Gharib, Sahih*.”²

Hadithi Nyingine

At-Tirmidhi alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ amesema,

«رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ ذَكِرْتُ عِنْدَهُ فَلَمْ يُصَلِّ عَلَيَّ، وَرَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ دَخَلَ عَلَيْهِ شَهْرُ رَمَضَانَ ثُمَّ انْسَلَخَ قَبْلَ أَنْ يُغْفَرَ لَهُ، وَرَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ أَدْرَكَ عِنْدَهُ أَبَوَاهُ الْكَبِيرَيْنِ فَلَمْ يُدْخِلَاهُ الْجَنَّةَ»

“Imeangamia pua ya mtu ambaye nimetajwa mbele yake hakuniswalia. Imeangamia pua ya mtu ambaye mwezi wa Ramadhani umeingia kisha ukaondoka kabla hajaghufuliwa, na aangamie mtu ambaye wazazi wake wamepatwa na uzee, lakini hawakumuingiza Peponi.”

Kisha (At-Tirmidhi) alisema, “*Hasan Gharib*.”³

Na imenukuliwa kutoka kwa bin Abbas رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ, “*Atakayeacha kunisalia atakuwa amekosa njia ya peponi.*” Kauli nyingine juu ya hili ni kwamba ndani yake kuna ushahidi wa kupasa kumsalia Mtume ﷺ kila anapotajwa. Na huu ni mtazamo wa baadhi ya wanazuoni akiwemo Twahawi na Halimi. Na baadhi yao wamesema kuwa ni wajibu kumsalia Mtume ﷺ katika baraza aliyotajwa mara moja tu. Na wala haipasi mara nyingine katika baraza hiyo. Bali inapendeza kama alivyonukuu At-Tirmidhi kutoka kwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema, “*Hawaachi kuwa*

¹ Ahmad 1:201.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:531.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:530.

watu wameketi katika baraza ambayo hawamtaji Allah, wala kumswalia Mtume wao, ila watu hao watapata hasara na majuto, Allah Akitaka Atawaadhibu na Akitaka Atawasamehe."

Matukio Ambamo Mtume ﷺ Husaliwa

Imekuja amri ya kumswalia Mtume ﷺ katika nyakati nyingi. Miongoni mwao ni baada ya wito kwa ajili ya Sala. Ni kutokana na Hadithi aliyoisimulia Imamu Ahmad kutoka kwa 'Abdullah bin 'Amri bin Al-'As رضي الله عنه. Alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema:

إِذَا سَمِعْتُمْ مُؤَذِّنًا فَقُولُوا مِثْلَمَا يَقُولُ، ثُمَّ صَلُّوا عَلَيَّ، فَإِنَّهُ مَنْ صَلَّى عَلَيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا، ثُمَّ سَلُوا اللَّهَ لِي الْوَسِيلَةَ، فَإِنَّهَا مَنْزِلَةٌ فِي الْجَنَّةِ لَا تَنْبَغِي إِلَّا لِعَبْدٍ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ، وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ، فَمَنْ سَأَلَ لِي الْوَسِيلَةَ حَلَّتْ عَلَيْهِ الشَّفَاعَةُ

*"Pindi mkimsikia Mwachini, basi semeni kama anavyosema, kisha mniswalie, kwani mwenye kuniswalia, Allah Atamswalia mara kumi. Halafu mniombea Al-Wasilah kwa Allah, ambayo ni makazi Peponi ambayo haitarajii isipokuwa mja mmoja tu katika waja wa Allah, na ninatarajia kwamba mimi ndiye nitakayekuwa. Mwenye kuniombea Al-Wasilah, basi atahalalikiwa kupata shufaa."*¹

Hadithi hii imenukuliwa na Muslim, Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai.²

Imamu Ahmad amesema kutoka kwa Ruwaif bin Thabiti رضي الله عنه kwamba: Mtume wa Allah ﷺ amesema: "Yeyote atakayemswalia Muhammad na akasema, 'Ewe Allah! mweke katika makazi yaliyo karibu na Wewe siku ya kiama, hivyo inampasa yeye uombezi wangu." Na hii ni Isnadi isiyokuwa na shaka ndani yake. Na waandishi wengine wa Hadithi hawakuitaja athari ya Bin Abbas رضي الله عنهما katika hilo.

Na amepokea Ismail Al-Qadhi kutoka kwa bin Abbas رضي الله عنهما: "Ewe Mola Wangu Ukubali uombaji mkubwa wa Muhammad na Uinue daraja yake ya

¹ Ahmad 2:168.

² Muslim 1:288, Abu Dawud 1:359, Tuhfat Al-Ahwadhi 1:83, An-Nasai 2:25

juu, na Umpe hitaji lake la dunia na akhera, kama Ulivyompa Ibrahim na Musa.”
Isnadi ya Hadithi ina nguvu na ni sahihi.

Pia, wakati wa kuingia na kutoka msikitini. Ni kutokana na Hadithi aliyoinukuu Imam Ahmad kutoka kwa Fatmah bint wa Mtume رضي الله عنها. Alisema: Mtume ﷺ alikuwa akiingia msikitini humswalia Muhammad ﷺ, kumtolea salamu, kisha husema:

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي وَافْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ»

“Ewe Allah! Nighufirie madhambi yangu na Unifungulie milango ya Rehema Zako.”

Na alipotoka humsalia Muhammad ﷺ, na kumtolea salamu, kisha husema

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي وَافْتَحْ لِي أَبْوَابَ فَضْلِكَ»

“Ewe Allah! Nighufirie madhambi yangu na unifungulie milango ya Fadhila Zako.”¹

Miongoni mwa nyakati hizo ni kumswalia wakati wa Sala ya Jeneza. Ni Sunna katika Takbira ya kwanza isomwe *Surat Al-Fatihah*, katika ya pili iletwe Sala ya Mtume ﷺ, katika ya tatu amwombe maiti, na katika ya nne, aseme, “Ewe Allah تعالى, Usitunyime malipo yake, wala Usitujaribu baada yake.”

Ash-Shafi رحمه الله تعالى, alinukuu kuwa Umaamah bin Sahl bin Hunayf kwamba aliambiwa na mmoja wa Masahaba wa Mtume ﷺ kwamba ni Sunna katika Swala ya Jeneza, Imam alete Takbira, kisha asome *Surat Al-Fatihah* moyoni baada ya Takbira ya kwanza, kisha amswalie Mtume ﷺ na amuombe dua huyo aliyefariki, na asisome Qur’an katika Takbira yoyote nyingine. Halafu amalizie kwa kutamka *Salaam* kimoyomoyo.² Na aliinukuu An-Nasai kutoka kwa Abu Umaamah mwenyewe, akasema kwamba “Hii ni katika Sunna.”³ Kwa mujibu wa rai sahihi, kauli kama hiyo, iliyosimuliwa na Sahaba inaingia katika hukumu ya Hadithi *Marfu*.⁴

¹ Ahmad 56:282.

² *Musnad Ash-Shafi’i* uk 210.

³ An-Nasai 4:75.

⁴ Maana yake hapa ni kwamba kauli; “hii ni Sunnah” inayotoka kwa Sahaba, yaani inachukuliwa kwamba imetoka kwa Mtume mwenyewe.

Imependekezwa kukamilisha dua kwa kumswalia Mtume ﷺ. At-Tirmidhi alimnukuu 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kuwa amesema:

«الدُّعَاءُ مَرْقُوفٌ بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، لَا يَضَعُهُ حَتَّى يُصَلِّيَ عَلَيَّ، فَلَا تَجْعَلُونِي
كَغَمْرِ الرَّأِيبِ، صَلُّوا عَلَيَّ، أَوَّلَ الدُّعَاءِ وَآخِرَهُ وَأَوْسَطَهُ»

“Dua huzuiliwa baina ya mbingu na ardhi, haipandi mpaka mtu aniswalie. Msinifanye kuwa kama chombo cha akiba cha kuwekea maji. Niswalieni kwa Allah mwanzoni mwa dua yako, mwishoni mwake na katikati yake.”¹

Pia ilisimuliwa na Mu'adh bin Al-Harith kutoka kwa Abu Qurrah kutoka kwa Sa'id bin Al-Musayyab, kutoka kwa 'Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema (*Marfu*).²

Miongoni mwa yenye kulitilia hilo nguvu ni dua ya *Qunut*, kwa mujibu wa alivyonukuu Ahmad na wanaonukuu katika *Sunan*, Ibn Khuzaymah, Ibn Hibban na Al-Hakim, kuwa Al-Hasan bin 'Ali رضي الله عنه alisema: Mtume wa Allah ﷺ alinifundisha maneno ya kuyasema katika Sala ya Witri:

«اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ، وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ، وَبَارِكْ لِي
فِيمَا أَعْطَيْتَ، وَفِي سِرِّ مَا قَضَيْتَ، فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ، وَإِنَّهُ لَا يَذُلُّ
مَنْ وَالَيْتَ، وَلَا يَعْرِضُ مَنْ عَادَيْتَ، تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ»

“Ewe Allah! Niongoze katika ambao Uliowaongoza, Unipe afya katika ambao Uliowapa afya, Unisaidie katika ambao Uliowasaidia wao, Unibariki katika Uliyoyotoa. Nikinge dhidi ya shari Uliyoihukumu. Wewe Ndiwe Unayehukumu wala Huhukumiwi. Kwa hakika! Unayemtukuza hadhaliliki, wala hatukuki Unayemfanya kuwa adui. Ewe Mola Wetu Umetakasika na Umetukuka.”³

Baada ya haya, An-Nasai aliongeza ndani ya *Sunan* yake,

¹ *Tuhfat ul-Ahwadhi* 2:610.

² *Takhrij Al-kashshaf* ya Ibn Hajar uk. 137.

³ *Jami' Al-Usul* 4:155.

«وَصَلَّى اللهُ عَلَى مُحَمَّدٍ»

“Na Allah mswalie Muhammad.” mwishoni mwa Qunut hiyo.¹

Miongoni mwa matukio hayo, imependekezwa kukithirisha kumswalia katika usiku na mchana wa siku ya Ijumaa. Imamu Ahmad alinukuu kuwa Aws bin Aws Ath-Thaqafi رضى الله عنه alisema, Mtume ﷺ amesema:

«مِنْ أَفْضَلِ أَيَّامِكُمْ يَوْمُ الْجُمُعَةِ، فِيهِ خُلِقَ آدَمُ وَفِيهِ قُبُورُ، وَفِيهِ النَّهْجُ، وَفِيهِ الصُّعْقَةُ، فَأَكْثِرُوا عَلَيَّ مِنَ الصَّلَاةِ فِيهِ، فَإِنَّ صَلَاتَكُمْ مَعْرُوضَةٌ عَلَيَّ»

“Miongoni mwa siku zenu bora kabisa ni siku ya Ijumaa. Katika siku hiyo aliumbwa Adam na alikufa. Ndiyo siku ambayo parapanda (Sur) litapulizwa, kisha kila kitu kitazimia. Basi kithirisheni kuniswalia katika siku hii, kwani Sala yenu itaoneshwa kwangu.”

Wakasema: “Ewe Mtume ﷺ! Utaletewa vipi, ilhali mwili wako utakuwa umeshamung’unyuka?” Akasema:

«إِنَّ اللَّهَ حَرَّمَ عَلَى الْأَرْضِ أَنْ تَأْكُلَ أَجْسَادَ الْأَنْبِيَاءِ»

“Hakika Allah Aliiharamisha ardhi kula miili ya Manabii.”

Ameinukuu Abu Dawud, An-Nasai na Ibn Majah. Abu Khuzaymah, Ibn Hibban na Ad-Daraqutni waliweka katika daraja la *Sahih*. Na Annawawi katika kitabu cha Adhkaary, na Al-Hasani Al-Basri رحمه الله تعالى anasema, “Mtume ﷺ amesema, “Moto hauwezi kuunguza mwili uliosemeshwa na Malaika Jibril.” Hadithi ina daraja ya Mursal Hasan.

Ukimswalia Mtume popote pale ulipo Sala humfikia. Imepokewa kutoka kwa Ali bin Husein bin Ali ya kuwa Mtu mmoja kila mchana hulifanyia ziara kaburi la Mtume ﷺ na kumswalia. Na hufanya hivyo hadi akawa Ali bin Husein amemzoea. Hivyo Ali bin Husein akamuambia: “Ni kwanini unafanya hivi?” Yule Mtu akasema: ‘Ninapenda kumtolea salamu Mtume ﷺ.’ Ali bin Husein akamuambia: “Je, nikujulishe maneno aliyosema baba yangu?” Yule mtu

¹ Ahmad 1:199, Abu Dawud 2:133, Tuhfatul Al-Ahwadhi 2:562, An-Nasai 3:248, Ibn Majah 1:372, Ibn Khuzaymah 2:151, Ibn Hibban 2:148, Al-Hakim 3:172

akasema: "Ndio." Ali bin Husein akamuambia amenihadithia baba yangu kutoka kwa babu yangu kwamba yeye amesema: Mtume ﷺ amesema: "Msiifanye kaburi yangu ni Sikukuu, na wala majumba yenu msiyafanye kuwa kaburi, na mniswalie na mnisalimie popote pale mlipo. Hivyo Swala na Salamu zitanifikia popote pale nilipo." Katika (Isnad) ya Hadithi hii kuna Mtu asiyejulikana ambaye hakutajwa jina. Hadithi imepokewa kwa njia (Isnad) nyingine kwa muundo wa *Mursal*. Na kutokana na Ali bin Husein imepokewa Hadithi ya kuwa yeye alimuona Mtu mmoja akiendea kaburi, akasema, "Ewe unayefanya hili, huna tofauti wewe na mtu aliyekuwa Hispania, "Andalusi" katika hili mpo sawa." Kwa maana nyote Sala zenu zinamfikia yeye Mtume ﷺ siku zote hadi siku ya Kiama. Na imepokelewa Hadithi kutoka kwa Abdillah bin Masudi رضي الله عنه ya kuwa Mtume ﷺ amesema: "Hakika Allah تعالی Ana Malaika wanatangatanga katika ardhi, hunifikishia mimi Salamu za umati wangu."

Na Qadhi amepokea kutoka kwa Umar bin Khattabi رضي الله عنه anasema: "Pindi mnapofika Makka fanyeni Twawafu - kuzunguka Kaaba mara saba, na mswali karibu na *Maqaam* Ibrahim rakaa mbili, kisha nendeni Safa msimame kiasi ambacho mtaiona Kaaba, Mlete takbira saba, takbira baina ya kumhimidi Allah تعالی na kumsifia Yeye, na kumswalia Mtume ﷺ. Na kutaja shida yako." Na Isnadi ya Hadithi hii ni nzuri (Hasan) na yenye nguvu.

Jopo la wanazuoni wamesema: "Hairuhusiwi kuwahusisha watu wengine wasiokuwa Mitume kwa kuwaswalia. Kwa sababu huu ni utambulisho mahususi kwa Mitume tu pindi wanapotajwa. Hivyo hairuhusiwi kuwahusisha watu wengine. Hivyo **haisemwi**: Abubakar ﷺ au Ali ﷺ ijapo kuwa maana ni sahihi kama ambavyo **haisemwi**, "Muhammad *Azza Wajallah*" - ijapokuwa Muhammad ni mtu Mtukufu. Kwa sababu utambulisho huu ni kwa ajili ya utajo wa Allah تعالی. Na matamko yanayokuja kueleza hivyo katika Qur'an na Hadithi wanazuoni wameyatafsiri kuwa ni kuwaombea wao dua. Na Mtazamu huu ni Mzuri.

Na Sheikhe Abuu Zakaria Annawawi رحمه الله تعالی amesema katika kitabu cha (*Adhkaar*). Na kauli sahihi ambayo wanazuoni wengi wanaifuata ni kwamba kufanya hivyo ni makuruhu inayokurubia katika uharamu. Na jambo makuruhu ni lile ambalo limekatazwa kwa kukusudiwa. Na Jafar bin Bargali amesema: Umar bin Abdul-Azizi رحمه الله تعالی ameandika "Ama baada ya utangulizi, hakika watu miongoni mwao wameitafuta dunia kwa matendo ya Akhera, na hakika miongoni mwa wasimulizi wa Visa, wamezusha jambo jipya kuwaswalia

viongozi na watawala wao, kwa kulinganisha na kumswalia Mtume ﷺ. Pindi utakapoipokea barua yangu hii, waamrishe wawaswalie Mitume na wawaombe dua waislamu wote. Na waachane na utaratibu usiokuwa huo. Hii ni athari Hasan.

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿٥٧﴾
وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بَغَيْرِ مَا كَتَبْنَا فَكُفِّرُوا بَعْثْنَا لَهُمْ جَنْدًا أَكْثَرًا ﴿٥٨﴾

57.“*Hakika wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, Mwenyezi Mungu Amewalaani duniani na Akhera, na Amewaandalia adhabu ya ifedheheshayo.*”

58.“*Na wale wanaowaudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri.*”

Mwenye Kumuudhi Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ Amelaaniwa Duniani na Akhera

Allah تعالى Anawaonya na Kuwakemea wanaomuudhi kwa kuzikhalifu amri Zake na kufanya Aliyoyakataza na kuendelea kwake katika hali hiyo, na kumsumbua Mtume Wake kwa kumsingizia kuwa na aibu na upungufu – Allah تعالى Atukinge dhidi ya hilo. ‘Ikrimah alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Hakika wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake...”

Iliteremshwa kuwahuu wanaofanya picha au kuchonga masanamu.¹ Katika Sahih Mbili kuna Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: يُؤْذِنِي ابْنُ آدَمَ، يَسُبُّ الدَّهْرَ وَأَنَا الدَّهْرُ أَقْلَبُ لَيْلَهُ وَنَهَارَهُ»

“Allah Anasema, ‘Mwanadamu Ananiudhi, Anaitukana dahari, lakini Mimi ni dahari, Nabadilisha usiku wake na mchana wake.’²

¹ At-Tabari 20:322.

² Fat’h Al-Bari 8:437, Muslim 4:1762.

Maana ya Hadithi hii, ni kwamba, majahili walikuwa wakisema: “Dahari ni mbaya mno, imetufanyia jambo kadha wa kadha. Walikuwa wakiyanasibisha mambo Ayafanyayo Allah تعالى na dahari. Ukweli ni kwamba, ayafanyayo hayo ni Allah تعالى, kwa hivyo Aliyakataza hayo. Al-'Awfi alisema kwa mujibu wa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ يُؤْذُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Hakika wanaomuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake...”

Iliteremshwa kuhusu waliomkashifu Mtume ﷺ kuhusu kumuoa Swafiyah bint Huyay bin Akhtab رضي الله عنها.¹

Lililo dhahiri ni kwamba, Aya inajumuisha kila mwenye kumuudhi kwa jambo lolote, na atakayefanya hivyo atakuwa Amemuudhi Allah تعالى, sawa na kwamba mwenye kumtii, basi anakuwa amemtii Allah تعالى.

Kemeo kwa Wazushi

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ بِغَيْرِ مَا اكْتَسَبُوا

“Na wale wanaowaudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote...”

Yaani, wanawanasibishia waumini wanaume au wanawake mambo ambayo hawakuyafanya,

فَقَدْ أَحْتَمَلُوا بُهْتَنَا وَإِنَّمَا مُبِينًا

“...bila ya shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zililo dhaahiri.”

Huu ni uzushi mkubwa, kueleza au kuhamisha toka kwa Waumini wanaume na wanawake, ambayo hawakuyatenda, kwa njia ya kuwatia kasoro na upungufu. Wanaoingia wengi wao katika karipio hili ni wanaomkufuru Allah na Mtume Wake, kisha, *Ar-Rafidhwah* (Mashia), ambao wanawatia ila na aibu masahaba kwa mambo ambayo Allah تعالى Ameshaeleza kwamba hawana

¹ At-Tabari 20:323.

makosa, na wanawaelezea wasifu wao kinyume na vile Alivyosema Allah تعالى. Allah تعالى Ameshaeleza kwamba Yeye Alikwishawaridhia Muhajirina na Ansvar na Akawasifu, lakini majahili hawa, na mazuzu hawa wanawatukana na kuwatia ila na wanawasingizia mambo ambayo hawayafanyi wala hawakuyafanya. Basi, wao kwa uhakika, ni wenye nyoyo zilizopotoka, kwa sababu wanawalaumu wanaostahiki kusifiwa na wanawasifu wanaopaswa kulaumiwa. Abu Dawud alinukuu kuwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنهما alisema, kulisemwa: “Ewe Mtume wa Allah! Ni nini kusengenywa?” Akasema:

«ذِكْرُكَ أَخَاكَ بِمَا يَكْرَهُ»

“Ni pale unapomtaja nduguyo kwa jambo linalomkera.”

Akasema: “Ni vipi ikiwa haya ninayoyasema kumhusu ndugu yangu, ikiwa ni ya kweli?” Akasema:

«إِنْ كَانَ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ اغْتَبْتَهُ، وَإِنْ لَمْ يَكُنْ فِيهِ مَا تَقُولُ فَقَدْ بَهْتَهُ»

“Ikiwa anayo unayoyasema, basi utakuwa umemsengenywa, na ikiwa hana unayoyasema, basi utakuwa umemzushia.”¹

Hadithi hii pia, ilinukuliwa na At-Tirmidhi, ambaye alisema ni: “*Hasan Sahih*.”²

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلٌّ لِأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلْبَابٍ مِّنْ ذَٰلِكَ
 أَدْنَىٰ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذِينَ ۗ وَكَرِهَ اللَّهُ عَفْوَراً رَّحِيماً ﴿٥٥﴾ لِّئِن لَّمْ يَنْتَهِ الْمُؤْمِنُونَ
 وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ وَالْمُرْجِفُونَ فِي الْمَدِينَةِ لَنُغْرِبَنَّكَ بِهِمْ ثُمَّ لَا يُجَاوِرُونَكَ
 فِيهَا إِلَّا قَلِيلاً ﴿٥٦﴾ مَلْعُونِينَ ۗ أَيُّهَا تُقْفُوا أَجْدُوا وَقْتَلُوا تَقْتِيلًا ﴿٥٧﴾ سُنَّةَ اللَّهِ فِي
 الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلُ ۗ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ﴿٥٨﴾

59. “Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wanawake Waumini wajiteremshie mwili wote nguo zao. Hivyo kutapelekea upesi kutambulikana na wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.”

¹ Abu Dawud 5:192.

² Muslim na. 2589, Tuhfatul Al-Ahwadhi 6:63.

60. "Kama wanaafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao, na waenezao fitna katika Madina hawatoacha, basi kwa yakini Tutakusalitisha juu yao, kisha hawatakaa humo karibu yako ila muda mchache tu."

61. "Wamelaanika! Popote waonekanapo wakamatwe na wauliwe kabisa."

62. "Hii ni ada ya Mwenyezi Mungu iliyokuwa kwa wale waliopita zamani. Wala hutapata mabadiliko katika ada ya Mwenyezi Mungu."

Amri ya Hijabu

Allah تعالی Anamuamuru Mtume Wake ﷺ kuwa awaamuru Wanawake wa Waumini – khususan wakeze na mabinti zake - kwa sababu ya nafasi yao ya heshima – wajiteremshie *Jilbab* zao katika miili yao ili wawe mfano bora kwa wanawake wa kijahili na wajakazi. *Jilbab* ni nguo inayovaliwa juu ya mtandio. Hayo aliyasema Ibn Mas'ud, 'Ubaydah, Qatadah, Al-Hasan Al-Basri, Sa'id bin Jubayr, Ibrahim An-Nakha'i, 'Atwaa Al-Khurasani na wengine. Ni kama *Izar* itumikayo siku hizi. Al-Jauhari alisema: "Ni nguo ya kujitanda kwa juu." Ali bin Abu Twalhah alisema: "Allah تعالی Aliwaamuru wanawake wa Waumini, pindi wanapotoka majumbani mwao kwa ajili ya haja, wajifunike nyuso zao, kutoka juu ya vichwa vyao kwa kutumia *Jilbab*, na kuacha wazi jicho moja."¹ Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالی alisema: "Nilimuuliza 'Ubaydah As-Salmani kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

يُدَيْنَنَّ عَلَيْنَّ مِنْ جَلْبَابِهِنَّ^٤

"...wajiteremshie nguo zao."

Akaufunika uso na kichwa chake, na kuliacha jicho moja tu la kushoto."² Kauli ya Allah تعالی:

ذَلِكَ أَذَىٰ أَنْ يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَنَنَّ^٥

"Hivyo ni karibu zaidi kuweza kutambulikana wasiudhiwe."

¹ At-Tabari 20:324.

² At-Tabari 20:325.

Yaani, wakifanya hivyo, watajulikana kwamba wao ni waungwana, si wajakazi wala makahaba. Kauli ya Allah تعالى:

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Yaani, kwa yaliyopita katika wakati wa ujahili, walipokuwa hawalijui hili.

Angalizo na Onyo Kali kwa Wanafiki Waovu

Kisha, Allah تعالى Aliwaonya wanafiki, ambao ni watu wanaodhihirisha Imani na kuuficha ukafiri wao,

وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ

“...na wale wenye maradhi nyoyoni mwao...”

‘Ikrimah na wengine walisema kuwa, hapa inarejea kwa wazunifu.¹

وَالْمُرْجُفُونَ فِي الْمَدِينَةِ

“...na waenezao fitna katika Madina...”

Yaani, wanaosema kuwa maadui wamekuja na vita vimeanza, hali ya kuwa ni uongo na uzushi. Iwapo hawatakoma kufanya hayo na kurejea kwenye ukweli,

لَنُغْرِبَنَّكَ بِهِمْ

“...basi kwa yakini Tutakusalitisha juu yao...”

‘Ali bin Abu Twalhah alisema kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Tutakupa nguvu juu yao.”²

Qatadah alisema: “Tutakupa ushawishi dhidi yao.”³ Assudi alisema: “Tutakupa habari zao.”

¹ At-Tabari 20:326.

² At-Tabari 20:328.

³ At-Tabari 20:328.

ثُمَّ لَا تَجَاوَزُونَكَ فِيهَا

“...kisha hawatakaa humo karibu yako...”

Yaani Madinah,

إِلَّا قَلِيلًا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ

“...ila muda mchache tu. Wamelaanika!

Muda mchache tu ulipita katika kukaa kwao Madinah, wakiwa katika kufukuzwa na kupelekwa mbali,

أَيَّمَا تُفَفُّوْا أُخِذُوا

“Popote watakapoonekana watakatwa...”

Yaani, watashambuliwa. Kwa sababu ya udhalili na uchache wao,

وَقُتِلُوا تَقْتِيلًا

“...na watauliwa kabisa.”

Kisha, Allah تعالی Akasema:

سُنَّةَ اللَّهِ فِي الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلُ

“Hii ni ada ya Mwenyezi Mungu iliyo kuwa kwa wale waliopita zamani.”

Yaani, hiyo ni kanuni ya Allah تعالی kwa wanafiki, wanapokaidi juu ya unafiki na ukafiri wao bila ya kuyaacha waliyo nayo. Wenye Imani watakuwa ni wenye nguvu zaidi yao na kuwashinda.

وَلَن نَّجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا

“Wala hutapata mabadiliko katika ada ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, utaratibu huo wa Allah تعالی haubadilishwi wala hauguzwi.

* * *

يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ ۗ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللَّهِ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴿٦٣﴾ إِنَّ اللَّهَ لَعَنَ الْكٰفِرِينَ وَأَعَدَّ لَهُمْ سَعِيرًا ﴿٦٤﴾ خٰلِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ لَا يَجِدُونَ وِلْيًا وَلَا نَصِيرًا ﴿٦٥﴾ يَوْمَ تَقَلَّبَ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يٰلَيْتَنَا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَ ﴿٦٦﴾ وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبْرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلًا ﴿٦٧﴾ رَبَّنَا آتِنَا مِنَّا مِنْ أَلْعَابِ الْعَذَابِ ۗ وَالْعَنِيمُ لَعْنَا كَبِيرًا ﴿٦٨﴾ يٰأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ ءَادَوْا مُوسَىٰ فَبَرَأَهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا ۗ وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِيهًا ﴿٦٩﴾ يٰأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَن يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدِ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾ إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَن تَحْمِلَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا الْإِنسَانُ ۗ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٢﴾ لِيُعَذِّبَ اللَّهُ الْمُنٰفِقِينَ وَالْمُنٰفِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٧٣﴾

يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ ۗ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللَّهِ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴿٦٣﴾ إِنَّ اللَّهَ لَعَنَ الْكٰفِرِينَ وَأَعَدَّ لَهُمْ سَعِيرًا ﴿٦٤﴾ خٰلِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ لَا يَجِدُونَ وِلْيًا وَلَا نَصِيرًا ﴿٦٥﴾ يَوْمَ تَقَلَّبَ وُجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يٰلَيْتَنَا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَ ﴿٦٦﴾ وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبْرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلًا ﴿٦٧﴾ رَبَّنَا آتِنَا مِنَّا مِنْ أَلْعَابِ الْعَذَابِ ۗ وَالْعَنِيمُ لَعْنَا كَبِيرًا ﴿٦٨﴾

63. "Watu wanakuuliza habari ya Saa (ya Kiyama). Sema: Ujuzi wake uko kwa Mwenyezi Mungu. Na nini kitakujuvya? Pengine hiyo Saa iko karibu."

64. "Hakika Mwenyezi Mungu Amewalaani makafiri

na Amewaandalia Moto unaowaka kwa nguvu."

65. "Watadumu humo milele. Hawatapata mlinzi wala wa kuwanusuru."

66. "Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungelimtii Mwenyezi Mungu, na Tungelimtii Mtume!"

67. "Na watasema: Mola Wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia."

68. "Mola Wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili, na uwalaani laana kubwa."

Hapana Yeyote Aijuaye Siku ya Kiyama, Isipokuwa Allah تعالى.

Allah تعالى Anamjulisha Mtume Wake ﷺ kwamba yeye hana ujuzi wa Saa, hata kama watu watamuuliza juu ya hilo, na akamuelekeza kujibu ya kuwa ujuzi wa jambo hilo upo kwa Allah تعالى.

Sawa na Alivyosema Allah تعالى katika *Surat Al-A'raaf* ambayo iliteremshwa Makkah, na hii Madinah. Jibu la swali hilo, likaendelea kubaki kwa Allah تعالى Ambaye Ndiye Atakayekileta. Lakini uwajulishe kwamba imekaribia.

Ni kwa Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا

"Na nini kitakujavya? Pengine hiyo Saa iko karibu."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَفَتَرَبَّ السَّاعَةَ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿١٠﴾

"Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!" (54:1)

أَفَتَرَبَّ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿٢١﴾

"Imewakaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuuza." (21:1)

أَتَىٰ أَمْرٌ مِّنَ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ

"Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize." (16:1)

Kulaaniwa Makafiri, Kukaa kwao Motoni Milele na Kujuta Kwao

Kisha, Allah تعالى Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَعَنَ الْكٰفِرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amewalaani makafiri...”

Yaani, Hatawarehemu,

وَأَعَدَّ لَهُمْ سَعِيرًا

“...na Amewaandalia Moto unaowaka kwa nguvu.”

Yaani, Akhera,

خٰلِدِينَ فِيهَا أَبَدًا

“Wataidumu humo milele.”

Yaani, watakaa kwa kuendelea bila kutoka wala kuondoka, Kisha, Amesema:

لَا يَجِدُونَ وِلِيًّا وَلَا نَصِيرًا

“Hawampati mlinzi wala wa kuwanusuru.”

Yaani, hawatakuwa na wa kuwaokoa wala wa kuwasaidia kwa ajili ya kuwatoa katika hali wanazuoni.

يَوْمَ تَقُفُّ أْجُوهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُولُونَ يَا لَيْتَنَّا أَطَعْنَا اللَّهَ وَأَطَعْنَا الرَّسُولَ ﴿٦٣﴾

“Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa pinduliwa katika Moto. Watasema: Laiti tungelimtii Mwenyezi Mungu, na tungelimtii Mtume!”

Yaani, wataburuzwa Motoni kwa nyuso zao ambazo zitakunjwa kunjwa katika Jahanamu. Watasema, ilhali wakiwa katika hali hiyo wakitamani, kwamba lau kama wangelikuwa duniani na kuwa miongoni mwa waliomtii Allah na Mtume Wake. Ni sawa na Alivyoieleza Allah تعالى kuhusu hali zao:

وَيَوْمَ يَعْصُ الظَّالِمُ عَلَى يَدَيْهِ يَقُولُ يَا لَيْتَنِي اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَبِيلًا ﴿٦٤﴾ يَا وَيْلَتَى

لَيْتَنِي لَمْ أَتَّخِذْ فُلَانًا خَلِيلًا ﴿٦٥﴾ لَقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذْ جَاءَنِي ۗ وَكَانَ

الشَّيْطٰنُ لِلْإِنْسٰنِ خَدُوْلًا ﴿٦٦﴾

“Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajijuma mikono yake, na huku anasema: Laiti ningelishika njia pamoja na Mtume! Ee Ole wangu! Laiti nisingelimfanya fulani kuwa rafiki! Amenipoteza, nikaacha Ukumbusho, baada ya kwisha njia, na kweli Shetani ni mwenye kukimbia mbali mwanadamu wakati anapomhitaji.”
(25:27-29)

رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿٢٧﴾

“Huenda ikawa waliokufuru wakatamani wangukuwa Waislamu.”
(15:2)

Kadhalika alitoa khabari zao kwamba wakiwa katika hali yao hii, watatamani lau wangelikuwa wamemtii Allah تعالى na Mtume Wake duniani,

وَقَالُوا رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبْرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلًا ﴿٢٨﴾

“Na watasema: Mola Wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia.”

Twawus alisema kuwa maana ya “bwana zetu” ni wakuu na “wakubwa wetu” ni wanazuoni.

رَبَّنَا ءَاتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ

“Mola Wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili...”

Yaani, kwa ukafiri wao na kwa kutupoteza sisi. Abu Al-Qasim At-Tabarani alimnukuu Rafi' katika kuyataja majina ya waliopigana pamoja na 'Ali رضي الله عنه, alikuwemo Al-Hajjaj bin 'Amri bin Ghaziyah, ambaye ni mmojawapo kati ya waliokuwa wakisema pindi walipokutana: “Enyi kundi la Answar! Je mnataka mseme kwa Mola Wetu pindi tutakapokutana Naye:

رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبْرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلًا ﴿٢٩﴾ رَبَّنَا ءَاتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ
وَالْعَذَابُ لَعَنًا كَبِيرًا ﴿٣٠﴾

“Mola Wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia. Mola Wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili, na Uwalaani laana kubwa.”

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ ءَادَوْا مُوسَىٰ فَبَرَّاهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ

وَجِبَاهًا ﴿٦٩﴾

69. "Enyi mlio amini! Msiwe kama wale waliomtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu Akamtakasa na waliyoyasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu."

Uzushi wa Wayahudi dhidi ya Nabii Musa عليه السلام

Al-Bukhari amenukuu katika Kitabu cha Hadithi habari za Mitume, kwamba Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ, amesema:

«إِنَّ مُوسَىٰ عَلَيْهِ السَّلَامُ كَانَ رَجُلًا حَيًّا سَيِّرًا لَا يُرَىٰ مِنْ جِلْدِهِ شَيْءٌ اسْتِخْيَاءً مِنْهُ، فَآذَاهُ مَنْ آذَاهُ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ فَقَالُوا: مَا يَسْتَرُ هَذَا التَّسْتُرُ إِلَّا مِنْ عَيْبٍ فِي جِلْدِهِ إِمَّا بَرَصٌ وَإِمَّا أُذْرَةٌ وَإِمَّا آتَةٌ. وَإِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ أَرَادَ أَنْ يُبْرِئَهُ مِمَّا قَالُوا لِمُوسَىٰ عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَخَلَا يَوْمًا وَحَدَهُ فَخَلَعَ ثِيَابَهُ عَلَىٰ حَجَرٍ ثُمَّ اغْتَسَلَ، فَلَمَّا فَرَغَ أَقْبَلَ إِلَىٰ ثِيَابِهِ لِيَأْخُذَهَا، وَإِنَّ الْحَجَرَ عَدَا بِثَوْبِهِ فَأَخَذَ مُوسَىٰ عَصَاهُ وَطَلَبَ الْحَجَرَ فَجَعَلَ يَقُولُ: تَوْبِي حَجْرٌ، تَوْبِي حَجْرٌ، حَتَّىٰ انْتَهَىٰ إِلَىٰ مَلَأٍ مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ، فَرَأَوْهُ عُرْيَانًا أَحْسَنَ مَا خَلَقَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ، وَأَبْرَاهُ مِمَّا يَقُولُونَ، وَقَامَ الْحَجْرُ، فَأَخَذَ ثَوْبَهُ فَلَبَسَهُ، وَطَفِقَ بِالْحَجَرِ ضَرْبًا بِعَصَاهُ، فَوَاللَّهِ إِنْ بِالْحَجَرِ لَنَدَبًا مِنْ أَثَرِ ضَرْبِهِ ثَلَاثًا أَوْ أَرْبَعًا أَوْ خَمْسًا - قَالَ: - فَذَلِكَ قَوْلُهُ تَعَالَىٰ: ﴿يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ ءَادَوْا مُوسَىٰ فَبَرَّاهُ اللَّهُ مِمَّا قَالُوا وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِبَاهًا﴾ ﴿٦٩﴾»

"Musa عليه السلام alikuwa mwenye haya na staha hakuonekana sehemu yoyote ya ngozi yake kwa sababu ya haya yake. Baadhi ya Waesraili wakamchokoza kwa kusema, '(Musa) hazui ngozi yake kwa kiasi hicho isipokuwa ni kwa sababu ya dosari katika ngozi yake kutokana na ugonjwa wa mbalanga au busha au ugonjwa mwingine.' Allah Akataka kumsafisha Musa عليه السلام dhidi ya madai yao. Siku moja, Musa عليه السلام alienda faragha peke yake, akavua nguo zake na kuziweka juu ya jiwwe halafu akaoga. Alipomaliza alielekea kuchukua nguo zake, lakini jiwwe lilichukua nguo zake na kuzificha, akachukua fimbo yake na akataka jiwwe litoe nguo zake huku akisema, "Nguo

zangu, ewe Jiwe, nguo zangu, ewe Jiwe! Mpaka akalifikia kundi la Bani Israel ambao walimuona akiwa uchi na kugundua kuwa (Musa) alikuwa mbora zaidi katika Aliowaumba Allah. Hivyo akasafishwa dhidi ya madai yao. Jiwe likatoa nguo zake palepale. Akachukua nguo zake na kuvaa. Akaanza kulipiga Jiwe hilo na kuacha alama kama tatu au nne au tano hivi. Hicho ndicho kinachokusudiwa katika Ayah, **“Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliomtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu Akamtakasa na waliyoyasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.”**

Hadithi hii ni katika zilionukuliwa na Al-Bukhari, lakini si Muslim.

Imamu Ahmad amemnukuu ‘Abdullah Ibn Mas‘ud رضى الله عنه kuwa alisema: “Siku moja, Mtume ﷺ aligawa ngawira. Akasema mtu mmoja katika Ansvar: ‘Ugawaji huu haukufanyika kwa ajili ya kutaka radhi za Allah تعالى.’ Nikasema, ‘Ewe adui wa Allah! Hakika, nitamjulisha Mtume ﷺ kuhusu uliyoyasema.’ Nikamtajia hayo Mtume ﷺ, uso wake ukawa mwekundu. Kisha akasema,

رَحْمَةُ اللَّهِ عَلَىٰ مُوسَىٰ لَقَدْ أُوذِيَ بِأَثَرٍ مِنْ هَذَا فَصَبَرَ

“Rehema ya Allah iwe juu ya Musa, aliudhiwa zaidi ya hili, na akasubiri.”

Imenukuliwa katika *Sahih Mbili*.¹

Kauli ya Allah تعالى:

وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِيهًا

“...naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, alikuwa na hadhi na heshima mbele ya Mola Wake. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Alikuwa ni mwenye kujibiwa dua mbele ya Allah تعالى.”²

Baadhi yao walisema, Miongoni mwa hadhi zake kubwa mbele ya Allah تعالى ni kuomba kwa ajili ya nduguye, Harun عليه السلام, Allah تعالى Amtume pamoja naye kama Mtume. Allah تعالى Akamjibu ombi lake, Akasema:

¹ Ahmad 1:380, Bukhari na. 3405, Muslim na. 1062.

² Al-Baghawi 3:545.

وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيًّا ﴿٥٣﴾

“Nasi kwa Rehema Zetu Tukampa nduguye, Harun, awe Nabii.”
(19:53)

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَقَوْلُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُضِلُّحَ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرَ لَكُمْ
ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

70. “Enyi mliaamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na semeni maneno ya sawasawa.”

71. “Apate Kukutengenezeeni vitendo vyenu na Akusameheni madhambi yenu. Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.”

Waumini Waamrisha Uchamungu na Ukweli

Allah تعالى Anawaamuru waja Wake Waumini kwamba wamche Yeye na wamuabudu kana kwamba wanamuona, na waseme:

قَوْلًا سَدِيدًا

“...maneno ya sawasawa.”

Yaani, yaliyonyooka. Allah تعالى Amewaahidi kwamba wakiyafanya hayo, Atawalipa kwa hayo: kwa Kuwatengenezea matendo. Yaani, Kuwawezesha kutenda amali njema, na Kuwasamehe madhambi yaliyopita. Kuhusu madhambi watakayoyafanya kwa siku za mbele, Atawafunulia kufanya toba kutokana nayo. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

“Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.”

Maana yake ni kwamba, Atamuepusha dhidi ya Moto wa Jahanamu na atakuwa katika neema ya kudumu.

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ تَحْمِلَهَا وَأَشْفَقْنَ مِنْهَا
 وَحَمَلَهَا الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا ﴿٧٢﴾ لِيُعَذِّبَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ
 وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا
 رَحِيمًا ﴿٧٣﴾

72. “Kwa hakika Sisi Tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhalimu mjinga.”

73. “Kwa hivyo Mwenyezi Mungu Anawaadhibu wanaafiki wanaume, na wanaafiki wanawake, na washirikina wanaume, na washirikina wanawake; na Anawapokelea toba Waumini wanaume, na Waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.”

Namna Mwanaadamu Alivyochukua Amana

Awfi amesema toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: “Maana ya *Al-Amana* ni utii. Mbingu, Ardhi na Majabali vilibebeshwa tangu hapo zamani, na hazikuweza kuihimili. Allah تعالى Akamuambia Adam عليه السلام, “Kwa hakika Sisi Tulizibebesha amana mbingu, ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Je, utaipokea wewe?” Akauliza, “Mola Wangu! Ina mambo gani?’ Akamuambia, ‘Kama utatenda wema utalipwa, na kama utatenda shari, utaadhibiwa.’ Adamu عليه السلام akachukua amana. Hiyo ndiyo maana inayokusudiwa katika Aya:

وَحَمَلَهَا الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا

“Lakini mwanadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhalimu mjinga.”¹

Ali bin Abi Twalha amesema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Maana ya *Al-Amanah* ni *Al-Faraidh* (mambo Aliyofaradhisha Allah). Allah تعالى Alizionesha

¹ At-Tabari 20:338.

mbingu, ardhi na milima kuwa wakiitekeleza Atawapa thawabu na wakiipoteza Atawaadhibu, hazikuwa tayari kufanya hayo, wakaiogopa, si kwamba makusudio yao yalikuwa ni kuasi, bali kwa kuadhimisha Dini ya Allah تعالى kama hawatatimiza wajibu wao. Allah تعالى Akamuonesha Adamu عليه السلام naye akaichukua. Hayo ndio makusudio ya Aya:

وَحَمَلَهَا إِلَىٰ نَسْنِ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا

“Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.”

Yaani, hakuipa uzito Amri ya Allah تعالى.¹

Hiyo pia ilikuwa rai ya Mujahid, Sa'id bin Jubayr, Adh-Dhahhak, Al-Hasan Al-Basri na wengine kuwa maana ya *Al-Amanah* ni *Al-Faraidh*.² Wengine walisema kuwa maana yake ni utii. Al-A'mash amesimulia kutoka kwa Abu Adh-Dhuha, kutoka kwa Masruq kuwa Ubay bin Ka'b رضي الله عنه alisema: “Ni Sehemu ya *Al-Amanah* kuwa mwanamke aliaminiwa kulinda ubikra wake.”³ Qatadah alisema, “Maana ya *Al-Amanah* ni Dini, mambo ya faradhi na adhabu zilizowekwa.”⁴

Malik alisimulia kuwa Zayd bin Aslam alisema: Maana ya “*Al-Amanah* ni mambo matatu: Sala, Swaumu na Kuoga ili kujitwaharisha dhidi ya janaba.”

Huu si mkanganyiko kati ya rai hizo, zote zinawafikiana na zinaonesha uwajibikaji na hali ya kukubali amri, makatazo na masharti ambatano, ambapo, anayetimiza wajibu, atalipwa, na mwenye kupuuzia ataadhibiwa. Mwanadamu akayakubali hayo licha ya udhaifu wake, ujinga na udhalimu wake - isipokuwa yule aliyewafikishwa na Allah تعالى, na Allah تعالى ni Mmoja, na Ndiye Tunayemuomba msaada Wake.

Na katika yanayohusiana na Amana ni Hadithi ambayo ameipokea Imamu Ahmad kutoka kwa Hudhaifa رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ alitusimulia sisi simulizi mbili, moja tayari nimeshaishuhudia na nangojea nyingine, Mtume

¹ At-Tabari 20:337.

² At-Tabari 20:337.

³ At-Tabari 20:338.

⁴ At-Tabari 20:339.

ﷺ ametusimulia kwamba Amana ilishuka katika shina la nyoyo za wanaume kisha ikashuka Qur'an, hivyo wakajua katika Qur'an na wakajua katika Sunna (Hadithi). Kisha akatusimulia kuhusu kuondoshwa kwa Amana, akasema:

«يَنَامُ الرَّجُلُ التَّوَمَةَ فَتُبْضُ الْأَمَانَةُ مِنْ قَلْبِهِ، فَيَطْلُ أَنْزَهَا مِثْلَ أَنْزِرِ الْمَجْلِي كَجَمْرِ دَخَرَجْتَهُ عَلَى رِجْلِكَ، تَرَاهُ مُتَبِيرًا وَلَيْسَ فِيهِ شَيْءٌ».

“Mtu analala usingizi, halafu amana itaondolewa moyoni mwake, na athari yake ikawa kama ya lengelenge lililoachwa na makaa ya mawe yaliyobingirishwa juu ya mguu wako, utaiona ikijitokeza huku ikiwa haina kitu ndani yake.”

Halafu akachukua changarawe moja na kuiviringa juu ya mguu wake, akasema:

«فَيُضِجُ النَّاسُ يَتَّبِعُونَ لَا يَكَادُ أَحَدٌ يُؤَدِّي الْأَمَانَةَ حَتَّى يُقَالَ: إِنَّ فِي بَنِي فُلَانٍ رَجُلًا أَيْمَانًا، حَتَّى يُقَالَ لِلرَّجُلِ مَا أَجْلَدَهُ وَأَطْرَفَهُ وَأَغْقَلَهُ! وَمَا فِي قَلْبِهِ حَبَّةٌ خَرْدَلٍ مِنْ إِيْمَانٍ»

“Kisha, watu wataanza kununua na kuuza, na vigumu kwa mmoja wao kutekeleza amana, mpaka kutasemwa: ‘Katika kabila fulani kuna mtu mwaminifu, na kutasemwa, namna gani alivyo na nguvu, mzuri na mwenye akili, ilhali hana imani hata chembe ya khardali moyoni mwake.”

Bila ya shaka, ulifika wakati ambapo sikujali kujishughulisha (kufanya mapatano) na yeyote kati yenu, kwani kama alikuwa Muislamu, basi Uislamu wake ungemsumkia kwenye kunilipa haki yangu, na kama alikuwa Mkristo au Myahudi, basi afisa Muislamu atamshurutisha anilipe haki yangu, lakini leo, sijishughulishi isipokuwa na mtu fulani tu kati yenu.¹

Pia imenukuliwa katika *Sahih* Mbili kutokana na Hadithi ya Al-A'mash.²

Imam Ahmad amenukuu kwamba 'Abdallah bin 'Amr رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

¹ Ahmad 5:383.

² Fat'h Al-Bari 11:341, Muslim 1:126.

«أَزْبِجْ إِذَا كُنَّ فِيكَ فَلَا عَلَيْكَ مَا فَاتَكَ مِنَ الدُّنْيَا: حِفْظُ أَمَانَةٍ، وَصِدْقُ حَدِيثٍ،
وَحُسْنُ خَلِيقَةٍ، وَعِنَّةُ طُعْمَةٍ»

“Mambo manne yakiwemo kwako, basi chochote utakachokikosa duniani kitakuwa hakina haja: kuhifadhi amana, mazungumzo ya kweli, tabia njema na ulaji wa wastani.”¹

Matokeo ya Kuichukua Amana

Kauli yake Allah تعالى:

لِيُعَذِّبَ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ

“Kwa hivyo Mwenyezi Mungu Anawaadhibu wanafiki wanaume, na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume, na washirikina wanawake...”

Yaani, kwa sababu wanadamu wamechukua amana na kuahidi kuitekeleza, ambayo ni majukumu wanayopaswa kuyatekeleza, Allah تعالى Atawaadhibu wanaume na wanawake walio wanafiki ambao hudhihirisha imani ya uongo wakijionesha tu kwa sababu ya kuwaogopa waumini, lakini wameficha ukafiri mioyoni mwao, na kwa hakika wao ni wafuasi wa makafiri

وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ

“...na washirikina wanaume, na washirikina wanawake...”

Hao ni wale ambao kwa siri na hadharani humshirikisha Allah تعالى na kuwakiuka Mitume,

وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ²

“...na Anawapokelea toba Waumini wanaume, na Waumini wanawake.”

Yaani, Atawarehemu waumini wenye kumuamini Allah تعالى na Malaika Wake, Vitabu na Wajumbe na wenye kumtii,

¹ Ahmad 2:177.

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.”

Huu ndio mwisho wa *Tafsir ya Suratul Ahzaab*. Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuongoza katika njia ya sawa.

* * *

Tafsiri ya Suratu Saba'

Sura ya 34

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَلَهُ
 أَلْحَمْدُ فِي الْآخِرَةِ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿١﴾ يَعْلَمُ مَا يَلْجُ
 فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا
 يَعْرُجُ فِيهَا وَهُوَ الرَّحِيمُ الْغَفُورُ ﴿٢﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا
 تَأْتِينَا السَّاعَةُ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ عِلْمِ الْغَيْبِ لَا
 يَعْزُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَلَا
 أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٣﴾
 لَيَجْزِيَنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ هُمْ
 مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٤﴾ وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي آيَاتِنَا
 مُعْجِرِينَ أُولَٰئِكَ هُمْ عَذَابٌ مِنْ رِجْزِ أَلِيمٍ ﴿٥﴾ وَبَرَى
 الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ الَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ هُوَ الْحَقُّ
 وَيَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٦﴾

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ
 وَمَا فِي الْأَرْضِ وَلَهُ أَلْحَمْدُ فِي الْآخِرَةِ
 وَهُوَ الْحَكِيمُ الْخَبِيرُ ﴿١﴾ يَعْلَمُ مَا
 يَلْجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا
 يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا
 وَهُوَ الرَّحِيمُ الْغَفُورُ ﴿٢﴾

1. "Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Ambaye ni Vyake vyote viliomo mbinguni na katika ardhi. Na Sifa ni Zake Yeye katika Akhera. Naye ni Mwenye Hikima, Mwenye Habari."

2. "Anajua yanayoingia katika ardhi na yanayotoka humo, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda huko. Na Yeye ni Mwingi wa Kurehemu, Mwingi wa Kusamehe."

Shukrani na Elimu ya Ghaibu ni vya Allah تعالی Peke Yake

Allah تعالی Anaeleza kuhusu Nafsi Yake Tukufu kwamba Shukrani ni Zake Yeye tu, duniani na Akhera, kwa sababu Yeye ni Mwenye Kuneemesha, Mwenye Fadhila kwa walio duniani na kwa walio Akhera. Ni Mmiliki wa vyote hivyo, ni Hakimu katika yote haya.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَهُوَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُولَى وَالْآخِرَةِ ۗ وَلَهُ الْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٧٠﴾

“Naye ni Mwenyezi Mungu Ambaye hapana Mola isipokuwa Yeye. Sifa zote njema ni Zake Yeye, mwanzo na mwisho. Na hukumu ni Yake Yeye. Na Kwake Yeye mtarejeshwa.” (28:70)

Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema katika Aya hii:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Ambaye ni Vyake vyote viliomo mbinguni na katika ardhi.”

Yaani, vyote viko katika Miliki Yake na vimetiishwa Kwake na vimedhalilishwa chini ya Udhhibiti Wake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَإِنَّا لَنَا لِلْآخِرَةِ وَالْأُولَىٰ ﴿٩٢﴾

“Na hakika ni Yetu Sisi Akhera na dunia.” (92:13)

Kisha alisema Allah تعالی:

وَلَهُ الْحَمْدُ فِي الْآخِرَةِ ۗ

“Na Sifa ni Zake Yeye katika Akhera.”

Kauli ya Allah تعالی:

وَهُوَ الْحَكِيمُ

“Naye ni Mwenye Hikima.”

Katika Kauli, Matendo, Sharia na Kudura Zake,

الْحَبِيرُ

"Mwenye Habari."

Ambaye Hafichikiwi na kitu, wala hapana kinachoghibu dhidi Yake. Malik alisema kuwa Az-Zuhri amesema: "Ni Mwenye Habari za viumbe Wake, ni Mwenye Hikima katika Amri Zake." Amesema Allah تعالى:

يَعْلَمُ مَا يَلْجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا

"Anajua yanayoingia katika ardhi na yanayotoka humo..."

Yaani, Anajua idadi ya matone ya mvua yanayozama ardhini, mbegu zilizopandwa na kilichoificha humo. Pia Anajua kinachotoka humo, idadi, namna na wasifu wake.

وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ

"...na yanayoteremka kutoka mbinguni."

Miongoni mwa matone ya mvua na riziki, na kinachopanda humo, yaani katika amali njema na ghairi yake,

وَهُوَ الرَّحِيمُ الْغَفُورُ ﴿٦﴾

"Na Yeye ni Mwingi wa Kurehemu, Mwingi wa Kusamehe."

Yaani, Yeye ni Rahimu kwa waja Wake, Hawaharakishii adhabu wenye kumuasi, na pia ni Mwingi wa Kusamehe madhambi ya wenye kutubu Kwake ambao wanamtegemea Yeye.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَأْتِينَا السَّاعَةُ ۗ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ عِلْمِ الْغَيْبِ ۗ لَا يُعْرَبُ

عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَلَا أَصْغَرُ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرُ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٧﴾ لَيَجْزِي الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمْ مَغْفِرَةٌ

وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٨﴾ وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي ءَايَاتِنَا مُعْجِزِينَ أُولَٰئِكَ هُمْ عَذَابٌ مِّن رَّجْزِ أَلِيمٍ

﴿٩﴾ وَيَرَى الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ الَّذِي أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ هُوَ الْحَقُّ وَيَهْدِي إِلَىٰ

صِرَاطٍ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿١٠﴾

3. ***“Na walisema waliokufuru: Haitatufikia Saa (ya Kiyama). Sema: Kwani? Hapana shaka itakufikieni, naapa kwa haki ya Mola Wangu Mlezi, Mwenye Kujua mambo ya siri! Hapana kinachofichikana Kwake hata chenye uzito wa chembe tu, si katika mbingu wala katika ardhi, wala kilicho kidogo kuliko hivyo, wala kikubwa zaidi; ila vyote hivyo vimo katika Kitabu (Chake) kielezacho.”***

4. ***“Ili Awalipe walioamini na wakatenda mema. Hao watapata msamaha na riziki ya heshima.”***

5. ***“Na wale waliojitahidi kuzipinga Ishara Zetu wakaona watashinda, hao watapata adhabu mbaya yenye uchungu.”***

6. ***“Na waliopewa ilimu wanaona ya kuwa ulioteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni haki, nayo huongoa kuendea njia ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kusifiwa.”***

Saa Itakuja Ili Kila Mtu Alipwe Kulingana na Amali Zake

Hii ni mojawapo ya ishara tatu tu – hakuna ya nne - ambapo Allah تعالى Alimuamuru Mtume wake ﷺ aape kwa Mola Mtukufu, kwamba jambo la Kurejeshwa hai ni lenye kutukia kwa hakika. Ni baada ya walio katika ukafiri na ukaidi kukataa. Kati ya ishara hizo, moja imo katika Surat Yunus. Nayoni Kauli ya Allah تعالى:

وَيَسْتَدْعُونَكَ أَحَقُّ هُوَ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقٌّ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٠﴾

“Na wanakuuliza: Je! Ni kweli hayo? Sema: Ehe! Naapa kwa Mola Wangu Mlezi! Hakika hayo ni kweli, na wala nyinyi hamshindi!”
(10:53)

Ya pili ni hii,

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَأْتِينَا السَّاعَةُ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ

“Na walisema waliokufuru: Hakitatuja hicho Kiyama. Sema: “Kwanini? kwa haki ya Mola wangu, bila shaka kitakujieni...” (34:3)

Ya tatu imo ndani ya Surat At-Taghabun. Nayoni Kauli ya Allah تعالى:

رَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ وَذَٰلِكَ عَلَىٰ
 اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾

“Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani? Naapa kwa Mola Wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyoyatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.” (64:7)

Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ

“Sema: “Kwanini? kwa haki ya Mola wangu, bila shaka kitakujeni...”

Kisha alimueleza katika namna inayolitilia nguvu hilo. Alisema:

عَلِيمِ الْغَيْبِ لَا يَعْرُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ وَلَا أَصْغُرُ مِنْ ذَٰلِكَ
 وَلَا أَكْبَرُ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾

“...Mwenye Kujua ya ghaibu! Hapana kinachofichikana Kwake hata chenye uzito wa chembe tu, si katika mbingu wala katika ardhi, wala kilicho kidogo kuliko hivyo, wala kikubwa zaidi; ila vyote hivyo vimo katika Kitabu (Chake) kielezacho.”

Mujahid na Qatadah walisema, “Hapana kinachofichikana kwake...” “Hakuna chenye kufichikana Kwake.”¹ Yaani, vyote vimezungukwa na ilimu Yake, basi hapana chenye kufichama Kwake. Hivyo, mifupa, hata ikichakaa, kusambaratika na kusagika, Yeye Anajua vyema mahali ilipo na ilipoachana. Kisha Atairejesha kama Alivyoianzisha mara ya kwanza, kwani Yeye ni Mwenye Kujua yote.

Kisha, Allah تعالى Alibainisha Hikima Yake katika Kuirejesha miili na kusimama kwa Saa. Kwa Kauli Yake Allah تعالى,

لَيَجْزِيَنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ؕ أُولَٰئِكَ هُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٩﴾
 وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي ءَايَاتِنَا مُعْجِزِينَ

¹ At-Tabari 20:350.

"Ili Awalipe walioamini na wakatenda mema. Hao watapata msamaha na riziki ya ukarimu." "Na wale waliojitahidi kuzipinga Ishara Zetu wakaona watashinda..."

Yaani, wametumia juhudi zao katika kuzuia dhidi ya Njia ya Allah تعالى na kuwakadhibisha Mitume Wake,

أُولَئِكَ هُمْ عَذَابٌ مِّن رَّجْزِ أَلِيمٍ

"...hao watapata adhabu mbaya yenye uchungu."

Yaani, ili wenye furaha, ambao ni Waumini, waneemeke, na Awaadhibu waovu, ambao ni makafiri. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

"Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu." (59:20)

أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ ﴿٢٨﴾

"Hivi Tuwafanye wale walioamini na kufanya vitendo vyema kama wanaofanya ufisadi katika ardhi? Au Tuwafanye wachamungu kama waovu?" (38:28).

Kauli ya Allah تعالى:

وَيَرَى الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ الَّذِي أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ هُوَ الْحَقُّ

"Na waliopewa ilimu wanaona ya kuwa ulioteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni haki..."

Hii ni hikima ya namna nyingine inayofuatia hiyo iliyotangulia. Nayo ni kwamba, walioamini walioteremshiwa Mitume, wakishashuhudia kusimama kwa Saa na kulipwa wema na waovu, mambo ambayo walikwishayajua kutoka katika Kitabu cha Allah duniani, basi wakati huo wanapoyakinisha hayo, watasema:

لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ^ط

“Hakika Mitume wa Mola Wetu Mlezi walileta Haki.” (7:43)

Pia patasemwa,

هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ

“Haya ndiyo aliyoyaahidi Mwingi wa Rehema na wakasema kweli Mitume.” (36:52)

لَقَدْ لَبِئْتُمْ فِي كِتَابِ اللَّهِ إِلَى يَوْمِ الْبَعْثِ^ط

“Hakika nyinyi mlikwishakaa katika hukumu ya Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya kufufuliwa.” (30:56)

وَيَرَى الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ الَّذِي أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ هُوَ الْحَقُّ وَيَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ الْعَزِيزِ

الْحَمِيدِ ﴿٥٦﴾

“Na waliopewa ilimu wanaona ya kuwa ulioteremshiwa kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni haki, nayo huongoa kuendea njia ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kusifiwa.”

Yeye ni Mwenye Kuzuia, Mwenye Nguvu Asiye shindwa wala hazuiliwi. Amekishinda kila kitu na Kukidhibiti. Yeye ni Mwenye Kusifiwa kwa Kauli, Matendo, Sharia na Kudura Zake, na Ndiye Anayestahiki Kusifiwa katika hayo yote.

* * *

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا هَلْ نَدُلُّكُمْ عَلَى
 رَجُلٍ يُدْبِكُمْ إِذَا مُمِرَّتْ كُلُّ مَمْرٍ
 إِنَّكُمْ لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿٧﴾ أَفَتَرَى عَلَى
 اللَّهِ كَذِبًا أَمْ بِهِ جِنَّةٌ ۚ بَلِ
 الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ فِي
 الْعَذَابِ وَالضَّلَالِ الْبَعِيدِ ﴿٨﴾ أَفَلَمْ يَرَوْا إِلَى مَا بَيْنَ
 أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ كُنْشًا
 نَخِيفَ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ نُسْقِطَ عَلَيْهِمُ السَّمَاءَ ۗ
 إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّكُلِّ عَبْدٍ مُنِيبٍ ﴿٩﴾ * وَلَقَدْ آتَيْنَا
 دَاوُدَ مِنَّا فَضْلًا ۖ يٰجِبَالُ أَوْبِي مَعَهُ وَالطَّيْرُ ۗ وَأَنَّا لَهُ
 الْحَدِيدُ ﴿١٠﴾ أَنْ أَعْمَلَ سَبْعِينَ قَدْرًا فِي السَّرْدِ ۖ وَأَعْمَلُوا
 صَالِحًا ۖ إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١١﴾ وَلَسَلِيمَانَ الرِّيحَ
 غَدُوها شَهْرًا وَرَوَّاحُها شَهْرًا ۖ وَأَسَلْنَا لَهُ عَيْنَ الْقِطْرِ ۖ وَمَنْ
 الْجِنِّ مَنْ يَعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِإِذْنِ رَبِّهِ ۖ وَمَنْ يَزِغْ مِنْهُمْ عَنْ
 أَمْرِنَا نُذِقْهُ مِنْ عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿١٢﴾ يَعْمَلُونَ لَهُ مَا يَشَاءُ
 مِنْ مَحْرَبٍ وَتَمَثِيلٍ ۖ وَجِفَانٍ كَالْجَوَابِ وَقُدُورٍ رَاسِيَتٍ ۗ
 أَعْمَلُوا ۗ أَلْ دَاوُدَ شُكْرًا ۖ وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٣﴾
 فَلَمَّا فَصَّيْنَا عَلَيْهِ الْمَوْتَ مَا دَهَمَ عَلَى مَوْتِهِ إِلَّا دَابَّةُ
 الْأَرْضِ تَأْكُلُ مِنسَأَتَهُ ۖ فَلَمَّا خَرَّ تَبَيَّنَتِ الْجِنُّ أَنْ لَوْ
 كَانُوا يَعْلَمُونَ الْغَيْبَ مَا لَبِثُوا فِي الْعَذَابِ الْمُهِينِ ﴿١٤﴾

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا هَلْ نَدُلُّكُمْ عَلَى
 رَجُلٍ يُدْبِكُمْ إِذَا مُمِرَّتْ كُلُّ مَمْرٍ
 إِنَّكُمْ لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿٧﴾ أَفَتَرَى
 عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَمْ بِهِ جِنَّةٌ ۚ بَلِ
 الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ فِي
 الْعَذَابِ وَالضَّلَالِ الْبَعِيدِ ﴿٨﴾ أَفَلَمْ يَرَوْا
 إِلَى مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ
 مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ كُنْشًا
 نَخِيفَ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ نُسْقِطَ عَلَيْهِمُ
 السَّمَاءَ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ
 لَآيَةً لِّكُلِّ عَبْدٍ مُنِيبٍ ﴿٩﴾

7. "Na waliokufuru wali-sema: Je! Tukujuulisheni mtu anayekuambieni kwamba mtakapochambuliwa mapande mapande kuwa mta- kuwa katika umbo jipya?"

8. "Ama amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au ana wazimu. Bali wasioamini Akhera wamo adhabuni na upotofu wa mbali kabisa."

9. "Kwani hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi? Tungelipenda Tungeliwadidimiza ndani ya ardhi, au Tungeliwa-

***teremshia juu yao vipande vya mbingu. Hakika katika haya zipo
Ishara kwa kila mja aliyetubia.***

Ukanaji Akhera wa Makafiri na Kujibiwa kwao

Hizi ni khabari Anazozieleza Allah تعالى kuhusu makafiri na waasi walivyokanusha kusimama kwa Saa, na kumfanyia stihizai Mtume ﷺ baada ya kulieleza hilo.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا هَلْ نَدُلُّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ يُنْفِكُكُمْ إِذَا مَرَّكُمْ كُلُّ مُمْرَقٍ

***“Na waliokufuru walisema: Je! Tukujuulisheni mtu anayekuambieni
kwamba mtakapochambuliwa mapande mapande...”***

Yaani, miili yao imeachanaachana ardhini na mapande yakasambaa na kuchakaa kabisa,

إِنكُمْ

“...mtakuwa...” Yaani, baada ya hali hii,

لَيْفَىٰ خَلْقٍ جَدِيدٍ

“...mtakuwa katika umbo jipya?”

Yaani, mtarejea mkiwa hai na mtaruzukiwa upya. Katika kuyaeleza haya, Allah تعالى Analieleza jambo Lake katika moja ya namna mbili: ama mkanushaji awe amekusudia kumzushia Allah تعالى uongo kuwa amefunuliwa hilo na Allah تعالى au analifanya hilo kutokana na kuhadaiwa kwake na kuwa kama alivyo mtu mwendawazimu au kichaa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَفَتَرَىٰ عَلَىٰ اللَّهِ كَذِبًا أَمْ بِهِ جِنَّةٌ

“Ama amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo, au ana wazimu.”

Katika kuwakanushia, Allah تعالى Amesema:

بَلِ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ فِي الْعَذَابِ وَالضَّلَالِ الْبَعِيدِ

***“Bali wasioamini Akhera wamo adhabuni na upotofu wa mbali
kabisa.”***

Yaani, jambo lilivyo, si kama walivyodai, wala si kama walivyoliendea, bali Muhammad ﷺ ndiye mkweli, mwema na muongofu. Ndiye aliyeleta ukweli. Wao hao ni waongo, majahili na wapumbavu,

فِي الْعَذَابِ

"...wamo adhabuni..."

Yaani, ukafiri wao, utawapeleka katika adhabu ya Allah تعالى,

وَالضَّلَالِ الْبَعِيدِ

"...na upotofu wa mbali kabisa." Dhidi ya ukweli duniani.

Kisha Allah تعالى Aliwajulisha kuhusu Kudura Zake katika Kuumba mbingu na ardhi. Allah تعالى Amesema:

أَفَلَمْ يَرَوْا إِلَى مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ مِمَّنِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

"Kwani hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi?"

Yaani, kokote wanakoelekea na kwenda, basi mbingu imewafunika juu yao, na ardhi chini yao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَالسَّمَاءِ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٤٧﴾ وَالْأَرْضِ فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ الْمَبْهُدُونَ ﴿٤٨﴾

"Na mbingu Tumezifanya kwa nguvu na uweza na hakika Sisi bila ya shaka ndio twenye Uweza wa Kuzitanua. Na ardhi Tumeitandaza; basi watandazaji wazuri namna gani Sisi!" (51:47-48)

Kauli ya Allah تعالى:

إِنْ نَشَأْ نُخِيفْ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ نُسْقِطْ عَلَيْهِمْ كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ

"Tungelipenda Tungeliwadidimiza ndani ya ardhi, au Tungeli-wateremshia juu yao vipande vya mbingu."

Yaani, lau Tungelitaka Tungeliwafanyia hayo kwa sababu ya dhuluma zao, kwa kuwa tuna uwezo mkubwa juu yao. Lakini, Tunayaakhirisha hayo, kwa sababu ya Ulatifu na Kuafu Kwetu. Kisha, Amesema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّكُلِّ عَبْدٍ مُنِيبٍ

“Hakika katika haya zipo Ishara kwa kila mja aliye tubia.”

Ma'mar alisimulia kutoka kwa Qatadah kuwa maana ya *Al-Munib* ni kila anayetubu.¹ Sufyan alisimulia kutoka kwa Qatadah, kwamba *Al-Munib* ni ambaye anarejea kwa Allah تعالى.² Yaani, hakika katika kuangalia juu ya kuumbwa mbingu na ardhi, kuna dalili kwa kila mja mtambuzi, mwenye hikima, anayerejea kwa Allah تعالى. Ni kuhusu Uweza wa Allah تعالى Kuvifufua viwiliwili na kutukia jambo la Kurejea. Kwa sababu Aliyeweza Kuziumba mbingu hizi, pamoja na kunyanyuka na kukunjuka kwake; na ardhi hizi kwa kuwa chini kwa marefu na mapana yake, basi ni Mweza wa Kurejeshwa viwiliwili na Kuikusanya tena mifupa iliyooza. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ بَلَىٰ

“Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi Kuwaumba mfano wao? Kwani!” (36:81)

لَخَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57)

وَلَقَدْ آتَيْنَا دَاوُدَ مِنَّا فَضْلًا ۖ يَجِبَالٌ أُوتِي مَعَهُ وَالطَّيْرُ ۗ وَالنَّا لَهُ الْحَدِيدَ ﴿٥٨﴾ أَنْ أَعْمَلَ سَيِّغَتٍ وَقَدَّرَ فِي السَّرْدِ ۖ وَأَعْمَلُوا صٰلِحًا ۗ إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٥٩﴾

10. “Na Tulimpa Daudi fadhila kutoka kwetu, (Tukasema): Enyi milima! Karirini kumtakasa Mwenyezi Mungu pamoja naye! Na ndege pia. Na Tukamlainishia chuma.”

11. “(Tukamuambia:) Tengeneza nguo za chuma pana, na kadiria sawa katika kuunganisha. Na tendeni mema. Hakika Mimi Nayaona vyema mnayoyatenda.”

¹ Abdur-Razzaq 3:126.

² At-Tabari 20:356.

Maelezo Juu ya Fadhila za Allah kwa Dawud عليه السلام.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Alivyomneemesha mja na Mtume Wake, Dawud عليه السلام kwa Kumpa fadhila bayana. Allah تعالى Alimpatia Unabii, pamoja na ufalme, majeshi yenye idadi kubwa ya wapiganaji na zana za kivita. Alimpatia sauti kubwa, ambayo alipoitumia katika kumtukuza Allah تعالى, basi milima mirefu, imara na migumu, ilishirikiana naye. Ndege warukao kwa khiyari yao waliokuwa wakitoka asubuhi na kurejea jioni walikuwa wakisimama kwa ajili yake na kuwasiliana nao kwa lugha mbalimbali. Katika *Sahih* kuna Hadithi kwamba, Mtume ﷺ alisikia sauti ya Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه akiwa anasoma wakati wa usiku. Akasimama na kusikiliza usomaji wake. Halafu Mtume ﷺ akasema:

«لَقَدْ أُوْتِيَتْ هَذَا مِزْمَارًا مِنْ مَزَامِيرِ آلِ دَاوُدَ»

*"Hakika Huyu amepewa zumari miongoni mwa zumari za watu wa Dawud."*¹

Abu 'Uthman An-Nahdi alisema, "Sikuyasikia matoasi yoyote, chombo au zeze ambazo zilikuwa nzuri zaidi kuliko sauti ya Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه.² Maana ya Kauli ya Allah تعالى:

أُوْتِيَتْ

"...Karirini kumtakasa..."

Ni Kumtakasa Allah تعالى. Hii ilikuwa rai ya Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na wengine.³ Maana ya *At-T'awiyb* katika lugha ya kiarabu ni kurejesha. Hivyo, milima na ndege waliamriwa kurejesha sauti pamoja naye. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَلْنَا لَهُ الْحَدِيدَ

"Na Tukamlainishia chuma."

Al-Hasan Al-Basri, Qatadah, Al-A'mash na wengine walisema: "Hakuhitaji kukichoma moto chuma au kukipiga kwa nyundo; alikikunja kwa mikono tu, kama nyuzi."⁴

¹ Muslim 1:546.

² *Fadhail Al-Qur'an* na Abu 'Ubayd uk. 79.

³ At-Tabari 20:357.

⁴ At-Tabari 20:359.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَنْ أَعْمَلَ سَدِغَتٍ

“(Tukamuambia:) Tengeneza nguo za chuma pana...”

Nayo ni deraya. Qatadah alisema, “Alikuwa mtu wa kwanza kutengeneza deraya; kabla ya hapo walikuwa wakivaa mabamba ya chuma.”¹

وَقَدَّرَ فِي السَّرْدِ

“...na kadiria sawa katika kuunganisha.”

Huu ni mwongozo utokao kwa Allah تعالى kwa ajili ya Nabii Wake, Dawud عليه السلام ili Kumfundisha utengenezaji wa ngao. Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَقَدَّرَ فِي السَّرْدِ

“...na kadiria sawa katika kuunganisha.”

Kuwa, “usigongeelee misumari itacheza cheza katika mzunguko, wala usikaze sana kwani haitaweza kwenda kabisa, bali ifanye kwa wastani.”² ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Neno *Sard* ni mzunguko wa chuma.” Baadhi yao walisema: “Husema kwamba deraya ni *Masrud* ikiwa mizunguko yake imetiwa ribiti. Hii imeungwa mkono na kauli ya mshairi: ‘Na juu yake kuna *Sard* mbili alizozitia Dawud عليه السلام, au alitengeneza *Sawabigh* zilizofuatana.” Kauli ya Allah تعالى:

وَأَعْمَلُوا صَالِحًا

“Na tendeni mema.” Yaani, kuhusu Neema Alizokupeni Allah تعالى,

إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

“Hakika Mimi Nayaona vyema mnayoyatenda.”

Yaani, ni Mwenye Kukuchungeni, Mwenye Kuziona amali na kauli zenu, hapana chochote katika hivyo ambacho hufichama dhidi Yake.

¹ At-Tabari 20:359.

² At-Tabari 20:361.

وَلَسَلِمْنَ الرِّيحَ غُدُوها شَهْرٌ وَرَوَّاحُها شَهْرٌ ۗ وَأَسَلْنَا لَهُ عَيْنَ الْقِطْرِ ۗ وَمِنَ الْجِنِّ مَن
يَعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِإِذْنِ رَبِّهٖ ۗ وَمَن يَزِغْ مِنْهُمْ عَنَ أَمْرِنَا نُنذِقْهُ مِن عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿١٢﴾
يَعْمَلُونَ لَهُ مَا يَشَاءُ مِن مَّحْرِبٍ وَتَمَثِيلٍ ۖ وَجَفَانٍ كَالْجَوَابِ وَقُدُورٍ رَّاسِيَتٍ ۗ أَعْمَلُوا ءَالَ
دَاوُدَ شُكْرًا وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّكُورِ ﴿١٣﴾

12. *“Na Suleiman Tuliufanya upepo umtumikie. Safari yake ya asubuhi ni mwendo wa mwezi mmoja, na safari yake ya jioni ni mwendo wa mwezi mmoja. Na Tukamyayushia chemchemi ya shaba. Na katika majini walikuwako waliokuwa wakifanya kazi mbele yake kwa Idhini ya Mola Wake Mlezi. Na kila anayejitenga na Amri Yetu katika wao, Tunamuonjesha adhabu ya Moto unaowaka.”*

13. *“Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama ngome, na masanamu, na madeste makubwa kama mahodhi, na masufuria makubwa yasiyoondolewa mahala pake. Enyi watu wa Daudi! Fanyeni kazi kwa kushukuru. Ni wachache katika waja wangu wanaoshukuru.”*

Fadhila za Allah عليه السلام juu ya Sulayman

Baada ya Kutaja Neema Zake kwa Dawud عليه السلام, Allah تعالى Alifuatishia Kutaja Alivyompatia mwanaye, Sulayman عليه السلام, kama vile kuutiisha upepo kwa ajili yake ili limbebee busati lake, kwenda kwake mwezi mzima na kurejea mwezi mwingine. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema: “Alikuwa akipanda juu ya busati lake wakati wa asubuhi kutoka Damaskas, anateremka Istwakhar, anakula chakula cha mchana hapo. Kisha akiondoka Istwakhar na kulala usiku sehemu ya Kabul.”¹ Baina ya Damaskas na Istwakhar ni safari ya kiasi cha mwezi mmoja kwa mwendo wa kawaida wa mnyama, kadhalika baina ya Istwakhar na Kabul.

¹ At-Tabari 20:362.

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَسَلْنَا لَهُ عَيْنَ الْقِطْرِ^ط

“Na Tukamyayushia chemchem ya shaba.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid, ‘Ikrimah, ‘Ata, Al-Khurasani, Qatadah, As-Suddi, Malik kutoka kwa Zayd bin Aslam, na wengine walisema, “*Qitr* ni shaba nyekundu.”² Qatadah alisema, “Tukio lilitukia Yemen.”³ Allah تعالى Alimpa Sulayman عليه السلام, vitu vyote avitengenezavyo mwanaadamu. Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنَ الْجِنَّ مَنْ يَعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِإِذْنِ رَبِّهِ^ط

“Na katika majini walikuwako waliokuwa wakifanya kazi mbele yake kwa Idhini ya Mola Wake Mlezi.”

Kwa maana, Tulimtiishia majini, wanafanya kazi mbele yake kwa Idhini ya Mola Wake. Yaani, kwa Kudura Yake na Kuwarahisishia wao kwa Utashi Wake kiasi Atakavyo, walimjengea majengo aliyoyataka na mengineyo.

وَمَنْ يَزِغْ مِنْهُمْ عَنْ أَمْرِنَا

“Na kila anayejitenga na Amri Yetu katika wao...”

Yaani, yeyote kati yao aliyejaribu kuasi na kutoka nje ya utii.

نُذِقُهُ مِنَ عَذَابِ السَّعِيرِ

“...Tunamuonjesha adhabu ya Moto unaowaka.”

Maana yake kuunguzwa. Kauli ya Allah تعالى:

يَعْمَلُونَ لَهُ مَا يَشَاءُ مِنْ مَّحْرِبٍ وَتَمَثِيلٍ

“Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama ngome na masanamu.”

¹ At-Tabari 20: 363, 364.

² At-Tabari 20:363.

Al-Mahaaryb ni majengo mazuri, sehemu nzuri zaidi ya ndani ya makazi na ndio katikati yake. Ibn Zayd amesema; "Hii inamaanisha makazi."¹ Kuhusu "*Tamaathyl*," Atwiyyah, Al-'Awfi, Adh-Dhahhak na As-Suddi walisema kwamba maana ya *Tamaathyl* ni picha."² Kauli ya Allah تعالى:

وَجَفَانَ كَأَجْوَابٍ وَقُدُورٍ رَأْسِيَتْ

"...na madeste makubwa kama mahodhi, na masufuria makubwa yasiyoondolewa mahala pake."

Al-Jawaab ni wingi wa neno *Jabiyah* ambalo humanisha tangi la maji. *Qudur Rraasiyaat* ni masufuria makubwa yenye kukaa sehemu moja na hayahamishwi kwa sababu ya ukubwa. Hii ilikuwa rai ya Mujahid, Adh-Dhahhak na wengine.³ Kauli ya Allah تعالى:

أَعْمَلُوا ءَالَ دَاوُدَ شُكْرًا

"Enyi watu wa Daudi! Fanyeni kazi kwa kushukuru."

Yaani, Tuliwaambia: 'Fanyeni kazi pamoja na kushukuru juu ya Aliyokunee mesheni duniani na akhera. Inaonesha kwamba, kushukuru ni kwa vitendo, kama ambavyo inakuwa kwa kauli na nia. Ni sawa na alivyosema mshairi: "Zimekufaidisheni neema za namna tatu kupitia kwangu, mkono wangu, ulimi wangu na dhamiri iliyo ndani."

Abu 'Abdur-Rahman Al-Hubuli alisema, "Sala ni shukurani, Saumu ni shukurani, kila amali njema uifanyayo kwa ajili ya Allah تعالى ni shukurani, na shukurani iliyo bora ni kusifu." Haya yalinukuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.⁴ Katika *Sahih* Mbili kuna Hadithi kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَحَبَّ الصَّلَاةِ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى صَلَاةُ دَاوُدَ، كَانَ يَنَامُ نِصْفَ اللَّيْلِ، وَيَقُومُ ثُلُثَهُ، وَيَنَامُ سُدُسَهُ، وَأَحَبَّ الصِّيَامِ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى صِيَامُ دَاوُدَ، كَانَ يَصُومُ يَوْمًا وَيَنْفِطِرُ يَوْمًا، وَلَا يَفْرُ إِذَا لَأَقَى»

¹ At-Tabari 20:365.

² At-Tabari 20:366.

³ At-Tabari 20:367.

⁴ At-Tabari 20:369.

"Hakika Sala ipendwayo sana kwa Allah ni Sala ya Dawud. Alikuwa akilala nusu ya usiku, anasimama theluthi yake (kwa Sala) na kulala sudusi yake. Na Saumu ipendwayo sana kwa Allah ni saumu ya Dawud. Alikuwa akifunga siku moja na kufungua siku moja, wala hakimbii anapopigana vita."¹

Abu Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Fudhwail aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

أَعْمَلُوا ءَالَ دَاوُدَ شُكْرًا

"Enyi watu wa Daud! Fanyeni kazi kwa kushukuru."

Dawud عليه السلام amesema: "Namna gani nikushukuru, ilhali shukurani pia ni neema kutoka Kwako." Alisema:

وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّاكِرُونَ

"Ni wachache katika waja Wangu wanaoshukuru."

فَلَمَّا قَضَيْنَا عَلَيْهِ الْمَوْتَ مَا دَهَمَهُمْ عَلَىٰ مَوْتِهِمْ إِلَّا دَابَّةُ الْأَرْضِ تَأْكُلُ مِنْسَأَتَهُمْ فَلَمَّا خَرَّ تَبَيَّنَتِ آيَاتُ أَنْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ الْغَيْبَ مَا لَبِثُوا فِي الْعَذَابِ الْمُهِينِ ﴿١٤﴾

14. "Na Tulipomhukumia kufa, hapana aliyewajuulisha kufa kwake ila mnyama wa ardhi aliyekula fimbo yake. Na alipoanguka majini walitambua lau kuwa wangelijua ya ghaibu wasingelika katika adhabu hiyo ya kufedhehesha."

Kufariki kwa Sulayman عليه السلام

Allah تعالى Anatueleza namna Sulayman عليه السلام alivyofariki na namna Allah تعالى Alivyowaficha majini ambao walitiishwa kwake wafanye kazi ngumu. Aliendelea kuegemea fimbo yake ambayo ilikuwa mkongojo wake, kwa mujibu wa ibnu 'Abbas, Mujahid, Al-Hasan, Qatadah na wengine walivyosema.² Alibakia hivyo kwa kipindi kirefu, kadiri ya mwaka mmoja. Baada ya fimbo

¹ Ad-Dur Al-Manthur 6:680.

² At-Tabari 20:370.

hiyo kuliwa na wadudu ardhini, nao ni mchwa, ilidhoofu na ikaanguka chini, ndipo ilipojulikana kwamba alishakufa tangu muda mrefu. Ikawadhihirikia majini na wanaadamu kwamba majini hawajui ghaibu, kama walivyokuwa wakidai hivyo na watu wengine wakiwaunga mkono. Hiyo ndiyo Kauli ya Allah تعالی:

مَا دَهُمَ عَلَىٰ مَوْتِهِمْ إِلَّا دَابَّةُ الْأَرْضِ تَأْكُلُ مِنسَاتِهِمْ ۗ فَلَمَّا خُرَّ تَبَيَّنَتْ لِجِنَّ أَن لَوْ كَانُوا
يَعْلَمُونَ الْغَيْبَ مَا لَبِثُوا فِي الْعَذَابِ الْمُهِينِ ﴿٧٤﴾

“...hapana aliyewajuulisha kufa kwake ila mnyama wa ardhi aliyekula fimbo yake. Na alipoanguka majini walitambua lau kuwa wangelijua ya ghaibu wasingelika katika adhabu hiyo ya kufedhehesha.”

Yaani, iliwadhihirikia watu kuwa wao (majini) walikuwa waongo.

* * *

لَقَدْ كَانَ لِسَبَإٍ فِي مَسْكِهُمْ آيَةٌ ۖ جَنَّتَانِ عَنْ يَمِينٍ
 وَشِمَالٍ ۖ كُلُوا مِنْ رِزْقِ رَبِّكُمْ وَاشْكُرُوا لَهُ ۗ بَلْدَةٌ طَيِّبَةٌ
 وَرَبٌّ غَفُورٌ ﴿١٥﴾ فَأَعْرَضُوا فَأَرْسَلْنَا سَيْلَ الْعَرِمِ
 وَبَدَّلْنَاهُمْ بِجَنَّتَيْهِمْ جَنَّتَيْنِ ذَوَاتِ أُكُلٍ خَمْطٍ وَأَثَلٍ ۚ وَشَيْءٍ
 مِنْ سِدْرٍ قَلِيلٍ ﴿١٦﴾ ذَلِكَ جَزَيْنَهُمْ بِمَا كَفَرُوا ۗ وَهَلْ
 تُجْزَىٰ إِلَّا الْكُفُورَ ﴿١٧﴾ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُم وَبَيْنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي
 بَرَكْنَا فِيهَا قَرْيَ ظَهْرَةَ وَقَدَرْنَا فِيهَا السَّيْرَ ۗ سَمُرُوا فِيهَا
 لَيَالِيًا وَأَيَّامًا ءَامِينَ ﴿١٨﴾ فَقَالُوا رَبَّنَا بَعْدَ بَيْنِ أَسْفَارِنَا
 وَظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ فَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ وَمَزَقْنَاهُمْ كُلَّ مُمَزِقٍ ۚ
 إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿١٩﴾ وَلَقَدْ صَدَقَ
 عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ فَاتَّبَعُوهُ إِلَّا فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٠﴾
 وَمَا كَانَ لَهُمْ عَلَيْهِمْ مِنْ سُلْطَانٍ إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يُؤْمِنُ
 بِالْآخِرَةِ ۖ مِمَّنْ هُوَ مِنْهَا فِي شَكٍ ۗ وَرَبُّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ
 حَفِيظٌ ﴿٢١﴾ قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ رَعِمْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ لَا
 يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ
 وَمَا هُمْ فِيهِمَا مِنْ شَرِكٍ ۗ وَمَا لَهُ مِنْهُمْ مِنْ ظَهِيرٍ ﴿٢٢﴾ وَلَا
 تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ ۗ لَهُ ۚ حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ
 عَنْ قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۗ قَالُوا الْحَقُّ ۖ وَهُوَ الْعَلِيُّ
 الْكَبِيرُ ﴿٢٣﴾

لَقَدْ كَانَ لِسَبَإٍ فِي مَسْكِهِمْ آيَةٌ ۖ
 جَنَّتَانِ عَنْ يَمِينٍ وَشِمَالٍ ۖ كُلُوا مِنْ
 رِزْقِ رَبِّكُمْ وَاشْكُرُوا لَهُ ۗ بَلْدَةٌ طَيِّبَةٌ
 وَرَبٌّ غَفُورٌ ﴿١٥﴾ فَأَعْرَضُوا فَأَرْسَلْنَا
 سَيْلَ الْعَرِمِ وَبَدَّلْنَاهُمْ بِجَنَّتَيْهِمْ
 جَنَّتَيْنِ ذَوَاتِ أُكُلٍ خَمْطٍ وَأَثَلٍ
 وَشَيْءٍ مِنْ سِدْرٍ قَلِيلٍ ﴿١٦﴾ ذَلِكَ
 جَزَيْنَهُمْ بِمَا كَفَرُوا ۗ وَهَلْ تُجْزَىٰ إِلَّا
 الْكُفُورَ ﴿١٧﴾

15. "Hakika ilikuwapo Ishara kwa (watu wa nchi ya) Sabai katika maskani yao - bustani mbili, kulia na kushoto. Kuleni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, na mumshukuru. Mji mzuri na Mola Mlezi Aliye Msa-mehevu."

16. "Lakini wakaacha. Tukawapelekea mafuriko makubwa, na Tukawa badilishia badala ya bustani zao hizo kwa bustani nyengine zenye matunda makali machungu, na mivinje, na kidogo katika miti ya kunazi."

17. "Hayo Tuliwalipa kwa sababu ya walivyokufuru. Nasi kwani Tunamuadhibu isipo kuwa anayekufuru?"

Ukafiri wa Sheba (Sabai) na Kuadhibiwa Kwao

Sabai (Sheba) inarejea kwa wafalme na watu wa Yemen. *At-Tabaaba'ah* (Lakabu ya wafalme wa zamani wa Yemen), na Bilqis, malkia aliyekutana na Sulayman عليه السلام walikuwa miongoni mwao. Walikuwa katika neema na anasa katika nchi na maisha yao kwa kuwa na ukunjufu wa riziki, mazao na matunda yao. Allah تعالى Akawatuma Mitume kwenda kwao kuwaamuru kwamba wale katika riziki Zake na wamshukuru kwa kumpwekesha katika ibada. Wakayafuata hayo kwa muda aliotaka Allah تعالى. Halafu wakayakataa waliyoamrisha. Wakaadhibiwa kwa kupelekewa mafuriko yaliyoenea nchi nzima ya Sheba, katika pande zote. Ni kama itakavyoelezwa na kubainishwa hapa karibuni, Inshaallah, na Kwake Yeye tunategemea.

Ibn Jarir رضي الله عنه alinukuu kwamba Farwah bin Musayk Al-Ghutwaifi رضي الله عنه kwamba alisema: "Ewe Mtume wa Allah! Nieleze, ni nini Sheba?" Ni ardhi au Mwanamke?" Akasema:

«لَيْسَ بِأَرْضٍ وَلَا امْرَأَةٍ، وَلَكِنَّهُ رَجُلٌ وُلِدَ لَهُ عَشْرَةٌ مِنَ الْوَالِدِ، فَتَيَّامَنَ مِثْنَةً وَتَشَاءَمَ
أَرْبَعَةً، فَأَمَّا الَّذِينَ تَشَاءَمُوا: فَلَحْمٌ وَجُدَامٌ وَعَامِلَةٌ وَعَسَّانٌ، وَأَمَّا الَّذِينَ تَيَّامَنُوا:
فَكِنْدَةٌ وَالْأَشْعَرِيُّونَ وَالْأَزْدُ وَمَذْحِجٌ وَحِمِيرٌ وَأَنْمَارٌ»

"Haikuwa ardhi wala mwanamke. Ni mtu aliyekuwa na watoto kumi ambapo sita kati yao walikwenda Yemen na wane walikwenda Ash-Sham. Waliokwenda Shamu ni Lakhm, Judham, 'Amilah na Ghassan. Waliokwenda Yemen ni Kindah, Al-Ashariyyuna, Al-Azad, Madh-hij, Himyar na Anmaar."

Mtu mmoja akasema: "Ni nini Anmaar?" Akasema Mtume ﷺ:

«الَّذِينَ مِنْهُمْ خَفَعُوا وَبَجَلَهُ»

"Wale ambao miongoni mwao ni Khath'am na Bajilah."¹

Hii ilinukuliwa na At-Tirmidhi katika *Jami'(Sunan)* yake kwa urefu zaidi ya hivi; kisha akasema, "Hadithi hii ni *Hasan Gharib*."²

¹ At-Tabari 20:375.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:88.

Maulamaa wa elimu ya nasaba walisema – Muhammad bin Is-haq رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى akiwa miongoni mwao – walisema, “Jina la Sheba, lilikuwa ‘Abdush-Shams bin Yashjab bin Ya’rub bin Qahtwan. Aliitwa *Sabai* kwa sababu alikuwa Mwarabu wa kwanza ku-*Sabai* (kutawanyika). Pia alijulikana kwa jina la *Ar-Raish*, kwa sababu alikuwa mtu wa kwanza kuchukua ngawira vitani, akawapatia kaumu yake. Akaitwa *Ar-Raish*. Waarabu walikuwa mali wakiita *Rish* au *Riyash*.”

Wamekhitilafiana juu ya Qahtwan kwa kauli tatu: **(Ya kwanza)** Kwamba yeye ni katika uzao wa Iram bin Sam bin Nuh عَلَيْهِ السَّلَام. Hapa kumekuwa na rai tatu tofauti kuhusu namna nasaba yake ilivyopatikana. **(Ya pili)** Kwamba alitokana na uzao wa ‘Abar, naye ni Hud عَلَيْهِ السَّلَام. Pia, walikhitilafiana katika rai tatu kuhusu namna nasaba yake ilivyoungana. **(Ya tatu)** Kuwa ametokana na uzao wa Ismail bin Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَام. Wamekhitilafiana juu ya mfuatano wa nasaba yake, kwa kupatikana maoni ya namna tatu. Haya yalielezwa kwa urefu na Imamu Al-Hafidh Abu ‘Umar bin ‘Abdul-Barr An-Namari, رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى, katika kitabu chake kilichoitwa, *Al-Inbaah ‘Alaa Dhikr Usul Al-Qabaail Arr-Ruwat*.

Maana ya kauli ya Mtume ﷺ:

«كَانَ رَجُلًا مِّنَ الْقَرَبِ»

“Alikuwa ni mtu katika Waarabu.”¹

Ni Waarabu halisi ambao walikuwepo kabla ya *Al-Khalil* Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَام, katika uzao wa Sam bin Nuh عَلَيْهِ السَّلَام. Kwa mujibu wa kauli ya tatu, alitokana na uzao wa *Al-Khalil* Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَام, lakini haikuwa mashuhuri kwao. Allah تَعَالَى Ndiye Mjuzi. Hata hivyo kuna nukuu katika *Sahih* Al-Bukhari kwamba Mtume ﷺ alipita katika kundi kutoka kabila la Aslam waliokuwa wakifanya mazoezi ya kupiga mishale, akawaambia:

«ارْمُوا بَنِي إِسْمَاعِيلَ فَإِنَّ آبَاءَكُمْ كَانَ رَايِيَا»

“Rusheni mishale, Enyi wana wa Ismail, kwani baba yenu alikuwa mrusha mishale.”²

¹ At-Tabari na. 28782.

² *Fat’h Al-Bari* 6:261.

Aslam lilikuwa kabila mojawapo katika Answar – ambao ni Aws na Khazraj, ambao walitokana na Ghassan, kutoka makabila ya Waarabu wa Yemen, kutokea Sabai – waliteremka Yathrib wakati Sabai walipotawanyika katika ardhi, pindi Allah Alipowapelekea mafuriko kutokana na kufurika kwa bwawa. Kundi lao jingine liliteremka Sham (Syria) na wakaitwa Ghassan, kutokana na maji yaliyokuwepo karibu na walipopiga kambi, ilisemekana kwamba ilikuwa Yemen, pia ilisemekana ni karibu na Al-Mushallal. Ni sawa na alivyosema Hasan bin Thabit رضي الله عنه: “Kama utauliza, basi sisi ni jamii ya uzao bora, ukoo wetu ni Al-Azad, na maji yetu ni Ghassan.”

Maana ya kauli ya Mtume ﷺ:

«وُلِدَ لَهُ عَشْرَةٌ مِنَ الْعَرَبِ»

“Alikuwa na watoto kumi katika Waarabu.”³

Yaani, uzao wake ulikuwa ni hao kumi ambao ndio asili ya makabila ya Waarabu wa Yemen, si kwamba wamezaliwa kutokana na mgongo wake. Kunawezekana kuwa kulikuwa na vizazi viwili au vitatu baina yake na baadhi yao, au zaidi au kidogo, kama ilivyoelezwa kwa urefu katika mahali panaponasibiana napo ndani ya vitabu vya elimu ya nasaba. Maana ya kauli ya Mtume ﷺ:

«فَتَيَّامَنَ مِنْهُمْ سِتَّةٌ وَتَنَاءَمَ مِنْهُمْ أَرْبَعَةٌ»

“Sita kati yao walikwenda Yemen, na wane wakaenda Shamu.”¹

Yaani, baada ya Allah تعالى Kuwapelekea mafuriko, baadhi yao walibakia katika nchi yao, na wengine waliondoka na kwenda kwingine.

Bwawa la Ma'arib na Mafuriko

Kisa cha bwawa ni kuhusu maji yaliyokuwa yakiwajia kutoka katika milima miwili, pamoja na mafuriko yaliyotokana na mvua na mabonde yao. Wafalme wao wa zamani walijenga bwawa kubwa na imara, na maji yakafikia usawa wa juu kabisa wa milima hii miwili. Kisha walipanda miti wakapata matunda

¹ At-Tabari na. 28782.

² At-Tabari na. 28782.

bora ambayo hawakuwahi kuyavuna, mengi na mazuri. *Salaf* wengi, akiwemo Qatadah, walisema kuwa mwanamke aliweza kutembea baina ya miti akiwa amebeba kikapu au chombo kama Jummu kinachotumika kukusanyia matunda – kichwani kwake. Na kwamba matunda yaliweza kuangukia kutoka katika miti na kukijaza kikapu, bila ya kuwepo haja kwake kuyaokota, kwa sababu ya wingi, kuiva na kustawi kwake.¹

Hili lilikuwa bwawa la Ma'arib, ardhi iliyo baina ya San'a kiasi cha mwendo wa siku tatu. Wengine walisema kwamba katika ardhi yao hakukuwa na nzi, mbu, viroboto, wala aina yoyote ya mnyama au mdudu mharibifu. Ilikuwa kwa sababu ya hali njema ya hewa iliyokuwepo na watu walikuwa na afya, pamoja na hifadhi ya Allah تعالى kwao ili wampwekeshe na kumuabudu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَقَدْ كَانَ لِسَبَإٍ فِي مَسْكِهُمْ آيَةٌ^ط

“Hakika ilikuwapo Ishara kwa (watu wa nchi ya) Sabai katika maskani yao...”

Kisha alilifasiri kwa Kauli Yake,

جَنَّاتٍ عَن يَمِينٍ وَشِمَالٍ^ط

“...bustani mbili, kulia na kushoto.”

Yaani, katika pande mbili za milima miwili, na mji ulikuwa baina yao,

كُلُوا مِن رِّزْقِ رَبِّكُمْ وَاشْكُرُوا لَهُ ۗ بَلَدَةٌ طَيِّبَةٌ وَرَبُّ غَفُورٌ

“Kuleni katika riziki ya Mwenyezi Mungu, na mumshukuru. Mji mzuri na Mola Mlezi Aliye Msamehevu.”

Yaani ni Msamehevu kwenu ikiwa mtadumu katika Tauhidi Yake. Kauli ya Allah تعالى:

فَاعْرَضُوا

“Lakini wakaacha.”

¹ At-Tabari 20:376.

Yaani, kumpwekesha na kumuabudu Allah تعالى na kumshukuru kwa neema Alizowapatia, na wakaanza kuliabudu jua badala ya Allah تعالى. Ni sawa na Hudihudi alivyomuambia Sulayman عليه السلام:

وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَأٍ بِنَبِيٍّ يَقِينٍ ﴿٢٢﴾ إِنِّي وَجَدْتُ أَمْرًا تَمَلِكُهُمْ وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ
 وَهَذَا عَرْشٌ عَظِيمٌ ﴿٢٣﴾ وَجَدْتُهَا وَقَوْمَهَا يَسْجُدُونَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَزَيَّنَ لَهُمُ
 الشَّيْطَانُ أَعْمَالَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيلِ فَهُمْ لَا يَهْتَدُونَ ﴿٢٤﴾

“...na ninakujia hivi kutoka nchi ya Sabai, na nakuletea khabari za yakini. Hakika mimi nimemkuta mwanamke anawatawala, naye amepewa kila kitu, na anacho kiti cha enzi kikubwa. Nimemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia Njia. Kwa hivyo hawakuongoka.” (27:22-24)

Kauli ya Allah تعالى:

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ سَيْلَ الْعَرِمِ

“Tukawapelekea mafuriko makubwa...”

Makusudio ya Al-'Aram, ni maji. Baadhi yao, akiwemo Ibn 'Abbas, Wahb bin Munabbih, Qatadah na Adh-Dhahhak walisema kwamba pindi Allah تعالى Alipotaka Kuwaadhibu kwa Kuwapelekea mafuriko, Aliwatuma wadudu wa ardhi kwenye bwawa, mapanya wakubwa ambao walifanya tundu humo.¹ Wahb bin Munabbih alisema, “Walikuta katika maandiko kwamba bwawa hilo lingeweza kubomolewa kwa sababu ya mapanya haya makubwa. Kwa hivyo, walileta mapaka kwa muda, lakini amri ilipopitishwa, mapanya yaliyashinda mapaka na yakaenda katika bwawa, na kutoboa tundu, likabomoka.”² Qatadah na wengine walisema, “Panya wakubwa ni wa jangwani. Waliguguna chini ya bwawa mpaka likadhoofika, kisha muda wa mafuriko ukawadia na maji yakalipiga jengo na kulibomoa. Maji yakatiririka kwenda bondeni na kukiangamiza kila kitu kilichokuwa katika mapito yake – majengo, miti, n.k.”³

¹ At-Tabari 20:378, 380.

² At-Tabari 20:381.

³ At-Tabari 20:381.

وَبَدَّلْنَاهُمْ بِجَنَّتَيْمَ جَنَّتَيْنِ ذَوَاتِ أُكُلٍ خَمْطٍ

“...na Tukawabadilishia badala ya bustani zao hizo kwa bustani nyengine zenye matunda makali machungu...”

Ibn ‘Abbas, Mujahid, ‘Ikrimah, ‘Ata Al-Khurasani, Qatadah na As-Suddi رضي الله عنهم walisema, “Mti wa mswaki Salvadora pervica.”¹

وَأَنْلٍ

“...na mivinje...”

Al-‘Awfi amesema, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: “Ni mkwaju.” Wengine walisema: “Ni mti unaoshabihiana na mkwaju.” Pia ilisemekana kwamba ni magunga. Allah تعالى Ndiye Mjuzi

وَشَيْءٍ مِّن سِدْرٍ قَلِيلٍ

“...na kidogo katika miti ya kunazi.”

Kwa sababu ndiyo iliyokuwa miti mizuri zaidi ya kubadilishia bustani.

وَشَيْءٍ مِّن سِدْرٍ قَلِيلٍ

“...na kidogo katika miti ya kunazi.”

Haya yalizipata bustani hizo baada ya matunda yake kuiva, mandhari nzuri, vivuli vinene na mito itiririkayo, ilibadilika na kuwa na miti ya araaki, migunga na mikunazi iliyokuwa na miiba mingi na matunda machache. Hayo ni kwa sababu ya kumkufuru na kumshirikisha Allah تعالى, kuukataa kwao ukweli na wakaifuata batili. Allah تعالى Amesema:

ذَٰلِكَ جَزَيْنَهُمْ بِمَا كَفَرُوا ۗ وَهَلْ نُجْزِي إِلَّا الْكَافِرِينَ ﴿٣٧﴾

“Hayo Tuliwalipa kwa sababu ya walivyokufuru. Nasi kwani Tunamuadhibu isipokuwa anayekufuru?”

¹ At-Tabari 20:282, 383.

Yaani, 'Tuliwaadhibu mintarafu ya kufuru yao.' Mujahid alisema, "Allah hamuadhibu yeyote, isipokuwa makafiri."¹ Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema: "Allah Amesema kweli, hapana wa kuadhibiwa kwa mithili ya kitendo (cha dhambi), isipokuwa makafiri."

وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ الْقُرَىٰ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا قُرَىٰ ظَنَهْرًا وَقَدَرْنَا فِيهَا أَلْسِيْرًا سِيرُوا فِيهَا لَيَالِيًۭا وَأَيَّامًا ءَامِنِينَ ﴿١٥﴾ فَقَالُوا رَبَّنَا بَعِدْ بَيْنَ أَسْفَارِنَا وَظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ فَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ وَمَزَقْنَاهُمْ كُلَّ مُمَزَّقٍ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُوْرٍ ﴿١٦﴾

18. "Na baina yao na miji mingine Tuliyoibariki Tuliweka miji iliyo dhaahiri, na Tukaweka humo vituo (vya safari). Tukawaambia: Nendeni humo usiku na mchana kwa amani."

19. "Lakini wakasema: Mola Wetu Mlezi! Weka mwendo mrefu baina ya safari zetu. Na wakazidhulumu nafsi zao. Basi Tukawafanya ni masimulizi tu, na Tukawatawanya tawanya. Hakika katika hayo bila ya shaka zimo Ishara kwa kila mwenye kusubiri sana na akashukuru."

Biashara ya Sabaa na Kuangamizwa Kwao

Allah تعالى Anaeleza furaha, maisha ya anasa, faraja, miji yenye neema, mahali pa amani na miji iliyokaribiana sana na kuungana, pamoja na miti mingi, mazao na matunda yake, kiasi kwamba, mwenye kusafiri huko hakuwa na haja ya kubeba masurufu wala maji, bali popote alipotaremka alipata maji na matunda, na waliweza kujipumzisha mchana katika mji mmoja na kupitisha usiku katika mji mwingine, kulingana na mahitaji yao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ الْقُرَىٰ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا

"Na baina yao na miji mingine Tuliyoibariki Tuliweka..."

Mujahid, Al-Hasan, Sa'id bin Jubayr na Malik, ambaye aliisimulia kutoka kwa

¹ Al-Baghawi 3:555.

Zayd bin Aslam, na Qatadah, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Ibn Zayd na wengine, wote walisema kuwa hii inamaanisha miji ya Syria. Maana yake, walikuwa wakisafiri baina ya Yemen na Syria kupitia miji ambayo ilikuwa rahisi kuonekana na kuunganishwa baina yao.¹ Al-'Awfi alieleza kwamba Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Ni miji Tuliyoibariki kwa kuiweka Jerusalem baina yao."²

قُرَى ظَهْرَةَ

"...miji iliyo dhaahiri..."

Yaani, bayana, waziwazi ambayo wasafiri wanajua, mchana wanapumzika katika mmojawapo na kulala usiku katika mwingine.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَقَدَرْنَا فِيهَا السَّيْرَ

"...na Tukaweka humo vituo (vya safari)."

Yaani, Tuliweka kulingana na mahitaji ya wasafiri,

سَمِرُوا فِيهَا لَيْالِي وَأَيَّامًا ءَامِنِينَ

"...Nendeni humo usiku na mchana kwa amani."

Yaani kuna usalama kwa ajili yao katika kwenda kwao usiku na mchana.

فَقَالُوا رَبَّنَا بَعِدَ بَيْنَ أَسْفَارِنَا وَظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ

"Lakini wakasema: Mola Wetu Mlezi! Weka mwendo mrefu baina ya safari zetu. Na wakazidhulumu nafsi zao."

Wengine walisoma neno *baa'id* kwa kuondoa herufi *alif* iliyo baada ya *ba* na kuitia shada herufi *'ain*. Maana yake ni kwamba walikanusha neema hizi. Ni sawa na alivyosema Ibn 'Abbas, Mujahid, Al-Hasan na wengine رضي الله عنهم: "Walipendelea kusafiri masafa marefu katika mwitu ulio mtupu ambapo wangelihitajika kubeba masurufu na vifaa vya safarini na kusafiri katika joto kali na khofu."

¹ At-Tabari 20:386, 387.

² At-Tabari 20:386.

فَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ وَمَزَقْنَاهُمْ كُلَّ مُمَزَّقٍ

“Basi Tukawafanya ni masimulizi tu, na Tukawatawanya tawanya.”

Yaani, Tuliifanya kuwa hadithi ya watu na jambo la kuzungumzwa usiku, namna Allah Alivyopanga mipango dhidi yao na Kuwatawanya baada ya kuwa kwao pamoja katika maisha ya faraja, mazoea, walisambaa katika nchi mbalimbali.

Kwa ajili hii, Waarabu huwaambia kaumu pindi wakitawanyika: “Wametawanyika kama Sabai, wamekwenda kila mahali.”

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ

“Hakika katika hayo bila ya shaka zimo Ishara kwa kila mwenye kusubiri sana na akashukuru.”

Yaani, hakika katika adhabu na shida zilizowasibu watu hawa, kubadilishwa kwa neema na kugeuzwa afya, ni adhabu kutokana na ukafiri na madhambi waliyoyafanya. Haya ni mafunzo na dalili kwa kila mja mwenye subira katika misiba, mwenye kushukuru juu ya neema. Imamu Ahmad alimnukuu Sa'd bin Abu Waqqaas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«عَجِبْتُ مِنْ قَضَاءِ اللَّهِ تَعَالَى لِلْمُؤْمِنِ إِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ حَمِدَ رَبَّهُ وَشَكَرَ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ مُصِيبَةٌ حَمِدَ رَبَّهُ وَصَبَرَ، يُؤَجِرُ الْمُؤْمِنُ فِي كُلِّ شَيْءٍ حَتَّى فِي اللَّقْمَةِ يَرْفَعُهَا إِلَى فِيهِ
أَمْرًا بِهِ»

“Nimestaajibishwa na hukumu ya Allah kwa Muumini, akipatwa na kheri, humhimidi Mola Wake na kumshukuru, akipatwa na msiba humhimidi Mola Wake na kusubiri. Muumini hulipwa katika kila kitu, hata tonge analolipeleka kinywani kwa mkewe.”¹

Hii ilinukuliwa na An-Nasai katika *Al-Yawm wal-Laylah*.² Pia ina uthibitisho katika *Sahih* Mbili, kutokana na Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه:

¹ Ahmad 1:173.

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:263.

«عَجَبًا لِلْمُؤْمِنِ لَا يَقْضِي اللَّهُ تَعَالَى لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ شَكَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ صَبَرَ فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَلَيْسَ ذَلِكَ لِأَحَدٍ إِلَّا لِلْمُؤْمِنِ»

“Ni ajabu kwa muumini, Allah Hamhukumii jambo, isipokuwa huwa la kheri kwake. Akipatwa na la furaha hushukuru. Hiyo huwa ni kheri kwake. Akipatwa na la madhara, husubiri. Hiyo nayo huwa kheri kwake. Wala hayo si kwa yeyote, bali kwa Muumini.”¹

Qatadah alisema juu ya Aya,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ

“Hakika katika hayo bila ya shaka zimo Ishara kwa kila mwenye kusubiri sana na akashukuru.”

Mutarrif alikuwa akisema: “Ni baraka iliyoje kwa mja mwenye kushukuru, mwenye subira. Akipatiwa kitu hushukuru, na akijaribiwa, hukabiliana na hali hiyo kwa subira.”²

وَلَقَدْ صَدَقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ فَاتَّبَعُوهُ إِلَّا فَرِيقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٠﴾ وَمَا كَانَ لَهُ عَلَيْهِمْ مِّن سُلْطٰنٍ إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يُؤْمِنُ بِالْآخِرَةِ مِمَّنْ هُوَ مِنهَا فِي شَكٍّ ۗ وَرَبُّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ ﴿٢١﴾

20. “Na bila ya shaka Iblisi alihakikisha ile dhana yake juu yao. Nao walimfuata, isipokuwa kundi la Waumini wa kweli kweli.”

21. “Na yeye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao, ila kwa sababu ya kuwajaribu Tujue nani mwenye kuamini Akhera, na nani anaye tilia shaka. Na Mola Wako Mlezi ni Mwenye Kuhifadhi kila kitu.”

¹ Fat’h Al-Bari 6:263.

² Muslim 4:1992.

Namna Dhana ya Ibilisi Inasadikishwa na Makafiri

Baada ya kutaja kisa cha Sabaa na mambo waliyokuwa nayo juu ya kufuata matamano yao na Shetani, Allah تعالی Alitoa khabari zao na mithili yao katika waliomfuata Ibilisi na tamaa zao na kukhalifu hekima na uongofu wa kweli.

Allah تعالی Amesema:

وَلَقَدْ صَدَقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ

“Na bila ya shaka Ibilisi alihakikisha ile dhana yake juu yao.”

Ibn ‘Abbas na wengine رضي الله عنهم¹ wamesema kuwa Aya hii ni sawa na Aya ambayo Allah تعالی Anatuambia juu ya Ibilisi ambaye alikataa kumsujudia Adam عليه السلام, kisha akasema:

أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْت عَلَىٰ لَيْلٍ أَخْرَجْتَ إِلَىٰ يَوْمِ الْآفِئِمَةِ لَأَحْتَنِكْ ۖ ذُرِّيَّتَهُ إِلَّا قَلِيلًا

“Akasema: Hebu nambie khabari ya huyu uliyemtukuza juu yangu. Ukiniakhirisha mpaka Siku ya Kiyama, hapana shaka nitawaangamiza dhuriya yake wasipokuwa wachache tu.” (17:62)

ثُمَّ لَأَتَيْنَهُمْ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ أَيْمَانِهِمْ وَعَنْ شَمَائِلِهِمْ ۗ وَلَا تَجِدُ أَكْثَرَهُمْ شَاكِرِينَ

“Kisha nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani.” (7:17)

Kauli ya Allah تعالی:

وَمَا كَانَ لَهُمْ عَلَيْهِمْ مِنْ سُلْطٰنٍ

“Na yeye hakuwa na mamlaka yoyote juu yao...”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa inamaanisha, ushahidi.

¹ At-Tabari 20:392.

Kauli ya Allah تعالى:

إِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يُؤْمِنُ بِالْآخِرَةِ مِمَّنْ هُوَ مِنْهَا فِي شَكٍّ

“...ila kwa sababu ya Kuwajaribu Tujue nani mwenye kuamini Akhera, na nani anayetilia shaka.”

Yaani, kwa hakika, Tulimpa mamlaka juu yao ili kumdhahirisha mwenye kuamini Akhera, Kiyama, Hesabu na malipo. Kwa ajili hiyo, anaifanya vyema ibada kwa Mola Wake Mlezi duniani na Kuwatofautisha na walio katika mashaka (nayo). Kauli ya Allah تعالى:

وَرَبُّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ

“Na Mola Wako Mlezi ni Mwenye Kuhifadhi kila kitu.”

Inamaanisha kuwa pamoja na Kuhifadhi Kwake, wafuasi wa Ibilisi wamepotea, lakini kwa Uhifadhi na Uangalizi Wake Waumini wanaowafuata Mitume walisalimika.

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ رَعَيْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ
وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا هُمْ فِيهِمَا مِنْ شَرِكٍ وَمَا لَهُ مِنْ ظَهِيرٍ ﴿٢٢﴾ وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ
عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ ۗ حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ عَنْ قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۗ قَالُوا الْحَقُّ
وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٢٣﴾

22. “Sema: Waite mnao wadai kuwa ni badala ya Mwenyezi Mungu. Hawamiliki hata uzito wa chembe katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao.”

23. “Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipokuwa kwa Aliyempa idhini. Hata itapoondolewa hofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola Wenu Mlezi kasema nini? Watasema: Yaliyo kweli! Na Yeye Ndiye Aliye juu, Mkubwa.”

Kushindwa kwa Miungu ya Washirikina.

Allah تعالى Amebainisha kwamba Yeye ni Mungu Mmoja, Mpweke, Mwenye kukusudiwa na viumbe, Ambaye hana wa kufanana wala mshirika, bali Yeye ni Mpweke katika Amri Yake, pasi na mshirika wala mwenye kugombana Naye wala mwenye kumpindua.

Allah تعالى Amesema:

قُلْ أَدْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Sema: Waite mnao wadaia kuwa ni badala ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, katika miungu iliyoabudiwa badala Yake,

لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ

“Hawamiliki hata uzito wa chembe katika mbingu wala ardhi.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِنْ قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾

“Na hao mnaowaomba badala Yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende.” (35:13)

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا لَهُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍَ

“Wala hawana ushirika wowote humo.”

Yaani, hawamiliki chochote, wao peke yao wala katika ushirika,

وَمَا لَهُمْ مِنْهُمْ مِّنْ ظَهِيرٍ

“Wala Yeye Hana msaidizi miongoni mwao.”

Yaani, Allah تعالى Hana msaidizi katika mambo yake kiasi cha Kutaka kusaidiwa na waungu wa uongo, bali viumbe wote wana haja Kwake, ni waja Wake. Kisha Alisema Allah تعالى:

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ^٤

**“Ni nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya Idhini Yake?”
(2:255)**

Yaani, kwa ajili ya Ukubwa, Utukufu na Kibri Chake, yeyote hapati ujasiri wa kufanya uombezi mbele Yake kitu chochote, isipokuwa baada ya Idhini Yake katika jambo hilo la uombezi.

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أِذِنَ لَهُ^٤

“Wala uombezi huo hautamfaa isipokuwa yule atakayekubaliwa na Yeye (Mwenyezi Mungu).” (21:28)

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَكَمْ مِنْ مَلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ

وَيَرْضَى^٢

“Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa Amtakaye na Kumridhia.” (53:26)

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنْ أَرَادَتْهُ مِنْ حَشِيَّتِهِ مُشْفِقُونَ

“Wala hawamuombi yeyote ila yule anayemridhia Yeye, nao kwa ajili ya kumuogopa wananyenyekea.” (21:28)

Kwa ajili hii, ilinukuliwa ndani ya *Sahih* Mbili zaidi ya isnadi moja kutoka kwa Mtume ﷺ, naye ni kiongozi wa wana wa Adam, na ndiye mkubwa kabisa wa wenye kushufaia mbele ya Allah تعالى, kwamba pindi atakaposimama katika *Al-Maqam Al-Mahmud* (Mahali pa kusifika) ili awaombe viumbe wote, pindi Mola wao Atakapokuja kupitisha hukumu juu yao. [Mtume ﷺ] amesema:

فَأَسْجُدْ لِلَّهِ تَعَالَى فَيَدْعُنِي مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَدْعَنِي، وَيَفْتَحْ عَلَيَّ بِمَحَامِدٍ لَا أَحْصِيهَا
الآن، ثُمَّ يُقَالُ: يَا مُحَمَّدُ! ارْفَعْ رَأْسَكَ وَقُلْ تُسْمَعُ، وَاسْمَعُ تُسْمَعُ،

*"Halafu nitasujudu kwa Allah. Ataniacha kadiri ya Atakavyo Yeye Allah. Atanifungulia nizungumze maneno ya kuhimidi ambayo siwezi kuyasema kwa sasa. Kisha kutasemwa: 'Ewe Muhammad! Inua kichwa chako, na useme, utasikilizwa, omba utapewa na omba utakubaliwa."*¹

حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۖ قَالُوا الْحَقُّ

"Hata itapoondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola Wenu Mlezi kasema nini? Watasema: Yaliyo kweli!"

Hii pia ni nafasi ya juu sana katika utukufu. Nayo ni kwamba, Allah تعالى Anapozungumza ufunuo, wakazi wa mbinguni watasikia meneno Yake, watatetemeka kwa khofu mpaka wapatawe mfano wa kuzimia. Hii ilikuwa rai ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه, Masruq na wengine.²

حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ عَن قُلُوبِهِمْ

"Hata itapoondolewa khofu kwenye nyoyo..."

Yaani, khofu juu ya hayo huondoka. Ibn 'Abbas na Ibn 'Umar na Abu 'Abdur-Rahman As-Sulami, Ash-Sha'bi, Ibrahim An-Nakha'i, Adh-Dhahhak, Al-Hasan na Qatadah رضي الله عنهم waliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ عَن قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ۖ قَالُوا الْحَقُّ

"Hata itapoondolewa khofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola Wenu Mlezi kasema nini? Watasema: Yaliyo kweli!"

Anasema: "Pindi khofu itakapoondolewa kutoka nyoyoni mwao." Baadhi ya Salaf walisoma kwa neno, "Furri^{gha}," kwa herufi *ghain*, na maana yake inarejea katika neno la kwanza, Fuzzi'a. Baada ya hayo kutokea, baadhi yao watawauliza wenzao: "Ni nini alichokisema Mola Wenu."

¹ Fat'h Al-Bari 8:248, Muslim 1:185.

² At-Tabari 20:396.

Malaika wanaobeba Arshi watawaambia walio karibu yao, na wao watawafikishia watakaowafuatia, kisha wanaowafuatia kwa chini yao, na kuendelea, mpaka khabari ziwafikie wakazi wa mbingu ya dunia. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

قَالُوا الْحَقُّ

“Watasema: Yaliyo kweli!”

Yaani, wataeleza juu ya Aliyoyasema pasi na ziada wala nuksani.

وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

“Na Yeye Ndiye Aliye juu, Mkubwa.”

Al-Bukhari alinukuu katika kuitafsiri Aya hii tukufu ndani ya *Sahih* yake, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema: “Nabii wa Allah ﷺ amesema,

«إِذَا قَضَى اللَّهُ تَعَالَى الْأَمْرَ فِي السَّمَاءِ صَرَبَتْ الْمَلَائِكَةُ بِأَجْنِحَتِهَا خُضْعَانًا لِقَوْلِهِ، كَأَنَّهُ سُلَيْلَةٌ عَلَى صَفْرَانٍ، فَإِذَا فُزِعَ عَنِ قُلُوبِهِمْ قَالُوا: مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ؟ قَالُوا لِلَّذِي قَالَ: الْحَقُّ، وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ، فَيَسْمَعُهَا مُسْتَرِقُ السَّمْعِ، وَمُسْتَرِقُ السَّمْعِ هَكَذَا بَعْضُهُ فَوْقَ بَعْضٍ - وَوَصَفَ سَفِيَانُ بِيَدِهِ فَحَرَّفَهَا، وَنَشَرَ بَيْنَ أَصَابِعِهِ - فَيَسْمَعُ الْكَلِمَةَ فَيُلْقِيهَا إِلَى مَنْ تَحْتَهُ، ثُمَّ يُلْقِيهَا الْآخَرَ إِلَى مَنْ تَحْتَهُ، حَتَّى يُلْقِيَهَا عَلَى لِسَانِ السَّاجِرِ أَوْ الْكَاهِنِ، فَرُبَّمَا أَذْرَكَهُ الشَّهَابُ قَبْلَ أَنْ يُلْقِيَهَا، وَرُبَّمَا أَلْقَاهَا قَبْلَ أَنْ يُذْرِكَهُ، فَيَكْذِبُ مَعَهَا مِائَةً كَذِبَةٍ فَيَقَالُ: أَلَيْسَ قَدْ قَالَ لَنَا يَوْمَ كَذَا وَكَذَا، كَذَا وَكَذَا؟ فَيُصَدِّقُ بِتِلْكَ الْكَلِمَةِ الَّتِي سَمِعَتْ مِنَ السَّمَاءِ»

“Pindi Allah Akilihukumu jambo mbinguni, Malaika hupiga mbawa zao kwa kuinyenyekea Kauli Yake na kufanya sauti kama ya mnyororo unaogonga katika mwamba laini. Khofu ikiwaingia katika nyoyo zao, husema: ‘Ni nini Alichokisema Mola Wenu?’ Husema ambalo Amelisema: ‘Ni ukweli, na Yeye ni Wa juu zaidi, Mkuu zaidi.’ Kisha mwenye kusikiliza husikia haya, na wanaoyasikia haya, namna hii, baadhi yao juu wenzao – Sufyan (mmoja wa wasimulizi) akaeleza kwa kuonesha kwa mkono wake, akiunyoosha na vidole akiviachanisha - basi husikiliza maneno na kuyapeleka kwa aliye chini yake, na huyo mwingine anayapeleka kwa wa chini yake, mpaka

yanaufikia ulimi wa mchawi au kuhani. Pengine kimondo kinaweza kumpiga kabla hajayafikisha, na pengine huyafikisha kabla hakijampiga. Kisha huongopa pamoja nayo uongo mia hayo maneno, lakini itasemwa, 'Kwani hakutuambia siku kadha wa kadha, kuhusu kadha wa kadha?' Kwa hivyo anasadikiwa na wengine kwa maneno ambayo yalisikilizwa kutoka mbinguni."

Hii ilinukuliwa na Al-Bukhari, na si Muslim.¹ Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah, pia waliinukuu.² Allah Ndiye Mjuzi.



¹ Fat'h Al-Bari 8:398.

² Abu Dawud 4:288, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:90, Ibn Majah 1:69.

* قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّهُ
 وَإِنَّا أَوْ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٢٤﴾
 قُلْ لَا تُسْأَلُونَ عَمَّا أَجْرَمْنَا وَلَا تُنْشَأُ عَمَّا تَعْمَلُونَ
 قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ
 الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿٢٥﴾ قُلْ أَرُونِي الَّذِينَ أَلْحَقْتُمْ بِهِ
 شُرَكَاءَ كَلَّا بَلْ هُوَ اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٦﴾ وَمَا
 أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ
 النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٧﴾ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ
 إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٨﴾ قُلْ لَكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا
 تَسْتَعْتِرُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَقْدِمُونَ ﴿٢٩﴾ وَقَالَ
 الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِهَذَا الْقُرْآنِ وَلَا بِالَّذِي بَيْنَ
 يَدَيْهِ ۗ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِندَ رَبِّهِمْ
 يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ الَّذِينَ
 اسْتَضَعُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنشَأَ لَكُم مَّوْمِنِينَ ﴿٣٠﴾
 قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعُوا أَخُنَّ صَدَدْتُمْ
 عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ۗ بَلْ كُنتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٣١﴾ وَقَالَ
 الَّذِينَ اسْتَضَعُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرَ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ
 إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَندَادًا ۗ وَأَسْرُوا
 النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي أَعْنَاقِ الَّذِينَ
 كَفَرُوا ۗ هَلْ يُحْزَنُونَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٢﴾

* قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّهُ ۗ وَإِنَّا أَوْ
 فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٢٤﴾
 قُلْ لَا تُسْأَلُونَ
 عَمَّا أَجْرَمْنَا وَلَا تُنْشَأُ عَمَّا تَعْمَلُونَ
 قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ
 بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿٢٥﴾
 قُلْ أَرُونِي الَّذِينَ أَلْحَقْتُمْ بِهِ
 شُرَكَاءَ كَلَّا ۗ بَلْ هُوَ اللَّهُ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ﴿٢٦﴾

24. "Sema: Ni nani anaye-
 kuruzukuni kutoka mbi-
 nguni na kwenye ardhi?
 Sema: Mwenyezi Mungu!
 Na hakika sisi au nyinyi bila
 ya shaka tuko kwenye
 uwongofu au upotofu ulio
 uliodhahiri."

25. "Sema: Nyinyi hamta-
 ulizwa kwa makosa tuliyo-
 yafanya, wala sisi hatuta-
 ulizwa kwa mnayoyatenda
 nyinyi."

26. "Sema: Mola Wetu
 Mlezi Atatukusanya, kisha

Atatuhukumu kwa haki; na Yeye Ndiye Hakimu Mwenye kujua."

27. "Sema: Nionesheni mliowaunganisha naye kuwa washirika. Haiwezekani! Bali Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima."

Allah Hana Mshiriki Katika Jambo Lolote

Allah تعالى Anaeleza kwamba Amepitisha hukumu kwamba Yeye ni Mpweke katika Kuumba, Utoaji riziki na Uungu. Kama ambavyo walikuwa wakikiri kwamba wao hawatoi riziki mbinguni wala ardhini, yaani kwa kuteremsha mvua na kuotesha mimea, isipokuwa Allah. Kadhalika watambue kwamba hapana mola wa haki kuabudiwa ghairi Yake. Kauli ya Allah تعالى:

وَأِنَّا أَوْ إِيَّاكُمْ لَعَلَّ هُدًى أَوْ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

"Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu ulio dhahiri."

Hii ni katika namna ya kuzunguka na kuenea kwamba kundi moja linadanganya, na jingine liko katika ukweli. Hakuna njia ya kukufanyeni nyinyi na sisi, sote kuwa katika uongofu au katika upotevu, bali kundi moja kati yetu ndilo liko sahihi, nasi tumekwishatoa ushahidi juu ya tauhidi na kuonesha ubatilifu wa yale mliyo nayo katika kumshirikisha Allah تعالى. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَأِنَّا أَوْ إِيَّاكُمْ لَعَلَّ هُدًى أَوْ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

"Na hakika sisi au nyinyi bila ya shaka tuko kwenye uwongofu au upotofu ulio dhahiri."

Qatadah alisema, "Masahaba wa Muhammad ﷺ waliwaambia washirikina kuhusu masuala haya: 'Wallah! Sisi na nyinyi hatutakuwa tukifuata kitu cha namna moja, ni upande mmoja tu kati yetu ndio waongofu kweli.'"¹ 'Ikrimah na Ziyad bin Abu Maryam walisema: "Yaani, sisi tumeongozwa kikweli, ilhali nyinyi mko katika batili dhahiri."²

¹ At-Tabari 20:401.

² At-Tabari 20:401.

Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ لَا تُسْأَلُونَ عَمَّا أَجْرَمْنَا وَلَا نُسْأَلُ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

“Sema: Nyinyi hamtaulizwa kwa makosa tuliyoyafanya, wala sisi hatutaulizwa kwa mnayoyatenda nyinyi.”

Maana yake, kuwakataa, yaani nyinyi si miongoni mwetu, wala sisi si miongoni mwenu, bali tunakulinganieni mje kwa Allah تعالى na kwenye Tauhidi Yake na kumpwekeshea ibada Kwake tu. Ikiwa mtaitika, basi nyinyi ni miongoni mwetu na si miongoni mwenu. Ikiwa mtakataa, basi sisi tuko mbali nanyi, nanyi mko mbali nasi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ أَنْتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

“Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina amali yangu, na nyinyi mna amali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo.” (10:41)

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿١٧﴾ لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿١٨﴾ وَلَا أَتَّبِعُ عِبَادُونَ مَا أَعْبُدُ ﴿١٩﴾ وَلَا أَنَا عَابِدٌ مَا عَبَدْتُمْ ﴿٢٠﴾ وَلَا أَتَّبِعُ عِبَادُونَ مَا أَعْبُدُ ﴿٢١﴾ لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِيَ دِينِ ﴿٢٢﴾

“Sema: Enyi makafiri! Siabudu mnacho kiabudu; Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu. Wala sitaabudu mnachoabudu. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu. Nyinyi mna dini yenu, nami nina Dini yangu.” (109:1-6)

Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا

“Sema: Mola wetu Mlezi Atatukusanya...”

Yaani, katika Siku ya Kiyama, Atawakusanya viumbe wote katika uwanja mmoja, halafu Atahukumu kwa haki na kwa uadilifu baina yetu. Kila mwenye amali atalipwa kulingana nayo, kama njema atalipwa kheri, na kama mbaya basi ni shari. Siku hiyo mtatambua kwamba utukufu, ushindi na furaha ya milele ni ya kina nani. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُنْفِرُونَ ﴿١٤﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
فَهُمْ فِي رَوْضَةٍ يُحْبَرُونَ ﴿١٥﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَاءِ الْآخِرَةِ
فَأُولَٰئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿١٦﴾

“Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika. Ama walioamini na wakatenda mema watafurahishwa katika Bustani. Na ama waliokufuru na wakazikanusha Ishara Zetu na mkutano wa Akhera, hao basi watahudhurishwa katika adhabu.” (30:14-16)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ

“...na Yeye Ndiye Hakimu Mwenye Kujua.”

Yaani, Hakimu Mwadilifu, Mwenye Kujua ukweli wa mambo, Kauli ya Allah:

قُلْ أَرُونِي الَّذِينَ أَلْحَقْتُمْ بِهِ شُرَكَاءَ ۗ

“Sema: Nionesheni mliowaunganisha naye kuwa washirika.”

Yaani, Nionesheni miungu hii ambayo mmeifanya kuwa washindani wa Allah تعالى na mkaifanya kuwa inalingana Nae,

كَلَّا ۗ

“Hasha!”

Yaani, hana mfanowe wala mpinzani, wala mshirika wala mlingani,

بَلْ هُوَ اللَّهُ

“Bali Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu...”

Yaani, Mmoja na Mpweke Ambaye hana mshirika,

الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“...Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Yaani, Mwenye Nguvu Ambaye Amekitiisha na Kukidhibiti kila kitu. Ni Mwenye Hikima katika Matendo, Kauli, Sharia na Kudura Zake. Ametukuka, ni Mkuu na Ametakasika dhidi ya wanayoyasema. Allah تعالى Ndiye Mjuzi.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٨﴾
 وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هٰذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٩﴾ قُلْ لَّكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا
 تَسْتَجِرُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَقْدِمُونَ ﴿٣٠﴾

28. "Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mtoaji wa habari nzuri na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui."

29. "Na wanasema: Ahadi hii itakuwa lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?"

30. "Sema: Nyinyi mnayo miadi ya Siku ambayo hamtaakhirika nayo hata kwa saa moja, wala hamtaitangulia."

Muhammad ﷺ ametumwa kwa Watu Wote

Allah تعالى Anamuambia mja na Mtume wake, Muhammad ﷺ,

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا

"Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji."

Yaani, wa viumbe wote ambao wanawajibika kwa amali zao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

قُلْ يٰٓأَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

"Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote..."
 (7:158),

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٢٥﴾

"Ametukuka Aliyeteremsha Furqani kwa mja Wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote." (25:1),

بَشِيرًا وَنَذِيرًا

"...Mtoaji wa habari nzuri na mwonyaji."

Yaani, wabashirie wale watakaokutii kwamba wataingia Peponi, na kuwaonya watakaokuasi kuwa wataingia Motoni,

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

"Lakini watu wengi hawajui."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَمَا أَكْثَرَ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

**"Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi."
(12:103)**

وَإِنْ تُطِيعْ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

**"Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza
na Njia ya Mwenyezi Mungu." (6:116)**

Muhammad bin Ka'b aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَّةً لِّلنَّاسِ

"Na Hatukukutuma ila kwa watu wote..."

Qatadah amesema kuhusu Aya hii, "Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ kwa Waarabu na wasiokuwa Waarabu, hivyo, mtukufu wao zaidi kwa Allah تعالى ni alie mchamungu zaidi."¹ Katika Sahih Mbili kuna Hadithi ya Jabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، فَأَيُّمَا رَجُلٍ مِنْ أُمَّتِي أَدْرَكْتُهُ الصَّلَاةَ فَلْيُصَلِّ، وَأَجَلْتُ لِي الْغَنَائِمُ وَلَمْ تَجُلْ لِأَحَدٍ قَبْلِي، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

¹ At-Tabari 20:405

"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa Nabii yeyote kabla yangu. Nimefanywa kuwa mshindi kwa njia ya hofu (ya kuwatishia maadui) kwa masafa ya mwendo wa mwezi mmoja, na ardhi imefanywa kuwa mahali pa kusali na pa kujitoharishia. Basi mahali popote mtu anapofikiwa na Sala basi asali. Nimehalalishiwa ghanima, na hakuhalalishiwa yeyote kabla yangu. Nimepewa uombezi (shufaa). Na ilikuwa kwamba kila Nabii alipelekwa kwa kaumu yake, mimi nimetumwa kwa watu wote."¹

Katika *Sahih*, kadhalika kuna Hadithi kwamba Mtume ﷺ amesema:

«بُعِثْتُ إِلَى الْأَسْوَدِ وَالْأَحْمَرِ»

"Nimetumwa kwa wekundu na weusi."

Mujahid alisema, Inamaanisha, kwa majini na wanadamu."² Wengine walisema: Inamaanisha Waarabu na wasio Waarabu. Maana zote ni sahihi.

Makafiri Walivyouliza Kuhusu Lini Kiyama Kitatukia

Kisha, Allah تعالى Anaeleza kuhusu makafiri walivyopinga kusimama kwa Kiyama:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٠﴾

"Na wanasema: Ahadi hii itakuwa lini, ikiwa nyinyi mnasema kweli?"

Aya hii, ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ هُمْ عَنْ آيَاتِنَا مُشْفِقُونَ ﴿٤١﴾ أَمْ نَجْعَلُهَا لَكُمْ آيَةً وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٢﴾

"Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli." (42:18)

¹ Fat'h Al-Bari 1:519, Muslim 1:370.

² Ahmad 5:145.

Kisha, Allah تعالى Amesema,

قُلْ لَكُمْ مِيعَادُ يَوْمٍ لَا تَسْتَعْرِفُونَ عَنْهُ سَاعَةً وَلَا تَسْتَقْدِمُونَ ﴿٢٤﴾

“Sema: Nyinyi mnayo miadi ya Siku ambayo hamtaakhirika nayo hata saa moja, wala hamtaitangulia.”

Yaani, ipo miadi kwa ajili yenu, ambayo imewekewa muda wake ulioandaliwa na kuandikwa. Hauongezwi wala haupunguzwi. Itakapofika, haitaakhirishwa kwa saa wala kutangulizwa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ ﴿٧١﴾

“Hakika muda wa Mwenyezi Mungu utapofika haucheleweshwi.”
(71:4)

وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مُّعَدودٍ ﴿٧١﴾ يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ فَمِنْهُمْ شَقِيحٌ
وَسَعِيدٌ ﴿٧٢﴾

“Na Sisi hatuiahirishi ila kwa muda unaohisabiwa. Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa Idhini Yake Mwenyezi Mungu. Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.” (11:104-105)

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِهَذَا الْقُرْآنِ وَلَا بِالَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ ۗ وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ
الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ الَّذِينَ
اسْتَضَعُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ
اسْتَضَعُوا لَحْنٌ صَدَدْتُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ۗ بَلْ كُنْتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٧٣﴾ وَقَالَ
الَّذِينَ اسْتَضَعُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرَ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ
وَجَعَلَ لَهُ أَندَادًا ۗ وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأُوا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَعْلَىٰ فِي أَعْنَاقِ الَّذِينَ
كَفَرُوا ۗ هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٤﴾

31. "Na walisema wale waliokufuru: Hatutaiamini Qur'ani hii, wala yaliyokuwa kabla yake. Na ungelibaona madhalimu watapo simamishwa mbele ya Mola Wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia waliotakabari: Lau kuwa si nyinyi, bila ya shaka sisi tungelikuwa Waumini."

32. "Waliotakabari watawaambia wanyonge: Kwani sisi ndio tuliokuziieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe mlikuwa waovu."

33. "Na wanyonge watawaambia waliotakabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu. Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliyokuwa wakiyatenda?"

Kuafikiana Makafiri duniani juu ya kuukataa ukweli na watakavyogombana Siku ya Kiyama

Allah تعالیٰ Anaeleza juu ya kuzidi sana kwa uovu wa makafiri na ukaidi wao wa kushikilia jambo la kutoamini Qur'an Tukufu na yale iliyoyaeleza kuhusu suala la kurejea. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِهَذَا الْقُرْآنِ وَلَا بِالَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ^٥

"Na walisema waliokufuru: Hatutaiamini Qur'ani hii, wala yaliyokuwa kabla yake."

Katika Kuwatisha, Kuwaonya na Kuwajulisha Kuhusu nafasi yao ya udhalili watakayokuwa nayo mbele Yake wakikhasimiana na kubishana wao kwa wao,

يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ الَّذِينَ اسْتَضَعُوا

"...wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia..."

Ambao ni wafuasi,

لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا

“...waliotakabari...”

Miongoni mwao, ambao ni viongozi na wakuu wao,

لَوْلَا أَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ

“...Lau kuwa si nyinyi, bila ya shaka tungelikuwa Waumini sisi.”

Yaani, “Kama msingetuzuia, tungewafuata Mitume na kuamini waliyotuletea. Viongozi na wakuu wao, ambao ndio waliofanya kiburi, watasema:

أَخْنُ صَدَدْتُمْ عَنْ أَلْهَدَى بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ط

“...Kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni?”

Yaani, sisi hatukukufanyieni zaidi ya kwamba tulikuiteni, mkatufuata pasi na dalili wala ushahidi, mkazikhalifu dalili, ushahidi na hoja walizokuja nazo Mitume. Hayo yalisababishwa na matamania yenu. Ilikuwa ni khiyari yenu.’ Watasema:

بَلْ كُنْتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٣٤﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعِفُوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ

“Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu. Na wanyonge watawaambia waliotakabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana...”

Yaani, bali mlikuwa mkitufanyia hila usiku na mchana, mlikuwa mkituhadaa na kutupa matumaini ya uongo, na kutuambia kuwa tulikuwa katika uongofu na kwamba tulikuwa tukifuata jambo la maana, lakini hayo yote ni batili na uongo. Qatadah na Ibn Zayd walisema:

بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ

“...Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana...”

Yaani, “Mlifanya njama usiku na mchana.”¹ Malik alisimulia maelezo sawa na hayo kutoka kwa Ziyad bin Aslam, kwamba maana yake, waliwafanyia vitimbi usiku na mchana.²

¹ At-Tabari 20:408.

² At-Tabari 20:408.

إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَنْدَادًا

“...mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika.”

Yaani, kuwaweka walingani na miungu ya uongo pamoja na Yeye. Mkatujengea shubuha na mambo ya hila yaliyotupoteza,

وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ

“Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu.”

Yaani, wote, viongozi na wafuasi, kila mmoja atayajutia mambo yake yaliyotangulia,

وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي أَعْنَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru.”

Nayo ni minyororo itakayowafunga mikono yao na shingo zao kwa pamoja,

هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Kwani wanalipwa ila kwa waliyokuwa wakiyatenda?”

Yaani, kwa hakika, Tunakulipeni kulingana na amali zenu. Viongozi kwa mujibu wa amali zao, na wafuasi kadhalika.

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ وَلَكِنْ لَا تَعْلَمُونَ

“Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui tu.” (7:38)

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ جَهَنَّمَ لَمَّا سِيقَ إِلَيْهَا أَهْلُهَا تَلَفَّاهُمْ لَهَا، ثُمَّ لَفَحْتَهُمْ لَفْحَةً فَلَمْ يَبْقَ لَحْمٌ إِلَّا سَقَطَ عَلَى الْعُرْقُوبِ»

*"Watu wa Motoni watakaposwagwa kwenda Jahannamu, itawakaribisha kwa miale yake, kisha Moto utazichoma nyuso zao na minofu haitasalia, bali itaanguka katika kano za mvungu wa magoti yake."*¹



¹ *Hilyat Awliyaa* 4:363, ambapo Abu Nu'aym anaonesha kwamba pengine ni *Mawquf*.

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا بِمَا
 أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿٣٤﴾ وَقَالُوا نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا
 وَأَوْلَدًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذِّبِينَ ﴿٣٥﴾ قُلْ إِن رَّبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ
 لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾
 وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِندَنَا زُلْفَىٰ إِلَّا مَن
 ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَأُولَٰئِكَ هُم جَزَاءُ الضَّعِيفِ بِمَا
 عَمِلُوا وَهُمْ فِي الْغُرُفَاتِ ءَامِنُونَ ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ يَسْعَوْنَ فِي
 ءَابِتَاتِنَا مُعْجِزِينَ أُولَٰئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿٣٨﴾ قُلْ
 إِن رَّبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ مِن عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ
 وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِن شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ ۗ وَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ﴿٣٩﴾
 وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ يَقُولُ لِلْمَلَائِكَةِ أَهْتُولَاءِ
 بِأَمْكُرِكُمْ كَأَن لَّهُمْ بَعْدُونَ ﴿٤٠﴾ قَالُوا سُبْحٰنَكَ أَنتَ وَلِيْنَا
 مِن دُونِهِمْ ۗ بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ الْجِنَّ أَكْثَرُهُم بِهِم
 مُّؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾ فَالْيَوْمَ لَا يَمْلِكُ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ نَّفْعًا وَلَا
 ضَرًّا وَنَقُولُ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ
 بِهَا تُكْذِبُونَ ﴿٤٢﴾

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ
 مُتْرَفُوهَا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ
 ﴿٣٤﴾ وَقَالُوا نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا
 وَأَوْلَدًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذِّبِينَ ﴿٣٥﴾ قُلْ
 إِن رَّبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ
 وَيَقْدِرُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلَا
 أَوْلَادُكُمْ بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِندَنَا زُلْفَىٰ
 إِلَّا مَن ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَأُولَٰئِكَ
 هُم جَزَاءُ الضَّعِيفِ بِمَا عَمِلُوا وَهُمْ فِي
 الْغُرُفَاتِ ءَامِنُونَ ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ
 يَسْعَوْنَ فِي ءَابِتَاتِنَا مُعْجِزِينَ أُولَٰئِكَ
 فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ ﴿٣٨﴾ قُلْ إِن
 رَّبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ مِن
 عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ ۗ وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِن
 شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ ۗ وَهُوَ خَيْرُ
 الرَّازِقِينَ ﴿٣٩﴾

34. "Na Hatukumtuma mwonyaji yeyote kwenye mji, ila wenyeji wake waliopewa mali za kidunia kwa starehe walisema: Hakika sisi tunayakataa hayo mliyotumwa nayo."

35. "Na wakasema: Sisi tuna mali nyingi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa."

36. "Sema: Hakika Mola Wangu Mlezi Humkunjulia riziki na Humdhikisha Amtakaye. Lakini watu wengi hawajui."

37. "Na si mali yenu wala watoto wenu watakaokukaribisheni Kwetu, isipokuwa aliyeamini na akatenda mema. Hao basi watapata malipo maradufu kwa walioyafanya. Nao watakuwa salama katika maghorofa."

38. "Na wanaojitahidi kuzipinga Ishara Zetu, wakaona watashinda, hao watahudhurishwa kwenye adhabu."

39. "Sema: Kwa hakika Mola Wangu Mlezi Humkunjulia riziki Amtakaye katika waja Wake na Humdhikisha Amtakaye. Na chochote mtakachokitoa Yeye Atakilipa. Naye ni M-bora wa wanaoruzuku."

Walioishi Maisha ya Anasa Walivyowakataa Mitume na Kughururiwa Kwao na Mali na Watoto

Allah تعالیٰ Anamfariji Mtume Wake ﷺ na Kumuamuru afuate mfano wa Mitume waliokuwepo kabla yake, na Anampa khabari kwamba hakuwahi kutumwa Nabii katika mji wowote, bali walioishi maisha ya anasa walimkataa, na akafuatwa na walio wanyonge. Watu wa Nuh عليه السلام wakamuambia:

أَنْتُمْ مِّنْ لَّكَ وَاتَّبَعَكَ الْأَرْذَالُونَ

**"Je! Tukuamini wewe, hali wanaokufuata ni watu wa chini?"
(26:110)**

وَمَا نَرْنَكَ أَتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادُوا بِادِّئِ الرَّأْيِ

"Wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni, wasiokuwa na akili." (11:27)

Viongozi katika kaumu ya Swalih عليه السلام walisema:

لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوْا لِمَنْ ءَامَنَ مِنْهُمْ اَتَعْلَمُوْنَ اَنْ صٰلِحًا مُّرْسَلٌ مِّن رَّبِّهِ ؕ قَالُوْا اِنَّا بِمَا اُرْسِلَ بِهٖ مُّؤْمِنُوْنَ ﴿٧٦﴾
 كٰفِرُوْنَ ﴿٧٧﴾

“Waheshimiwa wa kaumu yake wanaojivuna waliwaambia wanaoonewa wenye kuamini miongoni mwao: Je, mnaitakidi ya kwamba Saleh ametumwa na Mola Mlezi Wake? Wakasema: Hakika sisi tunayaamini yale aliyotumwa. Wakasema wale wanaojivuna: Sisi tunayakataa hayo mnayoyaamini.” (7:75-76)

Allah تعالى Amesema:

وَكَذٰلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لِّيَقُوْلُوْا اٰهْتُوْلَآءٍ مِّنْ اٰلِهٖهِمْ مِّنْ بَيْنِنَا ؕ اَلَيْسَ اَللّٰهُ بِاَعْلَمَ بِالشّٰكِرِيْنَ ﴿٥٣﴾

“Na hivi ndivyo Tunavyowajaribu wao kwa wao, ili waseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Umewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu Hawajui wanaoshukuru?” (6:53)

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنَا فِيْ كُلِّ قَرْيَةٍ اَكْبَرَ مُجْرِمِيْهَا لِيَمْكُرُوْا فِيْهَا ؕ

“Kadhaalika katika kila mji Tumewajaalia wakubwa wa wakosefu wao wafanye vitimbi ndani yake.” (6:123)

وَإِذَا اُرْدْنَا اَنْ نُهْلِكَ قَرْيَةً اَمَرْنَا مُتْرَفِيْهَا فَفَسَقُوْا فِيْهَا فَحَقَّ عَلَيَّهَا الْقَوْلُ فَمَدَدْنٰهَا تَدْمِيْرًا ﴿١٦﴾

“Na pindi Tukitaka Kuuteketeza mji Huwaamrisha wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo. Basi hapo Kauli huthibiti juu ya mji huo, Nasi Tukauangamiza kwa maangamizo makubwa.” (17:16)

Allah تعالى Amesema katika Aya hii:

وَمَا اَرْسَلْنَا فِيْ قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيْرٍ

“Na Hatukumtuma mwonyaji yeyote kwenye mji...” Yaani Nabii au Mtume,

إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا

“...ila walisema waliojidekeza kwa starehe zao wa mji huo...”

Yaani, wale walioyafurahia maisha ya utajiri na anasa, na nafasi za uongozi. Qatadah amesema: “Ni waasi, wakuu na viongozi katika maovu.”¹

إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ

“...Hakika sisi tunayakataa hayo mliyo tumwa nayo.”

Yaani, hatuyaamini, wala hatuyafuati,

وَقَالُوا خُنُّنْ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَدًا وَمَا خُنُّنْ بِمُعَدِّينَ ﴿٣٥﴾

“Na wakasema: Sisi tuna mali mengi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa.”

Allah تعالى Alizungumzia khabari za washirikina:

أُحْسِبُونَ أَنَّمَا نُعِدُّهُم بِهِ مِنْ مَالٍ وَبَنِينَ ﴿٣٦﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٣٧﴾

“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Yaani, walijifakharisha kwa wingi wa mali na watoto na wakitakidi kwamba hayo ni dalili ya mahaba ya Allah تعالى kwao na Kuwajali, na kwamba hakuwapa haya duniani kisha, Awaadhibu Akhera, wala haya hayatawafika wao. Allah تعالى Amesema:

فَلَا تَعْجَبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَرْهَقَ أَنفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٣٨﴾

“Yasikufurahishe mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.” (9:55)

¹ At-Tabari 20:409.

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا ﴿١١﴾ وَجَعَلْتُ لَهُ مَالًا مَمْدُودًا ﴿١٢﴾ وَبَيْنَ شُهُودًا ﴿١٣﴾
 وَمَهْدَتْ لَهُ تَمَهِيدًا ﴿١٤﴾ ثُمَّ يَطْمَعُ أَنْ أَزِيدَ ﴿١٥﴾ كَلَّا إِنَّهُ كَانَ لِآيَاتِنَا عَنِيدًا ﴿١٦﴾
 سَأَرْهُقُهُ صُعُودًا ﴿١٧﴾

“Niache Peke Yangu na Niliyemuumba; Na Nikamjaalia awe na mali nyingi, Na wana wanaoonekana, Na Nikamtengenezea mambo vizuri kabisa. Kisha anatamai Nimzidishie! Hasha! Kwani hakika yeye alikuwa akizifanyia inadi Aya Zetu! Nitamtesa kwa mateso yasiowezekana.” (74:11-17)

Allah تعالی Alikwishaeleza juu ya mmiliki wa bustani mbili, kwamba alikuwa na mali, matunda na watoto. Kisha, hayo hayakumfaa kitu, bali alipokonywa vyote hivyo duniani, kabla ya Akhera.

Kwa minajili hii, Allah تعالی Amesema katika Aya hii:

قُلْ إِنَّ رَبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ

“Sema: Kwa hakika Mola Wangu Mlezi Humkunjulia riziki na Humdhikisha...”

Kwa Kumpa mali Ampendaye na Asiyempenda. Humpa ufakiri Amtakaye na Kumtajirisha Amtakaye, na Yeye ni Mwenye Hikima timilifu kabisa na ushahidi dhahiri,

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini watu wengi hawajui.”

Halafu Allah تعالی Amesema:

وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ بِالَّتِي تُفَرِّبُكُمْ عِندَنَا زُلْفَىٰ

“Na si mali yenu wala watoto wenu watakaokukaribisheni Kwetu muwe karibu...”

Yaani, huu si ushahidi wa mahaba Yetu kwenu wala kukujalini. Imamu Ahmad, رحمه الله تعالی, alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى لَا يَنْظُرُ إِلَى صُورِكُمْ وَأَمْوَالِكُمْ، وَلَكِنْ إِنَّمَا يَنْظُرُ إِلَى قُلُوبِكُمْ وَأَعْمَالِكُمْ»

"Allah Hatazami sura zenu na mali zenu, bali Anatazama nyoyo zenu na amali zenu."¹

Pia, Muslim na Ibn Majah waliinukuu.² Kwa minajili hii, Allah تعالى Anasema,

إِلَّا مَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا

"...isipokuwa aliyeamini na akatenda mema."

Yaani, kwa hakika, kinachokukaribisheni Kwetu ni, imani na amali njema:

فَأُولَئِكَ هُم جَزَاءُ الَّذِي أَلْضَعِفَ بِمَا عَمِلُوا

"Hao basi watapata malipo maradufu kwa walioyafanya."

Yaani, mema yao huzidishwa mara kumi zaidi mpaka mara mia saba,

وَهُمْ فِي الْعُرْفَتِ ءَامِنُونَ

"Nao watakuwa salama katika maghorofa."

Yaani, wako katika makazi ya juu kabisa ya Peponi wakiwa salama dhidi ya mashaka, khofu, udhia na kila shari ya kujihadhari nayo.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu 'Ali رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ لَعُرْفًا تُرَى ظُهُورُهَا مِنْ بَطُونِهَا، وَيَبْطُونُهَا مِنْ ظُهُورِهَا»

"Hakika Peponi kuna vyumba ambavyo nje yake huonekana wa ndani yake na ndani yake huonekana wa nje yake."

Bedui mmoja akasema: "Hayo kwa ajili ya nani?" Mtume ﷺ akasema:

«لِمَنْ طَيَّبَ الْكَلَامَ، وَأَطْعَمَ الطَّعَامَ، وَأَدَامَ الصِّيَامَ، وَصَلَّى بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ نِيَامَ»

"Kwa mwenye maneno mazuri, akalisha chakula, akadumisha Saumu na akasali usiku ilhali watu wamelala."³

¹ Ahmad 2:539.

² Muslim 4:1987, Ibn Majah 2:1388.

³ Ibn Abu Shaybah 8:437.

وَالَّذِينَ يَسْعَوْنَ فِي آيَاتِنَا مُعْجِزِينَ

“Na wanao jitahidi kuzipinga Ishara Zetu wakaona watashinda...”

Yaani, wanakwenda kinyume na njia ya Allah تعالى na kuwafuata Mitume Wake na kuzisadiki Aya Zake:

أُولَئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُونَ

“...hao watahudhurishwa kwenye adhabu.”

Yaani, watapata malipo kulingana na amali zao. Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ إِنَّ رَبِّي يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ وَيَقْدِرُ لَهُ

“Sema: Kwa hakika Mola Wangu Mlezi Humkunjulia riziki na Humdhikisha Amtakaye katika waja Wake.

Yaani, Kwa kadiri ya alivyo navyo katika mali ni kutokana na hikima, Humkunjulia huyu mali nyingi na Kumdhikisha huyu na Anampa riziki kidogo sana. Yeye, katika haya, ni Mwenye Hikima ambayo hakuna wa kuipata asiye kuwa Yeye. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَنْظُرَ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ ۗ وَلَآ خِرَةُ أَكْبَرُ دَرَجَتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿٢١﴾

“Angalia vipi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wenginewe. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na Fadhila kubwa zaidi.”
(17:21)

Yaani, kama walivyotofautiana duniani, huyu ni fakiri aliye katika hali ya dhiki, na huyu ni tajiri aliyepewa ukunjufu wa mali. Kadhalika, katika Akhera watakuwa hivi hivi, huyu katika maghorofa katika daraja za juu na huyu katika matabaka ya chini kabisa. Na mtu mzuri zaidi duniani ni yule ambaye Mtume ﷺ amesema:

«قَدْ أَفْلَحَ مَنْ أَسْلَمَ وَرُزِقَ كَفَافًا وَقَتَّعَهُ اللهُ بِمَا آتَاهُ»

“Kwa hakika, amefaulu aliyejisalimisha na kunyenyekea (Kwa Mwenyezi Mungu) na akapewa riziki ya kumtoshеleza, na Allah Akamkinaisha kwa alichо mpa.”

Ilinukuliwa na Muslim.¹ Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُ^ط

“Na chochote mtakachokitoa Yeye Atakilipa.”

Yaani, kadiri mnavyotumia katika kitu ambacho Allah تعالى Amekuamrisheni na Kukuhalalishieni, basi Yeye Hukupeni badala yake, na katika Akhera kwa malipo na thawabu.

Ni sawa na ilivyonukuliwa katika Hadithi:

يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: أَنْفِقْ، أَنْفِقْ عَلَيْكَ.

“Allah Anasema: ‘Toa, Nami Nitakupa.’”

Katika Hadithi nyingine, ilielezwa kwamba, kila asubuhi, Malaika wawili huja na mmoja wao husema: “Ewe Allah! Peleka uharibifu kwa anayezuia (asiyetoa).” Mwingine husema: “Ewe Allah! Mpe kingine mwenye kutoa.”²

Na katika Hadithi nyingine, Mtume ﷺ amesema:

«أَنْفِقْ بِلَالٍ، وَلَا تَخَسَ مِنْ ذِي الْعَرْشِ إِقْلَالًا»

“Tumia, ewe Bilal, wala usichelee kwamba Aliye katika Arshi Atakuzuilia.”¹

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ يَقُولُ لِلْمَلَائِكَةِ أَهْتُولَاءِ ۖ لِإِيَّاكُمْ كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٤٠﴾ قَالُوا
سُبْحَانَكَ أَنْتَ وَلِيُّنَا مِنْ دُونِهِمْ ۗ بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ آلَ جِنٍّ أَكْثَرُهُمْ يَهُودٌ مُؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾
فَالْيَوْمَ لَا يَمْلِكُ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ نَفَعًا وَلَا ضَرًّا وَنَقُولُ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ
الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تَكْتَدُّونَ ﴿٤٢﴾

40. “Na siku Atakayowakusanya wote, kisha Atawaambia Malaika: Je! Hawa walikuwa wakikuabuduni?”

¹ Muslim 2:730.

² Muslim 1:700.

³ At-Tabarani 10:191.

41. "Waseme: (Subhanak), Umetakasika na kila upungufu. Wewe ndiye Kipenzi Chetu si hao. Bali wao walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao wakiwaamini hao."

42. "Hii leo hataweza yeyote kumletea nafuu wala madhara mwenzie. Na Tutawaambia waliodhulumu: Onjeni adhabu ya Moto mliokuwa mkiukanusha."

Malaika watawakataa Wenye Kuwaabudu Wao Katika Siku ya Kiyama

Allah تعالی Anaeleza Atawakemea washirikina Siku ya Kiyama mbele ya viumbe wote. Atawauliza Malaika ambao washirikina walikuwa wakidai kwamba wao walikuwa masanamu ambayo yalikuwa katika maumbo yao, ili yawaweke wao karibu na Allah تعالی Atawaambia Malaika:

أَهْتُولَاءِ إِيَّاكُمْ كَانُوا يَعْبُدُونَ

"...Je! Hawa walikuwa wakikuabuduni?"

Yaani, 'Nyinyi mliwaamuru wakuabuduni?' Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی katika Surat Al-Furqan:

ءَأَنْتُمْ أَضَلُّمٌ عِبَادِي هَتُولَاءِ أَمْ هُمْ ضَلُّوا السَّبِيلَ ﴿١٧﴾

"Je! Ni nyinyi ndio mliowapoteza waja Wangu hawa, au wao wenyewe walipotea njia?" (25:17)

Pia, kama Anavyomuambia Isa عليه السلام

ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمَّيَ إِلَهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقِّ ۗ

"Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Isa) atasema: Subhanaka, Wewe Umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu." (5:116)

Hivi ndivyo watakvayosema Malaika:

سُبْحَانَكَ

"...Umetakasika."

Yaani, Wewe ni juu zaidi na Umetakasika dhidi ya kuwa na mungu mwingine pamoja Nawe,

أَنْتَ وَلِيُّنَا مِنْ دُونِهِمْ

"Wewe Ndiye Kipenzi Chetu si hao."

Yaani, sisi ni waja Wako na tunawakataa watu hawa mbele Yako,

بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ آلِهَةً

"Bali wao walikuwa wakiwaabudu majini..."

Wanamaanisha, mashetani, kwa sababu hao ndio waliowapambia kuabudu masanamu na wakawapoteza,

أَكْثَرُهُمْ بِهِمْ مُؤْمِنُونَ

"...wengi wao wakiwaamini hao."

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنْ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ إِلَّا إِنْتَنَا وَإِنْ يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا مَرِيدًا ﴿١١٧﴾ لَعَنَهُ اللَّهُ

"...wala hawamuombi ila Shetani aliyeasi. Mwenyezi Mungu Amemlaani." (4:117-118)

Amesema Allah تعالى:

فَالْيَوْمَ لَا يَمْلِكُ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ نَفْعًا وَلَا ضَرًّا

"Hii leo hataweza yeyote kumletea nafuu wala madhara mwenzie."

Yaani, hamtanufaishwa na wale mliowataraji wakunufaisheni leo: miongoni mwa miungu ya uongo na masanamu mliyoyaabudu katika nyakati za shida na tabu zenu. Leo hawamiliki manufaa wala madhara yoyote kwa ajili yenu.

وَنَقُولُ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا

“Na Tutawaambia walio dhulumu...”

Yaani, washirikina,

ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ

“Onjeni adhabu ya Moto mliokuwa mkiukanusha.”

Yaani, wataambiwa haya kwa kukaripiwa na kukemewa.

* * *

وَإِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِمْ ءآيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالُوا مَا هَذَا إِلَّا رَجُلٌ يُرِيدُ أَنْ يَصُدَّكُمْ عَنْمَا كَانَ يَعْبُدُ ءَابَاؤَكُمْ وَقَالُوا مَا هَذَا إِلَّا إِفْكٌ مُفْتَرَىٰ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٣﴾ وَمَا ءَاتَيْنَهُمْ مِنْ كُتُبٍ يَدْرُسُونَهَا وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ ﴿٤٤﴾ وَكَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَمَا بَلَّغُوا مِعْشَارَ مَا ءَاتَيْنَهُمْ فَكَذَّبُوا رُسُلِي ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٥﴾ * قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَحْدَةِ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلَىٰ نَفْسٍ وَأَقْرَبَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا ۗ مَا بِصَاحِبِكُمْ مِنْ جِنَّةٍ ۗ إِنْ هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ لَكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٤٦﴾ قُلْ مَا سَأَلْتُكُمْ مِنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ ۗ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٤٧﴾ قُلْ إِنَّ نَبِيَّ يَقْدِفُ بِالْحَقِّ عَلَّمَ الْغُيُوبِ ﴿٤٨﴾ قُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبْدِيُ الْبَاطِلُ وَمَا يُعِيدُ ﴿٤٩﴾ قُلْ إِنْ ضَلَلْتُ فَإِنَّمَا أَضِلُّ عَلَىٰ نَفْسِي ۗ وَإِنِ اهْتَدَيْتُ فِيمَا يُوحِي إِلَيَّ رَبِّي ۗ إِنَّهُ سَمِيعٌ قَرِيبٌ ﴿٥٠﴾ وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ فَرَغُوا فَلَا قُوَّةَ وَأُخِذُوا مِنْ مَكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٥١﴾ وَقَالُوا ءَامَنَّا بِهِ ۗ وَأَنَّىٰ لَهُمُ التَّنَاقُشُ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٢﴾ وَقَدْ كَفَرُوا بِهِ مِنْ قَبْلُ ۗ وَيَقْدِرُونَ بِالْغَيْبِ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٣﴾ وَجِئِلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ كَمَا فُعِلَ بِأَشْيَاعِهِمْ مِنْ قَبْلُ ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا فِي شَكٍّ مُرِيبٍ ﴿٥٤﴾

وَإِذَا تَتَلَّى عَلَيْهِمْ ءآيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالُوا مَا هَذَا إِلَّا رَجُلٌ يُرِيدُ أَنْ يَصُدَّكُمْ عَنْمَا كَانَ يَعْبُدُ ءَابَاؤَكُمْ وَقَالُوا مَا هَذَا إِلَّا إِفْكٌ مُفْتَرَىٰ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٣﴾ وَمَا ءَاتَيْنَهُمْ مِنْ كُتُبٍ يَدْرُسُونَهَا وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ ﴿٤٤﴾ وَكَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَمَا بَلَّغُوا مِعْشَارَ مَا ءَاتَيْنَهُمْ فَكَذَّبُوا رُسُلِي ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٥﴾

43. "Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi wanasema: Huyu si chochote ila ni mtu anayetaka kukuzuieni na waliyokuwa wakiabudu baba zenu. Na wakasema: Haya si chochote ila ni uwongo uliozuliwa. Na waliokufuru waliambia Haki ilipowajia: Haya si chochote ila ni uchawi ulio dhaahiri."

44. "Wala hatukuwapa Vitabu wavisome, wala hatukuwatumia Mwonyaji kabla yako wewe."

45. "Na walikadhibisha waliokuwa kabla yao. Na hawakufikia hata sehemu moja katika kumi ya Tulivyowapa hao. Nao waliwakadhibisha Mitume wangu. Basi kuangamiza Kwangu kulikuwa namna gani!"

Kauli za Makafiri Juu ya Mtume ﷺ na Majibu yao

Allah تعالى Anaeleza kwamba makafiri wanastahiki adhabu kali sana kwa sababu, pindi waliposomewa Aya Zake zenye kubainisha, walikuwa wakizisikiliza moja kwa moja kutoka katika midomo ya Mtume wake ﷺ,

قَالُوا مَا هَذَا إِلَّا رَجُلٌ يُرِيدُ أَنْ يَصُدَّكُمْ عَمَّا كَانُوا يَعْبُدُونَ آبَاءَكُمْ

"...wanasema: Huyu si chochote ila ni mtu anayetaka kukuzuieni na waliyokuwa wakiabudu baba zenu."

Wanamaanisha kuwa dini ya baba zao ni haki, na kwamba yale aliyokuja nayo Mtume wao kuwa ni ya batili. Laana za Allah Ziwaendee wao na baba zao.

وَقَالُوا مَا هَذَا إِلَّا إِنْكَارٌ مِمَّا كَفَرْنَا

"Na wakasema: Haya si chochote ila ni uwongo uliozuliwa."

Wanakusudia, Qur'an,

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ

"Na waliokufuru waliambia Haki ilipowajia: Haya si chochote ila ni uchawi ulio dhaahiri."

Allah تعالى Amesema:

وَمَا آتَيْنَاهُمْ مِنْ كُتُبٍ يَدْرُسُونَهَا وَمَا أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَذِيرٍ ﴿٤٥﴾

"Wala Hatukuwapa Vitabu wavisome, wala hatukuwatumia Mwonyaji kabla yako wewe."

Yaani, Allah تعالى Hakuteremsha Kitabu kabla ya Qur'an kwa Waarabu ambacho wanakisoma, wala Hakuwapelekea nabii yeyote kabla ya Muhammad ﷺ, na

kabla ya hapo walikuwa wakilipenda hilo, huku wakisema: “Lau angelitujia mwonyaji au kuteremshiwa Kitabu, tungelikuwa tumeongoka zaidi ya wengine.” Baada ya Allah تعالی Kuwafadhilisha kwa hayo walimkadhibisha, wakampinga na kumfanyia ukaidi. Kisha Allah تعالی Amesema:

وَكَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Na walikadhibisha waliokuwa kabla yao.”

Yaani, Umma kadha.

وَمَا بَلَّغُوا مِعْشَارَ مَا آتَيْنَاهُمْ

“Na hawakufikilia hata sehemu moja katika kumi ya Tulivyowapa hao.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, “Katika nguvu za duniani.”¹ Pia, hii ilikuwa rai ya Qatadah, As-Suddi na Ibn Ziyad.² Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

وَلَقَدْ مَكَّنَّهُمْ فِيمَا إِنْ مَكَّنَّاكُمْ فِيهِ وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَرَ وَأَفِئدَةً فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ
سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَرُهُمْ وَلَا أَفِئدَتُهُمْ مِنْ شَيْءٍ إِذْ كَانُوا يَتَّخِذُونَ بَيِّنَاتِ اللَّهِ وَحَاقَ بِهِمْ مَا
كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٤٦﴾

“Na hakika Tuliwastawisha vyema kwa nguvu ambayo ninyi hatujakupeni! Na Tukawapa kusikia, kuona na nyoyo; lakini kusikia, kuona na nyoyo zao havikuwasaidia chochote kwa sababu walivitumia katika kukanusha Aya za Mwenyezi Mungu, na kwa hakika walizungukwa na yale waliyokuwa wakiyabeza” (46:26)

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ كَانُوا أَكْثَرَ مِنْهُمْ
وَأَشَدَّ قُوَّةً

“Kwani hawatembe katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hawa, na wamewashinda kwa nguvu...” (40:82)

¹ At-Tabari 20:416.

² At-Tabari 20:416, 417.

Yaani, wala hayo hayakuwaondolea adhabu ya Allah تعالى, wala hayakuizua isiwapike. Allah تعالى Aliwaangamiza baada ya kuwakataa Mitume Wake. Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema,

فَكَذَّبُوا رُسُلِي ۖ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ

“Nao waliwakadhibisha Mitume Wangu. Basi Kuangamiza Kwangu kulikuwa namna gani!”

Yaani, basi, ulikuwaje ukali wa adhabu Yangu na kuwanusuru Kwangu Mitume Wangu.

قُلْ إِنَّمَا أَعْظُمُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۚ أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلَ خِيَلٍ مُّنْجِبَةٍ وَأَنْ تَصَاحِبِكُمْ مِنْ جِنَّةٍ ۚ إِنَّ هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ لَكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٤٦﴾

46. “Sema: Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu - ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenu huyu hana wazimu. Yeye si chochote ila ni Mwonyaji kwenu kabla ya kufika adhabu kali.”

Kukanushwa kwa Madai Yao kwamba Mtume ﷺ Alikuwa Mwendawazimu

Allah تعالى Anasema: ‘Sema ewe Muhammad! Uwaambie hawa makafiri wanaodai kuwa wewe ni mwendawazimu:

إِنَّمَا أَعْظُمُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۚ

“...Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu...”

Yaani, kwa hakika, ninakuamuruni jambo moja tu, nalo ni,

أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلَ خِيَلٍ مُّنْجِبَةٍ وَأَنْ تَصَاحِبِكُمْ مِنْ جِنَّةٍ ۚ

“...ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenu huyu hana wazimu.”

Maana: Msimame kwa Utakasifu mbele ya Allah تعالى, pasi na matamanio au

fikra za kikabila, na muulizane nyinyi kwa nyinyi juu ya uendawazimu wa Muhammad ﷺ na mpeane nasaha baina yenu,

ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا^٤

"...kisha mfikiri."

Maana: Kila mtu katika nafsi yake aliangalie jambo linalomhusu Muhammad ﷺ, na awaulize watu wengine juu ya suala lake ikiwa yeye mwenyewe ametatizwa nalo. Halafu atafakuri katika hayo. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَنْ تَقُومُوا لِلَّهِ مِثْلِيَ وَفُرَادَىٰ ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا^٥ مَا بِصَاحِبِكُمْ مِنْ جِنَّةٍ^٦

"...ya kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili-wawili na mmoja-mmoja; kisha mfikiri. Mwenzenzi huyu hana wazimu."

Maana hii aliieleza Mujahid, Muhammad bin Ka'b, As-suddi, Qatadah na wengine.¹ Hayo ndio makusudio ya Aya hiyo. Kauli ya Allah تعالى:

إِنْ هُوَ إِلَّا نَذِيرٌ لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ

"Yeye si chochote ila ni Mwonyaji kwenu kabla ya kufika adhabu kali."

Bukhari alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kwamba aliizungumzia Aya hii, akasema: "Mtume ﷺ alipanda juu ya As-Safaa akasema:

«يَا صَبَاحَاهُ»

'Enyi watu!'

Makuraishi wakamkusanyikia, wakasema: 'Una nini?' Akasema:

«أَرَأَيْتُمْ لَوْ أَخْبَرْتُمْ أَنَّ الْعَدُوَّ يُصَبِّحُكُمْ أَوْ يَمْسِكُمْ أَمَا كُنْتُمْ تُصَدِّقُونِي»

'Mnaonaje lau nitakuambieni kwamba adui yenu wanakukaribieni kukufikieni asubuhi au jioni, mngekuwa ni wenye kunisadiki?'

¹ At-Tabari 20:418.

Wakasema: 'Ndiyo.' Mtume ﷺ akasema:

﴿فَأَنبِي نَذِيرٌ لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيدٍ﴾

"Mimi ni muonyaji kwenu mbele ya adhabu kali."

Abu Lahab akasema: 'Uangamie! Kwa jambo hili ndio umetukusanya.' Allah تعالى Akateremsha:

﴿تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ﴾

"Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na yeye pia ameangamia."
(111:1)

Tumekwishaitafsiri hii katika Kauli ya Allah تعالى:

﴿وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ﴾

*"Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe."*¹ (26:214)

﴿قُلْ مَا سَأَلْتُكُمْ مِنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ إِنَّ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ﴾⁽¹⁾
﴿قُلْ إِنَّ رَبِّي يَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَٰمَ الْغُيُوبِ﴾⁽²⁾ ﴿قُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبَدِّلُ الْبَاطِلَ وَمَا يُعِيدُ﴾⁽³⁾
﴿قُلْ إِنْ ضَلَلْتُ فَإِنَّمَا أَضِلُّ عَلَىٰ نَفْسِي وَإِنِ اهْتَدَيْتُ فِيمَا يُوحِي إِلَيَّ رَبِّي إِنَّهُ سَمِيعٌ قَرِيبٌ﴾⁽⁴⁾

47. *"Sema: Ujira nilio kuombeni ni wenu nyinyi. Sina ujira ila kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ni Shahidi juu ya kila kitu."*

48. *"Sema: Hakika Mola Wangu Mlezi Anaondoa upotovu kwa Haki. Yeye Ndiye Mwenye Kujua vyema mambo ya ghaibu."*

49. *"Sema: Kweli imefika, na uwongo haujitokezi, wala haurudi."*

50. *"Sema: Ikiwa mimi nimepotea, basi nimepotea kwa kudhuru nafsi yangu mwenyewe. Na ikiwa nimeongoka, basi ni kwa sababu ya kunifunulia Mola Wangu Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Aliye karibu."*

¹ Fat'h Al-Bari 8:400.

Siombi Kwenu Malipo Yoyote kwa Kuufikisha Ujumbe

Allah تعالی Anamuamuru Mtume Wake ﷺ awaambie washirikina:

مَا سَأَلْتُمْ مِّنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ

“...Ujira niliokuombeni ni wenu nyinyi.”

Yaani, ‘Sihitaji kitu chochote kutoka kwenu wala zawadi kwa kukufikishieni Ujumbe wa Allah تعالی na nasaha zangu kwenu na kukuamuruni kumuabudu Allah تعالی.’

إِن أَجْرِي إِلَّا عَلَى اللَّهِ

“Sina ujira ila kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, malipo ya kufanya hivyo nitayataka kutoka kwa Allah تعالی:

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Na Yeye ni Shahidi juu ya kila kitu.”

Maana yake, ni Mwenye Kuyajua mambo yote kuhusu mimi na namna ninavyoufikisha Ujumbe kwenu na namna ninyi mnavyouchukulia.

قُلْ إِنِّي يَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَّمَ الْغُيُوبِ

“Sema: Hakika Mola Wangu Mlezi Anaondoa upotovu kwa Haki. Yeye Ndiye Mwenye Kujua vyema yaliyoghaibu.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يُلْقِي الرُّوحَ مِن أَمْرِهِ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِن عِبَادِهِ

“Hupeleka Roho kwa Amri Yake juu ya Amtakaye katika waja Wake...” (40:15)

Yaani, Humpeleka Malaika kwa Amtakaye miongoni mwa waja Wake katika wakazi wa ardhini, na Yeye ni Mwenye Kujua ghaibu, na hakuna cha kujificha dhidi Yake, mbinguni wala ardhini. Kauli ya Allah تعالی:

قُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبَدِّلُ مَا يُبَدِّلُ وَمَا يُعِيدُ ﴿٤٣﴾

“Sema: Kweli imefika, na uwongo haujitokezi, wala haurudi.”

Maana: Haki na sharia tukufu kutoka kwa Allah تعالى imekuja, na uongo umeondoka, umemalizika na umetoweka. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah

تعالى:

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ ﴿٤٤﴾

“Bali Tunaitupa kweli juu ya uwongo ikauvunja na mara ukatoweka.” (21:18)

Hivyo, baada ya Mtume ﷺ kuingia Al-Masjid Al-Haram katika siku ya ukombozi wa Makkah, na kukuta masanamu yale yaliyosimamishwa kuzunguka Al-Ka ‘bah, alianza kuyachoma masanamu kwa upinde wake, huku akisoma:

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٤٥﴾

“Na sema: Kweli imefika, na uwongo umetoweka. Hakika uwongo lazima utoweke!” (17:81)

قُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبَدِّلُ مَا يُبَدِّلُ وَمَا يُعِيدُ ﴿٤٦﴾

“Sema: Kweli imefika, na uwongo haujitokezi, wala haurudi.”

Hii ilinukuliwa na Al-Bukhari, Muslim, At-Tirmidhi na An-Nasai.¹ Kauli ya Allah

تعالى:

قُلْ إِنْ صَلَّيْتُ فَإِنََّّمَا أَضِلُّ عَلَى نَفْسِي وَإِنْ أَهْتَدَيْتُ فِيمَا يُوحِي إِلَيَّ رَبِّي ﴿٤٧﴾

“Sema: Ikiwa mimi nimepotea, basi nimepotea kwa kudhuru nafsi yangu mwenyewe. Na ikiwa nimeongoka, basi ni kwa sababu ya kunifunulia Mola Wangu Mlezi.”

Maana: Kila jema hutoka kwa Allah تعالى, na katika ufunuo Anaouteremsha Allah تعالى na ukweli dhahiri, kuna uongofu na hikima. Kwa hivyo, yeyote anayepotoka, ni

¹ Fat'h Al-Bari 8:252, Muslim 3:1409, Tuhfat Al-Ahwardhi 8:573, An-Nasai katika Al-Kubra 6:483.

kutokana na yeye mwenyewe, kama alivyosema 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه pindi alipoulizwa jambo hilo. Alisema, "Ninaweza kusema ninachokifikiri, kama ni sahihi, basi ni kutoka kwa Allah تعالى, na kama sivyo, basi kinatokana nami na kutoka kwa Shetani, ilhali Allah تعالى na Mtume Wake hawahusiani nacho."¹ Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّهُ سَمِيعٌ قَرِيبٌ

"Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Aliye karibu."

Yaani, ni Mwenye Kuzisikia kauli za waja Wake, Yu karibu, Hujibu dua za muombaji akimuomba. An-Nasai alinukuu Hadithi ya Abu Musa رضي الله عنه iliyo ndani ya *Sahih*, kwamba:

«إِنَّكُمْ لَا تَدْعُونَ أَحْصَمَ وَلَا غَائِبًا، إِنَّمَا تَدْعُونَ سَمِيعًا قَرِيبًا مُجِيبًا»

*"Hakika Nyinyi hamumuombi kiziwi wala asiyekuwepo, bali mnamuomba Mwenye Kusikia, wa karibu sana na Mwenye Kujibu."*²

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ فَرَغُوا فَلَا قُوَّةَ وَأُخِذُوا مِنْ مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٥١﴾ وَقَالُوا ءَأَمَّنَّا بِهِ وَأَنَّىٰ لَهُمُ
الَّتَنَاقُشُ مِنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٢﴾ وَقَدْ كَفَرُوا بِهِ مِنْ قَبْلُ وَيَقْدِفُونَ بِالْغَيْبِ مِنْ
مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٣﴾ وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ كَمَا فُعِلَ بِأَشْيَاعِهِمْ مِّن قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا
فِي شَكٍّ مُّبِينٍ ﴿٥٤﴾

**51. "Na lau ungeliona watapobabaika, basi hapana pa kukimbilia!
Na watakamatwa mahala pa karibu."**

**52. "Na watasema: Tunaiamini! Lakini wataipata wapi kutoka huko
mahala mbali?"**

**53. "Na hapo kabla yake waliikataa, na wakiyatupilia mbali
maneno ya ghaibu kutoka mahali mbali."**

¹ Abu Dawud 2:589.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:438, Fat'h Al-Bari 9:157, Muslim 4:2076.

54. "Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayoyatamani, kama walivyofanyiwa wenzao zamani. Hakika hao walikuwa na shaka ya kutia wasiwasi."

"Hapa Allah تعالى Anasema, 'Kama tu utaweza kuona, Ewe Muhammad, wakanushaji hawa watakapotishika katika Siku ya Kiama, na hawatakuwa na njia ya kutorokea wala pa kukimbilia na hakuna hifadhi.'

وَأَخِذُوا مِن مَّكَانٍ قَرِيبٍ

"Na watakamatwa mahala pa karibu."

Maana: Hawatapewa fursa hata ndogo ya kutoroka, bali watakamatwa tangu mwanzoni. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, "Mara tu, watakapotoka makaburini."¹

وَقَالُوا ءَأَمَّنَّا بِهِ

"Na watasema: Tunaiamini!"

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا

نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿٥٤﴾

"Na ungelikiwaona wakosefu wanvyoinamisha vichwa vyao mbele ya Mola Wao Mlezi, (wakisema): Mola Wetu Mlezi! Tumeshiona, na tumeshasikia. Turejeshe tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwisha kuwa na yakini sasa." (32:12)

Allah تعالى Anasema,

وَأَنى لَهُمُ التَّنَاقُوشُ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ

"Lakini wataipata wapi kutoka huko mahala mbali?"

Yaani, wanawezaje kuwa na imani sasa ambapo wameondolewa mbali mahali wangeweza kukubaliwa, na wameingia Akhera ambao ni ulimwengu wa malipo na adhabu, si wa majaribio? Kama wangeyaamini hayo duniani ingekuwa vyema kwao, lakini kwa sasa wameingia Akhera, imani yao haitakubalika kwa vyovyote kama ambavyo si rahisi mtu kupata kitu alichomo mbali nacho.

¹ At-Tabari 20:123.

وَأَنى لَهُمُ التَّنَاضُؤُ

“Lakini wataipata wapi...?”

Yaani, “wataiwezaje kuipata?”¹ Az-Zuhri رحمه الله تعالى amesema, “Watatamani kupata imani hali ya kuwa wapo tayari Akhera, na hawana tena kutokuwa na mawasiliano na dunia.” Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى amesema, “Watatafuta kitu ambacho hakutakuwa na njia ya kukipata, watatafuta imani kutokea mbali.”

وَقَدْ كَفَرُوا بِمِءٍ مِّن قَبْلُ

“Na hapo kabla yake waliikataa...”

Yaani, watapata vipi Imani katika Akhera wakati duniani waliukataa ukweli na kuwakana Mitume?.

وَيَقْدِفُونَ بِالْغَيْبِ مِمَّنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ

“...na wakiyatupilia mbali maneno ya ghaibu kutoka mahali mbali.”

Malik alisimulia kutoka kwa Zayd bin Aslam kuwa alisema:

وَيَقْدِفُونَ بِالْغَيْبِ

“...na wakiyatupilia maneno ya ghaibu...”

Yaani kwa “kubuni,” ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

رَحْمًا بِالْغَيْبِ

“Wanavurumisha ovyo.” (18:22)

Wakati mwingine walisema kuwa Mtume ni mshairi, na wakati mwingine walisema kuwa mtabiri, na mara ni mchawi, na mara wanasema ni mwendawazimu, au madai mengine yasiyo ya msingi. Walikanusha ufufuo na wakasema,

إِن نَّظُنُّ إِلَّا ظَنًّا وَمَا نَحْنُ بِمُصْتَفِيِينَ

“...tunadhania dhana tu, wala hatuna yakini.” (45:32)

¹ Ad-Dur Al-Manthur 6:714.

Qatadah na Mujahid walisema: "Imani yao ya kutokuwepo ufufuo, pepo na moto, ilikuwa dhana tu."¹

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ

"Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayoyatamani..."

Al-Hasan Al-Basri, Adh-Dhahhak na wengine, "Maana yake ni imani."² Na Assudi amesema:

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ

"Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayo yatamani..."

Yaani, "Toba."³ Hii ilikuwa pia rai ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Mujahid amesema:

وَحِيلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُونَ

"Na watatiliwa kizuizi baina yao na hayo wanayo yatamani..."

Yaani, "dunia hii na mali zake, anasa na watu."⁴ Masimulizi kama hayo yalisimuliwa na Ibn 'Umar, Ibn 'Abbas na Ar-Rabi bin Anas. pia ndio rai ya Al-Bukhari na wengine. Rai sahihi ni kuwa, rai mbili hizi hazipingani, kwani watawekewa kizuizi baina yao na watakachotamani duniani, na hawatapewa wanachokitafuta huko Akhera.

كَمَا فُعِلَ بِأَشْيَاعِهِمْ مِّن قَبْلُ

"...kama walivyofanyiwa wenzao zamani."

Yaani, kama ilivyowatokea umma zingine zilizopita ambao waliwakataa Mitume pindi adhabu ya Allah ilipowafikia, watatamani kuwa wangeamini, lakini hayo hawatakubaliwa.

¹ At-Tabari 20:429.

² At-Tabari 20:430.

³ Ad-Dur Al-Manthur 6:715.

⁴ At-Tabari 20:431.

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدُّهُدٍ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٤٤﴾ فَلَمَّا يَكُ
 يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا سُنَّتَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ ۗ وَخَبِيرَ هُنَالِكَ
 الْكٰفِرُونَ ﴿٤٥﴾

“Walipoiona Adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee, na tunaikataa (miungu) tuliyoukuwa tukiishirikisha Naye. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona adhabu Yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja Wake. Na hapo waliokufuru wakapata hasara.” (40:84-85)

إِيْمَانُهُمْ كَانُوا فِي شَكٍّ مُّرِيبٍ

“Hakika hao walikuwa na shaka ya kutia wasiwasi.”

Kwamba, wana mashaka katika maisha haya kwa hiyo imani yao haitakubaliwa wakati watakaposhuhudia adhabu kwa macho yao. Qatadah amesema, “Jihadhari juu ya shaka, maana yeyote atakayekufa akiwa na shaka atafufuliwa akiwa mashakani, na kila atakayekufa akiwa muumini mwenye yakini atafufuliwa akiwa muumini wa kweli”.

Huu ndio mwisho wa *Tafsir ya Surat Saba*. Allah تعالیٰ Ndiye Mwenye Kuongoza katika njia ya sawa.

* * *

Tafsiri ya Suratu Fatir

Sura ya 35

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

سُورَةُ فَاطِرٍ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ جَاعِلِ الْمَلَكِئِكَةِ رُسُلًا أُولَىٰ أَجْنِحَةٍ مِّثْنَىٰ وَتُلُكَّتْ رُزْنَعٌ ۚ يَزِيدُ فِي الْخَلْقِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ جَاعِلِ الْمَلَكِئِكَةِ رُسُلًا أُولَىٰ أَجْنِحَةٍ مِّثْنَىٰ وَتُلُكَّتْ رُزْنَعٌ ۚ يَزِيدُ فِي الْخَلْقِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ مَا يَفْتَحِ اللَّهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۗ وَمَا يُمْسِكْ فَلَا مُرْسِلَ لَهُ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢﴾ يَتَأَيَّمُوا النَّاسُ أَذْكُرُوا يَعْجَمَتَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ۚ هَلْ مِنْ خَلْقٍ غَيْرِ اللَّهِ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَاِن تَوَفَّكُونَ ﴿٣﴾ وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٤﴾ يَتَأَيَّمُوا النَّاسُ إِنْ وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا ۗ وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿٥﴾ إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُرَّ عَدُوٍّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا ۗ إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٦﴾

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ جَاعِلِ الْمَلَكِئِكَةِ رُسُلًا أُولَىٰ أَجْنِحَةٍ مِّثْنَىٰ وَتُلُكَّتْ رُزْنَعٌ ۚ يَزِيدُ فِي الْخَلْقِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

1. "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi wa mbingu na ardhi, Aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa, mbili - mbili, na tatu - tatu, na nne-nne. Huzidisha katika Kuumba Apendavyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu."

Kutajwa Uwezo wa Allah

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما ali-sema, "Sikujua nini ilikuwa maana ya Fatwiri ssamaa-waati wal-ardhw mpaka mabedui wawili walipokuja kwangu wakigombania

kisima. Mmoja wao alimuambia mwenziye, 'Ana Fatwartuha,' Yaani 'Mimi ndiye niliyekianzisha.'"¹ Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema pia,

فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

"...Muumba wa mbingu na ardhi..."

Maana yake, "Mwanzilishi wa mbingu na ardhi."² Adh-Dhahhak alisema, "Kila mara ambapo kauli *Faatwirus-samaawaati wal-ardhw* linapotumika ndani ya Qur'an, humaanisha Muumbaji wa mbingu na ardhi."³

جَاعِلِ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا

"...Aliye wafanya Malaika kuwa wajumbe..."

Yaani, baina Yake na Manabii wake,

أُولَىٰ أَجْنَحَةٍ

"...wenye mbawa..."

Yaani, wanazozitumia kwa kuruka ili wayafikishe kwa haraka yale wanayoamrishwa,

مَثْنَىٰ وَثُلَاثَ وَرُبْعَآءَ

"...mbili-mbili, na tatu- tatu, na nne-nne."

Yaani, wapo miongoni mwao, wenye mbawa mbili na wengine tatu, wengine nne, wengine zaidi ya hizo.

Ni sawa na ilivyokuja katika Hadithi kuwa Mtume عليه السلام alimuona Jibril katika usiku wa Israel akiwa na mbawa mia sita. Baina ya kila mbawa mbili ni sawa na umbali kati ya mashariki na magharibi.¹

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:3.

² Ad-Dur Al-Manthur 7:3.

³ Ad-Dur Al-Manthur 7:3.

⁴ Fat-h Al-Bari 6:361.

يَزِيدُ فِي الْخَلْقِ مَا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Huzidisha katika Kuumba Apendavyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.”

As-Suddi alisema: “Yeye Huzidisha mbawa zao na Huziumba Atakavyo.”²

مَا يَفْتَحِ اللَّهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۗ وَمَا يُمْسِكُ فَلَا مُرْسِلَ لَهُ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦﴾

2. “Rehema Ambayo Mwenyezi Mungu Anawafungulia watu hapana wa kuizua. Na Anayoizua hapana wa kuipeleka isipo kuwa Yeye. Naye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Hapana wa Kuzuia Rehema ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anajulisha kwamba Ayatakayo Yeye Hutukia, na Asiyoyataka Hayawi. Hakuna wa kuyazuia Ayatoayo wala mwenye kuyatoa Aliyoyazuia. Imamu Ahmad alinukuu kwamba Warrad, mtumwa aliyeachwa huru na Al-Mughirah bin Shu’bah رضي الله عنه, alisema kuwa Mu’awiyah رضي الله عنه alimuandikia Al-Mughirah bin Shu’bah رضي الله عنه: “Niandikie ulichokisikia kutoka kwa Mtume ﷺ.” Al-Mughirah رضي الله عنه akaniita, nami nikamuandikia: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema katika nyakati anapoondoka kutoka katika Sala:

«سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ، اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ مِلْءُ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، وَمِثْلَهُ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ، اللَّهُمَّ أَهْلَ الشَّاءِ وَالْمَجْدِ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ وَكُنَّا لَكَ عَبْدًا، اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ»

“Allah Humsikia mwenye kumsifu. Ewe Allah, Mola Wetu, ni Zako Himdi, ujazo wa mbingu na ardhi na chochote Utakacho baada yake. Ewe Allah, Mwenye Haki ya Kusifiwa na Kutukuzwa, maneno ya kweli zaidi aliyoyasema mja – na sisi sote ni waja Wako – ni: ‘Ewe

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:4.

*Allah, hapana mwenye kuyazuia Uliyoyatoa, wala mwenye kutoa Uliyoyazuia, wala hanufaiki mwenye utajiri, Kwako Wewe ndio Unatoka Utajiri.*¹

‘Na nilimsikia akikataza umbeya, kuuliza maswali mengi na ufujaji wa mali, kuwazika watoto wachanga wa kike, kuwatukana wazazi wa kike na kuwanyima wengine wanapowaomba”² Haya pia, yalinukuliwa na Al-Bukhari na Muslim pia kwa isnadi kadha.³

Ilinukuliwa katika Sahih Muslim kuwa Abu Sa’id Al-Khudri رضى الله عنه alisema, Mtume ﷺ alikuwa akisema yafuatayo baada ya kunyanyua kichwa chake kutoka katika Rukuu:

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ،
اللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ وَلَا مُعْطِيٍّ لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ»

“Hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah Peke Yake, hana mshirika, ni Wake Ufalme na Himdi, na Yeye ni Muweza wa kila kitu. Ewe Allah, hapana mwenye kuyazuia Uliyoyatoa, wala mwenye kutoa Uliyoyazuia, wala hakuna bahati yoyote dhidi Yako itayomnufaisha mwenye sudi.”

Aya hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

«وَإِنْ يَمَسُّنَكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ وَإِنْ يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَادَّ لِفَضْلِهِ»⁴

“Na Mwenyezi Mungu Akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha Fadhila Yake.” (10:107)

Kuna Aya nyingi mithili ya hii.

¹ Ahmad 4:250.

² Fat’h Al-Bari 2:378, 11:137, 521, Muslim 1:414, 415.

³ Muslim 1:347.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ ۗ هَلْ مِنْ خَلْقٍ غَيْرِ اللَّهِ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ
وَالْأَرْضِ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَآءِىٰ تُوَفَّكُونَ ﴿٦﴾

3. “Enyi watu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu. Ati yupo muumba mwengine asiyekuwa Mwenyezi Mungu Anayekupeni riziki kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Hapana Mola ila Yeye tu. Basi wapi Mnageuka?”

Ushahidi Mbalimbali wa Tawhid

Allah تعالى Anawaonesha na Kuwaelekeza waja Wake juu ya Tauhidi Yake, kuhusu kumpwekesha katika ibada, kama ambavyo Yeye ni wa Pekee katika Uumbaji na Utoaji riziki, basi kadhalika, Awe ni Yeye Mmoja tu katika kuabudiwa, wala hana mshirika yeyote, si kutokana na masanamu na miungu batili. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَآءِىٰ تُوَفَّكُونَ

“Hapana muabudiwa ila Yeye tu. Basi wapi mnako geuzwa?”

Yaani, kwa namna gani mnageuka baada ya ubainifu huu pamoja na ushahidi dhahiri. Nanyi baada ya haya yote, bado mnaabudu miungu batili na masanamu. Allah تعالى Ndiye Mjuzi.

وَإِنْ يَكْذِبُوا لَكَ فَقَدْ كَذَّبَتْ رَسُولٌ مِّن قَبْلِكَ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٧﴾ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ
إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ ۗ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا ۗ وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ الْغُرُورُ ﴿٨﴾ إِنَّ
الشَّيْطَانَ لَكُرْهُدٌ ۗ فَآخِذُوهُ عَدُوًّا ۗ إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿٩﴾

4. “Na wakikukanusha, basi walikwisha kanushwa Mitume kabla yako. Na mambo yote yatarudishwa kwa Mwenyezi Mungu.”

5. “Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.”

6. “Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni.”

Mtume Muhammad ﷺ alipata upinzani kama Mitume waliopita, na angalizo juu ya uwepo wa Kiama.

Allah تعالى Anasema: “Ewe Muhammad! Kama hawa washirikina watakupinga juu ya Allah na kukukhalifu katika Tauhidi uliyokuja nayo, basi unacho kigezo chema kutoka kwa Mitume waliopita kabla yako. Wao halikadhalika, waliwajia kaumu zao kwa ubainifu na wakawaamuru kushikamana na Tauhidi, lakini wakawakadhibisha na kuwakhaliifu,

وَأِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ

“Na mambo yote yatarudishwa kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, Tutawalipa malipo mengi kwayo. Kisha, Allah تعالى Amesema:

يَتَأْتِيَا النَّاسُ إِنْ وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا

“Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli.”

Yaani, Marejeo yatakuwepo, bila ya shaka yoyote,

فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا

“...basi yasikudanganyeni maisha ya dunia.”

Yaani, maisha ya dunia, kwa mnasaba wa kheri kubwa kwa marafiki zake na wafuasi wa Mitume Wake. Kwa hivyo, msiyapuuze mazuri yenye kuendelea, kwa kufuata starehe hizi zenye mwisho,

وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِاللَّهِ الْغُرُورُ

“...wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu.”

Hii inamaanisha Shetani, kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما.¹ Yaani, Shetani asikufitinisheni na kukutoeni katika kumfuata Mtume ﷺ na kuyasadiki maneno yake. Shetani ni mwenye hadaa, muongo na mzushi. Aya hii ni kama iliyo katika Surat Luqman:

فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَلَا يَغُرَّنَّكُم بَإِلَّهِ الْغُرُورُ

“Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala asikudanganyeni na Mwenyezi Mungu mdanganyifu.” (31:33)

Kisha, Allah تعالى Alibainisha uadui wa Ibilisi kwa mwanaadamu. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ الشَّيْطَانَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوهُ عَدُوًّا

“Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui.”

Yaani, huko ni kukutangazieni uadui, kwa hivyo mfanyieni uadui mkali zaidi, mumkhalifu na mumkadhibishe anayokughurini nayo,

إِنَّمَا يَدْعُوا حِزْبَهُ لِيَكُونُوا مِنْ أَصْحَابِ السَّعِيرِ

“Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni.”

Yaani, anakusudia kukupotezeni ili muingie pamoja naye Motoni. Huyu ndiye adui aliye dhahiri. Tunamuomba Allah تعالى, Ambaye Ndiye Mwenye Nguvu na Muweza wa yote, Atujaalie tuwe maadui wa Shetani, na Aturuzuku kukifuata Kitabu Chake na njia ya Mtume Wake, kwani Yeye ni Muweza wa lolote Alitakalo na katika Kuyajibu maombi. Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ ۗ
أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

“Na Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipo kuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola Wake Mlezi. Je! Mnamshika yeye na dhuriya zake kuwa marafiki badala Yangu, hali wao ni adui zenu? Ni ovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.” (18:50)

* * *

¹ At-Tabari 20:438.

الَّذِينَ كَفَرُوا هُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۝ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا
 الصَّالِحَاتِ هُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٧﴾ أَفَمَنْ زُيِّنَ لَهُ سُوءُ
 عَمَلِهِ فَرَءَاهُ حَسَنًا ۖ فَإِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ
 يَشَاءُ ۖ فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَتٌ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا
 يَصْنَعُونَ ﴿٨﴾ وَاللَّهُ الَّذِي أَرْسَلَ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا
 فُسْقِنَهُ إِلَىٰ بَلَدٍ مَّيِّتٍ فَأَحْيَيْنَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۗ
 كَذَٰلِكَ النُّشُورُ ﴿٩﴾ مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا ۗ
 إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ ۗ
 وَالَّذِينَ يَمْكُرُونَ السَّيِّئَاتِ هُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۖ وَمَكْرُ
 أُولَٰئِكَ هُوَ يُبْوَءُ ﴿١٠﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ
 ثُمَّ جَعَلَكُمْ أَزْوَاجًا ۗ وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنْثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا
 بِعِلْمِهِ ۗ وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمُرِهِ إِلَّا فِي
 كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَىٰ اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿١١﴾ وَمَا يَسْتَوِي الْبَحْرَانِ
 هَٰذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ سَائِغٌ شَرَابُهُ ۖ وَهَٰذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ ۖ وَمِن
 كُلِّ تَاكُلُونَ لَحْمًا طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُونَ حَبْلَةً تَلْبَسُونَهَا ۗ
 وَتَرَىٰ الْفَلَكَ فِيهِ مَوَآخِرَ لِيَتَّبِعُوا مِنَ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ
 تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾

الَّذِينَ كَفَرُوا هُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۖ
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ
 مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٧﴾ أَفَمَنْ زُيِّنَ لَهُ
 سُوءُ عَمَلِهِ فَرَءَاهُ حَسَنًا ۖ فَإِنَّ اللَّهَ
 يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۖ فَلَا
 تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَتٌ ۚ إِنَّ اللَّهَ
 عَلِيمٌ بِمَا يَصْنَعُونَ ﴿٨﴾

7. "Waliokufuru watakuwa na adhabu kali; na walio-amini na wakatenda mema watapata msamaha na ujira mkubwa."

8. "Je! Yule aliyepambiwa amali zake mbaya na akazona ni njema - basi hakika Mwenyezi Mungu Humuacha akapotea Amtakaye, na Humuongoa Amtakaye. Basi nafsi yako isijihiliki kwa kuwasi-kitikia. Hakika Mwenyezi Mungu Anajua wanayo-yafanya."

Adhabu kwa Kafiri na Zawadi ya Malipo Muumini Siku ya Marejeo

Baada ya Allah تعالی Kutaja kwamba wafuasi wa Ibilisi wataishia Motoni, alitaja kwamba: Wale waliokufuru wana adhabu kali, kwa sababu wamemtii Shetani na kumkufuru *Ar-Rahman*, na kwamba waliomuamini Allah تعالی na Mitume Wake,

وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ مَغْفِرَةٌ

“...na wakatenda mema watapata msamaha...”

Yaani, kwa sababu ya madhambi waliyokuwa nayo,

وَأَجْرٌ كَبِيرٌ

“...na ujira mkubwa.”

Juu ya kheri walizozifanya. Kisha, Allah تعالی Amesema:

أَفَمَنْ زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ فَرَآهُ حَسَنًا

“Je! Yule aliyepambiwa amali zake mbaya na akazona ni njema...”

Maana yake, kama vile makafiri na waovu wanaofanya amali mbaya, ilhali wao, katika hayo, huitakidi na kudhani kwamba wanafanya vyema. Yaani, je mtu ambaye yuko namna hii ameachwa na Allah تعالی apotee, basi wewe una namna ya kumfanyia? Hutaweza kumsaidia.

فَإِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ

“...basi hakika Mwenyezi Mungu Humuacha akapotea Amtakaye, na Humuongoa Amtakaye.”

Yaani, kutokana na Kudura Yake hilo limekuwa,

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَاتٍ

“Basi nafsi yako isijihiliki kwa kuwasikitikia.”

Yaani, usiwahuzunikie, kwani Allah تعالی ni Mwenye Hikima katika Kudura Yake, kwa hakika Humuacha apotee yule Amtakaye, na Humuongoza Amtakaye. Ni kwa sababu ya hoja na elimu timilifu kabisa. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا يَصْنَعُونَ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anajua wanayoyafanya.”

وَاللَّهُ الَّذِي أَرْسَلَ الرِّيحَ فَتُثِيرُ سَحَابًا فَسُقْنَاهُ إِلَى بَلَدٍ مَيِّتٍ فَأَحْيَيْنَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا
 كَذَلِكَ النُّشُورُ ﴿٩﴾ مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا ۖ إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ
 وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ ۗ وَالَّذِينَ يَمْكُرُونَ السَّيِّئَاتِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۖ وَمَكْرُ أُولَئِكَ هُوَ
 يَبُورُ ﴿١٠﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ جَعَلَكُمْ أَزْوَاجًا ۗ وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنْثَىٰ
 وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ ۗ وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ ۗ إِنَّ ذَلِكَ
 عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿١١﴾

9. “Na Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezituma Pepo ziyatimue mawingu. Nasi Tukayafikisha kwenye nchi iliyo kufa, Tukaifufua ardhi baada ya kufa kwake. Ndivyo kama hivyo kutakavyo kuwa kufufuliwa.”

10. “Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye Hupanda neno zuri, na amali njema Yeye Huitukuza. Na wanaopanga vitimbi vya maovu watapata adhabu kali. Na vitimbi vya hao vitaonduka patupu.”

11. “Na Mwenyezi Mungu Amekuumbeni kutokana na udongo. Kisha kwa tone la manii. Kisha Akakufanyeni mwanamume na mwanamke. Na mwanamke yeyote habebi mimba, wala hazai, ila kwa Ilimu Yake. Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu. Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.”

Ushahidi wa Maisha Baada ya Mauti

Mara nyingi, Allah تعالى Hutoa dalili ya Marejeo kwa Kuhuisha Kwake ardhi baada ya kufa kwake. Ni sawa na ilivyo katika Surat Al-Hajj, Allah تعالى Anawaeleza waja Wake wayazingatie haya (marejeo) kutokana na hayo (kumea mimea),

أَهْتَرَّتْ وَرَزَّتْ وَأُنْبِتَتْ مِنْ كُلِّ رَوْحٍ بِهِيجِ

“...husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.” (22:5)

Kadhalika, Allah تعالى Akitaka Kuifufua na Kuikusanya miili, Huteremsha mvua kutoka chini ya Arshi, itakayoenea ardhi yote, itaifanya miili iweze kumea makaburini mwao kama vile mbegu ardhini. Kwa ajili hii, ilinukuliwa ndani ya Sahih,

«كُلُّ ابْنِ آدَمَ يَتَلَى إِلَّا عَجْبُ الذَّنْبِ، مِنْهُ خُلِقَ وَمِنْهُ يُرَكَّبُ»

“Kila sehemu ya mwanaadamu huoza isipokuwa kifandugu. Aliumbwa kutokana nacho na Atarudishwa tena kwa hicho.”¹

Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema:

كَذَلِكَ النُّشُورُ

“Ndivyo kama hivyo kutakavyo kuwa kufufuliwa.”

Katika Hadithi ya Abu Razin رضي الله عنه: “Nilimuambia: Ewe Mtume wa Allah! Ni namna gani Allah تعالى Atawahuisha maiti? Kuna ishara gani kuhusu hayo katika uumbaji Wake?” Akasema:

«يَا أَبَا رَزِينِ! أَمَا مَرَزَتْ بِوَادِي قَوْمِكَ مُمَجَّلًا ثُمَّ مَرَزَتْ بِهِ يَهْتَرُ خَصِرًا»

“Ewe Abu Razin! Umepita katika bonde la kaumu yako (na kuliona) likiwa jangwa na lisilootesha kitu, kisha ukapita na kulikuta likitikisika na kuwa la kijani?”

¹ Muslim 4:2271.

Nikasema: "Ndiyo." Akasema:

فَكَذَّبِكَ يُحِبِّي اللهُ الْمُؤْتَىٰ

"Basi, kama hivyo ndivyo Allah Atakavyowahuisha waliokufa."¹

Utukufu Duniani na Akhera Unapatikana kwa Kumtii Allah تعالى

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا

"Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu."

Yaani, mwenye kupenda utukufu duniani na Akhera, basi ashikamane na kumtii Allah تعالى, atapata makusudio yake, kwani Allah تعالى, Ndiye Mmiliki wa dunia na Akhera, na Ndiye Mwenye Nguvu zote. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يَتَّخِذُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ أَيْتَعْتُونَ عَنْدهُمْ الْعِزَّةَ فَإِنَّ الْعِزَّةَ

لِلَّهِ جَمِيعًا

"Wale ambao huwafanya makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je! Wanataka wapate kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu." (4:139)

وَلَا تَحْزَنْكَ قَوْلُهُمْ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

"Wala yasikuhzunishe maneno yao. Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu." (10:65)

وَاللَّهُ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُنَافِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ

"Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Utukufu - Yeye, na Mtume Wake, na Waumini. Lakini wanaafiki hawajui." (63:8)

Mujahid alisema:

¹ Ahmad 4:12.

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ

“Mwenye kutaka utukufu...”

Kwa kuyaabudu masanamu,

فَإِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

“...basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu.” (4:139)¹

Qatadah alisema tena:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا

“Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, atafute hadhi, nguvu na utukufu kupitia katika kumtii Allah Mtukufu.²

Amali Njema Hupanda kwa Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى:

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ

“Kwake Yeye hupanda neno zuri...”

Yaani, dhikri, kisomo na dua. Hayo yalisemwa na ulamaa wa Salaf zaidi ya mmoja. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Al-Mukhariq bin Sulaym kuwa alisema, ‘Abdullah bin Mas‘ud رضي الله عنه alituambia: “Pindi tunapokusimulieni Hadithi, basi hukuleteeni pamoja na usadikishwaji wake kutoka katika Kitabu cha Allah تعالى. Mja Muislamu akisema: ‘Utukufu ni wa Allah تعالى nami nashikamana na kumsifu. *Hamd* ni za Allah تعالى, Hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Allah تعالى ni Mkubwa na Ametakasika.’ Malaika huyachukua na kuyaweka chini ya ubawa wake na kupanda nayo mbinguni. Basi kila akiwapita kundi la Malaika, humombea maghufira aliyeyasema mpaka ayafikishe mbele ya Allah تعالى.” Halafu ‘Abdullah رضي الله عنه akasoma:

¹ At-Tabari 20:443.

² At-Tabari 20:444.

إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ¹

“Kwake Yeye hupanda neno zuri, na amali njema Yeye Huitukuza.”¹

Imamu Ahmad alimnukuu Nu‘man bin Bashir رضي الله عنه kwamba alisema: Mtume ﷺ alisema:

«الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ مِنْ جَلَالِ اللَّهِ مِنْ تَسْبِيحِهِ وَتَكْبِيرِهِ وَتَحْمِيدِهِ وَتَهْلِيلِهِ، يَتَعَاطَفْنَ حَوْلَ الْعَرْشِ لَهُنَّ دَرَجَاتٌ كَدَوِي السَّحَابِ، يَذْكُرْنَ بِصَاحِبِهِنَّ، أَلَا يُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَنْ لَا يَزَالَ لَهُ عِنْدَ اللَّهِ شَيْءٌ يُذَكَّرُ بِهِ»

“Wanaomkumbuka Allah kwa kusema: ‘Utukufu ni wa Allah, Utakasifu, Ukubwa, Hamdi ni Vyake, na La ilaaha illallah. Maneno haya yanaizunguka Arshi yakivuma kama nyuki, yakiwataja waliyoyasema. Mmoja wenu hapendi kiwepo kitu kwa Allah kinachomtaja yeye?’²

Hii ilinukuliwa na Ibn Majah pia.³ Kauli ya Allah تعالى:

وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ⁴

“...na amali njema Yeye huitukuza.”

‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Neno jema ni kumtaja Allah تعالى, inapandishwa mpaka kwa Allah تعالى, na amali njema ni kutekeleza faradhi. Mwenye kumtaja Allah تعالى wakati wa kutekeleza jambo lake la faradhi, basi amali yake huchukua ile dhikri na kupanda nayo hadi kwa Allah تعالى. Mwenye kumtaja Allah تعالى pasi na kutekeleza faradhi zake basi kauli zake zitakataliwa, na amali zake pia.”⁴ Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ يَمْكُرُونَ السَّيِّئَاتِ

“Na wanaopanga vitimbi vya maovu...”

¹ At-Tabari 20:444.

² Ahmad 4:268.

³ Ibn Majah 2:1252.

⁴ At-Tabari 20:445.

Mujahid, Sa'id bin Jubayr na Shahr bin Hawshab walisema: "Hii inarejea kwa wanaofanya riya katika matendo yao."¹ Yaani, wanawafanyia watu hila kwa kuwafanya wawaone kwamba wako katika kumtii Allah تعالی, ilhali wameghadhikiwa na Allah تعالی kwa riya yao.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

هَمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَكْرُؤٌ لَّيْسَ لَهُ مِيقَاتٌ

"...watapata adhabu kali. Na vitimbi vya hao vitaondokea patupu."

Yaani, vitaharibika na kubatilika, na uongo wao utadhihiri na kwa wenye uoni na utambuzi, kwani hapana yeyote aliyeificha siri, bali Allah تعالی Huiweka wazi usoni mwake au kwa kuteleza kwa ulimi wake, au atamsababisha mtu aivae kama nguo. Ikiwa ni njema basi ni kheri kwake, na kama ni mbaya, basi ni shari. Afanyaye riya hatoendelea kumhadaa yeyote isipokuwa mpumbavu, lakini Waumini wenye uoni hawahadaiki na hayo, bali hudhihirikiwa katika muda wa karibu sana. Naye Mjuzi wa ghaibu hafichikiwi na kitu chochote.

Allah تعالی Ndiye Muumbaji na Mjuzi wa Ghaibu

Kauli ya Allah تعالی:

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نَظْفٍ

"Na Mwenyezi Mungu Amekuumbeni kutokana na udongo Kisha kwa tone la manii.."

Yaani, alianza kumuumba baba yenu, Adam عليه السلام, kwa udongo, kisha Akajaalia kizazi chake kutokana na maji (manii) dhalili,

ثُمَّ جَعَلَكُمْ أَزْوَاجًا

"Kisha Akakufanyeni mwanamume na mwanamke."

Yaani, mwanamume na mwanamke. Kutokana na ulatifu na rehema Zake kwamba Amekuumbieni wanawake kutokana na jinsi yenu ili mpate utulivu kwao.

¹ At-Tabari 20:447

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أُنْثَىٰ وَلَا تَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ ۗ

“Na mwanamke yeyote hachukui mimba, wala hazai, ila kwa ilimu Yake.”

Yaani, Yeye Anajua sana hayo, hapana chochote cha kujificha dhidi Yake, bali,

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَتٍ إِلَّا يَابِسُ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

“Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha.”
(6:59)

Maelezo yamekwishatangulia katika Kauli ya Allah تعالى:

اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنْثَىٰ وَمَا تَغِيضُ الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ ۗ وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٥٨﴾ عَلِيمٌ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْكَبِيرِ ۗ أَلْمُتَعَالِ ﴿٥٩﴾

“Mwenyezi Mungu Anajua mimba abebayo kila mwanamke, na kinachopunguka na kuzidi matumboni. Na kila kitu Kwake ni kwa kipimo. Yeye Ndiye Mwenye Kujua yanayoonekana na yasioonekana; Mkuu Aliyetukuka.” (13:8-9)

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمُرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ ۗ

“...Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu.”

Yaani, baadhi ya manii yale hupewa umri mrefu, jambo ambalo Yeye Analijua na kuna nukuu ya hayo katika Kitabu cha Awali alichu nacho Yeye.

وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمْرِهِ

“...wala hapunguziwi katika umri wake...”

Dhamiri inarejea katika jinsi, si katika dhati, kwani umri mrefu ulio ndani ya Kitabu na katika Ujuzi wa Allah تعالى, hautapunguzwa. Imesimuliwa kupitia isnadi ya Al-'Awfi kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا يُعْمَرُ مِنْ مُعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمْرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

“...Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu. Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, Anasema: Hapana yeyote ambaye Nimemhukumu kuwa na umri mrefu, isipokuwa ataufikia muda huo Niliompangia. Imekwishahukumiwa kwamba ataufikisha umri ambao aliopangiwa, hazidishiwi. Wala hapana yeyote aliyepangiwa umri mfupi, bali ataufikia umri huo na ataufikia muda alioandikiwa. Hiyo ndiyo maana ya Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا يُنْقَصُ مِنْ عُمْرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

“...wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu. Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.”

Alisema: “Hayo yameandikwa katika Kitabu Alichu nacho.”¹ Baadhi yao kama hivyo amesema adh - Dhahak bin Muzahim: wamesema: Maana,

وَمَا يُعْمَرُ مِنْ مُعَمَّرٍ

“Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu...”

Yaani, kiasi Anachomjaalia katika muda wake wa kuishi,

وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمْرِهِ

“...wala hapunguziwi katika umri wake...”

¹ At-Tabari 20:447.

Muda wake unazidi kupungua kidogo kidogo. Yote hayo Anayajua Allah, mwaka hata mwaka, mwezi hadi mwezi, siku hadi siku, saa mpaka saa. Kila kitu kimeandikwa katika Kitabu Chake.”¹ Hayo ameyanukuu bin Jariri رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Malik. Na pia ndio mtazamo wa Assudi, Atwaa na Al-Khurasani. Katika kuitafsiri Aya hii tukufu, An-Nasai alinukuu Hadithi ya Anas bin Malik رضي الله عنه kwamba alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَنْ سَرَّهُ أَنْ يُبْسَطَ لَهُ فِي رِزْقِهِ وَيُنْسَأَ لَهُ فِي أَثَرِهِ فَلْيَصِلْ رَحِمَهُ»

“Mwenye kupenda akunjukiwe katika riziki yake na aongezewe umri mrefu, basi aunge undugu wake.”²

Ilinukuliwa na Al-Bukhari, Muslim na Abu Dawud.³ Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

“Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani ni jepesi na rahisi Kwake, Ana Ujuzi Mkubwa wa viumbe Wake, kwani Ilimu Yake inavienea vitu vyote, hapana chochote cha kujificha dhidi Yake.

وَمَا يَسْتَوِي الْبَحْرَانِ هَذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ سَائِغٌ شَرَابُهُ وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَمِن كُلِّ تَاكُلُونَ لَحْمًا طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُونَ حَلِيَّةً تَلْبَسُونَهَا وَتَرَى الْفُلْكَ فِيهِ مَوَاحِرَ لَتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِمْ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾

12. “Na bahari mbili haziwi sawa; haya ni matamu yenye ladha, mazuri kunywa. Na haya ni ya chumvi, machungu. Na kutokana na bahari zote mnakula nyama mpya (isiyo chacha). Na mnatoa mapambo mnayoyavaa. Na unaona ndani yake marikebu zinakata (maji) ili mtafute fadhila Zake, na ili mpate kushukuru.”

¹ At-Tabari 20:447.

² An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:321.

³ *Fat'h Al-Bari* 4:553, Muslim 4:1982, Abu Dawud 2:321.

Miongoni mwa Neema na Ishara za Allah

Allah تعالی Anaeleza kuhusu Kudura Yake kubwa katika Kuumba vitu mbalimbali. Aliumba maji ya namna mbili, mojawapo maji-baridi. Hayo ni katika mito hii iliyojitandaza baina ya watu, midogo na mikubwa, kulingana na haja, katika majimbo, miji midogo na mikubwa, katika makazi, katika nchi kavu na majangwani. Nayo ni maji-baridi na matamu kwa mwenye kuyanywa,

وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ

“Na haya ni ya chumvi, machungu.”

Yaani, machungu. Nayo ni bahari tulivu ambayo hupitiwa na meli kubwa. Nayo huwa ni ya chumvi na yasiyonyweka. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

وَهَذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ

“Na haya ni ya chumvi, machungu.”

Kisha, Allah تعالی Amesema:

وَمِنْ كُلِّ تَأْكُلُونَ لَحْمًا طَرِيًّا

“Na kutokana na bahari zote mnakula nyama mpya (isiyo chacha).”

Yaani, Samaki. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَتَسْتَخْرِجُونَ حِلْيَةً تَلْبَسُونَهَا

“Na mnatoa mapambo mnayoyavaa.”

يَخْرُجُ مِنْهَا الْوَلُؤُؤُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٣٥﴾ فَبِأَيِّ آيَاتِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٦﴾

“Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani. Basi ni ipi katika neema za Mola Wenu Mlezi mnayoikanusha?” (55:22-23)

وَتَرَى الْفُلْكَ فِيهِ مَوَاجِرَ

“Na unaona ndani yake marikebu zinakata maji...”

Yaani, zinasafiri na kuyapasua maji kwa omo, nayo ni sehemu ya mbele yenye umbo la nundu ambayo inashabihiana na kibyongo cha ndege. Sehemu hiyo ni usawa wa kifua chake. Mujahid alisema: “Majahazi huzipazua pepo na wala hayapasui pepo katika majahazi isipokuwa yale makubwa.” Kauli ya Allah تعالی:

لَتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ

“...ili mtafute Fadhila Zake...”

Yaani, kwa safari zenu za kibiashara kutoka nchi moja mpaka nyingine na jimbo moja hadi jingine.

وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“...na ili mpate kushukuru.”

Yaani, mnamshukuru Mola Wenu kwa kukudhalilishieni uumbaji huu mkubwa. Nayo ni bahari, mnaitumia namna mpendavyo, mnakwenda mahali mpatakapo, wala hakuna kizuizi dhidi yenu, bali kwa Kudura Yake Amekutiisheni vya mbinguni na ardhini. Yote kwa sababu ya Fadhila na Rehema Zake.

* * *

يُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَسَخَّرَ
 الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلًّا يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ذَٰلِكُمْ اللَّهُ
 رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۗ وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مَا
 يَمْلِكُونَ مِنْ قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾ إِنْ تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا
 دُعَاءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا مَا اسْتَجَابُوا لَكُمْ ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ
 يَكْفُرُونَ بِشِرْكِكُمْ ۗ وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ ﴿١٤﴾ * يَا أَيُّهَا
 النَّاسُ أَنْتُمُ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾
 إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٦﴾ وَمَا ذَٰلِكَ
 عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿١٧﴾ وَلَا تَرَوْا زُرَّةً وَزُرَّةً وَزُرَّةً أُخْرَى ۗ وَإِنْ تَدْعُ
 مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جِهْلِهَا لَا تَحْمِلْ مِنْهُ شَيْئًا وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ إِنَّمَا
 تُنذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ ۗ وَمَنْ
 تَرَكَ فَإِنَّمَا يَكْفُرُ لِنَفْسِهِ ۗ إِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿١٨﴾ وَمَا
 يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ﴿١٩﴾ وَلَا الظُّلُمَاتُ وَلَا النُّورُ
 ﴿٢٠﴾ وَلَا الظُّلُّ وَلَا الْحُرُورُ ﴿٢١﴾ وَمَا يَسْتَوِي الْأَحْيَاءُ وَلَا
 الْأَمْوَاتُ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُسْمِعُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَمَا أَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَّن
 فِي الْقُبُورِ ﴿٢٢﴾ إِنْ أَنْتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿٢٣﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ
 بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ۗ وَإِنْ مِنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴿٢٤﴾
 وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ جَاءَتْهُمْ
 رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالزُّبُرِ وَبِالْكِتَابِ الْأَمِينِ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ
 أَخَذْتُ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٢٦﴾

يُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوَلِّجُ النَّهَارَ
 فِي اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ
 كُلًّا يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ذَٰلِكُمْ
 اللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۗ وَالَّذِينَ
 تَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ
 مِنْ قِطْمِيرٍ ﴿١٣﴾ إِنْ تَدْعُوهُمْ لَا
 يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا مَا
 اسْتَجَابُوا لَكُمْ ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ
 يَكْفُرُونَ بِشِرْكِكُمْ ۗ وَلَا يُنَبِّئُكَ
 مِثْلُ خَبِيرٍ ﴿١٤﴾

13. "Anauingiza usiku katika mchana, na Anauingiza mchana katika usiku. Na amevitiisha jua na mwezi. Kila kimojapo kinakwenda kwa muda maalumu. Huyu Ndiye Mwenyezi Mungu Mola Wenu Mlezi. Ufalme ni Wake. Na hao mnaowaomba badala Yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende."

14. "Kama Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni.

Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakayekupa habari vilivyo kama Yeye Mwenye habari.”

Miungu ya Washirikina Haimiliki Hata ugozi wa Tende (Qitmir)

Kadhalika, katika Kudura Zake timilifu na Nguvu Zake kubwa ni Kuutiisha usiku kwa kiza chake na mchana kwa mwangaza wake. Pia Huchukua urefu wa kimojawapo na Kuuongeza katika ufupi wa kingine na Kuvifanya vilingane. Kisha Huchukua kutoka kimojawapo na Kuingiza katika kingine, na hivyo Kukirefusha kimojawapo na Kukifupisha kingine, na Husababisha majira ya joto na ya baridi.

وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ

“Na Amevitiisha jua na mwezi.”

Yaani, nyota zilizokwenda na zilizotulia, na zenye kuangaza vitu vingine angani. Vyote viko katika mwendo kwa kiasi kilichopangwa, na katika njia zilizowekewa na kuhukumiwa na Mwenye Nguvu, Mjuzi.

كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى

“Kila kimojapo kinakwenda kwa muda maalumu.”

Yaani, hadi Siku ya Kiyama,

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ

“Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola Wenu Mlezi.”

Yaani, Aliyeyafanya haya Ndiye Mola Mlezi, Ambaye hapana wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye.

وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ

“Na hao mnaowaomba badala Yake...”

Miongoni mwa masanamu na miungu ya uongo iliyo katika sura ya hao mnaodai, miongoni mwa Malaika wa karibu,

مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ

“...hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende.”

Ibn 'Abbas , Mujahid, 'Ikrimah, 'Ataa, Al-'Atwiyyah Al-'Awfi, Al-Hasan, Qatadah na wengine رضي الله عنهم walisema: "Qitmir ni nyuzi iliyojishikiza katika kokwa ya tende".¹ Yaani hawamiliki chochote mbinguni wala ardhini, japo kiasi hiki cha Qitmir. Kisha, Allah تعالى Amesema:

إِنْ تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ

"Mkiwaomba hawasikii maombi yenu..."

Yaani, miungu mnyodai badala ya Allah haisikii dua zenu, kwa sababu ni viumbe visivyo hai, havina roho ndani yao,

وَلَوْ سَمِعُوا مَا اسْتَجَابُوا لَكُمْ

"...na hata wakisikia hawakujibuni."

Yaani, hawawezi kitu chochte katika mnavyovitaka,

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُونَ بَشِرِكِكُمْ

"Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu."

Maana yake, watajitenga nanyi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ

دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٥﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٦﴾

"Na nani aliyepotea zaidi kuliko yule anayemuomba asiyekuwa Allah, ambaye hatamuitikia mpaka siku ya kiyama na kwamba hana habari kabisa na huko kumuomba kwao. Na watu watakapokusanywa, hao miungu watakuwa maadui zao na watakataa kuabudiwa kwao." (46:5-6)

وَأَتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ إِلَهاتٍ لِيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٧﴾ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ

عَلِيَهُمْ ضُفَاءً ﴿٨﴾

"Na wamechukua miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati iwape nguvu. Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao." (19:81-82)

¹ At-Tabari 20:453.

وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ

“Na hapana atakayekupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari.”

Yaani, wala hatakupasha khabari za matokeo ya mambo, na namna ya mwisho wake mithili ya Mwenye Kuzijua zaidi. Qatadah alisema: “Anamaanisha, Nafsi Yake Allah تعالى, kwani, bila shaka yoyote, Yeye ni Mwenye Kujua zaidi matukio.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَنْتُمْ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٥﴾ إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٦﴾ وَمَا ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿١٧﴾ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ وَإِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا لَا تُحْمَلْ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ إِنَّمَا تُنذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ ۗ وَمَنْ تَزَكَّىٰ فَإِنَّمَا يَتَزَكَّىٰ لِنَفْسِهِ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿١٨﴾

15. “Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitisha, Msifiwa.”

16. “Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe vipya.”

17. “Na hilo si gumu kwa Mwenyezi Mungu.”

18. “Na wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Na aliyetopewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, hata kama ni ndugu. Hakika wewe unawaonya wale wanaomcha Mola Wao Mlezi ya kuwa hawamuoni, na wanashika Swala. Na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.”

Watu ni mafukara kwa Allah na Kila Mtu Atabeba Mzigo Wake Siku ya Kiyama

Allah Anaeleza juu ya kutokuwa Kwake na haja ya wengine, na kwamba viumbe wote wanamhitaji Yeye na kudhalilika kwao mbele Yake. Allah تعالى Amesema:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَنْتُمْ الْفُقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ

“Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake, wao wana haja Kwake katika mienendo yao yote na kutulia kwao

kote. Allah تعالى Hana haja kwao kabisa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

“...na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitosha, Msifiwa.”

Yaani, Yeye ni Mpweke kwa Kujitosha Yeye Mwenyewe, Hana mshirika. Yeye ni Msifiwa katika kila Alifanyalo, Alisemalo, Analolihukumu na Analolilazimisha. Kauli ya Allah تعالى:

إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ

“Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe vipya.”

Yaani, Angetaka Angekuondoeni, enyi watu! na Kuwaleta watu wengine badala yenu. Wala hili si gumu wala halina wa kulizuia. Kwa ajili hii, Allah Amesema:

وَمَا ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ بَعْرِينٌ ﴿١٧﴾

“Na hilo si gumu kwa Mwenyezi Mungu.” (14:20)

Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَرُدُّ وَازِرَةً وِزْرًا أُخْرَى ۗ

“Na wala hatobeba mbebaji mzigo wa mwingine.”

Yaani, katika Siku ya Kiyama,

وَإِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا

“Na aliyetopewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe...”

Yaani, hata kama nafsi iliyoemewa na mizigo yake ikiomba msaada wa kubebewa mizigo yake au baadhi yake,

لَا تُحْمَلُ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ ۗ

“...hautachukuliwa hata kidogo, hata kama ni ndugu.”

Yaani, hata akiwa ana uhusiano wa karibu naye, kama vile baba au mwanaye, kila mmoja atashughulika na nafsi au hali yake. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِنَّمَا تُنذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ

“Hakika wewe unawaonya wale wanaomcha Mola Wao Mlezi kwa ghaibu, na wanashika Sala.”

Yaani, kwa hakika, wata kaopata mafunzo kutokana na uliyokuja nayo, ni wale wenye uoni na ufahamu, wenye kumkhofu Mola Wao, wenye kuyafanya waliyo amrisha kuyafanya,

وَمَنْ تَزَكَّى فَإِنَّمَا يَتَزَكَّى لِنَفْسِهِ

“Na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake.”

Yaani, mwenye kufanya jema, basi, manufaa yake humrudia yeye mwenyewe,

وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ

“Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, marejeo ni Kwake Yeye, Yeye ni Mwepesi wa hesabu na Atamlipa kila mtendaji kwa mujibu wa amali yake, kama ni njema basi ni kheri, na kama ni mbaya, basi ni shari.

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ ﴿١٩﴾ وَلَا الظُّلُمَاتُ وَلَا النُّورُ ﴿٢٠﴾ وَلَا الظُّلُمُ وَلَا النُّورُ ﴿٢١﴾ وَمَا يَسْتَوِي الْأَحْيَاءُ وَلَا الْأَمْوَاتُ ﴿٢٢﴾ إِنَّ اللَّهَ يُسْمِعُ مَن يَشَاءُ ﴿٢٣﴾ وَمَا أَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَّن فِي الْقُبُورِ ﴿٢٤﴾ إِنَّ أَنْتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿٢٥﴾ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ﴿٢٦﴾ وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴿٢٧﴾ وَإِن يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالزُّبُرِ وَبِالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿٢٨﴾ ثُمَّ أَخَذْتُ الَّذِينَ كَفَرُوا ﴿٢٩﴾ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٣٠﴾

19. “Na kipofu na mwenye kuona hawalingani.”

20. “Wala giza na mwangaza.”

21. “Wala kivuli na joto.”

22. “Wala hawalingani walio hai na wafu. Hakika Mwenyezi Mungu Humsikilizisha Amtakae. Wala wewe huwezi kuwasikilizisha walio makaburini.”

23. *“Hukuwa wewe ila ni mwonyaji.”*

24. *“Hakika Sisi Tumekutuma wewe kwa Haki, kuwa ni mtoa habari njema na mwonyaji. Na hapana umma wowote ila alipita muonyaji kati yao.”*

25. *“Na wakikukanusha basi walikwisha wakanusha waliokuwa kabla yao. Mitume wao waliwajia kwa dalili za wazi wazi na kwa maandiko na Kitabu chenye nuru.”*

26. *“Kisha Nikawakamata waliokufuru. Basi kuchukia Kwangu kulikuwaje?”*

Muumini na Kafiri Hawalingani

Allah تعالى Anasema, vitu hivyo ni kinyume, hutofautiana, kipofu na mwenye kuona hawalingani, vitu hivyo vinatofautiana mno. Giza na nuru havilingani, wala kivuli na joto la jua, walio hai na wafu. Huu ni mfano Alioupiga Allah kuhusu Waumini ambao ndio walio hai na makafiri ambao ndio maiti.

أَوْ مَنْ كَانَ مَيِّتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَنْ مَثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا

“Je, aliyekuwa maiti kisha Tukamhuisha, na Tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo?” (6:122)

مَثَلُ الْفَرِيقَيْنِ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصْمَىٰ وَالْبَصِيرِ وَالسَّمِيعِ ۗ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا

“Mfano wa makundi mawili ni kama kipofu kiziwi, na mwenye kuona na anasikia. Je, wawili hawa wanakuwa sawa kwa kufananishwa?” (11:24)

Basi, Muumini anasikia na kuona, yuko katika nuru, anatembea katika njia nyoofu duniani na Akhera, mpaka atakapotulia katika Pepo zenye vivuli na chemchemi. Kafiri ni kipofu na kiziwi, anatembea gizani, wala hawezi kutoka humo, bali amepotelea katika upotevu wake, duniani na Akhera, hadi

atakapomalizikia katika joto kali, upepo wa moto na maji yachemkayo na kivuli cha moshi mweusi, si wa baridi wala si chema. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ يُسْمِعُ مَنْ يَشَاءُ ۗ

“Hakika Mwenyezi Mungu Humsikilizisha Amtakaye.”

Yaani, Huwaongoza katika kusikiliza ushahidi na kuukubali na kuufuata,

وَمَا أَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَّن فِي الْقُبُورِ

“Wala wewe si wa kuwasikilizisha walio makaburini.”

Yaani, kama wafu wasivyonufaika na uongofu na wito kuuendea ukweli baada ya mauti yao na kuingia makaburini huku walishaukataa, ndivyo pia walivyo hawa washirikina walioandikiwa kuangamia wala hutaweza kuwaongoa,

إِنَّ أَنْتَ إِلَّا نَذِيرٌ ﴿٣٥﴾

“Hukuwa wewe ila ni mwonyaji.”

Yaani, jukumu lako ni kufikisha ujumbe na kuonya. Allah تعالى Humuacha Apotee Amtakaye na Humuongoza Amtakaye.

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ بِالْحَقِّ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ۗ

“Hakika Sisi Tumekutuma wewe kwa Haki, kuwa ni mbashiri na mwonyaji.”

Yaani mtoaji bishara kwa Waumini na mwenye kuwaonya makafiri.

وَإِنَّ مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

“Na hapana umma wowote ila ulipata mwonyaji kati yao.”

Yaani, hakuna umma uliopita kwa wanaadamu isipokuwa Allah تعالى Aliwapelekea waonyaji na kuwaondolea udhuru. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ ۗ وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ

“Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa.” (13:7)

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ۗ فَمِنْهُمْ مَن هَدَىٰ
 اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ

“Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo Aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao uliowathibitikia upotovu.” (16:36)

Kuna Aya nyingi kuhusu mada hii. Kauli ya Allah تعالى:

وَإِن يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ

“Na wakikukanusha basi walikwishawakanusha waliokuwa kabla yao. Mitume wao waliwajia kwa dalili wazi wazi...”

Nayo ni miujiza ya waziwazi na ushahidi mbalimbali wenye kukata hoja,

وَبِالزُّبُرِ

“...na kwa maandiko...” Navyo ni Vitabu,

وَبِالْكِتَابِ الْمُنِيرِ

“...na Kitabu chenye nuru.” Yaani, kilichodhahiri na bayana,

ثُمَّ أَخَذْتُ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Kisha Nikawakamata waliokufuru.”

Maana yake, pamoja na haya yote, hao waliwakadhibisha Mitume wao katika waliyokuja nayo, wakashikwa. Yaani kwa adhabu kali.

فَكَيْفَ كَانَتْ نِكْمِي

“Basi kuchukia Kwangu kulikuwaje?”

Maana, umeonaje ukubwa, ukali na ufikaji wa ghadhabu Zangu (katika Kuwaadhibu). Allah تعالى Ndiye Mjuzi.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ ثَمَرَاتٍ
 مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهَا ۖ وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌ بَيْضٌ وَحُمْرٌ مُخْتَلِفٌ
 أَلْوَانُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ ﴿٢٧﴾ وَمِنَ النَّاسِ وَالْدَّوَابِّ
 وَالْأَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ كَذَلِكَ ۗ إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ
 عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ ﴿٢٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ
 يَتْلُونَ كِتَابَ اللَّهِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ
 سِرًّا وَعَلَانِيَةً يَرْجُونَ تِجَارَةً لَّن تَبُورَ ﴿٢٩﴾ لِيُؤْتِيَهُمُ
 أُجُورَهُمْ وَيَزِيدَهُم مِّن فَضْلِهِ ۗ إِنَّهُ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٠﴾
 وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا
 بَيْنَ يَدَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٣١﴾ ثُمَّ أَوْرَثْنَا
 آلَ كِنَانَةَ الَّذِينَ أَصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا ۗ فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ
 لِّنَفْسِهِ وَمِنْهُمْ مُقْتَصِدٌ وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ إِذِنَ اللَّهُ
 ذَٰلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ﴿٣٢﴾ جَنَّتٌ عَدْنٌ يَدْخُلُونَهَا
 يُحَلِّونَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۗ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ
 ﴿٣٣﴾ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنَّا الْحَزْنَ ۗ إِنَّ
 رَبَّنَا لَغَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٤﴾ الَّذِي أَحَلَّنَا دَارَ الْمَقَامَةِ مِنْ
 فَضْلِهِ ۗ لَا يَمَسُّنَا فِيهَا نَصَبٌ وَلَا يَمَسُّنَا فِيهَا لُغُوبٌ ﴿٣٥﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً
 فَأَخْرَجْنَا بِهِ ثَمَرَاتٍ مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهَا ۖ
 وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌ بَيْضٌ وَحُمْرٌ
 مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٌ ﴿٢٧﴾
 وَمِنَ النَّاسِ وَالْدَّوَابِّ وَالْأَنْعَامِ
 مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ كَذَلِكَ ۗ إِنَّمَا يَخْشَى
 اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 عَزِيزٌ غَفُورٌ ﴿٢٨﴾

27. "Je! Huoni kwamba
 Mwenyezi Mungu Amete-
 remsha maji kutoka
 mbinguni, na kwayo Tume-
 yatoa matunda yenye rangi
 mbali mbali. Na katika
 milima imo mistari myeupe
 na myekundu yenye rangi
 mbali mbali, na myeusi
 sana."

28. "Na katika watu, na
 wanyama wanaotambaa,
 na mifugo, pia rangi zao ni
 mbalimbali. Kwa hakika
 wanaomcha Mwenyezi
 Mungu miongoni mwa waja
 wake ni wana- zuoni.

Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwingi wa Kusamehe."

Kudura Timilifu ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu ukamilifu wa Kudura Yake katika Kuumba Kwake vitu namna kwa namna kutokana na kitu kimoja. Nayo ni maji ambayo huyateremsha kutoka angani. Kwa maji hayo, hutoka matunda ya rangi tofauti tofauti, kama vile manjano, nyekundu, kijani, nyeupe na nyingine. Ni kama inavyoshuhudiwa kuwepo kwa namna mbalimbali za rangi, ladha na harufu za matunda. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ مُتَجَبَّرَاتٌ وَجَنَّاتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزُرْعٌ وَنَخِيلٌ وَصِنَوَانٌ وَغَيْرُ صِنَوَانٍ يُسْقَى
بِمَاءٍ وَحِدٍ وَنُفْضِلٌ بَعْضُهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ
يَعْقِلُونَ ﴿١٣﴾

“Na katika ardhi kuna mistari na bustani za zabibu na mbogamboga na mitende iliyoota miwili au mitatu katika shina moja na kadhalika zikinyeshewa kwa maji hayo hayo lakini baadhi yao Tunaifanya kuwa bora zaidi ya mingine kuliwa. Hakika katika haya kuna ishara kwa watu wanaoelewa.” (13:4)

Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌ بَيْضٌ وَحُمْرٌ مُّخْتَلِفٌ أَلْوَانُهَا

“Na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbali mbali...”

Yaani, kadhalika, Aliiumba milima na Kuitofautisha rangi zake. Pia ni kama inavyoshuhudiwa kuwepo myeupe na myekundu, na katika baadhi yake kuna njia. Hizo ndio *Judad*, neno ambalo umoja wake ni *Juddah*. Hiyo ni milima ya rangi tofauti tofauti pia. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema maana ya “*Al-Judad* ni njia.” Ndivyo pia, walivyosema Abu Malik, Al-Hasan, Qatadah na As-Suddi: “Na humo kuna *Al-Gharaabib* - nyeusi.” ‘Ikrimah alisema maana ya “*Al-Gharaabib* ni milima mirefu na nyeusi. Hii ilikuwa pia ndio rai ya Abu Malik, ‘Ata’ Al-Khurasani na Qatadah.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema: “Waarabu, pindi wakikieleza kitu cheusi sana, husema: *‘Aswad Gharbib*.” Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنَ النَّاسِ وَالْأَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُمْ كَذَلِكَ

“Na katika watu, na wanyama wanaotambaa, na mifugo, pia rangi zao mbalimbali.”

Maana yake, vivyo hivyo viumbe hai pia, kama vile watu na wanyama. Kwa maana ya kila kiumbe kitembeacho kwa miguu, **“na mifugo”**. Hapa pana kanuni ya lugha iliyotaja kitu cha ujumla kisha kinafuatiwa na makhususi. Hiyo nayo ni tofauti pia. Miongoni mwa watu, wapo Waberber, Wahabeshi, kuna watu weusi sana wasio Waarabu, Waslav (*As-Swaqaalibah*) na Warumi, ambao ni weupe sana. Waarabu ni baina ya hivyo, na Wahindi chini ya hivyo. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine:

وَإِخْتِلَافُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَانِكُمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٣٠﴾

“...na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi.” (30:22)

Wanyama na mifugo pia, ni wenye kutofautiana rangi, hata wa jinsi moja, bali hata wa namna moja, wamekhitilafiana. Mnyama mmoja huweza kuwa na rangi mbalimbali. Ametukuka Allah, Mbora wa Kuumba. Allah Amesema:

إِنَّمَا تَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

“Kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni.”

Yaani, wanaomkhofu ukweli wa kumkhofu ni maulamaa wanaomjua, kadiri ya kumjua Mtukufu, Muweza, Mwenye Kujua, Mwenye Sifa kamilifu, Mwenye kuitwa kwa Majina Mazuri zaidi, basi kumkhofu ndivyo kunavyozidi na kukithiri.

‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا تَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

“Kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni.”

Alisema: “Ni wale wanaojua kwamba Allah تعالى ni Muweza wa kila jambo.”¹ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Mjuzi zaidi juu ya *Ar-Rahman* katika waja Wake, ni yule ambaye hamshirikishi na kitu, akahalalisha cha halali na kuharamisha cha haramu, akahifadhi wasia Wake akayakinisha kwamba atakutana Naye na atahesabiwa kwa amali zake.’ Sa’id bin Jubayr alisema: “Khofu ndiyo inayoweka kizuizi baina yako na kumuasi Allah تعالى.” Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema: “Mwenye elimu ni yule mwenye kumkhofu *Ar-Rahman* kuhusu ghaibu, akayapenda anayoyapenda Allah تعالى, akayaacha yanayomgha- dhabisha Allah تعالى.” kisha, Al-Hasan alisoma:

إِنَّمَا نَحْنُ لِلَّهِ مِنَ عِبَادِهِ الَّذِينَ أَلْعَمْتُؤُا إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ غَفُورٌ

“Kwa hakika wanaomcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwingi wa Kusamehe.”

Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Abu Hayyan At-Taymi kutoka kwa mtu ambaye alisema: “Ilikuwa ikisemwa kwamba watu wenye elimu ni wa namna tatu, ‘Anayemjua Allah تعالى pamoja na Amri Zake, Anayemjua Allah تعالى pasi na kuzijua amri Zake na anayejua Amri za Allah تعالى pasi na kumjua Allah تعالى. Anayemjua Allah تعالى pamoja na Amri Zake ni anayemcha Allah تعالى, anajua mipaka na mambo ya faradhi. Anayemjua Allah تعالى pasi na kujua amri Zake ni anayemkhofu Allah تعالى bila kujua mipaka na faradhi. Anayejua amri za Allah تعالى bila kumjua Yeye, ni anayejua mipaka na mambo ya faradhi lakini hamuogopi Allah تعالى.

إِنَّ الَّذِينَ يَتْلُونَ كِتَابَ اللَّهِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً يَرْجُونَ تِجْرَةً لَّن تَبُورَ ﴿٢٩﴾ لِيُؤْفِقَهُمْ أَجْرَهُمْ وَيَزِيدَهُمْ مِّن فَضْلِهِ إِنَّهُ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٠﴾

29. “Hakika wale wanaosoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wakashika Sala, na wakatoa kwa siri na kwa dhaahiri katika Tulivyo waruzuku, hao hutaraji biashara yenye faida isiyomalizika.”

30. “Ili Yeye Awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na Awazidishie kutokana na Fadhila Zake. Hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe Mwingi wa Shukrani.”

¹ At-Tabari 20:462

Waislamu Ndio Watakaokuwa na Faida Akhera

Allah تعالى Anaeleza kuhusu waja Wake Waumini ambao wanakisoma Kitabu chake na wanakiamini, na wanayatenda yaliyo ndani yake, kama vile kusimamisha Sala na kutoa kutokana na Alivyowaruzuku Allah تعالى katika nyakati zilizifaradhishwa, usiku na mchana, kwa siri na kwa dhahiri,

يَرْجُونَ تِجْرَةً لَّان تَبُورَ

“...hao hutaraji biashara yenye faida isiyomalizika.”

Yaani, wanatumaini kupata malipo kwa Allah تعالى, ambayo hapana budi, watayapata tu.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

لِيُوقِفَهُمْ أَجْرَهُمْ وَيَزِيدَهُمْ مِّن فَضْلِهِ

“Ili Yeye Awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na Awazidishie kutokana na Fadhila Zake.”

Yaani, bila shaka, Atawalipa kutokana na waliyoyafanya na Kuwazidishia ziada ambayo hawajawahi kuiwaza,

إِنَّهُمْ غَفُورٌ

“Hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe...”

Yaani, kwa madhambi yao,

شَاكُورٌ

“Mwingi wa Shukrani.”

Kwa ajili ya amali zao chache.

وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَابِ هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ

بَصِيرٌ ﴿٣١﴾

31. “Na kitabu Tulichokuletea kwa wahyi ndicho cha haki kinasadikisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake. Hakika Mwenyezi Mungu kwa waja Wake ni Mwenye habari na Mwenye Kuona.”

Qur'an ni Kitabu cha Kweli cha Allah

Allah تعالیٰ Anasema:

وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ

“Na kitabu Tulichokuletea Wahy...”

Katika Kitabu (Qur'an), ewe Muhammad.

هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“...ndicho cha haki kinachosadilisha (vitabu) vilivyokuwa kabla yake.”

Yaani, Vitabu vilivyotangulia, kama ambavyo navyo vimetoa ushahidi wa kuja kwa Qur'an na kwamba ni yenye kuteremshwa kutoka kwa Mola wa ulimwengu.

إِنَّ اللَّهَ بِعِبَادِهِ لَخَبِيرٌ بَصِيرٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu kwa waja Wake ni Mwenye habari na Mwenye Kuona.”

Yaani, Anajua khabari zao na yule anayestahiki kupata fadhila juu ya wengine. Kwa ajili hii, Aliwafadhilisha Manabii na Wajumbe juu ya watu wengine, Akawafadhilisha baadhi ya Manabii juu ya wenzao, Akawanyanyua baadhi yao kwa daraja nyingi, na Akajaalia nafasi ya Muhammad ﷺ kuwa juu yao wote, Rehema na Amani ziwaendee wao wote.

ثُمَّ أَوْرَثْنَا الْكِتَابَ الَّذِينَ اصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا فَمَنْهُمْ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ وَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ

وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ إِذْنِ اللَّهِ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ﴿٣٥﴾

32. “Kisha Tumewarithisha Kitabu hao ambao Tuliowateua miongoni mwa waja wetu. Kati yao wapo waliojidhulumu nafsi zao, na wapo wa katikati, na wapo waliotangulia katika mambo ya kheri, kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Fadhila kuu.”

Warithi wa Qur'an wapo aina Tatu.

Allah Anasema: Kisha Tuliwajaalia walioshikamana na Kitabu, chenye kusadikisha Vitabu vilivyotangulia, ambao Tumewateua kutoka miongoni mwa waja wetu. Na hao ni umma huu, kisha Akawagawa katika namna tatu. Akasema:

فَمِنْهُمْ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ

“Kati yao wapo waliojidhulumu nafsi yake...”

huyu ni ambaye ni mzembe katika kuyafanya baadhi ya mambo ya wajibu na anayafanya baadhi ya mambo ya haramu,

وَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ

“...na wapo wa katikati...”

Huyu ni mwenye kutimiza mambo ya wajibu, anayaacha yaliyoharamishwa, lakini, huenda akawa anayaacha baadhi ya mambo mazuri na anayafanya baadhi ya mambo yasiyopendeza.

وَمِنْهُمْ سَابِقٌ بِالْخَيْرَاتِ إِذْنِ اللَّهِ

“...na wapo waliotangulia katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.”

Huyu hufanya mambo ya wajibu pamoja na mambo ya Sunna, na anayaacha ya haramu na ya kuchukiza na baadhi ya yaliyoruhusiwa. ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

ثُمَّ أَوْرَثْنَا الْكِتَابَ الَّذِينَ اصْطَفَيْنَا مِنْ عِبَادِنَا

“Kisha Tumewarithisha Kitabu hao ambao Tuliwateua miongoni mwa waja Wetu.”

Alisema: “Hawa ni umma wa Muhammad ﷺ. Allah Aliwarithisha wao kile Kitabu ambacho Allah Alikiteremsha; wale wanaojidhulumu nafsi zao watasamehewa, wanaofuata njia ya wastani watahesabiwa kwa wepesi na wanaowatangulia katika kufanya mema wataingia peponi bila ya kuhesabiwa.”¹

¹ At-Tabari 20:465.

Abu Al-Qasim At-Tabarani رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba siku moja alisema:

«شَفَاعَتِي لِأَهْلِ الْكِبَائِرِ مِنْ أُمَّتِي»

“Shufaa yangu ni kwa ajili ya wenye madhambi makubwa katika umma wangu.”

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: “Waliotangulia katika mambo ya kheri wataingia peponi bila ya hesabu, watu wa wastani, wataingia kwa Rehema za Allah تعالى na wenye kudhulumu nafsi zao na *As-hab Al-A'raaf* wataingia kwa uombezi wa Muhammad ﷺ.”²

Pia, ilinukuliwa na wengi katika *Salaf* kuwa watu wanaodhulumu nafsi zao miongoni mwa Ummah bado nao ni miongoni mwa wale Aliowachagua Allah تعالى, ingawa hawajakamilika na wana makosa (kwa kutoshikamana na njia iliyonyooka). Wengine wamesema kuwa wenye kudhulumu nafsi zao si sehemu ya Ummah huu na si miongoni mwa Aliowateua Allah تعالى na waliorithi Kitabu. Rai sahihi ni kuwa, wao pia ni sehemu ya Ummah huu.

Fadhila za Maulamaa

Maulamaa ndio waliobahatika zaidi kupata baraka na ndio wenye kustahiki zaidi neema hiyo. Imam Ahmad Abu Dawud رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Qais bin Kathir alisema, “Mtu mmoja wa Al-Madinah alikuja kwa Abu Darda رضي الله عنه alipokuwa huko Damaskasi. (Abu Darda) alisema, ‘Umekuja kufanya nini, ewe ndugu yangu?’ Alimjibu, ‘Ni Hadithi niliyoisikia kuwa unaisimulia kutoka kwa Mtume ﷺ.’ Akamuuliza, ‘Je, umekuja kufanya biashara?’ Akamjibu, ‘Hapana.’ Akamuuliza tena, ‘Je, umekuja kwa ajili ya Hadithi hii tu?’ Akamjibu, ‘Ndiyo.’ Akasema, ‘Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَنْ سَلَكَ طَرِيقًا يَطْلُبُ فِيهَا عِلْمًا، سَلَكَ اللَّهُ تَعَالَى بِهِ طَرِيقًا إِلَى الْجَنَّةِ، وَإِنَّ الْمَلَائِكَةَ لَتَضَعُ أَجْنِحَتَهَا رِضًا لِطَالِبِ الْعِلْمِ، وَإِنَّهُ لَيَسْتَعْفِرُ لِلْعَالِمِ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ حَتَّى الْجِبْتَانِ فِي الْمَاءِ، وَقَضَى الْعَالِمِ عَلَى الْعَابِدِ كَفْضِلِ الْقَمَرِ عَلَى سَائِرِ الْكَوَاكِبِ، وَإِنَّ الْعُلَمَاءَ هُمْ وَرَثَةُ الْأَنْبِيَاءِ، وَإِنَّ الْأَنْبِيَاءَ لَمْ يُوْرُثُوا دِينَارًا وَلَا دِرْهَمًا، وَإِنَّمَا وَرَثُوا الْعِلْمَ، فَمَنْ أَخَذَ بِهِ أَخَذَ بِحِطِّ وَافِرٍ»

¹ Angalia juzu ya nne, *Tafsir ya Surat Al-A'raaf*.

² At-Tabarani 11:189.

“Mwenye kufuata njia ya kutafuta ndani yake elimu, Allah Atampitisha njia ya kuelekea Peponi, Malaika nao kwa hakika, hushusha mbawa zao kumvidhia mwenye kutafuta elimu. Pia walio mbinguni na ardhini humuombea msamaha mwanazuoni, mpaka samaki majini. Ubora wa mwanazuoni juu ya mfanya ibada ni kama ubora wa mwezi juu ya nyota zingine. Kwa hakika Maulamaa wao ndio warithi wa Mitume, kwani Mitume hawakurithisha Dinari wala Dirhamu, lakini wamerithisha elimu; na mwenye kuipokea, atakuwa amepata hadhi kubwa sana.”¹

Pia imeandikwa na Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah.²

جَنَّتْ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا يُحَلِّوْنَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۖ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٣٥﴾
 وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنَّا الْحَزْنَ ۖ إِنَّ رَبَّنَا لَغَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٦﴾ الَّذِي أَحَلَّنَا دَارَ
 الْمُقَامَةِ مِنْ فَضْلِهِ ۗ لَا يَمَسُّنَا فِيهَا نَمَسٌ وَلَا يَمَسُّنَا فِيهَا لُغُوبٌ ﴿٣٧﴾

33. “Bustani ya milele wataiingia. Huko watavikwa bangili za dhahabu, na lulu, na nguo zao humo ni za hariri.”

34. “Na watasema: Alhamdulillah, Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetuondolea huzuni zote. Hakika Mola Wetu Mlezi bila ya shaka ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Shukrani.”

35. “Ambaye kwa Fadhila Yake Ametuweka makao ya kukaa daima; humu haitugusi taabu wala humu hakutugusi kuchoka.”

Allah تعالى Anaeleza kwamba wateule hawa wote kutoka kwa waja Wake, ambao wamerithishwa Kitabu kilichoteremshwa kutoka kwa Mola wa ulimwengu, watapata, katika Siku ya Kiyama, makazi ya milele Peponi, ambamo wataingia katika siku ya Marejeo yao na kukaribishwa kwa Allah تعالى,

يَدْخُلُونَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۖ

“Huko watavikwa bangili za dhahabu, na lulu...”

Ni sawa na ilivyonukuliwa ndani ya Sahih toka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema:

¹ Ahmad 5:196.

² Abu Dawud 4:157, Tuhfat Al-Ahwadhi 7:450, Ibn Majah 1:81.

«تَبْلُغُ الْجِلْيَةَ مِنَ الْمُؤْمِنِ حَيْثُ يَبْلُغُ الْوُضُوءُ»

“Mapambo ya Muumini yanafikia mahali udhu unapofikia.”¹

وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ

“...na nguo zao humo ni za hariri.”

Kwa ajili hii, walikatazwa duniani, lakini Allah تعالى Amewahalalishia katika Akhera.

Imenukuliwa ndani ya Sahih Muslim kwamba Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ لَيْسَ الْحَرِيرَ فِي الدُّنْيَا لَمْ يَنْبَسْهُ فِي الْآخِرَةِ»

“Mwenye kuvaa hariri duniani hatozivaa Akhera.”²

Na alisema pia,

«هِيَ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا، وَلَكُمْ فِي الْآخِرَةِ»

“Hayo ni yao duniani, na ni yenu huko Akhera.”³

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنَّا الْحَزْنَ

“Na watasema, Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetuondolea huzuni zote.

Hiyo ni khofu dhidi ya chochote chenye kukhofiwa, kimeshaondolewa kutoka kwetu na Akatupa faraja dhidi ya tuliyokuwa tukiyakhofu na kujihadhari nayo, miongoni mwa wasiwasi wa duniani na Akhera. Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine walisema: “Anawaghufiria madhambi mengi na anayapokea mema hata madogo madogo.”

الَّذِي أَحَلَّنَا دَارَ الْمَقَامَةِ مِن فَضْلِهِ

“Ambaye kwa Fadhila Yake Ametuweka makao ya kukaa daima...”

Wanasema: ‘Aliyetupatia makazi haya na nyadhifa hizi ni kwa Fadhila, Neema na Rehema Zake, amali zetu hazikuwa zikilingana na haya.’ Ni sawa na ilivyonukuliwa ndani ya Sahih kwamba Mtume ﷺ alisema:

¹ Muslim 1:219.

² Fat’h Al-Bari 10:296. Hii ni kwa wanaume tu.

³ Fat’h Al-Bari 10:296.

«لَنْ يُدْخِلَ أَحَدًا مِنْكُمْ عَمَلُهُ الْجَنَّةَ»

“Amali za yeyote kati yenu hazitamuingiza Peponi.”

Wakasema: “Hata wewe, ewe Mtume wa Allah?”

«وَلَا أَنَا إِلَّا أَنْ يَتَّعَمِدَنِي اللَّهُ تَعَالَى بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَفَضْلٍ»

“Hata mimi, isipokuwa Allah Atakaponifunika kwa Rehema na Fadhila Zake.”¹

لَا يَمَسُّنَا فِيهَا نَصَبٌ وَلَا يَمَسُّنَا فِيهَا لُغُوبٌ

“...humu haitugusi taabu wala humu hakutugusi kuchoka.”

Yaani, humu hautatugusa taabu wala uchovu. Maneno yote mawili (*Naswab* na *Lughub*) hutumika kumaanisha uchovu, kana kwamba maana yake, hawatakuwa na uchovu katika miili yao wala roho zao, Allah تعالی Ndiye Mjuzi. Katika hayo, ni kwamba, wao, walikuwa wakijichosha duniani kwa kufanya ibada, lakini kuwajibika kwao kutakwisha kwa kuingia Peponi, na kuwa katika mapumziko yenye kuendelea daima. Allah تعالی Amesema:

كُلُوا وَأَشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا أَسْلَفْتُمْ فِي الْأَيَّامِ الْخَالِيَةِ

“Waambiwe: Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya mlivyotanguliza katika siku zilizopita.” (69:24)

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 10:132.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِنْ عَذَابِهَا ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَافِرٍ ﴿٣٦﴾ وَهُمْ يَصْطَرِحُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۖ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَنْ تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ ۖ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿٣٧﴾ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ غَيْبٍ ۖ أَلَسْمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٣٨﴾ هُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ ۖ فَمَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ إِلَّا مَقْتًا ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرُهُمْ إِلَّا خَسَارًا ﴿٣٩﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ شُرَكَاءَكُمُ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ أَمْ آتَيْنَهُمْ كِتَابًا فَهُمْ عَلَىٰ بَيِّنَتٍ مِّنْهُ ۚ بَلْ إِن يَبْدُو لِلظَّالِمِينَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا إِلَّا غُرُورًا ﴿٤٠﴾ * إِنَّ اللَّهَ يُمَسِّكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا ۖ وَلَئِن زَالَتَا إِنْ أَمْسَكَهُمَا مِنْ أَحَدٍ مِّنْ بَعْدِهِ ۚ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤١﴾

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِنْ عَذَابِهَا ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَافِرٍ ﴿٣٦﴾ وَهُمْ يَصْطَرِحُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۖ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَنْ تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ ۖ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿٣٧﴾

36. "Na waliokufuru watakuwa na Moto wa Jahannamu, hawatahukumiwa kufa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivyo ndivyo Tunavyomlipa kila mwenye kuzidi ukafiri."

37. "Na humo watapiga makelele: Mola Wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale Tuliyokuwa tukiyafanya. Kwani hatukupeni umri wa kutosha

kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani waliodhulumu hawana wa kuwanusuru."

Malipo ya Makafiri na Hali yao Itakavyokuwa Ndani ya Jahanamu

Baada ya kutaja hali za wenye furaha, Allah تعالى Amezanza Kubainisha yatakayowasibu waovu. Allah تعالى Amesema:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا

“Na waliokufuru watakuwa na Moto wa Jahannamu, hawahukumiwi wakafa...”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿٧٤﴾

“Hafi humo wala haishi.” (20:74)

Imenukuliwa ndani ya Sahih Muslim kwamba Mtume ﷺ amesema:

«أَمَّا أَهْلُ النَّارِ الَّذِينَ هُمْ أَهْلِهَا، فَلَا يَمُوتُونَ فِيهَا وَلَا يُحْيَوْنَ»

“Ama watu wa Motoni ambao ndio wakazi wake, hawatakufa wala kuwa hai humo.”¹

Allah تعالى Amesema tena katika Aya nyingine:

وَنَادَوْا بِمَمْلِكٍ لِّيَقْضَىٰ عَلَيْنَا رُبُّكَ ۖ قَالَ إِن كُنتُمْ مِّنْكَثُوبٍ ﴿٧٧﴾

“Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik! Na Atufishe Mola wako Mlezi! Naye aseme: Hakika nyinyi mtakaa humo humo!” (43:77)

Hivyo, wao katika hali yao hiyo, watayaona mauti kuwa ni mapumziko kwao, lakini hakutakuwa na njia ya kuyafikia hayo. Allah تعالى Amesema:

لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِّنْ عَذَابِهَا ۗ

“...hawahukumiwi wakafa, wala hawatapunguziwa adhabu yake.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

¹ Muslim 1:172.

﴿٧٥﴾ إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّهِينٍ ﴿٧٦﴾ لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ وَهُمْ فِيهِ مُّبْلِسُونَ ﴿٧٧﴾

“Kwa hakika wakosefu watakaa katika adhabu ya Jahannamu. Hawatapumzishwa nayo na humo watakata tamaa.” (43:74-75)

﴿٧٨﴾ كَلَّمَا حَبَتِ زِدْنَهُمْ سَعِيرًا ﴿٧٩﴾

“Kila moto ukifanya kusinzia Tutazidi Kuuchochea uwake kwa nguvu.” (17:97)

﴿٨٠﴾ فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا ﴿٨١﴾

“Basi onjeni! Nasi hatutakuzidishieni ila adhabu!” (78:30)

Kisha, Allah تعالى Amesema:

كَذَلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَافِرٍ ﴿٨٢﴾

“Hivyo ndivyo Tunavyomlipa kila mwenye kuzidi ukafiri.”

Yaani, haya ni malipo ya kila mwenye kumkufuru Mola Wake na akaukadhibisha ukweli. Kauli ya Allah تعالى:

وَهُمْ يَصْطَرِحُونَ فِيهَا ﴿٨٣﴾

“Na humo watapiga makelele...”

Yaani, wataita huku wakiwa ndani yake, huku wakimsihi Allah تعالى kwa sauti zao,

رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ﴿٨٤﴾

“...Mola Wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyokuwa tukiyafanya.”

Yaani, wataomba kurejeshwa duniani ili wafanya amali tofauti na za awali, na Allah تعالى Anajua sana kwamba lau Atawarudisha duniani, wangeliyarejea yale waliyokatazwa, na kwamba wao wanaongopa.

Kwa ajili hii, Hatawajibu maombi yao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَهَلْ إِلَىٰ خُرُوجٍ مِّن سَبِيلٍ ﴿٤٠﴾ ذَٰلِكُمْ بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ^ط وَإِنْ يُشْرَكَ بِهِ

“Basi je, ipo njia ya kutoka? Hayo ni hivyo kwa sababu mlikuwa akiombwa Mwenyezi Mungu Peke Yake mnakataa. Na Akishirikishwa mnaamini.” (40:11-12)

Yaani, hatakujibuni hayo, kwani nyinyi mlikuwa hivyo hivyo, na lau kama mtarejeshwa mtayafanya mambo mliyokatazwa. Kwa ajili hii, Allah Amesema:

أُولَٰئِكَ نَعَمَّرَكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَن تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ الْآذِنُ^ط

“...Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Muonyaji?”

Yaani, je hamkuishi kwa muda mrefu duniani kiasi kwamba kama mngekuwa katika wenye kunufaika na ukweli, mngenufaika nao tangu mlipokuwa hai. Imamu Ahmad alimnukuu Abu Hurayrah رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَقَدْ أَعَدَّ اللَّهُ تَعَالَىٰ إِلَىٰ عَبْدٍ أَحْيَاهُ حَتَّىٰ بَلَغَ سِتِينَ أَوْ سَبْعِينَ سَنَةً، لَقَدْ أَعَدَّ اللَّهُ تَعَالَىٰ إِلَيْهِ، لَقَدْ أَعَدَّ اللَّهُ تَعَالَىٰ إِلَيْهِ»

“Allah Amekwishampa udhuru mja aliyempa umri mpaka akafikisha miaka sitini au sabini. Allah Ameshamaliza kumpa udhuru, Allah Amekwishamaliza kumpa udhuru.”¹

Kama hivi hivi alinukuu Imamu Al-Bukhari katika Mlango wa uhamasishaji wa kutenda mema ndani ya Sahih yake, kwamba alisema, Mtume ﷺ alisema:

«أَعَدَّ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِلَىٰ أَمْرِي أَوْ آخِرَ عُمُرِهِ حَتَّىٰ بَلَغَ سِتِينَ سَنَةً»

“Allah Ameshamaliza kumpa udhuru mtu ambaye Amempa umri hadi akafikisha miaka sitini.”²

¹ Ahmad 2:275.

² Fat-h Al-Bari 11:243.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa, Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ عَمَّرَهُ اللَّهُ تَعَالَى سِتِّينَ سَنَةً فَقَدْ أَعْدَرَ إِلَيْهِ فِي الْعُمُرِ

“Mtu ambaye Allah Kampa umri mpaka akafikisha miaka sitini, Amekwishampa udhuru.”¹

Hii iliandikwa pia na Imamu Ahmad na An-Nasai katika Mlango wa uhamasishaji wa kutenda mema *Ar-Riqaq*.² Imekuwa hivyo kwa sababu huu ndio umri ambao Allah تعالى Huwaondolea udhuru wowote waja wake, na ndio umri wa kawaida kwa umma huu, kama ilivyosimulia Hadithi hiyo. Abu Hurayrah عنه رضي الله alisema, Mtume ﷺ amesema:

«أَعْمَارُ أُمَّتِي مَا بَيْنَ السِّتِينَ إِلَى السَّبْعِينَ، وَأَقَلُّهُمْ مَنْ يَجُوزُ ذَلِكَ»

“Wastani wa umri wa umma wangu ni baina ya miaka sitini na sabini, na ni wachache sana wanaopitisha umri huo.”

Hii ilinukuliwa pia na At-Tirmidhi na Ibn Majah katika Kitabu cha *Az-Zuhd* (kuupa nyongo ulimwengu).³ Kauli ya Allah تعالى:

وَجَاءَكُمْ النَّذِيرُ^ط

“Na akakujieni Muonyaji?”

Ilisimuliwa kwamba Ibn ‘Abbas عنه رضي الله, ‘Ikrimah, Abu Ja’far Al-Baqir, Qatadah na Sufyan bin ‘Uyaynah walisema: “Inamaanisha mvi.”⁴ As-Suddi na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam wamesema maana yake ni, “Mtume ﷺ.” Kisha Ibn Zayd akasoma:

هَذَا نَذِيرٌ مِّنَ النَّذْرِ الْأُولَى ﴿٥٦﴾

“Hili ni Onyo katika maonyo yale yale ya zamani.” (53:56)⁵

¹ At-Tabari 20:478.

² Ahmad 2:417, Tuhfat Al-Ashraf 9:472.

³ At-Tirmidhi na. 3550, Ibn Majah na. 4236.

⁴ Al-Baghawi 3:573.

⁵ At-Tabari 20:478.

Rai hii ndiyo iliyo sahihi, kwa mujibu wa Shayban ambaye alisimulia kwamba Qatadah alisema: “Ushahidi dhidi yao utatolewa kuhusu umri na Mitume.”¹ Hii ndiyo pia, rai ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى, na ndiyo maana dhahiri ya Aya hizi:

وَنَادُوا يَمْلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رُبُّكَ ۗ قَالَ إِنَّكُمْ مَنِكُوتٌ ﴿٧٧﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ بِالْحَقِّ وَلَٰكِنَّا
أَكْثَرُكُمْ لِلْحَقِّ كَرِهُونَ ﴿٧٨﴾

“Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik! Na Atufishe Mola Wako Mlezi! Naye aseme: Hakika nyinyi mtakaa humo humo! Kwa yakini Tulikuleteeni Haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia Haki.” (43:77-78)

Maana yake, Tumekwisha kubainishieni ukweli kupitia ndimi za Mitume, nyinyi mkakataa na kuhalifu.

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا

“Wala Sisi hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume.” (17:15)

Kauli nyingine ya Allah تعالى:

كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلْتَهُمْ خَزَنَتُهُ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٨٨﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ فَكَذَّبْنَا
وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ إِنَّا نَتَمَرُّ إِلَّا فِي ضَلَالٍ كَبِيرٍ ﴿٨٩﴾

“Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni mwonyaji? Watasema: Kwani! Ametujia mwonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu Hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa!” (67:8-9)

Kauli ya Allah تعالى:

فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن نَّصِيرٍ

“Basi onjeni! Kwani waliodhulumu hawana wa kuwanusuru.”

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:32.

Yaani, onjeni adhabu ya Moto kama malipo ya kitendo chenu cha kuwakhaliifu Mitume katika amali zenu zote, basi leo hamtakuwa na wa kukunusuruni dhidi ya yale ambayo nyinyi mumo ndani yake, miongoni mwa adhabu kali na pingu.

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ غَيْبِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٣٦﴾ هُوَ الَّذِي
جَعَلَكُمْ خَلْقًا فِي الْأَرْضِ ۖ فَمَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرَهُمْ إِلَّا مَقْتًا ۖ وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرَهُمْ إِلَّا خَسَارًا ﴿٣٧﴾

38. “Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa siri za mbinguni na ardhini. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliomo vifuanii.”

39. “Yeye Ndiye Aliyekufanyeni manaibu katika ardhi. Na anayekufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola Wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila hasara.”

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Ujuzi Wake wa ghaibu ya mbingu na ardhi na kwamba Anayajua yote yaliyofichama katika siri mbalimbali na yaliyo nyuma ya dhamira, na Atamlipa kila mja kulingana na amali zake. Halafu Allah تعالى Amesema:

هُوَ الَّذِي جَعَلَكُمْ خَلْقًا فِي الْأَرْضِ ۚ

“Yeye Ndiye Aliyekufanyeni manaibu katika ardhi.”

Yaani, Anabadili kaumu moja kwa nyingine, na kizazi baada ya kizazi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاءَ الْأَرْضِ ۚ

“...na Akakufanyeni warithi wa ardhi?” (27:62)

فَمَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهُ ۖ

“Na anayekufuru, basi kufuru yake ni juu yake...”

Yaani, madhara yake yana mrudia mwenyewe, si kwa mwingine,

وَلَا يَزِيدُ الْكَافِرِينَ كُفْرَهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ إِلَّا مَقْتًا^ط

“...na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola Wao Mlezi ila kuchukiwa.”

Yaani, kila walipoendelea na kufuru yao, Allah تعالى Aliwa ghadhabikia, na kila wana vyoendelea hivyo watapata khasara nafsini mwao na katika familia zao katika Siku ya Kiyama.

Ni kinyume na Waumini, kwani kila unavyorefuka umri wa mmoja wao na amali zake kuwa njema, basi daraja zake na makazi yake Peponi hupanda zaidi, malipo yao huzidi; na Muumba Wake, Mola wa ulimwengu Humpenda.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ شُرَكَاءَكُمُ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أُرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ أَمْ آتَيْنَهُمْ كِتَابًا فَهُمْ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّنْهُ ۗ بَلْ إِنْ يَعِدُ الظَّالِمُونَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا إِلَّا غُرُورًا ﴿٤٠﴾ * إِنَّ اللَّهَ يُمِيسِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا ۗ وَلَئِن زَالَتَا إِنْ أَمْسَكَهُمَا مِنْ أَحَدٍ مِّنْ بَعْدِهِ ۗ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤١﴾

40. “Sema: Mnawaona hawa miungu wenu wa kishirikina mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu! Nionesheni wameumba sehemu gani katika ardhi? Au wana ushirika wowote katika mbingu? Au Tumewapa Kitabu nao kwa hicho wakawa na hoja zilizo wazi? Lakini madhalimu hawahidiani wao kwa wao ila udanganyifu tu.”

41. “Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke mahali pake. Na zikiondoka hapana yeyote wa kuzizuia isipokuwa Yeye. Hakika Yeye ni Mpole Mwenye Kusamehe.”

Maelezo Juu ya Kushindwa Miungu ya Washirikina na Kubainishwa Uwezo Mkubwa wa Allah تعالى.

Allah تعالى Anamuambia Mtume wake ﷺ Awaambie washirikina,

أَرَأَيْتُمْ شُرَكَاءَ كُمُ الَّذِينَ نَدَعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ

“Mnawaona hawa miungu wenu wa kishirikina mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu!”

Yaani, masanamu na washindani,

أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَوَاتِ

“Nionesheni wameumba sehemu gani katika ardhi? Au wana ushirika wowote katika mbingu?”

Yaani, hawana chochote katika hayo, hawamiliki japo ugozi wa kokwa ya tende. Kauli ya Allah تعالى:

أَمْ آتَيْنَاهُم كِتَابًا فَهُمْ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّنْهُ

“Au Tumewapa Kitabu nao kwa hicho wakawa na hoja zilizo wazi?”

Yaani, ‘Au Tumewateremshia kitabu wanachokitumia kama hoja ya ushirikina na ukafiri? Si hivyo,’

بَلْ إِن يَبْدُ الظَّالِمُونَ بَعْضُهُم بَعْضًا إِلَّا غُرُورًا

“Lakini madhalimu hawaahidiani wao kwa wao ila udanganyifu tu.”

Yaani, bali katika hayo wamefuata matamania, rai na haja zao walizotamani kwa ajili ya nafsi zao, nazo ni ghururi, batili na uongo. Kisha, Allah تعالى Alieleza kuhusu Uwezo Wake mkubwa, na kwa ajili Yake, mbingu na ardhi vimesimama kwa Amri Yake na nguvu Aliyojaalia baina ya hivyo inayovishikilia. Akasema:

إِنَّ اللَّهَ يُمَسِّكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا

“Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke mahali pake.”

Yaani, zisitoke mahali zilipo. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ^٥

“...na Amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa Idhini Yake.” (22:65)

وَمِنَ آيَاتِهِ أَنْ تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ^٤

“Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake.” (30:25)

وَلَئِنْ رَأَيْتَا إِنْ أَمْسَكْتُهُمَا مِنْ أَحَدٍ مِّنْ بَعْدِهِ^٤

“Na zikiondoka hapana yeyote wa kuzizuia isipokuwa Yeye.”

Maana yake, hakuna awezaye kuzidumisha wala kuzibakisha isipokuwa Yeye, pamoja na hayo, Yeye ni Mpole sana, Msamehevu sana. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا

“Hakika Yeye ni Mpole Mwingi wa Kusamehe.”

Yaani, Huwaona waja wake wakiwa wanamkufuru na kumuasi. Yeye Huvumilia na Kuakhirisha, Anaangalia na Anachelewesha, Aharikishi, na Anawasitiri wengine na Kuwaghufiria.

* * *

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَّيَكُونُنَّ
 أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ۗ فَلَمَّا جَاءَهُمْ نَذِيرٌ مَّا زَادَهُمْ
 إِلَّا نُفُورًا ﴿٤٢﴾ اسْتَكْبَارًا فِي الْأَرْضِ وَمَكْرَ السَّيِّئِ ۗ وَلَا
 يَحِيقُ الْمَكْرُ السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ ۗ فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا سُنَّتَ
 الْأَوَّلِينَ ۗ فَلَن نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ۗ وَلَن نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ
 تَحْوِيلًا ﴿٤٣﴾ أَوَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ
 عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَكُنُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۗ وَمَا كَانَ
 اللَّهُ لِيُعْجِزَهُ مِن شَيْءٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۗ إِنَّهُ
 كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا ﴿٤٤﴾ وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا
 كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرِهَا مِن دَابَّةٍ وَلَكِن يُؤَخِّرُهُمْ
 إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ
 كَانَ بِعِبَادِهِ بَصِيرًا ﴿٤٥﴾

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَّيَكُونُنَّ
 أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ۗ فَلَمَّا جَاءَهُمْ نَذِيرٌ مَّا
 زَادَهُمْ إِلَّا نُفُورًا ﴿٤٢﴾ اسْتَكْبَارًا فِي
 الْأَرْضِ وَمَكْرَ السَّيِّئِ ۗ وَلَا يَحِيقُ
 الْمَكْرُ السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ ۗ فَهَلْ
 يَنْظُرُونَ إِلَّا سُنَّتَ الْأَوَّلِينَ ۗ فَلَن
 نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَبْدِيلًا ۗ وَلَن نَجِدَ
 لِسُنَّتِ اللَّهِ تَحْوِيلًا ﴿٤٣﴾

42. "Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kuapa kwao, kwamba akiwajia mwonyaji bila ya shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine

lolote. Lakini alipowajia mwonyaji hakuwazidishia ila kuikimbia (hiyo Haki)."

43. "Kwa kutakabari kwao katika nchi, na kufanya vitimbi vya uovu. Na vitimbi viovu havimsibu ila mwenyewe aliyevifanya. Hebu hawangojei yaliowasibu watu wa kale? Basi hutapata mabadiliko katika mtindo wa Mwenyezi Mungu. Wala hutapata mageuko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu."

Makafiri Walitamani Mwonyaji Aje, Alipokuja, Walimkataa

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Makuraishi na Waarabu, kwamba waliapa kwa Allah تعالى kwa bidii, kabla ya Mtume ﷺ kupelekwa kwao,

لَئِنْ جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَّيَكُونُنَّ أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ۗ

“...kwamba akiwajia mwonyaji bila ya shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine lolote.”

Maana yake, kuliko umma wote ambao ulipelekewa Mitume. Hayo ni kwa mujibu wa Adh-Dhahhak na wengine.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

أَنْ تَقُولُوا إِنَّمَا أَنْزَلَ الْكِتَابَ عَلَيَّ طَائِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا وَإِنْ كُنَّا عَنْ دِرَاسَتِهِمْ لَغَنَفِيلِينَ ۚ

﴿١٦٦﴾ أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أَنْزَلْنَا الْكِتَابَ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۗ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ

رَبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةً ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ بِبَيِّنَاتِ اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ

“Msije mkasema: Hakika mataifa mawili kabla yetu yamete-remshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna habari ya waliyokuwa wakiyasoma. Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola Wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema. Basi nani aliye dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na akajitenga nazo?” (6:156-157)

وَإِنْ كَانُوا لَيَقُولُونَ ﴿١٦٧﴾ لَوْ أَنَّ عِنْدَنَا ذِكْرًا مِنَ الْأُولِينَ ﴿١٦٨﴾ لَكُنَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ

﴿١٦٩﴾ فَكَفَرُوا بِهِ ۗ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿١٧٠﴾

“Na walikuwapo waliokuwa wakisema: Tungelikuwa na Ukumbusho kama wa watu wa zamani. Bila ya shaka tungelikuwa ni waja wa Mwenyezi Mungu wenye ikhlasi. Lakini waliukataa. Basi watakuja jua.” (37:167-170)

Allah تعالى Amesema:

فَلَمَّا جَاءَهُمْ نَذِيرٌ

“Lakini alipowajia mwonyaji...”

Naye ni Muhammad ﷺ pamoja na Kitabu chake Kitukufu alichoteremshiwa, nayo ni Qur'an yenye kubainisha,

مَا زَادَهُمْ إِلَّا نُفُورًا

“...hakuwazidishia ila kuikimbia hiyo Haki.”

Yaani, hawakuongezekewa na kitu isipokuwa ukafiri. Allah تعالى Akalibainisha hilo kwa Kauli Yake:

أَسْتَكْبَرًا فِي الْأَرْضِ

“Kwa kutakabari kwao katika nchi...”

Yaani, walifanya kiburi katika kuzifuata Aya za Allah تعالى ,

وَمَكَرَ السَّيِّئُ

“Na vitimbi viovu...”

Yaani, waliwafanyia watu vitimbi katika kuwazuilia njia ya Allah تعالى,

وَلَا يَحْقِيقُ الْمَكْرُ السَّيِّئُ إِلَّا بِأَهْلِهِ

“Na vitimbi viovu havimsibu ila mwenyewe aliyevifanya.”

Yaani, uovu wa hayo utawaendea wao wenyewe, si wengine. Kauli ya Allah تعالى:

فَهَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا سُنَّتَ الْأَوَّلِينَ

“Hebu hawangojei yaliowasibu watu wa kale?”

Yaani, adhabu ya Allah تعالى juu yao kwa kuwakadhibisha kwao Mitume Wake na kukhalifu kwao Amri Zake.

فَلَنْ نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَبْدِيلًا

“Basi hutapata mabadiliko katika mtindo wa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hakuna kughairishwa wala kubadilishwa, bali hiyo ni yenye kwenda kama ilivyo kwa kila mkadhibishaji.

وَلَنْ نَجِدَ لِسُنَّتِ اللَّهِ تَحْوِيلًا

“Wala hutapata mageuko katika mwendo wa Mwenyezi Mungu.”

Yaani,

وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ^ع

“Na Mwenyezi Mungu Anapowatakia watu adhabu hakuna cha kuzuia...” (13:11)

Wala hakuna yeyote wa kuwaondolea hilo wala kuwakinga. Allah تعالى Ndiye Mjuzi.

أَوَلَمْ يَسْمُرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَكُنُوا أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً
وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعْجِزَهُ مِنْ شَيْءٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا
﴿٤٤﴾ وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرهَا مِنْ دَابَّةٍ وَلَكِنْ
يُؤَخِّرُهُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى^ط فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَارْتَبِ اللَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِمُ بَصِيرًا ﴿٤٥﴾

44. “Je! Hawakusafiri katika ardhi wakaona vipi ulikuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Na hao walikuwa wana nguvu zaidi kuliko wao. Na hapana kitu kinachoweza kumshinda Mwenyezi Mungu mbinguni wala katika ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye Kujua, Mwenye Uweza.”

45. “Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwatesa watu kwa waliyoyachuma, basi asingelimuacha juu ya ardhi kiumbe chochote kinachotembea. Lakini Yeye Anawaakhirisha mpaka ufike muda maalumu. Basi ukifika muda wao basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake barabara.”

Mwisho Mbaya wa Waliowapinga Mitume

Allah تعالى Anasema: “Ewe Muhammad! Waambie hao wanaokadhibisha wa Ujumbe uliokuja nao, ‘Tembeeni ardhini na muangalie mwisho wa waliowakadhibisha Mitume ulikuwaje. Waone jinsi Allah تعالى Alivyo-waangamiza. Makafiri nao na mithili yao kikamilifu. Makazi yao yaligeuzwa matupu na wapakonywa kila kitu, miongoni mwa neema baada ya kuishi kwa anasa na kuwa wengi na kuwa na vituo vingi, mali nyingi na watoto. Hayo hayakuwasaidia lolote, wala hayakuwaondolea japo chembe ya adhabu ya Allah تعالى, pindi Amri Yake ilipokuja.” Ni kwa sababu Yeye, Hakimshindi kitu pindi Akitaka kiwe, mbinguni na ardhini.

إِنَّهُ كَانَ عَلِيمًا قَدِيرًا

“Hakika Yeye ni Mwenye Kujua, Mwenye Uweza.”

Yaani, ni Mwenye Kujua kila kitu na ni Muweza wa vitu vyote.

Hekima ya kucheleweshwa Adhabu

Kisha, Allah تعالى Amesema:

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرهَا مِنْ دَابَّةٍ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwatesa watu kwa waliyoyachuma, basi asingelimuacha juu ya ardhi kiumbe chochote kinachotembea.”

Yaani, lau Allah تعالى Angeliwachukulia kwa dhambi zao zote, basi Angeliwa-angamiza watu wote wa duniani pamoja na riziki na wanyama wanaowamiliki. Sa’id bin Jubayr na As-Suddi walisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرهَا مِنْ دَابَّةٍ

“...basi Asingelimuacha juu ya ardhi kiumbe chochote kinachotembea.”

Yaani, Angelizuia mvua isinyeshe, kisha viumbe wote wangelikufa,

وَلَكِنَّ يُؤَخِّرُهُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ

“Lakini Yeye Anawaakhirisha mpaka ufike muda maalumu.”

Yaani, lakini Anawapa muda mpaka Siku ya Kiyama, kisha Atawahesabu katika siku hiyo, na kila mwenye amali atalipwa kulingana nayo. Hivyo, atawalipa thawabu wale waliomtii na Kuwaadhibu waliomuasi. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِعِبَادِهِ بَصِيرًا

“Basi ukifika muda wao basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake barabara.”

Mwisho wa Tafsiri ya *Suratu Faatwir*, Sifa Njema na Shukurani ni kwa Allah تعالیٰ.

* * *

Tafsiri ya Suratu Yasin

Sura ya 36

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za Suratu - Yasin

Al-Hafidhi Abu Ya'la رحمه الله تعالى amepokea riwaya kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَرَأَ يَسَ فِي لَيْلَةٍ أَصْبَحَ مَغْفُورًا لَهُ، وَمَنْ قَرَأَ حَمَّ الَّذِي يُذَكَّرُ فِيهَا الدُّخَانَ أَصْبَحَ مَغْفُورًا لَهُ»

"Mwenye kusoma Yasin usiku, ataamka akiwa amesamehewa madhambi yake, na mtu akisoma Ha-Mim ambayo ndani yake kuna Ad-Dukhan (Moshi) imetajwa ataamka akiwa amesamehewa (madhambi yake)."

Silisila ya riwaya hii ni nzuri (Jayyid).¹

Ibn Hibbani رحمه الله تعالى ameandika katika Sahihi yake kuwa Jundub bin Abdallah رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَرَأَ يَسَ فِي لَيْلَةٍ ابْتِغَاءً وَجِهَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ غُفِرَ لَهُ»

*"Mwenye kusoma Ya-Sin usiku akitaka radhi za Allah atasamehewa (madhambi yake)."*²

* * *

¹ *Musnad Abi Ya'laa*, 11:93. Hadithi hizo mbili si sahihi - Ama kauli ya Ibn Kathir kuwa isnadi ya Abu Hurayrah ni nzuri, ameisimulia kutoka kwa Al-Hasan, ambayo ni silsila isiyothibitishwa na wanazuoni wa Hadithi. Kwa hivyo, Ibn Hajar (*At-Taqrib*) alisema, "Al-Hasan hakumsikia Abu Hurayrah." Huenda Ibn Kathir alikuwa na rai kuwa inawezekana kuwa alisikia.

² Ibn Hibban 4:121

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْيَاسِيْنَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَسَّ ۝ وَالْقُرْآنِ الْحَكِيمِ ۝ إِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ۝
 عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۝ تَنْزِيلَ الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ۝
 لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أُنذِرَ ءَابَاؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ ۝ لَقَدْ حَقَّ
 الْقَوْلُ عَلَى أَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ۝ إِنَّا جَعَلْنَا فِي
 أَعْيُنِهِمْ أَغْلَظًا فَهِيَ إِلَى الْآذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ۝
 وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا وَمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا
 فَأَعْيَيْنَهُمْ فَهُمْ لَا يَبْصُرُونَ ۝ وَسَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ
 أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ۝ إِنَّمَا تُنذِرُ مَنِ اتَّبَعَ
 الذِّكْرَ وَخَشِيَ الرَّحْمَنَ الْغَيْبَ ۝ فَبَشِّرْهُ بِمَغْفِرَةٍ وَأَجْرٍ
 كَرِيمٍ ۝ إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا
 وَءَاتَرَهُمْ ۝ وَكُلُّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ ۝
 وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلًا أَصْحَابَ الْقَرْيَةِ إِذْ جَاءَهَا الْمُرْسَلُونَ ۝
 إِذْ أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمُ اثْنَيْنِ فَكَذَّبُوهُمَا فَعَزَّزْنَا بِثَالِثٍ فَقَالُوا إِنَّا
 إِلَيْكُمْ مُّرْسَلُونَ ۝ قَالُوا مَا أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا وَمَا أَنزَلَ
 الرَّحْمَنُ مِن شَيْءٍ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا تَكْذِبُونَ ۝ قَالُوا رَبُّنَا
 يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ۝ وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلَاغُ
 الْمُبِينُ ۝

يَسَّ ۝ وَالْقُرْآنِ الْحَكِيمِ ۝
 إِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ۝ عَلَى
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ۝ تَنْزِيلَ الْعَزِيزِ
 الرَّحِيمِ ۝ لِتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أُنذِرَ
 ءَابَاؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ ۝ لَقَدْ
 حَقَّ الْقَوْلُ عَلَى أَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا
 يُؤْمِنُونَ ۝

1. Ya-Sin (Y.S.).

2. Kwa Haki ya Qur'ani iliyojaa hikima!

3. Hakika wewe ni miongoni mwa mitume (waliotumwa).

4. Na uko Juu ya Njia Iliyonyooka.

5. Na hii Qur'an ni Uteremsho wa Mwenye Nguvu, Mwingi wa Kurehemu.

6. Ili uwaonye watu ambao baba zao hawakuonywa, basi wao wamekuwa wenye kughafilika.

7. Bila ya shaka kauli imekwishathibiti juu ya wengi katika wao, kwa hivyo hawaamini.

Mtume aliletwa kuwa Muonyaji.

Katika Sura *Al-Baqarah* tumeeleza kuhusu herufi moja moja.

وَأَلْقَاءِ الْحَكِيمِ ﴿١٠٠﴾

“Kwa Haki ya Qur’ani yenye hikima!”

Inamaanisha *Al-Muhkam*, ambayo haitafikwa na upotofu mbele yake wala nyuma yake.¹

إِنَّا

“...Hakika wewe...”

Ewe Muhammad.

لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٠١﴾ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٠٢﴾

“...ni miongoni mwa Mitume (waliotumwa) na uko Juu ya Njia Iliyonyooka.”

Yaani, kufuata njia iliyonyooka na Dini na Sheria ya haki,

تَنْزِيلَ الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿١٠٣﴾

“Uteremsho wa Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.”

Maana yake, ni kuwa njia hii ambayo ameileta ni wahyi kutoka kwa Bwana Mwenyezi Enzi, Ambaye Ana Huruma kwa waja Wake wenye kufuata na kutii Amri Zake.

Na hii kama ayah ya:-

وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٠٤﴾ صِرَاطِ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ أَلَا إِلَىٰ اللَّهِ تَصِيرُ الْأُمُورُ ﴿١٠٥﴾

“Na hakika wewe unaongoa kwenye Njia Iliyonyooka. Njia ya Mwenyezi Mungu Ambaye ni Vyake Yeye tu viliomo mbinguni na katika ardhi. Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.” (42:52-53)

¹ Angalia Surah *Fussilat* 41:42.

لَتُنذِرَ قَوْمًا مَّا أُنذِرَ ءَابَاؤُهُمْ فَهُمْ غَافِلُونَ ﴿١٥٨﴾

“Ili uwaonye watu ambao baba zao hawakuonywa, basi wao wamekuwa wenye kughafilika.”

Inawarejea Waarabu kwani hawakupata Muonyaji kabla ya Muhammad ﷺ. Kutajwa wao peke yao hakutoi wengine ambao hawakupata mjumbe kabla ya Muhammad ﷺ (makusudio ya kauli hiyo); bali nao wamo. Hayo tumeyasema kwa ushahidi wa Ayah na Hadithi *mutawatiri* (nyingi) zikieleza kuwa ujumbe wa Muhammad ﷺ ni kwa Ulimwengu wote. Hii inarejea katika ayah:

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote.” (7:158)

لَقَدْ حَقَّ الْقَوْلُ عَلَىٰ أَكْثَرِهِمْ

“Bila ya shaka kauli imekwishathibiti juu ya wengi katika wao...”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Imethibitika adhabu kwa watu wengi; kwa sababu hilo limo ndani ya Kitabu (*Al-Lauhu Al-Mahfudh*) kuwa hawatoamini.”

فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ

“...kwa hivyo hawaamini.”

Kumuamini Allah تعالى wala Mitume Wake.¹

إِنَّا جَعَلْنَا فِي أَعْنَاقِهِمْ أَغْلَالًا فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ﴿١٥٩﴾ وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا وَمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا فَأَغْشَيْنَاهُمْ فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ ﴿١٦٠﴾ وَسَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٦١﴾ إِنَّمَا تُنذِرُ مَنِ اتَّبَعَ الذِّكْرَ وَخَشِيَ الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ ۖ فَبَشِّرْهُ بِمَغْفِرَةٍ وَأَجْرٍ كَرِيمٍ ﴿١٦٢﴾ إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَءَاتَاهُمْ ۗ وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿١٦٣﴾

¹ At-Tabari 20:492.

8. Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni. Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu.

9. Tumeweka kizuizi mbele yao, na kizuizi nyuma yao, na Tumewafunika (macho yao); kwa hivyo hawaoni.

10. Ni sawa sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye, hawataamini.

11. Unaweza kumuonya yule mwenye kufuata ukumbusho, na akamcha (Arrahman), Mwingi wa Rehema, hali ya kuwa Humuoni. Basi mbashirie huyo msamaha na ujira mwema.

12. Kwa hakika sisi Tutawahuisha wafu, na Tunaziandika amali zao zile wanazofanya zisiache taathira nyuma na zile wanazofanya zikaacha taathira. Na kila kitu kimehifadhiwa kwa idadi yake katika Daftari lenye kubainisha.

Hali ya Wale Ambao Uovu umeshathibishwa juu yao.

Kasema Allah Karim, "Hali ya watu ambao uovu umeshathibishwa juu yao, hali yao katika kuufikia uongofu wanakuwa kama mtu aliyetiwa minyororo shingoni mwake na mikononi mwake, imetiwa pini chini ya kidevu chake kiasi kuwa kichwa chake kimeinuka (uso wake) juu." Kama Anavyosema Allah تعالى:

فَهُمْ مُقَمَّحُونَ

"Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu."

Hali ya kutaja minyororo shingoni inatosha wala hakuna haja ya kutaja mikono (chini ya videvu) inakuwa ishara ipo wazi. Al-Awfi alisema akinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما juu ya aya hii ya.

إِنَّا جَعَلْنَا فِي أَعْنَاقِهِمْ أَغْلَالًا فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ﴿١٧﴾

"Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni. Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu."

Na hiyo ni kama Aya,

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ

"Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako." (17-29).

Yaani mikono yao imefungwa shingoni mwao na hawawezi kuinyoosha, ili kufanya jema lolote.¹

فَهُمْ مُقَمَّرُونَ

“Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu.”

Mujahid anasema kuwa ayah hii ina maana vichwa vyao vimeinuliwa, na mikono yao imewekwa juu ya vinywa vyao na hivyo wamebanwa hawawezi kufanya jambo lolote zuri.²

وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا

“Tumeweka kizuizi mbele yao.”

Mujahid anasema “cha kuufahamu ukweli”.

وَمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا

“...na kizuizi nyuma yao...” Mujahid amesema, “kati yao na ukweli, hivyo wamechanganyikiwa.”³

Qatadah alisema, “anatoka katika hali moja ya upotovu na kuelekea hali nyingine (ya upotovu).”⁴

فَأَعَشَيْنَاهُم

“...na Tumewafunika (macho yao)”. Yaani, “Tumewatia upofu, na macho yao hayaoni ukweli.”

فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ

“...kwa hivyo hawaoni.” Maana yake, hawawezi kuondoka kuelekea kwenye heri, wala hawaongozeki katika kheri.

Ibn Jarir رضي الله عنهما alisema, “Ilinukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas رحمه الله تعالى kuwa alizoweya kusoma, “*Fa a 'shaynahum* (badala ya *Fa'agh'shaynahum*, yaani kwa herufi ‘ain badala ya *ghain*). Maana ya *Al-Asha* (ni udhaifu wa macho, upofu) ambao ni ugonjwa wa macho.”⁵

¹ At-Tabari 20:494.

² At-Tabari 20:494.

³ At-Tabari 20:495.

⁴ At-Tabari 20:495.

⁵ At-Tabari 20:496.

'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema: "Allah Aliwawekea kizuizi hiki baina yao, na *Islam* na *Iman*, hivyo walikuwa na matakwa ambayo kamwe hawakuyafikia." Na alisoma:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى
يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٦٧﴾

"Hakika wale ambao neno la Mola Wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini, Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu." (10:96-97).

Kisha alisema, "Yeyote aliyezuiwa na Allah تعالى (uongovu) hatoweza (kuongoka)."¹ Ikrimah alisema, "Abu Jahl alisema, "Nikimuona Muhammad, nitamfanyia kadhaa wa kadhaa." Kisha Allah تعالى Akashusha ayah hii.

إِنَّا جَعَلْنَا فِي أَعْنَاقِهِمْ أَغْلَالًا

"Tumeweka makongwa shingoni mwao..." mpaka

فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ

"...kwa hivyo hawaoni." Anaendelea Ikrimah kusema kuwa walikuwa watu wanasema, "Muhammad huyo" na yeye Abu Jahl alisema, "Yuko wapi?" na wala hakuweza kumuona (Mtume). Habari hizi pia zimenukuliwa na Ibn Jarir ². رحمه الله تعالى

وَسَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٨﴾

"Ni sawa sawa kwao ukiwaonya au usiwaonya, hawataamini."

Ina maana, Allah تعالى Ameishahukumu juu yao kuwa hawataokoka, hivyo kuwapa onyo au mwongozo hakutawasaidia kitu wala halitawaathiri. Maelezo kama haya yalishaelezwa hapo mwanzoni mwa *Surat Al-Baqarah*,³ Allah تعالى Akasema,

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٩﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى
يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٧٠﴾

¹ At-Tabari 20:495.

² Kama hapo juu (mtumwa aliyeachwa huru hakuwa shahidi katika mambo kama hayo.)

³ Angalia juzuu ya kwanza, *Tafsir ya Surat Al-Baqarah* (2:6).

“Hakika wale ambao neno la Mola Wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini, Ijapo kuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.” (10:96-97)

إِنَّمَا تُنذِرُ مَنِ اتَّبَعَ الذِّكْرَ

“Hakika wewe unamuonya mwenye kufuata ukumbusho...”

Yaani, waumini tu ndio watafaidika na kauli yako ya kuwaonya wale ambao wanaofuata mwongozo, yaani Qur’aani.

وَحَيْثُ الرَّحْمَنِ بِالْغَيْبِ

“...na akamcha (Arrahman), Mwingi wa Rehema, hali ya kuwa hamuoni.”

Na wale wanaomuogopa Allah تعالى wakijua kuwa Yeye Anawaangalia na Anawaona (matendo na mambo yao yote).

فَبَشِّرْهُ بِمَغْفِرَةٍ

“Basi mbashirie huyo msamaha...” Wa madhambi yake,

وَأَجْرٍ كَرِيمٍ

“...na ujira mwema.” Malipo na zawadi kubwa, nzito na nzuri.

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٦٧﴾

“Hakika wanaomuogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu, watapata maghira na ujira mkubwa.” (67:12)

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ

“Kwa hakika sisi Tutawahuisha wafu.” Yaani, hapo Siku ya Kiama. Inamaanisha kuwa Allah تعالى Atahuisha moyo wa Amtakaye katika makafiri ambao nyoyo zao zimekufa sababu ya upotovu wakaongoka na wakaelekea kwenye ukweli. Allah تعالى Anasema baada ya Kutaja ugumu wa nyoyo.

أَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ تَحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦٨﴾

“Jueni kwamba Mwenyezi Mungu Huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumekubainishieni Ishara ili mpate kuzingatia.” (57:17).

وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا

“...na Tunaziandika amali zao zile wanazofanya zisiache taathira nyuma ...”

Maana, matendo yao.

وَأَثَرَهُمْ

“...na zile wanazofanya zikaacha taathira.” Maana, “Tunayaandika matendo yao ambayo walikuwa wakiyafanya (wao wenyewe) na athari za matendo yao waliyoyaacha baada ya wao kuondoka, vile vile tunawalipa wao. Na kama yalikuwa ni mema watalipwa kwa mema walioyatenda, na kama ni ubaya basi wataadhibiwa kwa maovu yao. Hii ni kauli inayolingana na Hadithi.

«مَنْ سَنَّ فِي الْإِسْلَامِ سُنَّةً حَسَنَةً كَانَ لَهُ أَجْرُهَا، وَأَجْرُ مَنْ عَمِلَ بِهَا مِنْ بَعْدِهِ مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أَجْرِهِمْ شَيْئًا، وَمَنْ سَنَّ فِي الْإِسْلَامِ سُنَّةً سَيِّئَةً كَانَ عَلَيْهِ وِزْرُهَا وَوِزْرُ مَنْ عَمِلَ بِهَا مِنْ بَعْدِهِ مِنْ غَيْرِ أَنْ يَنْقُصَ مِنْ أَجْرِهِمْ شَيْئًا»

“Atakayeanzisha jambo zuri ndani ya Uislamu ana ujira wake na ujira wa mwenye kutenda baada yake, bila kupungua chochote katika malipo yao. Na atakayezuwa jambo baya katika Uislamu, basi mzigo anabeba yeye pamoja na watakaofanya makosa hayo baada yake, na wala hakipungui kitu katika malipo yao hayo.”

Hadithi hii imo katika kitabu cha Muslim kutoka kwa Jarir bin Abdallah Al-Bajali رضي الله عنه ambamo kuna kisa kirefu cha watu wa kabila la Mudhar, ambao walikuwa wamevaa nguo zilizochakaa.¹ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika Hadithi hii kwa urefu kutoka kwa Jarir bin Abdallah رضي الله عنه. Katika hadithi hiyo Mtume ﷺ alisoma ayah hii.

وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَأَثَرَهُمْ

“...Tunaziandika amali zao zile wanazofanya zisiache taathira nyuma na zile wanazofanya zikaacha taathira.”

Muslim naye aliandika katika Hadithi kwa mlolongo mwingine.² Na hivyo hivyo Hadithi nyingine ambayo ipo katika Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ alisema,

¹ Muslim 2:704

² Muslim 2:706. Angalia na. 2353 katika Kitabu cha *Zakah*, ambayo ni isnadi ya wasimulizi anayoikusudia Ibn Kathir. Aya hiyo imesomwa katika Hadithi aliyoiandika Abi Hatim رحمه الله تعالى katika maelezo ya Aya hii, si katika toleo la Muslim.

«إِذَا مَاتَ ابْنُ آدَمَ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثٍ: مِنْ عِلْمٍ يُتَّقِعُ بِهِ، أَوْ وَلَدٍ صَالِحٍ
يَدْعُو لَهُ، أَوْ صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ مِنْ بَعْدِهِ»

*"Mwanadamu anapokufa hukatika matendo yake, isipokuwa mambo matatu: elimu yenye kunufaisha (jamii) au mtoto mwema anayemuomba dua au sadaka endelevu."*¹

Sufiyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alitoa taarifa kuwa Abu Said alisema, "Nilimsikia Mujahid akisema kuhusu Aya hii:

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي الْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا وَآثَرَهُمْ

"Kwa hakika sisi Tutawahuisha wafu, na Tunaziandika amali zao zile wanazofanya zisiache taathira nyuma na zile wanazofanya zikaacha taathira."

"Yale walioacha nyuma katika upotovu na maasi." Ibn Abi Najih na wengine walisema, wakiwa wananukuu kutoka kwa Mujahid,

مَا قَدَّمُوا

"..amali zao zile wanazofanya zisiache taathira nyuma.."

"Hayo ni matendo yao."²

وَآثَرَهُمْ

"...na zile wanazofanya zikaacha taathira."

Alisema, "Nyayo zao."³ Vivyo hivyo pia huo ulikuwa muono wa Al-Hasan na Qatadah.⁴

وَآثَرَهُمْ

"...na zile wanazofanya zikaacha taathira...." "Nyayo zao."

Qatadah alisema, Lau Mwenyezi Mungu Angaliacha chochote kukuhusu wewe Mwana wa Adamu, basi Angelipuuzia kutoa uwezo katika upepo wa kufuta alama za nyayo hizo. Lakini si Anafuatilia kila hatua ya mwanadamu na matendo yake yote bali Anafuatilia nyayo hizo kwa hali yoyote katika kumtii Allah au katika kumuasi Kwake na taarifa kamili zinawekwa. Hivyo anayeweza kuweka kumbukumbu zake kwa matendo mema basi na afanye hivyo.

¹ Muslim 3:1255.

² At-Tabari 20:497.

³ At-Tabari 20:499.

⁴ At-Tabari 20:499.

Imam Ahmad aliandika katika riwaya ya Jabir bin Abdallah رضي الله عنه akisema, Palikuwa na sehemu iliyokuwa wazi karibu na Msikiti, na watu wa Bani Salamah walitaka kujongea karibu na msikiti. Mtume ﷺ aliposikia hayo aliwaambia:

«إِنَّهُ بَلَغَنِي أَنَّكُمْ تُرِيدُونَ أَنْ تَتَّقِلُوا قُرْبَ الْمَسْجِدِ؟»

"Nimesikia mnataka kuhamia karibu na Msikiti."

Wakasema, "Hayo kweli, Ya Rasula Llah hilo ndilo tulilolitaka." Akasema,

«يَا بَنِي سَلَمَةَ! دِيَارُكُمْ تُكْتَبُ آثَارُكُمْ، دِيَارُكُمْ تُكْتَبُ آثَارُكُمْ»

*"Enyi Bani Salamah! Bakini huko mliko, na nyayo zenu zitaandikwa na kuwa katika kumbukumbu."*¹

Taarifa kama hii pia ilipokelewa na Muslim kutoka kwa Jabir bin Abdallah رضي الله عنه.² Imam Ahmad aliandika kuwa Abdallah bin Amr رضي الله عنه alisema, "Kuna mtu alifariki Madinah na Mtume ﷺ akamsalia na kusema,

«يَا لَيْتَهُ مَاتَ فِي غَيْرِ مَوْلِدِهِ»

"Laiti angelifia mahali ambako sio alipozaliwa."

Mtu mmoja akauliza, "Kwa nini unasema hivyo ewe Mtume?" Mtume ﷺ akamjibu,

«إِنَّ الرَّجُلَ إِذَا تُوَفِّيَ فِي غَيْرِ مَوْلِدِهِ، قِيسَ لَهُ مِنْ مَوْلِدِهِ إِلَى مُنْقَطِعِ أَثَرِهِ فِي الْجَنَّةِ»

*"Hakika mtu akifia mbali na mahali alikozaliwa basi zitapimwa hatua kati ya sehemu hizo mbili hadi kule alikofia na masafa hayo ndio eneo atakalopewa huko Peponi."*³

Habari hizi pia zimenakiliwa na An-Nasai na Ibn Majah.⁴ Ibn Jarir رحمته الله تعالى alisimulia kuwa Thabit رضي الله عنه alisema, "Nilifuatana na Anas na nikaanza kwenda haraka. Alinishika mkono tukawa tunaenda pole pole. Baada ya muda (tukasali) na Zayd bin Thabit رضي الله عنه na nilikuwa natembea haraka haraka, basi aliniambia, kwa kusema, "Ewe Anas! Je hutambui kuwa hatua zako zote zinaandikiwa kumbukumbu?"⁵

¹ Ahmad 3:332.

² Muslim 1:492.

³ Ahmad 2:177.

⁴ An-Nasai 4:7, Ibn Majah 1:515.

⁵ At-Tabari 20:498.

Taarifa hii na ile ya mwanzo hazina mgongano, bali zinaashiria juu ya jambo lile lile na kutia msisitizo. Kwa kuwa kila hatua anaandikiwa basi yale mambo ambayo yanaletwa kama mfano wa mema au maovu basi hapana shaka kuwa yanaandikwa. Allah A'lamu.

وَكُلُّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ

“Na kila kitu Tumekihifadhi kwa idadi katika daftari lenye kubainisha.”

Maana yake ni kila kitu kilichopo kimeandikwa habari zake na kumbukumbu zake kwa ufasaha ndani ya *Al-Lawhu Al-Mahfudh*. *Al-Imam Al-Mubin* hapa inarejea kwenye asili ya maandiko yote (kumbukumbu zote). Huu ulikuwa ni msimamo wa Mujahid Qatadah na Abdurahman bin Zayd in Aslam.¹ Halikadhalika Allah تعالى Anasema:

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِْمَانِهِمْ

“Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa wakifuatacho...” (17:71)

Yaani Kitabu cha matendo yao ambayo kitatoa ushahidi juu ya matendo yao kama yalikuwa mema au maovu. Na ni kama ayah ya,

وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِئَءَ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ

“...na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi...” (39:69) na pia

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَا لَ هَذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظِلُّرْتُكَ أَحَدًا ﴿٦٩﴾

“Na kitawekwa kitabu. Basi utawaona waovu wanavyoogopa kwa yale yaliomo humo. Na watasema: Ole wetu! Kitabu hichi kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika? Na watayakuta yote waliyoyatenda yamehudhuria hapo. Na Mola Wako Mlezi hamdhulumu yeyote.” (18:49).

¹ At-Tabari 20:499.

وَأَضْرِبْ لَهُمْ مَثَلًا أَصْحَابَ الْقَرْيَةِ إِذْ جَاءَهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٣٦﴾ إِذْ أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمُ اتْنَيْنِ فَكَذَّبُوهُمَا فَعُزِّزْنَا بِثَالِثٍ فَقَالُوا إِنَّا إِلَيْكُمْ مُرْسَلُونَ ﴿٣٧﴾ قَالُوا مَا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِثْلُنَا وَمَا أَنْزَلَ الرَّحْمَنُ مِنْ شَيْءٍ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَكْذِبُونَ ﴿٣٨﴾ قَالُوا رَبُّنَا يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ﴿٣٩﴾ وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ ﴿٤٠﴾

13. Na wapigie mfano wa wakaazi wa mji walipowafikia wajumbe.

14. Tulipowatumia wawili, wakawakanusha. Basi Tukawazidishia nguvu kwa mwingine wa tatu. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwenu.

15. Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi. Na Mwingi wa Rehema hakuteremsha kitu. Nyinyi mnasema uwongo tu.

16. Wakasema: Mola Wetu Mlezi Anajua kwamba hakika sisi tumetumwa kwenu.

17. Wala si juu yetu ila kufikisha (ujumbe) wazi wazi.

Kisa cha Watu wa Mjini na Mitume Yao, ni Somo kwa Wale Waliokadhibisha Mitume na Wakaangamizwa.

Allah Anasema, "Ewe Muhammad, waambie watu wako ambao wanakukataa."

مَثَلًا أَصْحَابَ الْقَرْيَةِ إِذْ جَاءَهَا الْمُرْسَلُونَ

"Na wapigie mfano wa wakaazi wa mji walipowafikia walio tumwa."

Ibn Ishaq رحمه الله تعالى katika taarifa zilizopokelewa kutoka kwa Ibn Abbas, Ka'b Al-Ahbar na Wahb bin Munabbih, alisema kuwa mji huo ulikuwa Antiokia. Huko alikuwepo mfalme aliyeitwa Antiokas Ibn Antiokas Ibn Antiokas, ambaye alikuwa akiabudu masanamu. Mwenyezi Mungu Akampelekea Mitume watatu waliokuwa wakiitwa, Saadiq, Saduq na Shaluum na waliwakataa.¹ Pia imepokelewa kutoka kwa Buraydah bin Al-Husayb, Ikrimah, Qatadah na Az-

¹ At-Tabari 20:500.

Zuhr kuwa ulikuwa mji wa Antiokia.¹ Wasomi wengine hawana hakika kama mji huo ulikuwa ni Antiokia, kama tutakavyoona hapo baadaye baada ya kueleza kisa chote, Inshallah.

إِذْ أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمُ اتِّعِينَ فَكَذَّبُوهُمَا

“Tulipowatumia wawili, wakawakanusha.”

Yaani, wale watu (wa mji huo) walifanya haraka kuwakanusha wale Mitume..

فَعَزَّزْنَا بِثَالِثٍ

“Basi Tukawazidishia nguvu kwa mwingine wa tatu...”

Ina maana, “Tuliwaongezea nguvu kwa kupeleka Mtume mwingine wa tatu.” Ibn Jurayj alipokea taarifa kutoka kwa Wahb bin Sulayman, kutoka kwa Shu’ab Al-Jaba’i ikieleza kuwa, “Majina ya Mitume wawili wa mwanzo ni Sham’un na Yohanna; na jina la yule wa tatu lilikuwa Bulus na mji huo ulikuwa Antiokia (Antakiyah).

فَقَالُوا

“...Wakasema...”

Yaani, waliwaambia watu wa mji huo

إِنَّا إِلَيْكُمْ مُّرْسَلُونَ

“...Hakika sisi tumetumwa kwenu...”

Wakimaanisha, kutoka kwa Mola wenu ambaye Alikuumbeni ninyi na Anayekuamrisheni kumuabudu Yeye tu Peke Yake bila kumshirikisha na chochote.” Hii ilikuwa ni kauli ya Abu Al-Aliyah. Qatadah bin Di’amah alidai kuwa hawa walikuwa ni wajumbe kutoka kwa Masihi ambao aliwatuma waende Antiokia.

قَالُوا مَا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا

“Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi.”

¹ At-Tabari 20:500.

Yaani “Ah! Vipi mpokee ujumbe (ninyi) wakati ni binadamu kama sisi tulivyo, basi nasi kwa nini tusipokee ujumbe (wahyi) huo kama ninyi ?Ikiwa ninyi ni wajumbe, mnapaswa kuwa Malaika.” Kauli hii ni ya watu wengi ambao walikuwa wanawakadhibisha Mitume.

Na kama aya ya Allah تعالى،

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَعَالُوا أ_Bَشَرًا مِّمَّنْ هَدَيْنَا

“Hayo ni kwa kuwa walikuwa wakiwajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, nao wakasema: Hivyo binaadamu ndio atuongoe?” (64:6).

Yaani, walikuwa wanashangazwa na hayo na kisha wanayakanusha.

قَالُوا إِنَّا أَنْشَرْنَا بَشَرًا مِّمَّنْ تَرْيَدُونَ أَنْ تَصُدُّونَا عَمَّا كَانُوا يَعْبُدُ آبَاءَنَا قَاتُونَا بِسُلْطَانٍ

مُتَّبِعِينَ

“Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni wanaadamu kama sisi. Mnataka kutuzuilia na waliyokuwa wakiabudu baba zetu. Basi tuleteeni hoja ilio wazi.” (14:10).

Allah Karimu Anasema Akituambia kuwa walisema,“

وَلَيْنَ أَطَعْتُمْ بَشَرًا مِّمَّنْ كُنْتُمْ إِذَا لَخَسِرُونَ

“Na nyinyi mkimtii mtu kama nyinyi basi hakika mtakuwa khasarani.”(23:34).

Na Allah Anasema:

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَسُولًا

“Na nini kilichowazuilia watu kuamini ulipowajia uwongofu isipokuwa walisema: Je! Mwenyezi Mungu Humtuma mwanaadamu kuwa ni Mtume?” (17:94)

Watu hao walisema,

مَا أَنْتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا وَمَا أَنْزَلَ الرَّحْمَنُ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا أَنْتُمْ إِلَّا تَكْذِبُونَ ﴿١٦﴾ قَالُوا رَبُّنَا
يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ﴿١٧﴾

“Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi. Na Mwingi wa Rehema hakuteremsha kitu. Nyinyi mnasema uwongo tu. Wakasema: Mola Wetu Mlezi Anajua kwamba hakika sisi tumetumwa kwenu.”

Hii ina maana kuwa Mitume hao watatu walisema kuwajibu watu wao: Mola Wenu Anajua kuwa sisi tu wajumbe kwenu, na kama tungelikuwa tu – waongo basi angelichukua hatua kali sana dhidi yetu, lakini Atatuunga mkono na tutafanikiwa hamuezi kutushinda na baadaye mtatambua nani atakuwa na mwisho mzuri wa kupendeza Siku ya Kiama: Hii inalingana na Ayah,

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ شَهِيدًا ۗ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَالَّذِينَ
ءَامَنُوا بِالْبَاطِلِ وَكَفَرُوا بِاللَّهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٥٢﴾

“Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Shahidi baina yangu na nyinyi. Anayajua yaliomo katika mbingu na ardhi. Na wale wanaoamini upotovu na wakamkataa Mwenyezi Mungu, hao ndio waliokhasiri.” (29:52).

وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلِّغُ الْمُبِينُ ﴿٥٣﴾

“Wala si juu yetu ila kufikisha (ujumbe) wazi wazi.”

Ina maana kuwa, “hatuna jambo lingine ila kufikisha ujumbe ambao tulipewa kukuleteeni; kama mkikubali na kutii basi ni furaha na ushindi kwenu hapa duniani na Akhera; na kama hamtayakubali hayo basi punde si punde mtatambua mmeingia katika maovu gani.” Allah A'lamu.

* * *

قَالُوا إِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ^ط لَئِن لَّمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُمْ
 مِنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨﴾ قَالُوا طَيَّرْنَاكُمْ مَعَكُمْ^ع إِنْ دُكِّرْتُمْ^ع
 بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴿١٩﴾ وَجَاءَ مِنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ
 رَجُلٌ يَسْعَى قَالَ يَنْفُورِ آتِبِعُوا الْأَمْرُسَلِينَ ﴿٢٠﴾ آتِبِعُوا
 مَنْ لَا يَسْأَلُكُمْ أَجْرًا وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٢١﴾ وَمَا لِي لَا أَعْبُدُ
 الَّذِي فَطَرَنِي وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٢﴾ أَأَتَّخِذُ مِنْ دُونِهِ آلِهَةً
 إِنْ يُرِيدَنِ الرَّحْمَنُ بِضُرٍّ لَا تُغْنِي عَنِّي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا وَلَا
 يُنْقِذُونِ ﴿٢٣﴾ إِنِّي إِذًا لَئِنِّي ضَلَلْتُ مِثْلَ هَؤُلَاءِ إِنِّي - أَمَنْتُ
 بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُونِ ﴿٢٤﴾ قِيلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ^ط قَالَ يَلَيْتَ قَوْمِي
 يَعْلَمُونَ ﴿٢٥﴾ بِمَا عَفَرَ لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٢٦﴾
 * وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَى قَوْمِهِ مِنْ بَعْدِهِ مِنْ جُنْدٍ مِّنَ
 السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِينَ ﴿٢٧﴾ إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً
 فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿٢٨﴾ يَحْسِرَةَ عَلَى الْعِبَادِ^ع مَا يَأْتِيهِمْ
 مِنْ رَسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٩﴾ أَلَمْ يَرَوْا كَمْ
 أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُونِ أَنَّهُمْ إِلَيْهِمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٣٠﴾
 وَإِنْ كُلُّ لَمَّا حَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٣١﴾

قَالُوا إِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ^ط لَئِن لَّمْ
 تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُمْ مِنَّا
 عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨﴾ قَالُوا طَيَّرْنَاكُمْ
 مَعَكُمْ^ع إِنْ دُكِّرْتُمْ^ع بَلْ أَنْتُمْ
 قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴿١٩﴾

**18. Wakasema: Sisi tume-
 agua kuwa nyinyi ni
 wakorofi. Ikiwa hamta-
 acha basi kwa yakini
 tutakupigeni mawe, na
 mtapata adhabu chungu
 kutoka kwetu.**

**19. Wakasema: Ukorofi
 wenu mnao wenyewe! Je!
 Ni kwa kuwa mnaku-
 mbushwa? Ama nyinyi ni
 watu waliopindukia mipaka.**

Kisha watu wa mji huo
 walisema kuwajibu wajumbe,

طَيَّرْنَاكُمْ مَعَكُمْ^ع

**“Sisi tumeagua kuwa nyinyi
 ni wakorofi.”**

Ikimaanisha, “Tukiangalia nyuso zenu tunaona biashara mbovu wala hatuoni uzuri wowote mliotuletea sisi kakika sura zenu.” Qatadah alisema, “Walikuwa wanasema, “Sisi tukifikiwa na mabalaa ni kutokana na ninyi.”¹ Mujahid alisema, “Hawa watu walisema watu kama ninyi hawaingii katika mji ila huwaletea mabalaa na mateso watu wa mji huo.”

¹ At-Tabari 20:502.

لَئِن لَّمْ تَنْتَهُوا لَنَرْجُمَنَّكُمْ

"Ikiwa hamtaacha basi kwa yakini tutakupigeni mawe."

Qatada alisema, "Kwa kuwapiga mawe."²

وَلَيَمَسَّنَّكُم مِّنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ

"...na mtapata adhabu chungu kutoka kwetu..."

Yaani, adhabu kali iumizayo. Wale wajumbe wakawajibu,

طَهِّرْكُمْ مَعَكُمْ

"Ukorofi wenu mnao wenyewe!"

Hizo biashara mbovu na mikosi ni yenu wenyewe imerejeshwa kwenu. Na hii inafanana na Ayah ambayo Allah Anawaeleza watu wa Firauni.

فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَذِهِ ۗ وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَّعَهُ ۗ أَلَا إِنَّمَا طَهَّرْنَا عَنْدَ اللَّهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣١﴾

"Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unaowafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu." (7:131).

Na watu wa Saleh walisema,

أَطَّيَّرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَّعَكَ ۗ قَالَ طَهَّرْتُمُومَ عِنْدَ اللَّهِ ۗ

"Tuna kisirani nawe na wale walio pamoja nawe. Yeye akasema: Uguzi wa ukorofi wenu uko kwa Mwenyezi Mungu." (27:47).

Na Allah تعالی Akasema:

وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ ۗ مِنْ عِنْدِكَ ۗ قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ فَمَالِ هَؤُلَاءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا ﴿١٣٢﴾

¹ At-Tabari 20:502.

“Na likiwafikilia jema wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikilia ovu wanasema: Hili limetoka kwako wewe. Sema: Yote yanatokana na Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno?” (4:78).

إِن ذُكِّرْتُمْ ۚ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ

“Je! Ni kwa kuwa mnakumbushwa? Ama nyinyi ni watu walio pindukia mipaka.”

Yaani, kwa sababu yetu sisi, na sisi tumewakumbusha na tukawaamuru mumuabudu Mola, Mungu wenu, kwa Ikhlas, na badala yake mkasema mliyosema mkitutisha. Hapana! Hakika nyinyi ni watu watukutu na waovu.” Qatadah alisema, “Hii ina maana, “Kwa sababu tumekukumbusheni juu ya Mwenyezi Mungu, (eti) mmeona ndege mbaya (mikosi) kwetu. Hapana, bali nyinyi ni watu watukutu na waovu.”¹

وَجَاءَ مِنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ رَجُلٌ يَسْعَىٰ قَالَ يَا قَوْمِ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٨﴾ اتَّبِعُوا مَنْ لَا يَسْئَلُكُمْ أَجْرًا وَهُمْ مُّهْتَدُونَ ﴿١٩﴾ وَمَا لِي لَا أَعْبُدُ الَّذِي فَطَرَنِي وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٠﴾ ءَأَتَّخِذُ مِنْ دُونِهِ ءَالِهَةً إِن يُرِدْنِ الرَّحْمَنُ بِضُرٍّ لَا تُغْنِ عَنِّي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا وَلَا يُنقِذُونِ ﴿٢١﴾ إِنِّي إِذًا لَّفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٢﴾ إِنِّي ءَامَنْتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمِعُونِ ﴿٢٣﴾

20. Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa.

21. Wafuateni ambao hawakutakini ujira, hali ya kuwa wenyewe wameongoka.

22. Na kwa nini nisimuabudu yule aliyeniumba na Kwake mtarejeshwa?

23. Je! Niishike miungu mingine badala Yake? Arrahmani, Mwingi wa Rehema, Akinitakia madhara uombezi wa hao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa.

¹ At-Tabari 20:504.

24. Basi hakika mimi hapo nitakuwa katika upotovu ulio dhaahiri.

25. Hakika mimi nimemuamini Mola Wenu Mlezi, basi nisikilizeni!

Akinukuu yale yaliyomfikia kutoka kwa Ibn Abbas, Ka'b Al-Ahbar na Wahb bin Munabbih – Ibn Ishaq رحمه الله تعالى alisema, “Wakazi wa mji (huo) waliamua kawaua wajumbe hao, kisha akaja mtu mmoja mbio akitokea upande wa pili wa mji ili kuwahami wajumbe wasidhuriwe na wakazi wa mji. Walisema jina lake alikuwa Habib na kazi yake ilikuwa ni kutengeneza kamba. Alikuwa na afya hafifu na alikuwa ana maradhi makuu ya ukoma. Mtu huyu alikuwa mwepesi sana kutoa misaada ya hali na mali kwa watu; akitoa nusu ya pato lake kuwasaidia watu na alikuwa anafuata fitra kwa kumcha Mwenyezi Mungu.¹ Shahib bin Bishru alisema kutokana na mapokezi kutoka kwa Ikrimah kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa, “Mtu huyo aliyetajwa ndani ya Sura Yasin alikuwa anaitwa Habib An-Najja, na aliuawa na watu wake, wale wakazi wa mjini.”

قَالَ يَنْقُومِ أَتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ

“...akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa.”

Mtu huyo alikuwa akiwataka wakubali ujumbe wa wale Mitume ambao walikuwepo mjini hapo.

أَتَّبِعُوا مَنْ لَا يَسْئَلُكُمْ أَجْرًا

“Wafuateni ambao hawakutakini ujira.”

Yaani, “kwa kuwa ujumbe wao wanakufikishieni, na wao ni waongofu katika wanayokuitieni, kumuabudu Allah تعالى bila kumshirikishana chochote.”

وَمَا لِي لَا أَعْبُدُ الَّذِي فَطَرَنِي

“Na kwa nini nisimuabudu yule aliyeniumba...”

Yaani, “kuna nini cha kunizuia kumuabudu kwa unyoofu Yule Aliyeniumba na ibada hiyo iwe Kwake Peke Yake bila ya kumshirikisha na kitu?”

¹ At-Tabari 20:504.

وَالَيْهِ تُرْجَعُونَ

“...na Kwake mtarejeshwa?”

Yaani, “Na Siku ya Qiyamah mtarejea Kwake na Atakutakeni kujibu maswali Yake kuwa mlifanya nini duniani; kama mambo yenu ni mema mtalipwa malipo mema, na kama ni maovu basi mtaadhibiwa.”

ءَأَتَّخِذُ مِنْ دُونِهِ ءَالِهَةً

“Je! Niishike miungu mingine badala yake?”

Kauli hii ni ya kuuliza swali la kukemea na kuwaweka watu sawa.

إِنْ يُرَدِّنِ الرَّحْمَنُ بَصِيرًا لَّا تُغْنِي عَنْهُمْ شَيْئًا وَلَا يُنْقِذُونَ

“Arrahmani, Mwingi wa Rehema, Akinitakia madhara uombezi wa hao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa.”

Ina maana, “miungu hii (masanamu) mnayoyaabudu badala ya Allah haina uwezo wa chochote; na iwapo Mola Anataka jambo liwe basi (hii) miungu haiwezi kulizuia. Kwani Allah تعالى kama anataka mpatwe na baya.”

فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلاَّ هُوَ

“...basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye.” (6:17)

Miungu (hii) (masanamu) haina lolote, haikufaidisheni kwa chochote wala haiwezi kuzuia jambo ovu lisiwafikeni, wala haiwezi kunisaidia kutatua tatizo langu.”

إِنِّي إِذَا لَغِي صَلَّلِي مُبِينٍ ﴿١٨﴾

“Basi hakika mimi hapo nitakuwa katika upotovu ulio dhaahiri.”

Yaani, ina maana, “Kama ningeliwachukua kama miungu na kuwategemea badala ya Allah تعالى.”

إِنِّي ءَامَنْتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُونَ ﴿١٩﴾

“Hakika mimi nimemuamini Mola Wenu Mlezi, basi nisikilizeni!”

Ibn Ishaq رحمه الله تعالى alisema, akinukuu taarifa alizopata kutoka kwa Ibn Abbas, Ka'b na Wahb, alisema kuwaambia watu wake.

إِنِّي ءَامَنْتُ بِرَبِّكُمْ

"Hakika mimi nimemuamini Mola Wenu Mlezi."

Yaani: "Mimi namuamini Mola Wetu ambaye ninyi hamtaki kumuamini."

فَاسْمَعُونَ

"...basi nisikilizeni!"

Ina maana, "Nisikilizeni yale nisemayo."¹ Au inawezekana maneno haya kayaelekeza kwa wale wajumbe watatu, aliposema:

إِنِّي ءَامَنْتُ بِرَبِّكُمْ

"Hakika mimi nimemuamini Mola Wenu Mlezi."

Yaani: 'Aliyekutumeni.'

فَاسْمَعُونَ

"...basi nisikilizeni!"

Ina maana, "mshuhudie hayo mbele ya Mola." Kauli hii ilisimuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى ambaye alisema, "na wengine walisema kuwa kauli ya mtu huyo ilikuwa imeelekezwa kwa wajumbe watatu, na akasema, "Nisikilizeni nisemayo na mshuhudie yale niyasemayo mbele ya Mola Wangu, kuwa nimemuamini Mola Wenu na mimi nakufuateni kauli yenu. "Tafsiri hii iko wazi zaidi na Allah تعالى ni Mjuzi wa yote. Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema akiwa anaeleza kutumia mapokezi kutoka kwa Ibn Abbas, Ka'b na Wahb: "Aliposema maneno hayo basi wale watu wa mji walimgeukia kwa pamoja na wakamuua, akiwa hana mtu wa kumtetea wala kumnusuru na janga hilo."² Qatadah alisema, "Walianza kumpiga mawe wakati akisema, "Ewe Mola Wangu waongoe watu wangu maana hawajui haya, nao wakaendelea kumvurumishia mawe hadi akafariki kifo cha mateso, na alikuwa bado anaendelea na maombi yake akiwaombea wapate kuongoka." Allah تعالى Amrehemu.³

¹ At-Tabari 20:507.

² At-Tabari 20:508.

³ At-Tabari 20:501.

قِيلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ ط قَالَ يَلِيَّتْ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ بِمَا غَفَرَ لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ
 الْمُكْرَمِينَ ﴿٣٧﴾ * وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ قَوْمِهِ مِنْ بَعْدِهِ مِنْ جُنْدٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا
 مُنْزِلِينَ ﴿٣٨﴾ إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿٣٩﴾

26. Akaambiwa: Ingia Peponi! Akasema: Laiti kuwa watu wangu wangelijua.

27. Jinsi Mola Wangu Mlezi Alivyonisamehe, na Akanifanya miongoni mwa waliohishimiwa.

28. Na hatukuwateremshia kaumu yake baada yake jeshi kutoka mbinguni, wala sisi si wenye kuteremsha.

29. Hakukuwa ila ukelele mmoja tu; na mara walizimwa!

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa maswahibu wake kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuwa walimkanyaga hadi matumbo yake yakatokea katika sehemu za haja kubwa. Allah تعالى Akamuambia,

ادْخُلِ الْجَنَّةَ ط

“Ingia Peponi!”

“Akaingia na kukuta neema zake zote. Akiwa Mola tayari Kamuondolea maradhi yake, huzuni na machovu aliyo kuwa nayo duniani.”¹ Mujahid alisema “Habib An-Najjar aliambiwa, “Ingia Peponi.’ Ilikuwa haki yake kuingia Peponi kwa sababu alikuwa ameuawa. Alipoona malipo yake na neema zake,

قَالَ يَلِيَّتْ قَوْمِي يَعْلَمُونَ

“...Laiti kuwa watu wangu wangelijua.”²

Qatadah alisema, “Hutompata muumini bali lazima atakuwa mkweli na kamwe hawezi kuwa kigeugeu. Huyu mtu alipoyaona yale mambo aliyoandaliwa na Mola Wake akasema hayo kwa moyo mmoja.

¹ At-Tabari 20:508.

² At-Tabari 20:509.

قَالَ يَلَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ بِمَا غَفَر لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرِمِينَ ﴿٣٧﴾

“Akasema: Laiti kuwa watu wangu wangelijua, Jinsi Mola Wangu Mlezi Alivyonisamehe, na Akanifanya miongoni mwa waliohishimiwa.”

Alitamani watu wake wayajue hayo aliyoyakuta huko wayaone hayo anayoyaona juu ya zawadi alizopewa na Mola Wake.¹ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Aliwanasahi watu wake katika kipindi cha uhai wake kwa kusema:

يَنْقُومِ آتِيَعُوا الْمُزْسَلِينَ

“Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa.” Na hata baada ya kufa aliendelea kusema,

يَلَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ بِمَا غَفَر لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرِمِينَ ﴿٣٧﴾

“Laiti kuwa watu wangu wangelijua. Jinsi Mola Wangu Mlezi Alivyonisamehe, na Akanifanya miongoni mwa waliohishimiwa.”

Haya yalinakiliwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى. Sufyan Al-Thawri رحمه الله تعالى alieleza kutoka kwa Asim Al-Ahwal kutoka kwa Mijlaz:

بِمَا غَفَر لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرِمِينَ ﴿٣٧﴾

“Jinsi Mola Wangu Mlezi Alivyonisamehe, na Akanifanya miongoni mwa waliohishimiwa.”

“Kwa kumuamini kwangu Allah تعالى na kuwakubali Mitume.”² Akiwa na maana kuwa, kama wangeliona neema alizozawadiwa na baraka za milele alizofanikiwa kuzipata, basi hayo yangeliwafanya wakubali ujumbe wa wale Mitume aliowajia. Allah تعالى Amrehemu na Awe radhi naye kwa sababu alikuwa na pupa ya watu wake kuongoka.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Abdul Malik, yaani bin Umair amesema: Urwa bin Masudi Athaqafi رضي الله عنه amemuambia Mtume ﷺ: Nitume kwa watu wangu nikawahubirie Uislamu, Mtume ﷺ akasema: “Hakika mimi naogopa wasije kukuua.” Ur’wa رضي الله عنه akasema: Hivi Mtume lau wangelinikuta nimelala wasingeniamsha. Hivyo Mtume ﷺ akampa ruhusa ya

¹ At-Tabari 20:509.

² At-Tabari 29178, hakuna dosari ndani yake.

kwenda. Ur'wa رضي الله عنه akalipitia Sanamu la Lata na Uza, akasema: Kisha asubuhi nitakuudhini tu. Thaqaf wakakasirika, Ur'wa رضي الله عنه akasema: Enyi Jamaa zangu kabila la Thaqif! Hakika Sanamu la Lata halina uwezo wowote na Sanamu la Uza halina utukufu wowote, hivyo kuweni Waislamu mtasalimilka. Maneno haya aliyarudia mara tatu. Hivyo Mtu mmoja akampiga kwa kitu chenye ncha kali katika jicho lake akamuua. Habari hiyo ikamfikia Mtume ﷺ akasema, "Mfano wake huyu, ni kama Mtu wa kisa cha Yasin.

قَالَ يَلَيْتَ قَوْمِي يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾ بِمَا غَفَرَ لِي رَبِّي وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٣٧﴾

"Akasema: Laiti kuwa watu wangu wangelijua, Jinsi Mola Wangu Mlezi Alivyonisamehe, na Akanifanya miongoni mwa waliohishimiwa."¹

Allah تعالى Anatuambia kuwa watu wa mji huo waliadhibiwa kisasi kwa kosa la kuua mtu huyo. Hilo ni kwa sababu. Allah تعالى Alichukizwa na mwenendo wa watu wa mji huo, kwanza hawakutaka kufuata kauli ya ujumbe wa Mitume Wake na kisha walimuua kipenzi Chake. Allah تعالى Anasema hakupeleka jeshi la Malaika wala hapakuwa na haja ya kufanya hivyo, ili kuwaangamiza watu hao. Hili jambo lilikuwa jepesi sana. Ibn Is-haaq رحمه الله تعالى anasema kuwa huu ndio ulikuwa msimamo wa Ibn Mas'ud رضي الله عنه ikiwa ni kauli za baadhi ya maswahaba juu ya aya hii,

وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ قَوْمِهِ مِنْ بَعْدِهِ مِنْ جُنْدٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِينَ ﴿٣٨﴾

"Na hatukuwateremshia kaumu yake baada yake jeshi kutoka mbinguni, wala sisi si wenye kuteremsha."

Alisema, "Hatukuwa na haja ya kuwazidi idadi yao kwa majeshi yetu (kutoka mbinguni) kwa sababu lilikuwa jambo jepesi tu."

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَامِدُونَ ﴿٣٩﴾

"Hakukuwa ila ukelele mmoja tu; na mara walizimwa!"

Na akaendelea kusema, "Hivyo Allah تعالى Alimuangamiza Mfalme huyo fedhuli pamoja na watu wake wa mji wa Antiokia, na wakawa wamepotezwa kutoka uso wa dunia, bila kuacha nyuma athari yoyote."²

¹ Al-Hakim 3:615 Mursali dhaifu.

² At-Tabari 20:510.

Ilisemwa kuwa maana ya maneno,

وَمَا كُنَّا مُنْزِلِينَ

“...wala sisi si wenye kuteremsha.”

“Hatukupeleka Malaika dhidi ya mataifa jeuri na yenye ufedhuli, tulipotaka kuyaangamiza; ilikuwa ni kazi ndogo tu ya kupeleka adhabu iliyowamaliza.

وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَىٰ قَوْمِهِ مِن بَعْدِهِ مِن جُنْدٍ مِّنَ السَّمَاءِ

“Na hatukuwateremshia kaumu yake baada yake jeshi kutoka mbinguni...”

Na ilisemwa kuwa: maana yake; Ujumbe mwingine. Hii ilikuwa kauli ya Mujahidi na Qatadah.¹ Qatadah alisema, Allah تعالیٰ Hakuwakemea watu wa mji huo pale walipomuua mtu yule.

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ خَمِيدُونَ ﴿٣٦﴾

“Hakukuwa ila ukelele mmoja tu; na mara walizimwa!”²

Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ alisema, “Kauli ya mwanzo ni sahihi zaidi, kwa sababu ujumbe hauletwi na jeshi.”³ Wafasiri wengi wanasema Allah Alimtuma Jibril عليه السلام ambaye alichukua nguzo za lango la Mji wao na akapiga ukelele mmoja tu, ukawavurumishia basi wote wakawa wamekwisha hakuna aliyebakia hai. Wote walikwisha.

Tumekwishaeleza taarifa nyingi kutoka kwa *salaf*, kuwa mji huo ulikuwa Antiokia na kuwa wale wajumbe watatu walikuwa wametumwa na Masihi, Isa bin Mariam عليه السلام kama alivyosema Qatadah na wengine, ‘Haya hayakutajwa na mwanazuoni yeyote wa mwanzoni wa *Tafsir* ghairi yake, na suala hili lazima liangaliwe kwa mitazamo mbalimbali.

(Kwanza) ni kwamba, kama tutaiangalia habari hiyo haraka haraka, kauli hii inaonesha kuwa wajumbe hao walitumwa na Allah na si Masihi, sawa na Kauli ya Allah تعالیٰ isemayo,

¹ At-Tabari 20:510, 511.

² At-Tabari 20:510.

³ At-Tabari 20:511.

إِذْ أَرْسَلْنَا إِلَيْهِمُ اثْنَيْنِ فَكَذَّبُوهُمَا فَعَزَّزْنَا بِثَالِثٍ فَقَالُوا إِنَّا إِلَيْكُمْ مُّرْسَلُونَ ﴿١٤﴾

“Tulipowatumia wawili, wakawakanusha. Basi Tukawazidishia nguvu kwa mwingine wa tatu. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwenu.” (36:14) Mpaka:

رَبُّنَا يَعْلَمُ إِنَّا إِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُونَ ﴿١٦﴾ وَمَا عَلَيْنَا إِلَّا الْبَلْغُ الْمُبِينُ ﴿١٧﴾

“Mola Wetu Mlezi Anajua kwamba hakika sisi tumetumwa kwenu. Wala si juu yetu ila kufikisha ujumbe ulio wazi.” (36:16-17)

“Wala si juu yetu ila kufikisha ujumbe ulio wazi.” Kama wajumbe wale watatu wangelikuwa ni wafuasi wa Isa bin Maryamu عليه السلام basi wangesema Ibara inayojulisha kuwa wao wametoka kwa Masihi. Allah تعالى ni Mjuzi wa yote. Zaidi ya hapo kama wangelikuwa wafuasi wa Masihi, kwa nini wale watu wa mji waseme,

إِن أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا

“Nyinyi si chochote ila ni watu kama sisi.” (14:10)

(Pili) ni kuwa, watu wa Antiokia walikuwa wa kwanza kumkubali Masihi Isa bin Maryamu عليه السلام. Na ni miongoni mwa miji minne iliyokuwa na Makasisi wa Kikrisitu. Miji hiyo ni Jerusalem kwa sababu ndio mji wake Masihi: “Antiokia, ulikuwa mji wa kwanza ambao watu wake wote walipokea ujumbe wa Masihi na wote wakaamini. Alekzandria, kwa sababu katika mji huo ndipo walipokusudia kufanya marekebisho ya ngazi ya ukasisi kuwa ngazi ya Askofu Mkuu, kisha chini yake Askofu kisha mapadri, halafu wachungaji na Mapapa, na mji mwingine ni Roma kwa sababu ni mji wa mtawala Costantino ambaye alikubali Ukristo na kuunga mkono dini hiyo. Alipohamishia makao maku yake huko Constantinopo, Makasisi walihamia huko Constantinopo kama ilivyoelezwa na waandishi wa tarekhe wengi – wana historia – kama vile Said Batriq na wengine – wakiwemo Ahlu Al-Kitab na Waislamu. Tukikubali kuwa Antiokia walikuwa watu wa mwanzo kumkubali Masihi, basi wale wajumbe hawakuwa wafuasi wa Masihi maana Allah تعالى Anasema watu wa mji huo waliwapinga wajumbe wale na wakaangamizwa, Allah A’lamu.

(Tatu) Sura ya tatu ni kuwa kisa cha Antiokia na wafuasi wa Masihi kilitokea baada ya kuwa Taurati ilikuwa imekwishateremka zamani. Abu Said Al-Khudri

نه رضي الله عنه na wengine miongoni mwa *Salaf* walisema, baada ya Taurati kushuka. Allah تعالى Alisitisha mtindo wa kuangamiza taifa zima kwa mpigo mmoja.

Badala yake alikuwa anawatuma waumini kupambana na makafiri. Hao *Salaf* walisema hilo wakati wanajadili Ayah,

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونََ الْأُولَىٰ

“Na hakika bila ya shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo.” (28:43)

Kauli hii inaashiria kuwa mji uliotajwa katika Qur’ani si Antiokia, kama zilivyo kauli za *Salaf* wengi. Na kama tunataka mji huo ubaki kama ulivyo (Antiokia) utakuwa ni Antiokia nyingine, maana kihistoria, mji huu haukupata kuangamizwa katika enzi za Ukristo au kabla ya hapo. *Allah A’lamu.*

يَحْسِرَةٌ عَلَى الْعِبَادِ ۚ مَا يَأْتِيهِمْ مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٤٣﴾ أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُونِ أَنَّهُمْ إِلَيْهِمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٤٤﴾ وَإِن كُلُّ لَمَّا جَمِيعٌ لَّدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٤٥﴾

30. Inafaa kuwasikitikia waja Wangu. Hakuwajia Mtume ila wao humkejeli.

31. Je! Hawaoni umma ngapi Tulizoziangamiza kabla yao? Hakika hao hawarejei tena kwao.

32. Na hapana mmoja ila wote watakusanywa waletwe mbele Yetu.

Ole Wao Makafiri

Ali bin Abi Falhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza juu ya ayah,

يَحْسِرَةٌ عَلَى الْعِبَادِ ۚ

“Inafaa kuwasikitikia waja wangu.”

Maana yake, “Wamehasirika waja (Wangu).”¹ Qatadah kasema,

¹ At-Tabari 20:512.

يَحْسِرَةٌ عَلَى الْعِبَادِ^٤

“Nawasikitikia waja wangu.”

“Ole wao binadamu ambao wamepuuza Amri za Allah تعالى.”¹

Maana yake, ni kuwa watajuta na kusunoneka Siku ya Kiama. Wakiona adhabu kwa macho yao; watajali kwa nini waliwakadhibisha Mitume walioletwa na Allah تعالى na badala yake wakaenda kinyume na maamrishi ya Allah تعالى kwa sababu walikuwa wamezoea kubishana na kupingana na maamrishi hayo hapa duniani.

مَا يَأْتِيهِمْ مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ

“Hakuwajia Mtume ila wao humkejeli.”

Yaani, (Mtume alipoletwa) hawakumuamini na walipinga maneno yake na kisha walimfanyia mzaha na kutupilia mbali ujumbe wake ambao ulikuwa wa kweli na wenye maamrishi kama alivyotumwa na Allah تعالى.

Makafiri Wanakataa Kuwa Kuna Kufufuka

Kisha Allah تعالى Anasema:

أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُونِ أَنَّهُمْ إِلَيْهِمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٣٧﴾

“Je! Hawaoni umma ngapi Tulizoziangamiza kabla yao? Hakika hao hawarejei tena kwao.”

Yaani, “Je hupati funzo kutokana na Aliwaangamiza Allah تعالى Aliwaangamiza kabla yako kwa sababu waliwakataa Mitume? Walikuja hapa duniani mara moja tu na wala hawarejei tena.” Hii inapinga dhana ya wajinga wanaodai kuwa,

إِنَّ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا

“Hapana ni uhai wetu wa duniani tu, tunakufa na kuishi basi.”
(23:37)

¹ At-Tabari 20:512.

Hii ilikuwa imani ya watu wanaodhani kuwa wakifa hurudi duniani (kwa kuingia mwilini mwa kiumbe mwingine); kwa ujinga wao walifikiria na kuamini kuwa watarejeshwa duniani. Allah تعالى Alipinga hilo kuwa ni fikra potofu na Anasema:

أَلَمْ يَرَوْا كَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِمَّا الْقُرُونُ أَنَّهُمْ إِلَيْهِمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٨﴾

“Je! Hawaoni umma ngapi Tulizoziangamiza kabla yao? Hakika hao hawarejei tena kwao.”

Kauli ya Allah:

وَإِنْ كُلُّ لَمَّا جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿١٩﴾

“Na hapana mmoja ila wote watakusanywa waletwe mbele Yetu.”

Yaani, Mataifa yote yaliyopita na yatakayokuja yatakusanywa na kuulizwa mambo yao na matendo yao mbele ya Allah تعالى. Siku ya Kiyama na kila mtu atalipwa kutokana na amali zao njema na mbaya. Ni sawa na Aya:

وَإِنَّ كُلًّا لَّمَّا لِيُؤْفَيَّهُمْ رَبُّكَ أَعْمَلَهُمْ ۗ

“Na hakika Mola Wako Mlezi Atawatimilizia malipo ya vitendo vyao.” (11:111).

* * *

وَأَيُّهُمُ الَّذِينَ الْأَرْضُ الْمَيِّتَةُ أَحْيَيْتَنَاهَا
 وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ ﴿٣٣﴾
 وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ
 وَأَعْنَبٍ وَفَجْرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٣٤﴾
 لِيَأْكُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ وَمَا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ
 أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٣٥﴾ سُبْحَانَ
 الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنْبِتُ
 الْأَرْضُ وَمِمَّا تَنْبِتُ الْأَرْضُ وَمِن
 أَنْفُسِهِمْ وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾
 وَأَيُّهُمُ الَّذِينَ لَهُمُ اللَّيْلُ نَسْلَخُ
 مِنْهُ اللَّيْلَ فَإِذَا هُمْ مُظْلِمُونَ ﴿٣٧﴾
 وَالشَّمْسُ تَجْرِي
 لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ۚ ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ
 الْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾ وَالْقَمَرَ
 قَدَّرْنَاهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ
 الْقَدِيمِ ﴿٣٩﴾ لَا
 الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ
 وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ ۚ
 وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾
 وَأَيُّهُمُ الَّذِينَ أَنَا خَلَقْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ
 فِي الْفَلَكَ الْمَسْحُورِ ﴿٤١﴾ وَخَلَقْنَا
 لَهُمُ مِنْ مِثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ ﴿٤٢﴾
 وَإِن نُّشَأْ نُفِرْهُمْ فَلَا يَصْرِخْ
 لَهُمْ وَلَا هُمْ يُنْقَدُونَ ﴿٤٣﴾
 إِلَّا رَحْمَةً مِنَّا وَمَتَاعًا إِلَىٰ حِينٍ ﴿٤٤﴾
 وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّقُوا مَا بَيْنَ
 أَيْدِيكُمْ وَمَا خَلْفَكُمْ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ
 ﴿٤٥﴾ وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ
 رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا
 مُعْرِضِينَ ﴿٤٦﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ
 أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ قَالَ
 الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنْطَعِمُ
 مَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ أَنْطَعِمَهُ
 إِن نَّتَرْنَا إِلَّا فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٤٧﴾

وَأَيُّهُمُ الَّذِينَ الْأَرْضُ الْمَيِّتَةُ أَحْيَيْتَنَاهَا
 وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ
 وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ
 وَأَعْنَبٍ وَفَجْرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ
 لِيَأْكُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ وَمَا عَمِلَتْهُ
 أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ
 سُبْحَانَ الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا
 مِمَّا تُنْبِتُ الْأَرْضُ وَمِن أَنْفُسِهِمْ
 وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ

33. Na Alama juu yao -
ardhi iliyokufa, nasi
Tunaifufua, na Tukatoa
ndani yake nafaka, wakawa
wanazila!

34. Na Tukafanya ndani
yake bustani ya mitende na
mizabibu, na Tukatimbua
chemichemi ndani yake,

35. Ili wale matunda yake,
na hayo hayakufanywa na
mikono yao! Basi je,
hawashukuru?

36. Subhana, Ametakasika,
Aliyeumba dume na jike
vyote katika vinavyomea
katika ardhi na katika nafsi
zao, na katika wasivyo-
vijua.

Hoja ya Kuwepo Muumba Mbingu na Kuwepo Uhai Baada ya Mauti

Allah تعالی Amesema:

وَأَيُّهُمُ

“Na alama juu yao...”

Yaani, ushahidi wa kuwaonesha kuwa yupo Mola Muumba, na Uwezo Wake ni timilifu na Anaweza Kuhui baada ya mauti

الْأَرْضِ الْمَيِّتَةِ

“...ardhi iliyo kufa...”

Yaani, ikiwa imekufa na imekauka bila kuwepo mimea, basi Allah تعالی Hushusha maji juu yake, na hapo huanza harakati za uhai, ardhi inaumba na kutoa vitu vyake vizuri (uoto).

Allah تعالی Anasema,

أَحْيَيْتَنَهَا وَأَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَأْكُلُونَ

“...nasi Tunafufua, na Tukatoa ndani yake nafaka, wakawa wanazila!”

Yaani, “Tumefanya hazina kutoka humo wanapata vyakula vyao na mifugo yao.”

وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْنَابٍ وَفَجْرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٣٦﴾

“Na Tunafanya ndani yake bustani ya mitende na mizabibu, na Tukatimbia chemchem ndani yake.”

Ina maana, “Tumeumba ndani yake mito ambayo hupeleka maji yanakohitajika ili yapatikane matunda na mazao ya kulima.” Hapo ndio Allah تعالی Anapowakumbusha waja Wake juu ya neema Alizowawekea pale Alipoumba mimea na mazao tofauti, basi anataja aina mbali mbali za matunda na mazao.

Kisha Allah تعالی Anasema,

وَمَا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ

“...na hayo hayakufanywa na mikono yao!”

Maana yake, yote hayo yametokea kutokana na Rehema Zake na Huruma Zake Allah تعالى, wala hayapatikani kwa ujanja au juhudi za binadamu. Huu ulikuwa mtazamo wa Ibn Abbas, na Qatadah. Allah تعالى Anasema:

أَفَلَا يَشْكُرُونَ

“Basi je, hawashukuru?”

Ina maana, je hawatoi shukrani kwa neema kemkem walizoletewa na kuneemeshwa kwao. Ibn Jarir رحمه الله تعالى, kwa upande mwingine, alilielewa neno ‘Ma’ kuwa liko mahali pa ‘Alladhi’ (yaani ambavyo). Hivyo, katika hali hiyo maana ya Ayah itakuwa – wanakula matunda yaliyoletwa na Allah تعالى kwa Rehema Zake na ambavyo hufanywa na mikono yao ikiwa kwa kupanda mbegu na kisha kutunza mimea hadi kuvuna. Ibn Jarir رحمه الله تعالى ametoa rai kuwa hiyo ndiyo *tafsir* aliyoifadhilisha zaidi ya zingine zote. *Tafsir* hii inaendana sawa na jinsi Ibn Mas’ud رضي الله عنه alivyokuwa akisoma

(لِيَأْكُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ وَمِمَّا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ)

Liyaakulu min thamarihii wamimma ‘amilat-hu aydiyhim afalaa yashkurun (Ili wapate kula katika matunda yake na ambavyo vimefanywa na mikono yao, basi je hawashukuru).

Kisha Allah تعالى Alisema:

سُبْحَانَ الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنْبِتُ الْأَرْضُ

“Subhana, Ametakasika, Aliyeumba dume na jike vyote katika vinavyomea katika ardhi...”

Ina maana mazao, matunda na mimea.

وَمِنْ أَنْفُسِهِمْ

“...na katika nafsi zao”

Ana maana Allah تعالى Aliumba katika nafsi zao jinsia mbili dume na jike.’

وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ

“...na katika wasivyo vijua.”

Na maana yake: Kaumba jinsia mbili katika kila aina za viumbe ambavyo wao hawavijui. Hii ni kama aya:

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٣٦﴾

“Na katika kila kitu Tumeumba kwa jozi ili mzingatie.” (51:49)

وَأَيُّ لَيْلٍ لَهُمُ اللَّيْلُ نَسْلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَإِذَا هُمْ مُظْلِمُونَ ﴿٣٧﴾ وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا
ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٨﴾ وَالْقَمَرَ قَدَرْتَهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ
﴿٣٩﴾ لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ

يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

37. Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana, mara wao wanakuwa gizani.

38. Na jua linakwenda katika njia na mwelekeo maalumu mpaka kituoni pake. Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.

39. Na mwezi Tumeupimia vituo, mpaka unakuwa kama karara kongwe.

40. Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao.

Miongoni mwa Alama za Uwezo Mkubwa wa Allah تعالیٰ ni Usiku na Mchana, Jua na Mwezi:

Allah تعالیٰ Anatuambia ushahidi zaidi wa Nguvu na Uwezo Wake ni Kuumba usiku na mchana, kimoja kikiwa na giza lake na kingine na mwanga wake. Kavijalia vitu hivyo kufuatana kimoja baada ya kingine, yaani kimoja kinakuja wakati kingine kinaondoka na hali kama hiyo. Kauli ya Allah تعالیٰ:

يُغْشَى اللَّيْلُ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا

“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi.” (7:54)

Na Anasema tena hapa,

وَأَيُّ لَيْلٍ نَسَلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ

“Na usiku ni Ishara kwao. Tunauvua humo mchana.”

Ina maana, “Tunautoa usiku kwenye mchana hivyo mchana unapotea na usiku unaingia.” Allah تعالى Anasema,

فَإِذَا هُمْ مُظْلِمُونَ

“...mara wao wanakuwa gizani.”

Kama ilivyo katika Hadithi,

«إِذَا أَتَبَلَ اللَّيْلُ مِنْ هُنَا، وَأَذْبَرَ النَّهَارَ مِنْ هُنَا، وَعَزَبَتِ الشَّمْسُ، فَقَدْ أَفْطَرَ الصَّائِمُ»

“Usiku ukiingia kupitia hapa na mchana ukaondokea sehemu hii, na jua limezama, basi mwenye swaumu atapaswa kufuturu.”

Hii ni maana wazi ya Ayah.¹ Allah تعالى Anasema

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ۚ ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٦﴾

“Na jua linakwenda katika njia na mwelekeo maalumu mpaka kituoni pake. Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.”

Hapa kuna tafsiri mbili juu ya ibara hii.

لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ۚ

“...katika njia maalumu mpaka kituoni pake...”

(Rai ya kwanza) ni kuwa njia yake imepangwa na iko chini ya Arshi, juu ya ardhi katika uwelekeo huo. Popote liendako daima liko chini ya Arshi, na hata viumbe vyote pia. Kwani Arshi ndio paa la Ulimwengu, na wala si duara kama wanaanga wengi wanavyodai. Arshi ni kuba lililoegemezwa kwenye nguzo au miguu iliyobebwa na malaika na iko juu ya ulimwengu, juu ya vichwa vya watu. Jua linapokuwa katika mzunguko wake usawa na utosi huwa karibu na Arshi na jua linapopita katika mzunguko wa nne sehemu ya pili ya jua la utosini,

¹ Fat-h Al-Bari 4:231.

linakuwa mbali sana na Arshi. Likiwa hapo, jua husujudu na kuomba ruhusa ya kuchomoza tena kama ilivyoielezwa katika Hadithi.

Al-Bukhari alinakili kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema, "Nilikuwa pamoja na Mtume ﷺ ndani ya msikiti wakati jua likizama akasema,

«يَا أَبَا ذَرٍّ، أَتَدْرِي أَيْنَ تَغْرُبُ الشَّمْسُ؟»

"Ewe Abu Dharr, je wajua Jua linazama wapi?"

Nikasema, "Allah تعالى na Mtume Wake wanajua." Basi Mtume ﷺ akasema,

«فَإِنِّهَا تَذَهَبُ حَتَّى تَسْجُدَ تَحْتَ الْعَرْشِ، فَذَلِكَ قَوْلُهُ تَعَالَى: ﴿وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ﴾»

*"Huenda na kusujudu chini ya Arshi na hiyo ndiyo Kauli Yake Allah, 'Na jua linakwenda katika njia na mwelekeo maalumu mpaka kituoni pake. Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.'*¹

Pia kuna taarifa kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema, "Nilimuuliza Mtume ﷺ juu ya aya hii

«وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا»

"Na jua linakwenda katika njia na mwelekeo maalumu mpaka kituoni pake,"

Mtume ﷺ alisema ,

«مُسْتَقَرُّهَا تَحْتَ الْعَرْشِ»

*"Njia yake iko chini ya Arshi."*²

Kauli ya pili inaashiria pindi litakapofikia kikomo cha muda liliopangiwa, ambao ni Siku ya Kiama, ambapo njia yake itafutwa; Jua litaandama na hapo ndipo litasimama, hapo ndio utakuwa mwisho wa ulimwengu huu na ndio utafikia ukomo wake. Huo ni muda maalumu na masafa maalumu. Qatadah alisema,

¹ Fat-h Al-Bari 8:402.

² Fat-h Al-Bari 8:402.

لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا^ع

“...katika njia maalumu mpaka kituoni pake...”

Ina maana “Jua limepangiwa njia na muda wake wala haliwezi kukiuka viwango vyake ambavyo lilipangiwa.”¹ Pia ilielezwa kwamba jua huenda katika njia yake wakati wa masika mpaka mwisho wa masika na kisha huchukuwa njia nyengine na likaenda nayo katika kiangazi hadi muda huo nao ukafika mwisho na wala halizidishi katika njia yake wala muda wake; ikiwa ni kauli iliyopokelewa kutoka kwa Abdullah bin Amr, Ibn Mas’ud na Ibn Abbas رضي الله عنهم wameisoma aya hii

(وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا)

“Na jua linakwenda bila kuwa na kiwango chake maalumu.”

Yaani halina njia maalumu wala kituo, bali liko katika mwendo usiku na mchana, bila kupunguza kasi wala kusimama, kama ilivyo katika aya:

وَسَخَّرَ لَكُمْ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبِينَ^ط

“...na Akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu.” (14:33)

Yaani, mwezi na jua havitasita wala kupunguza mwendokasi hadi Siku ya Kiama.

ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ

“Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu.”

Yaani hakuna wa kupinga au kuzuia,

الْعَلِيمِ

“Mwenye Kujua.”

Ambaye anajua kila mwendo na kila inapotokea kasi ya mwendo wa kitu yeye anafahamu. Yeye Ndiye Aliyeliweka jua katika mwendo huo na Aliweka muda wake na lini na wapi litasimama na wala hakuna tofauti ya kitu kinyume na Alivyopanga, kama Alivyosema Allah تعالى:

¹ At-Tabari 20:517.

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٣٦﴾

“Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi; na Ameufanya usiku kwa mapumziko na utulivu, na jua na mwezi kwenda kwa hisabu. Hayo ndiyo makadirio ya Aliyetukuka Mwenye Nguvu, Mwenye Ujuzi.” (6:96)

Na hivi ndivyo aya hii inavyosema;

ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ

“Hayo ni makadirio ya Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.”

Kisha anasema Allah تعالی:

وَالْقَمَرَ قَدَرْتَهُ مَنَازِلَ

“Na mwezi Tumeupimia vituo,”

Maana yake ni, “Tumefanya upite katika njia nyingine, ambapo Masafa ya miezi yanaweza kupatikana kwa uwazi kabisa kama vile usiku na mchana vinavyotambulika kutokana na mwendo wa jua. Na hii inalingana na aya

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ

“Wanakuuliza khabari ya miezi. Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na Hija.” (2:189) na

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ اللَّيْلِ وَالْحِسَابَ

“Yeye Ndiye Aliyelijaalia jua kuwa na mwangaza, na mwezi ukawa na nuru, na Akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hisabu.” (10:5) pia

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَاتٍ فَمَحَوْنَا آيَةَ اللَّيْلِ وَجَعَلْنَا آيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً لِّتَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ اللَّيْلِ وَالْحِسَابَ وَكُلُّ شَيْءٍ فَصَلْنَاهُ تَفْصِيلًا ﴿٣٧﴾

“Na Tumefanya usiku na mchana kuwa ishara mbili. Tena Tukaifuta ishara ya usiku, na Tukaifanya ishara ya mchana ni yenye mwangaza ili mtafute Fadhila itokayo kwa Mola Wenu Mlezi, na mpate kujua idadi ya miaka na hisabu. Na kila kitu Tumekifafanua waziwazi.” (17:12)

Kwa hivyo; Allah تعالى Amelipa jua mwanga wake mahususi na mwezi hivyo hivyo, na kila kimoja kati ya hivyo viwili Amekiwekea njia yake. Jua huchomoza na kuchwa kila siku, na kutoa aina moja ya mwangaza kwa wakati wote, lakini hutembea na kufanya mawio na machweo yake kubadilika na kuleta misimu ya mwaka: masika na kiangazi na kufanya mchana kuwa mrefu au mfupi kuliko usiku. Ama mwezi, Allah تعالى Aameamuru kuwa upite katika hatua tofauti.

Kwa kuanzia, hapo mwanzoni mwa mwezi, mwezi mwandamo huonekana mdogo ukichomoza. Hutoa mwanga mdogo sana, kisha katika usiku wa pili wa mwezi mwanga wake huongezeka na huwa umepanda juu kuliko pale ulipoonekana (jioni ya jana yake) na kadiri siku zinavyoongezeka ndivyo mwezi huo unavyopanda juu kila Magharibi na kila unavyozidi kupanda juu ndivyo nuru yake inavyozidi kuongezeka pamoja na kuwa ni mwanga wa jua ambao unaakisiwa kwenye mwezi. Hali hiyo inaendelea hadi usiku wa kumi na nne baada ya mwezi kuandama, mwezi huwa umekamilika unaonekana duara kamili. Kisha baada ya hapo mwezi huu huanza tena kupungua na mwanga wake hupungua kadiri unavyoteremka kila usiku mpaka baadaye huonekana umepinda kama karara la mtende kongwe. Ibn Abbas رضي الله عنهما anasema kuwa. Hili (ni) karara na asili ya shina linalounga kole la tende kwenye mtende.¹

Waarabu wana majina ya kila usiku mitatu ya mwezi tangu uchomoze hadi mwisho – kulingana na misimu yake. Wanaita katika usiku wa siku tatu za mwanzo kuwa ni *Ghurar*, kisha wanaita mwezi katika siku tatu inazofuatia kama *Nufal*; na nyengine tena *Tusa* (tisa) maana usiku wa mwisho katika hizo tatu ni wa tisa; baada ya hapo huitwa *Ushar* (kumi) - kwa sababu ule usiku wa mwanzo wa fungu hili ni wa kumi. Fungu linalofuatia ni lile ambalo mwezi huwa umefikia kilele chake katika kung'aa na huitwa *Al-Biidh* (mweupe). Fungu la siku tatu zifuatazo huitwa *Dura* ambao ni wingi wa “*Dara*’ kwa sababu

¹ At-Tabari 20:518.

mwezi huchelewa kuchomoza na jua likizama basi huwa giza mpaka mwezi uchomoze. *Dar'a'* ni kufananishwa na mbuzi mweusi, yaani mwenye kichwa cheusi. Kisha usiku wa siku tatu baada ya hapo huitwa *Dhulam*; kisha *Hanaadis* na kufuatiwa na *Da'aadi*, kisha *Mihaaq* kwa kukosekana mbalamwezi mwishoni na Mwanzoni kwa mwezi mpya. Abu Ubayd hakutambua majina ya *Tusa* na *Ushar* katika kitabu, *Gharib Al-Musannaf*.

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ

“Haliwi jua kuufikia mwezi,”

Mujahid anasema, “(Jua na mwezi) kila kimoja kina mipaka yake ambayo haiwezi kuichupa au kuishia njiani bila ya kuifikia. Muda wa kimojawapo ukiwadia basi kingine huwa muda wake umekamilika na huondoka na kumpisha mwenziwe na muda wake umekuwa umefikia kikomo.”¹ Kuhusu ayah hii, ‘Ikrimah alisema.

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ

“Haliwi jua kuufikia mwezi.”

Yaani, kila kimoja kina muda wake wa kufanya kazi yake. Hivyo, si mahali pake jua kuchomoza wakati wa usiku,

وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ

“...wala usiku kuupita mchana.”

Yaani, baada ya usiku kuwa umepita, si sawa usiku mwingine kuja papo hapo, bali kwanza lazima uje wakati wa mchana. Mamlaka ya Jua ni mchana na ya mwezi ni usiku. Adh-Dhahhak alisema, “Usiku hauondoki kutoka hapa isipokuwa mpaka mchana uwe umekuja kutokea hapa – akaashiria upande wa Mashariki.”² Mujahid alisema,

وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ

“...wala usiku kuupita mchana.” “(Usiku na mchana) hutafutana Haraka sana.”³

¹ At-Tabari 20:520.

² At-Tabari 20:520.

³ At-Tabari 20:519.

Yaani hakuna kipindi kinachopita ila upo usiku au mchana, hakuna nafasi isipokuwa vitu hivi viwili vinafuatana kwa kuwa vimepangiwa hivyo.

وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ

“Na vyote vinaogelea katika njia zao.”

Yaani usiku na mchana, jua na mwezi daima vinaelea; vinazunguka katika njia zao huko angani. Hii ilikuwa ni kauli ya Ibn Abbas, Ikrimah, Adh-Dhahaak, Al-Hassan, Qatadah na Al-Khuraasani رضي الله عنهم.¹

Ibn Abbas رضي الله عنهما pamoja na *Salaf* wengine walisema, Mapito (ya jua na mwezi) ni kama (upinde) sehemu ya duara ya gurudumu linalozunguka.

وَأَيُّهُمْ أَنَا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ فِي الْفَلَكِ الْمَشْحُونِ ﴿٣٦﴾ وَخَلَقْنَا لَهُمْ مِن مِّثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ

﴿٣٧﴾ وَإِنْ نَشَأْ نُغْرِقْهُمْ فَلَا صَرِيحَ لَهُمْ وَلَا هُمْ يُنقَدُونَ ﴿٣٨﴾ إِلَّا رَحْمَةً مِنَّا وَمَتَاعًا إِلَىٰ

حِينٍ ﴿٣٩﴾

41. Na ni Ishara kwao kwamba Sisi Tuliwapakia vizazi vyao katika jahazi iliosheheni.

42. Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyovipanda.

43. Na Tukitaka Tutawazamisha, wala hapana wa kuwasaidia, wala hawataokolewa.

44. Isipokuwa kwa Rehema zitokazo Kwetu na starehe za muda mchache.

Miongoni mwa Dalili za Allah تعالى ni kuwa Aliwabeba katika Merikebu

Allah تعالى Anatuambia dalili nyingine za Utukufu Wake ni kuwa Kaitiisha bahari kubeba meli zilizoshehenezwa; ikiwemo bila shaka Safina ya Nuhu عليه السلام ambamo Allah تعالى Alimnusuru yeye na waumini wakiwa miongoni mwa vizazi vya Adam عليه السلام ambavyo vilikuwa katika ardhi. Allah تعالى Anasema,

¹ At-Tabari 20:520.

وَأَيُّهُمْ أَنَا حَمَلْنَا ذُرِّيَّتَهُمْ

“Na ni Ishara kwao kwamba Sisi Tuliwapakia dhuriya yao...”

Yaani, mababa zao wa kale.

فِي الْفُلْكِ الْمَشْحُونِ

“...katika jahazi iliosheheni.”

Yaani, katika meli iliyosheheni mizigo na wanyama ambao Allah تعالى Alimuamuru Nuhu عليه السلام kuwaweka wawili wawili kwa kila aina. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa iliyosheheni, ‘ni iliyoshehenezwa.’¹ Kauli hii pia ilikuwa ya Said bin Jubair, Ash-Sha’bi, Qatadah na As-Suddi.² Adh-Dhahaak, Qatadah na Ibn Zayd walisema: “Ilikuwa Safina ya Nuhu عليه السلام.”³

وَخَلَقْنَا لَهُمْ مِن مِّثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ

“Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyovipanda.”

Al-Awafi alisema akiwa anasimulia mapokezi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. “Hii maana yake ni ngamia, maana hii ni meli ya nchi kavu ambayo watu husheheni mizigo na pia hupanda.”⁴ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, “Je mwajua aya hii ina maana gani?”

وَخَلَقْنَا لَهُمْ مِن مِّثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ

“Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyovipanda.”

Tulisema, “Hapana,” Akasema, “Inamaanisha meli zilizoundwa baada ya Safinah ya Nuhu عليه السلام ambazo zilikuwa zimefanana sana.”⁵ Kauli hii pia ilikuwa ya Abu Malik, Adh-Dhahaak, Qatadah, Abu Salih na As-Suddi kuwa aya:

¹ At-Tabari 20:522.

² At-Tabari 20:522.

³ At-Tabari 20:522, 523.

⁴ At-Tabari 20:524.

⁵ At-Tabari 20:523.

وَحَلَقْنَا لَهُمْ مِنْ مِثْلِهِ مَا يَرْكَبُونَ ﴿٣٦﴾

“Na Tukawaumbia kutoka mfano wake wanavyovipanda.”

Inamaanisha meli.¹

وَإِنْ دُشُّوا نُغْرِقْهُمْ

“Na Tukitaka Tutawazamisha.”

Yaani abiria walio katika meli.

فَلَا صَرِيحَ لَهُمْ وَلَا

“...wala hapana wa kuwasaidia.”

Yaani, hakutakuwepo wa kuwaokoa kutokana na angamizo hilo.

وَلَا هُمْ يُنْقَدُونَ

“...wala hawataokolewa.”

Yaani, katika janga ambalo limewafika.

إِلَّا رَحْمَةً مِنَّا

“Isipokuwa kwa rehema zitokazo Kwetu.”

Yaani, isipokuwa Huruma Zetu tumerahisisha safari zenu za nchi kavu na baharini na tunakuwekeeni katika usalama mpaka ajali yenu (muda wenu) itapofika.” Allah تعالى Anasema:

وَمَتَّعْنَا إِلَىٰ حِينٍ

“...na starehe za muda mchache.”

Maana yake, mpaka utakapotimia na huo unajulikana Kwake Allah تعالى Peke Yake.

¹ At-Tabari 20:522-524.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اتَّقُوا مَا بَيْنَ أَيْدِيكُمْ وَمَا خَلْفَكُمْ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٣٤﴾ وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٣٥﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْطَعِمُ مَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ أَطَعَمَهُ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٣٦﴾

45. Na wanapoambiwa: Jilindeni na yalioko mbele yenu na yalioko nyuma yenu, ili mpate kurehemewa...

46. Na haiwafikii Ishara yoyote katika Ishara za Mola Wao Mlezi ila wao huwa ni wenye kuipuuza.

47. Na wanapoambiwa: Toeni katika aliyokupeni Mwenyezi Mungu, waliokufuru huwaambia walioamini: Je! Tuwalishe ambao Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwalisha mwenyewe? Nyinyi hammo ila katika upotofu uliodhahiri.

Ubainifu wa Kupotoka Washirikina

Allah تعالیٰ Anatuambia jinsi washirikina walivyong'ang'ana katika upotovu wao wala hawakujali maovu waliyokuwa wakiyatenda; pia hata yale waliyokwisha yafanya kabla ya hapo. Bali hawakujali jambo la kuwafaa katika siku za usoni hapo itakapofika Siku ya Kiama,

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اتَّقُوا مَا بَيْنَ أَيْدِيكُمْ وَمَا خَلْفَكُمْ

“Na wanapoambiwa: Jilindeni na yalioko mbele yenu na yalioko nyuma yenu.”

Mujahid akisema kuwa kauli hii inamaanisha madhambi. Wengine walisema ni kinyume chake.

لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

“...ili mpate kurehemewa...”

Maana yake, “hivyo basi, kama wataogopa (kuyafanya) mambo hayo, Allah تعالیٰ Atakuhurumieni na Atawaokoeni isiwafike adhabu yake.” Ibara inaonesha

kuwa bali hao watu hawataongoka bali watakengeuka na kuyadharau (waambiwayo) hayo, kama Anavyosema Allah تعالى.

وَمَا تَأْتِيهِمْ مِنْ آيَةٍ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِمْ

“Na haiwafikii Ishara yoyote katika Ishara za Mola Wao Mlezi...”

Yaani, Alama za Tauhidi (kupwekeka kwa Allah تعالى) na ukweli wa Mtume.

إِلَّا كَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ

“...ila wao huwa ni wenye kuipuuza.”

Maana yake ni kuwa hawakuzikubali hizo dalili na Ishara na wala hawakufaidika na dalili hizo wala ishara hizo.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ

“Na wanapoambiwa: Toeni katika Aliyokupeni Mwenyezi Mungu,”

Yaani, na wanapoambiwa kutoa sadaka kutokana na yale Allah تعالى Aliyoyaruzuku kwao, wawape masikini na wale wenye haja miongoni mwa Waislamu

قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا

“...waliokufuru huwaambia walioamini...”

Yaani, kuwaambia waumini ambao ni masikini walioamrisha kuwasaidia, huwaambia wao kwa kutoa hoja.

أَتُطْعِمُ مَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ

“Je! Tuwalishe ambao Mwenyezi Mungu Angependa Angeliwalisha mwenyewe?”

Yaani, “hawa ndio mnatuamuru tuwasaidie, kama Allah تعالى Angelitaka Kuwapa Angeliwapatia chakula na wakawa huru, hivyo sisi hatuwapi tukitekeleza utashi wa Mola Wao, ili wabakie hivyo hivyo wahitaji.”

إِنْ أَنتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ

“Nyinyi hammo ila katika upotofu ulio dhahiri.” Kwa kutuambia tufanye hayo.

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٨﴾ مَا يَنْظُرُونَ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً تَأْخُذُهُمْ وَهُمْ يَخِصِّمُونَ ﴿٤٩﴾ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ تَوْصِيَةً وَلَا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ يَرْجِعُونَ ﴿٥٠﴾ وَتُفْعَلُ فِي الصُّورِ فَإِذَا هُمْ مِنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنْسِلُونَ ﴿٥١﴾ قَالُوا يَا بَوَلَّيْنَا مِنْ بَعَثْنَا مِنْ مَرْقَدِنَا هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ ﴿٥٢﴾ إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٥٣﴾ فَالْيَوْمَ لَا تُظَلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَلَا تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٤﴾ إِنْ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ الْيَوْمَ فِي شُغْلٍ فَاكِهِونَ ﴿٥٥﴾ هُمْ وَأَزْوَاجُهُمْ فِي ظِلِّ عَلَى الْأَرَآئِكِ مُتَكِبُونَ ﴿٥٦﴾ هُمْ فِيهَا فَاكِهِونَ وَهُمْ مَا يَدْعُونَ ﴿٥٧﴾ سَلَّمَ قَوْلًا مِنْ رَبِّ رَحِيمٍ ﴿٥٨﴾ وَأَمْتَنُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٥٩﴾ * أَلَمْ أَعْهَدْ لَكُمْ يَبْنَئِي ءَادَمَ أَنْ لَا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ إِنَّهُ لَكُرٌّ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٦٠﴾ وَأَنْ أَعْبُدُونِي هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾ وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ ﴿٦٢﴾

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٨﴾ مَا يَنْظُرُونَ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً تَأْخُذُهُمْ وَهُمْ يَخِصِّمُونَ ﴿٤٩﴾ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ تَوْصِيَةً وَلَا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ يَرْجِعُونَ ﴿٥٠﴾

48. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi ni wa kweli?

49. Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakaowachukua nao wamo kuzozana.

50. Basi hawataweza kuusia, wala kwa watu wao hawarejei.

Makafiri Wanapinga Uwepo wa Siku ya Ufufuo.

Allah تعالیٰ Anatueleza jinsi washirikina walivyokuwa wanasema kuwa kamwe Qiyama hakitasimama kwa kauli yao,

مَتَى هَذَا الْوَعْدُ

“Ahadi hii itatokea lini.”

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا

“Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi.” (42:18)

Allah تعالیٰ Anasema:

مَا يَنْظُرُونَ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً تَأْخُذُهُمْ وَهُمْ يَخِصِّمُونَ ﴿٥١﴾

“Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakaowachukua nao wamo katika kuzozana.”

Yaani, wanasubiri ukelele mmoja kutoka kwenye baragumu, pindi watu wakiwa katika shughuli zao na sehemu wakibishana juu ya mambo yao kama kawaida. Wakiwa katika hali hiyo Allah تعالیٰ Atamuamuru Israfil kupuliza baragumu, atapuliza ukelele mara moja na mpulizo mrefu, halafu hakutabakia yeyote hai duniani, bali atatega sikio lake kusikiliza sauti hiyo kutoka angani. Kisha wote walio hai watakusanywa na moto kutoka kila upande. Allah تعالیٰ Anasema.

فَلَا يَسْتَطِيعُونَ نَوْصِيَّةً

“Basi hawataweza kuusia.”

Yaani, kuhusu mali zao (kuweka wasiya) kwa sababu hali hiyo inatisha na nzito (na muda hakuna).

وَلَا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ يَرْجِعُونَ

“...wala kwa watu wao hawarejei.”

Hadithi nyingi zinaeleza juu ya jambo hili ambalo tumelieleza mahali kwingine. Baada ya hapo kutasikika baragumu jingine na kitakufa kila kilicho hai isipokuwa yule Aliye Hai Daima milele. Baada ya hapo utapigwa upulizo wa parapanda wa tatu wa kufufua vilivyokufa.

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَإِذَا هُمْ مِنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنْسِلُونَ ﴿٥٢﴾ قَالُوا يَنْوِيلَنَا مِنْ

بَعَثْنَا مِنْ مَّرْقَدِنَا هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ ﴿٥٣﴾ إِنْ كَانَتْ إِلَّا

صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٥٤﴾ قَالِيَوْمَ لَا تُظَلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَلَا

تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾

51. Na litapulizwa barugumu, mara watatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola Wao Mlezi.

52. Watasema: Ole wetu! Nani aliyetufufua kwenye malazi yetu? Haya ndiyo aliyoyaahidi Mwingi wa Rehema na waliyoyasema kweli Mitume.

53. Haitakuwa ila ukelele mmoja tu, mara wote watahudhurishwa mbele yetu.

54. Basi leo nafsi yoyote haitadhulumiwa kitu, wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyatenda.

Parapanda la Ufufuo.

Huu utakuwa upulizo wa parapanda wa tatu¹ huu ni mpulizo ambao utawafanya watu watoke kwenye makaburi yao. Allah تعالى Anasema.

فَإِذَا هُمْ مِنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنْسِلُونَ

“...mara watatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola Wao Mlezi.”

Yansiluun maana yake watatembea haraka haraka. Hii inafanana na ayah,

يَوْمَ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَىٰ نُصُبٍ يُوفِضُونَ ﴿٧٠﴾

“Siku watakapotoka makaburini kwa upesi kama kwamba wanakimbilia mfundo.” (70:43).

قَالُوا يَنْوِيلُنَا مَنْ بَعَثَنَا مِنْ مَرْقَدِنَا

“Watasema: Ole wetu! Nani aliyetufufua kwenye malazi yetu?”

Maana yake ni kuwa watatoka katika makaburi yao ambayo walikuwa wanaamini kuwa hawatatoka ndani yake; (Watahangaa) wakiona kwa macho yao yanatokea yale ambayo waliyakanusha na hawakutaka kuyaamini..

قَالُوا يَنْوِيلُنَا مَنْ بَعَثَنَا مِنْ مَرْقَدِنَا

“Watasema: Ole wetu! Nani aliyetufufua kwenye malazi yetu?”

¹ Angalia juzu ya saba, Tafsir ya Surat An-Naml (22:87).

Kauli ya Ayah hii haipingani na ukweli kwamba wataadhibiwa makaburini (kabla ya kufufuliwa) kwa sababu muda wa (adhabu ya) kaburini ukilinganishwa na muda wa (adhabu ya) akhera ni kama kukwapua au kupepesa jicho (katika maisha ya mtu). Ubbay bin Ka'b, Mujahid, Al-Hasan na Qatadah walisema, "Watalala kabla ya kufufuliwa Siku ya Qiyamah."¹

Qatadah alisema, "(Usingizi huo) Utakuwa baina ya ukelele wa parapanda ya kwanza na ukelele wa pili, na kisha atasema, "Nani katuinua kutoka katika usingizi wetu."²

Watakaposema hayo, waumini watawajibu. Hiyo ni rai ya *Salaf* wengi,

هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ

"Haya ndiyo aliyoyaahidi Mwingi wa Rehema na wakasema kweli Mitume."

Al-Hasan alisema, "Malaika watawajibu namna hiyo. Hakuna mgongano wala mvutano kwa sababu yote mawili yanawezekana kutokea. *Allah A'lamu.*

إِنْ كَانَتْ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً فَإِذَا هُمْ جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿٦٧﴾

"Haitakuwa ila ukelele mmoja tu, mara wote watahudhurishwa mbele yetu."

Hii inafanana na aya ya:

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿٧٩﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٨٠﴾

"Kwa hakika hayo ni ukelele mmoja tu, Mara watakuwa kwenye uwanda wa mkutano!" (79:13-14) na

وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ إِلَّا كَلِمَةٍ أَلْبَصَرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ ﴿٧٧﴾

"Wala halikuwa jambo la Saa (ya Kiyama) ila kama kupepesa kwa jicho, au karibu ya hivyo." (16:77) na

¹ At-Tabari 20:333.

² At-Tabari 20:532.

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٧﴾

“Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.” (17:52).

Yaani, “Tutatoa Amri moja tu, wote watakusanyika pamoja,

فَالْيَوْمَ لَا تُظَلِّمُ نَفْسٌ شَيْئًا

“Basi leo nafsi yoyote haitadhulumiwa kitu.”

Kuhusiana na amali hizi,

وَلَا تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ

“...wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyatenda.”

إِنَّ أَصْحَابَ الْجَنَّةِ الْيَوْمَ فِي شُغْلٍ فَكَهُونَ ﴿٥٨﴾ هُمْ وَأَزْوَاجُهُمْ فِي ظِلِّ عَلَى الْأَرَائِكِ

مُتَّكُونَ ﴿٥٩﴾ هُمْ فِيهَا فَكَهَةٌ وَهُمْ مَا يَدْعُونَ ﴿٦٠﴾ سَلَّمَ قَوْلًا مِّن رَّبِّ رَحِيمٍ ﴿٦١﴾

55. Hakika watu wa Peponi leo wamo shughulini, wamefurahi.

56. Wao na wake zao wamo katika vivuli wameegemea juu ya viti vya fahari.

57. Watapata humo (kila namna ya) matunda na watapata kila watakachokitaka.

58. “Salama!” Hiyo ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mlezi Mwenye Kurehemu.

Ubainifu wa Maisha ya Watu wa Peponi

Allah تعالی Anatuambia kuwa katika siku hiyo ya Kiyama ambapo watu wa Peponi watakapotokea katika viwanja vya Malipo, kisha wakashuka na kutuwama katika bustani ya Peponi; watashughulishwa hapo Peponi kiasi hawatakuwa na muda wa kujali habari za watu wengine. Watu hawa watakuwa na furaha kwa ushindi wao wa milele (na kunusurika na adhabu ya Jahanamu). Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى na Ismail ibn Abi Khalid رحمه الله تعالى walisema:

Watashughulishwa na mambo mengi kiasi ambacho hawatopata fursa au muda wa kuanza kufikiria watu wa motoni wamo katika mambo yapi na mazito gani.” Mujahid alisema,

فِي شُغْلٍ

“...wamo shughulini.”

“Watashughulishwa na mambo yao ya furaha wanazozisherehekea.”¹ Kauli hii pia ya Qatadah. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa:

فَيَكْهُونَ

“Watakuwa wanasherehekea.”

Na Kauli ya Allah تعالى:

هُمْ وَأَزْوَاجُهُمْ

“Wao na wake zao...”

Mujahid anasema, “Wake zao.”

فِي ظِلِّلٍ

“...katika vivuli...”

Maana yake ni kuwa chini ya vivuli vya miti.²

عَلَى الْأَرْبَابِ مُتَّكُونَ

“...wamegemea juu ya viti vya fakhari.”

Ibn Abbas, Mujahid Ikrimah, Muhammad bin Ka’b, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na Khusayf رضي الله عنهم walisema,

عَلَى الْأَرْبَابِ

“...viti vya fakhari.”

Ni vitanda vilivyo chini ya vivuli vya upenu.³

¹ At-Tabari 20:535.

² At -Tabari 20:538.

³ At -Tabari 20:539, 540.

هُمْ فِيهَا فَكَيْهَةٌ

“Watapata humo (kila namna) ya matunda...”

Matunda ya aina zote.

وَهُمْ مَا يَدْعُونَ

“...na watapata kila watakachokitaka.”

Yaani, chochote na lolote wataloomba au kutaka bali litapatikana kwa namna yoyote ile.

سَلَامٌ قَوْلًا مِّن رَّبِّ رَحِيمٍ ﴿٤٨﴾

“Salama!” Hiyo ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mlezi Mwenye Kurehemu.”

Ibn Jurayji alisema, “Akasema, Ibn Abbas رضي الله عنهما juu ya ayah hii, “Mwenyezi Mungu Mwenyewe ambaye ndiye As-Salaam (Amani) Atatoa amani kwa watu wa Peponi. Kauli hii ya Ibn Abbas رضي الله عنهما inaendana sawa na ayah,

تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ سَلَامٌ ۗ

“Maamkiano yao siku ya kukutana naye yatakuwa: Salama!”
(33:44).

وَأَمْتَنُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٤٩﴾ * أَلَمْ أَعْهَدْ لَكُمْ يَبْنَئِي ۖ ءَادَمَ أَن لَّا تَعْبُدُوا
الشَّيْطَانَ ۗ إِنَّهُ لَكُرْمٌ عَدُوٌّ مِّبِينٌ ﴿٥٠﴾ وَأَنِ اعْبُدُونِي ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾ وَلَقَدْ
أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا ۗ أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ ﴿٥٢﴾

59. Na enyi wakosefu! Jitengeni leo!

60. Je! Sikuwapa Amri, enyi wanaadamu, kuwa msimuabudu Shetani? Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu.

61. Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo Njia Iliyonyooka.

¹ At -Tabari 20:539, 540.

62. Na bila ya shaka Yeye Amekwisha lipoteza kundi kubwa miongoni mwenu. Je, hamkuwa mkifikiri?

Kutenganishwa kwa Washirikina na Makemeo Watakatayopata Siku ya Kiama

Allah تعالى Anatueleza utakavyokuwa mwisho wa washirikina katika Siku ya Kiama; pale Atakapowaamuru kujitenga mbali na waumini, yaani wawe peke yao pembeni mbali ya waumini.

Hii ni kama aya,

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا مَكَانَكُمْ أَنْتُمْ وَشُرَكَاءُكُمْ فَزَلَّلْنَا بَيْنَهُمْ

“Na siku Tutakapowakusanya wote, kisha Tutawaambia walio shirikisha: Simameni mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika. Kisha Tutawatenga baina yao.” (10:20)

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُومِئُونَ بِتَفْرِقُونَ ﴿١٤﴾

“Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika.” (30:14) na

يَوْمِئِذٍ يَصَّدَّعُونَ ﴿١٥﴾

“Siku hiyo (watu) watatengana.” (30:43).

Hii ina maana kuwa (watu) watakuwa makundi mawili tofauti.

أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٢٢﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَأَهْدُوهُمْ إِلَىٰ

صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٣﴾

“Wakusanyeni waliodhulumu, na wake zao, na hao waliokuwa wakiwaabudu, badala ya Mwenyezi Mungu. Waongozeni njia ya Jahannamu!” (37:22-23)

الْمَرْأَعَهْدَ إِلَيْكُمْ بِنَبِيِّ آدَمَ أَبَ لَا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُبِينٌ ﴿٣٦﴾

“Je! Sikuagana nanyi, enyi wanaadamu, kuwa msimuabudu Shetani? Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu.”

Hili ni kemeo la Allah تعالى kwa makafiri miongoni mwa wana wa Adam, wale ambao wanamtii Shetani licha ya kuwa huyo (Shetani) ni adui yao wazi wazi; na wakamuasi *Ar-Rahman* Ambaye Aliwaumba wao na Kuwapatia neema zote na mafao kwa maisha yao yote. Anasema Allah تعالى,

وَأَنْ أَعْبُدُونِي هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

“Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo Njia Iliyonyooka.”

Yaani, Niliwaamuru duniani kumuasi Shetani na nilikuamrisheni kuniabudu Mimi na huo ndio uongofu, badala yake mkapita njia nyingine na mkafuata amri za Shetani, Allah تعالى Anasema,

وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا

“Na bila ya shaka yeye amekwishalipoteza kundi kubwa miongoni mwenu.”

Maana yake watu wengi (kawapoteza). Hii ilikuwa rai ya Mujahid, Qatadah, As-Suddi na Sufiyan Uyaynah.

أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ

“Je, hamkuwa mkifikiri?”

Ina maana, Je haya hamkuwa mnayaelewa; pale mlipomuasi Mola Wenu, na badala ya kumuabudu Yeye tu Peke Yake, mlimshirikisha na kumuekea wenza na mkachagua kumfuata Shetani.

* * *

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٦٣﴾ أَصْلَوْهَا الْيَوْمَ
 بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٦٤﴾ الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ أَفْوَاهِهِمْ
 وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٦٥﴾
 وَلَوْ نَشَاءُ لَطَمَسْنَا عَلَىٰ أَعْيُنِهِمْ فَاسْتَبَقُوا الصِّرَاطَ فَأَنَّى
 يُبْصِرُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَمَسَخْنَاهُمْ عَلَىٰ مَكَاتَتِهِمْ
 فَمَا اسْتَبَقُوا مُضِيًّا وَلَا يَرْجِعُونَ ﴿٦٧﴾ وَمَنْ نُعَمِّرْهُ
 نُنَكِّسْهُ فِي الْخَلْقِ أَفَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٦٨﴾ وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ
 وَمَا يَلْبَغِي لَهُ ؎ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْءَانٌ مُّبِينٌ ﴿٦٩﴾ لِيُنذِرَ
 مَنْ كَانَ حَيًّا وَيَحِقَّ الْقَوْلُ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٧٠﴾ أَوَلَمْ
 يَرَوْا أَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِنَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَمًا فَهُمْ لَهَا
 مَلِكُونَ ﴿٧١﴾ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ فَمِنهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنهَا يَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾
 وَهُمْ فِيهَا مَنفَعٌ وَمَشَارِبٌ ؕ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ
 ﴿٦٣﴾ أَصْلَوْهَا الْيَوْمَ بِمَا كُنْتُمْ
 تَكْفُرُونَ ﴿٦٤﴾ الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ
 أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ
 أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٦٥﴾ وَلَوْ
 نَشَاءُ لَطَمَسْنَا عَلَىٰ أَعْيُنِهِمْ فَاسْتَبَقُوا
 الصِّرَاطَ فَأَنَّى يُبْصِرُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ
 نَشَاءُ لَمَسَخْنَاهُمْ عَلَىٰ مَكَاتَتِهِمْ فَمَا
 اسْتَبَقُوا مُضِيًّا وَلَا يَرْجِعُونَ ﴿٦٧﴾

63. Hii basi ndiyo Jahannamu mliyokuwa mkiahidiwa.

64. Ingieni leo kwa vile mlivyokuwa mkikufuru.

65. Leo Tunaviziba vinywa vyao, na iseme Nasi mikono

yao, na itoe ushahidi miguu yao kwa waliyokuwa wakiyachuma.

66. Na Tungelipenda Tungeliyafutilia mbali macho yao, wakawa wanaiwania njia. Lakini wangeionaje?

67. Na Tungelitaka Tungewageuza sura hapo hapo walipo, basi wasingeweza kwenda wala kurudi.

Na Siku ya Kiyama washirikina miongoni mwa wanaadamu wataambiwa haya baada ya kuwa wameuona Moto wa *Jahim* ukiwa ni kuwafedhehesha na kuwatahariza.

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٦٣﴾

“Hii basi ndiyo Jahannamu mliyokuwa mkiahidiwa.”

Yaani, “Hiki ndicho Mitume walikuwa wakikuonyeni dhidi yake, lakini hamkuwaamini wao wala maneno yao.”

أَصْلَوْهَا الْيَوْمَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٦٣﴾

“Ingieni leo kwa vile mlivyokuwa mkikufuru.”

Hii ni kama hizi,

يَوْمَ يُدْعُونَ إِلَىٰ نَارِ جَهَنَّمَ دَعَا ﴿٦٤﴾ هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكذِّبُونَ ﴿٦٥﴾ أَفَسِحْرٌ
هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تَبْصُرُونَ ﴿٦٦﴾

“Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu, (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha! Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu?” (52:13-15)

Midomo ya Washirikina Itafungwa Siku ya Kiyama

Allah تعالیٰ Anasema:

الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٦٧﴾

“Leo Tunaviziba vinywa vyao, na iseme Nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu yao kwa waliyokuwa wakiyachuma.”

Hali ya midomo kufungwa isiseme lolote itakuwa kwa washirikina na makafiri siku hiyo ya Kiyama. Pale watakapokanusha kuwa hawakufanya madhambi hayo duniani na kuendelea kuapa kuwa hawakuyafanya hayo, Allah تعالیٰ Atafunga vinywa vyao na kufanya viungo vyao kutamka vikielezea juu ya yale waliyoyatenda.

Abi Hatim رضي الله عنه amenakili kutoka kwa Anas bin Malik عنه رضي الله تعالى akisema, “Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ na alitabasamu sana kiasi magego yake yalionekana kisha akasema,

«أَتَذَرُونَ مِنِّي أَضْحَكُ؟»

“Mwajua kwa nini ninacheka ?”

Tukasema, “Allah تعالیٰ na Mtume Wake ﷺ wanajua zaidi.” Akasema,

«مِنْ مُجَادَلَةِ الْعَبْدِ رَبَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، يَقُولُ: رَبِّ أَلَمْ تُجِرْنِي مِنَ الظُّلْمِ؟ يَقُولُ: بَلَى، يَقُولُ: لَا أُجِيزُ عَلَيَّ إِلَّا شَاهِدًا مِنْ نَفْسِي، يَقُولُ: كَفَى بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا، وَبِالْكَرَامِ الْكَاتِبِينَ شُهُودًا، فَيُخْتَمُ عَلَى فِيهِ، وَيُقَالُ لِأَرْكَانِهِ: انْطِقِي فَتَنْطِقِ بِعَمَلِهِ، ثُمَّ يُخَلِّي بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْكَلَامِ، يَقُولُ: بَعْدًا لَكُنَّ وَسُحْقًا، فَمَنْكُنَّ كُنْتُ أَنْأَصِلُ»

“Kutokana na mja atakavyobishana na Mola Wake Siku ya Kiyama Atasema,” Ya Rabi, Utanihifadhi na dhulma? “Allah Atasema, “Naam” Atasema mja, “Mimi sikubali ushahidi wa yeyote dhidi yangu isipokuwa ushahidi kutoka kwangu mwenyewe. Allah Atasema, “Leo hii wewe utakuwa Shahidi tosha dhidi ya nafsi yako na Malaika waandishi, Kiraman Kaatibin, watatoa ushahidi dhidi yako. Kisha mdomo wa mja utafungwa na kisha viungo vyake vitaambiwa, “Semeni.” Viungo vitasema matendo yake; kisha mdomo wake utarejeshewa kauli na atasema, kiviambia viungo vyake, “Kuangamia kutakuwa kwenu, mimi nilikuwa napigania kukuteteeni ninyi (viungo).”

Hadithi hii ilipokelewa na Muslim na An Nasai.¹

Ibn Jarir رضي الله عنه amepokea kutoka kwa Abu Musa Al-Ashari رحمه الله تعالى alisema, “Muumini ataitwa ili kueleza matendo yake Siku ya Kiyama, na Mola Wake atamuonesha matendo yake kwa siri yao wawili tu. Mja atakubali matendo yake na kusema, “Ya Rabi ni kweli niliyafanya hayo.” Kisha Allah تعالى Atamsamehe madhambi yake na kisha Atamfichia siri yake na hakuna kiumbe yeyote atakayeyaona hayo madhambi ya mja huyu, bali matendo yake mema yataonekana wazi wazi na angelipenda watu wote wayaone hayo matendo yake mema. Kisha makafiri na wanafiki wataletwa kila mmoja kujitetea dhidi ya madhambi yake. Mola Wake Atamuonesha matendo yake. Huyu atayakana kwa kusema “Ya Rabi, kwa Utukufu Wako, malaika huyu ameandika yale ambayo mimi sikuyafanya.” Malaika atamjibu kwa kusema, “Je hukufanya jambo fulani siku fulani na mahali fulani?” Mja huyo kafiri atasema, “La. Kwa Utukufu Wako hayo mimi sikuyafanya.” Wakati akisema hayo Allah Atamfunga kinywa chake.” Abu Musa Al-Ash’ari رضي الله عنه alisema, “Nadhani kuwa kiungo chake cha kwanza kunena katika mwili wake kitakuwa ni paja lake la kuume.”

¹ Muslim 4:2280, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:508.

Kisha akasoma,

الْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلَىٰ أَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَا أَيْدِيهِمْ وَتَشْهَدُ أَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٦٦﴾

“Leo Tunaviziba vinywa vyao, na iseme Nasi mikono yao, na itoe ushahidi miguu yao kwa waliyokuwa wakiyachuma.”¹

وَلَوْ نَشَاءُ لَطَمَسْنَا عَلَىٰ أَعْيُنِهِمْ فَاسْتَبَقُوا الصِّرَاطَ فَأَنَّىٰ يُبْصِرُونَ ﴿٦٧﴾

“Na kama Tungelipenda Tungeliyafutilia mbali macho yao, wakawa wanaiwania njia. Lakini wangeionaje?”

Ali bin Abi Talhah alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما maelezo ya Ayah hii akisema, “Allah تعالى Anasema, “Kama Tungelitaka, Tungeliwapotosha wote wakawa mbali ya ukweli, hivyo vipi wangeliongoka?” Na wakati mwingine alisema, “Tungeliwapofua.”² Al-Hasan Al-Basriy رحمه الله تعالى alisema, “Kama Mola Angelitaka Angeliyafumba macho yao na Kuwafanya vipofu wakienda kwa kutangatanga ovyo.” Mujahid, Abu Salih, Qatadah na As-Suddi walisema, “Hivyo wangelikuwa wakitangatanga na njia, yaani wakiitafuta njia iliyonyooka.” Ibn Zayd alisema, “Angeliona vipi wakati macho yao tumeyafumba?” Al-Awfi alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

فَأَنَّىٰ يُبْصِرُونَ

“Lakini wangeionaje?”

“Wasingeliweza kuona ukweli.”³

وَلَوْ نَشَاءُ لَمَسَخْنَاهُمْ عَلَىٰ مَكَانَتِهِمْ

“Na Tungelitaka Tungewageza sura hapo hapo walipo...”

Pia Al-Awfi amepokea habari za kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema maana yake ni, “Tungeliweza kuwaangamiza.”⁴ As-Suddi alisema, “Tungeliweza kuwabadilisha hali (maumbile) yao.” Abu Salih alisema, “Tungeliwageza

¹ At -Tabari 20:544.

² At -Tabari 20:545.

³ At -Tabari 20:547.

⁴ At -Tabari 20:547.

mawe." Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى na Qatadah رحمه الله تعالى walisema, "Tungeliwagandisha wakakalia miguu yao."¹

فَمَا اسْتَطَعُوا مُضِيًّا

"...basi wasingeweza kwenda..."

Yaani kwenda mbele.

وَلَا يَرْجِعُونَ ﴿٧٧﴾

"...wala kurudi."

Maana yake kusogea nyuma. Wangelibakia wameganda papo hapo, wakiwa hawana uwezo wa kuona mbele wala nyuma.

وَمَنْ نُعَمِّرْهُ نُنَكِّسْهُ فِي الْخَلْقِ أَفَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٧٨﴾ وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْبَغِي لَهُ إِنْ

هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْءَانٌ مُّبِينٌ ﴿٧٩﴾ لِيُنذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَيَحِقِّ الْقَوْلُ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٨٠﴾

68. Na Tunayemzeesha Tunamrudisha nyuma katika umbo. Basi je! hawazingatii?

69. Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala hayatakikani kwake hayo. Haukuwa huu ila ni ukumbusho na Qur'ani inayobainisha

70. Ili imwonye aliyehai, na neno litimie juu ya makafiri.

Allah تعالى Anasema kadiri mwanadamu anavyoishi ndiyo udhaifu unavyo-ongezeka mwilini mwake baada ya kuwa ni mwenye nguvu; anakuwa hajiwezi baada ya kuwa ni mwenye nishati. Hii aya inafanana na,

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ ضَعْفًا

وَشَيْبَةً ۗ خَلَقَ مَا يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴿٨١﴾

"Mwenyezi Mungu ndiye Aliyekuumbeni kutokana na udhaifu kisha Akajaalia nguvu baada ya unyonge, kisha Akajaalia baada

¹ At -Tabari 20:547.

ya nguvu unyonge tena na ukongwe. Anaumba Atakavyo. Naye Ndiye Mjuzi, Mwenye Uweza.” (30:54)

Na Anasema,

وَمِنْكُمْ مَّنْ يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِنْ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا

“...katika nyinyi wapo wanaorudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa, hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua.” (22:5)

Maana yake hapa “Allah Ndiye Mjuzi zaidi” ni kuwa Mola Anatuambia kuwa dunia ni ya mpito na kuna mwisho wake, si kitu cha milele. Allah تعالى Anasema,

أَفَلَا يَعْقِلُونَ

“Basi je! hawazingatii?”

Yaani, hawafikiri na kutumia akili zao jinsi gani walivyoumbwa (wachanga) kisha (wakakomaa) wakapata mvi, na baadaye kuwa wakongwe hawawezi kitu wala hawajiwezi; kwa hayo ili wapate kujitambua kuwa hapa duniani si mahali pa milele bali wao waliumbwa kwa ajili ya mahali pengine pa kudumu na hawana njia ya kupaepuka.

Allah تعالى Hakumfundisha Mtume Wake ﷺ Mashairi.

وَمَا عَلَّمْنَاهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْبَغِي لَهُ

“Wala hatukumfundisha (Muhammad) mashairi, wala hayatakikani kwake hayo.”

Allah تعالى Anasema kuwa hakumfundisha Mtume wake – Muhammad ﷺ mashairi,

وَمَا يَنْبَغِي لَهُ

“...wala hayatakikani kwake hayo.”

Yaani, hakuwa anajua kutunga shairi, wala kuyapenda wala hayakumvutia. Kuna riwaya inayoeleza kuwa Mtume ﷺ hakupata kuhifadhi hata mshororo mmoja wa shairi.

Bayhaqi ameleta riwaya ndani ya kitabu chake? *Ad-Dalail* inayoeleza kuwa Mtume ﷺ alimuambia Al-Abbas bin Mirdas As-Sulami akisema,

«أَنْتَ الْقَائِلُ: أَتَجْعَلُ نَهْيِي وَنَهْيَ الْعُبَيْدِ بَيْنَ الْأَقْرَعِ وَعَيْنَتَهُ»

“Wewe ndiye uliyesema, ‘Wagawa ngawira zangu na ngawira za watumishi miongoni mwa Al-Aqra’ na Uyainah”

Al-Abbas akasema, “Bali ni Uyainah na Al-Aqra.’ Mtume ﷺ akasema,

«الْكُلُّ سَوَاءٌ»

“Yote hayo ni sawa.”¹

Yaani katika maana; Rehema juu yake na Amani; *Allah A'lamu*. Hii ni kwa sababu Allah تعالى Alimfundisha Mtume wake Qur'an, ambayo ni,

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

“...*Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Msifiwa.*” (41:42)

Huu si ushairi kama majahili na makafiri wa Ki-Quraish walivyokuwa wakidai; na si mazing'aombwe, si uzushi wala uchawi kama wapotovu na makafiri wanavyodai. Mtume ﷺ alikuwa mbali na mashairi, na silka yake Mtume si kutunga mashairi kitabia na kisharia.

إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ وَقُرْءَانٌ مُّبِينٌ

“*Haukuwa huu ila ni ukumbusho na Qur'ani inayobainisha.*”

Yaani (Qur'an) iko wazi na inajieleza yenyewe kwa mwenye kuiangalia na kuitafakari huleta maana dhahiri kabisa. Kasema Allah تعالى,

لِيُنذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا

“*Ili imwonye aliye hai.*”

Yaani, ili Qu'an hii iliyo wazi impe onyo aliye hai hapa duniani. Inafanana na,

¹ *Dalail An-Nubuwwah* 5:181.

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

"...ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia." (6:19) pia

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالنَّارُ مَوْعِدُهُ

"...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao." (11:17)

Wale watakaofaidika na onyo hili ni wale ambao nyoyo zao ziko hai na zinapokea na kukubali mwongozo, kama alivyosema Qatadah, "Wako hai kati ya nyoyo zao na pia wako hai katika fikra zao."¹ Ad-Dhahaak alisema, "maana yake wale wenye busara."²

وَبِحَقِّ الْقَوْلِ عَلَى الْكَافِرِينَ

"...na neno litimie juu ya makafiri."

Na hiyo ni rahma kwa waumini na ni ushahidi dhidi ya makafiri.

أُولَئِكَ يَرَوْنَ أَنَا خَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَمًا فَهُمْ لَهَا مَلَائِكُونَ ﴿٧٦﴾ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ

فَمِنْهَا رَكُوعُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ ﴿٧٧﴾ وَهُمْ فِيهَا مَنَّاعٌ وَمَشَارِبٌ أَفْلا يَشْكُرُونَ ﴿٧٨﴾

71. Je! Hawaoni kwamba Tumewaumbia kutokana na iliyofanya mikono Yetu wanyama wa mifugo, na wao wakawa wenye kuwamiliki.

72. Na Sisi Tukawadhalilishia. Basi baadhi yao wako wanaowapanda, na baadhi yao wanawala.

73. Na wao wanapata kwao manufaa na vinywaji. Basi je, hawashukuru?

¹ At -Tabari 20:550

² At -Tabari 20:550

Kuna Alama za Utukufu wa Allah تعالی na Rahmah katika Wanyama

Allah تعالی Anataja Rahma na Neema Alizoziweka kwa ajili ya waja Wake kwa Kuifanya mifugo dhalili mbele yao ili wapate kuitumia.

فَهُمْ لَهَا مَلِكُونَ

“...na wao wakawa wenye kuwamiliki.”

Qatadah alisema, “Wanaimiliki mifugo, wao ndio mabwana.” Maana yake (Allah تعالی) Kawajalia uwezo wa kuwalainisha wanyama hao. Mifugo na wanyama hao wanakuwa watiifu kwa binadamu na wala hawaleti upinzani wala ujeuri; hata kijana mdogo anamuendea ngamia na kumuamuru apige magoti na pia akitaka anamuamuru kusimama tena na akamwongoza kokote atakako na Ngamia yule atafanya hayo bila kipingamizi. Na hata kama msafara huo una ngamia mia basi utaongozwa na kijana huyo mdogo.

فَمِنْهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ

“Basi baadhi yao wako wanaowapanda, na baadhi yao wanawala.”

Wanyama wengine, binadamu huwatumia kama vipando na wengine huwasheheneza mizigo wakakata masafa marefu na wakenda sehemu mbali mbali za karibu na mbali.

وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ

“...na baadhi yao wanawala.”

Maana yake wakitaka kufanya hivyo huwachinja na pia kutoa sadaqah katika ibada zao.

وَلَهُمْ فِيهَا مَنَافِعُ

“Na wao wanapata kwao manufaa...”

Yaani kutokana na sufi zao, hupata nguo, samani na vifaa mbali mbali vya matumizi yao kwa manufaa yao binadamu ya muda.

وَمَشَارِبٌ

“...na vinywaji...” Yaani, maziwa, na mkojo ambao hutumika kwa dawa n.k.

أَفَلَا يَشْكُرُونَ

“Basi je, hawashukuru?”

Maana: Je hawataki kumuabudu Allah تعالى ambaye Amewajalia neema na uwezo juu ya viumbe hivi. Anatumia neema hizo na fadhili hizo bila hata ya kugeuka nyuma na kutoa shukrani kwa hayo?

* * *

وَأَخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لَعَلَّهُمْ يُنصَرُونَ ﴿٧٤﴾ لَا
 يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَهُمْ وَهُمْ لَهُمْ جُنْدٌ مُحَضَّرُونَ ﴿٧٥﴾ فَلَا
 تَحْزُنكَ قَوْلُهُمْ إِنَّا نَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٦﴾
 أَوَلَمْ يَرِ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ إِذَا هُوَ حَصِيمٌ
 مُبِينٌ ﴿٧٧﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ط قَالَ مَنْ يُحْيِي
 الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ
 مَرَّةٍ ط وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ
 الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنْتُمْ مِنْهُ تُوقَدُونَ ﴿٨٠﴾ أَوَلَيْسَ
 الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ
 بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٨١﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ
 يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾ فَسُبْحَانَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ
 كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

وَأَخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لَعَلَّهُمْ
 يُنصَرُونَ ﴿٧٤﴾ لَا يَسْتَطِيعُونَ
 نَصْرَهُمْ وَهُمْ لَهُمْ جُنْدٌ مُحَضَّرُونَ ﴿٧٥﴾
 فَلَا تَحْزُنكَ قَوْلُهُمْ إِنَّا نَعْلَمُ مَا
 يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ﴿٧٦﴾

74. Na wameishika miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati wapate kusaidiwa!

75. Hawataweza kuwasaidia. Bali hao ndio watakuwa askari wao watakuo hudhurishwa.

76. Basi maneno yao yasi kuhuzunisha. Hakika Sisi Tunayajua wanayoyaweka siri na wanayoyatangaza.

Miungu ya Washirikina Haina Msaada Wowote wa Kuwasaidia

Allah تعالیٰ Anawakemea washirikina kwa kuyafanya masanamu miungu asiyekuwa Allah تعالیٰ kwa kutumaini kuwa yatawasaidia au kuwaruzuku au kuwakurubisha kwa Allah تعالیٰ. Allah تعالیٰ Anasema:

لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَهُمْ

“Hawataweza kuwasaidia.”

Maana: Hiyo miungu haiwezi kuwasaidia kwani ni dhaifu sana na si lolote wala chochote. Mbaya zaidi, hiyo miungu hata kujiondolea shida na haja zao yenyewe haiwezi, achilia mbali kuwasaidia wale wanaoviabudu. Miungu hiyo

haiwezi kufanya kisasi kwa wale wanaotaka kuidhuru, kwa sababu ni masanamu tu yasiyo uwezo wa kuelewa bali hata kusikia. Allah تعالیٰ Anasema:

وَهُمْ هُمْ جُنْدٌ مُّحْضَرُونَ

“Bali hao ndio watakuwa askari wao watakaohudhurishwa.”

Amesema Mujahid Siku ya hesabu (ya Qiyamah).¹ Maana yake ni kuwa ikifika miungu ya washirikina itakusanywa pamoja na itakuwepo wakati hao washirikina watakapoletwa kujibu makosa yao; na hii litawaongezea uchungu na huzuni na itakuwa ushahidi zaidi dhidi ya washirikina. Qatadah anasema:

لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَهُمْ

“Hawataweza kuwasaidia.”

Yaani hiyo miungu. Washirikina walikuwa na tabia ya kuchukia ili kuinusuru miungu yao duniani; lakini miungu hiyo haikuwasaidia chochote wala kuwaondolea mabalaa wala madhila na maudhi; achilia mbali kuwalinda na madhara yoyote, kwa sababu yalikuwa ni masanamu tu. Mwelekeo huu pia alikuwa nao Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى. Hii ni rai nzuri na alikuwa anaipendelea sana Ibn Jarir رحمه الله تعالى.

Faraja ya Allah تعالیٰ na Rahma Zake kwa Mtume ﷺ

فَلَا تَحْزُنْكَ قَوْلُهُمْ

“Basi maneno yao yasikuhuzunisha.”

Ina maana, “kukataa kwao ujumbe wako na pia kukufuru juu ya Allah تعالیٰ.”

إِنَّا نَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

“Hakika Sisi Tunayajua wanayoyaweka siri na wanayoyatangaza.”

Yaani, “Tunafahamu vitu vyote juu yao, na Tutawaadhibu kwa sababu ya madai yao ya uongo na Tutawafanyia hayo Siku ya Qiyamah; siku ambayo matendo

¹ At -Tabari 20:552.

yao yote madogo na makubwa, mazito na mepesi yataangaliwa moja moja, na hata kila kitu walichokifanya katika maisha yao yote duniani. Kila kitu kitakaguliwa.”

أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِن نُّطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٧٦﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا
وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٧﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ
وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٨﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنتُم مِّنْهُ
تُوقَدُونَ ﴿٧٩﴾

77. Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa mgomvi wa dhahiri!

78. Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakayeihusha mifupa nayo imekwisha oza na kumung'unyika?

79. Sema: Ataihusha huyo huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila aina ya Uumbaji.

80. Aliyekujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi mkawa kwa huo mnawasha.

Kukataa Kufufuliwa Baada ya Mauti na Kujibiwa kwao Madai hayo.

Mujahid, Ikrimah, Urwah bin Az-Zubair, As-Suddi na Qatadah walisema, “Ubbayy bin Khalaf (*Laanatullahi alaihi*) alikuja kwa Mtume ﷺ ameshika mfupa mkavu aliokuwa anausaga na kuwa mavumbi yaliyopeperuka hewani akasema, “Ewe Muhamad! Unadai kuwa Allah Atafufua haya yote?” Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ، يُبَيِّتُكَ اللَّهُ، ثُمَّ يُخَيِّبُكَ، ثُمَّ يُدْخِلُكَ جَهَنَّمَ»

“Naam, Allah Atakufisha wewe, na kisha Atakufufua na kukutupia ndani ya moto wa Jahanamu.”

Kisha aya hizi za Suratua Yasin zikateremshwa hadi mwisho wa Sura.

أَوَلَمْ يَرِ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ

“Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii?” Mpaka mwisho wake.¹

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Al-As bin Wail alichukua mfupa kutoka katika bonde na kisha akausagasaga mikononi mwake na kisha akamwambia Mtume ﷺ, “Je Allah Ataurejeshea uhai mfupa huu baada ya kusawajika hivi?” Mtume ﷺ akajibu.

«نَعَمْ، يُمِيتُكَ اللَّهُ، ثُمَّ يُحْيِيكَ، ثُمَّ يُدْخِلُكَ جَهَنَّمَ»

“Naam, Allah Atakufisha, kisha Atakurejeshea uhai, na kisha Atakufanya uingie moto wa Jahanamu.”

Kisha aya za mwisho wa *Surah Yasin* zikateremshwa. Habari hizi ziliandikwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutokana na mapokezi ya Said bin Jubayr.²

Aya ama zilishushwa kwa kusisitiza jibu kwa Ubbayy bin Khalaf au jibu kwa Al As bin Wail au wote, cha muhimu hapa ni kuwa kwa wote wawili jibu kamili linatosha, bali haliishi kwao wao tu, ni jibu kwa wote wanaokanusha uhai baada ya kifo na kuwepo Siku ya Kiama.

أَوَلَمْ يَرِ الْإِنْسَانُ

“Kwani mwanaadamu haoni...”

Hapa inajumuisha watu wote wanaokataa kufufuliwa na kusimama Qiyamah.

أَنَا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ

“...kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa mgomvi wa dhahiri!”

Maana: Yule anayekana kuwepo kufufuliwa hivi hajiulizi kuwa Aliyeanza Kuumba kitu kilichokuwa hakipo na kikawepo, kukirejesha umbo lake la asili

¹ At -Tabari 20:554.

² At -Tabari 20:554.

Kwake si kazi kubwa. Hakika Mola Alianza Kumuumba mtu kutokana na manii (maji maji yenye kudharaulika) kutoka kitu kisichokuwa na uzito; kilicho laini, dhaifu, chenye kudharaulika na akawa mtu (mbali kabisa na asili yake). Kama Anavyosema Allah تعالى،

أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِنْ مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٧٤﴾ فَجَعَلْنَاهُ فِي قَرَارٍ مَكِينٍ ﴿٧٥﴾ إِلَىٰ قَدَرٍ مَّعْلُومٍ ﴿٧٦﴾

“Kwani hatukukuumbeni kwa maji ya kudharauliwa? Kisha Tukayaweka mahali pa utulivu madhubuti? Mpaka muda maalumu?” (77-20-22)

إِنَّا خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ أَمْشَاجٍ

“Hakika Sisi Tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika...” (76:2)

Ina maana kutokana na mchanganyiko wa maji maji tofauti. Yule ambaye Aliweza Kumuumba mtu kutokana na hii “*Nutfah*” hawezi kushindwa kumrejeshea tena mwanadamu umbo lake baada ya kufa.

Ameandika Imam Ahmad katika Musnad, kuwa Bishir bin Jahhash رضي الله عنه alisema, “Siku moja Mtume ﷺ alitemea mate katika kiganja chake na akaweka kidole juu ya mate hayo, kisha akasema,

«قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: ابْنُ آدَمَ أَتَىٰ تُعْجِزِي وَوَقَدْ خَلَقْتِكُ مِنْ مِثْلِ هَدِيهِ، حَتَّىٰ إِذَا سَرَيْتُكَ وَعَدَلْتُكَ، مَشَيْتَ بَيْنَ بُرْدَيْكَ، وَلِلْأَرْضِ مِنْكَ وَنَيْدٌ، فَجَمَعْتَ وَمَنْعْتَ، حَتَّىٰ إِذَا بَلَغْتَ التَّرَافِي قُلْتَ: أَتَصَدَّقُ، وَأَتَىٰ أَوْ أُنُ الصَّدَقَةِ؟»

“Anasema Allah, utanikwepa namna gani wakati Nimekuumba kutokana na kitu kinachofanana na hiki, na nilipokupa umbo na nguvu unatembea na majoho yako juu ya ardhi, na ardhi nayo inatulia chini yako. Unalimbikiza mali na wala huzitumii mali hizo mpaka unapoona kifo kimekufika kooni ndipo unasema, “Nataka nitoe sadaqa.” Lakini umechelewa, wakati wa kutoa sadaqa.”¹

Habari hii pia iliandikwa na Ibn Majah.²

¹ Ahmad 4:210.

² Ibn Majah 2:903.

Anasema Allah تعالى،

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٤﴾

“Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakayeihisha mifupa nayo imekwisha oza na kumung’unyika?”

Yaani binadamu anafikiria kuwa ni muhali kwa Allah تعالى، ambaye Aliumba mbingu na ardhi Kuweza Kuwarejeshea uhai watu wakisha kufa na hata mifupa yao kukauka na kuoza. Anajisahau asili yake alikuwaje, anashindwa kuona kuwa Allah تعالى Alimuumba wakati hakuwa chochote akawa mtu. Na ili hali anajua kuwa vitu ambavyo ni zaidi yake, Allah تعالى Aliweza kuviumba. Anajua kwa kujiangalia mwenyewe kuwa kuna kilicho kikubwa kuliko yeye ambacho yeye anakikana na kudhani kuwa hilo haliwezekani. Allah تعالى Anasema:

قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٥﴾

“Sema: Ataihuisha huyo huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila aina ya uumbaji.”

Yaani, Anafahamu juu ya mifupa yote iliyopo kila mahali katika uso wa dunia, imekwenda wapi imesambaratika vipi na vipi hali zake.

Imam Ahmad aliandika kuwa Ribī alisema, “Uqbah bin Amri alisema alimuambia Hudhayfah رضي الله عنه، “Je unaweza kutuhabarisha yale uliyoyasikia kutoka kwa Mtume?” Akasema, “Nilimsikia akisema hivi:

«إِنَّ رَجُلًا حَضَرَ الْمَوْتَ، فَلَمَّا أَيْسَ مِنَ الْحَيَاةِ أَوْصَى أَهْلَهُ: إِذَا أَنَا مُتُّ فَاجْمَعُوا لِي حَطْبًا كَثِيرًا جَزَلًا، ثُمَّ أَوْقِدُوا فِيهِ نَارًا، حَتَّى إِذَا أَكَلْتُ لَحْمِي، وَخَلَصْتُ إِلَى عَظْمِي فَأَمْتِحْشْتُ، فَخُذُوهَا فَذَرُّوهَا فَذَرُّوهَا فِي النَّيْمِ، فَفَعَلُوا، فَجَمَعَهُ اللهُ تَعَالَى إِلَيْهِ، ثُمَّ قَالَ لَهُ: لِمَ فَعَلْتَ ذَلِكَ؟ قَالَ: مِنْ خَشْيَتِكَ، فَغَفَرَ اللهُ عَنِّي وَجَلَّ لَهُ»

“Mtu mmoja alipoona amekaribia kufa aliwaambia watu wake “Nikifa kusanyeni kuni nyingi kisha ichomeni maiti yangu mpaka (moto huo) utakapokula nyama ya mwili wangu na kufikia mifupa yangu na kuwa migumu (lakini myepesi kuvunjika), muichukue na kuisaga na muitupe mtoni.” Na ndivyo walivyofanya. Allah

*Alimkusanya na Akamuuliza, "Kwa nini umefanya hivyo?." Akajibu,
"Kwa sababu nilikuwa nikikuogopa wewe. Allah Alimsamehe."*

Uqbah bin Amri رضي الله عنه Alisema, "Na mimi nilimsikia Mtume ﷺ akisema hayo, na kuwa mtu huyo alikuwa mchimba makaburi."¹

Kuna mapokezi tofauti ya Hadithi hii, ambayo yamo katika vitabu vya Sahihi mbili. Riwaya moja inaeleza kuwa mtu huyo aliwaamuru watoto wake kumchoma kisha kusaga mwili uwe katika vipande vidogo vidogo na kisha nusu visambazwe nchi kavu na nusu nyingine isambazwe baharini siku yenye upepo mkali. Ndivyo walivyofanya, kisha Allah Aliamuru bahari kuvikusanya vipande vyake na pia ardhi iliamuriwa vivyo hivyo, kisha Allah تعالى Akamuamuru kwa kusema "Kuwa" yaani "Kun" na akawa mtu tena amesimama. Kisha Allah تعالى Akamuambia, "Wewe umefanya yote haya?" Akasema mtu yule, "Ni khofu juu yako, na Wewe Unajua zaidi. "Moja kwa moja Allah تعالى Alimsamehe mja Wake."²

الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنتُم مِّنْهُ تُوقَدُونَ ﴿٥٠﴾

***"Aliyekujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi
mkawa kwa huo mnawasha."***

Maana yake, Yule ambaye Alianza Kuumba mti huu kutokana na maji na sasa umekuwa kijani na unapendeza unazaa matunda, kisha Anaubadilisha na unakuwa mkavu na kuwa kuni ya kuwashia moto. Yeye anafanya lolote atakalo na Ana uwezo wa kufanya chochote atakacho na hakuna kitakachomzuia kwa hilo. Qaadah alisema juu ya Aya hii:

الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنتُم مِّنْهُ تُوقَدُونَ ﴿٥٠﴾

***"Aliyekujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi
mkawa kwa huo mnawasha."***

Inamaanisha kuwa Yule Aliyeleta moto kutokana na mti huu ana uwezo wa Kumfufua mfu. Ilikuwa inaashiria miti ya Marikh na Afar; inayopatikana Hijaz.

¹ Ahmad 5:395.

² Fat'h Al-Bari 6:594, Muslim 4:2110.

Kama mtu akitaka kuwasha moto na hana kibiriti basi anachukua matawi mawili ya miti hiyo na kuisugua, na mwishowe moto unatokea; hivyo ni kama kibiriti - Maneno haya yalipokelewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما

أُولَئِكَ الَّذِينَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ
 الْعَلِيمُ ﴿٥٦﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٧﴾ فَسُبْحَانَ الَّذِي
 بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٥٨﴾

81. Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye Ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi.

82. Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.

83. Basi Ametakasika Yule ambaye Mkononi Mwake umo Ufalme wa kila kitu; na Kwake Yeye mtarejeshwa.

Allah تعالی Anaashiria hapa kuwa kutokana na Nguvu na Uwezo Alionao Aliumba mbingu saba na nyota zake na sayari zake na ardhi saba na kila kila kitu kilichomo; na milima, michanga, bahari zake, nyika na miti yake, na kila kitu kati ya mbingu na ardhi. Anatueleza hayo ili tupate ushahidi na hoja kuwa ataweza kuihuisha miili yetu baada ya kufa kwetu kwa sababu hilo ni jepesi kulinganisha na uumbaji wa mbingu na ardhi. Na hii ni kama ayah

لَخَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu.” (40:57).

Kisha Kasema Allah تعالی ,,

أُولَئِكَ الَّذِينَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ

“Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi Kuwaumba mfano wao?”

Yaani mfano wa binadamu hivyo Atawahuisha hao binadamu kama Alivyowaumba hapo mwanzoni. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, Hii aya ni kama,

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزُبْ عَنْهُمُ جَبَلٌ مِّنْهُ يَخْلُقُهُمْ جِبَدًا مِّمَّا يَشَاءُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٣﴾

“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”
(46:33)

Allah تعالى Amesema hapa,

بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٣٣﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٣٤﴾

“Kwani! Naye ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.”

Yaani, Yeye Huamrisha kitu mara moja kinatokea wala hamna haja ya kurejea amri hiyo au kuthibitishwa. Allah Anapotaka jambo litokee basi Husema “Kuwa” mara moja na kitu hicho huwa.

Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَقُولُ: يَا عِبَادِي، كُلُّكُمْ مُذْنِبٌ إِلَّا مَنْ عَاقَبْتُ، فَاسْتَغْفِرُونِي أَعْفِرْ لَكُمْ، وَكُلُّكُمْ فَاقِرٌ إِلَّا مَنْ أَعْطَيْتُ، إِنِّي جَوَادٌ مَّاجِدٌ وَاجِدٌ أَفْعَلُ مَا أَشَاءُ، عَطَانِي كَلَامٌ، وَعَذَابِي كَلَامٌ، إِذَا أَرَدْتُ شَيْئًا فَإِنَّمَا أَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ»

“Allah Anasema,”Enyi Waja Wangu! Nyote ninyi ni watenda madhambi isipokuwa wale ambao Nimewahifadhi na madhambi. Basi niombeni maghufira Nitawasamehe. Nyote ninyi niwahitaji isipokuwa Niliyemtajirisha. Mimi ni Mkarimu wa Wakarimu, Mwenye Enzi na Nafanya lolote Nitakalo. Kipawa Changu ni Maneno na Adhabu Yangu ni Neno. Na Nikitaka jambo huliambia basi, “Kuwa” na linakuwa.”¹

¹ Ahmad 5:154.

فَسُبِّحْنَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٧٤﴾

“Basi Ametakasika Yule Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu; na Kwake Yeye mtarejeshwa.”

Yaani, Ametukuka Allah تعالى na Ametakasika na kila maovu, ambaye Yu Hai daima, Mwenye Kujitosheleza ambaye ndani ya Mikono Yake upo Ufalme wa mbingu na ardhi na Kwake vyote vitarejea. Yeye Ndiye Nuru ya Kuumba na Kuamuru, na Kwake watu wote watarejea Siku ya Qiyamah. Hapo Atamlipa kila mtu kwa mujibu wa amali yake. Na Yeye ni Muadilifu Mwenye Ukarimu na Fadhila. Na maana ya Kauli Yake Allah تعالى،

فَسُبِّحْنَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ

“Basi Ametakasika Yule Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu.”

Ni sawa na Aya،

قُلْ مَنْ بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ

“Sema: Ni nani Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu.” (23:88)

تَبْرَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمَلِكُ

“Ametukuka Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.” (67:1)

Al-Mulk na *Al-Malakut* ni lafudhi mbili zenye maana moja ingawa kuna baadhi ya watu wanayatenganisha kwa kusema *Al-Mulk* linamaanisha umiliki wa viwiliwili, na *Al-Malakut* linamaanisha umiliki wa roho. Na kauli ya kwanza ni yenye nguvu zaidi, na ndio mtazamo wa wafasiri wengi wa Qu’ani na ulamaa wengine.

Imam Ahmad aliandika kuwa Hudhayfah Al-Yaman رضي الله عنه alisema, “Usiku mmoja nilisimama kusali pamoja na Mtume ﷺ na akasoma sura saba ndefu katika rakaa saba. Alipoinuka kutoka kurukuu alisema،

«سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ»

“Allah Amemsikia aliyemhimidi.”

Kisha akasema:

«الْحَمْدُ لِلَّهِ ذِي الْمَلَكُوتِ وَالْجَبْرُوتِ وَالْكِبْرِيَاءِ وَالْعَظَمَةِ»

“Kuhimidiwa ni kwa Allah, Mwenye Ufalme, Ujabari, Mwenye Kibri na Ukubwa.”

Rukuu yake ilikuwa ndefu kama kisimamo chake na sujudu yake ilikuwa ndefu kama rukuu yake. Akamaliza Sala hiyo na miguu yangu ilikaribia kuvunjika.¹

Abu Dawud ameandika kuwa Awfi bin Malik Al-Ashjai رضي الله عنه alisema, “Nilisimama kusali na Mtume ﷺ usiku mmoja na alisoma Al-Baqarah. Hakuifikia Ayah inayotaja Rahma, bali alisita hapo na kuomba Rahma, na hakusoma ayah isemayo adhabu bali alisita hapo na kuomba hifadhi ya Allah تعالى kutokana na adhabu. Kisha alirukuu kwa muda mrefu kama alivyosimama, na akiwa amerukuu alisema,

«سُبْحَانَ ذِي الْجَبْرُوتِ وَالْمَلَكُوتِ وَالْكِبْرِيَاءِ وَالْعَظَمَةِ»

“Ametukuka Mwenye Ujabari, Ufalme, Kibri na Utukufu (Ukubwa).”

Kisha alisujudu kwa muda mrefu kama alivyorukuu na alisema kitu kama kile alichosema wakati wa kurukuu. Kisha alisimama na akasoma Al-Imran na kisha akasoma Sura moja baada ya nyengine.”² Hadithi hii pia iliandikwa na At-Tirmidhi katika mlango wa *Ash-Shamail* na An-Nasai.³

Huu ni mwisho wa *Tafsir* ya *Surah Yasin*. Shukrani zote zimwendee Allah تعالى.



¹ Ahmad 5:396.

² Abu Dawud 1:544.

³ *Shamail At-Tirmidhi* 164, An-Nasai 2:223.

Tafsiri ya Suratu As-Saffat

Sura ya 37

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za *Surat As-Saffat*

An-Nasa'i amemnukuu 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما, kuwa, "Mtume ﷺ alikuwa akituamuru kufupisha Sala zetu na alikuwa akisoma *As-Saffat* alipotuongoza katika Sala."¹ Haya yameandikwa na An-Nasa'i peke yake.



¹ An-Nasai 2:95.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ الصّٰفّٰتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَالصّٰفّٰتِ صَفًّا ﴿١﴾ فَالزّٰجِرَاتِ زَجْرًا ﴿٢﴾ فَالتّٰلِيٰتِ
 ذِكْرًا ﴿٣﴾ اِنَّ اِلٰهَكُمْ لَوٰحِدٌ ﴿٤﴾ رَبُّ السَّمٰوٰتِ
 وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَرَبُّ الْمَشْرِقِ ﴿٥﴾ اِنَّا زَيْنًا السَّمٰءِ
 الْاُدْنٰى بِرِيْنَةِ الْكَوٰكِبِ ﴿٦﴾ وَحِفْظًا مِّنْ كُلِّ شَيْطٰنٍ مَّارِدٍ
 ﴿٧﴾ لَا يَسْمَعُوْنَ اِلَى الْمَلٰٓئِكَةِ الْاَعْلٰى وَيُقَدّفُوْنَ مِنْ كُلِّ
 جَانِبٍ ﴿٨﴾ دُخُوْرًا وَّهُمْ عَدٰبٌ وَّاصِبٌ ﴿٩﴾ اِلَّا مَن
 حَطَفَ الْخَطْفَةَ فَاَتْبَعَهُ شِهَابٌ ثٰقِبٌ ﴿١٠﴾ فَاَسْتَفْتِمُ اَهُمْ
 اَشَدُّ خَلْقًا اَمْ مَن خَلَقْنَا اِنَّا خَلَقْنَهُمْ مِّنْ طِيْنٍ لَّا رِبِّ
 بَلْ عَجِبْتَ وَيَسْخَرُوْنَ ﴿١١﴾ وَاِذَا ذُكِرُوْا لَا يَذْكُرُوْنَ ﴿١٢﴾
 وَاِذَا رَاوْا آيَةً يَسْتَسْخَرُوْنَ ﴿١٣﴾ وَقَالُوْا اِنْ هٰذَا اِلَّا سِحْرٌ
 مُّبِيْنٌ ﴿١٤﴾ اِذًا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا اِءِنَّا لَمَتَّعُوْنُوْنَ
 ﴿١٥﴾ اَوْءَابَاوْنَا الْاَوْلُوْنَ ﴿١٦﴾ قُلْ نَعَمْ وَاَنْتُمْ دٰخِرُوْنَ ﴿١٧﴾
 فَاِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَّجِدَةٌ فَاِذَا هُمْ يَنْظُرُوْنَ ﴿١٨﴾

وَالصّٰفّٰتِ صَفًّا ﴿١﴾ فَالزّٰجِرَاتِ
 زَجْرًا ﴿٢﴾ فَالتّٰلِيٰتِ ذِكْرًا ﴿٣﴾
 اِنَّ اِلٰهَكُمْ لَوٰحِدٌ ﴿٤﴾ رَبُّ
 السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا
 وَرَبُّ الْمَشْرِقِ ﴿٥﴾

1. Naapa kwa wanao jipanga kwa safu.
2. Na kwa wenye kukataza mabaya.
3. Na kwa wenye kusoma Ukumbusho
4. Hakika Mungu Wenu bila ya shaka ni Mmoja.
5. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, na vilivyomo kati yao, na ni Mola Mlezi wa kila njia ambayo jua linachomoza.¹

Malaika Wanashuhudia Tawhid ya Allah تعالی

Imesimuliwa kuwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه, alisema:

¹ Al-Qurtubi (V.37:5)

وَالصَّافَّاتِ صَفًّا ﴿١٠﴾

“Naapa kwa wanaojipanga kwa safu.” Hao ni malaika;

فَالزَّاجِرَاتِ زَجْرًا ﴿١١﴾

“Na kwa wenye kukataza mabaya.”

Hao ni malaika;

فَالثَّلَاثِيتِ ذِكْرًا ﴿١٢﴾

“Na kwa wenye kusoma Ukumbusho.”

Hao ni malaika.¹ Hii ilikuwa pia rai ya Ibn ‘Abbas, Masruq, Sa’id bin Jubayr, ‘Ikrimah, Mujahid, As-Suddi, Qatadah na Ar-Rabi’ bin Anas.² Qatadah alisema, “Malaika hujipanga safu mbinguni.”³ Muslim amenukuu kuwa Hudhayfah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema:

«فُضِّلْنَا عَلَى النَّاسِ بِثَلَاثٍ: جُعِلَتْ صُفُوفُنَا كَصُفُوفِ الْمَلَائِكَةِ، وَجُعِلَتْ لَنَا الْأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدًا، وَجُعِلَ لَنَا تُرَابُهَا طَهُورًا، إِذَا لَمْ نَجِدِ الْمَاءَ»

“Tumefadhilishwa juu ya watu wengine kwa mambo matatu: safu zetu zimefanywa kama za malaika; ardhi yote imefanywa Masjid kwa ajili yetu; na mchanga wake umefanywa kitu cha kujitwahaarishia, pindi tunapoyakosa maji.”

Muslim, Abu Dawud, An-Nasa’i na Ibn Majah wamenukuu kuwa Jabir bin Samurah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema:

«أَلَا تَصْفُونَ كَمَا تَصِفُ الْمَلَائِكَةُ عِنْدَ رَبِّهِمْ؟»

“Je hamjipangi safu kama wajipangavyo malaika mbele ya Mola Wao Mlezi?”

Tukauliza, ‘Malaika wanajipangaje safu zao mbele ya Mola Wao Mlezi?’ Akajibu:

¹ At-Tabari 7:21.

² Al-Qurtubi 19:61-62.

³ At-Tabari 21:7.

⁴ Muslim 1:371.

«يُتِمُّونَ الصُّفُوفَ الْمُتَقَدِّمَةَ، وَيَتَرَاوُونَ فِي الصَّفِّ»

“Wanakamilisha safu za mbele na wanaunganisha safu.”¹

As-Suddi na wengine walisema kuwa Aya

﴿فَالزَّاجِرَاتِ زَجْرًا﴾

“Na kwa wenye kukataza mabaya.”

Yaani, wanaendesha mawingu.

﴿فَالسَّائِبَاتِ ذِكْرًا﴾

“Na kwa wenye kusoma Ukumbusho.”

As-Suddi alisema, “Malaika huwaletea wanadamu Vitabu Vitukufu na Qur’an kutoka kwa Allah تعالى.”

Allah تعالى Ndiye Pekee Anayestahiki Kuabudiwa kwa Haki

﴿إِنَّ إِلَهَهُمْ لَوَاحِدٌ﴾ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Hakika Mungu Wenu bila ya shaka ni Mmoja. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi...”

Huyu Ndiye Ambaye kiapo kinaelekezwa Kwake, kwa kusema kuwa hakuna mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye, Mola Mlezi wa mbingu na ardhi,

﴿وَمَا بَيْنَهُمَا﴾

“...na yaliyomo kati yao...” Yaani, viumbe.

﴿وَرَبُّ الْمَشْرِقِ﴾

“...na ni Mola Mlezi wa kila njia ambayo jua linachomoza.”

Yaani, Yeye ni Mmiliki Anayedhibiti viumbe Wake kwa kutiisha na vilivyomo humo kama vile nyota, sayari na viumbe vya angani vyenye kujitokeza upande wa mashariki na kuzama upande wa magharibi. Kutajwa mashariki kunatosha

¹ Muslim 1:223, Abu Dawud 1:431, An-Nasai 2:92, Ibn Majah 1:317

na hakuna haja ya kutajwa na magharibi pia, kwa sababu imeashiriwa na yaliyosemwa. Hayo yalishaelezwa wazi sehemu nyingine, katika Aya,

﴿فَلَا أُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ إِنَّا لَقَدِرُونَ﴾

“Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mashariki na magharibi kwamba Sisi Tunaweza.” (70:40)

﴿رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ﴾

“Mola Mlezi wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.” (55:17)

Inayorejea kwenye vituo vya mawio na machweo ya jua na mwezi wakati wa majira ya kusi na kaskazi.

﴿إِنَّا زَيْنَا أَلْسَمَاءَ أَلدُّنْيَا بَرِيَّةَ الْكَوَاكِبِ﴾ ﴿وَحِفْظًا مِّنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَّارِدٍ﴾ ﴿لَّا يَسْمَعُونَ إِلَى الْمَلَأِ الْأَعْلَىٰ وَيُقَذَّفُونَ مِنْ كُلِّ جَانِبٍ﴾ ﴿دُحُورًا ۗ وَهُمْ عَذَابٌ وَأَصِيبٌ﴾ ﴿إِلَّا مَن حَظِيَ الْحُطْفَةَ فَأَتْبَعَهُ شِهَابٌ ثَاقِبٌ﴾

6. Hakika Sisi Tumeipamba mbingu ya karibu kwa pambo la nyota.

7. Na kuilinda na kila shetani asi.

8. Wasiweze kuwasikiliza viumbe watukufu. Na wanafukuzwa huko kila upande.

9. Wakifurushwa. Na wanayo adhabu ya kudumu.

10. Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo, na mara humfatia kimondo kinachong'ara.

Upambaji wa Mbingu na Kuzihifadhi Kwake Hutoka kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Anatuambia kuwa Ameipamba mbingu ya chini kwa ajili ya wakazi wa ardhini wenye kuitazama. Nyota na sayari angani huwapa mwangaza wakazi wa ardhini, sawa na Kauli ya Allah تعالى:

﴿وَلَقَدْ زَيْنَا أَلْسَمَاءَ أَلدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ وَجَعَلْنَاهَا رُجُومًا لِلشَّيْطَانِ ۗ وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابٌ

﴿السَّعِيرِ﴾

“Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapigia mashetani, na Tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao kwa nguvu.” (67:5),

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَرَبُّنَهَا لِلنَّظِيرِينَ ﴿٦٧﴾ وَحَفِظْنَاهَا مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ رَجِيمٍ ﴿٦٨﴾ إِلَّا مَنْ أَسْرَقَ أَلْسَمَعُ فَأَتْبَعُهُ شِهَابٌ مُبِينٌ ﴿٦٩﴾

‘Na hakika Tumeweka katika mbingu vituo vya sayari, na Tumezipamba kwa wenye kuangalia. Na Tumezilinda na kila shetani afukuzwaye. Isipo kuwa mwenye kusikiliza kwa kuibia, naye hufuatwa na kijinga cha moto kinachoonekana.’ (15:16-18).

Na hapa Allah تعالى Anasema:

وَحَفِظًا

“Na kulinda...” Maana yake, kuihifadhi ipasavyo,

مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ مَّارِدٍ

“...na kila shetani asi.” Maana, kila shetani fidhuli, anapotaka kudukiza (habari za mbinguni), moto wenye kuchoma huja na kumuunguza. Allah تعالى Amesema:

لَا يَسْمَعُونَ إِلَى آلَمًا إِلَّا أَعْلَىٰ

“Wasiweze kuwasikiliza viumbe watukufu.”

Maana yake, hawataweza kulifikia kundi la juu zaidi – yaani mbingu ambayo Malaika wapo humo – wanapozungumzia sheria na amri zinazoshuka za Allah. Tumeshaeleza hili katika maelezo ya Hadithi zilizonukuliwa katika kuzungumzia Aya,

حَتَّىٰ إِذَا فُزِعَ عَنْ قُلُوبِهِمْ قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ ط قَالُوا الْحَقُّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٣٤﴾

“Hata itapoondolewa hofu kwenye nyoyo zao watasema: Mola Wenu Mlezi kasema nini? Watasema: Yaliyo kweli! Na Yeye Ndiye Aliye juu, Mkubwa.” (34:23).

Kauli ya Allah تعالى:

وَيُقَدِّفُونَ

“Na wanafukuzwa huko...” Yaani, wanapigwa,

مِن كُلِّ جَانِبٍ

“...*kila upande...*” Yaani, pande zote wanazojaribu kutumia ili kufka mbinguni.

دُحُورًا

“*Wakifurushwa...*” Yaani, wanakataliwa, na wanafukuzwa na kuzuiwa kuifikia, na wanapigwa.

وَهُمْ عَذَابٌ وَاصِبٌ

“*Na wanayo adhabu ya kudumu.*” Yaani, huko Akhera, watapata adhabu ya daima na inayoumiza, sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَأَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابَ أَلْسَعِيرٍ

“...*na Tumewaandalia adhabu ya Moto uwakao kwa nguvu.*” (67:5).

إِلَّا مَن خَطِئَ الْخَطِيئَةَ

“*Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo...*”

Yaani, isipokuwa kwa mmojawapo katika *Shayatin* anayemudu kupata jambo, ambalo ni neno analolisikia mbinguni. Basi humrushia wa chini yake, ambaye naye humrushia wa chini yake. Huenda kimondo kitampiga kabla hajaweza kumpasha wa chini yake – kwa kudura za Allah تعالى – kabla ya kupigwa na kimondo na kumuunguza. Hivyo, shetani mwingine humpelekea mtabiri, kama tulivyokwishaona katika Hadith. Kauli ya Allah تعالى:

إِلَّا مَن خَطِئَ الْخَطِيئَةَ فَاتَّبَعَهُ شِهَابٌ ثَائِبٌ ﴿٦٧﴾

“*Isipokuwa anayenyakua kitu kidogo, na mara humfwatia kimondo kinachong’ara.*”

Yaani, chenye kung’aa. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mashetani walikuwa na sehemu ambapo walikaa mbinguni ili kusikiliza kilichoteremshwa na Allah تعالى. Nyota hazikusogea na *mashetani* hawakupigwa. Waliposikia wahyi, walikuwa wakishuka ardhini na kwa kila neno moja, waliongeza mengine tisa ya kwao wenyewe. Mtume ﷺ alipotumwa, Shetani alitaka kuketi mbinguni, kimondo kilikuja na hakikumkosa; kilikuwa kikimuunguza kila mara. Wakapeleka malalamiko kwa Iblis, Allah تعالى

Amlaani, na akawaambia, 'Lazima kuna jambo limetokea.' Alituma vikosi vyake na vikamkuta Mtume ﷺ akiwa amesimama baina ya milima miwili katika bonde la Nakhlah." - "Wakarudi kwa Iblis na kumueleza hayo, na akasema, 'Hicho ndicho kilichotokea.'"¹

فَأَسْتَفْتِهِمْ أَهُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمْ مَنِ خَلَقْنَا إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِنْ طِينٍ لَازِبٍ ﴿١١﴾ بَلْ عَجِبْتَ
 وَدَسَخُرُونَ ﴿١٢﴾ وَإِذَا دُكِّرُوا لَا يَذْكُرُونَ ﴿١٣﴾ وَإِذَا رَأَوْا آيَةً يَسْتَسْخِرُونَ ﴿١٤﴾ وَقَالُوا إِن
 هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿١٥﴾ أَعْيَا أَبَاؤُنَا أَمْ إِنَّا لَمَبْعُوثُونَ ﴿١٦﴾ أَوْءَابَاؤُنَا
 الْآلُؤُونَ ﴿١٧﴾ فَلَنْ نَعْمَ وَأَنْتُمْ دَاخِرُونَ ﴿١٨﴾ فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ فَإِذَا هُمْ يَنْظُرُونَ ﴿١٩﴾

11. Hebu waulize: Je! Wao ni wenye umbo gumu zaidi au hao wengine Tuliwaumba. Hakika Sisi Tuliwaumba wao kwa udongo unaonata.

12. Bali unastaajabu, na wao wanafanya masikhara.

13. Na wanapokumbushwa hawakumbuki.

14. Na wanapoona Ishara, wanafanya masikhara.

15. Na husema: Haya si chochote ila ni uchawi tu uliodhahiri.

16. Ati tukishakufa na tukawa udongo na mifupa ndio kweli tutafufuliwa?

17. Hata baba zetu wa zamani?

18. Sema: Ndio! Hali nanyi ni madhalili.

19. Huko utapigwa ukelele mmoja tu! Na hapo ndio wataona!

Uhakika wa Uhai Baada ya Mauti

Allah تعالى Anasema: 'Waulize wenye kupinga ufufuo, kipi ni kigumu zaidi kuumba, wao ndio vigumu kuwaumba au mbingu, ardhi, malaika, mashetani, viumbe wakubwa – kila kilicho baina yake.' Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema kuwa walikiri kuwa vitu hivyo vilikuwa vigumu zaidi kuumbwa kuliko wao.²

¹ At-Tabari 12:21.

² At-Tabari 19:21.

Kama hivyo ndivyo, basi kwanini wanakanusha ufufuo, wanapoonu vitu vikubwa zaidi ya hivyo wanavyovikanusha? Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَئِنْ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾

“Bila ya shaka kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.” (40:57)

Kisha Allah تعالى Anaeleza kuwa waliumbwa kutokana na kitu dhaifu, Aliposema:

إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِنْ طِينٍ لَازِبٍ

“Hakika Sisi Tuliwaumba wao kwa udongo unaonata.”

Mujahid, Sa'id bin Jubayr na Adh-Dhahhak walisema, “Ni namna ya udongo mzuri wenye kunatana wenyewe kwa wenyewe.”¹ Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, na 'Ikrimah walisema, “Unanata na mzuri.” Qatadah alisema, “Ni unaonata mkononi.”

بَلْ عَجِبْتَ وَيَسْخَرُونَ ﴿٥٨﴾

“Bali unastaajabu, na wao wanafanya maskhara.”

Yaani, 'unastaajabu, ewe Muhammad, juu ya watu hawa wanaopinga ufufuo ilhali una uhakika kuwa hilo ni kweli, walipokufuru yale uliyoambiwa na Allah kuhusu jambo hili la kustaajibisha, ambalo ni kurejea upya viwiliwili vyao baada ya kuoza. Wanapinga unachosema kwa sababu ya kufuru yao kubwa na kufanyia masikhara unachowaambia kuhusu hilo.' Qatadah alisema, “Muhammad ﷺ alishangazwa na masikhara ya wapotevu miongoni mwa wana wa Adam.”³

وَإِذَا رَأَوْا آيَةً

“Na wanapoonu Ishara...” Yaani, ushahidi wao,

يَسْتَسْخَرُونَ

“...wanafanya masikhara.”

Mujahid na Qatadah walisema, “Wanafanyia masikhara.”³

¹ Al-Qurtubi 69:15, At-Tabari 21:22.

² At-Tabari 23:21.

³ At-Tabari 24:23.

وَقَالُوا إِن هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٣٧﴾

“...Na husema: Haya si chochote ila ni uchawi tu ulio dhahiri.”

Yaani, ‘Ulicholeta ni uchawi wa waziwazi.’

أَعِدَّا مَتَنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَعِنَّا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٣٨﴾ أَوْءَابَاؤُنَا الْأَوْلُونَ ﴿٣٩﴾

“Ati tukishakufa na tukawa udongo na mifupa ndio kweli tutafufuliwa? Hata baba zetu wa zamani?”

Walidhani kuwa hayo hayawezekani, na hawa kuamini.

قُلْ نَعَمْ وَأَنْتُمْ دَاخِرُونَ ﴿٤٠﴾

“Sema: Naam! Hali nanyi ni madhalili.”

Yaani, ‘Waambie, ewe Muhammad: “Ndiyo, mtafufuliwa Siku ya Kiama, baada ya kugeuka vumbi na mifupa, na mtadhalilika,’ Yaani, kuaibika mbele Yake. Ni sawa na Aya:

وَكُلُّ أُمَّتٍ دَاخِرِينَ

“Na wote watamfikia nao ni wanyonge.” (27:87), na

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhhalilike.” (40:60)

Kisha Allah تعالى Anasema:

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ فَإِذَا هُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٤١﴾

“Huko utapigwa ukelele mmoja tu! Na hapo ndio wataona!”

Yaani, itakuwa amri moja kutoka kwa Allah تعالى, Atawaita mara moja watoke ardhini, halafu watakuwa wamesimama mbele Yake, wakiangalia kitisho cha Siku ya Kiama. Allah تعالى Anajua zaidi.

وَقَالُوا يَبُولْنَا هَذَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿٢٠﴾ هَذَا يَوْمَ الْفَصْلِ
 الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢١﴾ * أَحْشَرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا
 وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٢٢﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَاهْدُوهُمْ
 إِلَى صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٣﴾ وَقَفُوهُمْ^ط إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ ﴿٢٤﴾ مَا
 لَكُمْ لَا تَتَّصِرُونَ ﴿٢٥﴾ بَلْ هُمْ الْيَوْمَ مُسْتَسْلِمُونَ ﴿٢٦﴾
 وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٧﴾ قَالُوا إِنَّا كُنَّا
 كُنْتُمْ تَأْتُونَنَا عَنِ الْيَمِينِ ﴿٢٨﴾ قَالُوا بَلْ لَمْ تَكُونُوا
 مُؤْمِنِينَ ﴿٢٩﴾ وَمَا كَانَ لَنَا عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطَانٍ^ط بَلْ كُنْتُمْ
 قَوْمًا طَٰغِينَ ﴿٣٠﴾ فَحَقَّ عَلَيْنَا قَوْلُ رَبِّنَا^ط إِنَّا لَذَائِقُونَ ﴿٣١﴾
 فَأَعْوَيْنَكُمْ إِنَّا كُنَّا عٰوِينَ ﴿٣٢﴾ فَأَيُّهُمْ يَوْمَئِذٍ فِي الْعَذَابِ
 مُشْتَرِكُونَ ﴿٣٣﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِينَ ﴿٣٤﴾ إِنَّهُمْ
 كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٣٥﴾
 وَيَقُولُونَ أَيُّنَا لَتَارِكُوآءِ الْهَيْتِنَا لِشَاعِرٍ مَجْنُونٍ ﴿٣٦﴾ بَلْ
 جَاءَ بِالْحَقِّ وَصَدَّقَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٧﴾ إِنَّكُمْ لَذَائِقُوا الْعَذَابِ
 الْأَلِيمِ ﴿٣٨﴾ وَمَا تَحْزَنُونَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا
 عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٠﴾ أُولَٰئِكَ هُمْ رِزْقُ مَعْلُومٍ ﴿٤١﴾
 فَوَٰكِهِ^ط وَهُمْ مُكْرَمُونَ ﴿٤٢﴾ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٤٣﴾ عَلَى
 سُرُرٍ مُتَقَابِلِينَ ﴿٤٤﴾ يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِكَأْسٍ مِنْ مَعِينٍ ﴿٤٥﴾
 بَيْضَاءَ لَذَّةٍ لِلشَّٰرِبِينَ ﴿٤٦﴾ لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا
 يُنزَفُونَ ﴿٤٧﴾ وَعِنْدَهُمْ قَاصِرَاتُ الطَّرْفِ عِينٌ ﴿٤٨﴾
 كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَكْنُونٌ ﴿٤٩﴾

وَقَالُوا يَبُولْنَا هَذَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿٢٠﴾
 هَذَا يَوْمَ الْفَصْلِ الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ
 تُكَذِّبُونَ ﴿٢١﴾ * أَحْشَرُوا الَّذِينَ
 ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ
 مِنْ دُونِ اللَّهِ فَاهْدُوهُمْ إِلَى
 صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٣﴾ وَقَفُوهُمْ^ط إِنَّهُمْ
 مَسْئُولُونَ ﴿٢٤﴾ مَا لَكُمْ لَا تَتَّصِرُونَ
 ﴿٢٥﴾ بَلْ هُمْ الْيَوْمَ مُسْتَسْلِمُونَ ﴿٢٦﴾

20. Watasema: Ole wetu!
Hii ndiyo Siku ya Malipo.

21. Hii ndiyo Siku ya Hukumu
mliyokuwa mkiikadhibisha.

22. Wakusanyeni waliodhulu-
lumu, na wake zao, na hao
waliokuwa wakiwaabudu.

23. Badala ya Mwenyezi
Mungu. Waongozeni njia ya
Jahannamu!

24. Na wasimamisheni.
Hakika hao wataulizwa:

25. Mna nini? Mbona
hamsaidiani?

26. Bali hii leo, watasalimu
amri.

Vitisho vya Siku ya Malipo

Allah تعالى Anatuambia watakachosema makafiri Siku ya Kiama, jinsi watakavyojilaumu na kukiri kuwa walijidhulumu duniani. Watakapoona vitisho vya Siku ya Kiama kwa macho yao wenyewe, watajuta sana lakini kwa wakati huo majuto hayatawasaidia chochote.

وَقَالُوا يَا وَيْلَنَا هَذَا يَوْمُ الَّذِينَ

“Hii ndiyo Siku ya Hukumu mliyokuwa mkiikadhibisha.”

Yatasemwa hayo kwa kuwakaripia. Allah تعالى Atawaamuru malaika kuwatenganisha makafiri na waumini katika mahali watakaposimama. Kauli ya Allah تعالى:

أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

“Wakusanyeni waliodhulumu, na wake zao...”

An-Nu'man bin Bashir alisema, “Wake zao ni wale walio kama wao.”¹ Hii ilikuwa pia rai ya Ibn ‘Abbas, Sa’id bin Jubayr, ‘Ikrimah, Mujahid, As-Suddi, Abu Salih, Abu Al-‘Aliyah na Zayd bin Aslam.”² Sharik, akisimulia kutoka kwa Simak, kutoka kwa An-Nu'man, amesema: “Nilimsikia ‘Umar رضي الله عنه akisema:

أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

“Wakusanyeni waliodhulumu, na wake zao...”

Yaani, ‘Walio kama wao. Hivyo, waliofanya uchafu wa *Zinaa* watakusanywa pamoja na wengine waliofanya *Zinaa*, walioshughulika na *Riba* watakusanywa pamoja na waliojishughulisha na *Riba*, waliotumia ulevi watakasanywa na wengine waliotumia ulevi.’ Mujahid na Sa’id bin Jubayr alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما:

وَأَزْوَاجَهُمْ

“...na wake zao...”

Yaani, marafiki zao.

¹ At-Tabari 21:27.

² At-Tabari 21:27, 28.

وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“...na hao waliokuwa wakiwaabudu. Badala ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, badala ya Allah. Yaani, masanamu na miungu yao bandia itakusanywa pamoja nao katika sehemu moja. Na Kauli Yake Allah تعالى،

فَأَهْدُوهُمْ إِلَىٰ صِرَاطِ الْجَحِيمِ

“Waongozeni njia ya Jahannamu!”

Yaani, wapelekeni Jahanamu. Ni sawa na:

وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمِيَٰ وَنُكَمَا وَصُمًا ۖ مَا وَلَّهُمْ جَهَنَّمَ كَلِمًا خَبِثَ

زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا ﴿٣٧﴾

“Na Tutawakusanya Siku ya Kiyama hali wakikokotwa juu ya nyuso zao, nao ni vipofu na mabubu na viziwi. Na makaazi yao ni Jahannamu. Kila moto ukifanya kusinzia tutazidi kuchochea uwake kwa nguvu.” (17:97).

وَقَفُوهُمْ ۖ إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ ﴿٣٨﴾

“Na wasimamisheni. Hakika hao wataulizwa.”

Yaani, wasimamisheni ili wahojiwe juu ya yale waliyoyafanya na kusema duniani. Kama alivyosema Adh-Dhahhak, akisimulia kutoka kwa Ibn `Abbas, maana hii, `wazuieni, ili waletwe kuhojiwa. `Abdullah bin Al-Mubarak alisema, “Nilimsikia `Uthman bin Za`idah akisema, `Jambo la kwanza atakaloulizwa mtu, ni kuhusu washirika wake. Halafu kwa namna ya karipio, wataambiwa:

مَا لَكُمْ لَا تَنَاصَرُونَ ﴿٣٩﴾

“Mna nini? Mbona hamsaidiani?” Yaani, ‘kama mlivyodai kuwa mngesaidiana.’

بَلْ هُمْ الْيَوْمَ مُسْتَسْلِمُونَ ﴿٤٠﴾

“Bali siku hiyo, watasalimu amri.” Yaani, watafikiwa na amri ya Allah تعالى، na hawataweza kuikataa wala kuikwepa. Allah تعالى Anajua zaidi.

وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٠﴾ قَالُوا إِنَّكُمْ كُنْتُمْ تَأْتُونَنَا عَنِ الْيَمِينِ ﴿٢١﴾
 قَالُوا بَلْ لَمْ تَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٢٢﴾ وَمَا كَانَ لَنَا عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ ۖ بَلْ كُنْتُمْ قَوْمًا طٰغِينَ
 ﴿٢٣﴾ فَحَقَّ عَلَيْنَا قَوْلُ رَبِّنَا ۖ إِنَّا لَذٰبِقُونَ ﴿٢٤﴾ فَأَغْوَيْنَاكُمْ إِنَّا كُنَّا غٰوِينَ ﴿٢٥﴾ فَلِئِهِمْ
 يَوْمَئِذٍ فِي الْعَذَابِ مُشْتَرِكُونَ ﴿٢٦﴾ إِنَّا كَذٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِينَ ﴿٢٧﴾ إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا
 قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٨﴾ وَيَقُولُونَ أَيٰنَا لَتَارِكُوآءِ الْهَيْتِنَا لِشَاعِرٍ مَّجْنُونٍ
 ﴿٢٩﴾ بَلْ جَاءَ بِالْحَقِّ وَصَدَقَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٠﴾

27. Watakabiliana wao kwa wao kuulizana.

28. Watasema: Kwa hakika nyinyi mlikuwa mkitujia upande wa kulia.

29. Watasema (wakubwa): Bali nyinyi wenyewe hamkuwa Waumini.

30. Sisi hatukuwa na mamlaka juu yenu, bali nyinyi wenyewe mlikuwa wapotovu.

31. Basi hukumu ya Mola Wetu Mlezi imekwisha tuthibitikia. Hakika bila ya shaka tutaonja (tu adhabu).

32. Tulikupotezeni kwa sababu sisi wenyewe tulikuwa wapotovu.

33. Basi kwa hakika siku hiyo watashirikiana katika adhabu.

34. Hivyo ndivyo tutakavyowafanyia wakosefu.

35. Wao walipokuwa wakiambiwa Hapana Mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna kwa kiburi.

36. Na wakisema: Hivyo sisi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu?

37. Bali huyu amekuja kwa Haki, na amewasadikisha Mitume.

Mabishano ya Washirikina Siku ya Kiama

Allah تعالی Anatuambia kuwa makafiri watalaumiana katika uwanja wa Kiama, kama watakavyogombana katika daraja za Jahanamu:

وَإِذْ يَتَحَاوَرُونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعْفَتَا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ
 أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا
 إِنَّ اللَّهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٨﴾

“Na watapohojiana huko Motoni, wanyonge watawaambia waliojitukuza: Hakika sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, hamtuondolei sehemu ya huu Moto? Watasema waliojitukuza: Hakika sote sisi tumo humo humo! Kwani Mwenyezi Mungu kesho hukumu baina ya waja!” (40:47-48)

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِندَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلَ يَقُولُ
 الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٤٩﴾ قَالَ الَّذِينَ
 اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوا أَلَمْ نَكُنْ صَدَقْتُنَّكُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ^ط بَلْ كُنْتُمْ
 مُجْرِمِينَ ﴿٥٠﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا
 أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُمْ أَدْدَاةً وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَعْلَالُ فِي
 أَعْنَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٥١﴾

“...Na ungelikiwaona madhaalimu wataposimamishwa mbele ya Mola Wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia waliotakabari: Lau kuwa si nyinyi, bila ya shaka tungelikuwa Waumini sisi. Waliotakabari watawaambia wanyonge: Kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu. Na wanyonge wakawaambia waliotakabari: Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu,

na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu. Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliyokuwa wakiyatenda?" (34:31-33)

Kadhalika, wameelezewa hapa kwa kusema:

إِنَّكُمْ كُنْتُمْ تَأْتُونَنَا عَنِ الْيَمِينِ

"Watasema: Kwa hakika nyinyi mlikuwa mkitujia upande wa kulia."

Adh-Dhahhak alisimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema; "Watasema, 'Mlikuwa mkitushurutisha kwa sababu ya nafasi yenu juu yetu, kwa kuwa tulikuwa wanyonge na nyinyi wenye nguvu.'" Qatadah alisema, "Wanadamu watawaambia Majini, 'Mlikuwa mkitujia kutokea upande wa kuume ili kuzuia amali zote njema, na mlituambia tusiifanye na mkatuwekea vikwazo katika njia zetu.'" As-Suddi alisema, "'Mlikuwa mkitujia ili kuzuia ukweli, na mlifanya upotovu upendeze kwetu, na mlituzuia tusiuone ukweli.'"¹ Ibn Zayd alisema, maana yake: "Mlisimama baina yetu na heri, na mlituweka mbali na Uislamu na imani na kufanya amali njema tulizoamrisha kuzifanya."² Yazid Ar-Rishk alisema, "kwa upande wa *La ilaha illallah*."

قَالُوا بَلْ لَمْ تَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

"Watasema (wakubwa): Bali nyinyi wenyewe hamkuwa Waumini."

Viongozi wa Majini na wanadamu watawaambia wafuasi wao, "Si kama mnavyosema; bali nyoyo zenu zilikataa imani na zikakubali ukafiri na dhambi."

وَمَا كَانَ لَنَا عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطٰنٍ

"Sisi hatukuwa na mamlaka juu yenu..."

Yaani, 'hatukuwa na ushahidi wa ukweli wa yale tuliokuitieni kwayo.'

¹ At-Tabari 21:32 Isnadi yake haijaswihi, Dhahaak hajamsikia Ibn Abbasi.

² At-Tabari 21:32.

بَلْ كُنْتُمْ قَوْمًا طَٰغِيْنَ

“...bali nyinyi wenyewe mlikuwa wapotovu.”

‘Nyinyi wenyewe mlikuwa waovu na manaokiuka mipaka dhidi ya ukweli, hivyo mkatuitikia na kuuacha ukweli walioleta Mitume pamoja na ushahidi, na mkaukengeuka.’

فَحَقَّ عَلَيْنَا قَوْلُ رَبِّنَا إِنَّا لَذَٰبِقُونَ ﴿٣٧﴾ فَأَعْوَيْنَكُمْ إِنَّا كُنَّا غٰوِيْنَ ﴿٣٨﴾

“Basi hukumu ya Mola Wetu Mlezi imekwisha tuthibitikia. Hakika bila ya shaka tutaonja tu adhabu. Tulikupotezeni kwa sababu sisi wenyewe tulikuwa wapotovu.”

Waliokuwa jeuri watawaambia waliokuwa wanyonge, ‘Neno la Allah تعالى limethibiti kwetu, kuwa sisi ni katika wenye kuonja adhabu katika Siku ya Kiama.’

فَأَعْوَيْنَكُمْ

“Tulikupotezeni...” Yaani, ‘hivyo, tukakuiteni kwenye upotevu,’

إِنَّا كُنَّا غٰوِيْنَ

“...kwa sababu sisi wenyewe tulikuwa wapotovu.”

Yaani, ‘tulikuiteni mfuata njia yetu, na mkaja.’ Kauli ya Allah تعالى:

فَلِيَّهِمْ يَوْمَئِذٍ فِي الْعَذَابِ مُشْتَرِكُونَ ﴿٣٩﴾

“Basi kwa hakika siku hiyo watashirikiana katika adhabu.”

Yaani, wote wataingia katika Jahanamu, kila mmoja kulingana na anachostahiki.

إِنَّا كَذٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِيْنَ ﴿٤٠﴾ اِيَّهَمْ كَانُوْا

“Hivyo ndivyo Tutakavyowafanyia wakosefu. Wao walipokuwa...”

Kwa maana, hapa duniani,

إِذَا قِيْلَ لَهُمْ لَا إِلٰهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٤١﴾

“...wakiambiwa hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna kwa kiburi.”

Yaani, duniani walikuwa jeuri sana kutamka maneno hayo kama waumini wanavyowaambia wao. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَمِرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَقُولُوا: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَمَنْ قَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَقَدْ غَضَمَ مِنِّي مَالَهُ وَنَفْسَهُ إِلَّا بِحَقِّهِ، وَحِسَابُهُ عَلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Nimeamrisha niwapige watu mpaka waseme La ilaha ill-Allah. Mwenye kusema La ilaha illallah, imesalimika kwangu mali yake na nafsi yake, isipokuwa kwa haki yake, na hesabu yake itakuwa kwa Allah, Mtukuka.”¹

Allah تعالى Alishusha katika Kitabu Chake kisa cha watu waliokuwa jeuri, kama Alivyosema:

إِنَّمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٠﴾ وَيَقُولُونَ إِنَّا لَتَارْكَوْا إِلَهَيْنَا لِشَاعِرٍ
مَجْنُونٍ ﴿٢١﴾

“Wao walipokuwa wakiambiwa hapana mungu ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna kwa kiburi. Na wakisema: Hivyo sisi tuiache miungu yetu kwa ajili ya huyu mtunga mashairi mwendawazimu?”

Maana yake, ‘Je, tuache kuabudu miungu yetu na miungu ya mababa zetu kwa sababu ya maneno tu ya mshairi huyu mwendawazimu.’ – Yaani, Mtume ﷺ. Allah تعالى Alisema katika Kukanusha tabia yao:

بَلْ جَاءَ بِالْحَقِّ

“Bali huyu amekuja kwa Haki...”

Yaani, Mtume ﷺ ameleta ukweli katika habari na amri zote alizomshushia Allah.

وَصَدَقَ الْمُرْسَلِينَ

“...na amewasadikisha Mitume.”

Yaani, anatimiza ubashiri wao juu ya tabia yake ya uaminifu, na kuwaeleza watu Sheria na Amri za Allah تعالى, kama alivyoahidi.

¹ Ibn Abi Hatim 8171, Muslim kwa ufupi 1/52.

مَا يُقَالُ لَكَ إِلَّا مَا قَدْ قِيلَ لِلرُّسُلِ مِن قَبْلِكَ^٤

“Huambiwi ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako.”
(41:43).

إِنكُمْ لَذَائِقُوا الْعَذَابِ الْأَلِيمِ ﴿٣٨﴾ وَمَا تُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَ
 اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٠﴾ أُولَئِكَ هُم رِزْقٌ مَّعْلُومٌ ﴿٤١﴾ فَوَاكِهِ^{٤٢} وَهُمْ مُكْرَمُونَ ﴿٤٢﴾ فِي جَنَّاتِ
 النَّعِيمِ ﴿٤٣﴾ عَلَى سُرُرٍ مُتَقَابِلِينَ ﴿٤٤﴾ يُطَافُ عَلَيْهِم بِكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٤٥﴾ بِيضَاءَ لَذَّةٍ
 لِلشَّارِبِينَ ﴿٤٦﴾ لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا يُنزَفُونَ ﴿٤٧﴾ وَعِنْدَهُمْ قَنَاصِرُ الْوَطْرِ عِينٌ
 ﴿٤٨﴾ كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٤٩﴾

38. Hakika nyinyi bila ya shaka mtaionja adhabu chungu.

39. Wala hamlipwi ila hayo mliyokuwa mkiyafanya.

40. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa.

41. Hao ndio watakaopata riziki maalumu.

42. Matunda, nao watahishimiwa.

43. Katika Bustani za neema.

44. Wako juu ya viti vya enzi wanatizamana.

45. Wanazungushiwa kikombe chenye mvinyo uliosafi.

46. Kinywaji cheupe, kitamu kwa wanywao.

47. Hakina madhara, wala hakiwaleweshi.

48. Na watakuwa nao wanawake wenye macho ya staha mazuri.

49. (Hao wanawake) kama mayai yaliyohifadhika.

Adhabu ya Washirikina na Malipo ya Waumini Wakweli

Kauli ya Allah تعالى, Anawaambia watu:

إِنكُمْ لَذَائِقُوا الْعَذَابِ الْأَلِيمِ ﴿٢٠﴾ وَمَا تُحِزُّونَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢١﴾

“Hakika nyinyi bila ya shaka mtaionja adhabu chungu. Wala hamlipwi ila hayo mliyokuwa mkiyafanya.”

Kisha anawaepusha waumini wa kweli. Hayo ni sawa na Aya:

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصُوا بِالْحَقِّ وَتَوَّصُوا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾

“Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara, ila wale walioamini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri.” (103:1-3),

Na Allah تعالى Amesema,

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿١﴾ ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٣﴾

“Bila ya shaka Tumemuumba mtu kwa umbo lililo bora kabisa. Kisha Tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini! Lakini wale walioamini na wakatenda mema, hao watapata ujira usio kwisha.” (95:4-6).

وَإِنْ مِنْكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَى رَبِّكَ حَتْمًا مَقْضِيًّا ﴿٧١﴾ ثُمَّ نُتِجِي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنَدَّرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثْيًا ﴿٧٢﴾

“Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola Wako Mlezi ambayo lazima itimizwe. Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu; na Tutawaacha madhalimu humo wamepiga magoti.” (19:71-72)

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾ إِلَّا أَصْحَابَ الْإِيمَانِ ﴿٣٩﴾

“Kila nafsi imo katika rehani kwa mabaya iliyoyachuma. Isipokuwa watu wa kuliani.” (74:38-39).

Kauli ya Allah تعالى hapa:

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿١١٠﴾

“Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa.”

Yaani, hawataonja adhabu iumizayo wala hawatahesabiwa. Matendo yao maovu, kama yatakuwepo, hayataangaliwa, na kila amali njema italipwa mara kumi mpaka mia saba, au kadiri Allah تعالى Atakavyo.

أُولَئِكَ هُمْ رِزْقٌ مَّعْلُومٌ ﴿١١١﴾

“Hao ndio watakaopata riziki maalumu.”

Qatadah na As-Suddi walisema, “Maana yake Pepo.”¹ Imeelezwa zaidi katika Ayah inayofuata,

فَوَاكِهُ

“Matunda...” Ya namna mbalimbali.

وَهُمْ مُكْرَمُونَ

“...nao watahishimiwa.”

Yaani, watahudumiwa na wataishi maisha ya anasa.

فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿١١٢﴾ عَلَى سُرُرٍ مُتَقَابِلِينَ ﴿١١٣﴾

“Katika Bustani za neema. Wako juu ya viti vya enzi wanatizamana.”

Mujahid alisema, “Hakuna atakayekuwa nyuma ya mwingine.”² Na Kauli ya Allah تعالى,

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿١١٤﴾ بَيْضَاءَ لَذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ ﴿١١٥﴾ لَا فِيهَا غَوْلٌ وَلَا هُمْ عَنْهَا يُنزَفُونَ ﴿١١٦﴾

“Wanazungushiwa kikombe chenye mvinyo safi, kinywaji cheupe, kitamu kwa wanywao. Hakina madhara, wala hakiwaleweshi.”

¹ At-Tabari 21:35.

² Al-Qurtubi 15:77.

Ni sawa na Aya hii:

يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ ﴿١٧﴾ بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقَ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿١٨﴾ لَا يُصَدَّعُونَ
عَنْهَا وَلَا يُنْفَوْنَ ﴿١٩﴾

“Wakitumikiwa na wavulana wa ujana wa milele, kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi. Hawataumwa kichwa kwa vinywaji hivyo wala hawatoleweshwa.” (56:17-19).

Allah تعالیٰ Ameiepusha pombe ya Peponi dhidi ya mabaya ya pombe ya duniani, ambayo huleta maumivu ya kichwa na tumbo – na ndio maana ya *Ghawl* – kwa kuwasababishia watu wakose akili kabisa. Hivyo Allah تعالیٰ Anasema hapa:

يُطَافُ عَلَيْهِم بِكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٢٠﴾

“Wanazungushiwa kikombe chenye mvinyo safi.”

Maana yake, pombe kutoka katika mto ambao hawahofii kwisha kwake. Malik amesimulia kuwa Zayd bin Aslam alisema, “Pombe nyeupe yenye kutiririka.” Maana yake, kwa rangi yenye kung’aa, si kama pombe ya duniani yenye rangi mbaya isiyovutia kwa wekundu, weusi, njano na iliyovurugika, na sifa nyingine zenye kumkirahisha yeyote mwenye hulka iliyosalimika.

لَذَّةٍ لِّلشَّرِيبِ

“...kitamu kwa wanywao...”

Yaani, ladha yake itakuwa nzuri kama rangi yake, na ladha nzuri inaashiria kuwa ina harufu nzuri, si kama pombe ya duniani.

لَا فِيهَا عََوْلٌ

“Hakina madhara...”

Yaani, haitakuwa na athari kama vile kuleta maumivu ya tumbo. Hiyo ilikuwa rai ya Ibn `Abbas, Mujahid, Qatadah na Ibn Zayd.¹ Hiyo ni tofauti na pombe ya

¹ At-Tabari 21:38.

duniani, inayosababisha msokoto wa tumbo na kadhalika, kwa sababu ni ya majimaji mno.

وَلَا هُمْ عَنْهَا يُرْفَعُونَ

“...wala hakiwaleweshi.”

Mujahid alisema, “Haitawasababishia kurukwa na akili.”¹ Hii ilikuwa pia rai ya Ibn`Abbas, Muhammad bin Ka`b, Al-Hasan. `Atay bin Abi Muslim Al-Khurasani, As-Suddi na wengine. Adh-Dhahhak alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Pombe husababisha mambo manne: kulewa, kuumwa kichwa, kutapika na mkojo.” Hivyo, Allah تعالى Anapoitaja pombe ya Peponi, Anaeleza kuwa haina sifa hizo,² kama alivyosema katika *Surat As-Saffat*. Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَعِنْدَهُمْ قَنْصِرَاتُ الْطَّرْفِ

“Na watakuwa nao wanawake wenye macho ya staha mazuri.”

Yaani, wanawake bikra, ambao hawatamuangalia yeyote isipokuwa waume wao, kama Ibn `Abbas, Mujahid, Zayd bin Aslam, Qatadah, As-Suddi na wengine walivyosema.³

عَيْنٌ

“...wenye macho ya staha mazuri.”

Yaani, macho mazuri. Husemwa pia kuwa inamaanisha macho makubwa, ambayo inaungana na maana ya kwanza. Ni macho makubwa na mazuri. Macho yao yamesifiwa kwa sababu ya uzuri wao kuwa Bikra. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

وَعِنْدَهُمْ قَنْصِرَاتُ الْطَّرْفِ عَيْنٌ ﴿٢٠﴾

“...Na watakuwa nao wanawake wenye macho ya staha mazuri.”

كَأَنَّهُنَّ بَيضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٢١﴾

“...kama mayai yaliyo hifadhika.” Miili yao inasifika kwa kuwa laini na yenye rangi nzuri. `Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn `Abbas رضي الله عنهما:

¹ At-Tabari 21:40.

² Ibn Abii Hatim 81770, Al-Qurtubi 15:79.

³ At-Tabari 21:41, 42.

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٣٧﴾

“...kama mayai yaliyohifadhika.”

Kama lulu zilizofichwa.¹ Al-Hasan alisema:

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٣٧﴾

“...kama mayai yaliyohifadhika.”

Yaliyohifadhika, hayajaguswa na yeyote. As-Suddi alisema, “Yai lililohifadhiwa vyema katika kiota chake.” Sa`id bin Jubayr alisema:

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٣٧﴾

“...kama mayai yaliyohifadhika.”

Yaani, “Ndani ya yai.” `Ata’ Al-Khurasani alisema, “Ni utandu baina ya ganda la nje na vilivyomo ndani.” As-Suddi alisema:

كَأَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُونٌ ﴿٣٧﴾

“...kama mayai yaliyohifadhika.”

Yaani, “Ute mweupe wa yai linapoondolewa ganda lake.” Rai ya Ibn Jarir kuhusu maana ya “*Maknun*”, (yaliyohifadhika) ni kwamba, ganda la nje huguswa na mbawa za ndege na kiota, na mikono ya watu, tofauti na ndani ya yai. Allah تعالی Anajua zaidi.

* * *

¹ At-Tabari 21:43.

فَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٥٠﴾ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ
 إِنِّي كَانَ لِي قَرِينٌ ﴿٥١﴾ يَقُولُ أَءِنتَكَ لَمِنَ الْمُصَدِّقِينَ ﴿٥٢﴾
 أَيُّدَا مِنَّا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَيُّنَا لَمَدِينُونَ ﴿٥٣﴾ قَالَ
 هَلْ أَنتُمْ مُطَّلِعُونَ ﴿٥٤﴾ فَاطَّلَعَ فَرَءَاهُ فِي سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٥٥﴾
 ﴿٥٦﴾ قَالَ تَاللَّهِ إِن كِدْتَ لَتُرِيدِينَ ﴿٥٧﴾ وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّي
 لَكُنْتُ مِنَ الْمُخْضَرِينَ ﴿٥٨﴾ أَفَمَا نَحْنُ بِمَعْتَبَرِينَ ﴿٥٩﴾ إِلَّا
 مَوْتَنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَدَّبِينَ ﴿٦٠﴾ إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَوْزُ
 الْعَظِيمُ ﴿٦١﴾ لِمِثْلِ هَذَا فَلْيَعْمَلِ الْعَامِلُونَ ﴿٦٢﴾ أذَلِكَ
 خَيْرٌ نُّزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزُّرُقُمِ ﴿٦٣﴾ إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً
 لِلظَّالِمِينَ ﴿٦٤﴾ إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٦٥﴾
 طَلَعَهَا كَأَنَّه رُءُوسُ الشَّيَاطِينِ ﴿٦٦﴾ فَإِنَّهُمْ لَا يَكُونُونَ مِنْهَا
 فَمَالُونَ مِنْهَا الْبُطُونَ ﴿٦٧﴾ ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ
 حَمِيمٍ ﴿٦٨﴾ ثُمَّ إِنَّ مَرْجِعَهُمْ لَإِلَى الْجَحِيمِ ﴿٦٩﴾ إِنَّهُمْ أَلْفَوْا
 ءَابَاءَهُمْ ضَالِّينَ ﴿٧٠﴾ فَهُمْ عَلَىٰ ءَأْتْرِهِمْ مُّرْعُونَ ﴿٧١﴾
 وَلَقَدْ ضَلَّ قَبْلَهُمْ أَكْثَرُ الْأُولِينَ ﴿٧٢﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا فِيهِمْ
 مُّذْرِبِينَ ﴿٧٣﴾ فَأَنْظَرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُؤَذَّرِينَ ﴿٧٤﴾
 إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ ﴿٧٥﴾

فَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ
 ﴿٥٠﴾ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ إِنِّي كَانَ لِي
 قَرِينٌ ﴿٥١﴾ يَقُولُ أَءِنتَكَ لَمِنَ
 الْمُصَدِّقِينَ ﴿٥٢﴾ أَيُّدَا مِنَّا وَكُنَّا
 تُرَابًا وَعِظْمًا أَيُّنَا لَمَدِينُونَ ﴿٥٣﴾
 قَالَ هَلْ أَنتُمْ مُطَّلِعُونَ ﴿٥٤﴾ فَاطَّلَعَ
 فَرَءَاهُ فِي سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٥٥﴾ قَالَ
 تَاللَّهِ إِن كِدْتَ لَتُرِيدِينَ ﴿٥٦﴾ وَلَوْلَا
 نِعْمَةُ رَبِّي لَكُنْتُ مِنَ الْمُخْضَرِينَ ﴿٥٧﴾
 أَفَمَا نَحْنُ بِمَعْتَبَرِينَ ﴿٥٨﴾ إِلَّا
 مَوْتَنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَدَّبِينَ ﴿٥٩﴾
 إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٠﴾
 لِمِثْلِ هَذَا فَلْيَعْمَلِ الْعَامِلُونَ ﴿٦١﴾

50. Waingie kuulizana wenyewe kwa wenyewe.

51. Aseme msemaji mmoja miongoni mwao: Hakika mimi nalikuwa na rafiki

52. Aliyekuwa akinambia: Hivyo wewe ni katika wanaosadiki

53. Ati tukishakufa tukawa udongo na mafupa, ndio tutalipwa na kuhisabiwa?

54. Atasema: Je! Mtamchungulia?

55. Basi atachungulia amuone katikati ya Jahannamu.

56. Atasema: Wallahi! Ulikaribia kunipoteza.

57. Na lau kuwa si neema ya Mola Wangu Mlezi bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa.

58. Je! Sisi hatutakufa,

59. Isipokuwa kifo chetu cha kwanza? Wala sisi hatutaadhibiwa.

60. Hakika huku bila ya shaka ndiko kufuzu kukubwa.

61. Kwa mfano wa haya nawatende watendao.

Kukusanyika Watu wa Peponi, na Mazungumzo Baina ya Mtu wa Peponi na Sahibu Yake Mshirika Aliye katika Jahanamu, na Shukrani Zake kwa Neema za Allah تعالى

Allah تعالى Anatuambia jinsi watu wa Pepo watakavyogeukiana na kuulizana hali zao, jinsi walivyokuwa duniani na walivyotaabika. Hii ni sehemu ya mazungumzo yao watakapokusanyika pamoja kuzungumza na kunywa, kuketi katika viti vyao vya enzi, huku wahudumu wakiwazunguka. Huku wakigawa vyakula tofauti tofauti, vinywaji mbalimbali, mavazi na raha zingine ambazo hakuna jicho lililopata kuziona, hakuna sikio lililopata kusikia, na wala hazikupita katika fikra za mwanadamu.

قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ إِنِّي كَانَ لِي قَرِينٌ ﴿٥٦﴾

“Aseme msemaji mmoja miongoni mwao: Hakika mimi nalikuwa na rafiki.”

Al-'Awfi alisimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Haya ni maneno ya mshirikina aliyekuwa rafiki miongoni mwa waumini duniani.”¹

يَقُولُ أَأُوْنَكَ لَمَنِ الْمُصَدِّقِينَ ﴿٥٧﴾

“Aliyekuwa akinambia: Hivyo wewe ni katika wanaosadiki.”

Maana, “Je, unaamini Ufufuo baada ya mauti, na kuhesabiwa na malipo au adhabu.” Alikuwa akisema hayo kwa kushangaa, kufuru na ujeuri.

¹ At-Tabari 21:45 Al-'Awfi pamoja na jamaa zake ni dhaifu kama tulivyotaja mara nyingi.

أَيْدَا مِيتَنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعَظْمًا أَيْنَا لَمَدِيرِيُونِ ﴿٥٧﴾

“Ati tukishakufa tukawa udongo na mifupa, ndio tutalipwa na kuhisabiwa?”

Mujahid na As-Suddi alisema, “Tutahesabiwa.”¹ Ibn `Abbas, رضي الله عنهما, na Muhammad bin Ka`b Al-Quradhi alisema, “Tutalipwa kulingana na amali zetu.”² Rai zote mbili ni sahihi.

قَالَ هَلْ أَنْتُمْ مُطَّلَعُونَ ﴿٥٨﴾

“Atasema: Je! Nyie mnawaona?”

Yaani, kuwaona. Muumini atawaambia sahibu zake katika watu wa Peponi.

فَاطَّلَعَ فَرَّاهُ فِي سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٥٩﴾

“Basi atachungulia amuone katikati ya Jahannamu.”

Ibn `Abbas, Sa`id bin Jubayr, Khulayd Al-`Usari, Qatadah, As-Suddi na `Ata' Al-Khurasani رضي الله عنهم walisema, “Inamaanisha, katikati ya Jahanamu.”³ Al-Hasan Al-Basri alisema, “Katikati ya Jahanamu kama vile alikuwa kijinga kinachoungua.”⁴

قَالَ تَأَلَّهَ إِنَّ كِدْتَ لَتُرْدِينَ ﴿٦٠﴾

“Atasema: Wallahi! Ulikaribia kunipoteza.”

Muumini atasema, kumuambia kafiri: ‘Wallahi, ulikaribia kuniangamiza, kama ningekutii.’

وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّي لَكُنْتُ مِنَ الْمُحْضَرِينَ ﴿٦١﴾

“Na lau kuwa si neema ya Mola Wangu Mlezi bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa.”

¹ At-Tabari 21:47.

² At-Tabari 21:47.

³ At-Tabari 21:48.

⁴ At-Tabari 21:48.

Maana, 'Lau isingelikuwa Fadhila za Mola Wangu Mlezi kwangu, ningekuwa kama wewe katikati ya Jahanamu, nikiwa nimeletwa pamoja nawe katika adhabu. Lakini amenipa Rehema Zake, Amenirehemu na Kuniongoza kwenye imani na nikamuamini Yeye Peke Yake.'

وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ^ط

“Wala hatukuwa wenye kuongoka wenyewe ingelikuwa Mwenyezi Mungu hakutuongoa.” (7:43)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

أَفَمَا نَحْنُ بِمَمِيّينَ ﴿٥٨﴾ إِلَّا مَوْتَنَا الْأَوَّلَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَدِّينَ ﴿٥٩﴾

“Je! Sisi hatutakufa, isipokuwa kifo chetu cha kwanza? Wala sisi hatutaadhibiwa.”

Muumini atasema hayo atakapofurahia alichopewa na Allah تعالى، Makazi Peponi ya milele bila ya adhabu na wala kufa. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema،

إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٠﴾

“Hakika huku bila ya shaka ndiko kufuzu kukubwa.”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Wanajua kuwa kifo hukata furaha zote, hivyo watasema،

أَفَمَا نَحْنُ بِمَمِيّينَ ﴿٦١﴾ إِلَّا مَوْتَنَا الْأَوَّلَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُعَدِّينَ ﴿٦٢﴾

“Je! Sisi hatutakufa, isipokuwa kifo chetu cha kwanza? Wala sisi hatutaadhibiwa.”

Wataambiwa, “Hapana.” Hapo watasema،

إِنَّ هَذَا هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾

“Hakika huku bila ya shaka ndiko kufuzu kukubwa.”¹

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:95.

Na Kauli ya Allah تعالیٰ،

لِمِثْلِ هَذَا فَلْيَعْمَلِ الْعَمِلُونَ ﴿٥٠﴾

“Kwa mfano wa haya na watende watendao.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Haya ni Maneno ya Allah تعالیٰ, na maana yake: Kwa mfano wa neema hizi na kufaulu huku, basi wanaofanyia kazi duniani wafanye hivyo, ili wayapate yaliyoko Akhera.”¹

Kisa cha Waisraili Wawili

Walitaja kisa cha watu wawili katika Bani Israil waliokuwa wabia ambao huingia katika maana ya Aya hii. Abu Ja’far bin Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Furat bin Tha’labah Al-Bahrani alisema kuhusu Aya,

إِنِّي كَانَ لِي قَرِينٌ

“Hakika mimi nilikuwa na rafiki.”

“Kulikuwa na watu wawili waliokuwa wabia na walikusanya Dinari elfu nane. Mmoja wao alikuwa na ujuzi wa kazi na mwingine hakuwa nao. Aliyekuwa na ujuzi alimuambia mwenzake, ‘Huna ujuzi, hivyo naona tugawane mali na kukuacha.’ Akamuacha. Mtu huyo akanunua nyumba, iliyokuwa ya mfalme aliyekuwa amefariki, kwa bei ya Dinari elfu moja. Akamuita sahibu yake na kumuambia, ‘Unafikiriaje kuhusu nyumba hii niliyo inunua kwa Dinari elfu moja.’ Akasema, ‘Ni nzuri mno.’ Alipoondoka alisema, ‘Ewe Allah, sahibu yangu huyu amenunua nyumba hii kwa Dinari elfu moja; Ninakuomba nyumba mojawapo ya Peponi - Hivyo akatoa sadaka ya Dinari elfu moja.’ Ukapita muda kadiri ya Alivyopenda Allah تعالیٰ. Mtu wa kwanza akaoa mwanamke kwa mahari ya Dinari elfu moja, na akamualika sahibu wake na kumwandalia chakula. Alipokuja, alisema, ‘Nimemuoa mwanamke huyu kwa mahari ya Dinari elfu moja.’ Alijibu; ‘Jambo zuri sana.’ Alipoondoka, alisema, ‘Ewe Mola Wangu Mlezi, sahibu wangu ameo kwa mahari ya Dinari elfu moja; Ninakuomba mke katika Al-Hur Al-Iyn’ - na akatoa sadaka ya Dinari elfu moja. Ukapita muda mrefu kadiri Alivyopenda Allah تعالیٰ. Mtu wa kwanza akanunua

¹ At-Tabari 21:52.

mashamba mawili kwa Dinari elfu mbili, kisha akamuita sahibu wake na kumuonesha. Akasema, 'Nimenunua mashamba haya mawili kwa Dinari elfu mbili.' Akajibu, 'Ni mazuri sana.' Alipoondoka, alisema, 'Ewe Mola Wangu Mlezi, sahibu wangu amenunua mashamba mawili kwa Dinari elfu mbili; ninakuomba mashamba mawili Peponi.' - Hivyo akatoa sadaka ya Dinari elfu mbili. Malaika akawajia na kuwatoa roho zao. Akamchukua aliyetoa sadaka mali yake na kumueka katika nyumba aliyoienda. Humo, kulikuwa na mwanamke mzuri sana mpaka ardhi ikawa inang'aa chini yake, kisha (malaika) akampeleka katika mashamba mawili na akampa vitu Anavyovijua Allah تَعَالَى Peke Yake. Mtu huyo akasema, 'Haya ni kama mtu mwenye kitu kadha na kadha.' Malaika akasema, 'Hivyo ndivyo haswa ilivyo; nyumba hii, mashamba haya na mke huyu, vyote ni vyako.' Mtu huyo akasema, 'Nilikuwa na sahibu yangu aliyekuwa akisema: "Je, wewe ni katika waumini?" Akaambiwa, 'Yuko Motoni.' Akasema, 'Angalia chini.' Basi atachungulia amuone katikati ya Jahannamu." Akasema:

تَاللّٰهِ اِنْ كِدْتَ لَتُرْدِيْنَ ﴿٥٠﴾ وَاَوْلٰٓءَا نِعْمَةٌ رَبِّيْ لَكُنْتُ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٥١﴾

"Wallahi! Ulakaribia kunipoteza. Na lau kuwa si neema ya Mola Wangu Mlezi bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa walio hudhurishwa."¹

Hadi mwisho wa Aya,

Na katika simulizi za Abuu Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Amekielezea kisa chote kwa urefu wake. Na kisha kubainisha: Ya kuwa kulikuwepo wabia wawili katika wana wa Israel, mmoja wao alikuwa Muumini na mwengine Kafiri. Hadi siku moja walipokuja kukutana. Kafiri akamuuliza Muumini: 'Hivi mali yako ile tuliyogawana umeifanyia nini?' Akamjibu, "Nimemkopesha." Akamuuliza, "Umemkopesha nani?" Muumini akasema: "Mkwasi Mtekelezaji." Kafiri akauliza: "Ni nani huyo?" Muumini akasema: "Allah Mola Wangu Mlezi." Analisema hilo Muumini huku akimshika mkono, Kafiri akautoa mkono wake, Kisha akasema: "Hivyo wewe ni katika wanaosadiki. Ati tukishakufa tukawa udongo na mafupa, ndio tutalipwa na kuhisabiwa?" Assudi amesema kuwa maana tutafidiwa tulichokitoa." Akasema: "Kafiri akaondoka na kumuacha Muumini. Hadi mwisho wa kisa."²

¹ At-Tabari 21:45, Isnadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abi Hatim 18191

أَذَلِكَ خَيْرٌ نُزُلًا أَمْ شَجَرَةُ الزُّقُومِ ﴿٥٧﴾ إِنَّا جَعَلْنَهَا فِتْنَةً لِلظَّالِمِينَ ﴿٥٨﴾ إِنَّهَا شَجَرَةٌ
تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٥٩﴾ طَلَعَهَا كَأَنَّه رُؤُوسُ الشَّيَاطِينِ ﴿٦٠﴾ فَإِنَّهُمْ لَأَكَلُونَ مِنْهَا
فَمَا لَوْ أَنَّ مِنَ الْبَطُونَ ﴿٦١﴾ ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيَّا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ﴿٦٢﴾ ثُمَّ إِنَّ مَرْجِعَهُمْ
لِإِلَى الْجَحِيمِ ﴿٦٣﴾ إِنَّهُمْ أَلْفَوْا آبَاءَهُمْ ضَالِينَ ﴿٦٤﴾ فَهُمْ عَلَىٰ آثَرِهِمْ يُرْعُونَ ﴿٦٥﴾

62. Je! Kukaribishwa hivi si ndio bora, au mti wa Zaqqum?

63. Hakika Sisi Tumeufanya huo kuwa ni mateso kwa waliodhulumu.

64. Hakika huo ni mti unaotoka katikati ya Jahannamu.

65. Mashada ya matunda yake kama kwamba vichwa vya mashetani.

66. Basi hakika bila ya shaka hao watayala hayo, na wajaze matumbo.

67. Kisha juu yake wanyweshwe maji ya moto yaliyochemka.

68. Kisha hakika marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannamu.

69. Hakika waliwakuta baba zao wapo katika njia iliypotea ili upatikane mchanganyiko.

70. Na wao wakafanya haraka kufuata nyayo zao.

Mti wa Zaqqum na Wenzi Wake

Allah تعالیٰ Anasema: Hivi haya yote aliyotaja miongoni mwa neema za peponi na vyakula vyake, vinywaji na mambo ya unyumba na mengineyo katika ladha si ni ukaribishaji na zawadi iliyo bora?

أَمْ شَجَرَةُ الزُّقُومِ

“...au mti wa Zaqqum?” Ambao uko katika Jahanamu.’ Yaani huu ni namna ya mti unaoitwa Zaqqum. Hii ni kama Aya:

وَشَجَرَةً تَخْرُجُ مِنْ طُورِ سَيْنَاءَ تَنْبُتُ بِالذَّهْنِ وَصَيْغٍ لِلآكِلِينَ ﴿٢٠﴾

“Na mti utokao katika mlima wa Sinai, unatoa mafuta na kuwa kitoweo kwa walao.” (23:20)

Ambao ni mzaituni. Inaungwa mkono na Aya:

ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيُّهَا الضَّالُّونَ الْمُكْذِبُونَ ﴿٥١﴾ لَأَكُونَنَّ مِنْ شَجَرٍ مِنْ زُقُومٍ ﴿٥٢﴾

“Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokanusha. Kwa yakini mtakula mti wa Zaqqumu.” (56:51-52).

إِنَّا جَعَلْنَاهَا فِتْنَةً لِلظَّالِمِينَ ﴿٥٣﴾

“Hakika Sisi Tumeufanya huo kuwa ni mateso kwa waliodhulumu.”

Qatadah alisema, “Mti wa Zaqqumu umetajwa kama mtihani kwa waliopotea.” Walisema, ‘Mwenzenu anakuambieni kuwa Motoni kuna mti, lakini moto hula miti.’ Allah تعالی Akashusha maneno:

إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٥٤﴾

“Hakika huo ni mti unaotoka katikati ya Jahannamu.”

Yaani, “unastawishwa na moto, kwa kuwa umeumbwa kutokana na moto.”¹ Mujahid alisema: Abu Jahl, Allah Amlaani, alisema, “Maana ya Zaqqumu ni tende na siagi ninazokula (Atazaqqamuh)”²

Ninasema kuwa maana ya Aya hiyo ni, “Tumekuambia, Ewe Muhammad, kuwa mti wa Zaqqumu ni mtihani ambao Tunawajaribia watu ili kuona watakaoamini na watakaokufuru.” Hii ni sawa na Aya:

وَمَا جَعَلْنَا آلَ رَأْيَا الَّتِي أَرَبْنَاكَ إِلَّا فِتْنَةً لِلنَّاسِ

وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ وَخَوْفُهُمْ فَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٥٥﴾

“Na hatukufanya muono Tuliyoukonesha ila ni Kuwajaribu watu, na mti uliolaaniwa katika Qur’ani. Na Tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa.” (17:60).

¹ At-Tabari 21:52.

² At-Tabari 21:53.

إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ﴿٦٤﴾

“Hakika huo ni mti unaotoka katikati ya Jahannamu.”

Yaani, mizizi yake inamea chini katika Jahanamu.

طَلَعَهَا كَأَنَّهٗ رُءُوسُ الشَّيَاطِينِ ﴿٦٥﴾

“Mashada ya matunda yake kama kwamba vichwa vya mashetani.”

Haya ni maelezo ya jinsi ulivyo mbaya na unavyokirahisha. Unafananishwa na,

رُءُوسُ الشَّيَاطِينِ

“...vichwa vya mashetani.”

Ingawa hawakupata kuviona, kwa sababu ni fikra iliyowekwa vyema katika akili za watu kuwa mashetani hulka zao ni mbaya.

Allah تعالى Amesema;

فَأَيُّهُمْ لَّا يَكُونُ مِنْهَا فَأَمَّا لُؤْلُؤًا مِنْهَا الْبُطُونَ ﴿٦٦﴾

“Basi hakika bila ya shaka hao watayala hayo, na wajaze matumbo.”

Allah تعالى Anaeleza kuwa watakula matunda ya mti huo mbaya, ingawa harufu yake ni mbaya mno; watashurutishwa kula kwa sababu hawatapata kingine chochote isipokuwa mti huo na unaofanana na huo.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِنْ ضَرِيعٍ ﴿٦٧﴾ لَا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِي مِنْ جُوعٍ ﴿٦٨﴾

“Hawatakuwa na chakula isipokuwa kichungu chenye miba. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.” (88:6-7).

ثُمَّ إِنَّ لَهُمْ عَلَيَّا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ﴿٦٩﴾

“Kisha juu yake wanyweshwe maji ya moto yaliyochemka ili upatikane mchanganyiko.”

Ibn `Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maana yake, watapewa mchanganyo wa *Hamim* wanywe baada ya kula *Zaqqum*.”¹ Kwa mujibu wa masimulizi mengine, alisema kuwa inamaanisha mchanganyiko ulioandaliwa kwa maji yaliyochemka.²

Mtu mwingine alisema kuwa inamaanisha maji yaliyochemka yatachanganywa na usaha na maji machafu yanayotoka katika sehemu za siri na machoni mwao. Ibn Abi Hatim تعالى amenukuu kuwa Sa`id bin Jubayr alisema, “Watu wa Jahanamu watakapohisi njaa, wataomba chakula kutoka katika mti wa *Zaqqum*. Watakula kutokana na mti huo, kisha ngozi za nyuso zao zitaanguka, kama mtu atawakuta, atawatambua kwa nyuso zao. kisha watapata kiu, nao wataomba wapewe kinywaji, na watapewa maji kama mafuta yaliyochemka mpaka kiwango cha mwisho cha joto. Kitakaposogezwa karibu na midomo yao, nyama za nyuso zao ambazo nyama zake zilianguka zitachomwa na joto lake, na chochote kilicho matumboni mwao kitayeyuka, kisha watapigwa kwa marungu ya chuma yenye miba. Halafu kila kiungo katika miili yao kitaanguka na watalalamika kwa sauti ya juu.

ثُمَّ إِنَّ مَرْجِعَهُمْ لَإِلَى الْجَحِيمِ ﴿٥٤﴾

“Kisha hakika marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannamu.”

Yaani, baada ya muda huo kupita, watarudishwa kwenye moto mkali, wenye joto lenye kuunguza na miale inayochoma, na watazunguka kutoka eneo moja hadi lingine. Ni sawa na Aya,

يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءَانِ ﴿٥٥﴾

“Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayo chemka.” (55:44).

Hivyo ndivyo Qatadah alivyosoma Aya mbili hizi. Hii ni tafsiri nzuri. `Abdullah bin Mas`ud رضي الله عنه aliisoma kwa namna tofauti, kwa maana ya “Kurejea

¹ At-Tabari 21:55.

² At-Tabari 21:52.

kwao wakati wa mchana ndio itakuwa motoni.” `Abdullah رضي الله عنه, alikuwa akisema: “Ninaapa kwa Ambaye Mkononi Mwake upo uhai wangu, mchana wa Siku ya Kiama hautafika isipokuwa mpaka watu wema watakuwa Peponi na watu waovu watakuwa wameingia jahanamu.” Kisha akasoma:

أَصْحَابُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَأَحْسَنُ مَقِيلًا ﴿٢٤﴾

“Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makazi bora na mahali penye starehe nzuri.” (25:24).¹

Kauli ya Allah تعالى:

فَهُمْ عَلَىٰ آثَرِهِمْ يُرْعَوْنَ ﴿٢٥﴾

“Na wao wakafanya haraka kufuata nyayo zao.”

Yaani, `Tutawaadhibu kwa hilo kwa sababu wamewakuta baba zao wakifuata upotovu na wao wakawafuata bila ya ushahidi au dalili.’ Kauli ya Allah:

إِنَّهُمْ أَلْفَوْا آبَاءَهُمْ ضَالِّينَ ﴿٢٦﴾

“Hakika waliwakuta baba zao wamepotea.”

Mujahid alisema, “Ni kama kukimbia.”² Sa’id bin Jubayr alisema, “Walifuata ujinga na upumbavu.”

وَلَقَدْ ضَلَّ قَبْلَهُمْ أَكْثَرُ الْأُولِينَ ﴿٢٧﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا فِيهِمْ مُّنْذِرِينَ ﴿٢٨﴾ فَأَنْظَرُوا كَيْفَ

كَانَ عَنَقِبَةُ الْمُنْذِرِينَ ﴿٢٩﴾ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿٣٠﴾

71. Na bila ya shaka walikwishapotea kabla yao wengi wa watu wa zamani.

72. Na Sisi hakika Tuliwapelekea waonyaji.

73. Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa walioonywa.

74. Isipo kuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa.

¹ At-Tabari 21:56.

² At-Tabari 21:57.

Allah تعالی Anatuambia kuwa umma nyingi zilizotangulia zilipotea, kwa kumshirikisha Allah تعالی na miungu yao. Anasema kuwa Aliwapelekea waonyaji miongoni mwao ili kuwahadharisha kuhusu ghadhabu na kisasi cha Allah تعالی dhidi ya waliomkufuru na kuwaabudu wasiokuwa Yeye. Anatuambia kuwa waliendelea kuwapinga Mitume, Akawaaangamiza waliomkufuru na Kuwaokoa waumini na Kuwapa ushindi. Kauli ya Allah تعالی:

فَأَنْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَنِيبَةُ الْمُنْذَرِينَ ﴿٥٧﴾ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ ﴿٥٨﴾

“Basi hebu angalia ulikuwaje mwisho wa walioonywa. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa.”

* * *

وَلَقَدْ نَادَانَا نُوحٌ فَلْيَعْمَ الْمُجِيبُونَ ﴿٧٥﴾ وَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ
 مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٧٦﴾ وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهُ هُرُ الْبَاقِينَ
 ﴿٧٧﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿٧٨﴾ سَلَّمْنَا عَلَىٰ نُوحٍ فِي
 الْعَالَمِينَ ﴿٧٩﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٠﴾ إِنَّهُ مِنْ
 عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨١﴾ ثُمَّ أَعْرَفْنَا الْآخِرِينَ ﴿٨٢﴾ *
 وَإِنَّ مِنْ شِيعَتِهِ لِإِبْرَاهِيمَ ﴿٨٣﴾ إِذْ جَاءَ رَبَّهُ بِقَلْبٍ
 سَلِيمٍ ﴿٨٤﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَاذَا تَعْبُدُونَ ﴿٨٥﴾
 أَفِيكُم مِّنْ آلِهَةٍ دُونَ اللَّهِ تُرِيدُونَ ﴿٨٦﴾ فَمَا ظَنُّكُمْ بِرَبِّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٨٧﴾ فَنظَرَ نَظْرَةً فِي النُّجُومِ ﴿٨٨﴾ فَقَالَ إِنِّي
 سَقِيمٌ ﴿٨٩﴾ فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٩٠﴾ فَرَاغَ إِلَىٰ آلِهِمِ
 فَقَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٩١﴾ مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُونَ ﴿٩٢﴾ فَرَاغَ
 عَلَيْهِمْ صَرْبًا بِالْيَمِينِ ﴿٩٣﴾ فَأَقْبَلُوا إِلَيْهِ يَرْفُونَ ﴿٩٤﴾ قَالَ
 أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْجِتُونَ ﴿٩٥﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾
 قَالُوا ابْنُوا لَهُ بُيُوتًا فَأَلْفَوْهُ فِي الْجَحِيمِ ﴿٩٧﴾ فَأَرَادُوا بِهِ
 كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَسْفَلِينَ ﴿٩٨﴾

وَلَقَدْ نَادَانَا نُوحٌ فَلْيَعْمَ الْمُجِيبُونَ
 ﴿٧٥﴾ وَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ
 الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٧٦﴾ وَجَعَلْنَا
 ذُرِّيَّتَهُ هُرُ الْبَاقِينَ ﴿٧٧﴾ وَتَرَكْنَا
 عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿٧٨﴾ سَلَّمْنَا عَلَىٰ
 نُوحٍ فِي الْعَالَمِينَ ﴿٧٩﴾ إِنَّا كَذَلِكَ
 نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٠﴾ إِنَّهُ مِنْ
 عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨١﴾ ثُمَّ أَعْرَفْنَا
 الْآخِرِينَ ﴿٨٢﴾

75. Na hakika Nuhu alituita, na Sisi ni bora wa waitikaji.

76. Na Tulimuokoa yeye na watu wake kutokana na msiba mkubwa.

77. Na Tuliwajaalia kizazi chake ndio wenye kubakia.

78. Na Tukamuachia (sifa njema) kwa waliokuja

baadaye.

79. Iwe salama kwa Nuhu ulimwenguni kote!

80. Kwa hakika hivi ndivyo Tunavyowalipa wanaofanya mema.

81. Hakika yeye ni katika waja wetu walioamini.

82. Kisha Tukawazamisha wale wengine.

Utajo wa Nuhu na Watu Wake

Allah تعالى Alipotuongia juu ya jinsi watu wengi wa zamani walivyopotea kutoka katika njia ya wokovu, Anaanza, kueleza kwa urefu habari ya Nuh عليه السلام na watu wake. Watu wachache tu wa Nuh عليه السلام walimuamini, licha ya muda mrefu alioishi pamoja nao. Aliishi pamoja nao kwa miaka elfu moja kasoro hamsini, na baada ya kuishi pamoja nao kwa muda mrefu huo, na ukafiri wao kuwa mkubwa kwake kustahamilika - kwani kila alipowaita, walimgeuzia mgongo zaidi – akamuomba Mola Wake Mlezi kwa kusema, “Nimezidiwa, hivyo nisaidie!” Hivyo Allah تعالى Akaghadhibika kwa sababu Nuh عليه السلام aliwakasirikia. Anasema:

وَلَقَدْ نَادَيْنَا نُوحًا فَلَنِعَمَ الْمُجِيبُونَ ﴿٧٥﴾

“Na hakika Nuhu alituita, na Sisi ni bora wa waitikiaji.”

Kwa maana Sisi ndio bora wa Kumjibu yeye,

وَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٧٦﴾

“Na Tulimuokoa yeye na watu wake kutokana na msiba mkubwa.”

Yaani, ukafiri wao na matusi yao.

وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهُ هُمُ الْبَاقِينَ ﴿٧٧﴾

“Na Tuliwajaalia kizazi chake ndio wenye kubakia.”

Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Walibakia watoto wa Nuh عليه السلام tu”¹ Sa`id bin Abi Arubah alisema, akisimulia kutoka kwa Qatadah kuhusu Aya,

وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهُ هُمُ الْبَاقِينَ ﴿٧٧﴾

“Na Tuliwajaalia kizazi chake ndio wenye kubakia.”

“Watu wote wametokana na kizazi cha Nuh عليه السلام.”² At-Tirmidhi, Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى walisimulia kutoka kwa Samurah رضي الله عنه, kuwa Mtume alisema, kuhusu Aya,

¹ At-Tabari 21:59.

² At-Tabari 21:59.

وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهُ هُرُ الْبَاقِينَ ﴿٧٥﴾

“Na Tuliwajaalia kizazi chake wenye kubakia.”

«سَامُ، وَحَامُ، وَيَافِثُ»

“Sam, Ham na Yafith.”¹

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Samurah رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alisema:

«سَامُ أَبُو الْعَرَبِ، وَحَامُ أَبُو الْحَبَشِيِّ، وَيَافِثُ أَبُو الرُّومِ»

“Sam alikuwa baba wa Waarabu, Ham alikuwa baba wa Wahabeshi na Yafith alikuwa baba wa Warumi.”²

Hayo pia yalinukuliwa na At-Tirmidhi.³ Hapa kinachomaanishwa kuhusu Warumi ni wale wa asili, yaani, wagiriki wanaodaiwa kuwa ni kizazi cha Ruma (Roma) bin Liti, bin Yunan, bin Yafith, mwana wa Nuh عليه السلام.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿٧٦﴾

“Na Tukamuachia (sifa njema) kwa waliokuja baadaye.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, alisema, “Anakumbukwa kwa mema.”⁴ Mujahid alisema inamaanisha “Kutajwa vyema kwa mitume wote.”⁵ Qatadah na As-Suddi alisema, “Allah تعالى Alimsababishia aendelee kusifiwa na wengine.”⁶ Adh-Dhahhak alisema maana yake “Salamu na sifa njema.”

سَلَّمُوا عَلَى نُوحٍ فِي الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾

“Iwe salama kwa Nuhu ulimwenguni kote!” Inatueleza mapana ya utajo mtukufu na sifa njema, kwani yeye husalimiwa kwa amani kutoka katika makundi na umma zote.

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 5:365, At-Tabari 21:59.

² Ahmad 5:9.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 9:98.

⁴ At-Tabari 21:60.

⁵ At-Tabari 21:60.

⁶ At-Tabari 21:60.

إِنَّا كَذَّابِكُمْ نَجْرَى الْمُحْسِنِينَ ﴿٧٥﴾

“Kwa hakika hivi ndivyo Tunavyowalipa wanaofanya mema.”

Yaani, ‘Hivi ndivyo Tunavyowalipa watumishi Wetu wanaofanya amali za kumtii Allah. Tumempa utajo mtukufu ili baada ya kifo chake, aendelee kukumbukwa kwa namna inayoendana na daraja yake.’ Kisha Allah تعالى Anasema:

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٦﴾

“Hakika yeye ni katika waja wetu walioamini.”

Maana yake, mmojawapo katika wenye kuamini kiukweli Tauhidi ya Allah, miongoni mwa waliokuwa na imani ya hakika.

ثُمَّ أَعْرَفْنَا الْأَخْرِينَ ﴿٧٧﴾

“Kisha Tukawazamisha wale wengine.”

Yaani, ‘Tuliwaangamiza, na hakukubakia alama yao yoyote, na wanajulikana kwa sifa zao mbaya tu.’

* وَإِنَّ مِنْ شِيعَتِهِمْ لِبَرَاهِيمَ ﴿٧٨﴾ إِذْ جَاءَ رَبَّهُ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٧٩﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ
 وَقَوْمِهِ مَاذَا تَعْبُدُونَ ﴿٨٠﴾ أَيْفَكَاءَ إِلَهَآءِ دُونَ اللَّهِ تُرِيدُونَ ﴿٨١﴾ فَمَا ظَنُّكُمْ بِرَبِّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٨٢﴾

83. Na hakika Ibrahim alikuwa katika kundi lake,

84. Alimuelekea Mola Wake Mlezi kwa moyo safi.

85. Alimuambia baba yake na watu wake: Mnaabudu nini?

86. Kwa kuzua tu mnataka miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu?

87. Mnamdhania nini Mola Mlezi wa walimwengu wote?

Kisa cha Ibrahim عليه السلام na Watu Wake

‘Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما:

وَإِنَّ مِنْ شِيعَتِهِ لَإِبْرَاهِيمَ ﴿٧٥﴾

“Na hakika Ibrahim alikuwa katika kundi lake.”

Yaani, alikuwa katika wafuasi wa Dini yake.¹ Mujahid alisema, “Alikuwa akifuata njia yake na mwenendo wake.”²

إِذْ جَاءَ رَبُّهُ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٧٦﴾

“Alipomuelekea Mola Wake Mlezi kwa moyo mzima.”

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Inamaanisha kuwa alishuhudia kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى.”³

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa ‘Awf alisema, “Nilimuambia Muhammad bin Sirin, ‘Ni upi moyo Salim?’ Akasema, ‘Unaojua kuwa kuwepo kwa Allah تعالى ni kweli na Kiyama bila ya shaka kitakuja, na kwamba Allah تعالى Atawafufua walio makaburini.’”⁴

Al-Hasan alisema, “Ulioepukana na Shirk.”⁵ ‘Urwah alisema, “Ambao haukulaaniwa.”⁶

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَاذَا تَعْبُدُونَ ﴿٧٧﴾

“Alimuambia baba yake na watu wake: Mnaabudu nini?”

Aliwakana watu wake kwa ibada yao ya masanamu na miungu bandia. Hivyo kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema:

أَفَكُلَّاءِ الْهَيْهَاتُ دُونَ اللَّهِ تُرِيدُونَ ﴿٧٨﴾ فَمَا ظَنُّكُمْ بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٩﴾

“Kwa kuzua tu mnataka miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu? Mnamdhanja nini Mola Mlezi wa walimwengu wote?”

¹ At-Tabari 21:61.

² At-Tabari 21:61.

³ Al-Qurtubi 15:91.

⁴ Al-Qurtubi 15:91.

⁵ At-Tabari 21:62.

⁶ At-Tabari 21:62.

Qatadah alisema, "Inamaanisha, Mnadhani Atakufanyeni nini mtakapokutana Naye, ilhali mmemshirikisha na wengine."¹

فَنظَرَ نَظْرَةً فِي النُّجُومِ ﴿٧٥﴾ فَقَالَ إِنِّي سَقِيمٌ ﴿٧٦﴾ فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٧٧﴾ فَرَاغَ إِلَى
 ءِالِهِمْ فَقَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٨﴾ مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُونَ ﴿٧٩﴾ فَرَاغَ عَلَيْهِمْ ضَرْبًا بِالْيَمِينِ ﴿٨٠﴾
 فَأَقْبَلُوا إِلَيْهِ يَزْفُونَ ﴿٨١﴾ قَالَ أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ ﴿٨٢﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨٣﴾
 قَالُوا آبْنَا لَهُ بُنَيَّنَا فَأَلْقُوهُ فِي الْجَحِيمِ ﴿٨٤﴾ فَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَسْفَلِينَ ﴿٨٥﴾

88. Kisha akapiga jicho kutazama nyota.

89. Akasema: Hakika mimi ni mgonjwa!

90. Nao wakamuacha, wakampa kisogo.

91. Basi akaiendea miungu yao kwa siri, akaiambia: Mbona hamli?

92. Mna nini hata hamsemi?

93. Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia.

94. Basi wakamjia upesi upesi.

95. Akasema: Mnaviabudu vitu mnavyovichonga wenyewe?

96. Na hali Mwenyezi Mungu ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya!

97. Wakasema: Mjengeeni jengo, na kisha mtupeni motoni humo!

98. Basi walitaka kumfanyia vitimbi, lakini Tukawafanya wao ndio wa chini.

Ibrahim عليه السلام, aliwaambia haya watu wake ili abakie katika mji pindi walipotoka kwenda katika dhifa zao. Muda wao wa kuondoka ulikaribia ili wakafanye sherehe zao, na yeye alitaka abakie peke yake pamoja na miungu yao ili aivunje, basi akawaambia jambo lililokuwa la kweli, kwani kwa hakika alikuwa anapata shida kufuatana na vitu walivyokuwa wa kiviabudu..

¹ At-Tabari 21:63.

فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٣٧﴾

“Nao wakamuacha, wakampa kisogo.”

Qatadah alisema, “Waarabu husema kuhusu mtu anayetafakari sana kuwa anaziangalia nyota.”¹

Alichomaanisha Qatadah ni kwamba, aliangalia mbinguni huku akitafakari vitu vinavyowashughulisha watu wake. Hivyo alisema,

إِنِّي سَقِيمٌ

“Hakika mimi ni mgonjwa!” Yaani, dhaifu.

Ibn Jarir رضي الله عنه amesimulia Hadith kutoka kwa Abu Hurayrah رحمه الله تعالى, inayoeleza kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَمْ يَكْذِبْ إِبْرَاهِيمُ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ غَيْرَ ثَلَاثَ كَذَبَاتٍ: يُشْتَبِنُ فِي ذَاتِ اللَّهِ تَعَالَى، قَوْلُهُ: ﴿إِنِّي سَقِيمٌ﴾ وَقَوْلُهُ: ﴿بَلْ فَعَلَهُ كَبْرُهُمْ هَذَا﴾ وَقَوْلُهُ فِي سَارَةِ: هِيَ أُخْتِي»

“Ibrahim hakuongopa isipokuwa katika hali tatu. Mbili zilikuwa kwa ajili ya Allah: (mojawapo ni) aliposema, “Hakika mimi ni mgonjwa!”; na (pili) aliposema, “Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao.” na (ya tatu) aliposema kuhusu (mkewe) Sarah, “Huyo ni dada yangu.”

Hadithi hii imeandikwa katika vitabu vya *Sahih* na *Sunan* kwa isnadi mbalimbali.² Lakini hii si namna ya uongo halisi ambapo mtu hupata lawama - La hashu! Mtu anauita uongo kutokana na kutokupata neno bora zaidi. Kwa sababu ni tungo tata inayotumika kwa ajili ya lengo halali la kidini, na ilisemekana kuwa kilichomaanishwa na maneno ni kweli.

¹ *Ad-Dur Al-Manthur* 7:100.

² *Fath Al-Bari* 6:447, *Muslim* 4:1840, *Abu Dawud* 2:659, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:5, *An-Nasai* katika *Al-Kubra* 6:440.

إِنِّي سَقِيمٌ

“Hakika mimi ni mgonjwa!”

Kilikuwa, Mimi ni mgonjwa moyoni juu ya kuabudu kwenu masanamu badala ya Allah تعالى. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Watu wa Ibrahim عليه السلام walikwenda kwenye sherehe zao na walitaka na yeye aende pia. Hivyo alilala chali na kusema,

إِنِّي سَقِيمٌ

“Hakika mimi ni mgonjwa!”

“Na akaanza kuangalia juu. Walipotoka, aliigeukia miungu yao na kuivunja.”¹ Haya yameandikwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى. Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Alisema:

فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِينَ ﴿٧٥﴾

“Nao wakamuacha, wakampa kisogo.”

Kuelekea katika Sherehe zao. Kwa maana akaiendea baada ya kuwa wao wametoka kwa upesi na haraka.

فَقَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ

“Mbona hamli?”

Waliwawekea chakula mbele yao kama sadaka ili kibarikiwe. Ibrahim عليه السلام, alipokiangalia chakula kilichokuwa mbele yao, alisema:

أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٦﴾ مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُونَ ﴿٧٧﴾

“Mbona hamli? Mna nini hata hamsemi?”

Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَرَاغَ عَلَيْهِمْ صَرْبًا يَأْتِمِنُ ﴿٧٨﴾

“Kisha akaigeukia kuipiga kwa mkono wa kulia.”

¹ At-Tabari 21:63.

Al-Farra' alisema, "Maana yake, alianza kuyapiga masanamu hayo kwa mkono wake wa kulia." Qatadah na Al-Jawhari walisema, "Akayageukia, akayapiga kwa mkono wake wa kulia."¹ Akayapiga kwa mkono wake wa kulia kwa sababu mkono wa kulia una nguvu zaidi. Kisha akayaacha yakiwa yamevunjika vipande vipande, (yote) isipokuwa kubwa lao, ili waligeukie, kama tulivyoona katika *Tafsir ya Surat Al-Anbiya'*.² Na Kauli Yake Allah تعالى:

فَأَقْبِلُوا إِلَيْهِ يَرْفُؤْنَ ﴿٧٦﴾

"Basi wakamjia upesi upesi."

Mujahid na wengine walisema, "Inamaanisha, walikuja mbio." Habari hiyo imeelezwa kwa kifupi hapa; katika *Surat Al-Anbiya'*, imeelezwa kwa kirefu zaidi. Waliporejea, mwanzo hawakumjua aliyefanya hayo, mpaka walipochunguza na kugundua kuwa alikuwa Ibrahim عليه السلام aliyefanya hayo. Walipokuja kumkaripia, alianza kuwabeza na kuviza akili zao kwa kusema:

قَالَ أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْجِتُونَ

"Hivyo mnaviabudu vitu mnavyovichonga wenyewe?"

Yaani, 'je, badala ya Allah تعالى mnayaabudu masanamu mliyoyachonga wenyewe kwa mikono yenu.'

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٧٧﴾

"Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya!"

Inamaanisha kuwa, 'Allah تعالى Amekuumbeni nyinyi na matendo yenu;' au inaweza kumaanisha, 'Allah تعالى Amekuumbeni nyinyi na mnayoyafanya.' Rai zote mbili zina maana zilizokaribiana. Ya kwanza iko wazi zaidi kwa sababu ya masimulizi yaliyonukuliwa katika Al-Bukhari katika Kitabu cha *Af'al Al-'Ibad*, kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه, ikinasibishwa kwa Mtume ﷺ:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَصْنَعُ كُلَّ صَانِعٍ وَصَنَعْتَهُ»

"Allah Ameumba kila mfanya amali na anachokifanya."

¹ At-Tabari 21:67.

² Angalia juzu ya sita, *Tafsir ya Surat Al-Anbiyaa* (21:58).

Akasoma:

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾

“Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya!”²

Ulipothibitika ushahidi dhidi yao, waliamua kumkamata kwa nguvu na wakasema:

أَبْنُوا لَهُ بُنْيَانًا فَأَلْقُوهُ فِي الْجَحِيمِ

“Wakasema: Mjengeeni jengo, na kisha mtupeni motoni humo!”

Yakatokea tuliyokwishayaeleza katika *Tafsir ya Surat Al-Anbiya'*, (21:68-70) na Allah تعالى Alimuokoa dhidi ya moto na Akampa ushindi juu yao, kwa Kuufanya ushahidi wake kuwa juu na Kuusaidia. Kauli ya Allah تعالى:

فَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَسْفَلِينَ ﴿٧٠﴾

“Basi walitaka kumfanyia vitimbi, lakini Tukawafanya wao ndio wa chini.”

* * *

¹ Khalqul - Af-aalil - Ibadi 117, kwa Isnadi sahihi 1:158.

وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَعِيدِينَ ﴿٩٩﴾ رَبِّ هَبْ لِي مِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾ فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ
 السَّعْيَ قَالَ يَبْنَؤِي إِنِّي أَرَىٰ فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْهَبُ فَانظُرْ
 مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ يَتَأْتٍ أَفْعَلٌ مَا تُؤْمَرُ ۗ سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ
 اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ ﴿١٠٢﴾ فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾
 وَنَدَيْنَاهُ أَنِ يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿١٠٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا ۗ إِنَّا
 كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٥﴾ إِنَّ هَذَا هُوَ الْبَلْتُوا
 الْمُمِينُ ﴿١٠٦﴾ وَفَدَيْنَاهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٠٧﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي
 الْآخِرِينَ ﴿١٠٨﴾ سَلَّمْ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿١٠٩﴾ كَذَلِكَ نَجْزِي
 الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٠﴾ إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾
 وَبَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٢﴾ وَبَارَكْنَا عَلَيْهِ
 وَعَلَىٰ إِسْحَاقَ ۗ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِمَا مُحْسِنٌ وَظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ
 مُبِينٌ ﴿١١٣﴾ وَلَقَدْ مَنَّا عَلَىٰ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١١٤﴾
 وَجَعَلْنَاهُمَا قَوْمَهُمَا مِنْ الْكُرْبِ الْعَظِيمِ ﴿١١٥﴾
 وَنَصَرْنَاهُمْ فَاكْتُوا هُمُ الْغَالِبِينَ ﴿١١٦﴾ وَءَاتَيْنَاهُمَا الْكِتَابَ
 الْمُسْتَبِينَ ﴿١١٧﴾ وَهَدَيْنَاهُمَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١١٨﴾
 وَتَرَكْنَا عَلَيْهِمَا فِي الْآخِرِينَ ﴿١١٩﴾ سَلَّمْ عَلَىٰ مُوسَىٰ
 وَهَارُونَ ﴿١٢٠﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢١﴾
 إِنَّهُمَا مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٢﴾

وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَعِيدِينَ ﴿٩٩﴾
 رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾
 فَبَشَّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾ فَلَمَّا بَلَغَ
 مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَبْنَؤِي إِنِّي أَرَىٰ فِي
 الْمَنَامِ أَنِّي أَذْهَبُ فَانظُرْ مَاذَا
 تَرَىٰ ۚ قَالَ يَتَأْتٍ أَفْعَلٌ مَا تُؤْمَرُ ۗ
 سَتَجِدُنِي إِن شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ
 ﴿١٠٢﴾ فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾
 وَنَدَيْنَاهُ أَنِ يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿١٠٤﴾ قَدْ
 صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا ۗ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي
 الْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٥﴾ إِنَّ هَذَا هُوَ
 الْبَلْتُوا الْمُمِينُ ﴿١٠٦﴾ وَفَدَيْنَاهُ بِذَبْحٍ
 عَظِيمٍ ﴿١٠٧﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي
 الْآخِرِينَ ﴿١٠٨﴾ سَلَّمْ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ
 ﴿١٠٩﴾ كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١١٠﴾
 إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾
 وَبَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿١١٢﴾ وَبَارَكْنَا عَلَيْهِ
 وَعَلَىٰ إِسْحَاقَ ۗ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِمَا مُحْسِنٌ
 وَظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ مُبِينٌ ﴿١١٣﴾

99. Na akasema: Hakika mimi, nakwenda kwa Mola Wangu Mlezi; Yeye Ataniongoa.

100. Ewe Mola Wangu Mlezi! Nitunukie aliye miongoni mwa watenda mema.

101. Basi Tukambashiria mwana aliye mpole.

102. Basi alipofika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimuambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje? Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyoamrisha, utanikuta mimi, Inshallah, katika wanao subiri.

103. Basi wote wawili wali pojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji.

104. Tulimuita: Ewe Ibrahim!

105. Umekwishaitimiliza ndoto. Hakika hivi ndivyo Tunavyowalipa wanaotenda mema.

106. Hakika haya ni majaribio yaliyo dhahiri.

107. Basi Tukamtolea fidia kwa mnyama mtukufu.

108. Na Tukamuachia (sifa njema) kwa watu waliokuja baadaye.

109. Iwe salama kwa Ibrahim!

110. Hivi ndivyo Tunavyowalipa wanaofanya mema.

111. Hakika yeye ni katika waja wetu walioamini.

112. Na Tukambashiria kuzaliwa Is-haqa, naye ni Nabii miongoni mwa watu wema.

113. Na Tukambarikia yeye na Is-haqa. Na miongoni mwa kizazi chao walitokea wema na wenye kudhulumu nafsi zao waziwazi.

Kuhama kwa Ibrahim عليه السلام, Kupewa kwake Mtihani wa Kumchinja Mwanaye Ismail عليه السلام na Neema ya Allah تعالى Juu Yake

Allah تعالى Anatuambia kuwa baada ya kumsaidia rafiki yake kipenzi, Ibrahim عليه السلام, dhidi ya watu wake, na baada ya Ibrahim عليه السلام kuacha kutumaini kuwa wataamini licha ya ishara zote kubwa walizoshuhudia, alihama kwao, na alisema:

وَقَالَ إِنِّي ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّي سَيَّئِرِينَ ﴿٩٩﴾ رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٠٠﴾

“Na akasema: Hakika mimi nahama, nakwenda kwa Mola Wangu Mlezi; Yeye Ataniongoa. Ewe Mola Wangu Mlezi! Nitunukie aliye miongoni mwa watenda mema.”

Yaani, watoto watiifu, badala ya watu wake na ndugu aliowaacha. Allah Amesema:

فَبَشِّرْنَاهُ بِغُلَامٍ حَلِيمٍ

“Basi Tukambashiria mwana aliye mpole.”

فَأَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ

“Basi alipofika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye.” Yaani, alipokua mkubwa na kuanza kutoka na kutembea na baba yake, kwani Ibrahim عليه السلام mara nyingi alikuwa akienda kumuona mwanaye na mama yake katika ardhi ya Faran (Makkah) kuwajulia hali. Ilisemwa kuwa alikuwa akipanda *Al-Buraq*, na kusafiri kwenda huko kwa haraka, na Allah Anajua zaidi. Imesimuliwa kutoka kwa Ibn `Abbas, Mujahid, `Ikrimah, Sa`id bin Jubayr, `Ata' Al-Khurasani, Zayd bin Aslam na wengine kuwa,

فَأَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ

“Basi alipofika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye.”

Yaani, alipokuwa kijana na kuweza kufanya kazi kama baba yake.¹

فَأَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يَبْنِيَّ إِنِّي أَرَىٰ فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْهَبُ فَأَنْظِرْ مَاذَا تَرَىٰ^٤

“Basi alipofika makamo ya kwenda na kurudi pamoja naye, alimuambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje?”

¹ At-Tabari 21:72, 73.

'Ubayd bin 'Umayr alisema, "Ndoto za mitume ni wahyi." Kisha akasoma Ayah:

قَالَ يَبْنَئِي إِنِّي أَرَىٰ فِي الْمَنَامِ أَنِّي أَذْهَبُكَ فَأَنْظُرُ مَاذَا تَرَىٰ^ط

"...alimuambia: Ewe mwanangu! Hakika mimi nimeona usingizini kuwa ninakuchinja. Basi angalia wewe, waonaje?"^ط

Alimuambia mwanaye ili iwe rahisi kwake, na ili kujaribu uvumilivu na azima yake, katika umri wa ujana, katika kumtii Allah na kumtii baba yake.

قَالَ يَتَأَبَّتْ أَفْعَلُ مَا تُؤْمُرُ^ط

"Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyoamrisha..."

Maana yake, 'Tii amri ya Allah na uniuue.'

سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ

"...utanikuta mimi, Inshallah, katika wanaosubiri."

Yaani, 'Nitavumilia na nitatafuta malipo ya hayo kutoka kwa Allah تعالى. Yeye, عليه السلام, aliamini alichohadiwa. Allah تعالى Alisema:

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ^ط إِنَّهُ كَانَ صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا ﴿٥٥﴾ وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا ﴿٥٦﴾

"Na mtaje katika Kitabu Ismail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola Wake Mlezi mwenye kuridhiwa." (19:54-55).

فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ ﴿٥٧﴾

"Basi wote wawili walipojisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji."

Yaani, wote wawili walipotamka Shahadah na kumkumbuka Allah تعالى - Ibrahim عليه السلام kwa kuwa alikaribia kumchinja na Ismail عليه السلام kwa kuwa alikaribia kufa. Na imesemwa kuwa "walijisalimisha." Yaani walijisalimisha na kufuata

^ط At-Tabari 21:75.

Amri ya Allah تعالى; Ibrahim عليه السلام alitii Amri ya Allah تعالى na Isma'il عليه السلام alimtii Allah تعالى na baba yake. Hii ilikuwa rai ya Mujahid, 'Ikrimah, Qatadah, As-Suddi na Ibn Ishaq,¹ na wengine .

Maana ya kifungu hiki cha maneno, "na akamlaza juu ya kipaji" alimuelekeza ardhini uso wake ili amchinje kutokea nyuma, na kutouona uso wake wakati wa kumchinja, ili iwe rahisi kwake. Ibn ` Abbas, Mujahid, Sa`id bin Jubayr, Adh-Dhahhak na Qatadah رضي الله عنهم walisema hilo:

وَتَلَّهُ لِلْجَبِينِ

"...na akamlaza juu ya kipaji."

Yaani, "Uso wake aliugeuzia chini."² Imam Ahmad amenukuu kuwa Ibn ` Abbas عليه السلام alisema, "Ibrahim عليه السلام alipoamriwa matendo ya ibada, *Shaytan* alimtokea huko *Mas'a* na akashindana naye mbio, lakini Ibrahim عليه السلام alitangulia kufika. Jibril عليه السلام, akampeleka mpaka *Jamrat Al-Aqabah* na *Shaytan* akamtokea, akampiga kwa changarawe saba, akatoweka. Kisha akamtokea katika *Al-Jamrah Al-Wusta* na akampiga kwa changarawe saba. Halafu akamlaza juu ya kipaji chake. Isma'il عليه السلام, alikuwa amevaa kanzu nyeupe, na alisema, 'Ewe baba yangu, sina nguo nitakayokafiniwa nayo isipokuwa hii niliyo nayo, nivue ili unikafinie.' Akaanza kuivua, kisha kukaitwa kwa nyuma:

أَنْ يُتَابِرَاهِمُ ﴿١٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ الرُّءْيَا

"Ewe Ibrahim! Umekwishaitimiliza ndoto."

Ibrahim عليه السلام akageuka, na kumuona kondoo dume mzuri, mweupe, aliyekuwa na pembe." Ibn ` Abbas رضي الله عنهما alisema, "Tulikuwa tukimtafuta kondoo anayefanana na huyo."³ Hisham ameitaja Hadithi hii kwa kirefu katika *Al-Manasik*.

وَتَنذِيئَهُ أَنْ يُتَابِرَاهِمُ ﴿١٤﴾ قَدْ صَدَّقْتَ الرُّءْيَا

"Tulimuita: Ewe Ibrahim! Umekwishaitimiliza ndoto."

¹ At-Tabari 21:77.

² At-Tabari 21:77, 78.

³ Ahmad 1:297.

Yaani, 'lengo la ndoto yako limeshatimia kwa kumlaza mwanao ili umchinje.' As-Suddi na wengine walisema kuwa alipitisha kisu shingoni mwa Isma'il, lakini hakikumkata hata kidogo, kwa sababu baina yake kuliwekwa kipande cha shaba. Ibrahim عليه السلام aliitwa katika hatua hiyo na kukasemwa:

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّيَا

"Umekwishaitimiliza ndoto."¹

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ

"Hakika hivi ndivyo Tunavyowalipa wanaotenda mema."

Yaani, 'Hivi ndivyo Tunavyowafanyia wenye kututii katika mambo yaliyo magumu kwao; Tuliwafanyia njia ya kutokea.' Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۚ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ بَلِغُ أَمْرِهِ ۗ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ۝

"Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea. Na Humruzuku kwa namna asiyotazamia. Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye Humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu Anatimiza Amri Yake. Mwenyezi Mungu Kajaalia kila kitu na kipimo chake." (65:2-3).

Kutokana na Ayah na kisa hiki, baadhi ya wanazuoni wa fani ya (misingi na kanuni za kisheria) *Usul* wamesema kuwa inasahi hukumu kufutwa kabla ya kutumika - tofauti na baadhi ya *Mu'tazilah*. Ushahidi wa hilo uko dhahiri, kwa sababu Allah تعالى Alimuamuru Ibrahim عليه السلام, kumchinja mwanaye, halafu Akaifuta hukumu hiyo na kumuelekezea kuchinja kondoo. Lengo la Amri Yake, kimsingi, lilikuwa Kumlipa thawabu rafiki yake mwandani kwa subira yake na azima ya kutaka kumchinja mwanaye. Kwa kuzingatia hilo.

¹ At-Tabari 21:74.

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ هَذَا هُوَ الْبَلْتُؤُا الْمُمِينُ ﴿٣٧﴾

“Hakika haya ni majaribio yaliyo dhaahiri.”

Yaani, ulidhihirika mtihani alipoamrisha kumchinja mwanaye, hivyo, akaharakisha kutekeleza, kwa ajili ya kunyenyekea Amri ya Allah تعالى na kumtii.

Allah تعالى Alisema:

وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿٣٧﴾

“Na Ibrahimu aliye timiza ahadi?” (53:37), na

وَقَدَّيْنَهُ بِذَبْحٍ عَظِيمٍ ﴿٣٧﴾

“Basi Tukamtolea fidia kwa mnyama mtukufu.”

Imesimuliwa kuwa Ibn `Abbas رضي الله عنهما, alisema, “Ni kondoo dume aliyeishi Peponi kwa miaka arubaini.”¹

Imam Ahmad amenukuu kuwa Safiyyah bint Shaybah alisema, “Mwanamke mmoja katika Bani Sulaym, aliyekuwa mkunga wa watu wengi nyumbani kwangu, aliniambia kuwa Mtume ﷺ aliagiza kuitiwa `Uthman bin Talhah.” Katika tukio moja alisema, “Nilimuuliza `Uthman رضي الله عنه, `Kwanini Mtume ﷺ alikuita?’ Akasema, Mtume ﷺ aliniambia,

«إِنِّي كُنْتُ رَأَيْتُ قَرْنِي الْكَبْشِ حِينَ دَخَلْتُ الْبَيْتَ فَنَسِيتُ أَنْ أَمُرَّكَ أَنْ تُحَمَّرَهُمَا فَحَمَّرَهُمَا، فَإِنَّهُ لَا يَتَّبِعِي أَنْ يَكُونَ فِي الْبَيْتِ شَيْءٌ يَسْغُلُ الْمُصَلِّيَّ»

“Niliona pembe za kondoo dume huyo nilipoingia katika Nyumba na nilisahau kukuambia uzifunike, zifunikeni, kwani haitakikani katika Nyumba kuwe na kitu cha kumshughulisha mwenye kusali.”

Sufyan alisema, “Pembe za kondoo huyo ziliendelea kunimg’inia katika Nyumba mpaka ilipoungua moto, nazo zikaungua pia.”²

¹ At-Tabari 21:90.

² Ahmad 4:68.

Hii inaleta ushahidi unaojitegemea kuwa aliyepatwa na masuala ya kuchinjwa ni Isma'il عليه السلام. Quraysh walirithishana pembe za kondoo aliyechinjwa na Ibrahim عليه السلام, na zilipita kizazi kimoja hadi kingine, mpaka Mtume ﷺ akatumwa. Allah تعالى Anajua zaidi.

Masimulizi Yenye Kueleza kuwa, Isma'il عليه السلام Ndiye Aliyekuwa Achinjwe na Ibrahim عليه السلام, na kwamba Hilo ni Sahihi Pasi na Shaka Yoyote

Sa'id bin Jubayr, 'Amir Ash-Sha'bi, Yusuf bin Mihran, Mujahid, 'Ata' na wengine walisimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa ni Isma'il عليه السلام. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Aliyekombolewa alikuwa Isma'il عليه السلام. Wayahudi walidai kuwa alikuwa Ishaq عليه السلام, lakini wayahudi wameongopa."¹ Imesimuliwa kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما alisema, "Aliyetaka kuchinjwa alikuwa Isma'il عليه السلام."² Ibn Abi Najih alisema, akisimulia kutoka kwa Mujahid, "Alikuwa Isma'il عليه السلام."³ Hii ilikuwa pia rai ya Yusuf bin Mihran.⁴ Ash-Sha'bi alisema, "Alikuwa Isma'il عليه السلام, na niliona Pembe za kondoo dume katika Ka'bah."⁵

وَدَشَّرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦١﴾

"Na Tukambashiria kuzaliwa Is-haqa, naye ni Nabii miongoni mwa watu wema." na,

فَبَشَّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ

"Basi Tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub."
(11:71).

Hapa Allah تعالى Anamtaja mwana na Mjukuu, hivyo hakumuamuru kumchinja Is'haq عليه السلام kwa kuwa Is'haqa عليه السلام amebeba ahadi ya Allah تعالى kuwa atazaa Mtoto huko mbele (ambaye ni Ya'qub عليه السلام). Kwa kuzingatia hilo, Aliyemuamuru kumchinja hawezi kuwa ghairi ya Isma'il عليه السلام.⁶ Ibn Ishaq

¹ At-Tabari 21:83.

² At-Tabari 21:82.

³ At-Tabari 21:84.

⁴ At-Tabari 21:84.

⁵ At-Tabari 21:84.

⁶ At-Tabari 21:84.

⁷ At-Tabari 21:85.

alisema, "Nilimsikia mara nyingi akisema hayo."⁷ Ibn Ishaq alisimulia kutoka kwa Buraydah bin Sufyan bin Farwah Al-Aslami kuwa Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi aliwaambia kuwa alimueleza hayo 'Umar bin 'Abd Al-'Aziz رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى, alipokuwa Khalifah, wakati akiwa pamoja naye huko Syria. 'Umar رضي الله عنه alimuambia, "Hili ni jambo ambalo kamwe sikulifikiria, lakini naliona kama unavyosema." Kisha akatuma aitiwe mtu aliyefuatana naye huko Syria, ambaye ni Myahudi aliyesilimu na kuwa imara katika Uislamu wake, na alidhani kuwa alishakuwa mmojawapo katika wanazuoni wao. 'Umar bin 'Abd Al-'Aziz رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى, alimuuliza kuhusu hilo. Muhammad bin Ka'b alisema, "Nilikuwa pamoja na 'Umar bin 'Abd Al-'Aziz رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى. 'Umar alimwambia, 'Yupi kati ya watoto wawili wa Ibrahim aliyeamrisha kumchinja?' Akajibu, 'Isma'il. Wallah!, Ewe Amiri wa Waumini, Wayahudi wanalijua hilo, lakini walikuoneeni wivu Waarabu kwa sababu ni baba yenu ambaye Allah تَعَالَى Alimtolea Amri hiyo na fadhila Alizotaja Allah تَعَالَى Ametaja zilikuwa kwa sababu ya subira yake katika kutii amri. Hivyo walikanusha hilo na wakadai kuwa alikuwa Ishaq, kwa sababu ni baba yao."¹ Na Allah تَعَالَى Anajua zaidi ni nani alikuwa yeye katika wawili hao, na kila mmoja kati yao ni mtu msafi, mzuri na mtiifu kwa Allah تَعَالَى.

'Abdullah bin Al-Imam Ahmad bin Hanbal رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى, alisema, "Nilimuuliza baba yangu kuhusu mtoto yupi aliyetaka kuchinjwa – alikuwa Isma'il au Ishaq?" Akajibu, "Isma'il." Hayo yametajwa katika *Kitab Az-Zuhd*.² Ibn Abi Hatim رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى alisema, "Nilimsikia baba yangu akisema, 'Rai sahihi ni kuwa aliyetaka kuchinjwa alikuwa Isma'il عَلَيْهِ السَّلَام.'" alisema. Na imesimuliwa kuwa 'Ali, Ibn 'Umar, Abu Hurayrah, Abu At-Tufayl, Sa'id bin Al-Musayyab, Sa'id bin Jubayr, Al-Hasan, Mujahid, Ash-Sha'bi, Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi, Abu Ja'far Muhammad bin 'Ali na Abu Salih رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ, alisema kuwa aliyetaka kuchinjwa alikuwa Isma'il."³

Al-Baghawi رَحْمَةَ اللَّهِ تَعَالَى alisema katika *Tafsir* yake, "Hii ilikuwa rai ya 'Abdullah bin 'Umar, Sa'id bin Al-Musayyab, As-Suddi, Al-Hasan Al-Basri, Mujahid, Ar-Rabi' bin Anas, Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi na Al-Kalbi."⁴ Hayo yalisimuliwa pia kutoka kwa Ibn 'Abbas na kutoka kwa Abu 'Amr bin Al-'Ala'.

¹ At-Tabari 21:85.

² Az-Zuhd, 'Abdullah bin Ahmad: 80.

³ At-Tabari 21:82, 84.

⁴ Al-Baghawi 4:32.

Na hakika bin Jariri رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Assunabihi amesema: Tulikuwa pamoja na Muawiya bin Sufiani watu wakataja aliyetaka kuchinjwa na Ibrahimu alikuwa mwanaye Ismail عليه السلام au Is'haqa عليه السلام? Akasema: Suala hilo mliloliuliza limefika mahala pake sasa. Siku moja tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ mtu mmoja akamjia yeye na kumuambia: Ewe Mtume wa Allah! Na mimi nihesabu katika kile alichokujaalia Allah تعالى, ewe mtoto unayetokana na uzao wa wachinjwa wawili, hilo likamfanya Mtume ﷺ aचेके. Mtume akaulizwa, 'nini maana ya wachinjwa wawili?' Mtume ﷺ akajibu: "Hakika babu yangu Abdul-Mutwalib alipoamuriwa akifukue upya kisima cha maji ya zamzam, aliweka nadhiri kwa Allah تعالى kama atamfanyia wepesi hilo, atamchinja mmoja wa watoto wake." Akasema: "Nadhiri hiyo ikamwangukia Mtoto wake Abdillah, wajomba wake wakalipinga hilo na kusema: Mfidie Mtoto wako kwa kutoa ngamia mia moja. Hivyo Abdul-Mutwalibu akatoa fidia ya Ngamia mia moja. Na Mtoto wa pili ni Ismail."

وَنَشَرْنَاهُ بِإِسْحَاقَ نَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٧﴾

"Na Tukambashiria kuzaliwa Is-haqa, naye ni Nabii miongoni mwa watu wema."

Baada ya kupewa bishara za aliyepaswa kuchinjwa, ambaye alikuwa Isma'il عليه السلام, Allah تعالى, hapohapo Anafuatishia kwa kutaja bishara za nduguye, Ishaq عليه السلام. Haya yametajwa pia katika Surah Hud (11:71) na katika Surat Al-Hijr (15:53-55).

نَبِيًّا

"...Nabii..."

Yaani, kutokea kwake atakuja nabii mwema.

وَبَرَكْنَا عَلَيْهِ وَعَلَىٰ إِسْحَاقَ وَمِن ذُرِّيَّتِهِمَا مُحْسِنٌ وَظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ مُبِينٌ ﴿٣٨﴾

"Na Tukambarikia yeye na Is-haqa. Na miongoni mwa vizazi vyao walitokea wema na wenye kudhulumu nafsi zao waziwazi."

Hii ni sawa na Aya:

قِيلَ يٰنُوحُ اٰهْبِطْ بِسَلٰمٍ مِّنَّا وَبَرَكَاتٍ عَلٰیكَ وَعَلٰى اٰمِرٍ مِّنْ مَّعٰنَا ؕ وَاُمُّ سَمٰنَةَ مِّنْهُمْ نَمُوۡا

بِمَا مَسَّهُم مِّنْ اَعْدَابِ اٰلِمِۡمٌ ﴿١١٠﴾

“Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo Kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe. Na zitakuwapo kaumu Tutakazo zistarehesha, na kisha zitashikwa na adhabu chungu itokayo Kwetu.” (11:48)

وَلَقَدْ مَنَّا عَلَىٰ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١١٤﴾ وَجَيَّبْنَاهُمَا وَقَوْمَهُمَا مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿١١٥﴾
 وَنَصَرْنَاهُمْ فَكَانُوا هُمُ الْغَالِبِينَ ﴿١١٦﴾ وَأَاتَيْنَاهُمَا الْكِتَابَ الْمُسْتَبِينَ ﴿١١٧﴾ وَهَدَيْنَاهُمَا
 الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١١٨﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِمَا فِي الْأَخْرَبِ ﴿١١٩﴾ سَلَّمْنَا عَلَىٰ مُوسَىٰ
 وَهَارُونَ ﴿١٢٠﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢١﴾ إِنَّهُمَا مِنْ عِبَادِنَا
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٢﴾

114. Na kwa hakika Tuliwafanyia hisani Musa na Haruni.

115. Na Tukawaokoa wao na watu wao kutokana na dhiki kubwa.

116. Na Tukawanusuru; na wakawa wao ndio wenye kushinda.

117. Na Tukawapa wawili hao Kitabu kinachobainisha.

118. Na Tukawaongoa kwenye njia lliyonyooka.

119. Na Tukawaachia (sifa njema) katika watu waliokuja baadaye.

120. Iwe salama kwa Musa na Haruni!

121. Hakika hivyo ndivyo Tunavyowalipa walio wema.

122. Hakika wawili hao ni katika waja wetu walioamini.

Utajo wa Musa عليه السلام na Harun عليه السلام.

Allah تعالى Anatuambia namna Alivyombariki Musa عليه السلام na Harun عليه السلام kwa kuwapa Utume na Alivyowaokoa wao, pamoja na waumini, dhidi ya ukandamizaji wa Fir'awn na watu wake, waliowatesa kwa kuwaua watoto wao wa kiume na kuwaacha wanawake wao. Na kuchukua ardhi yao na mali zao walizokusanya katika umri wao wote; na kuwashurutisha kufanya kazi za udhalili, halafu hatimaye Allah تعالى Akawapa ushindi juu yao. Allah تعالى Akamshushia Musa عليه السلام Kitabu adhimu na Kitukufu, ambacho ni Taurati. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ وَهَارُونَ الْفُرْقَانَ وَضِيَاءَ

“Na kwa yakini Tuliwapa Musa na Haruni kipambanuzi, na mwangaza.” (21:48).

Na hapa Allah تعالى Anasema:

وَأَتَيْنَهُمَا الْكِتَابَ الْمُسْتَبِينَ ۖ وَهَدَيْنَهُمَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٠٠﴾

**“Na Tukawapa wawili hao Kitabu kinachobainisha. Na Tukawa-
ongoa kwenye Njia Iliyonyooka.”**

Maana yake, kuhusu maneno na vitendo.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِمَا فِي الْأَخْرَبِ ﴿١٠١﴾

“Na Tukawaachia (sifa njema) katika watu waliokuja baadaye.”

Yaani, baada ya kufa kwao watatajwa vizuri na kusifiwa. Kisha Allah تعالى Anaeleza zaidi:

سَلَّمْنَا عَلَىٰ مُوسَىٰ وَهَارُونَ ﴿١٠٢﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٣﴾ إِنَّهُمَا
مِنَ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٤﴾

**“Iwe salama kwa Musa na Haruni! Hakika hivyo ndivyo Tunavyo-
walipa walio wema. Hakika wawili hao ni katika waja Wetu
walioamini.”**

* * *

وَإِنَّ إِلْيَاسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢٣﴾ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَلَا
 تَتَّقُونَ ﴿١٢٤﴾ أَتَدْعُونَ بَعْلًا وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ الْخَالِقِينَ
 اللَّهُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ﴿١٢٥﴾ فَكَذَّبُوهُ
 فَإِنَّهُمْ لَمُحْضَرُونَ ﴿١٢٦﴾ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿١٢٧﴾
 وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٢٨﴾ سَلَّمَ عَلَيَّ إِلَى يَأْسِينَ ﴿١٢٩﴾
 إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٠﴾ وَإِنْ لَوْطًا لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣١﴾ إِذْ نَجَّيْنَاهُ
 وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٣٢﴾ إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَابِرِينَ ﴿١٣٣﴾ ثُمَّ
 دَمَرْنَا الْآخَرِينَ ﴿١٣٤﴾ وَإِنَّا لَمَتَّمُونَ عَلَيْهِمْ مُصْحِحِينَ ﴿١٣٥﴾
 وَبِالْأَيْدِي أَمْثَلُ أَفْلا تَعْقِلُونَ ﴿١٣٦﴾ وَإِنَّ يُوسُفَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ
 ﴿١٣٧﴾ إِذْ أَبَقَ إِلَى الْفَلَكِ الْمَشْحُونِ ﴿١٣٨﴾ فَسَاهَمَ فَكَانَ
 مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٣٩﴾ فَالْتَقَمَهُ الْحَوْثُ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿١٤٠﴾
 فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٤١﴾ لَلَبِثَ فِي بَطْنِهِ إِلَى
 يَوْمٍ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٢﴾ * فَتَبَدَّنْهُ بِالْعَرَاءِ وَهُوَ سَقِيمٌ ﴿١٤٣﴾
 وَأُنبِئْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّنْ يَقْطِينٍ ﴿١٤٤﴾ وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَى مَائِدَةٍ
 أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٤٥﴾ فَامْتُوا فَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَى حِينٍ ﴿١٤٦﴾

وَإِنَّ إِلْيَاسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢٣﴾
 إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٢٤﴾
 أَتَدْعُونَ بَعْلًا وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ
 الْخَالِقِينَ ﴿١٢٥﴾ اللَّهُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ
 آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ﴿١٢٦﴾ فَكَذَّبُوهُ
 فَإِنَّهُمْ لَمُحْضَرُونَ ﴿١٢٧﴾ إِلَّا عِبَادَ
 اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿١٢٨﴾ وَتَرَكْنَا
 عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٢٩﴾ سَلَّمَ عَلَيَّ
 إِلَى يَأْسِينَ ﴿١٣٠﴾ إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي
 الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣١﴾ وَإِنْ لَوْطًا لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ
 ﴿١٣٢﴾ إِذْ نَجَّيْنَاهُ
 وَأَهْلَهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٣٣﴾ ثُمَّ
 دَمَرْنَا الْآخَرِينَ ﴿١٣٤﴾ وَإِنَّا لَمَتَّمُونَ
 عَلَيْهِمْ مُصْحِحِينَ ﴿١٣٥﴾ وَبِالْأَيْدِي
 أَمْثَلُ أَفْلا تَعْقِلُونَ ﴿١٣٦﴾ وَإِنَّ يُوسُفَ
 لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٣٧﴾ إِذْ أَبَقَ إِلَى
 الْفَلَكِ الْمَشْحُونِ ﴿١٣٨﴾ فَسَاهَمَ فَكَانَ
 مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٣٩﴾ فَالْتَقَمَهُ
 الْحَوْثُ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿١٤٠﴾ فَلَوْلَا
 أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٤١﴾ لَلَبِثَ
 فِي بَطْنِهِ إِلَى يَوْمٍ يُبْعَثُونَ ﴿١٤٢﴾ *
 فَتَبَدَّنْهُ بِالْعَرَاءِ وَهُوَ سَقِيمٌ ﴿١٤٣﴾
 وَأُنْبِئْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّنْ يَقْطِينٍ ﴿١٤٤﴾
 وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَى مَائِدَةٍ أَلْفٍ أَوْ
 يَزِيدُونَ ﴿١٤٥﴾ فَامْتُوا فَمَتَّعْنَاهُمْ
 إِلَى حِينٍ ﴿١٤٦﴾

123. Na hakika Ilyas bila ya shaka alikuwa miongoni mwa Mitume.

124. Alipowaambia watu wake: Hamuogopi?.

125. Mnamuomba Baa'li na mnamuacha Mbora wa waumbaji.

126. Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi Wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa zamani?

127. Wakamkadhibisha. Basi kwa hakika watahudhu rishwa.

128. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliosafishwa.

129. Na Tumemuachia (sifa nzuri) kwa waliokuja baadaye.

130. Iwe salama kwa Ilyas.

131. Hakika hivyo ndivyo Tunavyowalipa walio wema.

132. Hakika yeye ni katika waja Wetu walioamini.

Utajo wa Ilyasi عليه السلام.

Qatadah na Muhammad bin Ishaq walisema, "Ilyas ni jina jingine la Idris."¹ Ibn Abi Hatim رضي الله عنه amenukuu kuwa `Abdullah bin Mas`ud عنه رضي الله عنه alisema, "Ilyas ni Idris عليه السلام."² Hii ilikuwa pia rai ya Adh-Dhahhak.³ Wahb bin Munabbih alisema, "Ni Ilyas bin Yasin bin Finhas bin Al-`Izar bin Harun bin `Imran."⁴

Allah تعالى Alimtuma kwa Bani Israel baada ya Hizqil (Ezekiel), amani ziwaendee watu waliotumwa kwao. Walianza kuabudu sanamu lililoitwa *Baa`l*, na akawalingania kwa Allah تعالى, na akawakataza kumuabudu asiyekuwa Allah تعالى. Mfalme wao alimuamini, kisha akaritadi, na wakaendelea katika njia zao za upotovu, na hakuna hata mmoja wao aliyemuamini. Basi akamuomba Allah تعالى dhidi yao, na Allah تعالى Alizuia mvua dhidi yao kwa miaka mitatu. Wakamuomba awaondolee janga lao, na wakaahidi kuwa wangemuamini kama mvua ingewafikia. Akawaombea kwa Allah تعالى, na mvua ikanyesha, lakini wakaendelea na njia zao za ukafiri. Basi akamuomba Allah تعالى Amchukue Kwake. Al-Yasa` bin Akhtub alikulia chini ya ulezi wake, amani ziwaendee. Hivyo Ilyas aliamrisha aende mahali hapo, na kipando chochote kilichokuja kwake, alipaswa kukiendesha, sio kukiacha. Farasi wa moto aliletwa kwake, akamuendesha, na Allah تعالى Alimvalisha nuru na kumfunika kwa manyoya, na alikuwa akipaa pamoja na malaika kama vile mwanadamu wa kimalaika, wa mbinguni na ardhini. Hayo yamesimuliwa na Wahb bin Munabbih kutoka kwa Watu Waliopewa Kitabu; Allah تعالى Anajua zaidi ukweli wa hayo.

¹ At-Tabari 21:95.

² Al-Qurtubi 15:115.

³ At-Tabari 21:97.

⁴ At-Tabari 21:97.

إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ أَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٢٤﴾

“Alipowaambia watu wake: Hamuogopi?”

Yaani, ‘hamumuogopi Allah تعالى mnapowaabudu wasiokuwa Yeye.’

أَتَدْعُونَ بَعْلًا وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ الْخَلْقِينَ ﴿١٢٥﴾

“Mnamuomba Baa’li na mnamuacha Mbora wa waumbaji.”

Ibn `Abbas, Mujahid, `Ikrimah, Qatadah na As-Suddi walisema kuwa maana ya neno *Ba`l* ni mola mlezi.¹ `Ikrimah na Qatadah walisema, “Hii ni lugha ya watu wa Yemen.”² Kwa mujibu wa masimulizi mengine kutoka kwa Qatadah, ni lugha ya Azd Shanu’ah.³ `Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisimulia kutoka kwa baba yake kuwa ni jina la sanamu lililoabudiwa na watu wa mji ulioitwa *Ba`labak* (Baalbek) uliokuwepo upande wa magharibi mwa Damaskasi.⁴ Adh-Dhahhak alisema, “Ni sanamu walilokuwa wakiliabudu.”⁵

أَتَدْعُونَ بَعْلًا

“Mnamuomba Baa’li...” Yaani, ‘mnaabudu sanamu,’

وَتَذَرُونَ أَحْسَنَ الْخَلْقِينَ ﴿١٢٥﴾ اللَّهُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ﴿١٢٦﴾

“...na mnamuacha Mbora wa waumbaji, Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa zamani?”

Yaani, ‘Yeye Ndiye Pekee Mwenye Kustahiki kuabudiwa, bila ya washirika.’

فَكَذَّبُوهُ فَأَنجَبُوا لَهُمْ لِمُحْضَرُونَ ﴿١٢٧﴾

“Wakamkadhibisha. Basi kwa hakika watahudhurishwa.”

Yaani, kwa ajili ya adhabu hiyo katika Siku ya Hesabu.

¹ At-Tabari 21:96.

² At-Tabari 21:96.

³ *Ad-Dur Al-Manthur* 7:119.

⁴ At-Tabari 21:97.

⁵ At-Tabari 21:97.

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿١٢٣﴾

“Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu...”

Yaani, wenye kumuamini Yeye Peke Yake.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ ﴿١٢٤﴾

“Na Tumemuachia (sifa nzuri) kwa waliokuja baadaye.”

Yaani, mwenye sifa njema na kutukuzwa.

سَلَّمَ عَلَيَّ إِلَىٰ يَأْسِينَ ﴿١٢٥﴾

“Iwe salama kwa Ilyas.”

Kadhalika, mtu anaweza kusema kuhusu Isma`il عليه السلام, Isma`in. Hii ni lugha (lahaja) ya Bani Asad; wao husema Mikal, Mika'il, na Mika'in. Wanasema Ibrahim عليه السلام na Ibrahim; Isra'il, Isra'in; Tur Sina', Tur Sinin. Yote hayo ni sawa.

إِنَّا كَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٦﴾ إِنَّهُ مِن عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٧﴾

“Hakika hivyo ndivyo Tunavyowalipa walio wema. Hakika yeye ni katika waja wetu waumini.”

Tumeshaeleza maana yake hiyo hapo juu.¹ Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

وَإِنَّ لُوطًا لِّمَنِ الْمُرْسَلِينَ ﴿١٢٨﴾ إِذْ جَاءَتْهُ وَأَهْلُهُ أَجْمَعِينَ ﴿١٢٩﴾ إِلَّا عَجُوزًا فِي الْغَيْرِينَ ﴿١٣٠﴾

ثُمَّ دَمَرْنَا الْآخِرِينَ ﴿١٣١﴾ وَإِنكُم لَتَمُرُونَ عَلَيْهِمْ مُّصْبِحِينَ ﴿١٣٢﴾ وَيَالَيْلِ ۗ أَفَلَا

تَعْقِلُونَ ﴿١٣٣﴾

133. Na hakika Lut'i bila ya shaka ni miongoni mwa Mitume.

134. Tulipomwokoia yeye na watu wake wote.

135. Isipokuwa mwanamke mkongwe ambaye ni miongoni mwa wale waliobakia nyuma.

¹ Angalia Surat As-Saffat (37:80-81).

136. Kisha Tukawaangamiza wale wengineo.

137. Na hakika nyinyi mnawapitia wakati wa asubuhi.

138. Na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?

Utajo wa Kuangamizwa Watu wa Lut عليه السلام

Allah تعالى Anatuambia kuwa alimtuma mja na Mtume Wake Lut عليه السلام, kwa watu wake, na walimkataa, hivyo Allah تعالى Alimuokoa kutoka miongoni mwao, yeye na familia yake isipokuwa mkewe, aliyeangamizwa pamoja na watu wake. Allah تعالى Aliwaangamiza kwa adhabu za namna mbalimbali, na sehemu yao Akaigeuza kuwa ziwa la kuchukiza, lenye kunuka vibaya katika njia ya msafara uliopitwa sana na watu ambapo watu wanapita usiku na mchana. Yaani, Bahari ya Mauti, ambayo iko jirani na miji ya Sodom na Gomorrah katika njia kuu baina ya Uarabuni na Syria. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنكُمۡ لَتَمۡرُونَ عَلَیۡهِمۡ مُّصۡبِحِينَ ﴿١٣٧﴾ وَيَالۡلِیۡلِ أَفَلَا تَعۡقِلُونَ ﴿١٣٨﴾

“Na hakika nyinyi mnawapitia wakati wa asubuhi, na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?”

Yaani, ‘hamjifunzi kutokana nao na jinsi Allah تعالى Alivyowaangamiza, na kutambua kuwa mwisho kama huo unawangojea makafiri.’

وَإِنۡ یُوۡسُسَ لَعِنَ ٱلۡمُرۡسَلِیۡنَ ﴿١٣٦﴾ إِذۡ أَبۡقَىٰ إِلَى ٱلۡفَلَکِ ٱلۡمَشۡحُونِ ﴿١٣٧﴾ فَسَاهَمَ فَكَانَ مِنَ ٱلۡمُدۡحَضِیۡنَ ﴿١٣٨﴾ فَٱلتَّقَمَهُ ٱلۡحَوۡثُ وَهُوَ مُلِیۡمٌ ﴿١٣٩﴾ فَلَوۡلَا أَنۡهُ كَانَ مِنَ ٱلۡمُسۡبِحِیۡنَ ﴿١٤٠﴾ لَلَّیۡثَ فِی بَطۡنِہَا إِلَىٰ یَوۡمِ یُبۡعَثُونَ ﴿١٤١﴾ * فَتَبَدَّنہٗ بِٱلۡعَرَّاءِ وَهُوَ سَقِیۡمٌ ﴿١٤٢﴾ وَأُنۡبِتۡنَا عَلَیۡہِ شَجَرَةً مِّنۡ یَقۡطِیۡنَ ﴿١٤٣﴾ وَأَرۡسَلۡنَہٗ إِلَىٰ مِائَةِ ٱلۡأَلۡفِ أَوْ یَزِیۡدُونَ ﴿١٤٤﴾ فَفَٱمَنُوا فَتَعَنۡتَهُمۡ إِلَىٰ حَیۡنَ ﴿١٤٥﴾

139. Na hakika Yunus alikuwa miongoni mwa Mitume.

140. Alipokimbia katika jahazi liliosheheni.

141. **Akaingia katika kupigiwa kura, na akawa katika walioshindwa.**
142. **Samaki akammeza hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa.**
143. **Na ingelikuwa hakuwa katika wanaomtakasa Mwenyezi Mungu.**
144. **Bila ya shaka angelikaa ndani yake mpaka siku ya kufufuliwa.**
145. **Lakini Tulimtupa ufukweni patupu, hali yu mgonjwa.**
146. **Na Tukauotesha juu yake mmea wa kabila ya mung'unye.**
147. **Na Tulimtuma kwa (watu) laki moja au zaidi.**
148. **Basi wakaamini, na Tukawastarehesha kwa muda**

Utajo wa Kisa cha Yunus عليه السلام

Tumeshaeleza kisa cha Yunus عليه السلام, katika Surat Al-Anbiya' (21:87-88). katika Sahihi Mbili alisimulia, Mtume ﷺ alisema:

«مَا يَتَّبِعِي لِعَبْدٍ أَنْ يَقُولَ: أَنَا خَيْرٌ مِنْ يُونُسَ بْنِ مَتَّى»

"Haimfai mtu kusema: 'mimi ni bora kuliko Yunus bin Matta.'¹

إِذْ أَبَقَ إِلَى الْفُلِّ الْمَشْحُونِ ﴿١٠١﴾

"Alipokimbia katika jahazi liliosheheni."

Ibn `Abbas رضي الله عنهما, alisema, "ilisheheni mzigo."

فَسَاهَمَ

"Akaingia katika kupigiwa kura."

Yaani, wakapiga kura.²

¹ Fat'h Al-Bari 4:193, Muslim 4:1846.

² At-Tabari 21:106.

فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِينَ

“...na akawa katika walioshindwa.”

Yaani katika walioshindwa. Hii ilikuwa kwa sababu meli ilipigwa na mawimbi kutokea pande zote, na walikuwa katika hatari ya kuzama maji, wakapiga kura, na mwenye kuangukiwa na kura alipaswa kutupwa majini ili kupunguza uzito. Mtume wa Allah Yunus عليه السلام, aliangukiwa na kura mara tatu, lakini hawakutaka kumtupa majini. Akavua nguo zake ili ajirushe mwenyewe baharini, wakajaribu kumzuia. Allah تعالى Alimuamuru nyangumi kutoka Bahari ya Kijani (yaani, Bahari ya Kati au Mediterranean) apasue bahari hizo na kummeza Yunus عليه السلام, bila ya kumkata nyama au kumvunja mfupa. Nyangumi alikuja na Yunus عليه السلام, akaruka kutoka katika meli, na nyangumi huyo akammeza na kuondoka naye, huku akisafiri pamoja naye katika bahari zote. Yunus عليه السلام alipobakia tumboni mwa nyangumi huyo kwa muda, alidhania kuwa alishafariki; basi, akatikisa kichwa chake, miguu na mikono, na kujiona kuwa alikuwa angali hai. Akaomba dua tumboni mwa nyangumi, na miongoni mwa aliyoyasema katika dua yake kuu yalikuwa: “Mola Wangu Mlezi, nimepafanya mahali pa kukuabudu ambapo hakuna mtu yeyote aliyepata kufika.” Wanatofautiana juu ya muda aliopitisha tumboni mwa nyangumi huyo. Wapo waliosema siku tatu; hii ilikuwa rai ya Qatadah. Wengine walisema siku saba; hii ilikuwa rai ya Ja'far As-Sadiq رحمه الله تعالى. Baadhi yao walisema siku arobaini; hii ilikuwa rai ya Abu Malik.¹ Mujahid alisema, akisimulia kutoka kwa Ash-Sha'bi, “Alimmeza katika wakati wa asubuhi na kumtema wakati wa jioni.” Allah تعالى Anajua zaidi muda huo. Kauli ya Allah تعالى,

فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ ﴿١٢٣﴾ لَلَّيْتَ فِي بَطْنِهِ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٢٤﴾

**“Na ingelikuwa hakuwa katika wanaomtakasa Mwenyezi Mungu,
Bila ya shaka angelikaa ndani yake mpaka siku ya kufufuliwa.”**

Ilisemekana kuwa, kama asingekuwa amefanya amali njema wakati wa maisha yake ya faraja. Hii ilikuwa rai ya Adh-Dhahhak bin Qays, Abu Al-'Aliyah, Wahb bin Munabbih, Qatadah na wengine,² na ilikuwa rai iliyopendelewa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³

¹ At-Tabari 21:111.

² At-Tabari 21:108, 109.

³ At-Tabari 21:108.

Hicho ndicho kilichoashiriwa katika Hadith kama itakuwa Sahihi tunayoinukuu hapa chini, *Inshaallah*.

Katika Hadithi iliyosimuliwa kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, alisema:

«تَعْرِفُ إِلَى اللَّهِ فِي الرَّخَاءِ، يَعْرِفُكَ فِي الشَّدَّةِ»

“Mkumbuke Allah katika wakati wa faraja na Atakukumbuka katika wakati wa dhiki.”¹

Na ilisemwa kuwa kilichomaanishwa na Aya:

﴿فَلَوْلَا أَنَّهُ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِينَ﴾

“Na ingelikuwa hakuwa katika wanaomtakasa Mwenyezi Mungu,”

Ilikuwa maana ya Aya ifuatayo:

﴿فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ﴾
﴿فَأَسْتَجِبْنَا لَهُ وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْغَمِّ وَكَذَلِكَ نُخَيِّبُ الْمُؤْمِنِينَ﴾

“Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu. Basi Tukamuitikia na Tukamuokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo Tunavyowaokoa Waumini.” (21:87-88).

Hii ilikuwa rai ya Sa'id bin Jubayr na wengine.⁴

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى amenukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema-na sijui chochote kilichosimuliwa kutoka kwa Anas رضي الله عنه ambayo hakikunasibishwa kwa Mtume ﷺ:

«إِنَّ يُونُسَ النَّبِيَّ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ حِينَ بَدَأَ لَهُ أَنْ يَدْعُوَ بِهَذِهِ الْكَلِمَاتِ وَهُوَ فِي بَطْنِ الْحُوتِ فَقَالَ: اللَّهُمَّ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ، فَأَقْبَلَتْ الدَّعْوَةَ تَحْفًا بِالْعَرْسِ، قَالَتِ الْمَلَائِكَةُ: يَا رَبِّ هَذَا صَوْتُ ضَعِيفٍ مَعْرُوفٍ مِنْ

¹ Ahmad 1:307.

² At-Tabari 21:110.

بِلَادٍ بَعِيدَةٍ غَرِيبَةٍ فَقَالَ اللَّهُ تَعَالَى: أَمَا تَعْرِفُونَ ذَلِكَ؟ قَالُوا: يَا رَبِّ وَمَنْ هُوَ؟ قَالَ
عَزَّ وَجَلَّ: عَبْدِي يُونُسُ، قَالُوا: عَبْدُكَ يُونُسُ الَّذِي لَمْ يَزَلْ يُزْفَعُ لَهُ عَمَلٌ مُتَمَبِّلٌ
وَدَعْوَةٌ مُسْتَجَابَةٌ؟ قَالُوا: يَا رَبِّ أَوْلَا نَرْحَمُ مَا كَانَ يَضَعُ فِي الرَّخَاءِ فَتَنْجِيهِ فِي
الْبَلَاءِ، قَالَ: بَلَى، فَأَمَرَ الْحَوْتَ فَطَرَحَهُ بِالْعَرَاءِ»

“Nabii Yunus alipoanza kumuomba Allah kwa maneno haya alipokuwa katika tumbo la nyangumi, alisema, ‘Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.’ Wito huu ulikwenda na kuzunguka Kiti cha Enzi, na malaika wakasema, “Ewe Mola Mlezi, hii ni sauti ya mtu dhaifu lakini anayejulikana kutoka ardhi ngeni ya mbali. Allah, Mtukuka Akawauliza, “Mnayajuaje hayo.” Wakasema, “Ewe Mola Wetu Mlezi, ni nani huyo?” Allah Akasema, “Mja wangu Yunus.” Wakasema, “Mja wako Yunus, ambaye amali zake zilidumu kuinuliwa na kukubaliwa na dua zenye kujibiwa!” Wakasema, “Ewe Mola Mlezi, Je humrehemu kwa aliyoyafanya katika wakati wake wa faraja, na kumuokoa kutoka katika balaa hili.” Akasema, “Ndivyo.” Akamuamuru nyangumi, na akamtupa katika ufukwe mtupu.”¹

Kauli ya Allah تعالى:

فَتَبَدَّنَهُ

“Lakini Tulimtupa...”

Maana yake, ‘Tulimtupa nje,’

بِالْعَرَاءِ

“...ufukweni patupu,”

Ibn `Abbas رضي الله عنهما, na wengine walisema kuwa inamaanisha ardhi ambayo haikuwa na mimea wala majengo.

وَهُوَ سَقِيمٌ

“...hali yu mgonjwa.” Yaani, alikuwa mdhaifu kimwili,

¹ At-Tabari 21:109. Isnadi yake ni dhaifu.

وَأُنَبِّتْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّنْ يَقْطِينٍ ﴿١٢٤﴾

“Na Tukauotesha juu yake mmea wa kabila ya mung’unye.”

Ibn Mas’ud na Ibn ‘Abbas, Mujahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, Wahb bin Munabbih, Hilal bin Yasaf, ‘Abdullah bin Tawus, As-Suddi, Qatadah, Adh-Dhahhak, ‘Ata’ Al-Khurasani na wengine kadhaa رضي الله عنهم, walisema kuwa mung’unya ni boga.¹

Wengine walisema kuwa mung’unya lina manufaa mengi: hukua kwa haraka na kutanda kwa sababu ya ukubwa wake na ulaini, wadudu huwa hawalisogelei, na matunda yake ni chakula kizuri; yanaweza kuliwa yakiwa mabichi au yaliyopikwa, na nyama ya tunda hilo na ganda vinaweza kuliwa. Imesimuliwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa akipenda mamung’unya na alikuwa akiyafuata katika sahani ya chakula.²

وَأَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ مِائَةِ أَلْفٍ أَوْ يَزِيدُونَ ﴿١٢٥﴾

“Na Tulimtuma kwa watu laki moja au zaidi.”

Ni kama vile alikuwa akimuamuru, baada ya kutoka katika tumbo la samaki, kurejea kwa watu aliotumwa kwao hapo awali.

أَوْ يَزِيدُونَ

“...au zaidi.”

Mak’hul alisema, “Idadi yao likuwa laki moja na kumi elfu. Haya yalisimuliwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Baadhi ya wanazuoni wa Kiarabu, watu wa Basrah, walisema kuwa inamaanisha ni mpaka laki moja au zaidi.”³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliitafsiri Aya hii kama alivyotafsiri Aya:

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوبُكُمْ مِّنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَهِيَ كَالْحِجَارَةِ أَوْ أَشَدُّ قَسْوَةً

“Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi.” (2:74),

¹ At-Tabari 21:113 na 114, Ad-Dur Al-Manthur 7:130, 131.

² Al-Bukhari na. 2092.

³ At-Tabari 21:116.

إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً

“...mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumuogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi.” (4:77), na

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٥٣﴾

“Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi.” (53:9).

Yaani, si chini ya hapo, bali zaidi.

فَقَامُوا

“Basi wakaamini.”

Yaani, watu hawa ambao Yunus عليه السلام alitumwa kwao, walisilimu wote.

فَقَامُوا فَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ

“...na Tukawastarehesha kwa muda.”

Yaani, mpaka muda wao ulioteuliwa uishe. Hayo ni sawa na Aya,

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَنفَعَهَا إِيمَنُهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ ءَعْدَابَ

الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

“Kwa nini usiwepo mji mmoja ukaamini na Imani yake ikawafaa - isipokuwa kaumu Yunus? Waliamini na Sisi Tukawaondolea adhabu ya hizaya katika maisha ya dunia, na Tukawastarehesha kwa muda.” (10:98)

* * *

فَاسْتَفْتِهِمْ أَلِرَبِّكَ الْبَنَاتُ وَلَهُمُ الْبُنُونَ ﴿١٤٩﴾ أَمْ خَلَقْنَا
 الْمَلَائِكَةَ إِنثًا وَهُمْ شَاهِدُونَ ﴿١٥٠﴾ أَلَا لَهُمْ مِنْ
 إِبْرَاهِيمَ لَيَقُولُونَ ﴿١٥١﴾ وَلَدَ اللَّهِ وَإِثْمَ لَكَذِبُونَ ﴿١٥٢﴾
 أَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى الْبَنِينَ ﴿١٥٣﴾ مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ
 ﴿١٥٤﴾ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٥٥﴾ أَمْ لَكُمْ سُلْطٰنٌ مُّبِينٌ ﴿١٥٦﴾
 فَأْتُوا بِكِتَابِكُمْ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٥٧﴾ وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ
 آلِجَنَّةِ نَسْبًا ۖ وَلَقَدْ عَلِمْتِ الْإِنثَةَ إِثْمًا لَمْ حَضَرُونَ ﴿١٥٨﴾
 سُبْحٰنَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿١٥٩﴾ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ
 ﴿١٦٠﴾ فَإِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ ﴿١٦١﴾ مَا أَنتُمْ عَلَيْهِ بِفَاعِلِينَ ﴿١٦٢﴾
 إِلَّا مَنْ هُوَ صَالٍ الْجَحِيمِ ﴿١٦٣﴾ وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ
 مَّعْلُومٌ ﴿١٦٤﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ الصَّافُونَ ﴿١٦٥﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ
 الْمُسْتَحُونَ ﴿١٦٦﴾ وَإِن كَانُوا لَيَقُولُونَ ﴿١٦٧﴾ لَوْ أَنَّ عِندَنَا
 ذِكْرًا مِّنَ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦٨﴾ لَكُنَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿١٦٩﴾
 فَكْفَرُوا بِهِ ۖ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿١٧٠﴾ وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا
 لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧١﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنصُورُونَ ﴿١٧٢﴾ وَإِن
 جُنَدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿١٧٣﴾ فَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿١٧٤﴾
 وَأَبْصَرَهُمْ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿١٧٥﴾ أَفَعِدَّائِنَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٧٦﴾
 فَإِذَا نَزَلَ بِسَاحَتِهِمْ فَسَاءَ صَبَاحُ الْمُنذَرِينَ ﴿١٧٧﴾ وَتَوَلَّ
 عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿١٧٨﴾ وَأَبْصَرَ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿١٧٩﴾
 سُبْحٰنَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٨٠﴾ وَسَلٰمٌ عَلَى
 الْمُرْسَلِينَ ﴿١٨١﴾ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٨٢﴾

فَاسْتَفْتَيْهِمْ أَلِرَبِّكَ الْبَنَاتُ وَلَهُمْ
 الْبُنُونَ ﴿١٤٩﴾ أَمْ خَلَقْنَا
 الْمَلَائِكَةَ إِنثًا وَهُمْ شَاهِدُونَ
 ﴿١٥٠﴾ أَلَا لَهُمْ مِنْ
 إِبْرَاهِيمَ لَيَقُولُونَ ﴿١٥١﴾
 وَلَدَ اللَّهِ وَإِثْمَ
 لَكَذِبُونَ ﴿١٥٢﴾
 أَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى
 الْبَنِينَ ﴿١٥٣﴾ مَا لَكُمْ
 كَيْفَ تَحْكُمُونَ
 ﴿١٥٤﴾ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ
 ﴿١٥٥﴾ أَمْ لَكُمْ
 سُلْطٰنٌ مُّبِينٌ ﴿١٥٦﴾
 فَأْتُوا
 بِكِتَابِكُمْ إِن كُنْتُمْ
 صَادِقِينَ ﴿١٥٧﴾
 وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ
 آلِجَنَّةِ نَسْبًا ۖ وَلَقَدْ
 عَلِمْتِ الْإِنثَةَ
 إِثْمًا لَمْ حَضَرُونَ ﴿١٥٨﴾
 سُبْحٰنَ اللَّهِ عَمَّا
 يُصِفُونَ ﴿١٥٩﴾ إِلَّا

149. Basi waulize: Ati Mola Wako Mlezi ndiye mwenye watoto wa kike, na wao wanao watoto wa kiume?

150. Au Tumewaumba Malaika kuwa ni wanawake, na wao wakashuhudia?

151. Tambueni ni kwa uzushi wao ndio wanasema:

152. Mwenyezi Mungu Amezaa! Ama hakika bila ya shaka hao ni waongo!

153. Ati amekhiari watoto wa kike kuliko wanaume?

154. Mna nini? Mnahukumu vipi nyinyi?

155. Hamkumbuki?

156. Au mnayo hoja iliyo wazi?

157. Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.

158. Na wameweka mahusiano ya nasaba baina yake na majini; na majini wamekwishajua bila ya shaka kuwa wao watahudhurishwa.

159. Subhana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomsingizia.

160. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliosafishwa.

Kujibiwa Wenye Kumnasibishia Allah تعالی Watoto wa Kiume na kusema kuwa Malaika ni Binti Zake

Allah تعالی Anawakanushia washirikina wenye kumnasibishia mabinti - na wao kujinasibishia walivyovipenda, yaani, walitaka watoto wa kiume kwa ajili yao.

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٥٨﴾

“Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki.” (16:58),

Yaani, hilo lilimfadhaisha, na alijichagulia watoto wa kiume tu. Allah تعالی Anasema: ‘Basi wanawezaje kumnasibishia Allah fungu wasilojichagulia wenyewe.’ Kauli ya Allah تعالی:

فَأَسْتَفْتِيهِمْ

“Basi waulize...”

Yaani, waulize kwa namna ya kukanusha,

أَلرَّبِّكَ أَلْبَنَاتُ وَلَهُمُ أَلْبُنُورٌ

“Ati Mola Wako Mlezi ndiye mwenye watoto wa kike, na wao wanao watoto wa kiume?”

Hii ni sawa na Aya:

أَلْكُمُ أَلذِّكْرُ وَلَهُ أَلْأُنثَىٰ ﴿١٧﴾ تَلْكَ إِذًا فِسْمَةٌ ضِيزَىٰ ﴿١٨﴾

“Je! Nyinyi mnao watoto wa kiume na Yeye ndio Awe na wa kike? Huo ni mgawanyo wa dhulma!” (53:21-22).

أَمْ خَلَقْنَا أَلْمَلٰٓئِكَةَ إِنثًا وَهُمْ شٰهِدُونَ ﴿٢٠﴾

“Au Tumewaumba Malaika kuwa ni wanawake, na wao wakashuhudia?”

Yaani, wamekataje shauri kuwa malaika ni wa kike ilhali hawakushuhudia uumbwaji wao. Hii ni sawa na Aya:

وَجَعَلُوا أَلْمَلٰٓئِكَةَ أَلَّذِينَ هُمْ عِبْدُ أَلرَّحْمٰنِ إِنثًا ؕ أَشٰهَدُوا خَلْقَهُمْ ؕ سَتُكْتَبُ شٰهَدٰتُهُمْ
وَيُسْأَلُونَ ﴿٢١﴾

“Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake! Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wao watahojiwa!” (43:19),

Ambayo inamaanisha, wataulizwa kuhusu hilo katika Siku ya Kiama.

أَلَّا إِلٰهَ مِنۢ بَدَدِهِم

“Ati ni kwa uzushi wao...”

Yaani, ni sehemu ya uongo wao.

لَيَقُولُونَ ﴿٢٢﴾ وَلَدَ أَللّٰهُ

“...ndio wanasema: Mwenyezi Mungu Amezaa!”

Yaani, ana mtoto.

وَأَيْتَهُمْ لَكَذِبُونَ

“Ama hakika bila ya shaka hao ni waongo!”

Allah تعالى Anataja mambo matatu kati ya waliyoyasema kuhusu malaika, yaliyowatia katika kufuru kubwa zaidi na upotovu. Walisema kuwa walikuwa mabinti wa Allah na kwamba Allah تعالى Alikuwa na watoto - *Subhanallah*. Kisha watoto hao wakawafanya kuwa ni wanawake, halafu wakawaabudu badala ya Allah تعالى – kauli zao hizo ingetosha kuwapa adhabu ya kukaa Jahanamu milele. Kisha Allah تعالى Anasema, kwa Kuwakanushia:

أَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى الْبَنِينَ ﴿٣٧﴾

“Amechagua watoto wa kike kuliko wa kiume?”

Yaani, kipi kingemfanya achague mabinti badala ya watoto wa kiume. Hii ni sawa na Aya,

أَفَأَصْفَنكُمْ رَبُّكُمْ بِالْبَنِينَ وَاتَّخَذَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِنْتِثًا إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿١٧﴾

“Je! Mola wenu Mlezi Amekuteulieni wavulana, na Yeye Akawafanya Malaika ni banati zake? Kwa hakika nyinyi mnasema usemi mkubwa.” (17:40)

Kauli ya Allah تعالى:

مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿١٨﴾

“Mna nini? Mnahukumu vipi nyinyi?”

أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٩﴾ أَمْ لَكُمْ سُلْطٰنٌ مُّبِينٌ ﴿٢٠﴾

“Hamkumbuki? Au mnayo hoja iliyo wazi?” Inayothibitisha madai yenu.’

فَأْتُوا بِكِتٰبِكُمْ إِن كُمْ صٰدِقِينَ ﴿٢١﴾

“Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.”

Yaani, leteni ushahidi wa hilo kutoka katika Kitabu kilichoteremshwa na Allah, ili kuthibitisha kuwa mnayoyasema (yaani, watoto). Madai yenu hayana mantiki hata kidogo.’

وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجَنَّةِ نَسَبًا

“Na wameweka mahusiano ya nasaba baina yake na majini.”

Mujahid alisema, “Washirikina walisema kuwa malaika walikuwa mabinti wa Allah. Abubakr رضي الله عنه, alisema, ‘Basi mama zao ni kina nani?’ Wakajibu, ‘Mabinti wa wakuu wa Majini.’”¹ Oatadah na Ibn Zayd pia walisema hayo. Allah تعالى Anasema:

وَلَقَدْ عَلِمْتِ الْجِنَّةُ

“...na majini wamekwishajua...”

Yaani, walionasibishiwa hayo,

إِنَّهُمْ لَمُحْضَرُونَ

“...bila ya shaka kuwa wao watahudhurishwa.”

Yaani, kuwa wenye kusema kuwa watahudhurishwa kwa ajili ya adhabu katika Siku ya Kiama, kwa sababu ya uongo na upotovu waliotamka bila ya elimu.

سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ

“Subhana ‘Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayomsingizia.”

Yaani, Mtukufu, Ametakasika na Ameepukana mbali na jambo la kuwa na watoto na Ametakasika dhidi ya madhalimu.

إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ

“Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliosafishwa.”

Kiwakilishi nomino katika kitenzi kinatafsirika kama “wanaonasibisha” ni watu wote, halafu Allah Anawatoa katika upotofu huo baadhi ya watu wanaofuata ukweli aliopteremshiwa kila Mtume aliyetumwa.

¹ At-Tabari 21:121.

فَإِنْكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ بِفِتْنِينَ ﴿٣٨﴾ إِلَّا مَنْ هُوَ صَالٍ الْجَحِيمِ ﴿٣٩﴾
 وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿٤٠﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ الصَّافُونَ ﴿٤١﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ الْمُسَبِّحُونَ ﴿٤٢﴾
 وَإِن كَانُوا لَيَقُولُونَ ﴿٤٣﴾ لَوْ أَنَّ عِنْدَنَا ذِكْرًا مِنَ الْأُولِينَ ﴿٤٤﴾ لَكُنَّا عِبَادَ اللَّهِ
 الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٥﴾ فَكَفَرُوا بِهِ ۖ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٤٦﴾

161. Basi hakika nyinyi na mnaowaabudu.

162. Hamuezi kuwapoteza.

163. Isipokuwa wale watakaoingia Motoni.

164. Na hapana katika sisi (Malaika) ila anapo mahali pake maalumu.

165. Na hakika bila ya shaka sisi ndio wajipangao safu.

166. Na hakika sisi ndio wenye kusabihi na kutakasa.

167. Na walikuwapo waliokuwa wakisema:

168. Tungelikuwa na Ukumbusho kama wa watu wa zamani,

169. Bila ya shaka tungelikuwa ni waja wa Mwenyezi Mungu wenye ikhlasi.

170. Lakini waliukataa. Basi watakuja kujua.

Hakuna Anayeamini Maneno ya Washirikina Isipokuwa Ambao ni Wapotevu Zaidi Yao

Kauli ya Allah تعالى, kuwaambia washirikina:

فَإِنْكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ بِفِتْنِينَ ﴿٣٨﴾ إِلَّا مَنْ هُوَ صَالٍ الْجَحِيمِ ﴿٣٩﴾

“Basi hakika nyinyi na mnaowaabudu. Hamuezi kuwapoteza, Isipokuwa yule atakayeingia Motoni.

Yaani, ‘wale tu watakaoamini Tunachosema na watakaofuata njia zenu potofu za ibada potovu ni wale waliopotoka zaidi kuliko nyinyi na wameumbwa kwa ajili ya Jahannamu.’

هُم قُلُوبٌ لَا يَفْقَهُونَ بِهَا وَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَهُمْ أَعْيُنٌ لَا يُبْصِرُونَ بِهَا وَأُولَئِكَ كَالَّذِينَ نَجَّيْنَا مِنْهُمُ الضُّلُوكَ وَالَّذِينَ كَانُوا يُصَلُّونَ بِخَيْرٍ وَأُولَئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٩﴾

“Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika.” (7:179).

Huu ni mfano wa watu wanaofuata imani na fikra za ushirikina, kufuru na upotevu, sawa na Kauli ya Allah تعالى:

إِن كُنتُمْ لِي قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ﴿٥١﴾ يُؤَفِّكُ عَنْهُ مَنَافِكُ ﴿٥٢﴾

“Hakika nyinyi bila ya shaka mmo katika kauli inayokhitalifiana. Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.” (51:8-9)

Yaani, hakika si vingine anapotea yule aliyegeuzwa na akakanusha haki.

Hadhi ya Malaika na Kumtukuza kwao Allah تعالى Wakiwa katika Safu

Kisha Allah تعالى Akasema katika Kuwaepusha malaika kuwa katika nafasi waliyonasibishiwa na wale waliowakufuru na kuwazushia uongo – kuwa wao ni mabinti wa Allah -

وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٤٩﴾

“Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu.”

Yaani, kila mmoja ana mahali pake mbinguni na katika mahali pa ibada, ambako hakiuki. Adh-Dhahhak alisema katika *Tafsir* yake:

وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٤٩﴾

“Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu.”

Masruq alikuwa akisimulia kuwa ‘A’ishah رضي الله عنها alisema, ‘Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنَ السَّمَاءِ الدُّنْيَا مَوْضِعٌ إِلَّا عَلَيْهِ مَلَكٌ سَاجِدٌ أَوْ قَائِمٌ»

“Hakuna mahali katika mbingu ya dunia isipokuwa kuna malaika mwenye kusujudu au mwenye kusimama.”

Hicho ndicho Anachoeleza Allah تعالى:

وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٤٩﴾

“Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu.”¹

Imesimuliwa kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Miongoni mwa mbingu, ipo ambayo hakuna mahali pa ukubwa wa shubiri moja (nchi tisa) isipokuwa kuna paji la uso au mguu wa malaika juu yake.” Kisha akasoma:

وَمَا مِنَّا إِلَّا لَهُ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٥٠﴾

“Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu.”²

Kadhalika Sa’id bin Jubayr alisema:

وَإِنَّا لَنَحْنُ الصَّافُونَ ﴿١٥١﴾

“Na hakika bila ya shaka sisi ndio wajipangao safu.”

Yaani, tunasimama katika safu ili kufanya ibada, kama tulivyoeleza katika Aya,

وَالصَّافَّةِ صَافًا ﴿١٥٢﴾

“Naapa kwa wanaojipanga kwa safu.”

Abu Nadhrah alisema, “Iliposomwa *Iqamah*, `Umar رضي الله عنه, alikuwa akiwageukia watu na kusema: `Nyoosheni safu zenu, kwa kuwa Allah Anakutakeni mfuatae muongozo wa malaika.’ Kisha akasoma,

وَإِنَّا لَنَحْنُ السَّيِّحُونَ ﴿١٥٣﴾

“Na hakika bila ya shaka sisi ndio wajipangao safu.”

‘Sogea nyuma, ewe fulani, sogea mbele, ewe fulani.’ Halafu alikwenda mbele na kusema ‘*Allahu Akbar*’ Haya yameandikwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.³

¹ At-Tabari 21:127.

² At-Tabari 21:127.

³ At-Tabari 21:128.

Katika Sahih Muslim kumesimuliwa kuwa Hudhayfah رضي الله عنه, alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«فُضِّلْنَا عَلَى النَّاسِ بِثَلَاثٍ: جُعِلَتْ صُفُوفُنَا كَصُفُوفِ الْمَلَائِكَةِ، وَجُعِلَتْ لَنَا الْأَرْضُ مَسْجِدًا، وَتُرْبَتُهَا طَهُورًا»

*"Tumefadhilishwa juu ya watu kwa namna tatu: safu zetu zimefanywa kama safu za malaika; ardhi yote imefanywa Masjid kwa ajili yetu; na mchanga wake kitoharisha, yatakapokosekana maji."*¹

وَإِنَّا لَنَحْنُ الْمُسَبِّحُونَ ﴿٣٧﴾

"Na hakika sisi ndio wenye kusabihi na kutakasa."

Yaani, 'tunajipanga safu na kumtukuza Mola Mlezi, Kumsifu, Kumsabihi na Kumtakasa mbali na dosari na mapungufu. Sisi ni waja Wake na tunamhitaji na kumnyenyekea.'

Quraysh Walitamani Wangukuwa na Utajo katika Waliotangulia

Kauli ya Allah تعالى hapa:

وَإِنْ كَانُوا لَيَقُولُونَ ﴿٣٨﴾ لَوْ أَنَّ عِنْدَنَا ذِكْرًا مِنَ الْأُولِينَ ﴿٣٩﴾ لَكُنَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٠﴾

"Na walikuwapo waliokuwa wakisema: Tungelikuwa na Ukumbusho kama wa watu wa zamani. Bila ya shaka tungelikuwa ni waja wa Mwenyezi Mungu wenye ikhlasi."

Yaani, 'walikuwa wakitamani - kabla yenu, Ewe Muhammad, hujawajia – kuwa wangukuwa na mtu wa kuwakumbusha kuhusu Allah تعالى na yaliyotokea katika nyakati zilizotangulia, na kuwaletea Kitabu cha Allah تعالى.' Hii ni sawa na Aya:

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِنْ جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَيَكُونُنَّ أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ فَلَمَّا جَاءَهُمْ نَذِيرٌ مَّا زَادَهُمْ إِلَّا نُفُورًا ﴿٤١﴾

¹ Muslim 1:371.

“Na waliapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa kuapa kwao, kwamba akiwajia mwonyaji bila ya shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine lolote. Lakini alipowajia mwonyaji hakuwazidishia ila kuikimbia hiyo Haki.” (35:42), na

أَنْ تَقُولُوا إِنَّمَا أُنزِلَ الْكِتَابُ عَلَيَّ طَائِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا وَإِنْ كُنَّا عَنْ دِرَاسَتِهِمْ لَغَفْلِينَ ﴿٣٥﴾
 أَوْ تَقُولُوا لَوْ أَنَّا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْكِتَابُ لَكُنَّا أَهْدَىٰ مِنْهُمْ ۗ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَيِّنَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ ۗ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ بِقَايَتِ اللَّهِ وَصَدَفَ عَنْهَا ۗ سَنَجْزِي الَّذِينَ يَصْدِفُونَ عَنْ آيَاتِنَا سُوءَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا يَصْدِفُونَ ﴿٣٦﴾

“Msije mkasema: Hakika mataifa mawili kabla yetu yamete-remshiwa Kitabu; na sisi tulikuwa hatuna habari ya waliyokuwa wakiyasoma. Au mkasema: Lau kuwa tumeteremshiwa sisi Kitabu tungelikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola Wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema. Basi nani aliye dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekanusha Ishara za Mwenyezi Mungu, na akajitenga nazo? Tutawalipa wanaojitenga na Ishara Zetu adhabu kali kabisa kwa sababu ya kujitenga kwao.” (6:156-157)

Kauli ya Allah تعالیٰ hapa:

فَكْفُرُوا بِهِ ۗ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٣٧﴾

“Lakini waliukataa. Basi watakuja jua.”

Hili ni onyo kali na dhahiri kwa sababu ya ukafiri wao kwa Mola Wao Mlezi na kumkataa Mjumbe Wake.

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٧﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿٣٨﴾ وَإِنَّ جُنَدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٣٩﴾ فَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٤٠﴾ وَأَبْصَرَهُمْ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿٤١﴾ أَفِعْدَابِنَا يُسْتَعْجِلُونَ ﴿٤٢﴾ فَإِذَا نَزَلَ بِسَاحَتِهِمْ فَسَاءَ صَبَاحُ الْمُنْذَرِينَ ﴿٤٣﴾ وَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٤٤﴾ وَأَبْصَرَ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿٤٥﴾

171. *Na bila ya shaka neno letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa.*

172. *Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa.*

173. *Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda.*

174. *Basi waachilie mbali kwa muda.*

175. *Na watazame, nao wataona.*

176. *Je! Wanaihimiza adhabu Yetu?*

177. *Basi itakaposhuka uwanjani kwao, itakuwa asubuhi mbaya kwa walioonywa.*

178. *Na waache kwa muda.*

179. *Na tazama, na wao wataona.*

Ahadi ya Ushindi na Amri ya Kujitenga na Washirikina

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٤٩﴾

“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa.”

Yaani, tayari imeshaelezwa katika hukumu ya kwanza kuwa Mtume na wafuasi wao hatimaye watashinda duniani na Akhera. Hii ni sawa na Ayah:

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.” (58:21), na

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi.” (40:51).

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَأْمُنَّا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٤٩﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿١٥٠﴾

“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwisha tangulia kwa waja Wetu waliotumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa.”

Maana yake, ‘duniani na Akhera, kama tulivyoeleza kuwa watawashinda watu waliowakufuru na waliokuwa dhidi yao, na namna gani Allah تعالی Aliwaangamiza makafiri na Kuwaokoa waumini.’

وَإِنَّ جُنَدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿١٥١﴾

“Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda.”

Yaani, hatimaye watawashinda. Na Kauli Yake Allah تعالی.

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿١٥٢﴾

“Basi waachilie mbali kwa muda.”

Yaani, ‘vumilieni maudhi yao kwa subira na msubiri mpaka wakati ulioteuliwa, “Hakika Sisi Tutakupeni mwisho mzuri na Tutakupeni ushindi.”

وَأَبْصِرْهُمْ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿١٥٣﴾

“Na watazame, nao wataona.”

Yaani, ‘waangalieni na muone adhabu watakayoipata kwa kukupinga na kukukataa.’ Allah تعالی Alitoa tishio na onyo,

فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ

“...nao wataona.” Halafu Akasema:

أَفَبِعَدَابِنَا يَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٥٤﴾

“Je! Wanaihimiza adhabu Yetu?”

Maana yake, ‘wanatafuta kuharakisha adhabu hiyo kwa sababu wanakukufuru, na Allah تعالی Amewaghadhibikia kwa sababu ya hilo na Atawafanya wapate matokeo ya kuumiza, na kwa sababu ya ukafiri wao na ukaidi, Ataiharakisha adhabu.’

فَإِذَا نَزَلَ بِسَاحَتِهِمْ فَسَاءَ صَبَاحُ الْمُنْذَرِينَ ﴿١٤٩﴾

“Basi itakaposhuka uwanjani kwao, itakuwa asubuhi mbaya kwa walioonywa.”

Yaani, adhabu inapowashukia mahali walipo, siku hiyo itakuwa ya kutisha na maangamizo. As-Suddi alisema:

فَإِذَا نَزَلَ بِسَاحَتِهِمْ

“Basi itakaposhuka uwanjani kwao...”

Yaani, katika makazi yao;

فَسَاءَ صَبَاحُ الْمُنْذَرِينَ

“...itakuwa asubuhi mbaya kwa walioonywa.”

Yaani, asubuhi yao itakuwa ya kutisha mno. Imeandikwa katika Sahihi Mbili kuwa Anas رضي الله عنه, alisema, “Katika asubuhi ya Khaybar, watu walipotoka huku wakiwa na zana zao (kwenda kufanya kazi zao za kila siku) na wakaliona jeshi (la Waislamu), walirejea na kusema, ‘Muhammad wallahi! Muhammad na jeshi!’ Mtume ﷺ alisema:

«الله أكبر، خربت خيبر، إنا إذا نزلنا بساحة قوم فساء صباح المنذرين»

“Allahu Akbar! Khaybar imeangamia. Hakika sisi tunapowavamia watu katika makazi yao, itakuwa mbaya mno asubuhi ya wale walioonywa.”¹

وَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿١٥٠﴾ وَأَبْصَرَ فَسَوْفَ يُبْصِرُونَ ﴿١٥١﴾

“Na waache kwa muda. Na tazama, na wao wataona.”

Huku ni kuisitiza juu ya jambo lililotajwa hapo juu. Na Allah عزوجل Anajua zaidi.

سُبْحٰنَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصْفُونَ ﴿١٥٢﴾ وَسَلٰمٌ عَلٰى الْمُرْسَلِينَ ﴿١٥٣﴾ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ

رَبِّ الْعٰلَمِينَ ﴿١٥٤﴾

¹ Fat'h Al-Bari 2:107, Muslim 2:1043

180. Ametakasika Mola Mlezi Mwenye Enzi na yale wanayo-mzulia.

181. Na Amani juu ya Mitume.

182. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Allah تعالی Anajitukuza Mwenyewe na Anasema kuwa Ametakasika dhidi ya Madhalimu wenye kusema kumhusu Yeye; Ametakasika dhidi ya wanayoyasema. Kauli ya Allah تعالی:

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ

“Ametakasika Mola Mlezi Mwenye Enzi...”

Maana yake, Mwenye Nguvu na Uwezo Ambaye hakuna wa kumzuia.

عَمَّا يَصْفُونَ

“...na yale wanayo mzulia.”

Yaani, kutokana na wanachozusha waongo hao.

وَسَلِّمْ عَلَى الْمُرْسَلِينَ

“Na Salamu juu ya Mitume.”

Yaani, Amani ya Allah تعالی iwe juu yao huko Akhera, kwa sababu wanayo-yasema kumhusu Mola Wao Mlezi ni sahihi na kweli.

وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Na Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Yaani, Anastahiki Sifa Njema mwanzoni na mwishoni mwa mambo yote. Kwa sababu *Tasbih* (Kutukuza) ni tamko lenye kumaanisha kutokuwa na dosari yoyote, fikra hizo mbili zinajitokeza kwa pamoja hapa na katika sehemu nyingine nyingi katika Qur'an.

Kauli ya Allah تعالی:

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٤٩﴾ وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ ﴿١٥٠﴾ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ
رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٥١﴾

***“Ametakasika Mola Mlezi Mwenye Enzi na yale wanayomzulia.
Na Salamu juu ya Mitume. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi
Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.”***

Sa'id bin Abi 'Arubah amesimulia kuwa Qatadah alisema, "Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا سَلَّمْتُمْ عَلَيَّ، فَسَلِّمُوا عَلَيَّ الْمُرْسَلِينَ، فَأَنَا رَسُولٌ مِنَ الْمُرْسَلِينَ»

*“Mnaponisalimia, basi salimieni Mitume, kwani mimi ni miongoni
mwa Mitume.”*

Hayo yameandikwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى.¹ Abu Muhammad Al-Baghawi رحمه الله تعالى ameandika katika *Tafsir* yake kuwa 'Ali رضي الله عنه, alisema: "Mwenye kutaka malipo makubwa katika Siku ya Kiama, basi mwishoni mwa mkutano wowote aseme,

سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿١٤٩﴾ وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ ﴿١٥٠﴾ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ
رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٥١﴾

***“Ametakasika Mola Mlezi Mwenye Enzi na yale wanayomzulia.
Na Salamu juu ya Mitume. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi
Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.”²***

Zimepokewa Hadithi zingine kuhusu makosa yoyote yenye kutokea katika mabaraza kwa kusema: "Umetakasika, ewe Allah, na Una sifa njema. Hakuna mungu wa haki kuabudiwa isipokuwa Wewe; ninakuomba msamaha na ninatubu Kwako." Mimi Ibn Kathir, nimeandikia sura hiyo juzuu ya peke yake.

Huu ni mwisho wa *Tafsir* ya *Surat As-Saffat*. Allah تعالى, Anajua zaidi.

* * *

¹ At-Tabari 21:134.

² Al-Baghawi 4:46.

Tafsiri ya Suratu Swad

Sura ya 38

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُوْرَةُ الضُّحٰى

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

صَّ وَالْقُرْآنِ ذِي الذِّكْرِ ﴿١﴾ بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عِزِّهِ

وَشِقَاقِي ﴿٢﴾ كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ فَنَادَوا وَلا ت

حِينَ مَنَاصِرٍ ﴿٣﴾ وَغِجْبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنْذِرٌ مِنْهُمْ ط وَقَالَ

الْكٰفِرُونَ هٰذَا سَجْرٌ كٰذٰبٌ ﴿٤﴾ اٰجَعَلِ الْاٰلِهَةَ اِلٰهًا

وَاحِدًا ط اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجَابٌ ﴿٥﴾ وَاَنْطَلَقَ الْاَمَلُ مِنْهُمْ

اَنْ اَمْشَوْا وَاَصْبِرُوْا عَلٰى اَلِهَيْكَلٍ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ يُرَادُ ﴿٦﴾

مَا سَمِعْنَا بِهٰذَا فِي الْاَمَلَةِ الْاٰخِرَةِ اِنَّ هٰذَا اِلَّا اَخْتِلَافٌ ﴿٧﴾

اَهُنَزَلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ مِنْ بَيْنِنَا بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِنْ ذِكْرِي ط بَلِ

لَمَّا يَدُوْفُوْا عَذَابِ ﴿٨﴾ اَمْرٌ عِنْدَهُمْ خَزٰىنٌ رَحْمَةٍ مِنْ رَبِّكَ

الْعَزِيْزِ الْوَهَّابِ ﴿٩﴾ اَمْرٌ لَهُمْ مَلِكٌ اَلْسَمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

وَمَا بَيْنَهُمَا ط فَلْيَرْتَقُوا فِي الْاَسْبَابِ ﴿١٠﴾ جُنْدٌ مَّا هُمْ اِلَّا

مَهْزُوْمٌ مِّنَ الْاَحْزَابِ ﴿١١﴾

صَّ وَالْقُرْآنِ ذِي الذِّكْرِ ﴿١﴾ بَلِ

الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عِزِّهِ وَشِقَاقِي ﴿٢﴾ كَمْ

أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ فَنَادَوا

وَلا ت حِينَ مَنَاصِرٍ ﴿٣﴾

1. S'ad, Naapa kwa Qur'ani yenye mawaidha.

2. Lakini waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani.

3. Mataifa mangapi Tume-yaangamiza kabla yao, na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwishapita.

Tayari tumezungumza juu ya herufi zilizo pekee hapo katika mwanzo wa Surat Al-Baqarah; hakuna haja ya kurudia maelezo hayo hapa.

وَالْقُرْآنِ ذِي الذِّكْرِ

“Naapa kwa Qur'ani yenye mawaidha.”

Maana yake, Qur'an yenye kukumbusha na yenye faida kwa watu kwa maisha yao hapa duniani na Akhera. Alisema Adh-Dhahhak,

ذِي الذِّكْرِ

"...yenye mawaidha." Kama Aya hii,

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ

***"Na hakika Tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake kuna ukumbusho."* (21:10)**

Yaani, ukumbusho kwenu.¹ Kauli hii pia ilikuwa ya Qatadah na Ibn Jarir.² Ibn 'Abbas, Said bin Jubayr, Ismail bin Abi Khalid Ibn Uyayanah, Abu Husayn, Abu Salili na As Suddy walisema.

ذِي الذِّكْرِ

"...yenye mawaidha."

"Yenye utukufu na Jaha."³ Hakuna tofauti kati ya Kauli mbili kwa sababu hiki ni kitabu chenye heshima ambacho kimeleta habari za kukumbusha watu na kuwaonya kuwa wawe mbali na maovu. Sababu ya kiapo hiki inapatikana katika Aya:

إِنْ كُلُّ إِلَّا كَذَبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ عِقَابٌ ﴿١٤﴾

***"Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi wakastahiki adhabu Yangu."* (38:14)**

Qatadah alisema sababu yake (kiapo hicho) ni,

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عِزِّهِمْ وَشِقَاقِي ﴿١٤﴾

***"Lakini waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani."*⁴**

Mtazamo huu pia aliupendelea kuusema Ibn Jarir رحمه الله تعالى.⁵

¹ At Tabari 21:140.

² At Tabari 21:140.

³ At Tabari 21:139, 140.

⁴ At Tabari 21:140.

⁵ At Tabari 21:141.

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي عِزِّهِمْ وَشِقَاقِي ۝

“Lakini waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani.”

Maana yake, ndani ya hii Qur’an kuna ukumbusho kwa wale walio tayari kusikia na kuzingatia, lakini makafiri hawapati faida yoyote kwa sababu wao wapo.

فِي عِزِّهِ

“...katika majivuno...”

Yaani, wana ujeuri na wanapenda kubaguana kwa misingi ya ukabila,

وَشِقَاقِي

“...na upinzani.”

Na kuleta upinzani na wanakwenda kinyume na maonyo na maelekezo yake. Kisha Anawaonya kwa Kuwatisha. Anawapa habari jinsi watu wa kabila lao walivyokuwa wabishi na hawakukubali walipopelekewa Mitume. Pia hawakukubali ujumbe ndani ya vitabu vilivyoletwa na Allah kwao kupitia Mitume hawa. Allah تعالى Anasema,

كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ

“Mataifa mangapi Tumeyaangamiza kabla yao...”

Mataifa yaliyokufuru.

فَنَادُوا

“...na wakapiga kelele.”

Yaani, adhabu ilipowashukia walipiga kelele wakiomba msaada uwajie kutoka kwa Mwenyezi Mungu; lakini hizo kelele zao hazikuwasaidia kitu chochote. Na hayo ni kama,

فَلَمَّا أَحْسَبُوا أَنَّهَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَرْكُضُونَ ۝ لَا تَرْكُضُوا وَأَرْجِعُوا إِلَىٰ مَا أُتْرِفْتُمْ فِيهِ
وَمَسْكِنِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَعَلَّوْنَ ۝

“Basi walipoihisi adhabu Yetu, mara wakaanza kukimbia. Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu, na maskani zenu, mpate kuulizwa!” (21:12-13)

Abu Dawud At-Tayalisi alinukuu kuwa Abu Tamim alisema, "Nilimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنهما juu ya aya:

فَنَادُوا وَّلَاتَ حِينَ مَنَاصِرٍ

"...na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwisha pita."

Alisema kuwa ulikuwa si muda wao tena kukimbia au kukwepa (adhabu). Muhammad bin Ka'b alisema juu ya aya:

وَّلَاتَ حِينَ مَنَاصِرٍ

"...na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwishapita."

"Waliitwa kuelekea kwenye Tawhid baada ya umri wao kuisha na wakaanza kuomba maghufira wakati maisha tena kwao yalikuwa yamekoma. Qatadah anasema, "Walipoona adhabu imewashukia walitaka kuomba maghufira wakati usiokuwa muda wake." Mujahid alisema,

وَّلَاتَ حِينَ مَنَاصِرٍ

"...na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwishapita."

"Haikuwa ni muda wa kukimbia au kukwepa." Allah Amesema,

وَّلَاتَ حِينَ مَنَاصِرٍ

"...na wakapiga kelele, lakini wakati wa kuokoka ulikwishapita."

Yaani, hapakuwa na muda wa kukwepa wala kukimbia, wa Allahu A'lamu.

وَعَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنذِرٌ مِنْهُمْ ۗ وَقَالَ الْكٰفِرُونَ هٰذَا سَجْرٌ كٰذٰبٌ ﴿١١﴾ اٰجَعَلِ الْاٰلِهَةَ
 اِلٰهًا وَّحٰدًا ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجَابٌ ﴿١٢﴾ وَاَنْطَلَقَ الْمَلَآئِمُ مِنْهُمْ اَنْ اَمْشَوْا وَاَصْبِرُوْا عَلٰى
 ءَالِهَتِكُمْ ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ يُرٰٓءٰى ﴿١٣﴾ مَا سَمِعْنَا بِهٰذَا فِي الْاٰلِخَرَةِ اِنْ هٰذَا اِلَّا اَخْتِلَافٌ
 ﴿١٤﴾ اَنْزَلَ عَلَيْهِ الذِّكْرَ مِنْ بَيْنِنَا ۗ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ مِّنْ ذِكْرِي ۗ بَلْ لَمَّا يَدُوْقُوْا عَذَابِ ﴿١٥﴾
 اَمْرٌ عِنْدَهُمْ خَزَآئِنٌ رَّحْمَةً رَّبِّكَ اَلْعَزِيْزُ اَلْوَهَّابُ ﴿١٦﴾ اَمْرٌ لَّهُمْ مَّلِكٌ اَلْسَمٰوٰتِ وَاَلْاَرْضِ وَمَا
 بَيْنَهُمَا ۗ فَلْيَرْتَقُوْا فِي الْاَسْبَابِ ﴿١٧﴾ جُنْدٌ مَّا هُنَالِكَ مَهْزُوْمٌ مِّنَ الْاَحْزَابِ ﴿١٨﴾

4. Na walistaajabu kuwajia mwonyaji anayetokana nao wenyewe, na makafiri wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo.

5. Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu.

6. Na wakaondoka wakubwa wao wakiwaambia: Nendeni zenu na dumuni na miungu yenu, kwani hili ni jambo lililopangwa.

7. Sisi hatukusikia haya katika mila hii ya mwisho. Haya si chochote ila ni uzushi tu.

8. Ati yeye tu ndiye aliyeteremshiwa mawaidha (peke yake) katika sisi? Lakini hao wana shaka na Mawaidha Yangu, bali hawajaionja Adhabu Yangu.

9. Au wanazo wao hazina za rehema za Mola Wako Mlezi, Mwenye Nguvu, Mpaji?

10. Au wao wana Ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo kati yao? Basi nawazipande njia za kuendea huko!

11. Hao ni askari wataoshindwa miongoni mwa makundi yatayoshindwa.

Washirikina Walistaajabishwa na Ujumbe, Tauhidi na Qur'an

Allah تعالى Anatuambia kuwa washirikina walistaajabishwa walipoona kuwa Mtume Muhammad ﷺ amepelekwa kwao akiwa na habari njema pia na maonyo kwao. Hii pia ni Kauli Yake Allah تعالى,

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَى رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ

لَهُمْ قَدَمٌ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ قَالَ الْكٰفِرُونَ إِنَّ هٰذَا لَسَجْرٌ مُّؤْمِنٌ ﴿٢٠﴾

“Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu, na wabashirie wale walioamini ya kuwa watakuwa na cheo cha juu kwa Mola Wao Mlezi? Wakasema makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhaahiri!” (10:2)

Allah Anasema hapa,

وَعَجِبُوا أَنْ جَاءَهُمْ مُنْذِرٌ مِنْهُمْ

“Na walistaajabu kuwajia mwonyaji anayetokana nao wenyewe.”

Yaani, mtu, binadamu kama wao.

وَقَالَ الْكٰفِرُونَ هٰذَا سَجْرٌ كٰذٰبٌ ﴿١٠﴾

“...na makafiri wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo.”

أَجْعَلِ الْاٰلِهَةَ اِلٰهَهَا وَاحِدًا ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجَابٌ ﴿١١﴾

“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu.”

Yaani, je anadai kuwa yule ambaye anapaswa kuabudiwa ni Mmoja tu, na hakuna Mungu mwingine baada yake wala badala yake? Washirikina laana za Allah ziwe juu yao, walikataa hilo na walishangazwa kusikia kuwa waachilie mbali Ushirikina kwa sababu walikuwa wamejifunza na kurithi kutoka kwa wazee wao, ibada ya masanamu na vifua vyao na nyoyo zao zilikuwa zimejaa Ushirikina. Na pale Mtume ﷺ alipowaita na kuwaambia waachilie mbali ibada za masanamu ili vifua vyao viwe vyeupe kwa ajili ya ibada ya Mola Mmoja, Allah تعالى, ilikuwa jambo zito kwao na wakashangazwa nalo wakasema,

أَجْعَلِ الْاٰلِهَةَ اِلٰهَهَا وَاحِدًا ۗ اِنَّ هٰذَا لَشَيْءٌ عَجَابٌ ﴿١١﴾ وَأَنْطَلِقُ الْمَلَأُ مِنْهُمْ

“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu. Na wakaondoka wakubwa wao wakiwaambia...”

Yaani, wakubwa zao, viongozi wao na waheshimiwa. Wakasema,

أَمْشُوا

“Nendeni zenu...” Maana yake, “ng’ang’anieni hiyo dini yenu.”

وَأَصْبِرُوا عَلَىٰ ءِالِهَتِكُمْ

“...na dumuni na miungu yenu.”

Yaani, “wala msisikilize hayo asemayo Muhammad, wito wake wa *Tawhid*.”

إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ يُرَادُ

“...kwani hili ni jambo lililopangwa.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Tawhid ambayo Muhammad ﷺ anawalingania (ninyi) ajikweze na mwishowe anataka apate wafuasi kutokana nanyi, lakini hilo sisi hatulikubalii.”¹

Kutajwa Sababu za Kushushwa Aya Hizi Tukufu

Abu Ja'far bin Jarir رضي الله عنهما alinukuu kuwa Ibn Abbas رحمه الله تعالى alisema, “Abu Talib alipougua baadhi ya Maquraishi akiwemo Abu Jahl walienda kumuona na kusema, “Mtoto wa ndugu yako anatumia miungu yetu; anafanya kadha wa kadha, anasema haya na yale. Kwa nini usimuite na kumkanya aache kufanya hayo?” Hivyo Abu Talib alimuita Muhammad ﷺ; alipofika nyumbani kwa Abu Talib nyumba ilikuwa imejaa imebaki nafasi ya mtu mmoja tu ambayo ilikuwa karibu na mgonjwa. Abu Jahl, iwe laana juu yake, kwa kuhofia kuwa Muhammad ﷺ atakaa karibu ya Abu Talib na athari yake kwa Abu Talib itakuwa kubwa, basi alienda akaziba nafasi hiyo iliyo karibu na mgonjwa; Mtume ﷺ akawa hakupata mahali karibu na Ami yake, hivyo akaketi karibu na mlango. Abu Talib akamuambia, “Ewe mtoto wa ndugu yangu, kwa nini watu wako wanalalamika dhidi yako na wanadai kuwa unawatukania miungu yao, na unasema haya na yale.” Walisema vitu vingi sana dhidi ya Mtume ﷺ.

Mtume ﷺ akasema,

«يَا عَمَّ إِنِّي أُرِيدُهُمْ عَلَى كَلِمَةٍ وَاحِدَةٍ يَقُولُونَهَا تَدِينُ لَهُمْ بِهَا الْعَرَبُ، وَتُؤَدِّي إِلَيْهِمْ
بِهَا الْعَجْمُ الْجَزِيَّةُ»

“Ewe Ami yangu! Ninawataka hao juu ya neno moja tu ambalo, kama watalisema, watawafuata wao Waarabu na wasio Waarabu watawalipa Jizyah.”

¹ At-Tabari 21:152.

Waliogopa aliyoyasema. Wakahoji, 'Neno moja? Ndio, tunaapa kwa baba yako, (tutatamka) maneno kumi! Ni neno gani?' Abu Twalib aliuliza, 'Ni neno gani, ewe kijana wa kaka yangu?' Mtume ﷺ akasema:

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ»

"Laa ilaaha illallah (Hakuna wa haki wa kuabudiwa isipokuwa Allah)."

"Wakasimama kwa hamaki huku wakijipangusa nguo zao kwa mikono wakisema,

أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَهًا وَحِدًا إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ ﴿٢٠﴾

"Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu."

Kisha kipande hiki kikateremka kwa Mtume ﷺ.

بَل لَّمَّا يَدُوقُوا عَذَابَ

"...bali hawajaionja adhabu yangu."

Haya ni maneno ya Abuu Kurayb.¹ Habari kama hizi zilinukuliwa na Imam Ahmad, An-Nasai, At-Tirmidhi aliipa Hadithi hii daraja ya: *"Hasan."*²

مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي الْعَمَلِ الْآخِرَةِ

"Sisi hatukusikia haya katika mila hii ya mwisho."

Yaani, "Hatujasikia kauli kama hii ya Tawhid ambayo Muhammad anataka tuifuata, katika dini yake ya kisasa."

Al-Awfi alisema, "Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa walisema, "Hatujasikia haya katika hizi dini za hivi karibuni (yaani Ukristo) kama hii Qur'an ingelikuwa ya kweli, Wakrito wangetueleza hilo."³

¹ At-Tabari 21:149.

² Ahmad 1:362, An Nasai katika *Al-Kubra* 6:442; *Tuhfat Al-Ahwadh* 9:99.

³ At-Tabari 21:152. Al-Awfi pamoja na jamaa zake ni madhaifu.

إِنَّ هَذَا إِلَّا آخْتَلِقُ

“...Haya si chochote ila ni uzushi tu.”

Mujahid na Qatadah walisema ina maana, “Huo ni uongo.”¹ Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema ina maana ni maneno ya wazushi.²

أُنزِلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ مِنْ بَيْنِنَا

“Ati yeye tu ndiye aliyeteremshiwa mawaidha peke yake katika sisi?”

Waliona kuwa haielekei kuwa yeye ndiye kachaguliwa miongoni mwa watu wa kupokea ujumbe wa Qur’an. Hayo yanalingana na Ayah,

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَى رَجُلٍ مِّنَ الْقَرْيَتَيْنِ عَظِيمٍ ﴿٣١﴾

“Na walisema: Kwa nini Qur’ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?” (43:31).

Allah تعالى Amesema,

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ ۗ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَّعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ

“Kwani wao ndio wanaogawa Rehema za Mola Wako Mlezi? Sisi Tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na Tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi.”

Walipoyasema hayo, ilikuwa ni dalili ya ujinga wao na uzito wa kuelewa mambo pale walipoona si mahali pake Qur’an kushushwa kwa Mtume Muhammad ﷺ na siyo kwa mtu mwingine asiyekuwa Mtume ﷺ.

بَل لَّمَّا يَدُوقُوا عَذَابَ

“...bali hawajaionja Adhabu Yangu.”

¹ At-Tabari 21:155.

² At-Tabari 21:154.

Yaani wanayasema haya kwa sababu bado hawajaonja ukali wa Allah تعالى na Adhabu Yake. Lakini watakuja kutana nayo hayo na watatambua athari ya maneno yao kwa kukataa ujumbe huu, itakapofika siku ya Qiyamah watasukumizwa katika moto wa Jahanamu. Kisha Allah تعالى Anatangaza wazi kuwa Yeye Ndiye Anamiliki Ulimwengu Wake wote. Na Yeye Hufanya lile Atakalo na Apendalo. Hutoa chochote kwa yeyote Amtakaye. Humpa Utukufu Amtakaye na Humdhalilisha Amtakaye. Pia Humuongoa Amtakaye na Humpoteza Amtakaye. Ni Yeye tu Ndiye Humpeleka Roho (Jibril عليه السلام) kwa Amri Yake kwa yeyote Amtakaye na Hutia upofu roho za watu Atakao; hakuna atakayeongoka isipokuwa kwa Utashi Wake Allah تعالى. Katika viumbe Wake na waja Wake. Na Allah تعالى Hupiga Muhuri juu ya moyo wa mtu Amtakaye. Hivyo, hakuna yeyote atakayeweza kumuongoa baada ya Allah تعالى. Na hakika waja hawana umiliki wa jambo lolote na wao katika utawala wa Allah تعالى. Hawana amri yoyote japo ndogo kama mfano wa mdudu sisimizi. Na wala hawamiliki chochote hata uzito wa kokwa ya tende. Allah تعالى Anawakaripia na Kuwabishia walete hoja kama wanazo.

أَمْرٌ عِنْدَهُمْ خَزَائِنُ رَحْمَةِ رَبِّكَ الْعَزِيزِ الْوَهَّابِ ﴿٤٥﴾

“Au wanazo wao khazina za Rehema za Mola Wako Mlezi, Mwenye Nguvu, Mpaji?”

Yaani, Allah تعالى, Muweza wa yote, wala hakuna chochote kinachoweza kushindana Naye. Mwenye Uwezo wa kumilikisha, Atoaye Atakacho kwa Yeyote Amtakaye Yeye. Ayah hii inafanana na Kauli Yake Allah تعالى ,

أَمْ هُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمَلَكِ فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٤٦﴾ أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ فَقَدْ آتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَآتَيْنَاهُمْ مُلْكًا عَظِيمًا ﴿٤٧﴾ فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ بِهِ وَمِنْهُمْ مَّنْ صَدَّ عَنْهُ ۗ وَكَفَىٰ بِهِمْ سَعِيرًا ﴿٤٨﴾

“Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende. Au wanawahusudu watu kwa yale Aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa Fadhila Yake? Basi Tuliwapa ukoo wa Ibrahim Kitabu na Hikima na Tukawapa utawala mkubwa. Basi wapo miongoni mwao waliyoyaamini, na wapo walioyakataa. Na Jahannamu yatosha kuwa ni moto wa kuwateketeza.” (4:53-55)

قُلْ لَوْ أَنْتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنْفَاقِ وَكَانَ الْإِنْسَانُ قَتُورًا ﴿١٠٠﴾

“Sema: Lau kuwa nyinyi mnazimiliki khazina za Rehema za Mola Wangu Mlezi, basi hapana shaka mngelizuia kuzitumia kwa ajili ya kukhofu. Na mwanaadamu tangu hapo tabia yake ni mchoyo!” (17:100).

Maneno haya ni baada ya Allah تعالی Kutuambia kisa cha jinsi washirikina walivyokataa kukubali kuwa wamepelekewa mjumbe wa kibinaadamu Muhammad ﷺ; maneno ni kama Aliyoyaeleza Allah تعالی kuhusu watu wa Saleh عليه السلام walivyosema katika Aya,

أَلَيْسَ الذِّكْرُ عَلَيْهِ مِنْ بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَابٌ أَشْرٌ ﴿٢٥﴾ سَيَعْمُونَ غَدًا مِّنَ الْكَذَابِ الْآشِرِ ﴿٢٦﴾

“Ni yeye tu aliyeteremshiwa huo ukumbusho kati yetu sote? Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi! Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi.” (54:25-26).

أَمْرٌ لَهُم مَّلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا فَلْيَرْتَقُوا فِي الْأَسْبَابِ ﴿١٠١﴾

“Au wao wana ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo kati yao? Basi nawazipande njia za kuendea huko!”

Yaani, kama hayo wanayo, basi hebu wapande mbinguni kwa uwezo wao. Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Qatadah na wegine walisema, “Njia za kwenda mbinguni.”¹ Adh-Dhahhak alisema, “Hebu basi wapande waende huko mbingu ya saba.”² Kisha Allah تعالی Anasema,

جُنْدٌ مَّا هُنَالِكَ مَهْزُومٌ مِّنَ الْأَحْزَابِ ﴿١٠٢﴾

“Hao ni askari wataoshindwa miongoni mwa makundi yatayo-shindwa.”

Yaani, kundi hili la makafiri hujiona na kupenda upinzani ambao wanaopinga utume (na Amri za Allah تعالی) wataashindwa, watazidiwa nguvu na watataabika; kama vile makundi ya zama za kale walivyoaibika kabla yao.

¹ At-Tabari 21:156.

² At-Tabari 21:157.

Aya hii inafanana na Aya,

أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ مُنْتَصِرُونَ ﴿٤٤﴾ سَيَرَمُ الْجَمْعُ وَيُولُونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾

“Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda tu. Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma.” (54:44-45)

Kama ilivyotokea Siku ya Badri.

بَلِ السَّاعَةِ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَذْهَىٰ وَأَمْرٌ ﴿٥١﴾

“Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito zaidi na chungu zaidi.”

* * *

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ ذُو الْأَوْتَادِ ﴿١٢﴾
 وَثَمُودُ وَقَوْمُ لُوطٍ وَأَصْحَابُ لَيْكَةِ ؕ أُولَئِكَ الْأَحْزَابُ ﴿١٣﴾
 إِنْ كُلُّ إِلَّا كَذَّبَ الرَّسُلَ فَحَقَّ عِقَابِ ﴿١٤﴾ وَمَا يَنْظُرُ
 هَتُّوْلَاءِ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً مَّا لَهَا مِنْ فَوَاقٍ ﴿١٥﴾ وَقَالُوا
 رَبَّنَا عَجَلْ لَنَا قِطْعًا قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ﴿١٦﴾ أَصْبِرْ عَلَى
 مَا يَقُولُونَ وَادْكُرْ عَبْدَنَا دَاوُدَ ذَا الْأَيْدِ ؕ إِنَّهُ أَوَّابٌ ﴿١٧﴾
 إِنَّا سَخَّرْنَا الْجِبَالَ مَعَهُ يُسَبِّحْنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِشْرَاقِ ﴿١٨﴾
 وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً ؕ كُلُّ لَهْزٍ أَوَّابٌ ﴿١٩﴾ وَشَدَدْنَا مُلْكَهُ
 وَءَاتَيْنَاهُ الْحِكْمَةَ وَفَضَّلْنَا الْخِطَابِ ﴿٢٠﴾ * وَهَلْ أَتَاكَ نَبُؤُا
 الْخَصْمِ إِذْ تَسَوَّرُوا الْمِخْرَابِ ﴿٢١﴾ إِذْ دَخَلُوا عَلَى دَاوُدَ
 فَفَزِعَ مِنْهُمْ ؕ قَالُوا لَا تَخَفْ ؕ خَصْمَانِ بَغِي بَعْضُنَا عَلَى
 بَعْضٍ فَاحْكُم بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَاهْدِنَا إِلَى سَوَاءِ
 الصِّرَاطِ ﴿٢٢﴾ إِنَّ هَذَا أَخِي لَهُ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَعْجَةً وَاِ
 نَّ نَعْجَتِي وَاحِدَةٌ فَقَالَ أَكْفِلْنِيهَا وَعَزَّنِي فِي الْخِطَابِ ﴿٢٣﴾ قَالَ
 لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعَجَتِكَ إِلَى تَغَايِبِهِ ؕ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ
 الْخُلَطَاءِ لَيَبْتَغِي بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ ؕ وَظَنَّ دَاوُدُ أَنَّمَا فَتَنَّهٗ
 فَاسْتَغْفَرَ رَبَّهُ وَخَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ ﴿٢٤﴾ فَغَفَرْنَا لَهُ ذَٰلِكَ
 وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَّسَابِرِ ﴿٢٥﴾

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ
 ذُو الْأَوْتَادِ ﴿١٢﴾ وَثَمُودُ وَقَوْمُ لُوطٍ
 وَأَصْحَابُ لَيْكَةِ ؕ أُولَئِكَ الْأَحْزَابُ
 إِنْ كُلُّ إِلَّا كَذَّبَ الرَّسُلَ
 فَحَقَّ عِقَابِ ﴿١٤﴾ وَمَا يَنْظُرُ
 هَتُّوْلَاءِ
 إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً مَّا لَهَا مِنْ فَوَاقٍ
 وَقَالُوا رَبَّنَا عَجَلْ لَنَا قِطْعًا
 قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ﴿١٦﴾

12. *Walikanusha kabla yao kaumu ya Nuhu, na kina A'adi na Firauni mwenye majengo.*

13. *Na Thamud na kaumu Lut'i na watu wa Machakani. Hayo ndiyo makundi.*

14. *Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi wakastahiki adhabu yangu.*

15. *Na hawa hawangojei ila ukelele mmoja tu usio na muda.*

16. *Na wao husema: Mola Wetu Mlezi! Tuletee upesi sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Hisabu.*

Ukumbusho Juu ya Walioangamizwa katika Umma Zilizotangulia

Allah تعالى Anahabarisha habari za watu wa kale na adhabu zilizowaangukia kwa kufanya ukaidi dhidi ya Mitume; kwa kutokuwakubali wajumbe (Rehema na Amani ziwafikie.) Tumeona tayari visa vyao kwa undani katika sehemu mbali mbali ndani ya Qur'an. Allah تعالى Anasema

أُولَئِكَ الْأَحْزَابُ

"...Hayo ndiyo makundi."

Yaani, "Wao walikuwa wengi na wenye nguvu zaidi yenu, walikuwa na mali na watoto wengi, lakini yote hayo hayakuwasaidia kitu au kuwalinda na adhabu ya Allah تعالى Alipopitisha Amri Yake. Allah تعالى Anasema.

إِنْ كُلُّ إِلَّا كَذَبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ عِقَابٌ ﴿٥٠﴾

"Hao wote waliwakadhibisha Mitume; basi wakastahiki Adhabu Yangu."

"Sababu ya kuangamizwa kwao ilikuwa ni kukufuru Mitume na kuwakengeuka, hivyo ole wao wanaoelezwa haya, wawe macho na waogope."

وَمَا يَنْظُرُ هَتُوْلَاءِ إِلَّا صَيْحَةً وَاحِدَةً مَّا لَهَا مِنْ فَوَاقٍ ﴿٥١﴾

"Na hawa hawangojei ila ukelele mmoja tu usio na muda."

Malik amesimulia kutoka kwa Zayd bin Aslam, "Hakuna atakayezuia hilo wala kulipinga."¹ Yaani, watakingojea Kiama na kitawafikia kwa ghafla bila wao kutambua. Lakini baadhi ya dalili zake zimeshajitokeza, yaani kiko karibu sana. Hii *Sayhah* ni mpulizo wa parapanda ambapo Allah تعالى Atamuamuru Malaika Israfil عليه السلام kupuliza kwa sauti kubwa na kila aliye mbinguni au ardhini ataingiwa na hofu kubwa isipokuwa wale Mola Aliowahifadhi.

وَقَالُوا رَبَّنَا عَجِّلْ لَنَا قِطْنَآ قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٥٢﴾

"Na wao husema: Mola Wetu Mlezi! Tuletee upesi sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Hisabu."

¹ 'Abdur-Razzaq 21:161.

Hapa Allah تعالى Anawasuta makafiri kwa kutaka adhabu iwashukie upesi. *Qitt* maana yake kitabu au ilisemekana kuwa ni sehemu ya fungu analostahiki mtu. Ibn Abbas, Mujahid Adh-Dhahhak, 'Al-Hassan na wengine walisema, "Waliomba adhabu iharakishwe."¹ Qatadah aliongeza, hayo ni kama waliposema,

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنَّ كَاتِبَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ

أَوْ آتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٢﴾

"Na waliposema: Ee Mwe nyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu." (8:32).²

Ilisemekana pia hao makafiri waliomba pia wapate sehemu yao ya Pepo hapa hapa duniani, kama kweli ipo, ili wapate kuifaidi Pepo yao hapa hapa duniani; walisema hayo kwa sababu walikuwa hawayaamini hayo na waliona kuwa hayawezekani kutokea hayo kulingana na imani yao potofu ya kutokuamini kwa itikadi kuwa vitu hivyo havipo na hakuna siku ya Qiyamah. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa, "Waliomba haraka wapewe kile ambacho wanastahiki kukipata, kizuri au kibaya basi waletewe hapa hapa dunini."³ Alichosema Bin Jariri رحمه الله تعالى ni kizuri. Mtazamo huo vile vile ni wa Adh-Dhahhak na Ismail bin Khalid. *Allahu A'lamu*.⁴ Makafiri kwa kauli yao hii waliitoa ilikuwa kama kejeli na kufuru, hivyo Allah تعالى Akamuamuru Mtume Wake ﷺ kuwa mvumilivu anapopambana na maudhi, matusi, kejeli na kauli mbaya na mbovu kama hivi na papo hapo Akampa bishara kuwa subira zake na uvumilivu wake utaleta matunda ya ushindi na kufaulu.

أَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَاذْكُرْ عَبْدَنَا دَاوُدَ ذَا الْأَيْدِ إِنَّهُ أَوَّابٌ ﴿٣٣﴾ إِنَّا سَخَّرْنَا الْجِبَالَ

مَعَهُ يُسَبِّحُنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِشْرَاقِ ﴿٣٤﴾ وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً كُلٌّ لَهُ أَوَّابٌ ﴿٣٥﴾ وَشَدَدْنَا

مُلْكَهُ وَآتَيْنَاهُ الْحِكْمَةَ وَفَضَّلْنَا الْخَطَّابَ ﴿٣٦﴾

¹ At-Tabari 21:164, *Ad-Dur Al-Manthur* 7:148.

² At-Tabari 21:164.

³ At-Tabari 21:165.

⁴ At-Tabari 21:195.

17. Subiri kwa hayo wayasemayo, na umkumbuke mja Wetu Daudi, mwenye nguvu. Hakika yeye alikuwa mwingi wa kutubia.

18. Hakika Tuliidhalilisha milima pamoja naye ikisabihi jioni na asubuhi pamoja naye.

19. Na pia ndege waliokusanywa makundi kwa makundi; wote walikuwa wanyenyekevu kwake.

20. Na Tukautia nguvu ufalme wake, na Tukampa hikima, na kukata hukumu.

Utajo wa Dawud عليه السلام,

Allah تعالى Anatuambia kuwa mja Wake na Mjumbe Wake, Dawud عليه السلام alikuwa amejaaliwa maarifa mapana sana na nguvu nyingi. *Al-ayd* maana yake ni nguvu kubwa za maarifa na vitendo. Ibn Abbas, As-Suddi, na Ibn Zayd, walisema. "*Al-ayd* maana yake ni nguvu."¹ Mujahid alisema. "*Al-ayd* ni nguvu za utii kwa Allah تعالى."²

Qatadah alisema, "Dawud عليه السلام, alipewa nguvu za kuabudu na uwezo wa kuelewa katika Uislamu."³ Na tulielezwa ya kuwa, alikuwa anasali thuluthi ya usiku na anafunga nusu ya mwaka. 'Taarifa hizi zimo ndani ya vitabu vya Sahihi mbili ambapo Mtume ﷺ alisema,

«أَحَبُّ الصَّلَاةِ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى صَلَاةُ دَاوُدَ، وَأَحَبُّ الصِّيَامِ إِلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ صِيَامُ دَاوُدَ، كَانَ يَنَامُ نِصْفَ اللَّيْلِ، وَيَقُومُ ثُلُثَهُ، وَيَنَامُ سُدُسَهُ، وَكَانَ يَصُومُ يَوْمًا وَيُفْطِرُ يَوْمًا، وَلَا يَغْتَرُّ إِذَا لَأَقَى، وَأَنَّهُ كَانَ أَوْابًا»

"Sala ipendezayo zaidi mbele ya Allah ni Sala ya Dawud, na funga ipendezayo zaidi mbele ya Allah ni funga ya Dawud. Alikuwa analala nusu ya usiku na anasimama thuluthi yake na analala sudusi ya usiku. Anafunga siku moja na anafungua siku moja. Wala hakukimbia kutoka Medani ya vita anapopigana na daima alijiegemeza kwa Mola Wake."⁴

¹ At-Tabari 21:166, 167.

² At-Tabari 21:166.

³ At-Tabari 21:167.

⁴ Fat'h Al-Bari 20, Muslim 2:816.

Yaani, daima mambo yake yote alimuelekea Allah تعالى na kumtegemea.

إِنَّا سَخَرْنَا الْجِبَالَ مَعَهُ يُسَبِّحْنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِشْرَاقِ ﴿١٨﴾

“Hakika Tuliidhalilisha milima pamoja naye ikisabihi jioni na asubuhi pamoja naye.” (38:18).

Yaani, Allah تعالى Aliifanya milima ilete tasbihi na Kumtukuza Allah تعالى pamoja na Dawud kila jua linapochomoza na kila linapokuchwa. Aya hii inafanana na,

يَنْجِبَالُ أَوْيَىٰ مَعَهُ وَالطَّيِّرُ

“Enyi milima! Karirini kumtakasa Mwenyezi Mungu pamoja naye! Na ndege pia.” (34:10).

Ndege nao walikuwa wakimtukuza Allah تعالى pamoja na Dawud رحمه الله تعالى. Dawud رحمه الله تعالى alipokuwa akisoma Zaburi halafu ndege wa karibu akiisikia Sauti ya Dawud عليه السلام akisoma kitabu cha Allah تعالى, yule ndege hakuendelea na safari yake bali alijiunga na Mtume Dawud عليه السلام katika uradi huo huku akimzunguka Dawud عليه السلام wakiwa pamoja katika uradi huo. Milima nayo ilipokea sauti hizo na kul eta sauti zake kama mwangwi katika kumhimidi Allah تعالى. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea riwaya kutoka kwa Abdallah bin Al-Harith bin Nawafal alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alikuwa hasali Sala ya *Al-Dhuha*. (Nawafal) Akasema, “Basi nilimpeleka kwa Ummu Hani رضي الله عنها nikamuambia, “Muambie (huyu) yale uliyoniambia mimi.” Akasema (Umm Hani رضي الله عنها), “Mtume ﷺ aliingia kwangu siku Makka ilipofunguliwa. Aliomba maji ndani ya bakuli kubwa, kisha akaomba nguo akafanya pazia kati yangu na yeye na akaoga. Kisha alinyunyiza maji upande wa nyumba akasali raka nane. Hii ilikuwa ni Sala ya *Al-Dhuha*, kisimamo chake, sawa na kurukuu kwake, na ni sawa na sujudu yake na kikao chake vyote ni vifupi vifupi. Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema nimeisoma Qur’an mwanzo wake hadi mwisho wake na nilikuwa sijui Sala ya *Al-Dhuha* mpaka hivi leo.” Na kisha akasoma,

يُسَبِّحْنَ بِالْعَشِيِّ وَالْإِشْرَاقِ

“...ikisabihi jioni na asubuhi...”Siku zote nikijiuliza, “Sala ya *Ishraq* ikoje, lakini sasa nafahamu ni kitu gani.”¹ Allah تعالى Anasema

¹ At-Tabari 21:169.

وَالطَّيْرَ مَحْشُورَةً^ط

“Na pia ndege waliokusanywa makundi kwa makundi.”

Waliopaa na kuruka angani,

كُلٌّ لَهُمْ أَوَابٌ

“...wote walikuwa wanyenyekevu Kwake.”

Yaani, walimtii Allah تعالى na walimfuatia Daudi عليه السلام nyuma yake katika kumtukuza Allah تعالى. Said bin Jubayr, Qatadah na Malik walisema kauli kutoka kwa Zayd bin Aslam na Ibn Zayd,

كُلٌّ لَهُمْ أَوَابٌ

“...wote walikuwa wanyenyekevu kwake.”

Yaani, “walimtii Allah تعالى kwa kumuiga Daudi عليه السلام.”¹

وَشَدَدْنَا مُلْكَهُ

“Na Tukautia nguvu ufalme wake.”

Yaani, “Tulimpa dola kamili ambayo wafalme hutamani kuwa nayo.” Ibn Abi Najiih amepokea kutoka kwa Mujahid kuwa kasema, “Alikuwa ni mwenye nguvu kuliko watu wote wa ulimwengu huu.”

وَأَتَيْنَاهُ الْحِكْمَةَ

“...na Tukampa hikima...”

Mujahid alisema, “Maana yake ni uwezo wa kuelewa kutoa hoja kwa kupembua mambo na akili.” Qatadah alisema, “Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kufuata yote yaliyomo ndani yake.” As-Suddi alisema ,

الْحِكْمَةَ

“...hikima...” “Ni Utume”²

¹ At-Tabari 21:169.

² At-Tabari 21:171

وَفَصَّلَ الْخِطَابِ

“...na kukata hukumu.”

Shurayh Al-Qadhi na Ash-Sha’bi walisema, “Uwezo mkubwa wa kuamua mambo, ni katika utoaji ushahidi na kula viapo.”¹ Qatadah alisema, “Kupata mashahidi wawili kwa upande wa mdai au kiapo kwa mdaiwa ni uwezo mkubwa wa uamuzi.”² Hii ndiyo ilikuwa njia wanayotumia Manabii wajumbe wa Allah au alisema waumini na watu wema. Huu ndio msingi wa kutoa hukumu na uamuzi wa mambo katika ummah huu mpaka siku ya Qiyamah. Kauli hii ilikuwa ni ya Abu Abdur Rahman As-Sulami.³ Mujahid na As-Suddi wao walisema, “Maana yake ni kupitisha hukumu ya haki baada ya kuelewa kadhia (kesi).” Mujahid alisema pia, “Ni kutoa tafsiri sahihi katika maneno na maamuzi na inakusanya yote yaliyopo hapo juu.” Hii ndio kauli aliyoifadhilisha Ibn Jarir ⁴رحمَهُ اللهُ تعالى.

﴿ وَهَلْ أَتَاكَ نَبُؤُا الْخَصَمِ إِذْ تَسَوَّرُوا الْمِحْرَابَ ﴾ ﴿١٦﴾ إِذْ دَخَلُوا عَلَى دَاوُدَ فَفَرَعَ مِنْهُمْ ۖ قَالُوا لَا تَخَفْ خَصْمَانِ بَغَى بَعْضُنَا عَلَى بَعْضٍ فَاحْكُم بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَاهْدِنَا إِلَى سَوَاءِ الصِّرَاطِ ﴾ ﴿١٧﴾ إِنَّ هَذَا أَخِي لَهُ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَعَجَةً لِى نَعَجَةٌ وَاحِدَةٌ فَقَالَ أَكْفِلْنِيهَا وَعَزَّنِي فِي الْخِطَابِ ﴾ ﴿١٨﴾ قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعَجِكَ إِلَى نَعَاجِهِ ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْخُلَطَاءِ لِيَبْغَىٰ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ ۗ وَظَنَّ دَاوُدُ أَنَّمَا فَتَنَّاهُ فَاسْتَغْفَرَ رَبَّهُ وَخَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ ﴿١٩﴾ فَغَفَرْنَا لَهُ ۗ ذَٰلِكَ وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَّوَاسٍ ﴿٢٠﴾

21. Na je! Imekufikia khabari ya wagombanao walipopindukia ukuta kuingia chumbani?

22. Walipomuingilia Daudi, naye akawaogopa. Wakasema: Usiogope! Sisi ni wagombanao wawili, mmoja wetu amemdhulumu

¹ At-Tabari 21:173.

² At-Tabari 21:173.

³ At-Tabari 21:173.

⁴ At-Tabari 21:173.

mwenziwe. Basi tuhukumu kwa haki, wala usipendeleee. Na utuongoe kwenye njia iliyo sawa.

23. Hakika huyu ndugu yangu ana kondoo wa kike tisiini na tisa; na mimi ninaye kondoo mke mmoja. Akasema: Nipe huyo nikufugie! Na amenishinda kwa maneno.

24. Akasema: Kweli amekudhulumu kwa kumtaka kondoo wako mmoja kuongezea kwenye kondoo wake. Na hakika washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipokuwa walioamini na wakatenda mema. Na hao ni wachache. Na Daudi akajua kuwa Tumemfanyia mtihani. Basi akamuomba msamaha Mola Wake Mlezi, na akaanguka kusujudu na kutubia.

25. Basi Tukamsamehe kwa hayo. Naye kwa hakika anao mkaribisho mkubwa na marejeo mazuri Kwetu.

Kisa cha Mahasimu Wawili (Mbele ya Daudi عليه السلام)

Katika kueleza hili, ulamaa wengi wa *Tafsir* hueleza kisa ambacho huelemea katika visa vya *Israiliyati*. Hakuna Hadithi ya Mtume Muhammad ﷺ inayoeleza kisa hiki tunayoweza kusema kuwa ina mashiko. Hata hivyo Ibn Abi Hatim ametoa Hadithi ambayo mshororo wa wapokezi wake hauwezi kuitwa kuwa ni thabiti kwa sababu miongoni mwa wapokezi wake yumo Yazid Ar-Raqashi aliyepokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه. Licha ya kuwa Yazid anajulikana kwa tabia nzuri na uchamungu, Maimamu wa Hadithi wanaona kuwa Hadithi zake ni dhaifu. Ni bora basi kueleza kisa hcho kwa ufupi halafu tumuachie Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote; Qur'an ni ya kweli na yaliyo ndani yake ni kweli tupu.

فَفَرَّعَ مِنْهُمْ

"...naye akawaogopa."

Hali hiyo ilimtokea kwa sababu alikuwa katika *Mihrab* yake. Sehemu hii ilikuwa ndio sehemu tukufu ya nyumba yake na siku hiyo alikuwa ametoa Amri kuwa asiingie mtu yeyote pale alipo. Hivyo ghafla wakaingia watu wawili walioparamia wigo/ukuta uliozunguka *Mihrab* yake ili watoe mashitaka ya kadhia yao.

وَعَزَّنِي فِي الْخِطَابِ

“Na amenishinda kwa maneno.”

Yaani, “kanizidi hoja.”

وَوَطَّنَ دَاوُدُ أَنْمَا فَتَنَّهُ

“Na Daudi akajua kuwa Tumemfanyia mtihani.”

Ali Ibn Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema tafsiri yake ni “Tulimtahini.”¹

وَحَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ

“...na akaanguka kusujudu na kutubia.”

فَغَفَرْنَا لَهُ ذَلِكَ

“Basi Tukamsamehe kwa hayo.”

Kwa maana, hayo yaliyomtokea.

Sij'da Iliyomo Katika Surat Swad

Sijida iliyomo katika *Surat Swad* siyo ya lazima ni Sijida ya Shukrani. Kauli hiyo ni kutokana na maneno ya Imam Ahmad kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما ambaye alisema, “Sijida katika *Surat Swad* siyo wajibu: Nilimuona mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisujudu katika sura hiyo, “Sijida hiyo.”² Hadithi hii imo katika vitabu vya Al-Bukhari, Abu Dawud, At-Tirmidhi na tafsiri ya An-Nasai. At-Tirmidhi ameipa Hadithi hii daraja ya *Hasan Sahih*³ katika Tafsiri yake, An-Nasai amesema kuhusu aya hii maneno aliyoyanukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما Mtume ﷺ alisujudu katika *Surat Swad* na akasema:

«سَجَدَهَا دَاوُدُ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ تَوْبَةً، وَنَسَجَدُهَا شُكْرًا»

“Hii Sajda aliisujudu Dawud عليه السلام likiwa ni tendo la kutubia kwa Mola Wake, na sisi tunasujudu kumshukuru Mola Wetu.”

¹ At-Tabari 21:181.

² Ahmad 1:359.

³ *Fat'h Al-Bari* 2:643, *Abu Dawud* 2:123, *Tuhfat ul Al-Ahwadhi* 3:178, *An-Nasai* katika *Al-Kubra* 6:341.

Habari hizi zimeandikwa na An-Nasai tu.¹ Na wapokezi wa silsila yake wote wanategemewa. Katika kuitafsiri Aya hii Al-Bukhari ameleza katika tafsiri ya ayah hii kuwa *Al-Awaam* alisema kuwa alimuuliza Mujahid juu ya *'Sijda ya Surat Swad*. Alijibu kuwa, "Nilimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنهما: "Kwa nini unasujudu (hapa)." Alimjibu, "Je! Hujapata kusoma,

وَمِن ذُرِّيَّتِهِ دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ

"Na katika kizazi chake Tulimuongoa Daud na Suleiman..." (6:84) na,

أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهِدَانِهِمْ آقْتَدَهُ

"Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu Amewahidi. Basi fuata hidaya yao." (6:90)

Daudi عليه السلام ni Miongoni mwa Mitume Muhammad ﷺ Aliyoamrisha Kuuiga.

"Hivyo Dawud عليه السلام alisujudu hapa, hivyo naye mjumbe wa Allah ﷻ alisujudu hapa."²

Abu Dawud ameleza kuwa Abu Said Al-Khudri رضي الله عنه alisema, "Mtume Muhammad ﷺ alisoma *Surat Swad* akiwa kwenye Minbar; alipofika sehemu ya kusujudu alishuka kwenye Minbar na akasujudu na watu wakasujudu naye. Na wakati mwingine aliposoma sura hii na alipofika sehemu ya Sajdah na watu wakiwa tayari kusujudu naye alisema,

«إِنَّمَا هِيَ تَوْبَةٌ نَّبِيِّ، وَلَكِنِّي رَأَيْتُكُمْ تَشْرَتُنَّ»

"Hii (Sajdah) ni toba ya Nabii lakini naona mkiwa mmejitarisha kusujudu!"

Kisha alishuka kutoka katika Minbar na akasujudu.³ Habari hizi zimeandikwa na Abu Dawud tu, lakini silsila ya mapokezi yake imetimiza masharti ya maimamu wawili, Al-Bukhari na Muslim.

¹ An-Nasai 2:159.

² *Fat-h Al-Bari* 8:405.

³ Abu Dawud 1410.

وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَقَاسٍ ﴿٢٥﴾

“Naye kwa hakika anao mkaribisho mkubwa na marejeo mazuri Kwetu.”

Yaani, Siku ya Kiama atakuwa na amali njema zitakazomueka karibu na Mola Wake na atapewa makazi mazuri Peponi; Hayo ni kwa sababu ya toba yake na maamuzi yake kwa watu wa dola yake. Kama inavyosemwa katika Sahihi.

«الْمُقْسِطُونَ عَلَىٰ مَنَابِرٍ مِّنْ نُورٍ عَنِ يَمِينِ الرَّحْمَنِ، وَكَلَّمَا يَدَيْهِ يَمِينٌ، الَّذِينَ يُفْسِطُونَ فِي أَهْلِيهِمْ وَمَا وَلَوْ»

“Waadilifu watakuwa juu ya Minbar za nuru kuliani mwa Ar-Rahman, na Mikono Yake yote Miwili ni ya Kuume, ambao wanafanya uadilifu kwa familia zao na wanaowasimamia.”¹

* * *

¹ Muslim 3:1458.

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ
بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَىٰ فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّ الَّذِينَ
يُضِلُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا يَوْمَ
الْحِسَابِ ﴿٣٦﴾ وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا
بَطْلًا ۗ ذَلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنَ
النَّارِ ﴿٣٧﴾ أَمْ يَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ يَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفَجَارِ ﴿٣٨﴾
كَتَبْنَا أَنزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِّيَدَّبَّرُوا ءَايَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو
الْأَلْبَابِ ﴿٣٩﴾ وَوَهَبْنَا لِذَاوُدَ سُلَيْمَانَ ۗ نِعَمَ الْعَبْدِ ۗ إِنَّهُ
أَوَابٌ ﴿٤٠﴾ إِذْ عَرَضَ عَلَيْهِ بِالْعَشِيِّ الصَّفِيَنَتُ الْجِيَادُ ﴿٤١﴾
فَقَالَ إِنِّي أَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَن ذِكْرِ رَبِّي حَتَّى تَوَارَتْ
بِالْحِجَابِ ﴿٤٢﴾ رُدُّوهَا عَلَيَّ ۗ فَطَفِقَ مَسْحًا بِالسُّوقِ
وَالْأَعْنَاقِ ﴿٤٣﴾ وَلَقَدْ فَتَنَّا سُلَيْمَانَ وَأَلْقَيْنَا عَلَى كُرْسِيِّهِ
جَسَدًا ۖ ثُمَّ أَنَابَ ﴿٤٤﴾ قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكًا لَّا
يُنْبَغِي لِأَحَدٍ مِّنْ بَعْدِي ۗ إِنَّكَ أَنتَ الْوَهَّابُ ﴿٤٥﴾
فَسَخَرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُخَاءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٤٦﴾
وَالشَّيْطِينَ كُلَّ بَنَّاءٍ وَعَوَّاصٍ ﴿٤٧﴾ وَءآخِرِينَ مَّقْرِنِينَ فِي
الْأَصْفَادِ ﴿٤٨﴾ هَذَا عَطَاؤُنَا فَامْنُنْ أَوْ أَمْسِكْ بِغَيْرِ
حِسَابٍ ﴿٤٩﴾ وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحَسَنَ مَّقَابٍ ﴿٥٠﴾

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي
الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا
تَتَّبِعِ الْهَوَىٰ فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ
إِنَّ الَّذِينَ يُضِلُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ لَهُمْ
عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا يَوْمَ
الْحِسَابِ ﴿٣٦﴾

26. Ewe Daudi! Hakika Sisi Tumekufanya wewe uwe Khalifa katika nchi. Basi wahukumu watu kwa haki, wala usifuata matamaniao yakakupoteza kwenye njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika wanaoipotea njia ya Mwenyezi Mungu waka-iacha, watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau kwao Siku ya Hisabu.

Nasaha kwa watawala na viongozi.

Hizi ni nasaha zake Allah تعالى kwa wale watu ambao wamo katika nafasi za mamlaka. Wanapaswa kuwaongoza watu kwa kufuata haki na uadilifu ulioshushwa kutoka Kwake (تعالى Allah). Wasiwe wenye kuacha haki na uadilifu na wakaenda mbali na njia ya Allah تعالى.

Allah تعالى Ametoa onyo kali kuwa wale watakaoacha hayo na kufanya wanavyotaka kwa kusahau siku ya Qiyamah basi wataadhibiwa vikali.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibrahim Abu Zuraf ambaye alisoma vitabu vya Ahlu Al-Kitabi alisema kuwa Al-Walid bin Abdul Malik alimuuliza, "Je, kuna mtu mwenye haki ya kumuuliza Khalifa na maamuzi yake? Umesoma vitabu vilivyotangulia na Qur'an na umevielewa." Akasema, "Ewe Amirul Muuminina utaniruhusu niseme?" Akasema, "Sema uko chini ya ulinzi wa Allah تعالى."

Nikasema, "Ya Amirul Muuminina je we ni kipenzi zaidi kwa Allah تعالى kuliko Dawud عليه السلام, Mola Alimpa utume na utawala na kisha Alimpa onyo kali ndani ya Kitabu chake."

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَىٰ
فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ إِنَّ الَّذِينَ يَضِلُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

"Ewe Daudi! Hakika Sisi Tumekufanya wewe uwe Khalifa katika nchi. Basi wahukumu watu kwa haki, wala usifuate matamaniao yakakupoteza kwenye njia ya Mwenyezi Mungu."

لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا يَوْمَ الْحِسَابِ ﴿٣٨﴾

"... watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau kwao Siku ya Hisabu."

Ikrimah alisema. "Watapewa adhabu kali Siku ya Kiama kwa waliyoyasahau."¹ As-Suddi alisema, "Watapewa adhabu kali Siku ya Kiama kwa waliyoyadharau kuya fanya kwa ajili ya Siku ya Malipo."²

Tafsiri hii inae ndana na maana ya dhahiri ya aya. Allah تعالى Ndiye Mwongozaji katika njia ya haki.

¹ At-Tabari 21:189.

² At-Tabari 21:189.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطِيلاً ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ
كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٦٧﴾ أَمْ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ
أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِينَ كَالْفُجَّارِ ﴿٦٨﴾ كَتَبَ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِيَدَّبَّرُوا ءَايَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ
أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٦٩﴾

27. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilioomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya waliokufuru. Ole wao waliokufuru kwa Moto utaowapata.

28. Je! Tuwafanye walioamini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au Tuwafanye wachamngu kama waovu?

29. Na hiki Kitabu, Tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili.

Hekima ya kuumbwa Ulimwengu huu.

Allah تعالیٰ Anasema Hakuumba viumbe bila sababu. Aliviumba ili vimuabudu Yeye Peke Yake; kisha Atawakusanya waliopinga Siku ya Qiyamah na Kuwalipa thawabu wale waliokuwa wakimtii na Kuwaadhibu wale waliokufuru na kukaidi. Anasema Allah تعالیٰ,

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطِيلاً ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ

“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya waliokufuru.”

Yaani, wale ambao hawaoni kuwa kufufuliwa na siku ya kurejea vipo na vitatokea na kuona kuwa hakuna chochote tena baada ya Ulimwengu huu.

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنَ النَّارِ

“Ole wao waliokufuru kwa Moto utaowapata.”

Yaani Ole wao, maana Siku ya Kiama watafufuliwa na watapambana na Moto waliotayarishiwa wao. Hapo Allah تعالیٰ Anawaeleza kuwa kwa Uadilifu Wake

na Hekima Yake Hawaweki katika kundi moja wale walioamini na wale waliokufuru. Allah تعالى Anasema:

أَمْرٌ نَجْعَلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَالْمُفْسِدِينَ فِي الْأَرْضِ أَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّفِقِينَ
كَالْفُجَّارِ ۗ

“Je! Tuwafanye walioamini na wakatenda mema kama wafanyao uharibifu katika nchi? Au Tuwafanye wachamungu kama waovu?”

Yaani “Hatutafanya hilo.” Hawa watu hawako sawa mbele ya Allah تعالى; na kwa hilo, hivyo kutakuwa na makundi mawili, lile la wale waliomtii Allah wapewe zawadi zao na wale waovu wataadhibiwa. Hapa kuna mafunzo kwa wale ambao wana akili zao timamu ni kuwa lazima kuna siku ya kufufuliwa na ndiyo siku ya malipo. Hakika sisi tunashuhudia mtu dhalimu katili, mali yake na watoto wake wakizidi pamoja na kuishi katika neema. Ipo siku atakufa. Na kwa upande mwingine tunamuona mtu mtiifu aliyedhulumiwa akifa na udhalili wake. Na kwa Hekima Zake Allah تعالى Ambaye ni Mjuaji wa vitu vyote na Mwenye Hekima na Uadilifu na asiyedhulumu wala chembe Ataleta siku ambayo wale waliokuwa wakinyanyaswa na kudhulumiwa watafanyiwa uadilifu na kupata sitahiki zao. Hilo kama halikutokea hapa duniani basi kuna siku na mahali hayo yataokea na kila mtu atalipwa anachostahiki ama kwa ubaya au kwa wema. Qur’an inatoa mafunzo ambayo yamelenga kuleta uadilifu katika fikra sahihi. Allah تعالى Anasema:

كَتَبْنَا أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ مُبَارَكٌ لِيَدَّبَّرُوا ءَايَاتِهِ وَلِيَتَذَكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ۗ

“Na hiki Kitabu, Tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya Zake, na wawaidhike wenye akili.”

Yaani, wale ambao wamejaaliwa Hekima, akili na wanawaza kuelekea katika usawa wa mambo na kujenga hoja nzito na nzuri.

وَوَهَبْنَا لِدَاوُدَ سُلَيْمَانَ ۚ نِعَمَ الْعَبْدِ ۗ إِنَّهُ ءَأْوَابٌ ۗ ۙ إِذْ عَرَضَ عَلَيْهِ بِالْعَشيِّ الصَّلِيفَتُ

الْحِيَادِ ۗ ۙ فَقَالَ إِنِّي أَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَن ذِكْرِ رَبِّي حَتَّى تَوَارَتْ بِالْحِجَابِ ۗ

رُدُّوهَا عَلَيَّ ۗ فَطَفِقَ مَسْحًا بِالسُّوقِ وَالْأَعْتَابِ ۗ

30. Na Daudi Tukamtunukia Suleiman. Alikuwa mja mwema. Na hakika alikuwa mwingi wa kutubia.

31. Alipopelekewa jioni farasi wasimamao kidete, tayari kutoka shoti;

32. Basi akasema: Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola Wangu Mlezi. Kisha wakafichikana nyuma ya boma.

33. (Akasema:) Nirudishieni! Akaanza kuwapapasa miguu na shingo.

Utajo wa Sulayman عليه السلام, Mtoto wa Dawud عليه السلام.

Allah تعالى Anasema Mtume Dawud عليه السلام alitunukiwa mtoto ambaye alikuwa Mtume kama yeye. Allah تعالى Anasema,

وَوَرِثَ سُلَيْمٰنُ دَاوُدَ

“Na Sulayman alimrithi Daudi...” (27:16).

Yaani, alirithi utume kutoka kwake. Dawud عليه السلام alikuwa na watoto wengine zaidi ya Sulayman عليه السلام, kwani alikuwa na wake mia moja ambao walikuwa si masuria.

نَعَمْ اَلْعَبْدُ اِنَّهٗ اَوَّابٌ

“Alikuwa mja mwema. Na hakika alikuwa mwingi wa kutubia.”

Hii ni sifa anayopewa Sulayman عليه السلام, kwa sababu alikuwa mtiifu sana, akimuabudu Allah تعالى sana na daima alijiegemeza kwa Allah تعالى na kufanya toba.

اِذْ عَرَضَ عَلَيْهِ بِالْعَشِيِّ الصَّافِنَاتُ الْجِيَادُ ﴿٢١﴾

“Alipopelekewa jioni farasi wasimamao kidete, tayari kutoka shoti.”

Yaani, hawa walikuwa farasi waliopewa mafunzo ambao walioneshwa kwa Sulayman عليه السلام akiwa mfalme na mtawala. Mujahid alisema, “Walikuwa farasi waliosimama kwa miguu mitatu na wa wanne ukiwa wameuinua kwa ncha za kwato zao, na walikuwa wenye mwendo wa kasi sana.”¹ Kauli hii pia

¹ At-Tabari 21:192, 193.

ni ya ulamaa wengi wa *Salaf*. Alisema Abu Dawud, kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, baada ya kutoka katika vita vya Tabuk au Khaybar, Mtume ﷺ alirejea nyumbani na akakuta mapazia yanafunika chumba chake. Ulikuwa upepo na ukafunua lile pazia na vikaonekana vitu vya kuchezea vya wanasesere vya mama Aishah رضي الله عنها. Mtume ﷺ akasema,

«مَا هَذَا يَا غَائِثَةُ؟»

“Ewe Aishah nini hiki?”

Akajibu رضي الله عنها, “wanasesere wangu.” Katika kundi la wanasesere hao Mtume ﷺ alimuona farasi mwenye mbawa mbili waliotengenezwa na ngozi, akasema,

«مَا هَذَا الَّذِي أَرَى وَسَطَهُنَّ؟»

“Kile nini ambacho kipo katikati.”

Mama Aishah رضي الله عنها akajibu, “Farasi” Mtume ﷺ akasema,

«مَا هَذَا الَّذِي عَلَيْهِ؟»

“Na hivi ni nini alivyo navyo?”

Akajibu, “Mabawa” Rasuli Karim ﷺ akasema,

«فَرَسٌ لَهُ جَنَاحَانِ؟»

“Farasi mwenye mbawa?”

Akamjibu, “Je hukupata kusikia kuwa Sulayman عليه السلام alikuwa na farasi mweye mabawa.” Kisha Mama Aishah رضي الله عنها akaendelea kusema, “Rasulullahi ﷺ akacheka hadi nikaona magego yake.”¹

فَقَالَ إِنِّي أَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَن ذِكْرِ رَبِّي حَتَّى تَوَارَتْ بِالْحِجَابِ ﴿٢٦﴾

“Basi akasema: Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola Wangu Mlezi. Kisha wakafichikana nyuma ya boma.”

¹ *Fat'h Al-Bari* 2:82, *Muslim* 1:438.

Zaidi ya mmoja miongoni mwa *Salaf* na hata ulamaa wa Tafsiri wamepata kutaja habari hizi kuwa alikuwa ameshughulika na kuangalia hao farasi mpaka muda wa kusali Alasiri ulipita. Hakuacha kuisali Sala hiyo kwa kusudi bali kwa kusahau kama ilivyomtokea Mtume ﷺ katika vita vya Khandaq ambaye alishughulishwa kiasi muda wa Sala ya Alasiri ulipita na akasali baada ya jua kuzama. Habari hizi zimo ndani ya vitabu vya hadithi vya Sahihi kupitia njia mbalimbali ikiwemo riwaya ya Jabir رضي الله عنه ambaye alisema, "Siku ya Vita vya Khandaq Umar رضي الله عنه alifika kwa Mtume ﷺ akaanza kuwalaani makafiri wa Ki-Quraishi, akasema, "Ya Rasulallah, sikuweza kusali Alasiri mpaka karibu na jua kutua." Mtume ﷺ akasema,

«وَاللَّهِ مَا صَلَّيْتُهَا»

"Wallahi hata mimi sijaisali kabisa!"

Jabir رضي الله عنه akasema, "Hivyo tulisimama na tukaenda Buthan. Rasulullahi ﷺ alitawadha nasi tukatawadha. Alisali Alasiri baada ya jua kuzama, na kisha baada ya hapo alisali Maghrib."¹

رُدُّوَهَا عَلَيَّ فَطَفِقَ مَسْحًا بِالسُّوقِ وَالْأَعْنَاقِ ﴿٣٧﴾

"(Akasema:) Nirudishieni! Akaanza kuwapapasa miguu na shingo."

Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, "Alisema (Sulaiman عليه السلام). Hapana Wallahi, hamtanizuia tena kufanya ibada kwa Mola Wangu." Kisha aliamuru farasi wachinjwe."³ Pia ilikuwa ni kauli ya Qatadah. As-Suddi alisema, "Shingo zao na miguu yao zilikatwa kwa mapanga."²

Ali bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn Abbas عنهما رضي الله alisema, "Alianza kukuna na kupapasa vichwa vyao na miguu ya farasi hao kwa kuwapenda kwa uzuri wao."³ Na kauli hii ndio alioikubali Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Alisema, "Hilo ni kwa sababu hawezi kumpa adhabu mnyama kwa kumkata miguu yake, na pia hakuweza kuharibu mali yake kwa sababu tu ameshughulishwa na uzuri wake na akasahau kusali, wakati hilo halikuwa ni kosa la yule mnyama."

¹ At-Tabari 21:195.

² At-Tabari 21:195.

³ At-Tabari 21:196.

Kauli hii ambayo ameikubali Ibn Jarir رحمه الله تعالى inahitaji kuangaliwa kwa kina, kwa sababu kitendo hicho kinawezekana kilikuwa ni sawa katika zama hizo hasa ikizingatiwa kuwa alipata chuki kwa ajili ya Allah تعالى kwa kushughulishwa akili yake na kuangalia wale farasi mpaka, muda wa Sala ukampita, hivyo aliwaharibu kwa ajili ya Allah تعالى; Allah تعالى Alimletea kilicho bora zaidi ya hao farasi, upepo ambao ulivuma jioni taratibu kwa Amri Yake na kumpeleka kokote alikotaka. Ulivuma asubuhi mwendo wa mwezi na ulivuma kurejea mwendo wa mwezi. Kasi hii ilikuwa ni kali na bora kuliko mwendo wa farasi.

Imam Ahmad alisema kutoka kwa Qatadah na Abu Dahma' ambao walikuwa wakisafiri sana kwenda Ka'bah (Makkah) walisema, "Tulikutana na bedui ambaye alisema kutuambia, "Mtume ﷺ alinishika mkono akaanza kunifundisha baadhi ya vitu alivyofundishwa na Allah تعالى." Alisema,

«إِنَّكَ لَا تَدْعُ شَيْئًا اتَّقَاءَ اللَّهِ تَعَالَى إِلَّا أَعْطَاكَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ خَيْرًا مِنْهُ»

*"Hakika huachii jambo Fulani kwa ajili ya Allah, isipokuwa Mwenyezi Mungu Atakupa kile kilicho bora kuliko kile."*¹

وَلَقَدْ فَتَنَّا سُلَيْمَانَ وَأَلْقَيْنَا عَلَى كُرْسِيِّهِ جَسَدًا ثُمَّ أَنَابَ ﴿٣٨﴾ قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكًا لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ مِنْ بَعْدِي إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٣٩﴾ فَسَخَّرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُحَاءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٤٠﴾ وَالشَّيَاطِينَ كُلَّ بِنَاءٍ وَعَوَاصٍ ﴿٤١﴾ وَءَاخِرِينَ مُقَرَّبِينَ ﴿٤٢﴾ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٤٣﴾ هَذَا عَطَاؤُنَا فَامْنُنْ أَوْ أَمْسِكْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٤﴾ وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَقَابٍ ﴿٤٥﴾

34. Na Tulimtia mtihanini Suleiman, na Tukauweka mwili juu ya kiti chake, kisha akarejea kwa kutubu.

35. Akasema: Mola Wangu Mlezi! Nisamehe na Unipe ufalme usiomuelekea yeyote baada yangu. Hakika Wewe Ndiye Mpaji.

36. Basi Tukaufanya upepo umtumikie, ukenda kwa amri yake, popote alipotaka kufika.

¹ Ahmad 5:78.

37. Na Tukayafanya mashetani yamtumikie, wote wajenzi na wapiga mbizi.

38. Na wengine wafungwao kwa minyororo.

39. Hichi ndicho kipawa Chetu. Basi toa au zuia, bila ya hisabu.

40. Na hakika yeye Kwetu Sisi ana cheo cha kukaribishwa Kwetu, na pahala pazuri pa kurejea.

Jinsi Allah عليه السلام Alivyomtahini Sulayman Kisha Akamfadhilisha.

وَلَقَدْ فَتَنَّا سُلَيْمَانَ

“Na Tulimtia mtihanini Suleiman.”

Yaani, “Tulimpa mtihani.”

وَأَلْقَيْنَا عَلَى كُرْسِيِّهِ جَسَدًا

“...na Tukauweka mwili juu ya kiti chake.”¹

ثُمَّ أَنَابَ

“...kisha akarejea kwa kutubu.”

Baada ya mtihani huo, Nabii Sulayman عليه السلام alirejea tena kwenye kiti chake akaomba Toba na akaomba apewe ufalme na milki ambayo hatopata mtu mwingine baada yake.

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَهَبْ لِي مُلْكًا لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ مِّنْ بَعْدِي إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٣٨﴾

“Akasema: Mola Wangu Mlezi! Nisamehe na Unipe ufalme usiomuelekea yeyote baada yangu. Hakika Wewe Ndiye Mpaji.”

¹ Allah عليه السلام Haelezi mwili huo Aliouweka kwenye kiti cha kifalme ulikuwa nini. Tunaamini kuwa Allah عليه السلام Alimtahini kwa kumuekea *Jasad* kwenye kiti cha kifalme, ingawa hatujui nini. Kila lililosemwa juu yake limetokana na *Israilliyaat*, na hatujui yaliyo na ukweli. Kwa kuwa neno hilo linamaanisha “mwili”, basi tafsiri imejikita katika namna ya jini. *Allah A'lam*.

Baadhi ya wafasiri walisema maana yake hapa, "Mtu mwingine asipate haki ya kuomba milki na ufalme kama huo." Hiyo ndiyo maana dhahiri ya Ayah hiyo na kuna Hadithi zinazoeleza vitu vinavyoelekea kwenye maana hiyo. Katika Sahihi Al-Bukhari imeandikwa kuwa Abu Hurairah رضى الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ عِفْرِيئًا مِنَ الْجِنِّ تَمَلَّتْ عَلَيَّ الْبَارِحَةَ - أَوْ كَلِمَةً نَحْوَهَا - لِيَقْطَعَ عَلَيَّ الصَّلَاةَ فَأَمَكَّنَنِي اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى مِنْهُ، وَأَرَدْتُ أَنْ أَرْبِطَهُ إِلَى سَارِيَةٍ مِنْ سَوَارِي الْمَسْجِدِ حَتَّى نُضْبِحُوا، وَتَنْظُرُوا إِلَيْهِ كُلُّكُمْ، فَذَكَرْتُ قَوْلَ أَخِي سُلَيْمَانَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ: ﴿رَبِّ اغْفِرْ لِي وَفِيَّ لِي مُلْكًا لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ مِنْ بَدِيئَةٍ﴾»

"Hakika Ifrit, katika majini kanijia usiku wa jana - au alisema neno kama hilo. Alijaribu kunizuia kusali. Allah Aliniwezesha kumzidi nguvu na nilitaka kumfunga kwenye nguzo moja ya msikiti ili mumuone asubuhi. Nikakumbuka maneno ambayo ndugu yangu, Sulayman: 'Mola Wangu nisamehe na Unipe milki ambayo hatoipata mwingine zaidi yangu.'"

Rawh alisema, "akamuachia, akiwa amedhalilika."¹ Kauli hii pia imo ndani ya Sahihi Muslim na An-Nasai.² Imam Muslim anasema kuwa Abu Darda رضى الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisimama kusali na tukamsikia akisema,

«أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْكَ»

"Najilinda kwa Allah kutokana nawe."

Kisha akasema,

«أَلَعَنَّكَ بِعَنَتِهِ اللَّهُ»

"Nakulaani kwa laana ya Allah."

Mara tatu na akanyoosha mkono wake mbele kama vile anataka kushika kitu. Alipomaliza kusali tulisema, "Ewe Mjumbe wa Allah tumekusikia ukisema neno wakati ulikuwa ukisali hatujapata kukusikia ukilisema kabla ya hapo na tumekuona ukinyoosha mkono." Mtume ﷺ akasema,

¹ Fat-h Al-Bari 1:660.

² Muslim 1:384, An-Nasai katika Al-Kubra 6:443.

«إِنَّ عَدُوَّ اللَّهِ إِبْلِيسَ جَاءَ بِشَهَابٍ مِنْ نَارٍ لِيَجْعَلَهُ فِي وَجْهِ قُلْتُمْ: أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْكَ، ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ قُلْتُمْ: أَلَعَنْتَ لِلَّهِ الثَّامَةَ، فَلَمْ يَتَأَخَّرْ، ثَلَاثَ مَرَّاتٍ ثُمَّ أَرَدْتُ أَنْ أَخُذَهُ، وَاللَّهُ لَوْلَا دَعْوَةُ أَحِينَا سُلَيْمَانَ لَأَصْبَحَ مُوثَقًا، يَلْتَعِبُ بِهِ صِبْيَانُ أَهْلِ الْمَدِينَةِ»

“Adui wa Allah, Iblisi alikuja akiwa amebeba kimwenga (mwanga) wa moto akitaka kunitupia usoni hapo nikasemq, “Audhu billahi minka (yaani najikinga nawe kwa Mola Wangu) mara tatu kisha nikasema, “Nakulaani kwa laana ya Allah”, lakini hakurejea nyuma. Nilisema hivyo mara tatu. Kisha nilitaka kumshika. Wallahi kama si kauli ya ndugu yetu Sulayman angetungwa minyororo na akadhadhakiwa na watoto wa hapa Madinah.”¹

Kauli ya Allah تعالیٰ،

فَسَخَّرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُحَاءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٣٨﴾

“Basi Tukaufanya upepo umtumikie, ukienda kwa amri yake, popote alipotaka kufika.”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالیٰ alisema, “Sulayman alipoghadhibika na kuwachinja farasi wote kwa ajili ya Allah تعالیٰ. Allah تعالیٰ Alimpa kitu kizuri zaidi ya farasi na kinakwenda haraka sana, mwendo wa upepo huo asubuhi ni masafa ya mwendo wa mwezi na jioni marejeo ni mwendo wa mwezi pia.”²

حَيْثُ أَصَابَ

“...popote alipotaka kufika.”

Yaani, kokote alikoelekea au kutaka kwenda ulimwenguni.

وَالشَّيْطَانِ كُلِّ بَنَاءٍ وَعَوَاصٍ ﴿٣٩﴾

“...mashetani yamtumikie, wote wajenzi na wapiga mbizi.”

¹ Muslim 1:385.

² At-Tabari 21:201.

Yaani, miongoni mwao walikuwepo waliokuwa wajenzi wa majumba makubwa yenye mapambo ya namna mbali mbali, mabirika ya maji makubwa kama mabwawa na shughuli nyingi ambazo binadamu walikuwa hawaziwezi. Na kulikuwa na kundi lingine ambalo kazi yake lilikuwa ni kupiga mbizi baharini kuzamia lulu na vitu vingine vya thamani ambavyo havipatikani isipokuwa humo.

وَأَخْرَجْنَا مُقْرِنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

“Na wengine wafungwao kwa minyororo.”

Yaani, wamefungwa kwenye minyororo. Hawa walikuwa ni wale walioasi na wakakataa kufanya kazi au kazi zao zilikuwa mbaya na wakosefu.

هَذَا عَطَاؤُنَا فَامْنُنْ أَوْ أَمْسِكْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٩﴾

“Hichi ndicho kipawa Chetu. Basi toa au zuia, bila ya hisabu.”

Maana yake ni “chukua huu ufalme Tumekupatia, ni ufalme ambao Tumekupa wenye nguvu na uwezo mkubwa, kama ulivyoomba uwezo wa kumpa yeyote kitu au kumnyima na kutoulizwa kwa hayo. Chochote utakachofanya ni rukhsa kwako na pia ni uamuzi wako, ndio amri na utakuwa sahihi. Imethibiti Hadithi ndani ya Sahihi Bukhari na Muslim kuwa Mtume ﷺ alipotumwa kwetu alikhiarishwa kuchagua kati ya kuwa mtumwa na Mtume (Abdan Rasula) ambaye anafanya kile anachotumwa na anagawa vitu kwa watu kama Allah تعالیٰ Anavyomuamuru. Na awe Nabii na Mfalme ambaye anaweza kutoa chochote kwa yeyote atakavyo au kumnyima yeyote chochote bila kuwa na lawama juu ya hilo au lile. Mtume Muhammad alichagua kuwa mtumwa na Mtume (Abdan na Rasula) Alitaka ushauri kwa Jibril عليه السلام ambaye alimuambia, “Usijikweze”. Hivyo akachagua hali ya kwanza kwa sababu ni daraja kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na inampa nafasi kubwa mbele ya Allah تعالیٰ siku ya Kiyama, japokuwa Unabii na ufalme una nafasi kubwa hapa duniani na Akhera. Vilevile Allah تعالیٰ Anaposema kuwa Kampa Sulayman nafasi kubwa hapa duniani bado anasema kuwa Atampa hadhi kubwa Siku ya Kiyama.

وَأَنَّ لَهُمْ عِنْدَنَا لُزْفًا وَحُسْنَ مَقَابٍ ﴿٤٠﴾

“Na hakika yeye Kwetu Sisi ana cheo cha kukaribishwa Kwetu, na pahala pazuri pa kurejea.” Yaani katika dunia hii na Akhera.

وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا أَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الشَّيْطَانُ
 بِنُصْبٍ وَعَذَابٍ ﴿٤١﴾ أَرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسَلٌ بَارِدٌ
 وَشَرَابٌ ﴿٤٢﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةً مِنَّا
 وَذَكَرَى لِأُولَى الْأَلْبَابِ ﴿٤٣﴾ وَخُذْ بِيَدِكَ ضِغْثًا فَاصْرَبْ
 بِهِ وَلَا تَحْنُتْ ۗ إِنَّا وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نِعْمَ الْعَبْدُ ۗ إِنَّهُ أَوَّابٌ
 ﴿٤٤﴾ وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولَى
 الْأَيْدِي وَالْأَبْصَارِ ﴿٤٥﴾ إِنَّا أَخْلَصْنَاهُمْ بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى
 الدَّارِ ﴿٤٦﴾ وَإِلَيْهِمْ عِندَنَا لَمَنَ الْمُضْطَفِينَ الْأَخْيَارِ ﴿٤٧﴾
 وَأَذْكُرْ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ ۗ وَكُلٌّ مِّنَ الْأَخْيَارِ
 ﴿٤٨﴾ هَذَا ذِكْرٌ وَإِن لِلْمُتَّقِينَ لِحُسْنِ مَقَابِرٍ ﴿٤٩﴾ جَنَّتٍ
 عَدْنٍ مَّفْتَحَةٌ هُمُ الْأَبْوَابُ ﴿٥٠﴾ مُتَّكِئِينَ فِيهَا يَدْعُونَ فِيهَا
 بِفَيْكِهِمْ كَثِيرَةً وَشَرَابٍ ﴿٥١﴾ * وَعِنْدَهُمْ قَصِيرَاتٌ
 الطَّرْفِ أُنْتَابُ ﴿٥٢﴾ هَذَا مَا تُوْعَدُونَ لِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٥٣﴾
 إِنَّ هَذَا لَرِزْقُنَا مَا لَهُ مِن نَّفَادٍ ﴿٥٤﴾

وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا أَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ
 أَنِّي مَسَّنِيَ الشَّيْطَانُ بِنُصْبٍ وَعَذَابٍ
 ﴿٤١﴾ أَرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسَلٌ
 بَارِدٌ وَشَرَابٌ ﴿٤٢﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ أَهْلَهُ
 وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةً مِنَّا وَذَكَرَى
 لِأُولَى الْأَلْبَابِ ﴿٤٣﴾ وَخُذْ بِيَدِكَ
 ضِغْثًا فَاصْرَبْ بِهِ وَلَا تَحْنُتْ ۗ إِنَّا
 وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نِعْمَ الْعَبْدُ ۗ إِنَّهُ
 أَوَّابٌ ﴿٤٤﴾

41. Na mkumbuke mja
 Wetu Ayubu alipomuita
 Mola Wake Mlezi akasema:
 Kwa hakika Shetani
 amenifikishia udhia na
 adhabu.

42. (Akaambiwa:) Piga-piga
 ardhi kwa mguu wako! Basi
 haya maji baridi ya kuogea
 na ya kunywa.

43. Na Tukampa ahali zake na wengine kama wao pamoja nao, kuwa ni
 Rehema itokayo Kwetu, na iwe ukumbusho kwa watu wenye akili.

44. Na shika kicha cha vijiti tu mkononi mwako, kisha ndio upigie nacho,
 wala usivunje kiapo. Hakika Tulimkuta mwenye subira, mbora wa waja, kwa
 hakika alikuwa mwingi wa kutubu.

Utajo wa Ayyub عليه السلام

Hapa Allah تعالى Anatuambia habari juu ya mja Wake na Mtume Wake Ayyub عليه السلام na jinsi Alivyompa mitihani. Mitihani hii ilikuwa juu ya afya yake, mali na watoto wake, maradhi haya hayakuacha sehemu katika mwili wake salama isipokuwa moyo wake. Hapakuwa tena na chochote duniani ambacho alikitumia ili ajitibu maradhi yake, au aondoe mashaka yaliyokuwa yamemzingira zaidi ya mke wake ambaye alidumu naye kwa sababu ya Imani ya juu ya Mola Wake na Mtume Wake.

Katika hali hiyo mama huyo alikuwa akifanya kazi za kibarua kwa watu na akaapa kujikimu na kumhudumia mumewe Ayyub kwa miaka ipatayo kumi na nane. Kabla ya hapo Ayyub عليه السلام alikuwa ana uwezo wa kimali na alikuwa na watoto wengi, yaani alikuwa na nafasi nzuri katika mambo ya kidunia. Vyote hivyo viliondoka na kutoweka na akaishia kuwa katika jalala miongoni mwa majalala ya mjini kwa kipindi chote hicho akinyanyapaliwa na ndugu na watu wengine kwa pamoja isipokuwa mkewe tu. Hakumwacha mchana wala usiku isipokuwa pale alipokuwa akifanya kibarua ili apate mahitaji ya kujikimu na kumhudumia mumewe, na kisha hurejea kwake mara moja. Mambo yalipofika na kuwa mabaya zaidi, Ayyub عليه السلام aliomba kwa Mola wake akasema,

أَنِّي مَسْنِي الضُّرِّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٤١﴾

“Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye Unayerehemu kuliko wote wanaorehemu.”

Na kwa mujibu wa aya hii,

وَأَذْكُرُّ عَبْدَنَا أَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسْنِي الشَّيْطَانِ يَنْصُبْ وَعَذَابِ ﴿٤٢﴾

“Na mkumbuke mja Wetu Ayyubu alipomuita Mola wake Mlezi akasema: Kwa hakika Shetani amenifikishia udhia na adhabu.”

Yaani “madhila” haya ya kimwili na adhabu iliyotajwa ni kupotelewa mali na watoto. Kisha Allah تعالى alijibu dua yake kwa kumuambia asimame wima kisha apige guu lake chini. Hilo alilifanya na pakatokea kijito cha maji yakibubujika. Allah تعالى Alimuamuru (Ayyub عليه السلام) aoge humo katika hiyo chemchem na maumivu yake yote ya mwilini yalitoweka. Kisha akamuamuru tena apige kwa

mguu wake mahali pengine na alipofanya hivyo ikatokea chemchem kisha akapewa amri ya kunywa kutoka chemchem hiyo, hivyo matatizo yake yote ya ndani yakaisha akawa mtu mwenye afya kamili ndani na nje.

Allah Anasema,

أَرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسِلٌ بَارِدٌ وَشَرَابٌ ﴿٤١﴾

“(Akaambiwa:) Piga-piga ardhi kwa mguu wako! Basi haya maji baridi ya kuogea na ya kunywa.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى walisema kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ نَبِيَّ اللَّهِ أَيُّوبَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ لَبِثَ بِهِ بَلَاؤُهُ ثَمَانِي عَشْرَةَ سَنَةً، فَرَفَضَهُ الْقَرِيبُ وَالْبُعِيدُ، إِلَّا رَجُلَيْنِ كَانَا مِنْ أَحْصَى إِخْوَانِهِ بِهِ، كَانَا يَغْدُوَانِ إِلَيْهِ وَيُرْوِحَانِ، فَقَالَ أَحَدُهُمَا لِصَاحِبِهِ: تَعْلَمُ وَاللَّهِ لَقَدْ أَذْنَبَ أَيُّوبُ ذَنْبًا مَا أَذْنَبَهُ أَحَدٌ مِنَ الْعَالَمِينَ، قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ: وَمَا ذَاكَ؟ قَالَ: مُنْذُ ثَمَانِي عَشْرَةَ سَنَةً لَمْ يَرَحْمَهُ اللَّهُ فَيَكْشِفَ مَا بِهِ، فَلَمَّا رَاحَا إِلَيْهِ لَمْ يَضِرَّ الرَّجُلُ حَتَّى ذَكَرَ ذَلِكَ لَهُ، فَقَالَ أَيُّوبُ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ: لَا أَدْرِي مَا تَقُولُ، غَيْرَ أَنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يَعْلَمُ أَنِّي كُنْتُ أَمْرُ عَلَى الرَّجُلَيْنِ يَتَنَزَّعَانِ فَيَذَكُرَانِ اللَّهَ تَعَالَى، فَأَرْجِعْ إِلَى بَيْتِي فَأَكْفُرْ عَنْهُمَا كَرَاهِيَةً أَنْ يَذَكُرَ اللَّهُ تَعَالَى إِلَّا فِي حَقِّي، قَالَ: وَكَانَ يَخْرُجُ إِلَيَّ حَاجِيهِ، فَإِذَا قَضَاهَا أَمْسَكَتْ أَمْرَانَهُ بِيَدِهِ حَتَّى يَبْلُغَ، فَلَمَّا كَانَ ذَلِكَ يَوْمَ أَنْبَطَ عَلَيْهَا، فَأَوْحَى اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى إِلَيَّ أَيُّوبُ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ أَنْ ﴿أَرْكُضْ بِرِجْلِكَ هَذَا مُغْتَسِلٌ بَارِدٌ وَشَرَابٌ﴾ ﴿٤١﴾ فَاسْتَبَطَّأْتُهُ [فَتَلَقَّئْتُهُ] تَنْظُرُ، فَأَقْبَلَ عَلَيْهَا وَقَدْ أَذْهَبَ اللَّهُ مَا بِهِ مِنَ الْبَلَاءِ وَهُوَ عَلَى أَحْسَنِ مَا كَانَ، فَلَمَّا رَأَتْهُ قَالَتْ: أَيُّ بَارَكَ اللَّهُ فِيكَ، هَلْ رَأَيْتَ نَبِيَّ اللَّهِ هَذَا الْمُبْتَلَى، فَوَاللَّهِ عَلَى ذَلِكَ مَا رَأَيْتُ رَجُلًا أَشْبَهَ بِهِ مِنْكَ إِذْ كَانَ صَحِيحًا. قَالَ: فَإِنِّي أَنَا هُوَ، قَالَ: وَكَانَ لَهُ أَنْدَرَانِ: أَنْدَرٌ لِلْفَمْحِ وَأَنْدَرٌ لِلشَّعِيرِ، فَبَعَثَ اللَّهُ تَعَالَى سَحَابَتَيْنِ فَلَمَّا كَانَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى أَنْدَرِ الْفَمْحِ، أَفْرَعَتْ فِيهِ الذَّهَبَ حَتَّى فَاضَ، وَأَفْرَعَتْ الْأُخْرَى فِي أَنْدَرِ الشَّعِيرِ حَتَّى فَاضَ»

“Nabii wa Allah, Ayyub عليه السلام alikaa na balaa kwa miaka kumi na nane; walimkataa jamaa wa karibu na wa mbali isipokuwa watu

wawili ambao walikuwa watu mahususi zaidi kwake. Hawa wawili walimtembelea kila asubuhi na jioni, siku moja, mmoja wao alimuuliza mwenziwe, “Kwa miaka kumi na nane Allah Hajamletea Rahma Zake ili kumuondolea maradhi na taabu zake.” Walipomtembelea Nabii siku ya pili yake asubuhi, mwenziwe hakuvumilia kumuambia habari hizo Nabii wa Allah Ayyub, Mjumbe wa Allah akasema, “Sijui hayo uyasemayo, lakini Allah Anajua kuwa nilipita nikakuta njiani watu wawili wakibishana na kisha kutaja majina ya Allah, nikaona kuwa nirejee nyumbani nikatoe kafara huenda wale watu wawili wamesema na kutaja Majina ya Allah katika njia ya makosa.” Na kila alipomaliza haja yake, mkewe alimshika mkono na kumrejeshwa nyumbani. Siku moja alikawiya kurejea kutoka kukidhi haja, Allah Alikuwa Amempa wahyi, **“Piga ardhi kwa mguu wako. Haya ni maji ya kujisafisha nayo ni baridi na matamu kwa kunywa.”** Mke aliona mumewe kachelewa sana hivyo akaenda kumfuata akimtafuta ajue amepatwa na nini. Huko aliona kuwa Allah Amemuondolea balaa lililomhangaisha na alionekana akiwa mwenye hali nzuri na afya zaidi ya vile alivyopata kuwa hapo kabla. Alipomuona alimuambia, “Mola Akubariki, Je umemuona Nabii wa Allah ambaye amefikwa na mtihani? Wallah sijapata kumuona mtu anayefanana nawe kama kipindi chake cha afya njema!” Nabii Ayyub akasema, “Mimi hapa.” Alikuwa na uga mbili za kupigia ngano na shayiri. Mwenyezi Mungu Akashusha viwingu viwili.¹ Kimoja kilipofikia uga wa ngano kilinyesha dhahabu mpaka uga huo ukajaa. Na kingine kilinyesha dhahabu juu ya uga wa shayiri mpaka ukajaa.”

Maelezo haya ni kwa maelezo aliyoeleza Ibn Jarir رحمه الله تعالى.²

Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Alisema Mtume ﷺ,

¹ Mahali ambapo makapi huondolewa mbali na mbegu.

² At-Tabari 21:211. Riwaya sawa na hiyo iliandikwa na Al-Hakim na. 4115, na wengine.

«بَيْنَمَا أَيُّوبُ يُغْتَسِلُ غُرْيَانًا خَرَّ عَلَيْهِ جَرَادٌ مِنْ ذَهَبٍ فَجَعَلَ أَيُّوبُ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ
وَالسَّلَامُ يَخْتُو فِي نَوْبِهِ، فَنَادَاهُ رَبُّهُ عَزَّ وَجَلَّ يَا أَيُّوبُ، أَلَمْ أَكُنْ أَعْتَيْتَكَ عَمَّا تَرَى
قَالَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ: بَلَى يَا رَبِّ، وَلَكِنْ لَا غِنَى بِي عَنْ بَرِّكَتِكَ»

“Wakati Ayyub عليه السلام alikuwa akioga akiwa uchi walimwangukia nzige wa dhahabu. Ayyub عليه السلام akaanza kuwakusanya ndani ya nguo yake. Kisha Allah Akamuita, “Ewe Ayyub je sijakufanya wewe tajiri kiasi kuwa huhitaji hayo unayoyaona?” Ayyub عليه السلام akasema, “Naam Yarabi lakini mimi sitosheki na baraka Zako!”

Hizi habari ziko katika Bukhari tu.¹

وَوَهَبْنَا لَهُدْ أَهْلَهُدْ وَمِثْلَهُم مَّعَهُم رَحْمَةً مِنَّا وَذَكَرْنَا لِأُولَى الْأَلْبَابِ ﴿٤١﴾

“Na Tukampa ahali zake na wengine kama wao pamoja nao, kuwa ni Rehema itokayo Kwetu, na iwe kumbusho kwa watu wenye akili.”

Al-Hasan na Qatada walisema Allah تعالى Aliirejesha familia ya Ayyub عليه السلام katika uhai wao na kumuongezea watoto wengine kama hao.”²

رَحْمَةً مِنَّا

“...kuwa ni Rehema itokayo Kwetu.”

Yaani, ikiwa ni jibu la subira zake na uvumilivu wake na umakini wake, kutubu kwake, asiyetaka makuu na daima kuwa mwenye kumuelekea Allah تعالى.

وَذَكَرْنَا لِأُولَى الْأَلْبَابِ

“...na iwe kumbusho kwa watu wenye akili.”

Yaani ni watu wale ambao wanaelewa mambo kuwa subira ndio suluhisho ya mashaka yote.

وَخُذْ بِيَدِكَ ضِعْفًا فَاصْرَبْ بِهِ وَلَا تَحْتَسِبْ

“Na shika kicha cha vijiti tu mkononi mwako, kisha ndio upigie nacho, wala usivunje kiapo.”

¹ Al-Bukhari 279, 3391, 7493.

² At-Tabari 21:212.

Sababu ya Ayyub عليه السلام kuapa, alikuwa amemkasirikia mkewe juu ya jambo alilolifanya mkewe na akaweka nadhiri kuwa iwapo Allah تعالى Atampa afya njema atamtandika mijeledi mia moja. Na kweli Allah تعالى Akamrejeshea afya njema, sasa vipi huyu mama kwa uvumilivu wake, huruma zake, huduma zake na ukarimu wake alipizwe kwa kuchapwa bakora? Allah تعالى Akamuonesha njia ya kusuluhisha hilo ambayo ilikuwa ni kuchukua kitita cha usamba wenye vijiti mia moja. Hivyo avipige mara moja. Hivyo akawa ametimiza nadhiri yake. Hili ndilo lilikuwa suluhisho kwa mtu aliye na Taqwa ya Allah تعالى na kurejea Kwake kwa kufanya toba.

Allah تعالى Anasema.

إِنَّا وَجَدْنَاهُ صَابِرًا نَعْمَ الْعَبْدُ إِنَّهُ أَوَّابٌ

"Hakika Tulimkuta mwenye subira, mbora wa waja, kwa hakika alikuwa mwingi wa kutubu."

Allah تعالى Anamsifu na Kumnyanyua makamu yake; na Anasema,

نَعْمَ الْعَبْدُ إِنَّهُ أَوَّابٌ

"...mbora wa waja, kwa hakika alikuwa mwingi wa kutubu."

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۚ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ بَلِغٌ أَمْرِهِ ۗ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴿٢٦﴾

"Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea. Na Humruzuku kwa jiha asiyotazamia. Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu Yeye Humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu Anatimiza Amri Yake. Mwenyezi Mungu Kajaalia kila kitu na kipimo chake." (65:2-3).

وَأَذْكُرْ عِبْدَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولَى الْأَيْدِي وَالْأَبْصَارِ ﴿٢٧﴾ إِنَّا أَخْلَصْنَاهُمْ بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى الدَّارِ ﴿٢٨﴾ وَإِنَّمْ عِنْدَنَا لِمَنْ الْمُصْطَفَيْنَ الْأَخْيَارِ ﴿٢٩﴾ وَأَذْكُرْ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ ۗ وَكُلٌّ مِنَ الْأَخْيَارِ ﴿٣٠﴾

45. Na wakumbuke waja Wetu, Ibrahim na Is-haqa na Yaa'qubu waliokuwa na nguvu na busara.

46. Sisi Tumewakhusisha wao kwa sifa ya ukumbusho wa Akhera.

47. Na hakika wao Kwetu sisi ni wateuliwa walio bora.

48. Na mkumbuke Ismail na Alyasaa na Dhulkifli, na wote hao ni katika walio bora.

Utajo wa Mitume Wateule Bora Zaidi

Allah تعالى Anatuambia juu ya matendo mema ya waja wake miongoni mwa Manabii wake na Mitume.

وَأَذْكُرْ عَبْدَنَا إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ أُولَى الْأَيْدِي وَالْأَبْصَارِ ﴿٤٥﴾

“Na wakumbuke waja Wetu, Ibrahim na Is-haqa na Yaa'qubu waliokuwa na nguvu na busara.”

Yaani, matendo mema, elimu yenye manufaa, nguvu kubwa katika kufanya ibada na busara. Ali bin Abi Talhah alisema, kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema.

أُولَى الْأَيْدِي

“...walio kuwa na nguvu...”

“Wenye nguvu nyingi na ibada nyingi.”

وَالْأَبْصَارِ

“...na busara.”

Yaani, maarifa na utambuzi katika werevu wa dini, Qatadah na As Suddi walisema, “Walipewa uwezo mkubwa wa kufanya ibada na ufahamu wa dini?”¹

إِنَّا أَخْلَصْنَاهُمْ بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى الدَّارِ ﴿٤٦﴾

“Sisi Tumewakhusisha wao kwa sifa ya ukumbusho wa Akhera.”

¹ At-Tabari 21:215.

Mujahid alisema, “Maana yake ni, “Tuliwaonya wafanye juhudi kubwa kwa ajili ya Akhera, na hapakuwa na lingine lolote ambalo walilielekea zaidi ya hilo.”¹ As Suddi naye alisema, “Wanakumbuka Akhera na kuweka juhudi nyingi ili kuipata Akhera.”² Malik bin Dinari alisema, “Allah تعالی Aliwaondolea hali ya kuipenda hii dunia katika nyoyo zao na Akawateua kwa kuwa wenye kukumbuka mambo ya Akhera.” Qatadah alisema, “Walikuwa wakiwakumbusha watu juu ya makazi ya Akhera na kuwalingania wawe wenye kuitaka Pepo huko akhera.”³

وَأَيُّهُمْ عِنْدَنَا لَمِنَ الْمُصْطَفَيْنَ الْأَخْيَارِ ﴿٤٧﴾

“Na hakika wao Kwetu sisi ni wateuliwa walio bora.”

Yaani, wao ni miongoni mwa wale walioteuliwa na kuchaguliwa na wao hawa ni wabora miongoni mwa wale waliochaguliwa,

وَأَذْكُرْ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ وَكُلٌّ مِنَ الْأَخْيَارِ ﴿٥١﴾

“Na mkumbuke Ismail na Alyasaa na Dhulkifli, na wote hao ni katika walio bora.”

Mitume tayari tumekwisha eleza tabia zao na visa juu yao kwa kirefu katika Surat Al-Anbiya, hivyo hamna haja ya kurejea habari hizo hapa.

هَذَا ذِكْرٌ

“Huu ni ukumbusho.”

Yaani ukumbusho kwa wale ambao watazingatia. As Suddi alisema, “Maana yake hapa ni Qur’an Tukufu.”⁴

هَذَا ذِكْرٌ وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَقَابٍ ﴿٥٢﴾ جَنَّاتٍ عَدْنٍ مُمْتَحِنَةً هُمْ فِيهَا يَدْخُلُونَ ﴿٥٣﴾ وَعِنْدَهُمْ قَصِيرَاتُ الْإِبْرَةِ ﴿٥٤﴾ هَذَا مَا تُوَعَّدُونَ لِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٥٥﴾ إِنَّ هَذَا لَرِزْقُنَا مَا لَهُ مِنْ نَفَادٍ ﴿٥٦﴾

¹ At-Tabari 21:218.

² At-Tabari 21:218.

³ At-Tabari 21:217.

⁴ At-Tabari 21:220.

49. Huu ni ukumbusho. Na hakika wachamungu wana marudio mazuri.

50. Bustani za milele zitazofunguliwa milango yao kwa ajili yao.

51. Humo wataegemea matakia, wawe wanaagiza humo matunda mengi na vinywaji.

52. Na pamoja nao wake zao wenye kutuliza macho, hirimu zao.

53. Haya ndiyo mliyoahidiwa kwa Siku ya Hisabu.

54. Hakika hii ndiyo riziki yetu isiyomalizika.

Ubainisho wa Marejeo ya Waliobarikiwa

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa waja Wake waliobarikiwa wachamungu watakuwa na marejeo mazuri huko Akhera ambako ndio mahali pa mwisho. Kisha Anafafanua zaidi kwa undani kama ifuatavyo:

جَنَّاتٍ عَدْنٍ

"Bustani za milele..." Yaani, bustani ya milele Peponi.

مُفْتَحَةً لَهُمُ الْأَبْوَابُ

"...zitazofunguliwa milango yao kwa ajili yao."

Na pale watakapoziendea (bustani) milango yake itafunguliwa (ili waingie).

مُتَّكِنِينَ فِيهَا

"Humo wataegemea..."

Ilikuwa ikisemwa kuwa watakaa mkao wa tarabui (wamekunja miguu yao) juu ya viti wakiwa chini ya vivuli.

يَدْعُونَ فِيهَا بِفَلَاحِهِمْ كَثِيرَةً

"...wawe wanaagiza humo matunda mengi..."

Yaani, chochote watakachotaka, watakipata na kitakuwa kimetayarishwa katika hali ambayo wao wanakitaka.

وَشَرَابٍ

“...na vinywaji.”

Yaani, kinywaji chochote watakachokitaka basi watumishi wao watawaletea. Ni kama Aya,

بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقَ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿٥٦﴾

“Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.” (56:18)

وَعِنْدَهُمْ قَصِيرَاتُ الْطَّرْفِ

“Na pamoja nao wake zao wenye kutuliza macho...”

Yaani, wanahifadhi tupu zao dhidi ya wote, isipokuwa waume wao, na hawamtazami mwingine yeyote.

أُتْرَابٍ

“...hirimu zao.” Yaani, wa umri mmoja.

Hivi ndivyo alivyoelewa Ibn Abbas رضي الله عنهما pia vivyo hivyo Mujahid, Said bin Jubayri Muhammad bin Ka'b na As-Suddi.¹

هَذَا مَا تُوْعَدُونَ لِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٥٧﴾

“Haya ndiyo mliyoahidiwa kwa Siku ya Hisabu.”

Maana yake Allah تعالى Amevitayarisha vyote hivi kwa ajili ya wachamungu ambao watafikia huko baada ya kufufuliwa na kutoka ndani ya makaburi wakiwa wameokolewa na moto wa Jahanamu. Kisha Allah تعالى Anatuambia kuwa Pepo haina mwisho wala haitapotea au kuacha kuendelea kuwepo. Allah تعالى Anasema,

إِنَّ هَذَا لَرِزْقُنَا مَا لَهُ مِن نَّفَادٍ ﴿٥٨﴾

“Hakika hii ndiyo Riziki Yetu isiyomalizika.”

Hii aya ni kama Aya:

¹ At-Tabari 21:218.

مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ ۗ

"Mlavyonavyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyobakia." (16:96)

عَطَاءٌ غَيْرٌ مَّجْدُودٍ ﴿١١٠﴾

"Hicho ni kipawa kisio na ukomo." (11:108),

هُمْ أَجْرٌ غَيْرٌ مَّمْنُونٍ ﴿٨٤﴾

"...hao watakuwa na ujira usiomalizika." (84:25) na

أَكُلُهَا دَائِمًا وَظِلُّهَا تِلْكَ عُقْبَى الَّذِينَ اتَّقَوْا وَعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ ﴿١٣﴾

"...matunda yake ni ya daima, na pia kivuli chake. Huu ndio mwisho wa wale waliojilinda. Na mwisho wa makafiri ni Moto." (13:35).

Na kuna aya kama hizo nyingi.

* * *

هَذَا وَإِنَّ لِلطَّغِيْنَ لَشَرَّ مَقَابٍ ﴿٥٥﴾ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا
 فَيَسَّسَ الْإِهَادُ ﴿٥٦﴾ هَذَا فَلْيَذُوقُوهُ حَمِيمٌ وَعَسَاقٌ ﴿٥٧﴾
 وَآخِرُ مِنْ شَكْلِيَّةِ أَزْوَاجٍ ﴿٥٨﴾ هَذَا فَوْجٌ مُّقْتَحِمٌ مَّعَكُمْ
 لَا مَرْحَبًا بِهِمْ ﴿٥٩﴾ إِنَّهُمْ صَالُوا النَّارِ ﴿٦٠﴾ قَالُوا بَلْ أَنتُمْ لَا
 مَرْحَبًا بِكُمْ ﴿٦١﴾ أَنتُمْ قَدَّمْتُمُوهُ لَنَا فَيَسَّسَ الْقَرَارُ ﴿٦٢﴾ قَالُوا
 رَبَّنَا مَنْ قَدَّمَ لَنَا هَذَا فَرِذَّةً عَذَابًا ضِعْفًا فِي النَّارِ ﴿٦٣﴾
 وَقَالُوا مَا لَنَا لَا نَرَى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِنَ الْأَشْرَارِ ﴿٦٤﴾
 أَخَذْنَاهُمْ سِجْرِيًّا أَمْ زَاغَتْ عَنْهُمْ الْأَبْصَارُ ﴿٦٥﴾ إِنَّ ذَلِكَ
 لَحَقٌّ تَخَاصُمُ أَهْلِ النَّارِ ﴿٦٦﴾ قُلْ إِنَّمَا أَنَا مُنذِرٌ وَمَا مِنْ
 إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٦٧﴾ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَمَا بَيْنَهُمَا الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٦٨﴾ قُلْ هُوَ نَبَوُّا عَظِيمٌ ﴿٦٩﴾
 أَنْتُمْ عَنْهُ مُعْرِضُونَ ﴿٧٠﴾ مَا كَانَ لِي مِنْ عِلْمٍ بِالْمَلَأِ
 الْأَعْلَى إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٧١﴾ إِنْ يُوحَىٰ إِلَيَّ إِلَّا أَنَّمَا أَنَا
 نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٧٢﴾

هَذَا وَإِنَّ لِلطَّغِيْنَ لَشَرَّ مَقَابٍ ﴿٥٥﴾ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا
 فَيَسَّسَ الْإِهَادُ ﴿٥٦﴾ هَذَا فَلْيَذُوقُوهُ حَمِيمٌ وَعَسَاقٌ ﴿٥٧﴾
 وَآخِرُ مِنْ شَكْلِيَّةِ أَزْوَاجٍ ﴿٥٨﴾ هَذَا فَوْجٌ مُّقْتَحِمٌ مَّعَكُمْ
 لَا مَرْحَبًا بِهِمْ ﴿٥٩﴾ إِنَّهُمْ صَالُوا النَّارِ ﴿٦٠﴾ قَالُوا بَلْ أَنتُمْ لَا
 مَرْحَبًا بِكُمْ ﴿٦١﴾ أَنتُمْ قَدَّمْتُمُوهُ لَنَا فَيَسَّسَ الْقَرَارُ ﴿٦٢﴾ قَالُوا
 رَبَّنَا مَنْ قَدَّمَ لَنَا هَذَا فَرِذَّةً عَذَابًا ضِعْفًا فِي النَّارِ ﴿٦٣﴾
 وَقَالُوا مَا لَنَا لَا نَرَى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِنَ الْأَشْرَارِ ﴿٦٤﴾
 أَخَذْنَاهُمْ سِجْرِيًّا أَمْ زَاغَتْ عَنْهُمْ الْأَبْصَارُ ﴿٦٥﴾ إِنَّ ذَلِكَ
 لَحَقٌّ تَخَاصُمُ أَهْلِ النَّارِ ﴿٦٦﴾ قُلْ إِنَّمَا أَنَا مُنذِرٌ وَمَا مِنْ
 إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٦٧﴾ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 وَمَا بَيْنَهُمَا الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٦٨﴾ قُلْ هُوَ نَبَوُّا عَظِيمٌ ﴿٦٩﴾
 أَنْتُمْ عَنْهُ مُعْرِضُونَ ﴿٧٠﴾ مَا كَانَ لِي مِنْ عِلْمٍ بِالْمَلَأِ
 الْأَعْلَى إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٧١﴾ إِنْ يُوحَىٰ إِلَيَّ إِلَّا أَنَّمَا أَنَا
 نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٧٢﴾

55. Ndio hivi! Na hakika wenye kuasi bila ya shaka watapata marudio maovu kabisa;

56. Nayo ni Jahannamu! Wataingia humo. Nacho hicho ni kitanda kiovu mno cha kulalia.

57. Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto na ya usaha!

58. Na adhabu nyenginezo za namna hii.

59. Hili ndilo kundi litakaloingia pamoja nanyi. Hapana makaribisho mema kwao. Hakika hao wanaingia Motoni.

60. Waseme: Lakini nyinyi! Hamna mapokezi mazuri! Nyinyi ndio mliotusababishia haya, napo ni pahala paovu kabisa!

61. Waseme: Mola Wetu Mlezi! aliyetusababishia haya mzdishie adhabu mara mbili Motoni.

62. Watasema: Tuna nini hata hatuwaoni wale watu ambao Tukiwahisabu ndio katika waovu?

63. Tulikosea tulipo wafanyia maskhara, au macho yetu tu hayawaoni?

64. Hakika hayo bila ya shaka ndiyo makhasimiano ya watu wa Motoni.

Ubainisho wa Mwisho wa Ovu

Baada ya kueleza mwisho wa (watu) waliobarikiwa, Allah تعالی Anaeleza marejeo ya walioangamia watakapofufuliwa na kuletwa kuhojiwa. Allah تعالی Anasema:

هَذَا وَإِنَّ لِلطَّيغِينَ

“Ndio hivi! Na hakika wenye kuasi...”

Ni maelekezo kwa wale waliomuasi Allah تعالی, waliowapinga Mitume wa Allah.

لَثَرَّ مَثَابٍ

“...bila ya shaka watapata marudio maovu kabisa.”

Yaani, marejeo maovu.

جَهَنَّمَ يَصَلُّونَهَا

“Nayo ni Jahannamu! Wataingia humo.”

Kisha Allah تعالی Anaelezea hayo kwa kusema, yaani wataingia na itawazingira kila upande.

فَبَيْسَ الْمُهَادِّ هَذَا فَلْيَذُوقُوهُ حَمِيمٌ وَغَسَّاقٌ

“Nacho hicho ni kitanda kiovu mno cha kulalia. Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto na ya usaha!”

Hamim ni kile kitu ambacho kimekwisha chemshwa na kupata upeo wa juu wa joto; na *Ghassaq* ni kinyume chake yaani kitu kile ambacho kimepata ubaridi wa kiwango ambacho hakivumiliki. Allah تعالی Anasema,

وَأَخْرَجْنَا مِنْ شَكْلَةٍ أَزْوَاجًا ﴿٥٥﴾

“Na adhabu nyenginezo za namna hii.”

Yaani, vitu vingine vya aina hiyo, yaani vitu vinginevyo aina hiyo na kinyume chake vikiletwa kama adhabu. Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema juu ya ayah hii.

وَأَخْرَجْنَا مِنْ شَكْلَةٍ أَزْوَاجًا ﴿٥٦﴾

“Na adhabu nyenginezo za namna hii.”

Adhabu mbali mbali tofauti, Wafasiri wengine walisema kuwa (adhabu hizo) kama baridi kali kama hiyo au joto kali kama hilo, kunywa *Hamim* na kula vitu kama mti mchungu wa *Zaqum*; au kuinuliwa juu na kutupwa chini na adhabu nyingine tofauti¹ ambazo zina kinyume chake kichungu. Yote hayo ni katika aina mbalimbali watakozoadhibiwa na kuteswa kwa sababu yake.

Kugombana Watu wa Motoni

هَذَا فَوْجٌ مُّقْتَحِمٌ مَّعَكُمْ لَا مَرْحَبًا بِهِمْ إِنَّهُمْ صَالُوا النَّارِ ﴿٥٧﴾

“Hili ndilo kundi litakaloingia pamoja nanyi. Hapana makaribisho mema kwao. Hakika hao wanaingia Motoni.”

Hapa Allah تعالی Anatueleza upande wa Motoni watasemezana wenyewe kwa wenyewe. Hii ni kama aya,

كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ أُخْتَهَا ﴿٥٨﴾

“Kila utakapoingia umma utawalaani wenzake.” (7:38),

Yaani, badala ya kusalimiana, watatukanana na kulaumiana kwa uongo na kususiana. Kila kundi jipya linapoingia wahudumu wa Motoni watasema,

¹ At-Tabari 21:230.

هَذَا فَوْجٌ مُّقْتَحِمٌ مَّعَكُمْ لَا مَرْحَبًا بِهِمْ إِنَّهُمْ صَالُوا النَّارِ

“Hili ndilo kundi litakaloingia pamoja nanyi. Hapana makaribisho mema kwao. Hakika hao wanaingia Motoni.”

Yaani, kwa sababu ni watu wa Motoni.

قَالُوا بَلْ أَنْتُمْ لَا مَرْحَبًا بِكُمْ

“Waseme: Lakini nyinyi! Hamna mapokezi mazuri!”

Wale wanaoingia watasema hayo.

بَلْ أَنْتُمْ لَا مَرْحَبًا بِكُمْ أَنْتُمْ قَدْ مَتَمُّوهُ لَنَا

“Lakini nyinyi! Hamna mapokezi mazuri! Nyinyi ndio mliotusababishia haya.”

Yaani, mlituita (tulipoitikia) sasa tumefikia huu mwisho (mbaya).

فَبُئْسَ الْقَرَارُ

“...napo ni pahala paovu kabisa!” Yaani mahali na makazi mabaya kabisa.

قَالُوا رَبَّنَا مَنْ قَدَّمَ لَنَا هَذَا فَرَدَّهُ عَدَابًا ضِعْفًا فِي النَّارِ ﴿٣٨﴾

“Waseme: Mola Wetu Mlezi! Aliyetusababishia haya mzidishie adhabu mara mbili Motoni.”

Yaani mwisho huu na makazi haya ni mabaya. Inafanana na aya,

قَالَتْ أُحْرِنُهُمْ لِأَوْلِيهِمْ رَبَّنَا هَؤُلَاءِ أَضَلُّونَا فَفَاتِهِمْ عَذَابًا ضِعْفًا مِّنَ النَّارِ قَالَ لِكُلِّ

ضِعْفٌ وَلٰكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

“...wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola Wetu Mlezi! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Motoni marudufu. Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui tu.” (7:38).

Yaani, kila mmoja ataadhibiwa adhabu anayostahiki.

وَقَالُوا مَا لَنَا لَا نَرَى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِنَ الْأَشْرَارِ ﴿٥٥﴾ أَخَذْتَنَّهُمْ سِخْرِيًّا أَمْ زَاغَتْ
عَيْنُهُمْ الْآبْصَارُ ﴿٥٦﴾

Watasema: Tuna nini hata hatuwaoni wale watu ambao tukiwahisabu ndio katika waovu? Tulikosea tulipowafanyia maskhara, au macho yetu tu hayawaoni?"

Hapa Allah تعالى Anatuambia kuwa hawa waovu wakiwa Motoni watagundua kuwa miongoni mwao hawapo, watu wale waliokuwa wakiwadhanja huko duniani kuwa walipotea wakati wakijiona wao ndio wako katika ukweli na haki. Watasema, "Kwa nini hawako nasi huko Motoni?" Mujahid alisema, "Hivi ndivyo atasema Abu Jahl, "kuna nini, mbona simwoni Bilal, simwoni Ammar simwoni Suhayb, na Fulani na Fulani."¹ Huu ni mfano. Makafiri wote wako namna hiyo, wanadhania kuwa waumini wataingia Motoni. Makafiri wakiingia Motoni wataangaza macho kuwaangalia waumini bila kuwaona na ndipo watasema,

مَا لَنَا لَا نَرَى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِنَ الْأَشْرَارِ ﴿٥٥﴾ أَخَذْتَنَّهُمْ سِخْرِيًّا

"Tuna nini hata hatuwaoni wale watu ambao tukiwahisabu ndio katika waovu? Tulikosea tulipowafanyia maskhara."

Yaani, katika ulimwengu huu.

أَمْ زَاغَتْ عَنْهُمْ الْآبْصَارُ

"...au macho yetu tu hayawaoni?"

Yaani, watajaribu kufarijiana kwa fikra hizi za kutamani, watasema, huenda wako humu Jahanamu pamoja nasi, lakini hatujawaona. Halafu watagundua kuwa hao (waumini) wako katika daraja za juu Peponi. Allah تعالى Anasema:

وَنَادَى أَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابَ النَّارِ أَنْ قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ وَجَدْتُمْ مَا
وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا قَالُوا نَعَمْ فَأَذَّنَ مُؤَذِّنٌ بَيْنَهُمْ أَنْ لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٥٧﴾

¹ At-Tabari 21:32.

“Na watu wa Peponi watawanadia watu wa Motoni: Sisi tumekuta aliyotuahidi Mola Wetu Mlezi kuwa ni kweli. Je, na nyinyi pia mmekuta aliyokuahidini Mola Wenu Mlezi kuwa ni kweli? Watasema: Ndiyo! Basi mtangazaji atawatangazia: Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate waliodhulumu,...” mpaka

أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمْ وَلَا أَنْتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٤٩﴾

“Ingieni Peponi, hapana khofu kwenu, wala hamtahuzunika!”
(7:44-49).

إِنَّ ذَلِكَ لَحَقٌّ تَخَاصُمُ أَهْلِ النَّارِ ﴿٥٠﴾

“Hakika hayo bila ya shaka ndiyo makhasimiano ya watu wa Motoni.”

Yaani, “haya ndiyo tuliyokwambia, Ewe Muhammad juu ya watu wa Motoni na jinsi wanavyotukanana. Na hayo ni kweli hakuna shaka juu yake”.

قُلْ إِنَّمَا أَنَا مُنذِرٌ وَمَا مِنَّ إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٥١﴾ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
وَمَا بَيْنَهُمَا الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٥٢﴾ قُلْ هُوَ تَبَوُّؤُا عَظِيمٌ ﴿٥٣﴾ أَنْتُمْ عَنْهُ مُعْرِضُونَ ﴿٥٤﴾ مَا كَانَ
لِي مِن عِلْمٍ بِالْمَلَإِ الْأَعْلَى إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٥٥﴾ إِنَّ يُوحَىٰ إِلَىٰ إِلَآ أَنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٦﴾

65. Sema: Hakika mimi ni mwonyaji tu; na hapana mungu ila Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenza nguvu,

66. Mlezi Mola wa mbingu na ardhi na viliomo baina yake, Mwenye Nguvu, Mwingi wa Msamaha.

67. Sema: Hii ni khabari kubwa kabisa.

68. Ambayo nyinyi mnaipuuza.

69. Sikuwa na ilimu ya mambo ya viumbe wakuu watukufu walipo kuwa wakishindana.

70. Haikufunuliwa kwangu isipokuwa ya kwamba hakika mimi ni mwonyaji dhaahiri.

Ujumbe wa Mtume (Muhammad ﷺ) ni Habari Kubwa

Allah تعالى Anamwambia Mtume wake ﷺ awaambie makafiri, na washirikina wanaomwabudu Allah na vitu vingine na wanampinga mjumbe wake aseme, “Hakika mimi ni mwonyaji tu, sio kama mnavyodai.”

وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ

“...na hapana mungu ila Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Nguvu,”

Yaani, Yeye Pekee Amevitweza vitu vyote na Ana Uweza juu ya kila kitu.

رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا

“Mlezi Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake.”

Maana yake, Yeye ni Mfalme wa vyote hivyo na Ana Uweza wa kila kitu.

الْعَزِيزُ الْغَفُورُ

“...Mwenye Nguvu, Mwenye Kusamehe.”

Yaani, Yeye ni Mwingi wa Kusamehe juu ya kuwa Yeye ni Muweza wa kila kitu na Ana Nguvu zisizo na ukomo

قُلْ هُوَ نَبَأٌ عَظِيمٌ

“Sema: Hii ni khabari kubwa kabisa.”

Maana yake ni kuwa ni kitu muhimu sana ambacho Allah تعالى Ameniletea mimi nikufikishieni ninyi.

أَنْتُمْ عَنْهُ مُعْرِضُونَ

“Ambayo nyinyi mnaipuuza.”

Yaani, mnaidharau (Qur'an).

مَا كَانَ لِي مِنْ عِلْمٍ بِالْمَلَائِكَةِ الْأَعْلَىٰ إِذْ تَخْتَصِمُونَ

“Sikuwa na ilimu ya mambo ya viumbe wakuu watukufu walipo kuwa wakishindana.”

Maana yake, “kama isingelikuwa ni wahyi kutoka Kwake Allah, haya ningeliyajuaje, kuwa kulikuwa na mvutano miongoni mwa wale walio juu (malaika)?

Huu mvutano ni juu ya Adamu عليه السلام na jinsi Iblisi alivyogoma kumsujudia (Adam عليه السلام) na akaanza kubishana na Mola wake kwa kuwa Adam kapewa upendeleo kuliko yeye. Hapo Allah تعالى Anasema,

* * *

إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰئِكَةِ اِنِّىْ خَلَقْتُ بَشَرًا ﴿٧٦﴾ فَاِذَا
 مِّنْ طٰىنٍ ﴿٧٧﴾ فَاِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ
 فِيْهِ مِنْ رُّوْحِىْ فَقَعُوۡا لَهٗۥ سَاجِدِيْنَ ﴿٧٨﴾
 فَسَجَدَ الّٰمَلٰئِكَةُ كُلُّهُمۡ اَجْمَعُوْنَ ﴿٧٩﴾ اِلَّاۤ اِبْلِيسَ
 اَسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٨٠﴾ قَالَ يَتَّبِعِىْ مَا مَنَعَكَ
 اَنْ تَسْجُدَ لِمَا خَلَقْتُ بِیَدِیْۗۤ اَسْتَكْبَرْتَ اَمْ كُنْتَ مِنَ
 الْعٰلٰیۡنَ ﴿٨١﴾ قَالَ اَنَا خَيْرٌ مِّنْهُ خَلَقْتَنِیْ مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُۥ
 مِنْ طٰىنٍ ﴿٨٢﴾ قَالَ فَاخْرِجْ مِنْهَا فَاِنَّكَ رَجِيْمٌ ﴿٨٣﴾ وَاِنَّ
 عَلَیْكَ لَعْنَتِیْۤ اِلٰى یَوْمِ الدِّیْنِ ﴿٨٤﴾ قَالَ رَبِّ فَاَنْظِرْنِیْۤ اِلٰى
 یَوْمِ یُبْعَثُوْنَ ﴿٨٥﴾ قَالَ فَاِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِيْنَ ﴿٨٦﴾ اِلٰى یَوْمِ
 اَلْوَقْتِ الْمَعْلُوْمِ ﴿٨٧﴾ قَالَ فَبِعِزَّتِكَ لَاۤ اُغْوِبَنَّهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٨٨﴾
 اِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلِصِيْنَ ﴿٨٩﴾ قَالَ فَالْحَقُّ وَالْحَقُّ
 اَقُوْلُ ﴿٩٠﴾ لَاۤ اَمْلَآءَ جَهَنَّمَ مِنْكَ وَیَمِّنُ تَبَعَكَ مِنْهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٩١﴾
 قُلْ مَاۤ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَیْهِ مِنْۢ اَجْرٍ وَّمَاۤ اَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِيْنَ ﴿٩٢﴾
 اِنْ هُوَ اِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿٩٣﴾ وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَاَهُۥۭ بَعْدَ
 حِيٍۡٔ ﴿٩٤﴾

لَاۤ اُغْوِبَنَّهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٨٨﴾ اِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلِصِيْنَ ﴿٨٩﴾ قَالَ فَالْحَقُّ وَالْحَقُّ اَقُوْلُ ﴿٩٠﴾ لَاۤ اَمْلَآءَ
 جَهَنَّمَ مِنْكَ وَیَمِّنُ تَبَعَكَ مِنْهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٩١﴾

71. Mola Wako Mlezi Alipo waambia Malaika: Hakika Mimi Nitaumba mtu kutokana na udongo.

72. Na Nitakapomkamilisha na Kumpulizia roho inayotokana na mimi, basi muangukieni kwa kumtii.

73. Basi Malaika wakat'ii wote pamoja.

74. Isipokuwa Iblisi; alijivuna na akawa katika makafiri.

75. Mwenyezi Mungu Akamwambia: Ewe Iblisi! Kipi kilichokuzuia kumt'ii yule Niliyemuumba kwa Mikono Yangu? Je! Umejiona mkubwa, au umekuwa katika wakuu kweli?

76. Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, na yeye Umemuumba kwa udongo.

77. Akasema: Basi toka humo, kwani hakika wewe uko mbali na Rehema.

78. Na hakika laana Yangu itakuwa juu yako mpaka Siku ya Malipo.

79. Akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe muda mpaka siku watayofufuliwa viumbe.

80. Mwenyezi Mungu Akasema: Basi umekwishakuwa miongoni mwa waliopewa muda.

81. Mpaka wakati wa siku maalumu.

82. Akasema (Iblisi): Naapa kwa utukufu wako, bila ya shaka nitawapoteza wote.

83. Isipokuwa wale waja wako miongoni mwao waliotakaswa.

84. Akasema: Haki! Na haki Ninaisema.

85. Bila ya shaka Nitajaza Jahannamu kwa wewe na kwa hao wote wenye kukufuata miongoni mwao.

Kisa cha Adam عليه السلام na Ibilisi

Allah تعالى Amekitaja kisa hichi katika *Surat Al-Baqarah*, pia katika mwanzo wa *Suratu Al-Araf*, na *Surat ya Al-Hijr*, *Al-Isra* na *Al-Kahf* na hapa kabla hajamuumba Adam عليه السلام Allah تعالى Aliwaambia malaika kuwa Atamuumba mtu kutokana na udongo utoao sauti kutokana na matope laini meusi. Aliwaambia kuwa akisha muumba basi Malaika wamsujudie kama ishara ya adabu na heshima ikiwa ni utiifu kwa amri ya Allah تعالى. Malaika wote waliitii

amri hii isipokuwa Iblisi, ambaye alikuwa si miongoni mwao. Yeye huyo alikuwa ni miongoni mwa majini, na hali hiyo ilimdanganya na kumsaliti wakati ambapo alikuwa katika shida kubwa na anahitaji uongofu. Alikataa kumsujudia Adam na akaleta mabishano makubwa na Mola wake juu ya hilo, akidai kuwa yeye alikuwa ni bora kuliko Adam عليه السلام kwa sababu aliumbwa kwa moto na Adam kaumbwa kwa udongo wa mfinyanzi, na akasema katika madai yake kuwa moto ni bora kuliko udongo. Hilo lilikuwa ni kosa kusema hivyo na akawa ameasi Amri ya Allah تعالى na kufanya dhambi ya kukufuru. Allah تعالى Alimfedhesha na Akamtupa nje ya rehema Zake na kumfukuza aondoke asiwe mbele ya hadhira tukufu ya Allah تعالى na Akamwita kuwa ni "Iblisi" kutokana na kalima *"Ablasa min-Rahmah* (amekata tamaa kutoka Rahma ya Allah) –na hakuwa na tamaa tena ya kupata rahma ya Allah تعالى. Alimfukuza toka Peponi, akiwa amefedheheka na hatamaniki, akatupwa ardhini. Iblisi aliomba apewe muhula awepo hai hadi siku ya Kiyama. Allah تعالى ambaye hana papara ya kuwaadhibu wanaomuasi alimpa Iblisi muhula huo. Alipoona kuwa yu salama hadi Siku ya Kiyama akaasi zaidi na kukiuka mipaka.

﴿٧١﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٧٢﴾

"Akasema (Iblisi): Naapa kwa utukufu wako, bila ya shaka nitawapoteza wote, isipo kuwa wale waja wako miongoni mwao waliokhitarwa."

Hii ni kama aya,

﴿٧٣﴾ قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْت عَلَيَّ لَئِنِ أَخَّرْتَنِي إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لِأَحْتَسِبَ بِذُنُوبِي زُجْرَةً ﴿٧٤﴾ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٧٥﴾

"Akasema: Hebu nambie khabari ya huyu uliyemtukuza juu yangu. Ukiniakhirisha mpaka Siku ya Kiyama, hapana shaka nitawaangamiza dhuriya zake wasipokuwa wachache tu." (17:62)

Hao wachache ni wale waliobaguliwa katika aya nyingine ambayo ni Aya,

﴿٧٦﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٧٧﴾

"Hakika wewe huna mamlaka juu ya waja Wangu. Na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa ni wa kutegemewa." (17:65).

قَالَ فَالْحَقُّ وَالْحَقُّ أَقُولُ ﴿٣٨﴾ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنْكَ وَمِمَّن تَبِعَكَ مِنْهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾

“Akasema: Haki! Na haki Ninaisema. Bila ya shaka Nitaijaza Jahannamu kwa wewe na kwa hao wote wenye kukufuata miongoni mwao.”

Baadhi ya wafasiri akiwemo Mujahid wametafsiri kwa maana ya: Mimi ni Kweli na Ninasema ukweli.” Taarifa nyingine kutoka kwa Mujahid inasema, “Ukweli ni kutoka Kwangu Nami Nasema kweli.”¹ Wengine kama vile As-Suddi alitafsiri kama ni kiapo Alichopa Allah تعالی.² Aya hii inafanana na aya,

وَلَكِنَّ حَقَّ الْقَوْلِ مِنِّي لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾

“Lakini imekwisha kuwa kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahannamu kwa wote hawa, majini na watu.” (32:13),
na

قَالَ أَذْهَبَ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاءُكُمْ جَزَاءً مَوْفُورًا ﴿٤٠﴾

“Akasema Mwenyezi Mungu: Ondokelea mbali! Atakayekufuata katika wao, basi Jahannamu itakuwa ndiyo malipo yenu, malipo ya kutimia.” (17:63).

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ ﴿٤١﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٤٢﴾
وَلِتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ ﴿٤٣﴾

86. Sema (Ewe Mtume): Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wanaojilazimisha.

87. Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.

88. Na bila ya shaka mtajua khabari zake baada ya muda mchache.

Allah تعالی Anasema, “Ewe Muhammad waambie hawa washirikina, “sikuombeni malipo yoyote mnipe kama zawadi kutokana na mazuri ya hapa duniani kwa ajili ya kukuleteeni ujumbe huu mimi nakupeni nasaha tu.”

¹ At-Tabari 21:242.

² At-Tabari 21:242.

وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ

“...wala mimi si katika wadanganyifu.”

Yaani, mimi siongezi chochote katika ujumbe huo katika yale ambayo Allah Amenipa nikufikishieni. Chochote ninachoambiwa kufanya basi nafanya siongezi kitu wala sipunguzi chochote. Kwa kufanya hivyo natafuta Uongofu Wake Allah na radhi Zake, ili nipate Akhera (njema). Sufiyan Ath-Thawri alipokea kutoka kwa Al-Amash na Mansur kutoka kwa Abu Adhi-Dhuha kuwa Masruq alisema, “Tulikwenda kwa Abdallah bin Mas’ud akatuambia “Enyi watu! Yeyote ajuaye kitu basi akisema na asiye kijua aseme: Allahu A’lam.” Ni sehemu ya ilimu kama mtu hajui kitu na akasema, “Allah A’lam.” Yaani, “Allah تعالى Anajua zaidi”; na Allah تعالى Alimwambia Mtume wenu,

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ ﴿٤٧﴾

“Sema (Ewe Mtume): Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.”

Hayo yamo ndani ya Al-Bukhari na Muslim¹

إِنَّ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿٤٧﴾

“Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.”

Yaani, Qur’an ni ukumbusho wa viumbe wote, majini na watu, ambao watakuta hesabu zao kwa Allah تعالى Siku ya Kiyama. Hii kauli ilikuwa ni ya Ibn Abbas رضي الله عنهما. Aya hii inafanana na Aya,

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“...ili kwayo nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia.” (6:19) na

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَأَلْنَاوْهُ مَوْعِدُهُ

“...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao.”(11:17).

¹ Fat-hul - Bari 8 / 409, Muslim 2 / 2155.

وَلَتَعْلَمَنَّ نَبَأَهُ

“Na bila ya shaka mtajua khabari zake...”

Yaani, mtakujakupata uhakika kuwa yote ayasemayo ni kweli.

بَعْدَ حَيْبٍ

“...baada ya muda.”

Yaani, hivi karibuni tu. Qatadah alisema, “Baada ya kufa.” Ikrimah alisema, “Ina maana Siku ya Kiyama. Hakuna ukinzani kati ya kauli hizo mbili, kwa sababu kila anayekufa anakuwa tayari yupo chini ya hukumu ya Siku ya Kiyama.”

Hapa ndio mwisho wa Tafsiri wa *Surat-Swad- Al-hamdulillah* na shukani zote ni Zake Allah تعالی. Allah تعالی Ndiye Mjuzi zaidi.

* * *

Tafsiri ya Suratu Az-Zumar

Sura ya 39

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za *Surat Az-Zumar*

An-Nasai aliandika kuwa mama Aishah رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ alikuwa anaweza kufunga kwa mfululizo mpaka tunasema kuwa hataacha kufunga. Na anaacha kufunga hadi tunasema hafungi tena. Yeye alizowea kusoma *Surat Bani Isra'* na *Az Zumar* kila usiku."¹



¹An - Nasaai katika Al-Kubra 6:444.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الزُّمَرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١﴾ إِنَّا أَنْزَلْنَا
 إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ
 ﴿٢﴾ أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ ۗ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ
 دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى
 اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَضْحَكُ بَيْنَهُمْ فِي مَا
 هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي
 مَنْ هُوَ كَذِبٌ كَفَّارٌ ﴿٣﴾ لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا
 لَأَصْطَفَىٰ مِمَّا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللَّهُ الْوَاحِدُ
 الْقَهَّارُ ﴿٤﴾ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ يُكَوِّرُ اللَّيْلَ
 عَلَى النَّهَارِ وَيُكَوِّرُ النَّهَارَ عَلَى اللَّيْلِ ۗ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ
 وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ أَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ
 ﴿٥﴾ خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا
 وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ الْأَنْعَامِ ثَمَنِيةَ أَزْوَاجٍ ۗ يَخْلُقُكُمْ فِي بُطُونِ
 أُمَّهَاتِكُمْ خَلْقًا مِّنْ بَعْدِ خَلْقٍ فِي ظُلُمَاتٍ ثَلَاثٍ ۗ ذٰلِكُمْ
 اللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَآَنَىٰ تُصْرَفُونَ ﴿٦﴾

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ
 ﴿١﴾ إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ
 بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ
 الدِّينَ ﴿٢﴾ أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ
 ۗ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ
 أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى
 اللَّهِ زُلْفَىٰ إِنَّ اللَّهَ يَضْحَكُ بَيْنَهُمْ فِي مَا
 هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا
 يَهْدِي مَنْ هُوَ كَذِبٌ كَفَّارٌ ﴿٣﴾
 لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا
 لَأَصْطَفَىٰ مِمَّا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللَّهُ
 الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٤﴾

1. Uteremsho wa Kitabu hiki umetokana na Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

2. Hakika Sisi Tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Mwe-

nyezi Mungu ukimsafia Dini Yeye tu.

3. Hakika Dini Safi ni ya Mwenyezi Mungu tu. Na wale wanaowafanya wenginewe kuwa ni walinzi wakisema: Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu - Hakika Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yao katika wanayokhitalifiana. Hakika Mwenyezi Mungu Hamuongoi aliye muongo kafiri.

4. Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka kuwa na mtoto, basi bila ya shaka Angemchagua amtakaye katika Aliowaumba. Subhanahu, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Atakalo.

Amri ya Tauhidi na Kukatazwa Ushirikina

Allah تعالى Anatuambia, "Kuteremshwa kwa Kitabu hiki, ambacho ni Qur'an Tukufu ni kutoka Kwake, na huo ni ukweli usio na shaka yoyote." Hii ni kama Aya:

وَإِنَّهُ لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٩٢﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾ بِلسَانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ ﴿١٩٥﴾

"Na bila ya shaka huu ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameteremsha Roho muaminifu, Juu ya moyo wako, ili uwe katika waonyaji, kwa lugha ya Kiarabu iliyo wazi."
(26:192-195)

وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ ﴿٤١﴾ لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

"...na hiki bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu. Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Asifiwaye." (41:41-42)

Allah تعالى Anasema hapa,

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ

"Mteremsho wa Kitabu hiki umetokana na Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima."

Maana yake, “Mueza wa kila kitu Mwenye Nguvu zote.”

الْحَكِيمِ

“Mwenye Hikima.”

Ina maana katika yote yale Ayasemayo, Ayatendayo, Anayoyapitishia Uamuzi na yale yote Anayoamuru.

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ﴿١﴾

“Hakika Sisi Tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Mwenyezi Mungu ukimsafia Dini Yeye tu.”

Yaani, hivyo Mumuabudu Allah تعالی Peke Yake bila kumuwekea washirika au wasaidizi na waite binadamu wote wafanye hilo. Yaani wafundishe kuwa siyo sawa kuabudu kitu kingine isipokuwa Allah تعالی Peke Yake, na Yeye Hana mshirika, Hana kinacholingana Naye au kinachofanana Naye. Allah تعالی Anasema:

أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ

“Hakika Dini Safi ni ya Mwenyezi Mungu tu.”

Yaani, hatolikubali jambo lolote isipokuwa lile lililotendwa kwa kumuelekea Yeye kwa Ikhlasu Peke Yake bila washirika wala wasaidizi. Kisha Allah تعالی Anasema Akituambia kuwa washirikina wanasema:

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

“Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu.”

Yaani, kile kinachowafanya wao kuabudu kwa asiyekuwa Allah تعالی ni ile hali ya kuwa wameyafanya masanamu katika sura wanayodai ya malaika. Hivyo wakiyaabudu hayo masanamu inakuwa kama vile wanawaabudu Malaika, na Malaika hao watasimama kuwaombea kwa Allah تعالی ili wapate mahitaji yao au waondokewe na matatizo yao. Lakini Siku ya Kiyama washirikina hawakubali kuwa kitasimama wala hawakubali wazo la kufufuliwa. Qatadah, As-Suddi na Malik walisema wakinukuu kutoka kwa Zayd bin Aslam na Ibn Zayd,

إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

“...ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu.”

Yaani, “Ili hiyo miungu itukurubishe kwa Allah تعالى.”¹ Katika siku za *Jahiliya*, Waarabu wakati wa Hija walikuwa wakisema *Talbiya* yao ifuatayo: “Tuko chini ya amri yako, huna washirika isipokuwa wale ulio nao, na vyote vilivyo vyao ni mali yako.” Hali kama hiyo wameitumia washirikina wa zamani na wa sasa. Na ili kuondoa hali hiyo na kuonesha kuwa ni kauli chafu, Mitume, wamekuwa wakija na kutumwa kupinga kauli na msimamo huo wa kumshirikisha Allah kisha Mitume wamekuwa wakikataza ushirikina. Na wanawaita watu katika Tauhidi ya Allah تعالى katika ibada bila kumshirikisha au kuona kuwa ana wasaidizi. Habari za kumuekea Allah تعالى washirika na wasaidizi ni uzushi wa washirikina; Allah تعالى Hakuruhusu na hatoi ruhusa ya hilo hata kidogo. bali kwa hakika Analichukia na Analikataza.

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

“Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na tulimpeleka Shetani.” (16:36)

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

“Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.” (21:25).

Allah تعالى Anatuambia juu ya Malaika walio mbinguni na vyote vilivyo karibu Yake ni waja Wake. Hakuna awezaye kusimama na kufanya uombezi kwa mtu au kitu bila ya Idhini ya Allah تعالى; Na idhini ni kwa yule ambaye Allah تعالى yuko radhi naye. Hawako katika nafasi ya mawaziri kwa wafalme wao ambao wanakuwa waombezi wao ama kwa mapenzi yao au chuki zao hao wafalme.

فَلَا تَضُرُّوهُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ

“Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano.” (16:74)

¹ At-Tabari 21:251, 252.

Ametakasika mbali na yote hayo.

إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yao.”

Yaani, Siku ya Kiyama.

فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

“...katika wanayokhitalifiana.”

Yaani, Atawahukumu viumbe Wake na Kuwapa zawadi au Kuwaadhibu; kila mmoja kutokana na matendo yake aliyoyafanya hapa duniani. Kama Aya:

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ يَقُولُ لِلْمَلَائِكَةِ أَهْتُولَاءِ ۚ لِأَيَّكُمْ كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٤٠﴾ قَالُوا
سُبْحٰنَكَ أَنْتَ وَلِيِّنَا مِّنْ دُونِهِمْ ۗ بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ الْجِنَّ أَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنُونَ ﴿٤١﴾

“Na siku Atakayowakusanya wote, kisha Atawaambia Malaika: Je! Hawa walikuwa wakikuabuduni? Waseme: Subhanak, Umetakasika. Wewe Ndiye Kipenzi Chetu si hao. Bali wao walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao wakiwaamini hao.”
(34:40-41).

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hamuongoi aliye muongo kafiri.”

Yaani, Yeye Allah تعالی hatomwongoa mtu ambaye kwa makusudi anasema uongo juu ya Allah تعالی, na yule ambaye moyo wake unakataa kukubali aya za Allah تعالی na ushahidi juu ya Utukufu wa Allah تعالی. Kisha Allah تعالی Anasema, Yeye hana kizazi wala watoto kama washirikina wanavyodai kuwa malaika ni wana wa Allah, au kama walivyokazana kusema kwa ujeuri Mayahudi na Wakristo (Manasara) wakidai kuwa, “Uzayr na Isa ni wana wa Mungu. Allah تعالی Anasema,

لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا لَّأَصْطَفَىٰ مِمَّا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ

“Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka kuwa na mwana, basi bila ya shaka Angeliteua Amtakaye katika Aliowaumba.”

Yaani, jambo la kuwa na watoto kama wanavyodai, basi kwa Allah lisingelikuwa kama wasemavyo. Jumla hii (fungu) la maneno haya ina masharti ambayo jawabu lake ni kuwa hayo hayakufanyika wala hayakutokea, na wala fursa hiyo haipo, bali hilo ni mwiko kamwe halikutokea na halitokei. Lengo lake hapa ni kuonesha jinsi madai yao yalivyokuwa ya kipuuzi na hayana maana wala mashiko wala msingi.

Hiyo ni kama aya,

لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ هَؤُلَاءِ لَاتَّخِذْتَهُ مِنْ لَدُنَّا إِنْ كُنَّا فَعَالِينَ ﴿١٧﴾

“Kama Tungelitaka kufanya mchezo Tungejifanyia Sisi wenyewe, lau kwamba Tungelikuwa ni wafanyao mchezo.” (21:17)

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِ ﴿٨١﴾

“Sema: Ingeli kuwa Rahmani Ana mtoto, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu.” (43:81).

Aya zote hizi zimo katika mfumo wa masharti; ni rukhsa kutengeneza au kutunga jumla ya maneno au sentensi yenye msingi wa sharti, kuelekeza jambo lililowezekana katu kwa mzungumzaji wa jumla au maneno hayo.

سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللّٰهُ الْوٰحِدُ الْقَهَّارُ

“Subhanahu, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Atakalo.”

Yaani, Ametukuka na Kuta kasika Allah تعالى, mbali kabisa na fikra kuwa Anaweza kuwa na mtoto yeyote.

Yeye ni Peke Yake, asiye na mfano, Anayejitosheleza. Bwana na Mlezi wa kila kitu na kila mtu na kitu ni waja Wake wanahitajia na kumtegemea Mola wao Mtukufu Mwenye Rahma. Yuko Pekee na Ana uhuru kamili bila Kutegemea chochote wala lolote.

Yeye Ameweka vitu vyote chini Yake na vinasalimu amri Kwake kwa unyenyekevu wote. Yuko juu na mbali ya yote yale makafiri na washirikina wayasemayo.

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۗ يُكَوِّرُ اللَّيْلَ عَلَى النَّهَارِ وَيُكَوِّرُ النَّهَارَ عَلَى اللَّيْلِ ۗ
 وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ لِّأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ أَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٦﴾ خَلَقَكُمْ
 مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَأُنزِلَ لَكُمْ مِنْ الْأَنْعَامِ ثَمَنِيَّةَ أَزْوَاجٍ ۗ تَخَلَّقَكُمْ فِي
 بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ خَلْقًا مِّنْ بَعْدِ خَلْقٍ فِي ظُلُمَاتٍ ثَلَاثٍ ۗ ذَلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۗ لَا
 إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَآَنِي تُصِرُّونَ ﴿٦﴾

5. Ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Hufunika usiku juu ya mchana, na Hufunika mchana juu ya usiku. Na Amefanya jua na mwezi vitumike. Kila kimojapo kinakwenda kwa kipindi kilichowekewa. Jueni mtanabahi! Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwingi wa Kusamehe!

6. Amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Kisha Akamfanya mwenziwe katika nafsi ile ile. Na Akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane. Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu. Huyu Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Ufalme ni Wake. Hapana mola isipokuwa Yeye. Basi nyinyi mnageuzwa wapi?

Ushahidi Juu ya Nguvu na Uwezo wa Allah تعالى na Kuwa Yeye Yuko Pekee

Allah تعالى Anatuambia kuwa Yeye Muumba wa vyote vilivyoko mbinguni na ardhini na hata vile vilivyo kati ya sehemu hizo mbili. Yeye Ndiye Bwana Mfalme na Mwendeshaji wa vitu vyote hivyo Akibadili usiku na mchana.

يُكَوِّرُ اللَّيْلَ عَلَى النَّهَارِ وَيُكَوِّرُ النَّهَارَ عَلَى اللَّيْلِ ۗ

“Hufunika usiku juu ya mchana, na Hufunika mchana juu ya usiku.”

Yaani, Amevitweza kwa Kuvifanya vibadilishane bila kusita kila kimoja kikimtafuta na kumfuata mwenziwe kwa kasi.

Kama Asemavyo katika aya,

يُغْشَى اللَّيْلَ اللَّيْلَ يَطْلُبُهُ حَيْثُ

“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi.” (7:54).

Hii ni maana iliyonukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما pia kutoka kwa Mujahid, Qatadah, As-Suddi na wengine.¹

وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلَّ يَوْمٍ لِلَّذِينَ يُحِبُّونَ لِأَجْلِ مُوسَىٰ

“Na Amefanya jua na mwezi vitumike. Kila kimojapo kinakwenda kwa kipindi kilichowekewa.”

Yaani, kwa muda Anaoujua Allah تعالى vitafikia ukomo wake Siku ya Kiyama.

أَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ

“Jueni mtanabahi! Yeye Ndiye Mwenye Nguvu.”

Yaani, Nguvu Zake, Uweza Wake Mkubwa na Kiburi Chake, Yeye ni Mwenye Kuwasamehe daima waja wake wanaofanya maasi lakini baadaye wakarejea Kwake na kutubu.

خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Amekuumbeni kutokana na nafsi moja.”

Maana yake ni kuwa Amekuumbeni nyinyi pamoja na kuwa mumo katika mataifa mbali mbali, aina mbali mbali, lugha tofauti na rangi zenu nyingi, kutokana nafsi moja tu na nafsi hiyo ni Adam عليه السلام,

ثُمَّ جَعَلْنَا مِنْهَا زَوْجَهَا

“Kisha Akamfanya mwenziwe...”

Ambaye alikuwa Hawwa. Hii ni kama Aya ifuatayo,

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً

¹ Al-Qurtubi 15:235.

"Enyi watu! Mcheni Mola Wenu Mlezi Aliyekuumbeni kutokana na nafsi moja, na Akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na Akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi." (4:1)

وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ الْأَنْعَامِ ثَمَنِيَّةً أَزْوَاجًا

"Na Akakuleteeni wanyama wa mifugo jozi nane."

Yaani, Amekuteremshieni mifugo katika jozi nane.¹ Wanyama hawa ni wale ambao wametajwa katika Surat Al-An'aam, aina nane, jozi ya kondoo, jozi ya mbuzi, jozi ya ngamia na jozi ya ng'ombe.

مَخْلُوقًا فِي بَطُونٍ أُمَّهَاتِكُمْ

"Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu."

Yaani, anakutengenezeni katika matumbo ya mama zenu.

خَلَقًا مِنْ بَعْدِ خَلْقِ

"...umbo baada ya umbo."

Yaani kila mmoja wenu asili yake huko tumboni ni 'Nutfah' tone la manii kisha akawa 'Alaqah' pande la damu na baadaye akawa *Mudghah*.² Kisha anaumbwa na kuwa nyama na mifupa, akiwa na mishipa ya fahamu na mishipa ya damu na kisha Roho ikapuliziwa ndani yake, na kisha anakuwa kiumbe kingine.

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ

"Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji." (23:14)

فِي ظُلُمَاتٍ ثَلَاثٍ

"...katika viza vitatu."

¹ Ili kuelewa stilahi hizi kwa uzuri zaidi angalia tafsiri ya (23:12-14).

² Ingawa neno An'am kwa kawaida hutafsiriwa kuwa ni ng'ombe, maana yake ni pana zaidi na hujumuisha pia aina zote za mifugo, kama vile kondoo, mbuzi na ngamia. Angalia juzu ya tatu, *Tafsir ya Surat Al-An'am* (6:142)

Yaani, ndani ya kiza cha mji wa mimba na kiza cha kondo la uzazi ambalo humgubika mtoto na kumhifadhi na kisha kiza cha tumbo. Hii ilikuwa ni kauli ya Ibn Abbas رضي الله عنهما na ya Mujahid, Ikrimah, Abu Malik, Adh-Dhahak, As-Suddi na Ibn Zayd.¹

ذَٰلِكُمْ أَلَّهُ رَبُّكُمْ

“Huyu Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi.”

Maana yake, Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi na kila kitu ndani yake na katikati ya hivyo na Amekuumbeni nyinyi na mababu zenu, ni Bwana na Mola. Na Utawala wote na Uendeshaji wa mambo hurejea Kwake.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Hapana mola isipokuwa Yeye.”

Yaani, hakuna mwingine anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Yeye Peke Yake asiyekuwa na mshirika wala msaidizi.

فَأَن تَصْرُفُونَ

“Basi nyinyi mnageuzwa wapi?”

Yaani vipi waweza kuabudu kingine badala au zaidi Yake Allah? Akili zenu zinapelekwa wapi?

* * *

¹ At-Tabari 21:258, 259; Ad-Dur Al Manthur 7:236.

١٦ ۞ وَإِن تَكَفَّرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ ۗ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۗ وَإِن تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُم مَّرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٧﴾ * وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا حَوَّلَهُ نِعْمَةً مِّنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ يَدْعُوًا إِلَيْهِ مِنْ قَبْلُ وَجَعَلَ لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ قُلْ تَمَتَّعْ بِكُفْرِكَ قَلِيلًا ۗ إِنَّكَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ ﴿٨﴾ أَمَّنْ هُوَ قَبِيٓئٌ ءَآنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذَرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٩﴾ قُلْ يٰٓعِبَادِ الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا رَبَّكُمُ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ۗ وَأَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةٌ ۗ إِنَّمَا يُوَفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿١٠﴾ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ﴿١١﴾ وَأُمِرْتُ لِأَنْ أَكُونَ أَوَّلَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٢﴾ قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٣﴾ قُلِ اللَّهُ أَعْبُدْهُ مُخْلِصًا لَهُ دِينِي ﴿١٤﴾ فَأَعْبُدُوا مَا شِئْتُمْ مِنْ دُونِهِ ۗ قُلْ إِنَّ أَحْسَنَ الَّذِينَ خَلَقْتُ أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ أَلَّا ذَلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿١٥﴾ هُمْ مِّنْ قَوْمِهِمْ طَلَّلَ مِنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظِلٌّ ۗ ذَلِكَ يُخَوِّفُ اللَّهُ بِهِ عِبَادَهُ ۗ

﴿١٦﴾ فَاتَّقُونِ ﴿١٦﴾

١٦ ۞ وَإِن تَكَفَّرُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ ۗ وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۗ وَإِن تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُم مَّرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٧﴾ * وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ ثُمَّ إِذَا حَوَّلَهُ نِعْمَةً مِّنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ يَدْعُوًا إِلَيْهِ مِنْ قَبْلُ وَجَعَلَ لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ قُلْ تَمَتَّعْ بِكُفْرِكَ قَلِيلًا ۗ إِنَّكَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ ﴿٨﴾

7. Mkikufuru basi Mwenyezi Mungu si mwenye haja nanyi, lakini hafurahii kufuru kwa waja wake. Na mkishukuru hayo yanamridhisha kwenu. Wala mbebaji habebi mzigo wa mwi-ngine. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi. Hapo Atakuambieni mliyo-kuwa mkiyafanya. Hakika Yeye ni Mwenye Kuyajua vyema yaliyomo vifuani.

8. Na taabu inapomfikia mtu humuomba Mola wake Mlezi hali ya kuelekea kwake. Kisha Akimpa neema kutoka Kwake, husahau yale aliyokuwa akimuitia zamani, na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu kutokana na Njia Yake. Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.

Allah تعالیٰ Anachukia Ukafiri na Anaridhia Shukrani

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa Yuko huru na Hana Haja ya chochote kutoka kwa viumbe wake. Hii ni kama kauli yake *عليه السلام* Mussa.

إِن تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٤﴾

“Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Mwenye Kujitoshia, na Kustahiki Kusifiwa.” (14:8)

Katika Sahihi Muslim imekuja katika hadithi Qudsi; anasema Allah تعالیٰ

«يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَخْرَكُم وَإِنْسَكُمْ وَجَنَّكُمْ كَانُوا عَلَىٰ أَفْجَرِ قَلْبِ رَجُلٍ مِّنْكُمْ، مَا نَقَصَ ذَلِكَ مِنْ مُلْكِي شَيْئًا»

“Enyi waja Wangu, kama mngejumuika kwa pamoja nyinyi tangu wa mwanzoni mwenu na wa mwishoni mwenu, binadamu na majini, mngekuwa waovu mno kama mtu mwovu zaidi kati yenu, basi hilo lisingepunguza chochote katika miliki yangu.”

وَلَا يَرْضَىٰ لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ^ط

“...lakini Hafurahii kufuru kwa waja Wake.”

Yaani, Hapendi hilo wala Haliungi mkono au Haliruhusu lifanyike,

وَإِن تَشْكُرُوا يَرْضَهُ لَكُمْ^٤

“Na mkishukuru Yeye Hufurahika nanyi.”

¹ Muslim 4:1994.

Kwa Kuzidisha neema na mapenzi Yake kwenu.

وَلَا تَرْرُ وَأَزْرَةَ وَزَرَ أُخْرَىٰ

“Wala mbebaji habebi mzigo wa mwingine.”

Yaani, hakuna mtu atakayebeba mzigo wa mtu mwingine katika lawama, majukumu na matendo yote; kila mmoja ataulizwa mambo aliyoyafanya na kuyatenda mwenyewe.

ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

“Kisha marejeo yenu ni kwa Mola wenu Mlezi. Hapo Atakuambieni mliyokuwa mkiyafanya. Hakika Yeye ni Mwenye Kuyajua vyema yaliyomo vifua ni.”

Maana yake, hakuna kilichofichikana kwa Mola wenu vyote (vikubwa kwa vidogo) viko wazi Kwake.

Ukarofi wa Binadamu na Kumkumbuka Allah تعالى Wakati wa Shida, na Kumshirikisha Mola Wake Mlezi Baada ya Faraja

وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهُ مُنِيبًا إِلَيْهِ

“Na taabu inapomfikia mtu humuomba Mola wake Mlezi naye ameelekea Kwake.”

Maana yake, wakati wa shida, binadamu anaomba dua na ibada zake huzielekeza kwa Mola wake akitafuta msaada na nusura bila kumshirikisha Allah تعالى. Kauli hii ni kama Aya,

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَهُهُ فَأَمَّا جَنْبُكُمْ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ ۗ وَكَانَ

الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾

“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na anapokuo kweni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha.”
(17:67). Allah تعالى Anasema:

ثُمَّ إِذَا حَوَّلَهُ نِعْمَةً مِّنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ يَدْعُوًّا إِلَيْهِ مِن قَبْلُ

“Kisha Akimpa neema kutoka Kwake, husahau yale aliyokuwa akimuitia zamani.”

Maana yake, wakati wa raha, pasipokuwa na shida huachilia mbali hali hiyo ya kuomba Dua na kunyenyekea kwa Allah تعالى. Hiyo inafanana na ayah,

وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبِهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَى ضُرِّ مَسَّهُ

“Na mtu akiguswa na shida hutuomba hali ya kulala ubavu au kukaa au kusimama, au kasimama. Lakini Tukimuondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba tumuondoshee shida iliyompata.” (10:12).

وَجَعَلَ لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّيُضِلَّ عَن سَبِيلِهِ

“...na akamfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili apoteze watu njia yake.”

Yaani, wakati wa faraja, anawashirikisha na Allah تعالى katika ibada na kumuekea Yeye washindani.

قُلْ تَمَتَّعْ بِكُفْرِكَ قَلِيلًا إِنَّكَ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ

“Sema: Starehe na ukafiri wako kwa muda mchache. Kwani hakika wewe utakuwa miongoni mwa watu wa Motoni.”

Yaani, Waambie hao wenye kuabudu asiyekuwa Allah تعالى au kuabudu vitu vingine pamoja na kumuabudu Allah تعالى kuwa “furahini hiyo hali ya ukafiri kwenu kwa muda (mfupi tu).” Hili ni onyo kali ambalo ni kama Aya,

قُلْ تَمَتَّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ

“Sema: Stareheni! Kwani marejeo yenu ni Motoni!” (14:30).

ثُمَّ تُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

“Tunawastarehesha kwa muda mchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24)

أَمَّنْ هُوَ قَنِيتُ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا مَّحَذَّرُ الْآخِرَةِ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٩﴾

9. Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake Mlezi. Sema: Ati watakuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? Hakika wanaokumbuka ni watu wenye akili.

Mchamungu Halingani na Muasi (Mtenda Dhambi)

Allah تعالی Anasema, “Je yule ambaye yuko hivi yuko sawa na yule anayemshirikisha Mola wake katika ibada, ama kwa kuabudu vingine visivyokuwa Allah تعالی au kwa kumshirikisha Mola wake katika ibada na vile visivyopaswa kuabudiwa? Watu hawa wawili hawako sawa mbele ya Mola wao; kama Anavyosema: Aya

لَيْسُوا سَوَاءً ۗ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١١٣﴾

“Wote hao hawawi sawa. Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu waliosimama baraabara, wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu.” (3:113).

Kisha Allah تعالی Anasema hapa:

أَمَّنْ هُوَ قَنِيتُ ءَأَنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا

“Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama...”

Yaani, Yule aliye mnyenyekevu na anamuogopa Allah تعالی wakati anaposujudu na kusimama katika Sala. Ilipokelewa kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Mchamungu ni yule anayefuata amri za Allah تعالی na Mtume Wake.¹ Ibn Abbas Al-Hasan, As Suddi na Ibn Zayd walisema ‘Ana’a Al-Layl’ ni usiku wa manane.²

مَّحَذَّرُ الْآخِرَةِ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِ ۗ

“...akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola Wake Mlezi...”

¹ Al-Qurtubi 15:239.

² Al-Qurtubi 15:239.

Yaani, katika ibada na Sala zake anakuwa ana woga na matumaini. Vitu hivi viwili ni muhimu katika ibada na woga unapaswa uwe katika hali ya juu kwa mtu anapokuwa bado yu hai duniani. Allah تعالى Anasema.

تَحَذَّرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُوا رَحْمَةَ رَبِّهِمْ¹

“...akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola Wake Mlezi...”

Wakati wa kufikwa na umauti basi matumaini yawe yako juu, kama alivyonukuu Imam Abd bin Humayd katika Musnadi yake kutoka kwa Anas رضي الله عنه ambaye alisema, “Mtume ﷺ alifika kwa mtu ambaye alikuwa yupo katika hali ya kutokwa na roho na akamuambia,

«كَيْفَ تَجِدُكَ؟»

“Je unajisikiaje?”

Akajibu kuwa ana hofu na matumaini. Mtume ﷺ akasema,

«لَا يَجْتَمِعَانِ فِي قَلْبِ عَبْدٍ فِي مِثْلِ هَذَا الْمَوْطِنِ إِلَّا أَعْطَاهُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ الَّذِي يَرْجُو، وَأَمَّنَهُ الَّذِي يَخَافُهُ»

“Vitu hivi viwili havitangamani ndani ya moyo wa mja katika wakati kama huu ila Allah Subhanahu, Humpa anachokitarajia na Akamhifadhi na anachokiogopa.”¹

Kauli hii ilipokelewa na Tirmidhi na An-Nasai ndani ya kitabu cha *Al-Yawm wal-layl*, na Ibn Majah, Sayyar Ibn Hatima kutoka kwa Ja’far bin Sulayman. At Tirmidhi amesema kuwa hii ni hadithi “*Gharib*”.² Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Tamim Ad-Dari رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَرَأَ بِمِائَةِ آيَةٍ فِي لَيْلَةٍ كُتِبَ لَهُ قُرْآنٌ لَيْلَةٍ»

“Atakayesoma aya mia moja katika usiku mmoja ataandikiwa kusimama usiku.”

Hii riwaya pia iko kwa An-Nasai ndani ya *Al-Yawm Wal-Laylah*.³

¹ Abd bin Humayd: 404.

² *Tuhfat ul Al-Ahwadhi* 7:57, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:262, Ibn Majah 2:1423.

³ Ahmad 4:103.

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ۗ

“Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasiojua?”

Yaani, je analingana na anayemshirikisha Mola na vingine na kumuekea Allah تعالى washindani ili awapotoshe watu mbali na njia Yake Allah تعالى (Tawhid).

إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ

“Hakika wanaokumbuka ni watu wenye akili.”

Yaani, mwerevu tu ndiye anajua (kuwa hawa hawako sawa) na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

قُلْ يَاعِبَادِ الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا رَبَّكُمْ ۚ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ۗ وَأَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةٌ ۗ إِنَّمَا يُوَفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿١٠﴾ قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ﴿١١﴾ وَأُمِرْتُ لِأَنْ أَكُونَ أَوَّلَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٢﴾

10. Sema: Enyi waja Wangu mlioamini! Mcheni Mola Wenu Mlezi. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu. Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.

11. Sema: Hakika mimi nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini Yeye tu.

12. Na nimeamrisha niwe wa mwanzo wa waliosilimu.

Amri ya Kumcha Allah تعالى Kuhama na Kumuabudu Allah تعالى kwa Ikhiasi

Allah تعالى Anawaamuru waja wake wema kubakia katika njia nyoofu na kuendelea kumuogopa Mola wao na kumcha yeye.

قُلْ يَاعِبَادِ الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا رَبَّكُمْ ۚ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ۗ

“Sema: Enyi waja Wangu mlioamini! Mcheni Mola Wenu Mlezi. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema.”

Yaani mwenye kutenda mema hapa duniani atapata malipo mema Akhera.

وَأَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةٌ

“Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu.”

Mujahid alisema, “Basi hamieni kwingine duniani na mjitahidi kutenda mema na muepuke masanamu.”¹

إِنَّمَا يُؤْتِي الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.”

Al-Awza alisema, “Malipo hayatapimwa kwa uzito au kwa urefu na mapana; Hakika watapewa malipo makubwa ajabu.”

As-Suddi alisema:

إِنَّمَا يُؤْتِي الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.”

Yaani, “Ni Peponi.”

قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ ﴿١٠١﴾

“Sema: Hakika mimi nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu.”

Yaani, “Nimepewa amri ya kumuabudu Allah تعالیٰ Peke Yake kwa ukweli wote bila kumshirikisha na kumuekea wasaidizi.

وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٠٢﴾

“Na nimeamrisha niwe wa mwanzo wa waliosilimu.”

¹ At-Tabari 21:269.

² At-Tabari 21:270.

قُلْ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٣٩﴾ قُلِ اللَّهُ أَعْبُدُ مُخْلِصًا لَهُ دِينِي ﴿٤٠﴾
 فَاعْبُدُوا مَا شِئْتُمْ مِنْ دُونِهِ ۗ قُلْ إِنَّ الْخَاسِرِينَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
 ۗ أَلَا ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿٤١﴾ لَهُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ ظُلَلٌ مِنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظُلَلٌ
 ۗ ذَٰلِكَ يُخَوِّفُ اللَّهُ بِهِ عِبَادَهُ ۗ يَنْعَبِدُونَ ﴿٤٢﴾

13. Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya Siku Kubwa nikimuasi Mola Wangu Mlezi.

14. Sema: Mwenyezi Mungu tu namuabudu kwa kumsafishia Yeye tu Dini Yangu.

15. Basi nyinyi abuduni mpendacho badala yake Yeye. Sema: Hakika waliopata hasara ni wale waliozitia hasara nafsi zao na watu wao Siku ya Kiyama. Angalieni kuwa hiyo ndiyo hasara iliyo wazi.

16. Yatawekwa juu yao mawingu ya moto, na chini yao mawingu. Kwa hayo Mwenyezi Mungu Anawakhofisha waja Wake. Enyi waja Wangu! Nicheni Mimi!.

Kuhofisha Adhabu ya Allah تعالى

Allah تعالى Anasema, "Sema ewe Muhammad, hali ya kuwa wewe ni Mtume ﷺ,

إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ

"Hakika mimi ninaogopa adhabu ya Siku Kubwa nikimuasi Mola Wangu Mlezi."

Yaani, Siku ya Kiyama. Hii ni sentensi yenye masharti; na hayo yaliyotajwa hapa ikiwa Mtume ﷺ anaambiwa hivi, basi mtu mwengine anatakiwa achukue tahadhari zaidi.

قُلِ اللَّهُ أَعْبُدُ مُخْلِصًا لَهُ دِينِي ﴿٤٠﴾ فَاعْبُدُوا مَا شِئْتُمْ مِنْ دُونِهِ ۗ

"Sema: Mwenyezi Mungu tu namuabudu kwa kumsafishia Yeye tu Dini yangu. Basi nyinyi abuduni mpendacho badala yake Yeye."

Hili pia ni onyo na kujitenga na yule anayemuabudu asiyekuwa Allah.

قُلْ إِنَّ الْخَاسِرِينَ

“Hakika waliokhasirika...”

Yaani ni wenye hasara kabisa kabisa kuliko watu wote.

الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَأَهْلِيَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“...ni wale waliojikasiri nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama.”

Mana yake, watatenganishwa na hawatakutana tena abadani kama familia zao zimekwenda Peponi, na wao wakaenda Motoni, au wote watakuwa motoni, lakini huko hakuna tena kuzungumza na kufurahi.

أَلَا ذَلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ

“Tambueni kuwa hiyo ndiyo khasara iliyo dhaahiri.”

Yaani, hii ni wazi kabisa kuwa ni hasara kubwa. Kisha akaeleza hali zao motoni.

هُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ ظَلَلٌ مِنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظُلَلٌ

“Yatawekwa juu yao mat’abaka ya moto, na chini yao mat’abaka.”

Hii ni kama Aya:

هُمْ مِنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ۚ وَكَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾

“Jahannamu itakuwa kitanda chao na juu yao nguo za moto za kujifunika. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa madhaalimu.” (7:41)

يَوْمَ يَغْشَاهُمْ الْعَذَابُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ وَيَقُولُ ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥٥﴾

“Siku itapowafunika adhabu hiyo kutoka juu yao na chini ya miguu yao, na atasema: Onjeni hayo mliyokuwa mkiyatenda!” (29:55)

ذَلِكَ تَخَوُّفٌ بِاللَّهِ بِهِ عِبَادُهُ

“Kwa hayo Mwenyezi Mungu Anawakhofisha waja Wake.”

Yaani, Allah تعالى Anatueleza juu ya jambo hili lisilo na shaka kutokea, ili kuwaogopesha na kuwatia hofu waja Wake, ili waepuke haramu na madhambi.

يَعْبَادِ فَاتَّقُونِ

“Enyi waja Wangu! Nicheni Mimi!”

Yaani, “Ogopeni ukali, Hasira na Adhabu Zangu.”

* * *

وَالَّذِينَ اجْتَنَبُوا الطُّغُوتَ أَنْ يَعْبُدُوهَا وَأَنَابُوا إِلَى اللَّهِ لَهُمُ
 الْبِشْرَىٰ ۚ فَبَشِّرْ عِبَادِ ﴿١٧﴾ الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ
 فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ ۚ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّهُ ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمْ
 أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٨﴾ أَفَمَنْ حَقَّ عَلَيْهِ كَلِمَةُ الْعَذَابِ أَفَأَنْتَ
 تُنقِذُ مَنْ فِي النَّارِ ﴿١٩﴾ لَكِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ هُمْ غُرَفٌ
 مِّنْ فَوْقِهَا غُرَفٌ مَّيْبُتَةٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ وَعَدَّ اللَّهُ
 لَا يُخْلِفُ اللَّهُ الْمِعَادَ ﴿٢٠﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ
 السَّمَاءِ مَاءً فَسَلَكَهُ يَنْبِيعٌ فِي الْأَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهِ
 زَرْعًا مُّخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَاهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَجْعَلُهُ
 حُطَبًا ۖ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرًا لِأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿٢١﴾ أَفَمَنْ
 شَرَحَ اللَّهُ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّنْ رَبِّهِ ۖ فَوَيْلٌ
 لِلْفَاسِقِينَ قُلُوبُهُمْ مِّنْ ذِكْرِ اللَّهِ ۖ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٢﴾
 اللَّهُ نَزَّلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانِيَ تَقْشَعُرُ مِنْهُ
 جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ
 ذِكْرِ اللَّهِ ۖ ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ ۖ وَمَن
 يُضَلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن هَادٍ ﴿٢٣﴾ أَفَمَنْ يَتَّبِعِ بَوَاجِهِ
 سُوءَ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۖ وَقِيلَ لِلظَّالِمِينَ ذُوقُوا مَا كُنتُمْ
 تَكْسِبُونَ ﴿٢٤﴾ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَآتَتْهُمْ الْعَذَابُ مِنْ
 حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٥﴾ فَأَذَاقَهُمُ اللَّهُ الْخِزْيَ فِي الْحَيَاةِ
 الدُّنْيَا ۖ وَالْعَذَابُ الْآخِرَةُ أَكْبَرُ ۖ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٢٦﴾

وَالَّذِينَ اجْتَنَبُوا الطُّغُوتَ أَنْ
 يَعْبُدُوهَا وَأَنَابُوا إِلَى اللَّهِ لَهُمُ
 الْبِشْرَىٰ ۚ فَبَشِّرْ عِبَادِ ﴿١٧﴾ الَّذِينَ
 يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ ۚ
 أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّهُ ۖ وَأُولَٰئِكَ
 هُمْ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٨﴾

17. Na wale wanaojiepusha na ibada ya masanamu, na wakarejea kwa Mwenyezi Mungu, watapata bishara njema. Basi wabashirie waja wangu.

18. Ambao husikiliza maneno, wakafuata yaliyo bora yao. Hao ndio Aliwaongoa Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili.

Habari Njema kwa Watu Wema

Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam akipokea kutoka kwa baba yake, alisema:

وَالَّذِينَ اجْتَنَبُوا الطُّغُوتَ أَنْ يَعْبُدُوهَا

“Na wale wanaojiepusha na ibada potovu.”

Aya hii iliteremshwa kuwahusu Zayd bin Amr bin Nafayl, Abu Dhar na Salman Al-Farisi رضي الله عنهم.¹ Ukweli ni kuwa inawahusu wao hao na wengine wanaoepuka kuabudu masanamu, na wakaelekeza ibada zao kwa *Ar-Rahman*. Hawa ndio wanapewa habari njema hapa duniani na Akhera. Kisha Allah تعالى Anasema.

فَبَشِّرْ عِبَادِ ﴿١٧﴾ الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ

“Basi wabashirie waja wangu. Ambao husikiliza maneno, wakafuata lilio bora yao.”

Yaani, wale wanaoelewa kauli hiyo na kisha wakafuatisha vitendo vyao kulingana na kauli hiyo wakiwa wanaitii. Hii ni kama Kauli ya Allah تعالى, akimuambia Musa عليه السلام, pale alipompa Tawrati Aya,

فَخَذَهَا بِقُوَّةٍ وَأَمَرَ قَوْمَكِ يَا خَدُّوْا بِأَحْسَنِهَا

“Basi yashike kwa nguvu na uwaamrishe watu wako wayashike kwa ubora wake.” (7:145)

أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ

“Hao ndio aliowaongoa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hao wanaoelezwa hapa wakiwa na hali hiyo ni wale ambao Allah تعالى Amewaongoa hapa duniani na huko Akhera.

وَأُولَئِكَ هُمُ أَوْلُوا الْأَلْبَابِ

“...na hao ndio wenye akili.”

Yaani, ni wale watu ambao wana uwezo wa kuweza kufikiri na kisha kutambua na kuleta uamuzi sahihi na hao ni wale wenye tabia njema.

أَفَمَنْ حَقَّ عَلَيْهِ كَلِمَةُ الْعَذَابِ أَفَأَنْتَ تُنقِذُ مَنْ فِي النَّارِ ﴿١٨﴾ لَكِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ هُمْ

عُرِفُوا مِنْ فَوْقِهَا عُرْفٌ مَبِيئَةٌ تَجْرِي مِنَ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَعَدَّ اللَّهُ لَا تُخْلِفُ اللَّهُ الْمِيعَادَ ﴿١٩﴾

¹ At-Tabari 21:274. Isnadi yake ni dhaifu.

19. Je! Yule mwenye kustahiki hukumu ya adhabu, je, wewe unaweza kumuokoa aliyomo katika Moto?

20. Lakini waliomcha Mola wao Mlezi watapata ghorofa zilizojengwa juu ya ghorofa; chini yake hupita mito. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Havunji ahadi Yake.

Allah تعالى Anasema, "Ikiwa Amethibitisha kwa mtu kuwa yu miongoni mwa walioangamia, je waweza kumuokoa kutoka katika njia potovu na ya kuangamia? Hiyo ina maana hakuna mtu ambaye anaweza kumuongoa isipokuwa Allah تعالى; kwa sababu yule anayeachwa na Allah تعالى apotee hawezi kuongozwa wala haongoki na yule ambaye Anayemuongoa hawezi kupotoka wala kwenda pogo. Kisha Allah تعالى Anatuambia Akisema kuwa waja Wake wema watapata vyumba vilivyopambwa huko Peponi. Nayo ni maghorofa na Kasri ndefu.

مِنْ فَوْقَهَا عُرْفٌ مَبْنِيَةٌ

"...zilizojengwa juu ya ghorofa..."

"Ghorofa juu ya ghorofa, zimejengwa imara na kupambwa vizuri sana. Abdallah bin Al-Imam Ahmad anasema kuwa Ali رضي الله عنه, alisema, "Alisema Mtume ﷺ,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ لَعُرْفًا يُرَى بُطُونُهَا مِنْ ظُهُورِهَا، وَظُهُورُهَا مِنْ بُطُونِهَا»

"Hakika Peponi kuna vyumba ambavyo vilivyoko ndani yake huonekana kwa nje yake na vile vilivyoko nje yake vinaonekana kwa ndani yake."

Akauliza bedui, "Hivyo vyumba ni kwa ajili ya nani ya Rasulullah?" Mtume ﷺ akajibu,

«لِمَنْ أَطَابَ الْكَلَامَ، وَأَطْعَمَ الطَّعَامَ، وَصَلَّى بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ نِيَامَ»

"Ni kwa ajili ya wale ambao husema kwa wema, wanalisha maskini, na wanasimama usiku kusali wakati watu wamelala."¹

¹ Ahmad 6:1:155.

Maneno haya pia yalinukuliwa na At-Tirmidhi ambaye aliipa daraja hadithi hii ya "Hasan Gharib."¹ Imam Ahmad katika riwaya ya Sahl bin Sa'd رضي الله عنه ameeleza kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ أَهْلَ الْجَنَّةِ لَيَتَرَاءُونَ فِي الْعُرْفَةِ فِي الْجَنَّةِ، كَمَا تَرَاءُونَ الْكَوْكَبَ فِي أَفْقِ السَّمَاءِ»

"Hakika watu wa Peponi wataangaliana wenyewe kwa wenyewe wakiwa katika sehemu zilizopandishwa juu Peponi kama vile mnavyoziangalia nyota angani."

Akasema, "Nilimuambia maneno haya An-Numan bin Dyyash naye akasema, "Nilimsikia Said Al-Khudri رضي الله عنه akisimulia hivi:

«كَمَا تَرَاءُونَ الْكَوْكَبَ الَّذِي فِي الْأَفْقِ الشَّرْقِيِّ أَوْ الْغَرْبِيِّ»

"Kama mnavyoziona nyota katika anga za mashariki na pia katika anga za magharibi."²

Habari hizi pia zimo katika Sahihi Mbili.³

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema, "Amesema Mtume ﷺ,

«إِنَّ أَهْلَ الْجَنَّةِ لَيَتَرَاءُونَ فِي الْجَنَّةِ أَهْلَ الْعُرْفِ، كَمَا تَرَاءُونَ الْكَوْكَبَ الدَّرِّيَّ الْغَارِبَ فِي الْأَفْقِ الطَّلَعِ، فِي تَفَاضُلِ أَهْلِ الدَّرَجَاتِ»

"Hakika watu wa Peponi wataangaliana wenyewe kwa wenyewe katika sehemu zilizoinuliwa juu za Peponi kama vile ambavyo mnaziangalia nyota zing'aazo huko juu angani. Na hivyo ndivyo zitakuwa tofauti za madaraja yao hao watu wa huko Peponi."

Wakasema masahaba, "Ya Rasulullah! je hizo ni sehemu za Mitume?" Akasema,

¹ Tuhfatul Ahwadhi 7:231.

² Ahmad 5:340.

³ Fat'hul - Bari: 11/424, Muslim 4:2177.

«بَلَىٰ، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، وَأَقْوَامٌ آمَنُوا بِاللَّهِ وَصَدَّقُوا الرَّسُولَ»

“La, Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, ni makazi ya watu wa kawaida ambao walimuamini Allah na wakawasadikisha Mitume Wake.”

Na At-Tirmidhi naye ameyanukuu hayo na akasema hadithi hiyo ni “*Hasan Sahihi.*”

تَجْرِي مِنَ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ^ط

“...chini yake hupita mito.”

Yaani, mito inabubujika maji na kuyapeleka kule ambako watu wanataka yaelekee.

وَعَدَّ اللَّهُ^ط

“Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, “yote yale tuliyoyataja hapa ni yale ambayo Allah تعالى Ameahidi kuwapatia waja Wake wema.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَلَكَهُ يَنْبِيعَ فِي الْأَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا
مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ثُمَّ يَهيجُ فَتَرْتَهُ مُضْفَرًا ثُمَّ يَجْعَلُهُ حُطْبًا^ع إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرًا لِأُولِي
الْأَلْبَابِ ﴿٦٠﴾ أَفَمَنْ شَرَحَ اللَّهُ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّن رَّبِّهِ^ع فَوَيْلٌ لِلْقَاسِيَةِ
قُلُوبِهِمْ مِّنْ ذِكْرِ اللَّهِ^ع أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٦١﴾

21. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu Ameteremsha maji kutoka mbinguni. Kisha Akayapitisha kwenye chemchem katika ardhi, kisha kwa maji hayo akaotesha kwayo mimea yenye rangi mbali mbali? Kisha Hunyauka ukaiona imekuwa kimanjano, na kisha huifanya mapepe. Bila ya shaka katika hayo upo ukumbusho kwa wenye akili.

22. Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola

wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi adhabu kali itawapata wenye nyoyo ngumu zisizomkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.

Kitendawili cha Maisha ya Hapa Duniani

Allah تعالى Anatuambia kuwa asili ya maji ni mbinguni. Hii ni kama Aya.

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا

“...na Tunayateremsha kutoka mbinguni maji safi.” (25:48)

Hivyo Allah تعالى Anateremsha maji kutoka mbinguni na maji hayo yanatuama ardhini na Huyafanya yatiririke kuelekea kokote atakako, na Hutoa chemchem kubwa na ndogo kwa kiasi cha haja.

فَسَلَكَهُمُ الْيَنْبِيعَ فِي الْأَرْضِ

“Kisha Akayapitisha kwenye chemchem katika ardhi,”

Said bin Jubayr na Amir Ash-Sha’bi walisema, maji yote yaliyoko ardhini asili yake ni mbinguni.¹

Said bin Jubayr alisema asili yake iko kwenye barafu, yaani barafu inalundikana huko milimani na kisha hutuama na kuanzisha vijito na chemchem ambazo hutoa maji kutoka chini yake.

ثُمَّ يُخْرَجُ بِهِمُ زُرْعًا مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ

“...kisha kwa maji hayo Akatoa mimea yenye rangi mbali mbali?”

Yaani, kutokana na maji yateremkayo kutoka mawinguni au chemchem na vijito, Allah تعالى Husababisha yaje mazao ya rangi mbali mbali na maumbo tofauti, ladha, harufu mbalimbali na faida zake na mambo mengine mengi.

ثُمَّ يَهَيِّجُ

“Kisha hunyauka ukaiona imekuwa kimanjano.”

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:219.

Yaani baada ya matunda hayo kukomaa na kuiva, hubadilika maumbo na rangi hata kuwa njano na kukauka kabisa.

ثُمَّ يَجْعَلُهُ حُطْمًا ۝

"...kisha Huifanya mapepe."

Maana yake huwa makavu kuukuu.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِأُولِي الْأَلْبَابِ

"Bila ya shaka katika hayo upo ukumbusho kwa wenye akili."

Yaani wanaokumbushwa na maneno haya na wale ambao wanatambua hivyo na kusema kuwa dunia hii iko hivyo. Yaani leo inavutia iko kijani na mbichi, kesho itakuwa kongwe na isiyovutia. Kijana atazeeke na kuwa mwenye kuchoka na dhaifu, mtu mzima asiyejiweza na baada yake atakufa. Aliyebarikiwa ni yule ambaye hali yake baada ya kufa itakuwa ni nzuri. Daima Allah تعالى Hutoa ufananisho wa maisha ya hapa duniani na hali ya maji yanayoteremshwa kutoka Mbinguni. Kisha mimea na mazao kuota na kustawi na kuleta matunda mazuri ambayo hukomaa na kisha kukauka yakawa kukuu.

Hii ni kama aya,

وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلًا الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَا أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيحُ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

"Na wapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji Tunayo yateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vinavyopeperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu." (18:45).

Watu wa Haki Hawalingani na Watu Waliopotea

أَفَمَنْ شَرَحَ اللَّهُ صَدْرَهُ لِلْإِسْلَامِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٍ مِّن رَّبِّهِ ۗ

"Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu Amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?)."

Yaani je huyu mtu atakuwa sawa na yule ambaye roho yake ni ngumu na iko mbali na ukweli?

Hii inafanana na Aya:

أُوْمَن كَانَ مَيِّتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ كَمَن مَّثَلُهُ فِي الظُّلُمَاتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا كَذَلِكَ زُيِّنَ لِلْكَافِرِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

“Je, aliyekuwa maiti kisha Tukamuhisha, na Tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo?” (6:122)

Allah Anasema:

فَوَيْلٌ لِلْفُئْسِيَةِ قُلُوبُهُم مِّنْ ذِكْرِ اللَّهِ

“Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisiomkumbuka Mwenyezi Mungu!”

Yaani, nyoyo zao hazilainiki Allah تعالى Anapotajwa wala hawasikii kunyenyekea au kuogopa na wala hawaelewi kitu.

أُولَئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

“Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.”

اللَّهُ نَزَلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُّتَشَدِّدًا مَّثَانِيَ تَقْشَعِرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ

تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَمَن يُضَلِّ

اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن هَادٍ ﴿١٨﴾

23. Mwenyezi Mungu Ameteremsha Hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo Humuongoa amtakaye. Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumuongoa.

Wasifu wa Qur'an

Allah تعالى Anakisifu Kitabu Chake Qur'an Tukufu ambacho kilishushwa kwa Mtume wake Mtukufu Muhammad ﷺ na Anasema:

اللَّهُ نَزَلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُتَشَبِهًا مَثَانِي

"Mwenyezi Mungu Ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa."

Mujahid alisema, "Hapa maana yake ni kuwa sehemu zote za Qur'an zinalingana na zinarejeana zenyewe kwa zenyewe."¹ Qatadah alisema, "Aya moja inafanana na nyingine; Herufi inafanana na nyingine."² Adh-Dhahhak alisema, "Inajerejea rejea ili watu wapate kufahamu yale ambayo wao anayowaambia." Ikrimah na Al-Hasan walisema, "Allah تعالى Amesifu hukumu zilizomo ndani yake." Na Hassan amezidisha, "Kunaweza kuwa na Aya katika Surah moja ikifanana na aya nyingine katika Surah nyingine." Sa'd bin Jubayr alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, "Inarejewarejewa maana yake, sehemu za Qur'an zinajirejea na zinajikariri na kurudiana."³ Baadhi ya ulamaa wanasema kuwa kauli hiyo ilipokelewa kutoka kwa Sufiyan bin Uyaynah akisema.

مُتَشَبِهًا مَثَانِي

"Kitabu chenye kufanana na kukaririwa."

Maana yake ni kuwa ibara kadhaa za Qur'an zinaweza kuwa zinaashiria kitu kimoja; hivyo aya hizo zinafanana; na hutokea Aya hizo zikataja kitu au jambo na papo hapo kutaja kile kilicho kinyume chake. Mfano wa hilo pale panapotajwa Wachamungu na kisha wakatajwa makafiri; au Pepo na Jahanamu vinapotolewa sifa zake na hali kadhalika; hiyo ndiyo maana ya aya zake kukaririwa na kurudiwa mara kwa mara. Mifano ni ayah,

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٣﴾ وَإِنَّ الْفُجَّارَ لَفِي حَيْمٍ ﴿١٤﴾

"Hakika wema bila ya shaka watakuwa katika neema, na hakika waovu bila ya shaka watakuwa Motoni." (82:13-14)

¹ At-Tabari 21:279.

² At-Tabari 21:279.

³ At-Tabari 21:279.

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْفُجَارِ لَفِي سِجِّينٍ ﴿١٧﴾

"Hasha! Hakika maandiko ya wakosefu bila ya shaka yamo katika Sijjin." mpaka kusema,

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ ﴿١٨﴾

"Hasha! Hakika maandiko ya watu wema bila ya shaka yamo katika I'liyyin." (83:7-18)

هَذَا ذِكْرٌ وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَقَابِرٍ ﴿٤٤﴾

"Huu ni ukumbusho. Na hakika wachamungu wana marudio mazuri." (38:49-55) mpaka,

هَذَا وَابٍ لِلطَّغْيِينِ كَثْرٌ مَقَابِرٍ ﴿٤٥﴾

"Ndio hivi! Na hakika wenye kuasi bila ya shaka watapata marudio maovu kabisa."

Kuna ibara nyingi kama hizo ambazo hukariri aya zake na kuzirudiarudia yaani kuwa kitu kimoja kina maana inayorejewa. Lakini kama ibara ina maana moja na baadhi ya vitu vyake vinafanana hapa husemwa kitu ambacho kina viungo/maungo yanayofanana."

Hapa si maana yake kama *mutashabihat* iliyotajwa ndani ya Aya,

مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخْرٌ مُتَشَابِهَاتٌ ﴿٣٧﴾

"Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi. Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi. Na ziko nyengine za mifano." (3:7)

Inakusudia jambo jingine kabisa.

تَقْشَعُرُّ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ﴿٢٠﴾

"...husingimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu."

Hii ndio sifa ya waja wema; wanaposikia neno kutoka kwa Mola wao Mlezi wao na Anayetweza nguvu kila kitu, Mwenye Kusamehe daima, kwa kuwa wanafahamu ahadi Zake na maonyo Yake ambayo yamo ndani ya neno hilo. Maneno hayo yenye kutisha na yenye maonyo makali hufanya ngozi zao zikasinyaa na kutetemeka kwa woga.

ثُمَّ تَلَيْنُ جُلُودَهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ۗ

“Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.”

Kwa kutumaini kupata Rahma za Mola wao na Huruma Zake. Wao sio kama wale wengine, waovu, watendao madhambi. Tofauti zao ziko za aina tatu.

Tofauti ya Kwanza.

Wanaposomewa au zinaposomwa aya (za Qur’an) wakati wale wengine (waovu) wanasikiliza mashairi na nyimbo zinazoimbwa na wanawake.

Tofauti ya Pili.

Hawa (wao) wanaposikia Aya za Allah تعالیٰ Huanguka na kusujudu huku wakilia wakiwa na hali halisi ya woga, matumaini, mapenzi na uelewa, fahamu na maarifa, kama Anavyosema Allah تعالیٰ.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ

إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢٠﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ

﴿٢١﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا ۚ هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٢٢﴾

“Hakika Waumini ni wale ambao Anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposomewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi. Hao ambao wanashika Swala na wanatoa katika yale Tunayowaruzuku. Hao kweli ndio Waumini. Wao wana vyeo, na msamaha, na riziki bora kutoka, kwa Mola wao Mlezi.” (8:2-4)

وَالَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوا عَلَيْهَا صُمًّا وَعُمْيَانًا ﴿٧٦﴾

“Na wale ambao wanapokumbushwa Aya za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu.” (25:73).

Hawa watu wanaposikia aya za Allah تعالى hakiwashughulishi kingine zaidi ya aya hizo, wanatulia na kusikiliza na kuchukua maana yake (na kuifanyia kazi). Hivyo wanatenda kwa mujibu wa aya na wanasujudu anapozisikia kutokana na kuzielewa kwao na siyo kwa ajili ya ujinga, hawafanyi hivyo kibubusa.

Tofauti ya Tatu

Wanashikamana na maadili halisi ya Uislamu wanapozisikia Aya za Qur’an. Hawa wanafanya kama vile walivyokuwa wakifanya masahaba pale ambapo Mtume ﷺ alipokuwa akisoma Qur’an. Ngozi zao huvingia simanzi na nyoyo zao kulainika kwa kumkumbuka Allah تعالى. Hawakuwa wakipiga makelele wala kuzungumza maneno ya kipuuzi, badala yake walitulia kimya wakiwa katika hali ya woga, umakini, adabu na ithibati, ambayo hawakuwa nayo watu wengine, walipata kusifiwa na Mola wao kwa sifa njema duniani na Akhera. Abdur-Razaaq alisema, “Ma’amar alituambia kuwa Qatadah alisoma Aya hii.

تَقْشَعْرُ مِنْهُ جُلُودُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ثُمَّ تَلِينُ جُلُودُهُمْ وَقُلُوبُهُمْ إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ ۗ

“...hisisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.”

Na akasema, “Hizi ndizo sifa na tabia za mawalii wa Allah تعالى; Allah تعالى Amewaelezea na kutaja sifa na tabia zao namna hii, kuwa ngozi zao husisimka, macho yao hutoa machozi na nyoyo zao hutulia katika kumkumbuka Allah تعالى. Hakusema kuwa hupotelewa na akili na wakapayuka; hizo ni tabia na sifa za wale wanaofuata mambo ya uzushi; na hayo yanatoka kwa shetani. Allah تعالى Anasema,

ذَٰلِكَ هُدَىٰ اللَّهِ يَهْدِي بِهِ مَن يَشَاءُ مِن عِبَادِهِ ۗ

“Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo Humuongoa Amtakaye.” (6:88)

Yaani, hizo ni tabia na sifa za wale walioongolewa na Allah تعالى, mwenye kufanya tofauti na hayo ni katika wale ambao Allah تعالى Amewanyima uongofu na Akawaacha wapotee.

وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ

“Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumuongoa.”

أَفَمَنْ يَتَّقِ بِوَجْهِهِ سُوءَ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَقِيلَ لِلظَّالِمِينَ ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٤١﴾ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَآتَاهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٢﴾ فَأَذَاقَهُمُ اللَّهُ الْخِزْيَ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤٣﴾

24. Je! Atakayekuwa anapambana kwa uso wake na adhabu mbaya kabisa Siku ya Kiyama (ni sawa na watenda wema?) Na wataambiwa wenye kudhulumu: Onjeni hayo mliyokuwa mkiyachuma!

25. Waliokuwa kabla yao walikadhibisha, na ikawajia adhabu kutoka pahala wasipopatambua.

26. Basi Mwenyezi Mungu Akawaonjesha hizaya katika uhai wa duniani. Na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi; laiti wangeli jua!

Mwisho wa Makafiri

Allah تعالى Amesema,

أَفَمَنْ يَتَّقِ بِوَجْهِهِ سُوءَ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Je! Atakayekuwa anapambana kwa uso wake na adhabu mbaya kabisa Siku ya Kiyama (ni sawa na watenda wema?)”

Atakemewa yeye na watenda maovu wenziwe kama yeye na wataambiwa:

ذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ

“Onjeni hayo mliyokuwa mkiyachuma!”

Je huyu ni kama anayekuja Siku ya Kiama akiwa salama? Kama Asemavyo Allah تعالى،

أَفَمَنْ يَمْشِي مُكِبًّا عَلَىٰ وَجْهِهِ أَهْدَىٰ أَمَّنْ يَمْشِي سَوِيًّا عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦٧﴾

“Je! Anayekwenda akisinukia juu ya uso wake ni muongofu zaidi, au yule anayekwenda sawasawa katika Njia Iliyo Nyooka?” (67:22)

يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٤٨﴾

“Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!” (54:48) na,

أَفَمَنْ يُلْقَىٰ فِي النَّارِ خَيْرٌ أَمْ مَنْ يَأْتِي ءَامِنًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ﴿٤٠﴾

“Je! Atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja kwa amani Siku ya Kiyama?” (41:40).

Katika aya hizi zote ingeliweza kutosheleza na kuleta maana kamili kwa kutaja kundi moja tu la watu kati ya makundi mawili.

كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَأَتَنَّهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٠﴾

“Waliokuwa kabla yao walikadhibisha, na ikawajia adhabu kutoka pahala wasipopatambua.”

Yaani watu wa karne za nyuma ambao waliwakana Mitume, Allah تعالى Aliwaangamiza kwa sababu ya madhambi yao. Na walikuwa hawana wa kuwazuia na adhabu au kuwahifadhi wasiharibiwe na adhabu ya Allah تعالى.

فَأَذَاقَهُمُ اللَّهُ الْحَزْنَ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ﴿٥١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Akawaonjesha hizaya katika uhai wa duniani.”

Yaani kwa njia ya adhabu na kisasi ambacho Allah تعالى Alichowateremshia, na furaha ya waumini kwa yaliyowapata hao. Hivyo wale walioambiwa hayo watambue kuwa, kwa sababu wao wamemkataa Mtukufu wa Mitume yote, na Mtume wa Manabii ﷺ. Na yale yote ambayo Allah تعالى Ameyaahidi kuwa katika adhabu kali huko Akhera, wataipata adhabu hiyo kali zaidi kuliko masaiibu ya duniani. Allah تعالى Anasema:

وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

“Na bila ya shaka adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi; laiti wangelijua!”

* * *

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ لَعَلَّهُمْ
 يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾ قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ
 ﴿٢٨﴾ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلًا فِيهِ شُرَكَاءُ مُتَشَبِكُونَ وَرَجُلًا
 سَلَمًا لِرَجُلٍ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۗ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿٢٩﴾ إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ﴿٣١﴾ * فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن
 كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ إِذْ جَاءَهُ ۗ أَلَيْسَ فِي
 جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ ﴿٣٢﴾ وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ
 بِهِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٣٣﴾ هُمْ مَّا يَشَاءُونَ ۖ عِنْدَ
 رَبِّهِمْ ۗ ذَٰلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٤﴾ لِيُكَفِّرَ اللَّهُ عَنْهُمْ أَسْوَأَ
 الَّذِي عَمِلُوا وَيَجْزِيَهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ
 ﴿٣٥﴾ أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ وَتُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِنْ
 دُونِهِ ۗ وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٦﴾ وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ
 فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ ذِي انْتِقَامٍ ﴿٣٧﴾ وَإِنْ
 سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ ۗ اللَّهُ ۗ قُلْ
 أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ
 كَاشِفَاتُ ضُرِّيهِ أَوْ أَرَادَنِيَ بِرَحْمَةٍ هَلْ هِيَ مُمْسِكَةٌ
 بِرَحْمَتِهِ ۗ قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ ۗ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٣٨﴾
 قُلْ يَنْقُورِ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَمِلٌ ۗ فَسَوْفَ
 نَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ مُخْتَلِفٌ وَّجِلٌّ عَلَيْهِ
 عَذَابٌ مُّغِيبٌ ﴿٤٠﴾

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ
 مِنْ كُلِّ مَثَلٍ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾
 قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَعَلَّهُمْ
 يَتَّقُونَ ﴿٢٨﴾ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلًا
 فِيهِ شُرَكَاءُ مُتَشَبِكُونَ وَرَجُلًا سَلَمًا
 لِرَجُلٍ هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۗ الْحَمْدُ لِلَّهِ
 ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٩﴾ إِنَّكَ
 مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ ﴿٣٠﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ
 يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ
 تَخْتَصِمُونَ ﴿٣١﴾

27. Na bila ya shaka Tume-wapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qur'ani ili wapate kuku-mbuka.

28. Qur'ani iliyoteremka kwa lugha ya Kiarabu isiyo na upogo, ili wamche Mungu.

29. Mwenyezi Mungu Amapiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanaogombana, na wa mtu mwengine aliye-khusika na bwana mmoja tu. Je! Wako sawa katika hali zao? Alhamdulillah,

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu! Lakini wengi wao hawajui.

30. Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.

31. Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu Mlezi.

Mfano wa Ushirikina

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ

“Na bila ya shaka Tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qur’ani...”

Yaani, Tumewafafanulia binadamu (katika Qur’an) kwa kuwapa mifano na methali.

لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“...ili wapate kukumbuka.”

Kwa kuwa methali huleta maana ya karibu zaidi na ya wazi kwenye fikra za watu. Allah تعالى Anasema,

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ

“Amekupigieni mfano kutokana na nafsi zenu.” (30:28)

Yaani ili mpate kujifunza wenyewe na kufahamu. Allah تعالى Anasema,

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ

“Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu.” (29:43)

قُرْآنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِي عِوَجٍ

“Qur’ani ya Kiarabu isiyo na upogo.”

Yaani: (Ujumbe) umo katika lugha ya Kiarabu iliyo nyepesi bila kuwepo mafumbo au, hali ya kuzungusha maneno au mkanganyiko. Ni nyepesi na ni ushahidi ulio wazi. Allah تعالى Ameifanya hiyo Qur’an hivyo na Akaishusha kama ilivyo.

لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

“...ili wamche Mungu.”

Yaani, ili wapate kufahamu yaliyomo na waogope maonyo yake na wajitahidi kuelekeza juhudi zao kwenye mambo ambayo wameahidiwa kutolewa kwa watu wema. Kisha Allah تعالى Anasema;

ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلًا فِيهِ شُرَكَاءُ مُتَشَبِكُونَ

“Mwenyezi Mungu Amepiga mfano wa mtu mwenye mabwana washirika wanaogombana.”

Maana yake, watu ambao walikuwa wana mtumwa mmoja walianza mvutano juu ya mtu wao huyo.

وَرَجُلًا سَلَمًا لِرَجُلٍ

“...na wa mtu mwengine aliye khusika na bwana mmoja tu.”

Maana yake, hakuna aliyemiliki isipokuwa mtu mmoja tu.

هَلْ يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا

“Je! Wako sawa katika hali zao?”

Watu hawa wawili hawalingani. Kwa mfano huo, wale ambao wanamuabudu Allah تعالى na zaidi ya hapo wakaabudu vitu vingine, hao ni washirikina; hawalingani na yule ambaye anamuabudu Allah تعالى Peke Yake. Hawa waja wawili hawalingani na hawafanani. Ibn Abbas رضي الله عنهما Mujahid na wengine wengi walisema, “Aya hii ni methali ielezayo (tofauti) kati ya mshirikina na Mchamungu.”¹

Kwa kuwa mfano huu uko wazi kabisa, na ndipo Allah تعالى Akasema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ

“Alhamdulillah, Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu!”

Maana yake baada ya kuweka wazi hoja nzito dhidi ya washirikina.

¹ At-Tabari 21:285.

بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini wengi wao hawajui.” Yaani, (kwa kutokujua kwao) ndio maana wengi wao wanamshirikisha Allah تعالى.

Mauti ya Mtume ﷺ na Makuraishi, na Kugombana Kwao Mbele ya Allah تعالى

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِلَيْهِمْ مَرْثَتُونَ ﴿٣٩﴾

“Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa.”

Hii ni miongoni mwa aya ambazo Abubakr As-Sadiq رضي الله عنه alitolea hoja pale alipofariki Mtume ﷺ ili watu wafahamu na kuzingatia ukweli kuwa amefariki.

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَلَا يَنْبَغِي أَنْ يَكُونَ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ
وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقْبَيْهِ فَلَنَ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿٣٩﴾

“Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtagauka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Atawalipa wanaomshukuru.” (3:144.)

Maana ya Aya hii ni kuwa bila shaka mtaihama hii dunia na mkusanywe mbele ya Allah تعالى huko Akhera. Na hapo mambo yatakuwa ni mawili tu ama Tawhid au Shiriki; na Allah تعالى Atahukumu juu yake kulingana na matendo ya watu duniani bila kupendelea, (walikuwa kwenye Tawhid au walikuwa wakifanya Shiriki). Yeye (Allah تعالى) Ndiye Hakimu, Mjuzi wa mambo yote. Hivyo Atawanusuru na adhabu wale waliokuwa wakimuabudu Yeye bila kumshirikisha na Atawaadhibu waliokufuru na kukataa Tawhid (au kwa kukanusha Uungu Wake au kumshirikisha). Hawa makafiri na washirikina watabisha huko Akhera; kama wanavyobisha duniani. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alisema kuwa Az-Zubayr رضي الله عنه alisema, “Wakati ilipoteremshwa Aya,

ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ﴿٣٩﴾

“Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola Wenu Mlezi.”

Az-zubayr رضي الله عنه alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! vipi tutarejea tena huko Akhera katika mabishano yetu?" Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ»

"Naam." Az-zubayr رضي الله عنه akasema, "Jambo hili zito sana."¹

Ahmad alipokea riwaya kutoka kwa Az-Zubayr bin Al-Awwam رضي الله عنه kuwa pale Surah hii iliposhuka kwa Mtume ﷺ,

إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ ﴿٣٩﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ﴿٤٠﴾

"Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa. Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu Mlezi."

Az-Zubayr رضي الله عنه alisema, "Ewe Mjumbe wa Allah! je madhambi tuliyoafanya hapa duniani yatarejewa (huko Akhera) tuyaone?" Mtume ﷺ alisema.

«نَعَمْ، لَيُكْرَرَنَّ عَلَيْكُمْ حَتَّى يُؤَدَّى إِلَى كُلِّ ذِي حَقٍّ حَقُّهُ»

"Naam, yatarejewa mpaka kila mmoja ajue haki yake ni ipi."

Az-Zubayr رضي الله عنه akasema, "Wallahi hili ni jambo zito sana."² Naye At-Tirmidhi aliandika na kuipa Hadithi hii daraja ya "Hasan Sahihi."³ akasema, Ali bin Abi Talha alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa,

ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ﴿٣٩﴾

"Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu Mlezi."

Maana yake, wale walio wa kweli watabishana na warongo, waliodhulumiwa watabishana na madhalimu, na yule aliyongoka atabishana na aliyepotea na dhaifu atabishana na jabari na mwenye mabavu.

Ibn Manda رحمه الله تعالى ameandika katika Kitab *Ar-Ruh* kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Watu watabishana Siku ya Kiama kiasi cha kufikia hatua roho nayo itahasimiana na mwili, Roho itasema kuuambia mwili wewe ndiye

¹ *Ad-Dur Al-Manthur* 5:614.

² Ahmad 1:164.

³ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:289.

uliyetenda. Na mwili nao utaiambia roho: na wewe umeamrisha na kulipamba jambo hili." Kisha Allah تعالى Atapeleka malaika kuwa hukumu; na atasema, "Ninyi ni kama watu wawili; mmoja hawezi kutembea lakini anaona na mwingine ana weza kutembea lakini haoni. wawili hawa waliingia ndani ya bustani. Yule anayeona akamuambia mwenziwe kipofu, "Naona tunda lakini siwezi kulifikia." Kipofu akamuambia kiwete, "Panda juu yangu, ulifikie." Kiwete akapanda juu ya kipofu na akalifikia hilo tunda. Sasa nani mkosaji kati yao." Jawabu ni, "wote wawili." Malaika atawaambia "Mmeji hukumu wenyewe." Mwili ulikuwa ni kama kipando cha usafiri kwa roho."

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Said bin Jubayr kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Aya hii iliteremka na hatukujua sababu yake nini."

ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ ﴿٣٩﴾

"Kisha bila ya shaka mtagombana Siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu Mlezi."

Akasema, "Tulisema kwa nini tubishane? Hakuna cha upinzani kati yetu na *Ahlul kitab*, hivyo ubishi unatoka wapi? Mpaka ikatokea fitnah." Kisha Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Haya ndiyo Mola Wetu Aliyotuahidi kwa Kutuambia kuwa tubishane ndani yake." Kauli hii iliandikwa na An-Nasai.¹

* فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصَّدَقِ إِذْ جَاءَهُۥٓ أَلْبَسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى
لِّلْكَافِرِينَ ﴿٣٩﴾ وَالَّذِي جَاءَ بِالصَّدَقِ وَصَدَّقَ بِهِۦٓ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ ﴿٤٠﴾ هُمْ
مَا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ ذَٰلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿٤١﴾ لِيُكَفِّرَ اللَّهُ عَنْهُمْ أَسْوَأَ الَّذِي
عَمَلُوا وَيَجْزِيَهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٤٢﴾

32. Basi ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule aliyemsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikanusha kweli imfikiapo? Je! Siyo katika Jahannamu makaazi ya hao makafiri?

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* na.11447. Isnadi yake ni dhaifu. Hii inakusudia machafuko ya wenyewe kwa wenyewe yaliyoanza baada ya kuuliwa Sayyidna Uthman رضي الله عنه

33. Na aliyeileta Kweli na akaithibitisha - hao ndio wachamungu.

34. Watapata watakachotaka kwa Mola wao Mlezi. Hayo ndiyo malipo ya watendao mema.

35. Ili Mwenyezi Mungu Awafutie maovu waliyoyafanya na Awalipe ujira wao kwa mujibu wa ukomo wa wema waliokuwa wakiutenda.

Adhabu ya Makafiri na Waongo na Malipo Mema kwa Wachamungu

Washirikina wamekuwa wakisema uongo juu ya Allah تعالى, wakieleza kuwa kuna Mungu mwingine na wakadai Malaika walikuwa ni mabinti wa Allah; na hata wamesema kuwa Allah تعالى Ana mtoto. Allah تعالى Ametakasika na yote hayo. Zaidi ya hapo wameukataa ukweli ulipowajia kupitia midomo ya Mitume (reheema na amani ya Allah تعالى iwafikie). Allah تعالى Anasema.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ عَلَى اللَّهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ إِذْ جَاءَهُ^٤

“Basi ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule aliyemsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na kuikanusha kweli imfikiapo?”

Yaani, hakuna anayekosea zaidi ya huyo, kwa sababu anachanganya vitu viwili vizito, uongo na kisha kumkufuru Allah تعالى na kutokuamini Mitume wa Allah. Walileta madai ya uongo na kukataa ukweli, na Allah تعالى Akawapa onyo kali.

أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكَافِرِينَ

“Je! Siyo katika Jahannamu makaazi ya hao makafiri?”

Wale wanaokufuru na kuukataa ukweli. Kisha Allah تعالى Anasema,

وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهِ^٥

“Na aliyeileta Kweli na akaithibitisha.”

Mujahid, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas na Ibn Zayd walisema, “Yule aliyeleta ukweli alikuwa ni Mtume ﷺ.”¹

¹ At-Tabari 21:289, Al-Qurtubi 15:256.

Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema,

وَالَّذِي جَاءَ بِالصِّدْقِ

“Na aliyeileta Kweli...”

Yaani, Mtume ﷺ,

وَصَدَّقَ بِهِ

“...na akaithibitisha...”

Maana yake, ni kuwa hao ni Waislamu.¹

أُولَئِكَ هُمُ الْمُتَّقُونَ

“...hao ndio wachamungu.”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Wanaogopa na kuikwepa Shiriki.”²

هُم مَّا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Watapata watakachotaka kwa Mola wao Mlezi.”

Yaani, Peponi, chochote wanachotaka wanapata.

ذَلِكَ جَزَاءُ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٦﴾ لِيُكَفِّرَ اللَّهُ عَنْهُمْ أَسْوَأَ الَّذِي عَمِلُوا وَيَجْزِيَهُمْ أَجْرَهُمْ
بِأَحْسَنِ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

“Hayo ndiyo malipo ya watendao mema. Ili Mwenyezi Mungu Awafutie ukomo wa uovu walioufanya na Awalipe ujira wao kwa mujibu wa ukomo wa wema waliokuwa wakiutenda.”

Hii kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya Nyingine,

أُولَئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَتَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّئَاتِهِمْ فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ وَعَدَّ
الصِّدْقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٨﴾

¹ At-Tabari 21:290

² At-Tabari 21:292

"Hao ndio Tunaowapokelea bora ya vitendo vyao walivyovitenda, na Tunayasamehe makosa yao. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi. Miadi ya kweli hiyo walioahidiwa." (46:16).

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ ۗ مِنْ دُونِهِ ۗ وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ۖ وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ ذِي انْتِقَامٍ ۖ ﴿٣٦﴾
 سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ ۗ اللَّهُ ۗ قُلْ أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كَاشِفَاتُ ضُرِّهِ ۚ أَوْ أَرَادَنِي بِرَحْمَةٍ هَلْ هِيَ مُمْسِكَةٌ بِرَحْمَتِهِ ۗ قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ ۖ ﴿٣٧﴾
 قُلْ يَنْقُورِ أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَانَتِكُمْ إِنِّي عَمِلٌ ۗ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ۖ ﴿٣٨﴾
 مَنْ يَأْتِهِ عَذَابٌ مُخْتَزِعٌ مِمَّنْ هَلْ يَمَسُّهُ مِنْ عَذَابٍ مُقِيمٍ ۖ ﴿٣٩﴾

36. Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtoshela mja wake? Na ati wanakutishia kwa hao wenginewe wasiokuwa Yeye! Na aliye hukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa.

37. Na ambaye Mwenyezi Mungu Anamuongoa hakuna awezae kumpoteza. Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye Nguvu Anayeweza kulipiza?

38. Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Sema: Je! Mnawaonaje wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa Mwenyezi Mungu Akitaka kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara Yake? Au Akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema Yake? Sema: Mwenyezi Mungu Ananitoshela. Kwake Yeye wategemea wanaotegemea.

39. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muezavyo, mimi pia nafanya. Basi mtakuja ona.

40. Ni nani itakayemfikia adhabu ya kumfedhehesha, na itakayemshukia adhabu yenye kudumu.

Mungu Anawatosheleza Waja Wake

Allah تعالی Amesema,

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ

“Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtosheleza mja Wake?”

Baadhi ya watu huisoma aya hii kwa wingi wa “waja wake.” Ina maana Allah تعالی Anatosha kwa mja Wake mmoja anayemuabudu Yeye tu na akamtegemea Yeye tu.

وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِنْ دُونِهِ

“Na ati wanakutishia kwa hao wengine wasiokuwa Yeye.!”

Yaani, washirikina walijaribu kumtisha Mtume ﷺ na masanamu yao na miungu yao ambayo waliabudu asiyekuwa Allah. Kwa sababu ya ujinga wao na kukosa kwao uongofu wa Allah تعالی.

Allah تعالی Anasema,

وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٩﴾ وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُضِلٍّ ۗ أَلَيْسَ اللَّهُ بِعَزِيزٍ

ذِي أَنْتِقَامٍ ﴿٤٠﴾

“Na aliye hukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa. Na ambaye Mwenyezi Mungu Anamuongoa hakuna awezae kumpoteza. Je! Mwenyezi Mungu si Mwenye Nguvu Anayeweza kulipiza? ?”

Maana yake ni kuwa yeyote anayemtegemea Allah تعالی na akamgeukia Yeye tu daima hatoachwa kuangamia, kwa sababu Allah تعالی Ndiye Muweza wa kila kitu na hakuna chochote kitakachomshinda.

Hakuna aliye kama Allah تعالی katika Kutoa haki kwa wale ambao wamemkufuru au wamemshirikisha na vitu vingine katika ibada na wale ambao hawako tayari kumkubali Mtume Muhammad ﷺ.

Washirikina Wanaungama kuwa Allah تعالى Ndiye Muombwaji Pekee kwa sababu Miungu yao Wanaijua kuwa Haiwezi Kufanya Hilo.

Allah تعالى Amesema,

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ ۗ اللَّهُ

“Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu.”

Allah تعالى Ndiye Muumba wa vitu vyote, lakini licha ya hivyo bado waliabudu miungu mingine pamoja Naye, miungu ambayo ilikuwa haina uwezo, wala nguvu za kuleta faida na manufaa au kudhuru. Allah تعالى Anasema.

قُلْ أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِمَّا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كَاشِفَاتُ ضُرِّيهِ أَوْ أَرَادَنِي بِرَحْمَةٍ هَلْ هِيَ مُمْسِكَةٌ بِرَحْمَتِهِ

“Sema: Je! Mnawaonaje wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa Mwenyezi Mungu Akitaka Kunidhuru, wao wanaweza kuniondolea dhara Yake? Au Akitaka Kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema Yake?”

Maana: Hiyo (miungu) haiwezi kufanya lolote hata kidogo. Ibn Abi Hatim رضي الله عنهما alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رحمه الله تعالى kauli ambayo aliinasibisha kwa Mtume ﷺ,

«احْفَظِ اللَّهَ يَحْفَظْكَ، احْفَظِ اللَّهَ تَجِدَهُ تُجَاهَكَ، تَعَرَّفَ إِلَى اللَّهِ فِي الرَّخَاءِ يَعْرِفَكَ فِي الشَّدَةِ، إِذَا سَأَلْتَ فَاسْأَلِ اللَّهَ، وَإِذَا اسْتَعْنَيْتَ فَاسْتَعِنْ بِاللَّهِ، وَاعْلَمْ أَنَّ الْأُمَّةَ لَوِ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَضُرُّوكَ بِشَيْءٍ لَمْ يَكْتُبْهُ اللَّهُ عَلَيْكَ لَمْ يَضُرُّوكَ، وَلَوْ اجْتَمَعُوا عَلَى أَنْ يَنْفَعُوكَ بِشَيْءٍ لَمْ يَكْتُبْهُ اللَّهُ لَكَ لَمْ يَنْفَعُوكَ، جَمَّتِ الصُّحُفُ وَرَفِعَتِ الْأَقْلَامُ، وَاعْمَلْ لِلَّهِ بِالشُّكْرِ فِي الْيَقِينِ. وَاعْلَمْ أَنَّ فِي الصَّبْرِ عَلَى مَا تَكَرَّرَ خَيْرًا كَثِيرًا، وَأَنَّ النَّصْرَ مَعَ الصَّبْرِ، وَأَنَّ الْفَرْجَ مَعَ الْكُرْبِ، وَأَنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا»

“Mhifadhi Allah Atakulinda, Mhifadhi Allah utampata mbele yako, Mgeukie Mola wako wakati wa raha Atakuangalia wakati wa shida. pindi uombapo, basi muombe Allah; kama wahitaji msaada basi omba msaada wa Allah. Tambua kuwa lau kama taifa zima

lingejumuika ili kukuletea madhara ambayo Mola wako hajapitisha Uamuzi Wake, hawataweza kukudhuru; na kama walikusanyana ili kukuletea jambo ambalo ni zuri kwako lakini Mola wako Mlezi hakulipitisha basi hawatofanikiwa. Maandishi yamekwisha (andikwa na) kukauka na kalamu kuondolewa. Weka juhudi zako zote kwa ajili ya Allah, ukiwa mwenye shukrani Kwake na mwenye imani tele juu Yake; na tambua kuwa kuna mambo mazuri kwako unapokuwa na subira na uvumilivu yanapokufika mambo (mazito). Ushindi hupatikana kutokana na subira, furaha huja kutokana na shida na kila magumu hufuatiwa na mepesi.¹

قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ

“Sema: Mwenyezi Mungu Ananitosheleza.”

Maana yake, “Mungu Ananitosha”. Ni kama aya,

وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٧٧﴾

“Juu Yake Yeye mimi nimetegemea, na juu Yake Yeye wategemee wanao tegemea.” (12:67).

Haya ni kama yale maneno aliyosema Hud عليه السلام kwa watu wake,

إِنْ نَقُولُ إِلَّا أَعْرَضْنَا بَعْضُ الْهَيْئَاتِ بِسُوءٍ ۗ قَالَ إِنْ أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا
تُشْرِكُونَ ﴿٧٧﴾ مِنْ دُونِهِ ۗ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونَ ﴿٧٨﴾ إِنْ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي
وَرَبِّكُمْ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِعَاصِيَتِهَا ۗ إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٩﴾

“Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa. Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnao wafanya washirika, Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula! Hakika mimi nimetegemea

¹ Ahmad 1:307.

Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi Wangu na Mola Mlezi Wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamuendesha Atakavyo. Hakika Mola Wangu Mlezi Yuko juu ya njia Iliyonyooka. (11:54-56).

قُلْ يَنْقُورِ أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَاتِبِكُمْ

“Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni muwezavyo.”

Hili ni onyo na tishio,

إِنِّي عَمِلٌ

“...mimi pia nafanya.”

Yaani, “kama ninavyotaka kufanya.”

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

“Basi mtakujaona,”

Yaani, mtakuja tambua athari ya maneno na matendo yenu hapo baadaye na mtajuta.

مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ مُّخْزٍ

“Ni nani itakayemfikia adhabu ya kumfedhehesha.”

Yaani, hapa duniani.

وَيُحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ

“Na itakayemshukia adhabu yenye kudumu. ”

Maana yake, inayoendelea milele, isiyokwepeka, ambayo itawajieni Siku ya Kiyama. Allah تعالیٰ Atulinde nayo hiyo adhabu.

* * *

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ ۖ فَمَنِ اهْتَدَىٰ
 فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ
 بِوَكِيلٍ ﴿٤١﴾ اللَّهُ يَتَوَقَّى الْأَنْفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ
 تَمُتْ فِي مَنَامِهَا ۖ فَيُمْسِكُ الَّتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا الْمَوْتَ
 وَيُرْسِلُ الْأُخْرَىٰ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾ أَمْ أَخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ شُفَعَاءَ ۗ
 قُلْ أَوْلَوْ كَانُوا لَا يَمْلِكُونَ شَيْئًا وَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٣﴾
 قُلْ لِلَّهِ الشَّفَعَةُ جَمِيعًا ۗ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ ثُمَّ
 إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٤٤﴾ وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ اشْمَأَزَّتْ قُلُوبُ
 الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ ۖ وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ
 إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٥﴾ قُلِ اللَّهُمَّ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ عَلِيمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِي
 مَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٤٦﴾ وَلَوْ أَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا مَا
 فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لَافْتَدَوْا بِهِ مِنْ سُوءِ
 الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَبَدَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُوا
 يَحْتَسِبُونَ ﴿٤٧﴾ وَبَدَا لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَحَاقَ بِهِمْ
 مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٤٨﴾

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ
 بِالْحَقِّ ۖ فَمَنِ اهْتَدَىٰ فَلِنَفْسِهِ ۖ
 وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَمَا
 أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ﴿٤١﴾ اللَّهُ يَتَوَقَّى
 الْأَنْفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ
 فِي مَنَامِهَا ۖ فَيُمْسِكُ الَّتِي قَضَىٰ
 عَلَيْهَا الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْأُخْرَىٰ إِلَىٰ
 أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٢﴾

**41. Hakika Sisi Tumeku-
 teremshia Kitabu kwa ajili
 ya watu wote kwa kuwa-
 wekea wazi Haki. Basi
 mwenye kuongoka ni kwa
 manufaa ya nafsi yake, na
 mwenye kupotoka bila ya
 shaka amepotoka kwa
 khasara yake. Na wewe si
 mlinzi juu yao.**

**42. Mwenyezi Mungu
 Huzipokea roho zinapokufa.
 Na zile zisizokufa wakati
 wa kulala kwake, Huzishika
 zilizohukumiwa kufa, na**

**Huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila
 ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaofikiri.**

Allah تعالیٰ Anasema Akielekeza Kauli Yake kwa Mjumbe Wake Muhammad ﷺ

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ

“Hakika Sisi Tumekuteremshia Kitabu ...” Yaani, Qur’an.

لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ

“...kwa ajili ya watu wote kwa Haki.”

Yaani kwa viumbe vyote, binadamu na majini ili awape mwongozo na kuwaonya na maovu kutokana na Kitabu hicho.

فَمَنْ أَهْتَدَىٰ فَلِنَفْسِهِ

“Basi mwenye kuongoka ni kwa nafsi yake.”

Yaani, faida na manufaa yake vitarejea kwake mwenyewe (akikubali).

وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا

“...na mwenye kupotoka bila ya shaka amepotoka kwa khasara yake.”

Maana yake athari za kwenda kombo zitamrejea mwenyewe (aliyekataa).

وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ

“Na wewe si mlinzi juu yao.”

Yaani si jukumu lako wala huwajibiki na kuongoka kwao au kutokuongoka kwao.

إِنَّمَا أَنْتَ نَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

“Wewe ni mwonyaji tu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa kila kitu.” (11:12)

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

“...juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu.” (13:40).

Allah تعالى Pekee Ndiye Ambaye Hufisha na Kuhuisha

Hapa Allah تعالى Anatuambia kuwa Yeye Anamiliki vitu vyote, na Anatawala mienendo yake yote na Yeye Ndiye Anafanya vile atakavyo. Anawaitea binadamu mauti (kifo kikubwa) pale Anapopeleka Malaika kwenda kuchukua roho zao kutoka mwilini mwao na huwafisha “kifo kidogo” pale wanapolala. Allah تعالى anasema,

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ بِاللَّيْلِ وَيَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ ثُمَّ يَبْعَثُكُمْ فِيهِ لِيُقْضَىٰ أَجَلٌ مُّسَيِّئٌ ثُمَّ إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ يُنْفِخُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٤٦﴾ وَهُوَ الْغَافِرُ فَوْقَ عِبَادِهِ ۗ وَيُرْسِلُ عَلَيْكُمْ حَفَظَةً حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَكُمْ الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفْرِطُونَ ﴿٤٧﴾

“Naye Ndiye Anayekufisheni usiku, na Anayajua mnyoyafanya mchana. Kisha Yeye Hukufufueni humo mchana ili muda ulio wekwa utimizwe. Kisha Kwake Yeye ndiyo marejeo yenu, na tena Akuwambieni mliyokuwa mkiyafanya. Naye Ndiye Mwenye Nguvu za Kushinda, Aliye juu ya waja Wake. Na Hukupelekeeni waangalizi, mpaka mmoja wenu yakimjia mauti wajumbe Wetu humfisha, nao hawafanyi makosa.” (6:60-61).

Allah تعالى Anataja aina mbili za kifo, kifo kidogo na kifo kikubwa baada yake, katika Aya hapo juu (39:42). Allah تعالى Anataja kifo kikubwa kwanza kisha kidogo:

اللَّهُ يَتَوَفَّى الْأَنْفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا ۗ فِيمِمْسَلِئٍ أَلَّتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْأَخْرَىٰ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَيِّئٍ ۗ

“Mwenyezi Mungu Huzipokea roho zinapokufa. Na zile zisio kufa wakati wa kulala kwake, Huzishika zilizohukumiwa kufa, na Huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa.”

Hapa inaashiriwa kuwa roho hukutana mahali pamoja huko mbinguni, kama ilivyoelezwa ndani ya Hadithi ya Mtume ﷺ iliyopokelewa na Ibn Mandah na wengine. Ndani ya Sahihi Mbili, Bukhari na Muslim, imepokelewa kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa, Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا أَوْىٰ أَحَدُكُمْ إِلَىٰ فِرَاشِهِ فَلْيَنْفِضْهُ بِدَاخِلَةِ إِزَارِهِ، فَإِنَّهُ لَا يَدْرِي مَا خَلْفَهُ عَلَيْهِ، ثُمَّ لِيَقُلْ: بِاسْمِكَ رَبِّي وَضَعْتَ جَنِّي، وَبِكَ أَرْفَعُهُ، إِنْ أَمْسَكَتَ نَفْسِي فَارْحَمْهَا، وَإِنْ أَرْسَلْتَهَا فَاحْفَظْهَا بِمَا تَحْفَظُ بِهِ عِبَادَكَ الصَّالِحِينَ»

"Mmoja wenu akienda kulala basi akung'ute kitanda chake na izari yake (shuka, kitima) kwa sababu hajui kitu gani kimekuja kitandani kwake tangu aondoke. Kisha aseme, "Kwa Jina Lako, Mola Wangu naweka chini ubavu wangu na kwa Jina Lako nauinua, kama Utaichukua roho yangu basi Iteremshie Rahma Zako, na kama Utairejesha Ihifadhi pamoja na vile Unavyohifadhia waja Wako wema."¹

فَيَمْسِكُ أَلْتِي قَضَىٰ عَلَيْهَا أَلْمَوْتَ

"...Huzishika zilizohukumiwa kufa."

Maana yake zile roho ambazo zimekwisha kufariki na Kuzirejesha zile ambazo muda wake bado kufika. As-Suddi alisema, "Kwa muda wote wa uhai wao."²

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Huziba kisha pale pale zile roho za wale waliokwishakufa na Kuzirejesha roho za wale ambao bado wako hai, na Hafanyi kosa wala Hakosei hata kidogo."

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

"Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri."

أَمِرٌ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ شُفَعَاءَ ۗ قُلْ أُولَٰئِكَ كَانُوا لَا يَمْلِكُونَ شَيْئًا وَلَا يَعْقِلُونَ ﴿٤١﴾

قُلْ لِلَّهِ الشَّفَعَةُ جَمِيعًا ۗ لَهُ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٤٢﴾ وَإِذَا ذُكِرَ

اللَّهُ وَحْدَهُ أَشْمَازَتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ ۗ وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ إِذَا

هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٣﴾

¹ Fat'h Al-Bari 11:130, Muslim 4:2084

² At-Tabari 21:298

43. Au ndio wamejifanyia waombezi badala ya Mwenyezi Mungu? Sema: Ingawa hawana mamlaka juu ya kitu chochote, wala hawatambui lolote?

44. Sema: Uombezi wote uko juu ya Amri Mwenyezi Mungu. Ni Wake Yeye tu ufalme wa mbingu na ardhi. Kisha mtarejeshwa Kwake.

45. Na anapotajwa Mwenyezi Mungu Peke Yake nyoyo za wasio iamini Akhera hujikusanya kwa chuki. Na wanapotajwa wenginewe asiye kuwa Yeye basi wao hufurahi.

Hakuna Maombezi Isipokuwa kwa Idhini ya Allah ﷻ; Jinsi Gani Washirikina Hughadhibika Anapotajwa Allah ﷻ Peke Yake

Allah ﷻ Anawalaumu washirikina kwa kuyafanya kuwa masanamu maombezi badala ya Allah ﷻ. Yaani masanamu na miungu mingine ya uongo ambayo wameifanya kama waombezi wao kwa fikra zao tupu bila kuwepo na ushahidi au hoja. Masanamu haya hayana uwezo wa kufanya lolote; hayana akili za kufikiri na wala hawasikii wala kuona. Ni madude tu yasiyokuwa na uhai yakiwa na hali mbaya zaidi ya wanyama.

Kisha Allah ﷻ Anasema, “Sema Ewe Muhammad – waambie watu hawa ambao wameyafanya masanamu waombezi kwa Mola wao, kuwa hakuna uombezi isipokuwa ule ambao Mola Ameuruhusu na Kudhihirisha kuwa pawepo na uombezi. Mambo yote yako Mikononi Mwake Allah ﷻ.

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

“Ni nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya idhini Yake?” (2:255).

لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ni Wake Yeye tu ufalme wa mbingu na ardhi.”

Maana: Ni Yeye Ndiye Anatawala mienendo ya mambo na vitu vyote.

ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

“Kisha mtarejeshwa Kwake.”

Yaani, Siku ya Kiyama, kisha Atatoa hukumu kati yenu kwa uadilifu Wake na Amlipe mazuri au Kumuadhibu kila mtu kulingana na stahiki yake kufuatia mienendo yake hapa duniani. Kisha Anawalaani washirikina zaidi.

وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ

“Na anapotajwa Mwenyezi Mungu Peke Yake...”

Yaani, inapotamkwa kuwa hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Peke Yake.

أَشْمَأَزَّتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ

“...nyoyo za wasioiamini Akhera huchafuka.”

Mujahid alisema, “Nyoyo zao zina chuki. Yaani zimesinyaa kwa vitisho.”¹

Hii ni kama aya,

إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ

“Wao walipokuwa waki ambiwa La ilaha illa ‘Llahu Hapana mola ila Mwenyezi Mungu tu, wakijivuna.” (37:35).

Yaani, walijitutumua kwa maringo na kwa ajili hiyo hawakutaka kuamini. Nyoyo zao hazikutaka kukubali chochote kizuri, na asiye kubali jema atakubali uovu.

Allah تعالى Anasema:

وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ

“Na wanapotajwa wenginewe asiyekuwa Yeye...”

Yaani, masanamu na miungu batili. Ilikuwa rai ya Mujahid,

إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ

“...basi wao hufurahi.”

Yaani, wanajisikia kuwa ni wenye furaha na raha.

¹ At-Tabari 21:301

قُلِ اللَّهُمَّ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ عَلِيمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِي مَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٤١﴾ وَلَوْ أَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لَافْتَدَوْا بِهِ مِنْ سُوءِ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَبَدَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُوا يَحْتَسِبُونَ ﴿٤٢﴾ وَبَدَا لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٤٣﴾

46. Sema: Ewe Mwenyezi Mungu! Muumba mbingu na ardhi! Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana! Wewe Utahukumu baina ya waja wako katika waliyokuwa wakikhitalifiana.

47. Na lau kuwa waliodhulumu wangelikuwa na vyote vilimo duniani na pamoja navyo vingine kama hivyo, bila ya shaka wangeli vitoa kujikomboa katika adhabu mbaya hiyo Siku ya Kiyama. Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu wasiyokuwa wakiya-tarajia.

48. Na utawadhihirikia ubaya wa waliyoyachuma, yatawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

Kuegemezwa Mambo ya Washirikina kwa Allah تعالى

Baada ya kuwalaani washirikina kwa kupenda kwao ushirikina na masanamu na kuchukia Tawhid. Allah تعالى Anasema.

قُلِ اللَّهُمَّ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ عَلِيمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ

“Sema: Ewe Mwenyezi Mungu! Muumba mbingu na ardhi! Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana!”

Yaani, “Muombe Allah تعالى Peke Yake Ambaye Aliumba mbingu na ardhi kwa asili zake. Yaani, Amezifanya kuwa vilivyo bila kuwepo kitu kabla yake ambacho kilikuwa ndicho chanzo au asili yake.”

عَلِيمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ

“Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana!”

أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِي مَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

“Wewe Utahukumu baina ya waja Wako katika waliyokuwa wakikhitalifiana.”

Yaani duniani, “Utahukumu baina yao katika Siku ya Kiama watakapofufuliwa na kutolewa makaburini mwao.” Katika sahihi Muslim kuna riwaya kutoka kwa Abuu Salama bin Abdurrahman amesema, “Nilimuuliza mama Aisha رضي الله عنها jinsi Mtume ﷺ alivyokuwa akianza Sala zake za usiku.” Akasema, “Mtume ﷺ aliposimama kusali usiku, alizoea kusema maneno haya mwanzoni,

«اللَّهُمَّ رَبَّ جِبْرِيلَ وَمِيكَائِيلَ وَإِسْرَافِيلَ، فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ، عَالِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ، أَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ، اهْدِنِي لِمَا اخْتَلَفَ فِيهِ مِنَ الْحَقِّ بِإِذْنِكَ، إِنَّكَ تَهْدِي مَنْ تَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ»

“Ewe Allah, Mola Mlezi wa Jibril, Mikail na Israfil, Muumba mbingu na ardhi, Mjuaji wa ghaibu na ya dhahiri, Utahukumu baina ya waja wako katika yale waliokuwa wanatofautiana. Niongoe katika yale waliyotofautiana, Uniweke katika haki kwa mapenzi Yako. Hakika Wewe Unamuongoa katika haki Umpendaye.”

Fidia Haitakubaliwa Siku ya Kiama

وَلَوْ أَنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا

“Na lau kuwa waliodhulumu...” Yaani, washirikina na makafiri.

مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ

“...vyote viliomo duniani na pamoja navyo vingine kama hivyo,”

لَأَقْتَدُوا بِهِ مِنْ سُوءِ الْعَذَابِ

“...bila ya shaka wangelivitoa kujikomboa katika adhabu mbaya...”

Yaani, ni kuwa Allah تعالى Amepitisha hukumu Yake juu yao Siku ya Kiyama, lakini hakuna fidia itakayokubalika au kutoka kwao, hata kama fidia hiyo ilikuwa

ni dunia iliyojaa dhahabu, kama ilivyotajwa mahali pengine (3:91). Kisha Allah تعالی Anasema:

وَبَدَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مَا لَمْ يَكُونُوا يَحْتَسِبُونَ

“Na yatawadhihirikia kwa Mwenyezi Mungu wasiyokuwa wakiyatarajia.”

Yaani, hapo watakuja kufahamu nini adhabu yao itakuwa kama Alivyowapangia Allah تعالی, jambo ambalo hawajakaa kuliwazia hapo siku za nyuma.

وَبَدَا لَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا

“Na utawadhihirikia ubaya wa waliyoyachuma.”

Yaani, wataadhibiwa kwa amali walizoharamishiwa na madhambi waliyoyatenda duniani.

وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِئْسَ يَسْتَهْزِءُونَ

“...yatawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.”

Yaani, ile adhabu ambayo walikuwa wakiambiwa kuwa ipo itawajia; wao wakaifanyia mzaha na utani sasa itawazingira na kuwameza.

* * *

فَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَاَنَا ثُمَّ إِذَا
 حَوَّلْنَاهُ نِعْمَةً مِنَّا قَالَ إِنَّمَا أُوتِيتُهُ
 عَلَىٰ عِلْمٍ ۗ بَلْ هِيَ فِتْنَةٌ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ
 لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾ قَدْ قَاهَا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
 فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٥٠﴾
 فَأَصَابَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا ۗ
 وَالَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ هَتُولَاءِ سَيُصِيبُهُمْ
 سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٥١﴾
 أَوْلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ
 لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾ قُلْ يَاعِبَادِيَ
 الَّذِينَ اسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا
 مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ
 جَمِيعًا ۗ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٣﴾
 وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ
 مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا
 تُنصَرُونَ ﴿٥٤﴾ وَأَتَّبِعُوا أَحْسَنَ
 مَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ مِنْ رَبِّكُمْ مِنْ قَبْلِ
 أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً
 وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٥٥﴾ أَنْ تَقُولَ
 نَفْسٌ يَنْحَرِقُنِي عَلَىٰ مَا قَرَأْتُ فِي
 جَنْبِ اللَّهِ وَإِنْ كُنْتُ لَمِنَ السَّخِرِينَ ﴿٥٦﴾
 أَوْ تَقُولَ لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي
 لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾ أَوْ تَقُولَ
 حِينَ تَرَىٰ الْعَذَابَ لَوْ أَنَّ لِي كَرَّةٌ
 فَأَكُونَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾ بَلَىٰ قَدْ
 جَاءَتْكَ آيَاتِي فَكَذَّبْتَ بِهَا
 وَاسْتَكْبَرْتَ وَكُنْتَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٥٩﴾

فَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَاَنَا ثُمَّ إِذَا
 حَوَّلْنَاهُ نِعْمَةً مِنَّا قَالَ إِنَّمَا أُوتِيتُهُ
 عَلَىٰ عِلْمٍ ۗ بَلْ هِيَ فِتْنَةٌ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ
 لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾ قَدْ قَاهَا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
 فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٥٠﴾
 فَأَصَابَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا ۗ
 وَالَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ هَتُولَاءِ سَيُصِيبُهُمْ
 سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٥١﴾
 أَوْلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ
 لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٢﴾

49. Na dhara inapomgusa mtu hutuomba. Kisha Tunapompa neema zitokazo Kwetu, husema: Nimepewa haya kwa sababu ya ilimu yangu. Sio! Huo ni mtihani! Lakini wengi wao hawajui!

50. Waliyasema haya wali yokuwa kabla yao, lakini hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.

51. Basi ukawasibu uovu wa waliyoyachuma. Na wale walio dhulumu miongoni mwa hawa utawasibu uovu wa waliyoyachuma vile vile. Nao si wenye kushinda.

52. Kwani wao hawajui kwamba Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye na Akamkadiria? Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanaoamini.

Mtu Anavyobadilika Anapopata Faraja Baada ya Madhara

Allah تعالی Anatuambia jinsi mtu ambaye anakuwa katika shida, basi humuita Allah تعالی na kumuomba; humnyenyekea Mola wake akafanya toba na kuita kwa hali zote ili atoke katika shida hizo; lakini mara Mola wake Anapomuondolea shida hizo na mambo kuwa mepesi kwake na mazuri, huchupa mipaka na kisha hufanya madhambi na maovu mengi.

إِنَّمَا أُوتِيْتُهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ

“Nimepewa haya kwa sababu ya ilimu yangu.”

Yaani, ni kuwa, “Haya nimeyapata kwa sababu Allah تعالی Anajua kuwa nastahiki haya; na kama ingelikuwa Mola wangu hakuniona kuwa ni mtu muhimu Asingelinipa hayo: Qatadah alisema, “Kwa sababu najua kuwa nastahiki haya.”¹ Allah تعالی Anasema,

بَلْ هِيَ فِتْنَةٌ

“Sio! Huo ni mtihani!”

Yaani, ni kuwa, “hivyo sivyo kama anavyosema, bali ni kinyume chake, “Tumempa hivyo vitu ikiwa ni mtihani ili ionekane kama atakuwa mtii au muasi, licha ya kuwa tunayajua hayo toka zamani. Kwa ukweli huo ni mtihani.”

وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

“Lakini wengi wao hawajui!”

Hivyo wanasema yale wayasemayo na kuleta madai yao kama wanavyodai.

قَدْ قَالَهَا الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Waliyasema haya waliokuwa kabla yao.” Yaani, mataifa yaliyotangulia walisema na kudai hayo hayo,

¹ At-Tabari 21:301.

فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٥٩﴾

“...lakini hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.”

Yaani, ni kuwa maneno yao yalikuwa si ya kweli na yote yale waliyoyakusanya (duniani) hayakuwafaa kitu wala kuwaokoa (na adhabu ya Mola wao).

فَأَصَابَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا وَالَّذِينَ ظَلَمُوا مِن هَتُولَاءِ

“Basi ukawasibu uovu wa waliyoyachuma. Na wale waliodhulumu miongoni mwa hawa...”

Yaani, wale watu wanaoelekezewa katika hili.

سَيُصِيبُهُمْ سَيِّئَاتُ مَا كَسَبُوا

“...utawasibu uovu wa waliyoyachuma...”

Kama ilivyowatokea watu waliopita kabla yao.

وَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ

“Nao si wenye kushinda.”

Hii ni kama anavyotuambia Allah تعالى kuhusu Qarun, watu wake walipomuambia,

لَا تَفْرَحْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِينَ ﴿٦٠﴾ وَابْتَغِ فِيمَا آتَاكَ اللَّهُ الدَّارَ الْآخِرَةَ ۗ وَلَا تَنْسَ نَصِيبَكَ مِنَ الدُّنْيَا ۗ وَأَحْسِنَ ۗ كَمَا أَحْسَنَ اللَّهُ إِلَيْكَ ۗ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْأَرْضِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ ﴿٦١﴾ قَالَ إِنَّمَا أُوتِيتُهُ عَلَىٰ عِلْمٍ عِنْدِي ۗ أَوَلَمْ يَعْلَم أَنَّ اللَّهَ قَدْ أَهْلَكَ مِن قَبْلِهِ مِن الْقُرُونِ مَن هُوَ أَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَأَكْثَرُ جَمْعًا ۗ وَلَا يُسْأَلُ عَن ذُنُوبِهِمُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٦٢﴾

“...Usijigambe! Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wanao-jigamba. Na utafute, kwa aliyokupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu Alivyokufanyia wema wewe. Wala

usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi mafisadi. Akasema: Kwa hakika nimepewa haya kwa sababu ya ilimu niliyo nayo. Je! Hakujuu kwamba Mwenyezi Mungu kesha waangamiza, katika vizazi vya walio kabla yake, watu waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye, na wenye makundi makubwa zaidi kuliko yake. Na wakosefu hawataulizwa khabari ya dhambi zao.” (28:76-78)

Na Allah تعالى Amesema,

وَقَالُوا نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَدًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِينَ ﴿٣٥﴾

“Na wakasema: Sisi tuna mali mengi zaidi na watoto, wala sisi hatutaadhibiwa.” (34:35).

أَوَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ

“Kwani wao hawajui kwamba Mwenyezi Mungu Humku njulia riziki Amtakaye na Akamkadiria?”

Yaani, Allah تعالى Anawapa watu wengine (katika riziki Zake) sana, na wengine Anawabania na Kuwapa kidogo.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

“Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao amini.”

Yaani kuna somo na ushahidi.

* قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَرْفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ
الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۗ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٣٦﴾ وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ مِن قَبْلِ أَن
يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ ﴿٣٧﴾ وَأَتَّبِعُوا أَحْسَنَ مَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ مِّن
قَبْلِ أَن يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٣٨﴾ أَن تَقُولَ نَفْسٌ يَنْحَسِرْتَنِي

عَلَىٰ مَا فَرَطْتُ فِي جَنْبِ اللَّهِ وَإِن كُنْتُ لَمِنَ السَّخِرِينَ ﴿٥١﴾ أَوْ تَقُولَ لَوْ أَنَّ اللَّهَ
 هَدَانِي لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٥٢﴾ أَوْ تَقُولَ حِينَ تَرَى الْعَذَابَ لَوْ أَنَّ لِي كَرَّةً
 فَأَكُونَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٣﴾ بَلَىٰ قَدْ جَاءَتْكَ آيَاتِي فَكَذَّبْتَ بِهَا وَاسْتَكْبَرْتَ وَكُنْتَ
 مِنَ الْكٰفِرِينَ ﴿٥٤﴾

53. Sema: Enyi waja Wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.

54. Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na jisalimisheni Kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa.

55. Na fuateni yaliyo bora kabisa katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui.

56. Isije ikasema nafsi: Ee majuto yangu kwa yale niliyapuuza upande wa Mwenyezi Mungu, na hakika nilikuwa miongoni mwa wanaofanya maskhara!

57. Au ikasema: Kama Mwenyezi Mungu angeniongoa, bila ya shaka ningeli kuwa miongoni mwa wenye kumchamungu.

58. Au ikasema inapooni adhabu: Lau kuwa ningelipata fursa nyengine, ningeli kuwa miongoni mwa wafanya mema.

59. Wapi! Bila ya shaka zilikuja Ishara zangu, nawe ukazika-dhibisha, na ukajivuna, na ukawa miongoni mwa makafiri!.

Wito wa Kutubu Kabla Haijafika Adhabu

Aya hii ni kwa wale walio na madhambi; wawe makafiri au la; wanapaswa kutubu na kumuelekea Allah تعالی, Mola wao. Ayah hii inatuambia kuwa Allah تعالی Anasamehe na Atasamehe madhambi ya wote wanaotubu Kwake bila kujali dhambi gani au madhambi kiasi gani hayo hata kama ni wingi wa povu la bahari.

Hapa ijulikane kuwa madhambi hayatasamehewa bila kutubu, kwa sababu Shirki haisameheki ila kwa toba, Mtu aliyefanya Shirki anapaswa kutubu ndipo atasamehewa. Katika Sahihi Al-Bukhari, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa, “Baadhi ya washirikina waliwaua watu wengi, na walizini sana; wakaja kwa Muhammad ﷺ na wakasema, “Maneno yako ni mazuri na wito wako unavutia lakini hebu tuambie nini kitafuta mabaya yetu tuliyoyafanya hapo awali.” Kisha aya zifuatazo zilishushwa,

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا
يَزْنُونَ^٤

“Na wale wasiomuomba mungu mwingine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi aliyoiharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini.” (25:68).

قُلْ يٰۤاَعْبَادِيَ الّٰذِينَ اَسْرَفُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوْا مِنْ رَّحْمَةِ اللّٰهِ^٥

“Sema: Enyi waja Wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu.”

Habari hizi pia zimo ndani ya kitabu cha Muslim, Abu Dawud na An Nasai.¹ Maana ya aya 25:68 ni,

اِلَّا مَنْ تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صٰلِحًا

“Isipokuwa atakayetubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema.” (25:70).

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Amri bin Abbas رضي الله عنه amesema: “Mtu mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ alikuwa ni mtu mzima anayetembea kwa kusaidiwa na bakora yake, akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Hakika nimefanya hiyana sana na uovu mwingi, je, nafasi ya kusamehewa yote hayo kwangu mimi ipo?” Mtume akamjibu: “Kwani wewe si unakiri ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah?” Mtu yule Mzee akasema: “Ndio. Na si hivyo tu, bali ninakiri ya kuwa wewe ni Mtume ﷺ’ Mtume ﷺ

¹ Fat'h Al-Bari 2:411, Muslim 1:113, Abu Dawud 4:166, An-Nasai katika Al-Kubra 446.

akasema: "Hakika Allah تعالى Amekusamehe wewe hiyana zako zote na uovu wako." Hadithi hii ameinukuu Imam Muslim peke yake.

Imam Ahmad aliandika kuwa Asma' bint Yazid رضي الله عنها alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisoma aya,

إِنَّهُ عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ

"Mwendo wake si mwema." (11:46)

Na nikamsikia akisema,

* قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَرْفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ
الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٤٦﴾

"Sema, Enyi waja Wangu mliojifanyia israfu wenyewe! Msikatie tamaa rehema za Allah. Hakika Allah Huwa Anasamehe madhambi yote na wala hajali. Hakika Yeye ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Kurehemu."¹

Habari hizi pia zimeandikwa na Abu Dawud na At Tirmidhi.² Hadithi hizo zote zinaashiria kuwa Allah تعالى Anasamehe madhambi yote. Kwa msingi kuwa huyo mtu anayo nafasi ya kutubu. Zaidi ya hapo mtu asikate tamaa na Rehema za Allah تعالى hata kama madhambi yake ni makubwa au mengi sana, maana mlango wa toba uko wazi na rahma za Allah تعالى ni nyingi bila kifani. Allah تعالى Anasema:

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

"Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anapokea toba ya waja Wake." (9:104).

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٤٧﴾

"Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mwenye Kurehemu." (4:110).

¹ Ahmad 6:454.

² Abu Dawud 4:285, Tuhfat Al-ahwadhi 9:111.

Kuhusu wanafiki, Allah تعالى Anasema:

إِنَّ الْمُنْفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا ﴿٤٩﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا
وَأَصْلَحُوا

“Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni, wala hutompata yeyote wa kuwanusuru. Isipokuwa wale walio tubu, na wakatengeneza...” (4:145-146)

Na Allah تعالى Anasema;

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهُ وَاحِدٌ وَإِن لَّمْ يَنْتَهُوا
عَمَّا يَقُولُونَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٥٠﴾

“Kwa hakika wamekufuru waliosema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna mungu ila Mungu Mmoja. Na ikiwa hawaachi hayo wanayoyasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanaokufuru.” (5:73).

Kisha Anasema,

أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَهُ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥١﴾

“Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwingi wa Kurehemu.” (5:74).

Na Allah تعالى Anaendelea Kusema,

إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا

“Hakika waliowafitini Waumini wanaume na Waumini wanawake, kisha hawakutubu.” (85:10)

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Angalia ukarimu huu na wema, waliwau vipenzi vya Allah wa karibu, lakini Amewataka waje Kwake kutubu ili Awasamehe.” Kuna aya nyingi juu ya maudhui hii.

Katika vitabu vya Sahihi (mbili) amesema Abu Said akitoa kauli ya Mtume ﷺ juu ya mtu aliyewa watu tisini na tisa. Baadaye, alijuta na kumuuliza mfanya ibada mmoja katika Bani Israel kuhusu uwezekano wa yeye kutubu. Alimkatalia, akamuua na yeye, na kukamilisha idadi ya watu mia moja aliowaua. Kisha akamuuliza mwanazuoni wao mmoja kuhusu uwezekano wa yeye kutubu. Akasema, “Kitu gani kinachokuzuia kutubu?” Akamuambia aende katika mji mmoja ambako watu walikuwa wakimuabudu Allah ﷻ. Mtu yule akafunga safari ya kwenda katika mji huo, lakini mauti yalimkuta alipokuwa njiani.

Malaika wa rehema na wa adhabu wakamgombania, Allah ﷻ Akawaamuru Malaika kupima masafa baina ya miji hiyo miwili; na Akawataka wazingatie ukaribu wa yeye na miji hiyo. Wakakuta kuwa alikuwa karibu zaidi na mji aliokuwa akienda, basi Malaika wa rehema wakamchukua. Ilisemekana kuwa alipokuwa akikata roho, alijisogeza mwenyewe (kuuelekea mji huo), na Allah ﷻ Akauamuru mji ule mwema umsogelee karibu, na ule mji mwingine wa watu wabaya usogee mbali.¹

Hiyo ndiyo maana kuu ya Hadithi hiyo; tumeinukuu kwa ukamilifu katika sehemu nyingine.

‘Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa rai juu ya Aya:

قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَفْؤُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا

“Sema: Enyi waja wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote.”

Allah ﷻ Anawaita wote kwenye Msamaha Wake; wale wanaodai kuwa Masihi ni Mungu, wale wanaodai kuwa Masihi ni mwana wa Mungu, wale wanaodai kuwa ‘Uzayr ni mwana wa Mungu, wale wanaodai kuwa Allah ﷻ ni fukara, wale wanaodai kuwa Mkono wa Allah ﷻ Umefungwa, kwa maana ya ubakhili, na wale wanaosema kuwa Allah ﷻ ni mmojawapo katika nafsi ya Utatu. Allah ﷻ Anawaambia wote hao:

¹ Fat’h Al-Bari 5:591.

أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لَهُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٧٤﴾

“Je! Hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.” (5:74).

Na Anamuita kufanya toba mwenye kutamka jambo baya hata zaidi ya hayo, anayesema, ‘Mimi ni Mola wenu Mlezi,’ na Anasema,

مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِّنْ إِلَهٍ غَيْرِي

“Sijui kama mnaye mungu asiyekuwa mimi.” (28:38).

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, alisema, “Mwenye kuwakatisha tamaa waja wa Allah تعالى juu ya Rehema Zake baada ya hapa, amekikana Kitabu cha Allah تعالى, lakini mtu hawezi kutubu isipokuwa mpaka Allah تعالى Ahukumu kuwa anapaswa kutubu.”¹

At-Tabarani ameandika kuwa Shutayri bin Shakal alisema, “Nimemsikia Ibn Mas’ud رضي الله عنه akisema, ‘Aya tukufu zaidi katika Kitabu cha Allah تعالى ni:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ

“Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliyehai, Msimamia mambo yote milele.” (2:255).

Ayah pana katika Qur’an kuhusu heri na shari ni:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani.” (16:90).

Aya katika Qur’an yenye kuleta faraja zaidi ipo katika Surat Az-Zumar:

قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَرْفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ

“Sema: Enyi waja Wangu waliojidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na Rehema ya Mwenyezi Mungu.”

¹ Imenukuliwa na Ibn Jarir na Ibn Al-Mundhir, Angalia *Ad-Dur Al-Manthur* 5:621

Na Aya ya dhahiri zaidi katika Qur'an kuhusu kumtegemea Allah ni:

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۗ

“Na anayemcha Mwenyezi Mungu Humtengezea njia ya kutokea. Na Humruzuku kwa jiha asiyotazamia.” (65:2-3).

Masruq alimuambia; ‘Umesema kweli.’¹

Utajo wa Hadithi Zinazokataza Kukata Tamaa

Imam Ahmad ameandika kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه, alisema, “Nimemsikia Mtume ﷺ, akisema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَوْ أَخْطَأْتُمْ حَتَّى تَمَلَأَ خَطَابَاكُمْ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، ثُمَّ اسْتَفْتَرْتُمْ اللَّهَ تَعَالَى لَعَفَرَ لَكُمْ، وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ! لَوْ لَمْ تُخْطِئُوا لَجَاءَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ بِقَوْمٍ يُخْطِئُونَ، ثُمَّ يَسْتَغْفِرُونَ اللَّهَ فَيَغْفِرُ لَهُمْ»

“Naapa kwa Ambaye Mkononi Mwake ipo nafsi yangu, kama mnetenda madhambi mengi mpaka yakajaza nafasi baina ya mbingu na ardhi, kisha mkaomba msamaha wa Allah, Angeku-sameheni. Naapa kwa Ambaye Mkononi Mwake ipo roho ya Muhammad, kama hamkutenda madhambi, Allah Angewaleta wengine ambao wangetenda madhambi halafu wakaomba msamaha kwa Allah ili Awasamehe.”²

Hadithi hii imenukuliwa na Ahmad peke yake. Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Ayyub Al-Ansari رضي الله عنه, alisema, alipokuwa katika kitanda cha mauti yake, “Nimekuficheni jambo nililolisikia kutoka kwa Mtume ﷺ; akasema:

«لَوْلَا أَنْكُمْ تُذَيِّبُونَ لَخَلَقَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ قَوْمًا يُذَيِّبُونَ، فَيَغْفِرُ لَهُمْ»

“Kama msingekuwa wenye kutenda madhambi, Allah Angewaumba watu ambao wangepanya madhambi ili Awasamehe.”

¹ At-Tabarani 9:142.

² Ahmad 3:238.

Haya yaliandikwa na Imam Ahmad; pia yameandikwa na Muslim katika *Sahih* yake, na At -Tirmidhi.¹

Naye Abu Hatim رحمه الله تعالى amesema: Imesimuliwa kutoka kwa Abdillah bin Umar رضي الله عنهما amesema: Hakika Iblisi - Allah Amlaani - amesema: "Ewe Mola wangu! Hakika mimi Umenifukuza peponi kwa sababu ya Adam. Na Hakika mimi siwezi kukabiliana naye isipokuwa kwa Uwezo Wako." Allah تعالى Akasema: "Wewe juu ya hilo umepewa Uwezo." Iblisi akasema: "Ewe Mola Wangu Mlezi! Niongozee zaidi ya hilo". Allah تعالى Akasema: "Hatozaliwa mtoto isipokuwa mmoja atakuwa mithili yako." Iblisi akasema: "Ewe Mola Wangu Mlezi! Niongozee zaidi ya hilo." Allah تعالى Akasema: "Nitavifanya vifua vya wanadamu kuwa maskani yenu, na mtakuwa mnapita humo kupitia mishipa ya damu." Iblisi akasema: "Ewe Mola Wangu Mlezi niongozee zaidi ya hilo." Allah تعالى Akasema:

وَأَجَلِبْتَ عَلَيْهِمْ بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ وَشَارِكْتَهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ وَعَدْتَهُمْ وَمَا يَعِدُهُمُ

الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦٤﴾

“...na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali na wana, na waahidi. Na Shet’ani hawapi ahadi ila ya udanganyifu.” (17:64)

Adam عليه السلام akasema: "Ewe Mola Wangu Hakika Iblisi Umempa nguvu juu yangu, Na mimi sina kinga nyingine isipokuwa ya Kwako." Allah تعالى Akasema: "Hatozaliwa mtoto katika kizazi chako isipokuwa nitamuekea yeye ambaye atamlinda na waovu." Adam عليه السلام akasema: "Ewe Mola Wangu Mlezi Niongozee zaidi ya hilo." Allah تعالى Akasema: "Jema moja atendalo mwanadamu atalipwa hasanati kumi au zaidi yake, na kama akitenda baya moja, atalipwa hilo hilo, au litafutwa kabisa." Adam عليه السلام akasema: "Ewe Mola wangu Mlezi! Niongozee zaidi ya hilo." Allah تعالى Akasema, "Mlango wa kuleta toba upo wazi, muda wa kuwa roho bado ipo katika kiwiliwili." Adam عليه السلام akasema: "Ewe Mola Wangu Mlezi! Niongozee zaidi ya hilo." Allah تعالى Akasema,

يَعْبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ

جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٦٥﴾

¹ Ahmad 5:414, Muslim 4:2105, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:223.

“...Enyi waja Wangu mliojifanyia israfu wenyewe! Msikatie tamaa na Rehema za Allah . Hakika Allah Huwa Anasamehe madhambi yote na wala hajali. Hakika Yeye ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Kurehemu.”

Muhammad bin Is’haq رضي الله عنه amesema kuwa Umar رضي الله عنه amesema katika mazungumzo yake: “Tulikuwa tukisema: Allah تعالى Hawezi Kuwakubalia waliofitiniwa kwa hali yoyote ile, wala hawana toba, yaani kwa kuwa tayari wameshamjua Allah تعالى, Kisha wamereja tena katika ukafiri kwa sababu tu ya balaa lililowasibu.” Umar akasema: “Haya tulikuwa tukiyasema sisi.” Umar رضي الله عنه akasema, “Mtume ﷺ alipofika Madina, Allah تعالى Aliteremsha aya kuhusu watu waliofitiniwa, na kadhalika Kauli yao:

✽ قُلْ يَبْعَادَى الَّذِينَ اسْتَرْفَوْا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ
الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٤﴾ وَأَنبِئُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ مِن قَبْلِ أَنْ
يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ ﴿٥٥﴾ وَأَتَّبِعُوا أَحْسَنَ مَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ مِّن
قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٥٦﴾

“Sema, Enyi waja Wangu mliochupa mipaka ya kufanya maasi! Msikatie tamaa Rehema za Allah. Hakika Allah Huwa Anasamehe madhambi yote na wala hajali. Hakika Yeye ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Kurehemu. Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na mjisalimishe Kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa. Na fuateni yaliyo bora kabisa katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, kabla hajakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui.” (39:53-55)

Umar رضي الله عنه akasema: Aya hiyo nikaiandika mwenyewe katika mbao. Na nikampelekea Hishaam bin Al-Asi. Hisham akasema, “Iliponijia aya hiyo nilikuwa napanda katika Mlima Tuwa huku nikiisoma kwa sauti bila ya kufahamu maana yake. Mpaka nikasema: “Ewe Allah تعالى hebu nifahamishe undani wake.” Hishaam akasema: “Allah تعالى Akamuezesha kujua ya kuwa aya hiyo imeteremshwa kwa ajili yetu. Katika yale tuliyokuwa tukiyasema sisi wenyewe, na yale waliyokuwa watu wakitusema.” Nikarejea kwa Ngamia

wangu na kukaa juu yake. Kisha nikafunga safari ya kumuendea Mtume ﷺ Madina.¹

Allah تعالیٰ Anawashajiisha waja Wake kuharakisha kutubu, kama Anavyosema:

وَأَيُّبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ

“Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni Kwake,”

Maana yake, kurejea kwa Allah تعالیٰ na kumnyenyekea.

مِن قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ

“...kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa.”

Yaani, harakisheni kutubu na mtende wema kabla ghadhabu hazijakuangukieni.

وَاتَّبِعُوا أَحْسَنَ مَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ مِن رَّبِّكُمْ

“Na fuateni yaliyo bora kabisa katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi,”

Yaani, Qur'an tukufu.

مِنَ الْقَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ

“...kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui.”

Yaani, bila ya nyinyi kuitambua.

أَنْ تَقُولَ نَفْسٌ يَلْحَسِرُنِي عَلَىٰ مَا فَرَطْتُ فِي جَنْبِ اللَّهِ

“Isije ikasema nafsi: Ee majuto yangu kwa yale niliyopoteza upande wa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, katika Siku ya Kiama, mtenda dhambi aliyepuuzia kutubu na kurejea kwa Allah تعالیٰ atajuta, na atatamani angekuwa katika waja wema waliomtii Allah تعالیٰ.

¹ Sira ya Ibn Hishaam 2/472. Isnadi sahihi.

وَإِنْ كُنْتُمْ لَمِنَ السَّخِرِينَ

“...na hakika nilikuwa miongoni mwa wanaofanya maskhara!”

Yaani, ‘vitendo vyangu duniani vilikuwa vya kukejeli na masikhara, si vya mwenye kuimarisha imani na unyoofu.’

أَوْ تَقُولَ لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٥٧﴾ أَوْ تَقُولَ حِينَ تَرَى الْعَذَابَ
لَوْ أَنَّ لِي كَرَّةً فَأَكُونَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٨﴾

“Au ikasema: Ingelikuwa Mwenyezi Mungu ameniongoa, bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa wenye kumchamungu. Au ikasema inapoona adhabu: Lau kuwa ningelipata fursa nyengine, ningelikuwa miongoni mwa wafanya mema.”

Yaani, itatamani nafsi kurejea duniani, ili ifanye amali njema. ‘Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, alisema, “Allah تعالى Anatuambia watakachosema waja Wake kabla hawajasema na watakachofanya kabla hawajafanya. Anasema:

وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ

“Na hapana atakayekupa khabari vilivyo kama Yeye Mwenye khabari.” (35:14).

أَنْ تَقُولَ نَفْسٌ يَحْسَرُنِي عَلَىٰ مَا فَرَّطْتُ فِي جَنْبِ اللَّهِ وَإِنْ كُنْتُ لَمِنَ السَّخِرِينَ ﴿٥٩﴾ أَوْ
تَقُولَ لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٦٠﴾ أَوْ تَقُولَ حِينَ تَرَى الْعَذَابَ
لَوْ أَنَّ لِي كَرَّةً فَأَكُونَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٦١﴾

“Isije ikasema nafsi: Ee majuto yangu kwa yale niliyopoteza upande wa Mwenyezi Mungu, na hakika nilikuwa miongoni mwa wanaofanya maskhara! Au ikasema: Ingelikuwa Mwenyezi Mungu ameniongoa, bila ya shaka ningelikuwa miongoni mwa wenye kumchamungu. Au ikasema inapoona adhabu: Lau kuwa ningelipata fursa nyengine, ningelikuwa miongoni mwa wafanya mema.”¹

¹ At-Tabari 21:316.

Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa, "Mtume ﷺ alisema:

«كُلُّ أَهْلِ النَّارِ يَرَى مَقْعَدَهُ مِنَ الْجَنَّةِ يَقُولُ: لَوْ أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي! فَتَكُونُ عَلَيْهِ حَسْرَةً،
قال: وَكُلُّ أَهْلِ الْجَنَّةِ يَرَى مَقْعَدَهُ مِنَ النَّارِ يَقُولُ: لَوْلَا أَنَّ اللَّهَ هَدَانِي، قال:
فَيَكُونُ لَهُ شُكْرًا»

"Kila mmoja katika watu wa Jahanamu ataoneshwa mahali pake Peponi na atasema, "Kama tu Allah Angeniongoza!" Basi itakuwa sababu ya kujutia kwake. Na kila mtu wa Peponi ataoneshwa mahali pake Jahanamu na atasema, "Kama Allah Asingeniongoa." "Basi hiyo itakua shukrani yake."¹

Pia imesimuliwa na An-Nasa'i.²

Watu wenye madhambi watakapotamani kuwa wangerejeshwa duniani ili waamini Aya za Allah تعالى na kuwafuata Mitume Wake, Allah تعالى Atasema:

بَلَىٰ قَدْ جَاءَ تَاكِتِكُ آيَاتِي فَكَذَّبْتَ بِهَا وَاسْتَكْبَرْتَ وَكُنتَ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٥١﴾

"Wapi! Bila ya shaka zilikuja Ishara Zangu, nawe ukazikadhibisha, na ukajivuna, na ukawa miongoni mwa makafiri!"

Maana yake, 'Enyi mnaojutia matendo yenu, Aya Zangu zilikufikieni duniani, na dalili Zangu zilifikishwa dhidi yenu, lakini mlikanusha na mlikuwa jeuri katika kuzifuata, na mlikuwa miongoni mwa waliokufuru."

* * *

¹ Ahmad 5:512.

² Ahmad na. 10660, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:447

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ تَرَى الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَى اللَّهِ وُجُوهُهُمُ
 مُسْوَدَّةٌ ۗ أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٦٠﴾
 وَيُنَجِّي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّقَوْا بِمَفَازَتِهِمْ لَا يَمَسُّهُمُ السُّوءُ وَلَا
 هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦١﴾ اللَّهُ خَلِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ
 شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿٦٢﴾ لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٦٣﴾
 قُلْ أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَأْمُرُونِي أَعْبُدُ أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦٤﴾ وَلَقَدْ
 أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِن أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ
 عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٥﴾ بَلِ اللَّهُ فَاعْبُدْ وَكُنْ
 مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٦٦﴾ وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ
 جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ
 بِيَمِينِهِ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعٰلَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٦٧﴾

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ تَرَى الَّذِينَ كَذَبُوا
 عَلَى اللَّهِ وُجُوهُهُمُ مُسْوَدَّةٌ ۗ أَلَيْسَ فِي
 جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٦٠﴾
 وَيُنَجِّي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّقَوْا بِمَفَازَتِهِمْ
 لَا يَمَسُّهُمُ السُّوءُ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦١﴾
 اللَّهُ خَلِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ
 عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿٦٢﴾

60. Na Siku ya Kiyama utawaona waliomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimesawijika. Je! Si katika Jahannamu makaazi ya wanaotakabari?

61. Na Mwenyezi Mungu Atawaoka wenye kuji-

kinga kwa ajili ya kufuzu kwao. Hapana uovu utaowagusa, wala hawatahuzunika.

62. Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu, na Yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.

Mwisho wa Waliosema Uongo Dhidi ya Allah تعالیٰ na Waliokuwa na Taqwa

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa katika Siku ya Kiama, baadhi ya nyuso zitakuwa nyeusi na zingine nyeupe. Nyuso za waliofuata makundi na hitilafu zitakuwa nyeusi, na nyuso za Ahlus-Sunnah wal-Jama'ah zitakuwa nyeupe. Allah تعالیٰ Anasema hapa:

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ تَرَى الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَى اللَّهِ

“Na Siku ya Kiyama utawaona waliomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu...”

Maana yake, kwa madai yao kuwa Ana washirika au watoto.

وَجُوهُهُمْ مُسْوَدَّةٌ

"...nyuso zao zimesawijika."

Kwa sababu ya uongo na uzushi wao.

أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ

"Je! Si katika Jahannamu makaazi ya wanaotakabari?"

Yaani, kwani Jahanamu haiwatoshi kama jela na makazi dhalili kwao, kwa sababu ya kiburi chao, ujeuri na kukataa kufuata ukweli

وَيُنَجِّي اللَّهُ الَّذِينَ اتَّقَوْا بِمَفَازَتِهِمْ

"Na Mwenyezi Mungu Atawaokoa wenye kujikinga kwa ajili ya kufuzu kwao."

Yaani, kwa sababu ya hukumu ya Allah تعالى juu yao juu ya furaha na ushindi.

لَا يَمَسُّهُمُ السُّوءُ

"Hapana uovu utaowagusa."

Yaani, katika Siku ya Kiama.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

"...wala hawatahuzunika." Yaani, tishio kubwa (katika Siku hiyo) halitawafanya wajute, kwani watasalimika dhidi ya huzuni zote na kuondolewa mbali na shari, na watapata mema.

اللَّهُ خَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿٦٠﴾ لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ
وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِعَايَةِ اللَّهِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٦١﴾ قُلْ أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَأْمُرُونِي أَعْبُدُ
أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦٢﴾ وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِن أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ
وَلَتَكُونَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٣﴾ بَلِ اللَّهُ فَاعْبُدْ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٦٤﴾

62. Mwenyezi Mungu Ndiye Muumba wa kila kitu, na Yeye Ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.

63. Yeye Anazo funguo za mbingu na ardhi. Na wale waliozikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, hao ndio wenye kupata hasara.

64. Sema: Je! Mnaniamrisha nimuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, enyi wajinga?

65. Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri.

66. Bali muabudu Mwenyezi Mungu tu, na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.

Allah تعالیٰ ni Muumbaji na Mmiliki, na Kumshirikisha Hufuta Amali Njema

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa Yeye ni Muumbaji, Mola Mlezi, Mwenye Mamlaka na Mdhhibiti wa yote; kila kitu kimetiishwa chini ya Mamlaka Yake, Uweza na Ulezi Wake.

لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^١

“Yeye Anazo funguo za mbingu na ardhi.”

Mujahid alisema, “Maqalid” Yaani ‘funguo (nyingi)’ kwa kiajemi. “Hii ilikuwa pia rai ya Qatadah, Ibn Zayd na Sufyan bin ‘Uyaynah.”¹ As-Suddi alisema:

لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^٢

“Yeye anazo funguo za mbingu na ardhi.”

“Hazina za mbingu na ardhi.”² Rai zote mbili zinamaanisha kuwa vitu vyote vinadhhibitiwa na Allah تعالیٰ, kwani mamlaka ni Yake na Anastahiki sifa, na Yeye ni Muweza wa kufanya yote. Anasema:

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:243, At-Tabari 21:321.

² At-Tabari 21:321.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ

“Na wale waliozikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hoja Zake,

أُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ

“...hao ndio wenye khasara.”

قُلْ أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَأْمُرُونَ أَعْبُدُ أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦٨﴾

“Sema: Je! Mnaniamrisha nimuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, enyi majaahili?”

Sababu za kushuka Aya hii imesimuliwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى na wengine kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, kuwa washirikina kwa ujinga wao walimuita Mtume ﷺ kwenye kuabudu miungu yao, halafu nao wangeabudu Mola wake pamoja naye. Basi maneno yafuatayo yakashushwa:

قُلْ أَفَغَيْرَ اللَّهِ تَأْمُرُونَ أَعْبُدُ أَيُّهَا الْجَاهِلُونَ ﴿٦٨﴾ وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكَ
لَإِنْ أَشْرَكَتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٦٩﴾

“Sema: Je! Mnaniamrisha nimuabudu asiye kuwa Mwenyezi Mungu, enyi majaahili? Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Mwenyezi Mungu amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri.”¹

Hii inafanana na Aya:

وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

“Na lau wangelimshirikisha yangeliwaharibikia waliyokuwa wakiyatenda.” (6:88).

¹ Angalia At-Tabari, *Tafsir ya Surat Al-Kafirun*.

بَلِ اللَّهِ فَاعْبُدْ وَكُن مِّنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٦٦﴾

“Bali muabudu Mwenyezi Mungu tu, na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.”

Yaani, ‘wewe na waliokufuata na kukuamini wafanye ibada zao nyooфу kwa ajili ya Allah تعالى Peke Yake, bila ya mwenza au mshirika.’

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِّمِمينِهِ ؕ سُبْحٰنَهُ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٧﴾

67. Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyo stahiki Kadiri Yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa Mkononi Mwake, na mbingu zitakunjwa katika Mkono Wake wa Kuume. Ametakasika na Ametukuka na hayo wanayo mshirikisha nayo.

Washirikina Hawakumheshimu Allah تعالى Anavyostahiki

Allah تعالى Anasema:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

“Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyo stahiki Kadiri Yake.”

Yaani, washirikina hawakumpa Allah تعالى Haki Yake walipoabudu miungu mingine pamoja na Yeye. Yeye ni Mwenye Enzi, na hakuna mwenye nguvu zaidi Yake; Yeye ni Mmoja Mwenye Uwezo wa yote; Yeye ni Mmiliki wa vitu vyote na kila kitu kiko chini ya Udhhibiti na Usimamizi Wake. Mujahid alisema, “Aya hii ilishuka kuwahusu Quraysh.” As-Suddi alisema, “Hawakumtukuza Allah تعالى Alivyostahiki.”¹ Muhammad bin Ka’b alisema, “Kama wangempa Allah تعالى stahiki Yake, wasingeongopa.” Ali bin Abi Talha alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema:

¹ At-Tabari 21:321.

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

“Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyo stahiki Kadiri Yake.”

“Hawa ni makafiri ambao hawakuamini kuwa Allah تعالى ni Muweza juu yao. Anayeamini kuwa Allah تعالى ni Muweza wa yote, amempa Allah تعالى stahiki Yake, na asiyeamini hivyo, hajamheshimu Allah تعالى Anavyostahiki.”¹

Hadithi nyingi zimesimuliwa kuhusu Ayah hii tukufu na namna nzuri ya kuitafsiri aya hii na inayofanana na hii, ni njia waliofuata salafu (wema waliotangulia) Na njia yenyewe ni kuitafsiri kama ilivyo bila ya kupindisha au kubadilisha maana yake.

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

“Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyostahiki Kadiri Yake.”

Al-Bukhari ameandika kuwa ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Mwanazuoni mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ na kumuambia, ‘Ewe Muhammad! Tunajifundisha kuwa Allah تعالى Ataziweka mbingu katika Kidole Kimoja, ardhi katika Kidole Kimoja, miti katika Kidole Kimoja, maji na vumbi katika Kidole Kimoja, na viumbe wengine waliosalia katika Kidole Kimoja, kisha Atasema: ‘Mimi ni Mfalme.’ Mtume ﷺ alileta tabasamu pana mpaka magego yake yakaonekana, katika kuthibitisha maneno ya Mwanazuoni huyo. Kisha Mtume ﷺ alisoma:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyostahiki Kadiri Yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa Mkononi Mwake,”²

Al-Bukhari pia ameandika hayo katika sehemu zingine za *Sahih* yake. Pia yameandikwa na Imam Ahmad, Muslim, At -Tirmidhi na An-Nasa’i katika (vitabu vya) *Tafsir* katika *Sunan* zao.³

¹ At-Tabari 21:321.

² *Fat’h Al-Bari* 8:412.

³ *Fat’h Al-Bari* 13:404, Ahmad 1:429, Muslim 4:2147, *Tuhfat Al-Ahadhi* 9:112-113.

Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema, "Nimemsikia Mtume ﷺ anasema:

«يَقْبِضُ اللَّهُ تَعَالَى الْأَرْضَ، وَيَطْرِي السَّمَاءَ بِيَمِينِهِ، ثُمَّ يَقُولُ: أَنَا الْمَلِكُ، أَيْنَ مُلْكُ الْأَرْضِ؟»

"Allah Ataikamata ardhi Mkononi na Kuzikunja mbingu katika Mkono Wake wa Kulia, kisha Atasema: "Mimi Mfalme, wako wapi wafalme wa ardhini?"¹

Riwaya hii imeandikwa na Al-Bukhari peke yake; Imamu Ahmad amesimulia.²

Al-Bukhari pia ameandika kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما, kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ اللَّهَ تَبَارَكَ وَتَعَالَى يَقْبِضُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ الْأَرْضِينَ عَلَى أُصْبُعٍ، وَتَكُونُ السَّمَوَاتُ بِيَمِينِهِ، ثُمَّ يَقُولُ: أَنَا الْمَلِكُ.»

"Katika Siku ya Kiama, Allah Taala, Ataishika ardhi kwa Kidole Kimoja, na mbingu zitakuwa katika Mkono Wake wa Kulia, kisha Atasema, "Mimi ni Mfalme."³

Riwaya hii pia iliandikwa na Al-Bukhari. Imamu Ahmad amesimulia kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما, alisema, "Siku moja, Mtume ﷺ alisoma Aya ifuatayo huku akiwa juu ya Minbar:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَالسَّمَوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ بِيَمِينِهِ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٧٧﴾

"Na wala hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama Anavyostahiki Kadiri Yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa Mkononi Mwake, na mbingu zitakunjwa katika Mkono Wake wa Kuume. Ametakasika na Ametukuka na hayo wanayomshirikisha nayo."

Mtume ﷺ akasema huku akipitisha mkono wake kwenda mbele na nyuma,

¹ Fat'h Al-Bari 8:413.

² Muslim 4:2148.

³ Fat'h Al-Bari 13:404.

«يُمَجِّدُ الرَّبَّ نَفْسَهُ: أَنَا الْجَبَّارُ، أَنَا الْمُتَكَبِّرُ، أَنَا الْمَلِكُ، أَنَا الْعَزِيزُ، أَنَا الْكَرِيمُ»

“Na Mola Mlezi Anajitukuza Mwenyewe, Anasema “Mimi ni Mshurutishaji, Mimi mi Mwenye Kiburi, Mimi ni Mfalme, Mimi Nina Nguvu Kubwa, Mimi ni Mkarimu sana.”

Na Minbar ilingishika sana mpaka tukahofia kuwa Mtume ﷺ angeanguka.¹
Hii iliandikwa pia na Muslim, An-Nasa’i na Ibn Majah.²

* * *

¹ Ahmad 2:72.

² Muslim 4:2148, An-Nasai katika *Al-Kubra* 4:400, Ibn Majah 2:1429.

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ ۗ ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخْرَىٰ فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ ﴿٦٨﴾ وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِيءَ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٦٩﴾ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٧٠﴾ وَسِيقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا فُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا قَالُوا بَلَىٰ وَلَكِنْ حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَىٰ الْكَافِرِينَ ﴿٧١﴾ قِيلَ ادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ فَبِئْسَ مَثْوَىٰ الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٢﴾ وَسِيقَ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ إِلَىٰ الْجَنَّةِ زُمَرًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلِّمٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَادْخُلُوهَا خَالِدِينَ ﴿٧٣﴾ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي صَدَقَنَا وَعْدَهُ وَأَوْرَثَنَا الْأَرْضَ نَتَّبِعُوهُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَاءُ ۗ فَبِعَمِّ أَجْرِ الْعَمَلِينَ ﴿٧٤﴾ وَتَرَى الْمَلَائِكَةَ حَافِينَ مِنْ حَوْلِ الْعَرْشِ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ ۗ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَقِيلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٥﴾

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ ۗ ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخْرَىٰ فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ ﴿٦٨﴾ وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِيءَ بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٦٩﴾ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٧٠﴾

68. Na litapulizwa baru-gumu, wazimie waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi, isipokuwa aliyemtaka Mwenyezi Mungu. Kisha litapulizwa mara nyengine. Hapo watainuka wawe wana-ngojea.

69. Na ardhi itang'ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi, na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi, na patahukumiwa baina yao kwa

haki, wala hawatadhulumiwa.

70. Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyoyafanya, na Yeye Anayajua sana wanayoyatenda.

Kupulizwa Parapanda, Hukumu na Jazaa

Allah تعالى Anatuambia kuhusu kitisho cha Siku ya Hukumu, pamoja na ishara Zake kubwa na mitikisiko mikubwa,

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ

“Na litapulizwa barugumu, wazimie waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi, isipokuwa aliyemtaka Mwenyezi Mungu.”

Hilo litakuwa pulizo la pili la parapanda, litakalosababisha watu wafe. Kwa mpulizo huo wa parapanda, kila aliye hai mbinguni na juu ya ardhi atakufa, isipokuwa atakayemtaka Allah تعالى. Kama ambavyo limebainishwa kwa uwazi katika Hadithi ya parapanda iliyo mashuhuri. Kisha roho za viumbe waliosalia zitachukuliwa, mpaka wa mwisho kufariki atakuwa Malaika wa Mauti, na Atabakia Mmoja tu Aliye Hai Daima, Ambaye Alikuwepo tangu hapo kabla na Atakuwepo Milele, Atasema mara tatu,

لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ

“Ufalme ni wa nani leo?”

Kisha Atajibu Mwenyewe:

لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ

“Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenza nguvu.” (40:16).

‘Mimi Nimebakia Peke Yangu, Nimekitiisha kila kitu na Nilishatoa hukumu kuwa kila kitu kitafikia ukomo.’ Kisha wa kwanza kufufuliwa atakuwa Malaika Israfil, na Allah تعالى Atamuamuru apulize tena Parapanda. Huu utakuwa mpulizo wa tatu wa parapanda, parapanda la Ufufuo. Allah تعالى Anasema:

ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخْرَىٰ فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ

“Kisha litapulizwa mara nyengine. Hapo watainuka wawe wanangojea.”

Yaani, baada ya wao kuwa mifupa na vumbi, watakuwa hai, wakiangalia vitisho vya Siku ya Kiama. Hii inafanana na Aya:

فَأِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٣﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾

“Kwa hakika hayo ni ukelele mmoja tu, mara watakuwa kwenye ardhi ya mkusanyiko!” (79:13-14)

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَنْظُنُونَ إِن لَّبِثْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾

“Siku atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.” (17:52), na

وَمِنَ آيَاتِنَا أَن تَقُومَ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ بِأَمْرِهِ ۗ ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِّنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٢٥﴾

“Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa Amri Yake. Kisha Atakapokuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi.” (30:25)

Imam Ahmad ameandika kuwa mtu mmoja alimuambia ‘Abdullah bin ‘Amr, رضي الله عنهما, “Unasema kuwa Saa itakuja katika wakati kadha wa kadha.” Akasema, “Nilidhani kuwa sitakusimulia tena. Nilichosema muda mfupi uliopita wakati ungeweza kuona jambo lenye umuhimu mkubwa.” ‘ Abdullah bin ‘Amr, رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«يَخْرُجُ الدَّجَالُ فِي أُمَّتِي فَيَمُكُّ فِيهِمْ أَرْبَعِينَ

“Dajjal atajitokeza katika Ummah wangu na atakuwa kati yao kwa arubaini.”

Sijui kama alisema michana arobaini au miezi arobaini au miaka arobaini au siku arobaini.

«يَبْعَثُ اللَّهُ تَعَالَى عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ، كَأَنَّهُ عُرْوَةٌ بَيْنَ مَسْعُودِ التَّقْفِيِّ، فَيُظْهِرُ فِيهِلِكُهُ اللَّهُ تَعَالَى، ثُمَّ يَلْبُثُ النَّاسُ بَعْدَهُ سِتِينَ سَبْعًا، لَيْسَ بَيْنَ اثْنَيْنِ عِدَاوَةٌ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ تَعَالَى رِيحًا بَارِدَةً مِنْ قِبَلِ الشَّامِ، فَلَا يَبْقَى أَحَدٌ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ مِنْ إِيمَانٍ إِلَّا قَبَضَتْهُ، حَتَّى لَوْ أَنَّ أَحَدَهُمْ كَانَ فِي كَيْدِ جَبَلٍ لَدَخَلَتْ عَلَيْهِ»

"Kisha Allah Atamtuma 'Isa bin Maryam, ambaye anafanana na 'Urwah bin Mas'ud Ath-Thaqafi, na atashinda. Allah Atamua-ngamiza (Dajjal), kisha baada ya hapo, watu wataishi kwa miaka sabini bila ya uadui baina ya mtu yeyote na mwingine. Kisha Allah Atatuma upepo baridi kutokea upande wa Sham, kwa hiyo hatabakia yoyote katika moyo wake kuna uzito wa punje ya dharr ya Imani isipokuwa utamtoa roho; hata kama atakuwa ndani ya kiini cha mlima, utaingia na kumfikia."

Alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ:

«وَيَبْقَى شِرَارُ النَّاسِ فِي خِفَّةِ الطَّيْرِ وَأَخْلَامِ السَّبَاعِ، لَا يَغْرِفُونَ مَعْرُوفًا، وَلَا يُنْكِرُونَ مُنْكَرًا، قَالَ: فَيَمْتَلِئُ لَهُمُ الشَّيْطَانُ فَيَقُولُ: أَلَا تَسْتَجِيبُونَ؟ فَيَأْمُرُهُمْ بِعِبَادَةِ الْأَوْثَانِ فَيَعْبُدُونَهَا، وَهُمْ فِي ذَلِكَ دَارَةٌ أَرْزَاقُهُمْ، حَسَنٌ عَيْشُهُمْ، ثُمَّ يَنْفَخُ فِي الصُّورِ، فَلَا يَسْمَعُهُ أَحَدٌ إِلَّا أَصْعَقَى لَهُ، وَأَوَّلُ مَنْ يَسْمَعُهُ، رَجُلٌ يَلُوطُ حَوْضَهُ فَيَصْعَقُ، ثُمَّ لَا يَبْقَى أَحَدٌ إِلَّا صَعِقَ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ تَعَالَى - أَوْ يُنَزِّلُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ - مَطَرًا كَأَنَّهُ الطَّلُّ - أَوْ الطَّلُّ شَكَّ نَعْمَانَ - فَتَنْبِتُ مِنْهُ أَجْسَادُ النَّاسِ، ثُمَّ يَنْفَخُ فِيهِ أُخْرَى فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ، ثُمَّ يَقَالُ: أَيُّهَا النَّاسُ هَلُمُّوا إِلَى رَبِّكُمْ ﴿وَقَوْمًا مِنْهُمْ﴾ مَسْئُولُونَ ﴿١٤﴾»

"Kutabakia watu waovu wepesi kama ndege na wenye nyoyo ngumu za wanyama wawindaji. Hawatatambua jema lolote au kukataa ovu. Kisha Shetani atawatokea na kuwaambia, "Hamtanitii?" Kisha atawaamuru waabudu masanamu na watayaabudu. Katika wakati huo, watakuwa na mali nyingi na maisha mazuri. Kisha Parapanda litapulizwa, na hakuna atakayelisikia, bali atainamisha kichwa chake kusikiliza. Wa kwanza kulisikia atakuwa mtu ambaye atakuwa anajaza maji kwenye hodhi na atakufa atakapolisikia. Kisha hakutabakia yeyote aliye hai. Kisha Allah Atatuma- au - atateremsha (mvua kama rasharasha) - au - kivuli - An-Nu'man, msimulizi hakuwa na hakika juu ya neno lipi kati ya hayo mawili, "ambapo viwiliwili vya watu vitamea. Kisha Parapanda litapulizwa tena, na watakuwa wamesimama, wakiangalia. Halafu kutasemwa, "Na wasimamisheni kwani wao wataulizwa, (37:24).

Kisha kutasemwa,

«أَخْرِجُوا بَعَثَ النَّارِ، قَالَ: فَيَقَالُ: كَمْ؟ فَيَقَالُ: مِنْ كُلِّ أَلْفٍ تِسْعِمَائَةٍ وَتِسْعَةَ
وَتِسْعِينَ، فَيَوْمَئِذٍ يُبْعَثُ الْوِلْدَانُ شَبَابًا، وَيَوْمَئِذٍ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ»

“Watoeni watu wa motoni, kutasemwa, “Wangapi?” Kutasemwa, “Katika kila elfu moja, mia tisa tisini na tisa.” Katika Siku hiyo, “Watoto watafufuliwa wakiwa na mvi kichwani, na katika Siku hiyo miundi itafunuliwa.”¹

Haya yaliandikwa na Muslim katika *Sahih* yake.²

Al-Bukhari ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا بَيْنَ التَّفَحْتَيْنِ أَرْبَعُونَ»

“Kutakuwa na arobaini, baina ya mipulizo miwili.”

Wakauliza, “Ewe Abu Hurayrah, siku arobaini?” Akawajibu, “Sijui.” Wakauliza, “Miaka arobaini?” Akajibu, “Sijui.” Wakauliza, “Miezi arobaini.” Akajibu, “Sijui.”

«وَيَتَلَى كُلُّ شَيْءٍ مِنَ الْإِنْسَانِ إِلَّا عَجَبَ ذَنْبِهِ فِيهِ يُرْكَبُ الْخَلْقُ»

“Kila kiungo cha mwanadamu kitajitenga na uti wa mgongo wake, isipokuwa mfupa wa kiunoni mwake, na ataumbwa upya kutokana nao.”³

وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا

“Na ardhi itang’ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi,”

Yaani, itang’aa sana katika Siku ya Kiama wakati ambapo Mkweli (Allah تعالى), Atajidhihirisha kwa viumbe Wake, ili Kutoa hukumu.

وَوُضِعَ الْكِتَابُ

“...na Kitabu kitawekwa,”

¹ Ahmad 2:166.

² Muslim 4:2258.

³ *Fat’hul-Bari* 18:414.

Qatadah alisema, "Kitabu cha amali."¹

وَجَاءَ بِالنَّبِيِّنَ

"...na wataletwa Manabii..."

Ibn 'Abbas, رضي الله عنه, alisema, "Watatoa ushahidi dhidi ya mataifa, kwa kuthibitisha kuwa waliwafikishia Ujumbe wa Allah."²

وَالشُّهَدَاءِ

"...na mashahidi." Yaani, mashahidi kutoka miongoni mwa Malaika walioandika amali za wote, heri na shari.

وَقَضَىٰ بَيْنَهُم بِالْحَقِّ

"...na patahukumiwa baina yao kwa haki."

وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

"...wala hawatadhulumiwa." Allah Anasema:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ
مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِمَا حَسِبْتُمْ

"Nasi Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaiteta. Nasi Tunatosha kuwa washika hisabu." (21:47)

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُّضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِن لَّدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا

"Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha na Hutoa kutoka kwake malipo makubwa." (4:40)

Allah تعالى Anasema:

وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ

"Na kila nafsi italipwa kwa yale iliyoyafanya." Maana yake, mema na maovu.

¹ At-Tabari 21:335.

² At-Tabari 21:336.

وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُونَ

“Na Yeye Anajua sana wanayoyatenda.”

وَسِيقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُرَّارًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا فَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا ۗ قَالُوا بَلَىٰ وَلَٰكِن حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَىٰ الْكَافِرِينَ ﴿٦٧﴾ قِيلَ ادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ فَبِئْسَ مَثْوَىٰ لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٦٨﴾

71. Na waliokufuru wataongozwa kuendea Jahannamu kwa makundi. Mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake watawambia: Kwani hawakukujilieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni Aya za Mola wenu Mlezi na Kukuonyeni mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Kwani! Lakini limekwishathibiti neno la adhabu juu ya makafiri.

72. Itasemwa: Ingieni milango ya Jahannamu mdumu humo. Basi nayo ni ubaya ulioje wa makaazi ya wanaotakabari!

Makafiri Wataswagwa Kuelekea Jahanamu

Allah تعالیٰ Anatuambia namna walioangamia watakavyosukumizwa kuingia kwa nguvu Jahanamu, pamoja na vitisho na maonyo. Hii inafanana na Aya:

يَوْمَ يَدْعُوتُ إِلَىٰ نَارِ جَهَنَّمَ دَعَاً ﴿٦٩﴾

“Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu.”
(52:13)

Yaani, watasukumwa na kulazimishwa kuiendea, na watakuwa na kiu kikali sana, kama Anavyosema Allah تعالیٰ:

يَوْمَ يَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَىٰ الرَّحْمَنِ وَفَدًا ﴿٧٠﴾ وَتَسُوقُ الْمُجْرِمِينَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ وِرْدًا ﴿٧١﴾

“Siku Tutayowakusanya wachamungu kuwapeleka kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni Wake. Na Tukawachunga wakhalifu kuwapeleka Jahannamu hali ya kuwa wana kiu.”(19:85-86)

Watakaokuwa katika hali hiyo, watakuwa vipofu, mabubu na viziwi, na baadhi yao wakitembea juu ya nyuso zao:

وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمِيَٰ وَنُكَمَا وَصُمَّا ۖ مَا أُولَٰئِكَ جَهَنَّمَ ۖ كُلَّمَا حَبَتْ
زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا ﴿٧٧﴾

“Na Tutawakusanya Siku ya Kiyama hali wakikokotwa juu ya nyuso zao, nao ni vipofu na mabubu na viziwi. Na makaazi yao ni Jahannamu. Kila moto ukifanya kusinzia Tutazidi kuchochea uwake kwa nguvu.” (17:97).

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهَا فَتَحَتْ أَبْوَابَهَا

“Mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake.”

Yaani, mara tu baada ya wao kufika, milango itafunguliwa upesi, ili kuwaharakishia adhabu yao. Kisha walinzi wa Jahanamu, ambao ni malaika wagumu, wakali na wenye nguvu, watawaambia kwa kuwakaripia:

أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ

“Kwani hawakukujilieni Mitume miongoni mwenu...”

Yaani, ‘wa namna yenu, ili muweze kuzungumza nao na kujifunza kutoka kwao,’

يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُم

“...wakikusomeeni Aya za Mola wenu Mlezi...”

Yaani, ‘kwa kukupeni dalili kuwa kweli walitumwa kuja kwenu,’

وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا

“...na kukuonyeni mkutano wa siku yenu hii?”

Yaani, ‘kukuonyeni juu ya ubaya wa Siku hii.’ Kafiri atawaambia:

بَلَىٰ

“...Kwani!”

Maana yake, ‘walitujia na kutuonya na kutupa dalili na ushuhuda,’

وَلَيْكِن حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَى الْكَافِرِينَ

“Lakini limekwishathibiti neno la adhabu juu ya makafiri.”

Yaani, ‘lakini tuliwapinga na tukawa dhidi yao, kwa sababu tayari tulishaangamia, kama ambavyo ilishahukumiwa iwe, kwa sababu tuliupa mgongo ukweli na kuiendea batili.’ Hii inafanana na Aya:

كُلَّمَا أَلْفَىٰ فِيهَا فَوْجٌ سَأَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿٨﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ
فَكَذَّبْنَا وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ كَبِيرٍ ﴿٩﴾ وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ
أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١٠﴾

“Kila mara likitupwa kundi humo walinzi wake huwauliza: Kwani hakukujieni mwonyaji? Watasema: Kwani! Ametujia mwonyaji, lakini tulimkadhibisha, na tukasema: Mwenyezi Mungu Hakuteremsha chochote. Nyinyi hamumo ila katika upotovu mkubwa! Na watasema: Lau kuwa tungelisikia, au tungelikuwa na akili, tusingelikuwa katika watu wa Motoni!” (67:8-10)

Inayomaanisha, watajuta na kujilaumu wenyewe.

فَاعْتَرَفُوا بِذَنبِهِمْ فَسُحِقًا لِأَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١١﴾

“Wakakiri dhambi zao. Basi kuangamia kumewastahiki!” (67:11)

Yaani, wamepotea na wameangamia. Na Neno Lake Allah تعالى hapa,

قِيلَ ادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا

“Itasemwa: Ingieni milango ya Jahannamu mdumu humo.”

Yaani kila mwenye kuwaona na hali yao waliyomo, atakiri kuwa wanastahiki adhabu hiyo. Maneno hayo hayakunasibishwa na mtu yeyote, bali yamesemwa kama ishara kuwa ulimwengu wote utashuhudia kuwa wanastahiki adhabu hiyo, kwa mujibu wa hukumu ya (Allah تعالى) Muadilifu, Mjuzi wa Yote. Allah تعالى Anasema:

قِيلَ ادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا

"Itasemwa: Ingieni milango ya Jahannamu mdumu humo."

Maana yake, 'kukaa humo milele; hamtaondoka au kupaacha.'

فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ

"Basi nayo ni ubaya ulioje wa makaazi ya wanaotakabari!"

Yaani, 'ni mabaya mno makazi hayo, kwa sababu ya kiburi chenu duniani na kukataa kwenu kufuata ukweli; hayo ndiyo yaliyokusababishieni, ni hali mbaya mno na makazi mabaya zaidi!'

وَسِيقَ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ إِلَى الْجَنَّةِ زُمَرًا حَتَّى إِذَا جَاءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلَامٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَادْخُلُوهَا خَالِدِينَ ﴿٧٣﴾ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي صَدَقَنَا وَعْدَهُ وَأَوْرَثَنَا الْأَرْضَ نَتَّبِعُوهُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَاءُ ﴿٧٤﴾ فَنِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ ﴿٧٥﴾

73. Na waliomcha Mola wao Mlezi wataongozwa kuendea Peponi kwa makundi, mpaka watakapofikilia, nayo milango yake imekwishafunguliwa. Walinzi wake watawaambia: Salaam Alaikum, Amani iwe juu yenu! Mmet'ahirika. Basi ingieni humu mkae milele.

74. Nao watasema: Alhamdulillah, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetutimizia ahadi Yake, na Akaturithisha ardhi, tunakaa katika Bustani popote tupendapo. Basi ni malipo mazuri yaliyoje ya watendao!

Waumini Watapelekwa Peponi

Allah تعالى Anatuambia kuhusu waumini wabarikiwa, ambao watapelekwa Peponi kwa makundi, moja baada ya jingine, kwa kuanza na lililo bora zaidi, walio karibu zaidi na Allah تعالى, kisha Waja wema zaidi, kisha linalofuatia kwa ubora na kuendelea. Kila kundi litakuwa pamoja na wengine kama wao, Mitume pamoja na Mitume, waumini wa kweli pamoja na wenzao, Wafia dini na wenzao, wanazuoni na wenzao, kila kundi likiwa na watu wanaofanana.

حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا

“...mpaka watakapofikilia...”

Yaani, watakapofika katika milango ya Peponi, baada ya kupita juu ya *Sirat*, ambapo watazuiliwa juu ya daraja baina ya Pepo na Jahanamu, na dhuluma zozote zilizokuwepo baina yao duniani zitahukumiwa mpaka wasiwe na dhambi. Kisha wataruhusiwa kuingia Peponi. Na imeandikwa katika Hadithi kuhusu Parapanda ambapo waumini watafika katika milango ya Peponi, watashauriana kuhusu nani wa kuwaombea ruhusa ya kuingia. Watamuuliza Adam عليه السلام, kisha Nuh عليه السلام, kisha Ibrahim عليه السلام, kisha Musa عليه السلام, kisha ‘Isa عليه السلام - Amani iwe juu yao, kisha Muhammad ﷺ. Haya yanafanana na yatakayotokea katika uwanja wa hukumu, watakapomuomba mtu wa kuwaombea shufaa kwa Allah تعالى wakati Atakapohukumu. Haya ni kuonesha nafasi ya Muhammad ﷺ juu ya watu wengine katika hali zote. Katika *Sahih* Muslim, kumesimuliwa kuwa Anas رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«أَنَا أَوَّلُ سَفِيحٍ فِي الْجَنَّةِ»

“Nitakuwa muombezi wa kwanza Peponi.”¹

Kwa mujibu wa tamko la Muslim:

«وَأَنَا أَوَّلُ مَنْ يَفْرَعُ بَابَ الْجَنَّةِ»

“Nitakuwa wa kwanza kugonga mlango wa Peponi.”²

Imam Ahmad ameandika kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«أَتَيْتُ بَابَ الْجَنَّةِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَأَسْتَفْتِحُ فَيَقُولُ الْخَازِنُ: مَنْ أَنْتَ؟ فَأَقُولُ: مُحَمَّدٌ - قَالَ: - فَيَقُولُ: بِكَ أَمْرٌ أَنْ لَا أَفْتَحَ لِأَحَدٍ قَبْلَكَ»

“Nitakuja katika mlango wa Peponi katika Siku ya Kiama na nitaomba kufunguliwa. Mlinzi wa mlangoni atauliza, “Wewe ni nani?” Nitamjibu, “Muhammad.” Atasema, “Niliambiwa habari zako na kwamba nisimfungulie yeyote kabla yako.”³

¹ Muslim 1:188.

² Muslim 1:188.

³ Ahmad 3:136.

Pia yameandikwa na Muslim.¹

Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema, "Mtume ﷺ alisema:

«أَوَّلُ زُمْرَةٍ تَلِجُ الْجَنَّةَ، صُورُهُمْ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ، لَا يَنْصُفُونَ فِيهَا، وَلَا يَمْتَخِطُونَ فِيهَا، وَلَا يَتَغَوَّطُونَ فِيهَا، آتَيْتُهُمْ وَأَمْسَاطُهُمُ الذَّهَبُ وَالْفِضَّةُ، وَمَجَامِرُهُمُ الْأَلْوَةُ وَرَشْحُهُمُ الْمِسْكُ، وَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِنْهُمْ زَوْجَاتٍ، يُرَى مَخُّ سَاقِيهِمَا مِنْ وَرَاءِ اللَّحْمِ مِنَ الْحُسْنِ، لَا اخْتِلَافَ بَيْنَهُمْ وَلَا تَبَاغُضَ، قُلُوبُهُمْ عَلَى قَلْبٍ وَاحِدٍ، يُسَبِّحُونَ اللَّهَ تَعَالَى بِكُرَّةٍ وَعَشِيًّا»

"Kundi la kwanza kuingia Peponi, sura zao ni kama Mwezi katika usiku wa mbalamwezi kamili, humo hawatatema mate wala kupenga kamasi, wala kwenda haja. Vyombo na vitana vyao ni dhahabu na fedha, manukato yao yatakuwa Al-Aluwwah na jasho lao litakuwa miski. Kila mmoja wao atakuwa na wake wawili, Uboho wa mifupa ya miundi utaonekana chini ya ngozi kwa sababu ya uzuri wake. Hakutakuwa na ubishani baina yao na hakutakuwa na chuki; nyoyo zao zitakuwa kama moyo mmoja. Watamtukuza Allah asubuhi na jioni."²

Hayo yameandikwa na Al-Bukhari na Muslim.³

Al-Hafidh Abu Ya'la رحمه الله تعالى ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisema:

«أَوَّلُ زُمْرَةٍ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ، وَالَّذِينَ يَلُونَهُمْ عَلَى صُورِهِ أَشَدُّ كَوَكَبِ دُرِّيٍّ فِي السَّمَاءِ إِصْاءَةً، لَا يَبُولُونَ، وَلَا يَتَغَوَّطُونَ، وَلَا يَتَمَلَّوْنَ، وَلَا يَمْتَخِطُونَ، أَمْسَاطُهُمُ الذَّهَبُ، وَرَشْحُهُمُ الْمِسْكُ، وَمَجَامِرُهُمُ الْأَلْوَةُ، وَأَرْوَاجُهُمُ الْحُورُ الْعَيْنُ، أَخْلَافُهُمْ عَلَى خُلُقِ رَجُلٍ وَاحِدٍ، عَلَى صُورَةِ أَبِيهِمْ آدَمَ، سَيَتُونَ ذِرَاعًا فِي السَّمَاءِ»

¹ Muslim 1:188.

² Ahmad 2:316.

³ Fat'h Al-Bari 6:367, Muslim 4:2180.

“Kundi la kwanza kuingia Peponi litaonekana kama Mwezi katika usiku wa mbalamwezi kamili. Watafuatiwa na kundi ambalo litaonekana kama nyota yenye kung’aa angani. Hawataenda haja kubwa au ndogo au kutema mate au kupenga kamasi. Vitana vyao vitakuwa dhahabu, jasho lao litakuwa miski na manukato yao yatakuwa ya Al-Aluwwah. Wake zao watakuwa Al-Hur Al-‘lyn, na wote watafanana, kama vile ni mtu mmoja katika taswira ya baba yao Adam, urefu wa dhira sitini.”¹

Al-Bukhari na Muslim pia wameinukuu hiyo kutoka katika Hadithi ya Jariri ².رحمَهُ اللهُ تَعَالَى

Imesimuliwa kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مِنْ أُمَّتِي زُمْرَةٌ، هُمْ سَبْعُونَ أَلْفًا، تُضِيءُ وُجُوهُهُمْ إِضَاءَةَ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ»

“Kundi la Ummah wangu, elfu sabini, litaingia Peponi huku nyuso zao ziking’aa kama Mwezi katika usiku wa mbalamwezi kamili.”

‘Ukkashah bin Mihsan رضي الله عنه alisimama na kusema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah ﷺ, mwombe Allah تَعَالَى Anijaalie niwe mmoja wao.’ Akasema,

«اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ مِنْهُمْ»

“Ewe Allah, mjaalie awe mmoja wao.”

Akasimama mtu mmoja katika Ansar, akasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, muombe Allah تَعَالَى Anijaalie niwe mmoja wao.’ Akasema,

«سَبَقَكَ بِهَا عُنَاثُهُ»

“Ukkashah ameshakutangulia.”

Imenukuliwa Hadithi hii na Al-Bukhari na Muslim.³

¹ Musnadi Abu Ya’la 10:470

² Fat’h Al-Bari 4:417, Muslim 4:2179.

³ Fat’h Al-Bari 11:413, Muslim 1:197.

Hadithi hii - inahusu watu elfu sabini watakaoingia Peponi bila ya kuhesabiwa – pia imeandikwa na Al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Jabir bin ‘Abdullah, ‘Imran bin Husayn, Ibn Mas‘ud, Rifa‘ah bin ‘Arabah Al-Juhani na Umm Qays bint Mihsan – رضي الله عنهم - na pia kutoka kwa Abu Hazim kutoka kwa Sahl bin Sa‘d رضي الله عنهم, kwamba, Mtume ﷺ alisema:

«لَيَدْخُلَنَّ الْجَنَّةَ مِنْ أُمَّتِي سَبْعُونَ أَلْفًا - أَوْ سَبْعِمِائَةَ أَلْفٍ - آخِذٌ بَعْضُهُمْ بَعْضًا،
حَتَّى يَدْخُلَ أَوْلَاهُمْ وَأَخْرَجَهُمُ الْجَنَّةَ، وَجُوهُهُمْ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ»

“Watu Eflu sabini au laki saba katika Ummah wangu wataingia Peponi, wakishikana, kiasi kwamba, wa mwanzo na wa mwisho wao wataingia Peponi kwa pamoja, huku nyuso zao zikionekana kama Mwezi katika usiku wa mbala mwezi kamili.”¹

حَتَّى إِذَا جَاءَهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلَامٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَادْخُلُوهَا
خَالِدِينَ

“...mpaka watakapofikilia, nayo milango yake imekwisha funguliwa. Walinzi wake watawaambia: Salaam Alaikum, Amani iwe juu yenu! Mmet’ahirika. Basi ingieni humu mkae milele.”

Hii ni kauli ya kimasharti ambayo haijakamilika. Inaashiria kuwa watakapofika katika milango ya Peponi itafunguliwa kwa ajili yao kama alama ya utukufu, na Malaika walinzi wa milango watawalaki kwa bishara, salamu za amani na sifa. Tofauti na walinzi wa Jahanamu watakaowalaki makafiri kwa makaripio makali, waumini watajaa furaha, kila mmoja kulingana na kiwango chake cha starehe na furaha. Kitakachofuatia baada ya hayo hakijatajwa; imeachiwa fikra ya utashi wa mambo mazuri zaidi na kutimizwa kwa matumaini. Inajulikana kutokana na Hadithi Sahihi kuwa Peponi kuna milango minane.

Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisema:

¹ Fat’h Al-Bari 11:414, Muslim 1:198.

«مَنْ أَنْفَقَ زَوْجَيْنِ مِنْ مَالِهِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ تَعَالَى دُعِيَ مِنْ أَبْوَابِ الْجَنَّةِ، وَلِلْجَنَّةِ أَبْوَابٌ، فَمَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الصَّلَاةِ دُعِيَ مِنْ بَابِ الصَّلَاةِ، وَمَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الصَّدَقَةِ دُعِيَ مِنْ بَابِ الصَّدَقَةِ، وَمَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الْجِهَادِ دُعِيَ مِنْ بَابِ الْجِهَادِ، وَمَنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الصِّيَامِ دُعِيَ مِنْ بَابِ الرِّيَّانِ»

"Mwenye kutoa jozi ya kitu kutoka katika mali yake kwa ajili ya Allah, ataitwa katika milango ya Peponi. Pepo ina milango kadhaa. Mtu ambaye ni miongoni mwa watu wa Sala, ataitwa katika mlango wa Sala; aliye katika watu wa sadaka, ataitwa katika mlango wa Sadaka; aliye miongoni mwa watu wa Jihad, ataitwa katika mlango wa Jihad; aliye miongoni mwa watu wa saumu, ataitwa katika mlango wa Ar-Rayyan."

Abubakr رضي الله عنه aliuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allah, Je, mtu ataitwa kwenye milango hiyo yote?' Mtume ﷺ akasema,

«نَعَمْ، وَأَرْجُو أَنْ تَكُونَ مِنْهُمْ»

"Ndiyo, na ninatumaini kuwa utakuwa mmoja wao."¹

Masimulizi sawa na hayo pia yameandikwa na Al-Bukhari na Muslim.²

Imesimuliwa na Sahl bin Sa'd, رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ ثَمَانِيَةَ أَبْوَابٍ، بَابٌ مِنْهَا يُسَمَّى الرِّيَّانَ، لَا يَدْخُلُهُ إِلَّا الصَّائِمُونَ»

"Hakika Peponi kuna milango minane; mmoja unaitwa Ar-Rayyan, na hakuna atakayeingia hapo isipokuwa waliofunga saumu."³

Imenukuliwa katika *Sahih* Muslim, kuwa 'Umar bin Al-Khattab, رضي الله عنهما, alisema, "Mtume ﷺ alisema:

¹ Ahmad 2:268.

² *Fat'h Al-Bari* 4:133, Muslim 2:711.

³ *Fat'h Al-Bari* 6:378, Muslim 2:808.

«مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ يَتَوَصَّأُ فَيَبْلُغُ - أَوْ فَيَسْئَعُ - الرُّضُوءَ، ثُمَّ يَقُولُ: أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، إِلَّا فُتِحَتْ لَهُ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ الثَّمَانِيَةِ، يَدْخُلُ مِنْ أَيِّهَا شَاءَ»

“Hakuna yeyote miongoni mwenu atakayechukua udhu na kuufanya vyema, au - kikamilifu -, kisha akasema: “Ninashuhudia kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mja Wake na Mjumbe Wake.” ila milango minane ya Peponi itafunguliwa kwa ajili yake na ataingia kupitia mlango wowote atakaotaka.”¹

Upana wa Milango ya Peponi

Tunamuomba Allah تعالى Atujaalie tuwe miongoni mwa watu wa Peponi. Katika Sahihi Mbili, imesimuliwa Hadithi kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, katika Hadith ndefu kuhusu uombezi (ambao Mtume ﷺ alisema):

«قَبَّلَ اللَّهُ تَعَالَى: يَا مُحَمَّدُ، أَدْخِلْ مَنْ لَا حِسَابَ عَلَيْهِ مِنْ أُمَّتِكَ مِنَ الْبَابِ الْأَيْمَنِ، وَهُمْ شُرَكَاءُ النَّاسِ فِي الْأَبْوَابِ الْأُخْرَى، وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ! إِنَّ مَا بَيْنَ الْمِصْرَاعَيْنِ مِنْ مَصَارِيعِ الْجَنَّةِ - مَا بَيْنَ عِضَادَتِي الْبَابِ - لَكُمْ بَيْنَ مَكَّةَ وَهَجَرَ - أَوْ هَجَرَ وَمَكَّةَ - وَفِي رَوَايَةٍ - مَكَّةَ وَبُصْرَى»

“Allah Atasema: “Ewe Muhammad, waachie watu wa Ummah wako ambao hawatahesabiwa, wapite katika mlango wa upande wa kulia, na watahesabika miongoni mwa watakaoingia kupitia milango mingine pia.” “Naapa kwa Ambaye Mkononi Mwake ipo roho ya Muhammad, masafa baina ya nguzo mbili za milango ya Peponi ni kama masafa baina ya Makkah na Hajar - au Hajar na Makkah.”

Katika masimulizi mengine:

مَكَّةَ وَبُصْرَى

“Baina ya Makkah na Busra.”²

¹ Muslim 1:209.

² Fat'h Al-Bari 8:247, Muslim 1:184.

Imeandikwa katika Sahih Muslim kutoka kwa 'Utbah bin Ghazwan رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliwahutubia ambapo aliwaambia kuwa masafa baina ya nguzo mbili za milango ya Peponi ni masafa ya safari ya miaka arobaini, lakini itafika siku itajaa sana watu.¹ Allah تعالى Anasema,

وَقَالَ هُمْ حَزَنَتْهَا سَلَامٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ

"Walinzi wake watawaambia: Salaam Alaikum, Amani iwe juu yenu! Mmetahirika."

Yaani, 'vitendo na kauli zenu zilikuwa njema, jitihada zenu na jaza yenu kadhalika zilikuwa njema.' Mtume ﷺ aliamuru wakati wa mojawapo ya kampeni zake za kijeshi kuwa Waislamu waambiwe kwa sauti kubwa:

«إِنَّ الْجَنَّةَ لَا يَدْخُلُهَا إِلَّا نَفْسٌ مُنْصِلِمَةٌ - وَفِي رِوَايَةٍ - مُؤْمِنَةٌ»

"Hakuna atakayeingia Peponi isipokuwa roho ya Muislamu, au, katika riwaya nyingine, "ya Muumini."²

Allah تعالى Anasema,

فَادْخُلُوهَا خَلِيدِينَ

"Basi ingieni humu mkae milele."

Yaani, kukaa humo, bila kutaka mabadiliko yoyote.

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي صَدَقْنَا وَعَدَهُ.

"Nao watasema: Alhamdulillah, Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetutimizia Ahadi Yake."

Yaani, waumini watakapoona malipo makubwa na fahari, neema na ukarimu mkubwa, watasema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي صَدَقْنَا وَعَدَهُ.

"Alhamdulillah, Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetutimizia Ahadi Yake."

¹ Muslim 4:2278.

² Fat'h Al-Bari 11:385.

Yaani, 'Aliyotuahidi kupitia kwa Mitume Wake waliotulingania hili Duniani.'

رَبَّنَا وَإِنَّا مَا وَعَدْتَنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ وَلَا نَحْزَنُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْمِيعَادَ ﴿١٩٤﴾

"Mola wetu Mlezi! Na Utupe Uliyotuahidi kwa Mitume Wako, wala Usituhuzunisha Siku ya Kiyama. Hakika Wewe Huvunji miadi." (3:194),

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِيَ لَوْلَا أَنْ هَدَانَا اللَّهُ لَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ ﴿١٩٤﴾

"Na watasema: Alhamdulillah! Sifa Njema zote zinampasa Mwenyezi Mungu, Ambaye Aliyetuongoa kufikia haya. Wala hatukuwa wenye kuongoka wenyewe ingelikuwa Mwenyezi Mungu Asingetuongoza. Hakika Mitume wa Mola Wetu Mlezi walileta Haki." (7:43), na

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَذْهَبَ عَنَّا الْحَزْنَ إِنَّ رَبَّنَا لَغَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٣٥﴾ الَّذِي أَحَلَّنَا دَارَ الْمُقَامَةِ مِن فَضْلِهِ لَا يَمَسُّنَا فِيهَا نَصَبٌ وَلَا يَمَسُّنَا فِيهَا لُغُوبٌ ﴿٣٦﴾

"Na watasema: Alhamdulillah, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetuondolea huzuni zote. Hakika Mola Wetu Mlezi bila ya shaka ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Shukrani. Ambaye kwa Fadhila Yake Ametuweka makao ya kukaa daima; humu haitugusi taabu wala humu hakutugusi kuchoka." (35:34-35)

وَأَوْزَنَّا الْأَرْضَ نَتَبَوُّا مِن الْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَاءُ فَنِعْمَ أَجْرُ الْعَمَلِينَ

"...na Akaturithisha ardhi, tunakaa katika Bustani popote tupendapo. Basi ni malipo mazuri yaliyoje ya watendao!"

Abu Al-Aliyah, Abu Salih, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd alisema, "Inamaanisha ardhi ya Peponi."¹

Hii inafanana na Aya:

¹ Al-Qurtubi 15:287.

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿٦٨﴾

“Na hakika Tulikwisha andika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu, ya kwamba Ardhi watairithi waja Wangu walio wema.”
(21:105)

Watasema:

نَتَّبِعُوا مِنْ الْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَاءُ^ط

“...tunakaa katika Bustani popote tupendapo.”

Yaani, ‘popote tunapopataka, ni halali kwetu; malipo yetu bora ni kwa sababu ya amali zetu.’ Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa katika kisa cha Mi’raj kilichosimuliwa na Anas bin Malik رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَدْخِلْتُ الْجَنَّةَ، فَإِذَا فِيهَا جَنَابِدُ اللُّؤْلُؤِ، وَإِذَا تُرَابُهَا الْمِسْكُ»

“Niliruhusiwa kuingia Peponi ambapo niliona makuba yake ya lulu na udongo wa miski.”¹

وَتَرَى الْمَلَائِكَةَ حَافِينَ مِنْ حَوْلِ الْعَرْشِ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ^ط وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْحَقِّ

وَقِيلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٥﴾

75. Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa Kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu, wakimtakasa na kumsifu Mola wao Mlezi. Na patahukumiwa baina yao kwa haki na patasemwa: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote!.

Allah تعالی Anatueleza jinsi Atavyohukumu watu wa Peponi na Jahanamu, na Kumueka kila mmoja wao anapostahili; hii ni Haki Yake na kamwe Hadhulumu. Kisha Anatueleza kuhusu Malaika Wake wanaozunguka Arshi Yake Tukufu, huku wakimtukuza na kumsifu Mola wao Mlezi, na kumtakasa dhidi ya ila au dhuluma yoyote, kwani Amehukumu kwa Uadilifu mkubwa. Anasema:

¹ Fat’h Al-Bari 1:547, Muslim 1:148.

وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ

“Na patahukumiwa baina yao...”

Maana yake, viumbe wote.

بِالْحَقِّ

“...kwa haki...”

Kisha Anasema:

وَقِيلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“ Na kutasemwa Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote!”¹

Maana yake, viumbe wote, wenye uhai na wasio na uhai, watazungumza maneno ya kumsifu Allah تعالى, Mola Mlezi wa vyote, kwa Hekima Yake na Uadilifu Wake. Maneno haya hayanasibishwi na msemaji yeyote mahsusi, ambayo yanaashiria kuwa viumbe wote watashuhudia Sifa Zake.

Qatadah alisema, “Allah تعالى Alianza Uumbaji Wake kwa Sifa, Aliposema,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

“Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyeumba mbingu na ardhi.” (6:1).

Na Alimalizia kwa Sifa, Aliposema:

وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْحَقِّ وَقِيلَ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Na patahukumiwa baina yao kwa haki na patasemwa: Sifa zote Njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote!”

* * *

¹ At - Tabari 21:344.

Tafsiri ya Suratu Ghafir Sura ya 40 Iliteremshwa Makkah

Fadhila za Surah Zenye Kuanza na *Ha Mim*

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, alisema, "Kila kitu kina kiini na kiini cha Qur'an ni sura zenye kuanza na *Ha Mim*." au alisema, "*Hawaamim*"¹ (wingi wa *Ha Mim*). "Mis'ar bin Kidam alisema, "Zilikuwa zikiitwa 'mabibi arusi.² Yote hayo yaliandikwa na Imam, mwanazuoni mkubwa, Abu 'Ubayd Al-Qasim bin Sallam, Allah Amrehemu, katika kitabu chake *Fadha'il Al-Qur'an*.³

Humayd bin Zanjuyah amesimulia kuwa 'Abdullah رضي الله عنه, alisema, "Hakika mfano wa Qur'an ni kama mithili ya mtu anayetoka kwenda kutafuta mahali pa kuishi familia yake, na akafika mahali paliponyeshewa na mvua huku akitembea tembea na kupastaajabia, mara anakuta mashamba mazuri sana. Akasema, 'Nilipendezewa mahali paliponyeshewa na mvua mwanzo lakini hapa ni pazuri mno.' Hivyo akaambiwa, 'Sehemu ya mwanzo ni kama Qur'an, na mashamba haya mazuri ni kama uzuri wa familia ya *Ha Mim* ikilinganishwa na sehemu zilizobakia katika Qur'an.'" Haya yameandikwa na Al-Baghawi.⁴ Ibn Mas'ud رضي الله عنه, alisema, "Ninapofika katika familia ya *Ha Mim*, ni kama kufika kwenye shamba zuri, hivyo sifanyi haraka."⁵



¹ *Ad-Dur Al-Manthur* 7:268

² Al-Qurtubi 15:288

³ *Fadhailul - Qur'an*, Uk. 137,138

⁴ Al-Baghawi 4:90

⁵ Al-Baghawi 4:90

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْغَافِرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمِّ ۝ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ۝ غَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيدِ الْعِقَابِ ذِي الطَّلَوِّ ۝ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ إِلَهُ الْمَصِيرِ ۝ مَا مُجْدِلٌ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَا يَغْرُرَكَ تَقْلُبُهُمْ فِي الْبَلَدِ ۝ كَذَبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَالْأَحْزَابُ مِنْ بَعْدِهِمْ ۝ وَهَمَّتْ كُلُّ أُمَّةٍ بِرُسُولِهِمْ لِيَأْخُذُوهُ ۝ وَجَدَلُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ فَأَخَذْتَهُمْ ۝ فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ۝ وَكَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ۝ الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ۝ رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدْتَهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ ءَابَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ ۝ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝ وَقِهِمُ السَّيِّئَاتِ ۝ وَمَنْ تَقَى السَّيِّئَاتِ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمْتَهُ ۝ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ۝

حَمِّ ۝ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ۝ غَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيدِ الْعِقَابِ ذِي الطَّلَوِّ ۝ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۝ إِلَهُ الْمَصِيرِ ۝

1. H'a, Mim.

2. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.

3. Anayesamehe dhambi na Anayepokea toba, Mkali wa Kuadhibu, Mwenye Ukarimu, hakuna mungu ila Yeye; marejeo ni Kwake.

Tumeshaeleza herufi za mkato mwanzoni mwa Surat Al-Baqarah, na hakuna haja ya kukariri tena hapa.

Katika Hadithi iliyoandikwa na Abu Dawud na At - Tirmidhi kutoka kwa mtu aliyeisikia kutoka kwa Mtume ﷺ, inaeleza:

«إِنْ يَشَأْ اللَّيْلَةَ قُلُوبًا: حَمَّ لَا يُنْصَرُونَ»

“Mnapouingia usiku, soma Ha Mim, La Yunsarun.”¹

Silsila ya wasimuliaji ni Sahih.

تَنْزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

“Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu, Mwenye Kujua.”

Yaani, kitabu hiki - Qur'an - ni kutoka kwa Allah تعالى, Mwenye Nguvu na Elimu, Ambaye Hashindwi na hakuna chenye kufichikana dhidi Yake. Hata sisimizi aliyejificha chini ya matabaka mengi.

غَافِرِ الذَّنْبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ

“Anayesamehe dhambi na Anayepokea toba.”

Yaani, Anasamehe madhambi yaliyofanywa hapo siku za nyuma, na Anapokea toba ya madhambi ambayo huenda yakatendeka hapo baadaye, kutoka kwa mwenye kutubu na kumnyenyekea Yeye.

شَدِيدِ الْعِقَابِ

“Mkali wa kuadhibu.”

Yaani, kwa anayedumu katika kuruka mipaka na kupendelea maisha ya kidunia, ambaye kwa kiburi, huzipa mgongo amri za Allah na anatenda madhambi. Hii inafanana na Aya:

يَتَىٰ عِبَادِيَ أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٥٠﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿٥١﴾

“Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Na kwamba adhabu Yangu ndio adhabu iliyochungu!” (15:49-50).

Sifa hizi mbili (rehema na adhabu) mara nyingi hutajwa kwa pamoja katika Qur'an, ili watu wabakie katika hali zote mbili, matumaini na hofu.

¹ Abu Dawud:74 Tuhfat Al-ahwadhi 8:74.

ذِي الطَّوْلِ^ط

"Mwenye ukarimu."

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, alisema, "Inamaanisha kuwa Yeye ni Mkarimu na Tajiri. (Anayejitegemea)."¹ Yaani, Mkarimu sana kwa waja Wake, kwa Kuwapa neema zizizokwisha ambazo hawataweza kumshukuru kiasi cha kutosha.

وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا^ط

"Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamuwezi kuzidhibiti." (16:18).

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ^ط

"La ilaha illa Huwa."

Yaani, hakuna chenye kulingana na Yeye katika Sifa Zake zote; hakuna Mungu au Mola Mlezi asiyekuwa Yeye.

إِلَيْهِ الْمَصِيرُ

"...marejeo ni Kwake."

Yaani, vitu vyote vitarejea Kwake na Yeye Atamlipa au Kumuadhibu kila mmoja kwa mujibu wa amali zake.

وَهُوَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤١﴾

"...naye ni Mwepesi wa Kuhisabu." (13:41).

مَا يُجَدِّدُ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَا يَغْرُزُكَ تَقْلُبُهُمْ فِي الْبَلَدِ ﴿٤٠﴾ كَذَّبَتْ
 قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَالْأَحْزَابُ مِنْ بَعْدِهِمْ^ط وَهَمَّتْ كُلُّ أُمَّةٍ بِرُسُولِهِمْ لِيَأْخُذُوهُ^ط وَجَدَلُوا
 بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ فَأَخَذْتُهُمْ^ط فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ﴿٤١﴾ وَكَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ
 رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٤٢﴾

¹ At-Tabari 21:351.

4. Hawazibishi Aya za Mwenyezi Mungu ila waliokufuru; basi Kusikudanganye wewe kutangatanga kwao katika nchi.

5. Kabla yao walikadhibisha watu wa Nuhu na makundi mengine baada yao. Na kila taifa lilikuwa na pupa juu ya Mtume wao wamkamate. Na walibishana kwa upotovu ili kuipindua haki. Kwa hivyo niliwakamata. Basi ilikuwaje adhabu Yangu!

6. Namna hivi limewathibitikia makafiri neno la Mola Wako Mlezi ya kwamba wao ni watu wa Motoni.

Sifa Mojawapo ya Makafiri ni Kupinga Aya za Allah تعالى na Matokeo yake

Allah تعالى Anatuambia kuwa hakuna anayekataa ishara Zake baada ya dalili za wazi kufika,

إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا

“...ila waliokufuru.”Yaani, waliokataa ishara za Allah na Dalili Zake na ushahidi.

“Basi kusikughuri wewe kutangatanga kwao katika nchi.”

Yaani, mali zao na maisha ya anasa. Hii inafanana na Aya:

لَا يَغْرُنَكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي الْبَلَدِ ﴿٣١٦﴾ مَتَّعٌ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَيَتَسَاءَلُونَ ﴿٣١٧﴾

“Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa waliokufuru katika nchi. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makaazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia.” (3:196-197)

ثُمَّ تُعْتَبُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضَّضْتَهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24).

Kisha Allah تعالى Anamfariji Mtume Wake Muhammad ﷺ kwa kupingwa na watu wake. Anamuambia kwamba anao mfano kwa Mitume waliokuja kabla yake, rehema na amani za Allah تعالى Ziwapikie wote, kwani umma uliwakataa na kuwapinga, na wachache tu ndio waliowaamini.

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ

“Kabla yao walikadhibisha kaumu ya Nuhu...”

Nuh عليه السلام alikuwa Mtume wa kwanza aliyetumwa na Allah تعالى kwenda kukataza ibada ya sanamu.

وَالْأَحْزَابُ مِنْ بَعْدِهِمْ

“na makundi mengine baada yao.” Yaani, katika kila umma.

وَهَمَّتْ كُلُّ أُمَّةٍ بِرَسُولِهِمْ لِيَأْخُذُوهُ

“Na kila taifa lilikuwa na hamu juu ya Mtume wao wamkamate.”

Yaani, walitaka kumuua kwa vyovyote ilivyowezezana, na baadhi yao kuna walioua Mitume wao.

وَجَدَلُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ

“Na walibishana kwa upotovu ili kuipindua haki.”

Yaani, walikuja na hoja za uongo ili kuupinga ukweli ambao ulikuwa wazi wazi.

فَأَخَذْتَهُمْ

“Kwa hivyo Niliwakamata.”

Yaani, ‘Niliwaangamiza, kwa sababu ya madhambi waliyoyatenda.’

فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ

“Basi ilikuwaje Adhabu Yangu!”

Yaani, mmesikia jinsi Adhabu Yangu na Kisasi Changu kinavyoumiza.’ Qatadah alisema, “Adhabu Anayotoa Allah تعالى ni kali mno.”¹

وَكَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٤٠﴾

“Namna hivi limewathibitikia makafiri neno la Mola wako Mlezi ya kwamba wao ni watu wa Motoni.”

¹ At-Tabari 21:351.

Yaani, 'kama mataifa yaliyotangulia yalivyothibitikiwa na neno la adhabu baada ya kukufuru, basi ndivyo pia litakavyowathibitikia makafiri hawa waliokukataa na wakawa dhidi yako, Ewe Muhammad, na wao linawathibitikia zaidi kwa sababu wamekupinga, hakuna uhakika kuwa wangemuamini Mtume yeyote.' *Allah Aalam.*

الَّذِينَ سَخِمُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِهِمْ
 عَذَابَ الْجَحِيمِ ﴿٧﴾ رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدْتَهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ ءَابَائِهِمْ
 وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٨﴾ وَقِهِمُ السَّيِّئَاتِ وَمَنْ تَقِ السَّيِّئَاتِ
 يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمْتَهُ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٩﴾

7. Wale wanaobeba Arshi, na wanaoizunguka, wana mtukuza na kumsifu Mola wao Mlezi, na wanamu amini, na wanawaombea msamaha walioamini kwa kusema: Mola wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi. Basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia Yako, na waepushe na adhabu ya Jahannamu.

8. Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele Ulizowaahidi. Na Uwape haya pia wale waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao. Hakika Wewe ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

9. Na waepushe na maovu; kwani Umepushaye maovu siku hiyo, hakika Umemrehemu; na huko ndiko kufaulu kukubwa.

Wanaobeba Arshi Wanamsifu Allah na Wanawaombea Msamaha Waumini

Allah تعالی Anatumbea kuwa Malaika walio karibu Naye, wanaobeba Arshi, na Malaika walioizunguka – wote wanamtukuza na kumsifu Mola wao Mlezi. Wanaunganisha utukuzaji 'Tasbih' unaoonesha kuwa Allah تعالی Ametakasika mbali na ila yoyote, pamoja na 'Tahmid' ambayo ni kukiri sifa.

وَيُؤْمِنُونَ بِهِ

“...na wanamuamini.” Yaani, wanamnyenyekea.

وَدَسْتَفِرُّونَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا

“...na wanawaombea msamaha walioamini...”

Yaani, watu wa duniani wanaoamini katika ghaibu. Allah تعالى Aliwaamuru Malaika Wake wa karibu Yake wawaombea waumini wakati hawapo, hivyo ni katika tabia ya Malaika kuitikia *Amin* pindi muumini anapomuomba nduguye wakati hayupo. Katika *Sahih* Muslim inasema:

«إِذَا دَعَا الْمُسْلِمُ لِأَخِيهِ بِظَهْرِ الْغَيْبِ قَالَ الْمَلَكُ: آمِينَ وَلَكَ بِإِخِيهِ»

“Muislamu anapomuomba nduguye bila kuwepo kwake, Malaika huitikia, ‘Amin, nawe mfano wako.”¹

Shahr bin Hawshab alisema, “Malaika wanaobeba Arshi ni wanane; wanne kati yao husema, ‘Utukufu na Sifa Njema ni Zako, Ewe Allah تعالى, Sifa Njema ni Zako kwa Stahmala Yako, kwa Ujuzi Wako.’ Wanne kati yao nao husema, ‘Utukufu na Sifa Njema ni Zako, ewe Allah تعالى, Sifa Njema ni Zako kwa Msamaha baada ya nguvu Zako.’ Wanapowaombea msamaha waumini, husema:

رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا

“Mola wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi.”

Maana yake, ‘Rehema Zako Huyaenea madhambi yao na Ujuzi Wako unazienea haja zao zote, maneno yote na amali zao.’

فَاعْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ

“Basi wasamehe waliotubu na wakaifuata njia yako.”²

Yaani, ‘wasamehe wenye madhambi wanapotubu Kwako na kurejea Kwako na kuacha taratibu zao, kufuata Amri Zako, kwenye mema na kukataza maovu.’

وَقِهِمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ

“...na waepushe na adhabu ya Jahannamu.”

Yaani, ‘waondolee adhabu ya Jahanamu, ambayo ni kali na inaumiza.’

¹ Muslim 4:2094.

² Al-Baghawi 4:93.

رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدْتُهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ^٤

“Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele Ulizo waahidi. Na Uwape haya pia wale waliofanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na dhuriya zao.”

Maana yake, ‘wakutanishe ili wafurahi kwa pamoja katika makazi jirani.’ Hii inafanana na Aya:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ^٥

“Na wale walioamini na wakafuatwa na vizazi vyao na watoto woa katika Imani Tutawakutanisha nao jamaa zao, na wala Hatutawapunja hata kitu kidogo katika vitendo vyao.” (52:21).

Inamaanisha, ‘kwamba wote watawekwa katika daraja la sawa. Kwa namna hii watafurahi kwa pamoja, wa daraja ya juu hatapoteza chochote. Badala yake, Tutaziinua amali za wale wa daraja ya chini walingane sawa, kama Fadhila na Neema kutoka Kwetu.’

Sa’id bin Jubayr alisema kuwa Muumini anapoingia Peponi, atauliza baba yake, mwanaye na kaka yake mahali walipo. Ataambiwa, ‘hawakufikia daraja sawa na yako ya amali njema.’ Atasema, ‘lakini niliyafanya hayo kwa ajili yangu mimi na wao.’ Kisha wataunganishwa nao katika daraja hiyo ya juu. Kisha Sa’id bin Jubayr akasoma Aya hii:

رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدْتُهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ^٤

إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٥﴾

“Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele Ulizowaahidi. Na Uwape haya pia wale waliofanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na dhuriya zao. Hakika Wewe ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”¹

¹ At-Tabari 21:357.

Mutarrif bin 'Abdillah bin Ash-Shikh- khiir alisema, "Walio wanyoofu zaidi katika waja wa Allah تعالى kwa waumini ni Malaika." Kisha akasoma Aya hii:

رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتِ عَدْنِ الَّتِي وَعَدْتَهُمْ

"Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Bustani za Milele ulizo waahidi."

Kisha akasema, "Waja wa Allah waliowasaliti zaidi kwa waumini ni Mashetani."¹

إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

"Hakika Wewe ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima."

Yaani, 'Mmoja Ambaye hakuna wa kumfanyia ukinzani au kumuelemea; Unachokitaka huwa na Usichokitaka hakiwi; Wewe ni Mwingi wa Hekima, katika Hukumu na Amri Zako zote.'

وَقِهِمُ السَّيِّئَاتِ

"Na waepushe na maovu."

Yaani, Matendo na matokeo.

وَمَنْ تَقِ السَّيِّئَاتِ يَوْمَئِذٍ

"...kwani umuepushaye maovu siku hiyo."

Yaani, Siku ya Kiama,

فَقَدْ رَجَمْتَهُ

"...hakika umemrehemu."

Yaani, 'Umemhifadhi na kumnusuru dhidi ya adhabu.'

وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

"...na huko ndiko kufuzu kukubwa."

* * *

¹ Al-Qurtubi 15:295.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنَادُونَ لِمَقْتُ اللَّهِ أَكْبَرُ مِنْ مَقْتِكُمْ
 أَنْفُسَكُمْ إِذْ تُدْعَوْنَ إِلَى الْإِيمَانِ فَتَكْفُرُونَ ﴿١٠﴾
 قَالُوا رَبَّنَا أَمَتْنَا اثْنَتَيْنِ وَأَحْيَيْتَنَا فَاعْتَرَفْنَا بِذُنُوبِنَا
 فَهَلْ إِلَى خُرُوجٍ مِنْ سَبِيلٍ ﴿١١﴾ ذَلِكُمْ بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ
 وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ وَإِنْ يُشْرَكَ بِهِ تُؤْمِنُوا فَالْحُكْمُ لِلَّهِ
 الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ ﴿١٢﴾ هُوَ الَّذِي يُرِيكُمْ آيَاتِهِ وَيُنَزِّلْ لَكُمْ
 مِنَ السَّمَاءِ رِزْقًا وَمَا يَتَذَكَّرُ إِلَّا مَنْ يُنِيبُ ﴿١٣﴾
 فَادْعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿١٤﴾
 رَفِيعَ الدَّرَجَاتِ ذُو الْعَرْشِ يُلْقِي الرُّوحَ مِنْ أَمْرِهِ عَلَى مَنْ
 يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ لِيُنذِرَ يَوْمَ التَّلَاقِ ﴿١٥﴾ يَوْمَ هُمْ بَدْرُونَ
 لَا يَخْفَى عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ لِلَّهِ
 الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٦﴾ الْيَوْمَ نُجْزِي كُلَّ نَفْسٍ بِمَا
 كَسَبَتْ لَا ظُلْمَ الْيَوْمَ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٧﴾
 وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْآزِفَةِ إِذِ الْقُلُوبُ لَدَى الْحَنَاجِرِ كَظِيمِينَ
 مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ ﴿١٨﴾ يَعْلَمُ خَائِنَةَ
 الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفَى الصُّدُورُ ﴿١٩﴾ وَاللَّهُ يَقْضِي بِالْحَقِّ
 وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَقْضُونَ بِشَيْءٍ إِنَّ اللَّهَ هُوَ

السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿٢٠﴾

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنَادُونَ لِمَقْتُ
 اللَّهُ أَكْبَرُ مِنْ مَقْتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ إِذْ
 تُدْعَوْنَ إِلَى الْإِيمَانِ فَتَكْفُرُونَ
 ﴿١٠﴾ قَالُوا رَبَّنَا أَمَتْنَا اثْنَتَيْنِ
 وَأَحْيَيْتَنَا فَاعْتَرَفْنَا بِذُنُوبِنَا
 فَهَلْ إِلَى خُرُوجٍ مِنْ سَبِيلٍ ﴿١١﴾
 ذَلِكُمْ بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ وَحْدَهُ
 كَفَرْتُمْ وَإِنْ يُشْرَكَ بِهِ تُؤْمِنُوا
 فَالْحُكْمُ لِلَّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ ﴿١٢﴾ هُوَ
 الَّذِي يُرِيكُمْ آيَاتِهِ وَيُنَزِّلْ لَكُمْ
 مِنَ السَّمَاءِ رِزْقًا وَمَا يَتَذَكَّرُ إِلَّا
 مَنْ يُنِيبُ ﴿١٣﴾ فَادْعُوا اللَّهَ
 مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ
 الْكَافِرُونَ ﴿١٤﴾

10. Kwa hakika wale walio-
 kufuru watanadiwa: Bila ya
 shaka Kukuchukieni Mwe-
 nyezi Mungu ni kukubwa
 kuliko kujichukia nyinyi
 nafsi zenu, mlipokuwa
 mnaitwa kwenye Imani
 nanyi mkakataa.

11. Watasema: Mola wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili, na Umetuhuisha
 mara mbili! Basi tunakiri madhambi yetu. Basi je, ipo njia ya kutoka?

12. Hayo ni hivyo kwa sababu mlikuwa akiombwa Mwenyezi Mungu Peke Yake mnakataa. Na akishirikishwa mnaamini. Basi hukumu ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mkuu.

13. Yeye Ndiye Anayekuonesheni Ishara Zake, na Anakuteremshieni kutoka mbinguni riziki. Na hapana anayekumbuka ila anayerejea.

14. Basi muombeni Mwenyezi Mungu mkimsafia Dini Yeye tu, na hata kama watachukia makafiri.

Majuto ya Makafiri Baada ya Kuingia Jahanamu

Allah تعالى Anatuambia majuto ya makafiri katika Siku ya Kiama, watakapoingia Jahanamu na kuzama katika kina kirefu cha moto mkali. Watapewa adhabu isiyostahamilika, watazichukia mno nafsi zao kwa sababu ya dhambi zao zilizosababisha waingie Motoni. Wakati huo huo Malaika watawaambia kwa sauti kubwa kuwa walipotangaziwa imani duniani na wakaikataa, Allah تعالى Aliwaghadhibikia zaidi kuliko wao wanavyochukia nafsi zao. Qatadah alisema:

لَمَقَّتْ اللَّهُ أَكْبَرُ مِنْ مَقَّتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ إِذْ تُدْعَوْنَ إِلَى الْإِيمَانِ فَتَكْفُرُونَ

“Bila ya shaka Kukuchukieni Mwenyezi Mungu ni kukubwa kuliko kujichukia nyinyi nafsi zenu, mlipokuwa mnaitwa kwenye Imani nanyi mkakataa.”

Ghadhabu za Allah تعالى kwa wapotevu - wakati walipoletewa Imani duniani, na wao kuipa mgongo na kuikataa - ni kubwa zaidi kuliko kuchukia kwao nafsi zao walipoona adhabu ya Allah تعالى kwa macho yao wenyewe katika Siku ya Kiama.¹ “Hii pia ilikuwa rai ya Al-Hasan Al-Basri, Mujahid, As-Suddi, Dharr bin ‘Ubaydullah Al-Hamdani, ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na Ibn Jarir At -Tabari, Allah تعالى Awarehemu wote.²

قَالُوا رَبَّنَا أَمَتْنَا أَتْنَيْنِ وَأَحْيَيْتَنَا أَتْنَيْنِ

“Watasema: Mola wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili, na umetuhuisha mara mbili!”

¹ At-Tabari 21:359.

² At-Tabari 21:358, 359.

Ath-Thawri رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Abu Ishaq kutoka kwa Abu Al-Ahwas kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه: "Aya hii ni kama Aya:

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَاتًا فَأَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمَيِّتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٨﴾

"Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu na hali mlikuwa wafu Akakufufueni! Kisha Atakufisheni, tena Atakufufueni, kisha Kwake mtarejeshwa?" (2:28)¹

Hii ilikuwa pia rai ya Ibn 'Abbas, Adh-Dhahhak, Qatadah na Abu Malik.² Hii bila ya shaka ndio rai sahihi. Kilichoelezwa na yote hayo ni kwamba, watakaposimama mbele ya Allah katika uwanja wa Kiama, makafiri wataomba kurejea, kama Allah تعالى Anavyosema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿٣٢﴾

"Na ungelikiwaona waovu wanavyoinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, (wakisema): Mola wetu Mlezi! Tumashaona, na Tumeshasikia. Turejeshe tukatende mema, kwani hakika sisi tumekwisha kuwa na yakini sasa." (32:12),

Hata hivyo, hawatajibiwa. Kisha watakapoona Moto na wao kuinuliwa juu yake na kuona adhabu za humo, wataomba kurejea duniani kwa msisitizo wa hali ya juu, lakini hawatajibiwa. Allah تعالى Anasema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ وَقُفُوا عَلَى النَّارِ فَمَا لَوْ يَلَيْتُنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِعَايَتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٧﴾ بَلْ بَدَأَ هُمْ مَّا كَانُوا يُخْفُونَ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٣٨﴾

¹ At-Tabari 21:360.

² At-Tabari 21:360.

“Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini. Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeyarejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo.” (6:27-28).

Watakapoingia Jahanamu na kuonja joto lake, marungu yenye ndoana na minyororo, ombi lao la kurejea litakuwa kubwa zaidi.

وَهُمْ يَصْطَرِحُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۖ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَن تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن نَّصِيرٍ ﴿٣٧﴾

“Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyokuwa tukiyafanya. Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani waliodhulumu hawana wa kuwanusuru.” (35:37)

رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِن عُدْنَا فَإِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٠٧﴾ قَالَ آخِضُوا فِيهَا وَلَا تُكَلِّمُونِ ﴿١٠٨﴾

“Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi tutakuwa madhalimu. Atasema Mwenyezi Mungu: Tokomeeni humo, wala msinisemeze.” (23:107-108).

Kwa mujibu wa Aya hii, watazungumza kwa upole zaidi, na watatangeliza ombi lao kwa maneno:

رَبَّنَا أُمَّتَنَا أَتْنَتَيْنِ وَأَحْيَيْتَنَا أَتْنَتَيْنِ

“Mola wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili, na Umetuhuisha mara mbili!”

Yaani, kwa Nguvu Zako Tukufu, Umetuhuisha baada ya mauti yetu, kisha Ukatufisha baada ya kuwa hai; Una Uweza wa kufanya chochote Utakacho. Tunakiri madhambi yetu na na tunakubali kuwa tulizidhulumu nafsi zetu duniani,

فَهَلْ إِلَىٰ خُرُوجٍ مِّن سَبِيلٍ

“Basi je, ipo njia ya kutoka?”

Yaani, ‘je, utatuitikia maombi yetu ya kurejea duniani, kwani Wewe unaweza hayo, ili tufanye amali tofauti na tuliyokuwa tukiyafanya. Halafu kama tutarudia mienendo yetu, ya zamani, hakika tutakuwa madhalimu.’ Jibu litakuwa: ‘Hakuna namna ya kurudi duniani.’ Kisha sababu ya hilo itatajwa: ‘Tabia yenu haikukubali ukweli na kuongozwa nayo, mkaukataa na kuuacha.’

Allah تعالى Anasema:

ذَٰلِكُمْ بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ ۖ وَإِنْ يُشْرَكَ بِهِ تُؤْمِنُونَ

“Hayo ni hivyo kwa sababu mlikuwa akiombwa Mwenyezi Mungu Peke Yake mnakataa. Na akishirikishwa mnaamini.”

Yaani, ‘kama mtarudi, hivi ndivyo ambavyo mngekuwa.’ Hii inafanana na Aya:

وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوْا لِمَا نَجَّوْا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

“Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeparejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo.” (6:28).

فَآخِذْكُمْ بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيْرِ

“Basi hukumu ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Mkuu.”

Yaani, Yeye ni Hakimu wa viumbe Wake, Mwadilifu kuliko WoteAmbaye kamwe Hadhulumu. Humuongoa yeyote Amtakaye na kumuacha apotee yeyote Amtakaye; Anamrehemu yeyote Amtakaye na Anamwadhibu yeyote Amtakaye; hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye.

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمْ ءَايَاتِهِ

“Yeye Ndiye Anayekuonesheni Ishara Zake.”

Yaani, Hudhihirisha Uweza Wake kwa waja Wake kupitia miujiza Mikubwa inayofahamisha juu ya ukamilifu wa Uumbaji Wake, na kwamba Yeye Ndiye Mwazilishi katika Kuumba.

وَيُنزِّلُ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ رِزْقًا

“...na Anakuteremshieni kutoka mbinguni riziki.”

Hii inakusudia mvua, ambayo huleta mazao na matunda, ambayo kwa rangi zake mbalimbali, ladha, harufu, umbo na dalili za Muumbaji. Ni aina mojawapo ya maji, lakini kwa uwezo Wake mkubwa, Yeye hutofautisha vitu hivyo.

وَمَا يَتَذَكَّرُ

“Na hapana anayekumbuka ila anayerejea.”

Yaani, hakuna anayejifundisha somo au kukumbushwa na vitu hivyo, au anavichukulia kama dalili ya Muumbaji Mwenye Nguvu,

إِلَّا مَنْ يُنِيبُ

“...ila anaye rejea.”

Yaani, wenye uoni na kurejea kwa Allah تعالى.

Waumini Wanaamrisha Kumuabudu Allah تعالى Peke Yake Bila ya Kujali Mazingira.

Allah تعالى Anasema:

فَادْعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿١٠٦﴾

“Basi muombeni Mwenyezi Mungu mkimsafia Dini Yeye tu, na hata kama watachukia makafiri.”

Inamaanisha, kumuabudu na kumuomba Allah تعالى Peke Yake kwa unyoofu wote. Msiwe kama washirikina kitabia na kiimani. Imam Ahmad ameandika kuwa mwishoni mwa kila Sala, ‘Abdullah bin Az-Zubayr رضي الله عنه alikuwa akisema: “Hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah Peke Yake bila mshirika, Ufalme ni Wake na Sifa Njema ni Zake, Naye ni Mweza wa yote; Hakuna hila wala ujanja isipokuwa kwa utashi wa Allah; hakuna Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hatumuabudu yeyote isipokuwa Yeye; Yeye ni Mwenye Neema, Fadhila na Sifa Njema; hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah, tunamuabudu kwa unyoofu hata kama makafiri wanachukia hilo.”

Alisema, "Mtume ﷻ alikuwa akisoma *Tahliil* baada ya kila Sala."¹ Riwaya kama hiyo pia iliandikwa na Muslim, Abu Dawud na An-Nasa'i.²

Imesimuliwa katika *Sahih* kutoka kwa Ibn Az-Zubayr رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷻ alikuwa akisema yafuatayo baada ya Sala za faradhi:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَلَا نَعْبُدُ إِلَّا إِيَّاهُ، لَهُ النِّعْمَةُ وَلَهُ الْفَضْلُ وَلَهُ الثَّنَاءُ الْحَسَنُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ،

*"Hakuna mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah Peke Yake bila ya mshirika, ni Yake Mamlaka na Sifa Njema, kwani Yeye ni Muweza wa Kufanya kila kitu; hakuna hila wala ujanja isipokuwa kwa Utashi Wake; hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na hatumuabudu yeyote isipokuwa Yeye; hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah, tunamuabudu Yeye kwa unyoofu wote, hata kama makafiri wanachukia hilo."*³

رَفِيعُ الدَّرَجَاتِ ذُو الْعَرْشِ يُلْقِي الرُّوحَ مِنْ أَمْرِهِ عَلَى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ لِيُنذِرَ يَوْمَ التَّلَاقِ ﴿١٠٠﴾ يَوْمَ هُمْ بَارِزُونَ لَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ ﴿١٠١﴾ لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ ۗ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٠٢﴾ الْيَوْمَ يُجْزَىٰ كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ ۗ لَا ظُلْمَ الْيَوْمَ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٠٣﴾

15. Yeye Ndiye Mwenye vyeo vya juu, Mwenye A'rshi. Hupeleka Wahyi kwa Amri Yake juu ya Amtakaye katika waja Wake, ili kuonya kwa Siku ya kukutana (na Mola wao).

16. Siku watakadhihiriri wao. Hapana kitachofichikana chochote chao kwa Mwenyezi Mungu. Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenza Nguvu.

¹ Ahmad 4:4.

² Muslim 1:416, Abu Dawud 2 173, An-Nasai 3:78, 79

³ Muslim 1:415

17. Leo kila nafsi italipwa kwa iliyochuma. Hapana dhulma leo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.

Wahyi wa Allah تعالى kwa Kuwaonya Waja Wake Siku ya Kukutana Naye

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Utukufu Wake na Kiburi Chake na Arshi Tukufu Yake kuwa ipo juu ya viumbe wote kama paa.

مِنَ اللَّهِ ذِي الْمَعَارِجِ ﴿٦٧﴾ تَعْرُجُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ إِلَيْهِ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ
خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ ﴿٦٨﴾

“Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye mbingu za daraja. Malaika na Roho hupanda kwenda Kwake katika siku ambayo muda wake ni miaka khamsini elfu!” (70:3-4).

Allah تعالى Akipenda, tutaeleza hapa chini rai sahihi zaidi kuhusu masafa baina ya Arshi na ardhi ya saba kwa mujibu wa wanazuoni wengi wa zamani na wa sasa. Wengi walisema kuwa Arshi imejengwa kwa madini ya rubi nyekundu. Upana baina ya nguzo mbili ni masafa ya mwendo wa miaka elfu hamsini na kimo chake juu ya ardhi saba ni sawa na safari ya miaka elfu hamsini.

يُلْقَى الرُّوحَ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ

“Hupeleka wahyi kwa Amri Yake juu ya amtakaye katika waja wake,”

Hii inafanana na Aya:

يُنزِلُ الْمَلَائِكَةَ بِالرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ أَنْ أَنْذِرُوا أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا
فَاتَّقُونِ ﴿٦٩﴾

“Huwateremsha Malaika na Wahyi kwa Amri Yake juu ya amtakaye katika waja Wake ili nyinyi muonye kwamba hapana mungu ila Mimi, basi nicheni Mimi.” (16:2), na,

وَإِنَّهُمْ لَتُنزِلُونَ رَبَّ الْعَالَمِينَ ﴿٧٠﴾ نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿٧١﴾ عَلَىٰ قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ
الْمُنذِرِينَ ﴿٧٢﴾

“Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameuteremsha Roho muaminifu, Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji.” (26:192-194)

Allah تعالیٰ Anasema:

لِيُنذِرَ يَوْمَ التَّلَاقِ

“...ili kuonya kwa Siku ya Mkutano.”

‘Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Siku ya kukutana ni mojawapo ya majina ya Siku ya Kiama, ambalo Allah تعالیٰ Anawaonya waja Wake.”¹ Hiyo ni siku ambayo kila mmoja atajua amali zake, njema na mbaya.

يَوْمَ هُمْ بَارِزُونَ لَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ

“Siku watakayodhihiri wao. Hapana kitachofichikana chochote chao kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, wote watakuwepo katika mahali pa wazi, bila ya stara wala kivuli, wala kifuniko juu yao. Allah تعالیٰ Anasema:

يَوْمَ هُمْ بَارِزُونَ لَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ

“Siku watakayodhihiri wao. Hapana kitachofichikana chochote chao kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake, kila kitu kitajulikana Kwake.

لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ

“Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenda nguvu. ”

Tumeshataja Hadithi ya Ibn ‘Umar رضي الله عنهما, kuwa Allah تعالیٰ Atazikunja mbingu na ardhi Mkononi Mwake na Atasema,

¹ At-Tabari 21:364.

«أَنَا الْمَلِكُ، أَنَا الْجَبَّارُ، أَنَا الْمُتَكَبِّرُ، أَيْنَ مُلْكُ الْأَرْضِ؟ أَيْنَ الْجَبَّارُونَ؟ أَيْنَ الْمُتَكَبِّرُونَ؟»

“Mimi ni Mfalme, Mimi ni Jabbari, Mimi ni Mwenye Kiburi, wako wapi wafalme wa ardhini? Wako wapi majabbari? Wako wapi wenye kiburi.”¹

Katika Hadithi kuhusu Parapanda, inasema kuwa Allah تعالى Atatoa roho za viumbe Wake wote, hatabakia yeyote isipokuwa Yeye Peke Yake, bila ya mshirika. Kisha Atasema, “Ufalme ni wa nani leo?” mara tatu, na baada ya hapo, Allah تعالى Atajijibu Mwenyewe kwa Kusema,

لِلَّهِ الْوَحْدِ الْقَهَّارِ

“Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenda Nguvu.”²

Yaani, Yeye ni Mmoja wa Pekee Aliyevitiisha vitu vyote.

الْيَوْمَ تُجْزَى كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ لَا ظُلْمَ الْيَوْمَ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٧٠﴾

“Leo kila nafsi italipwa kwa iliyochuma. Hapana dhulma leo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.”

Allah تعالى Anatuambia kuhusu Uadilifu Wake Anapohukumu baina ya viumbe Wake; Hadhulumu hata kiasi cha chembe ya uzito wa vumbi, wema au uovu. Kwa kila jema moja, Analipa mara kumi, kwa kila ovu moja Anaadhibu mara moja tu. Allah تعالى Anasema:

لَا ظُلْمَ الْيَوْمَ

“Hapana dhulma leo.” Imesimuliwa katika Sahih Muslim kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alisema kuwa Allah تعالى Alisema:

«يَا عِبَادِي إِنِّي حَرَمْتُ الظَّلْمَ عَلَى نَفْسِي وَجَعَلْتُهُ بَيْنَكُمْ مُحَرَّمًا فَلَا تَظَالَمُوا - إِلَى أَنْ قَالَ - يَا عِبَادِي إِنَّمَا هِيَ أَعْمَالُكُمْ أَحْصَيْهَا عَلَيْكُمْ ثُمَّ أَوْفَيْكُمْ بِهَا، فَمَنْ وَجَدَ خَيْرًا فَلْيُحْمَدِ اللَّهَ تَبَارَكَ وَتَعَالَى، وَمَنْ وَجَدَ غَيْرَ ذَلِكَ فَلَا يُلُومَنَّ إِلَّا نَفْسَهُ»

¹ 70:51, At-Tabari 21:327.

² At-Tabari katika At-Tiwal uk. 270.

“Enyi Waja Wangu, Mimi Nimeharamisha dhuluma katika Nafsi Yangu, na Nimeifanya baina yenu yenye kuharamishwa, basi msidhulumiane.’ hadi aliposema: “Enyi Waja Wangu, hizi ni amali zenu, Nimekuhifadhieni, kisha Nitakulipeni kwa amali hizo. Mwenye kupata heri, amsifu Allah, na mwenye kupata tofauti na hilo, ajilaumu nafsi yake mwenyewe.”¹

إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.” Yaani, Atawahesabu viumbe Wake wote kama Anavyomhesabu mtu mmoja. Hii inafanana na Aya:

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا نَبْعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ^٤

“Hakukuwa Kuumbwa kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu.” (31:28).

وَمَا أُمْرًا إِلَّا وَاحِدَةً كَلَّمَجٍ بِالْبَصْرِ ﴿٥٠﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50)

وَأَنْذَرْتَهُمْ يَوْمَ الْأَرْزَاقِ إِذْ أَتَقْلُوبُ لَدَى الْحَنَاجِرِ كَظَمِينَ^٥ مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ ﴿٥١﴾ يَعْلَمُ خَائِنَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفَى الصُّدُورُ ﴿٥٢﴾ وَاللَّهُ يَقْضِي بِالْحَقِّ^٦ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَقْضُونَ بِشَيْءٍ^٧ إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿٥٣﴾

18. Na waonye siku inayokurubia, wakati nyoyo zitakapofika kooni, nao wamejaa huzuni. Madhaalimu hawatakuwa na rafiki, wala muombezi wa kuitikiwa.

19. (Mwenyezi Mungu) Anajua khiyana ya macho na yanayoficha vifua.

20. Na Mwenyezi Mungu Huhukumu kwa haki; lakini hao wanaowaomba badala yake hawahukumu chochote. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.

¹ Muslim 4:1994.

Onyo la Siku ya Kiama na Hukumu ya Allah تعالى katika Siku Hiyo

'Siku inayokaribia' ni mojawapo ya jina la Siku ya Qiyama. Inaitwa hivyo kwa sababu imekaribia, kama Allah تعالى Anavyosema:

أَزِفَتِ الْآزِفَةُ ﴿٥٣﴾ لَيْسَ لَهَا مِنْ دُونِ اللَّهِ كَاشِفَةٌ ﴿٥٤﴾

"Kiyama kimekaribia! Hapana wa kukifichua isipo kuwa Mwenyezi Mungu." (53:57-58)

أَقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿٥٤﴾

"Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!" (54:1)

أَقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ

"Imekaribia watu hisabu yao." (21:1),

أَتَىٰ أَمْرُ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ ۗ

"Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize." (16:1),

فَلَمَّا رَأَوْهُ زُلْفَةً سَيِّئَتْ وُجُوهُ الَّذِينَ كَفَرُوا

"Lakini watakapoiona karibu, nyuso za waliokufuru zitahu zunishwa." (67:27), na

إِذِ الْقُلُوبُ لَدَى الْحَنَاجِرِ كَظِيمٍ ۗ

"...wakati nyoyo zitakapofika kooni, nao wamejaa huzuni."

Qatadah alisema, "Roho zitakapofika kooni kwa sababu ya hofu, na hazitatoka wala kurudi zilikutoka."¹ Hii ilikuwa pia rai ya 'Ikrimah, As-Suddi na wengine.

كَظِيمٍ ۗ

"...nao wamejaa huzuni."

Yaani wako kimya, kwani hakuna atakayeongea bila ya ruhusa Yake:

¹ At-Tabari 21:368.

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أُذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

“Siku atakaposimama Roho na Malaika kwa safu. Hawatasema ila Mwingi wa Rehema Aliyemruhusu, na atasema yaliyosawa tu.” (78:38).

Ibn Jurayj alisema:

كَظِيمِينَ

“...nao wamejaa huzuni.” “Inamaanisha kulia.”¹

مَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ

“Madhaalimu hawatakuwa na rafiki, wala muombezi wa kuitikiwa.”

Waliodhulumu nafsi zao kwa kumshirikisha Allah تعالى, hawatakuwa na jamaa wa kuwasaidia na wala muombezi atakayewaombea; hawatakuwa na heri yoyote.

يَعْلَمُ خَائِبَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ ﴿٣٩﴾

“(Mwenyezi Mungu) Anajua khiyana ya macho na yanayoficha vifua.”

Allah تعالى Anatuambia kuhusu Elimu Yake kamili Yenye Kuvienea vitu vyote, vikubwa na vidogo, ili watu wajue kuwa Anawajua na watakuwa na hisia sahihi ya aibu mbele ya Allah تعالى. Watazingatia ukweli kuwa Anawaona, kwani Yeye Anajua hila za macho, hata kama macho yanaonesha kutokuwa na hatia, na Anajua kilicho jificha nyoyoni, miongoni mwa siri na dhamira. Adh-Dhahhak alisema:

خَائِبَةَ الْأَعْيُنِ

“...Anajua khiyana ya macho...” “Mpepeso wa jicho na mtu kudai ameona kitu ilhali hakuona, au kuwa hajaona huku ameona.”² Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Allah تعالى Anajua pindi jicho linapoangalia, kama linataka kufanya usaliti ama la.”³ Hii ilikuwa pia rai ya Mujahid na Qatadah.⁴ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, alitoa rai juu ya Aya:

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:281.

² Al-Qurtubi 15:303.

³ At-Tabari 21:369.

⁴ At-Tabari 21:370.

“Anajua, kama ulikusudia zinaa na mwanamke ama laa.”¹ As-Suddi alisema:

وَمَا تُخْفَى الصُّدُورُ

“...na yanayoficha vifua.”

Yaani, minong’ono inayojipenyeza ya wasiwasi.

وَاللَّهُ يَقْضِي بِالْحَقِّ

“Na Mwenyezi Mungu Huhukumu kwa haki.”

Yaani, Anahukumu kwa haki. Al-A’ mash amesimulia kutoka kwa Sa’id bin Jubayr kutoka kwa Ibn ‘Abbas, رضي الله عنهما, kuwa Ayah hii inamaanisha: “Yeye ni Muweza wa Kuwalipa waliotenda mema na waliofanya maovu.”²

إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.”

Hivi ndivyo ilivyotafsiriwa na Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما. Hii inafanana na Aya:

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى

“...ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na walio tenda mema Awalipe mema.” (53:31).

وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ

“...lakini hao wanaowaomba badala yake...”

Yaani, masanamu na miungu potovu,

لَا يَقْضُونَ بِشَيْءٍ

“...hawahukumu chochote.”

Yaani, hawana lolote na hawatahukumu chochote.

¹ At-Tabari 21:369.

² At-Tabari 21:369.

إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.”

Yaani, Anasikia yote wanayoyasema viumbe Wake wote na anayajua yote yanayowahusu, hivyo Humuongoza yeyote amtakaye na Humuacha yeyote amtakaye apotoke. na Anahukumu kwa haki kabisa katika yote hayo.

* * *

* أَوْلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ
 كَانُوا مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا هُمْ أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَءَانَارًا فِي
 الْأَرْضِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ وَمَا كَانَ لَهُم مِّنَ اللَّهِ مِن
 وَاقٍ ﴿٢١﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ
 فَكَفَرُوا فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ ۚ إِنَّهُ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢٢﴾
 وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٢٣﴾ إِلَىٰ
 فِرْعَوْنَ وَهَمٰنَ وَقُرُوتَ فَقَالُوا سِحْرٌ كَذٰبٌ ﴿٢٤﴾
 فَلَمَّا جَاءَهُم بِالْحَقِّ مِن عِنْدِنَا قَالُوا اقْتُلُوا أَبْنَاءَ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا مَعَهُ وَاسْتَحْيُوا نِسَاءَهُمْ ۚ وَمَا كَيْدُ الْكٰفِرِينَ إِلَّا
 فِي ضَلٰلٍ ﴿٢٥﴾ وَقَالَ فِرْعَوْنُ ذُرِّيَّتِي أَقْتُلْ مُوسَىٰ
 وَلْيَدْعُ رَبَّهُ ۗ إِنِّي أَخَافُ أَن يُبَدِّلَ دِينَكُمْ أَوْ أَن يُظْهِرَ فِي
 الْأَرْضِ الْفَسَادَ ﴿٢٦﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي
 وَرَبِّكُمْ مِن كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٢٧﴾
 وَقَالَ رَجُلٌ مُّؤْمِنٌ مِّنَ ءَالِ فِرْعَوْنَ يَكْتُمُ إِيمٰنَهُ
 أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَن يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ وَقَدْ جَاءَكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ
 مِن رَّبِّكُمْ ۗ وَإِن يَكُ كٰذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهُ ۗ وَإِن يَكُ صَادِقًا
 يُصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِي يَعِدْكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ
 مُسْرِفٌ كَذٰبٌ ﴿٢٨﴾ يَنْقَوِرَ لَكُمْ ءالْمَلِكُ ءالْيَوْمِ ظٰهِرِينَ فِي
 الْأَرْضِ فَمَن يَنْصُرُنَا مِن بَاسِ اللَّهِ إِن جَاءَنَا ۗ قَالَ فِرْعَوْنُ
 مَا أُرِيكُمْ إِلَّا مَا أَرَىٰ وَمَا أَهْدِيكُمْ إِلَّا سَبِيلَ الرَّشَادِ ﴿٢٩﴾

* أَوْلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ كَانُوا مِن
 قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا هُمْ أَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً
 وَءَانَارًا فِي الْأَرْضِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ
 بِذُنُوبِهِمْ وَمَا كَانَ لَهُم مِّنَ اللَّهِ مِن
 وَاقٍ ﴿٢١﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانَتْ
 تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَكَفَرُوا
 فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ ۚ إِنَّهُ قَوِيٌّ شَدِيدُ
 الْعِقَابِ ﴿٢٢﴾

21. Kwani hawakutembea katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Hao walikuwa wamewazidi hawa kwa nguvu na athari katika nchi. Na Mwenyezi Mungu Aliwatia Mkononi kwa sababu ya madhambi yao. Na wala hapakuwa wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.

22. Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi, lakini wakawakataa, ndipo Mwenyezi Mungu Akawakamata. Bila ya shaka Yeye ni Mwenye Nguvu, Mkali wa Kuadhibu.

Mwisho Mbaya kwa Makafiri

أَوَلَمْ يَسِيرُوا

“Kwani hawatembe...”

‘Hao waliokataa Ujumbe wako, Ewe Muhammad’,

فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ كَانُوا مِنْ قَبْلِهِمْ

“...katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao?”

Yaani, umma uliotangulia uliowakataa Mitume wao, ambao waliadhibiwa japokuwa ulikuwa na nguvu kuliko Maquraysh.

وَأَثَارًا فِي الْأَرْضِ

“...na athari katika nchi.” Yaani, waliacha alama katika ardhi, kama vile miundo mbinu, majengo na makazi ambayo watu hawa yaani, Maquraysh hawawezi kulingana. Hii inafanana na Aya:

وَلَقَدْ مَكَّنَّهُمْ فِيمَا إِنْ مَكَّنَّاكُمْ فِيهِ

“Na bila ya shaka Tuliwaweka vizuri sio kama Tulivyokuwekeni nyinyi.” (46:26)

وَأَثَارُوا الْأَرْضِ وَعَمَرُوهَا أَكْثَرَ مِمَّا عَمَرُوهَا

“...na wakiilima ardhi na wakaistawisha zaidi kuliko wao walivyoistawisha.” (30:9).

Licha ya nguvu hiyo kubwa, Allah تعالى Aliwaadhibu kwa sababu ya dhambi yao, ambayo ilikuwa kuwakataa Mitume wao.

وَمَا كَانَ لَهُمْ مِّنَ اللَّهِ مِن وَّاقٍ

“Na wala hapakuwa wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hawakuwa na yeyote wa kuwalinda au kuwaondolea adhabu. Kisha Allah تعالى Akataja sababu ya Kuwaadhibu, na madhambi waliyofanya.

Allah تعالیٰ Anasema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ

“Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawajia Mitume wao kwa hoja zilizo wazi.”

Yaani kwa dalili za waziwazi na ushahidi madhubuti.

فَكْفَرُوا

“...lakini wakawakataa.”

Yaani, licha ya dalili zote hizo, walikufuru na kuukataa.

فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ

“...ndipo Mwenyezi Mungu Akawakamata.”

Yaani, Aliwaangamiza kabisa, na janga kama hilo litawafika makafiri.

إِنَّهُ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ

“Bila ya shaka Yeye ni Mwenye nguvu.” Yaani, Yeye ni Mwenye Nguvu na Uwezo Mkubwa.

شَدِيدُ الْعِقَابِ

“Mkali wa Kuadhibu.” Yaani, adhabu Yake ni kali na inaumiza; tunamuomba Allah تعالیٰ Atukinge.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٢١﴾ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَهٰمٰنَ وَقُرُوٰنَ

فَقَالُوا سِحْرٌ كَذٰبٌ ﴿٢٢﴾ فَلَمَّا جَاءَهُم بِآلْحَقِّ مِنۢ عِنْدِنَا قَالُوا اقْتُلُوا أَبْنَاءَ الَّذِينَ

ءَامَنُوا مَعَهُ وَاسْتَحْيُوا نِسَاءَهُمْ ﴿٢٣﴾ وَمَا كَيْدُ الْكٰفِرِينَ إِلَّا فِي ضَلٰلٍ ﴿٢٤﴾ وَقَالَ

فِرْعَوْنُ ذَرُونِي أَقْتُلْ مُوسَىٰ وَلْيَدْعُ رَبَّهُ ۗ إِنِّي أَخَافُ أَن يُبَدِّلَ دِينَكُمْ أَوْ أَن يُظْهِرَ فِي

الْأَرْضِ الْفَسَادَ ﴿٢٥﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِنۢ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ

23. Na kwa yakini Tulimtuma Musa pamoja na miujiza yetu na hoja zilizo wazi.

24. Kumpelekea Firauni na Hamana na Qaruni, wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo mkubwa.

25. Basi alipowaletea Haki inayotoka Kwetu, walisema: Waueni watoto wanaume wa wale waliomuamini na wawacheni hai wanawake wao. Na haviwi vitimbi vya makafiri ila katika upotovu.

26. Na Firauni akasema: Niachieni nimuue Musa, naye amwite Mola wake Mlezi! Mimi nachelea asije kubadilishieni dini yenu, au kuleta uharibifu katika nchi.

27. Na Musa akasema: Mimi najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Mola Wenu Mlezi Anilinde na kila mwenye jeuri asiyeiamini Siku ya Hisabu.

Kisa cha Musa عليه السلام na Firauni.

Allah تعالى Anamfariji Mtume Wake Muhammad ﷺ kuhusu ukafiri wa watu wake na Anampa bishara ya mwisho mwema na ushindi duniani na Akhera, kama ilivyomtokea Musa bin 'Imran عليه السلام, ambaye Allah تعالى Alimpa dalili waziwazi na ushahidi madhubuti.

Allah تعالى Anasema:

بِعَايِنَتِنَا وَسُلْطَانِ مُبِينٍ

“...pamoja na Ishara Zetu na uthibitisho uliowazi.”

Maana ya *Sultan* ni dalili na ushahidi.

إِلَىٰ فِرْعَوْنَ

“Kumpelekea Firauni...”

Aliyekuwa mfalme wa Makhufti wa Misri.

وَهَمَّٰنٌ

“...na Hamana...”

Aliyekuwa mshauri wake.

وَقَارُونَ

“...na Qaruni.”

Aliyekuwa mfanyabiashara tajiri sana kwa watu wa wakati wake.

فَقَالُوا سَجْرٌ كَذَّابٌ

“...wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo mkubwa.”

Yaani, walimkataa na walimchukulia kuwa alikuwa mchawi, mwendawazimu na mwongo aliyedanganya kuwa alitumwa na Allah تعالى. Hii inafanana na Aya:

كَذَّٰلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْتَوٍ ۗ أَتَوَاصَوْا بِهِ ۗ
بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَٰغُونَ ۗ

“Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia waliokuwa kabla yao Mtume yeyote ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu. Je! Wameambizana kwa haya? Bali hawa ni watu waasi.” (51:52-53)

فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِالْحَقِّ مِنْ عِنْدِنَا

“Basi alipowaletea Haki inayotoka kwetu.”

Yaani, ushahidi wa uhakika kuwa Allah تعالى Alimtuma kwao,

قَالُوا أَقْتُلُوا أَبْنَاءَ الَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ وَاسْتَحْيُوا نِسَاءَهُمْ

“...walisema: Waueni watoto wanaume wa wale waliomuamini na wawacheni hai wanawake wao.”

Hii ilikuwa amri ya pili kutoka kwa Firauni ya kuwaua wanaume katika Bani Israel. Amri ya kwanza ilikuwa ya tahadhari dhidi ya kuibuka mtu kama Musa, au kitendo cha kuwakandamiza watu hao au kupunguza idadi yao au yote mawili. Amri ya pili ilikuwa kwa ajili ya sababu ya pili, kuwakandamiza watu ili wamuone Musa عليه السلام mwenye mkosi. Walisema:

أُوذِينَا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَأْتِيَنَا وَمِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا قَالَ عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ
وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿٢١﴾

“Tumeudhiwa kabla hujatufikia, na baada ya wewe kutujia! Musa akasema: Huenda Mola Wenu Mlezi Akamuangamiza adui wenu, na Akakutawalisheni katika nchi, ili Aone vipi mtakavyofanya.” (7:129).

Qatadah alisema, hii ilikuwa amri moja baada ya nyingine.¹

وَمَا كَيْدُ الْكٰفِرِينَ إِلَّا فِي ضَلٰلٍ

“...haviwi vitimbi vya makafiri ila katika upotovu.”

Yaani, njama na nia zao – kutaka kupunguza idadi ya Bani Israel ili wasikushindeni – zilianguka vibaya.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ذُرِّيَّتِيْ اَقْتُلْ مُوسٰى وَلْيَدْعُ رَبَّهُ

“Na Firauni akasema: Niachieni nimuue Musa, naye amuite Mola Wake Mlezi!”

Firauni, Allah تعالى Amlaani, aliazimia kumuua Musa عليه السلام, yaani, aliwaambia watu wake, ‘ngoja nimuue kwa ajili yenu.’

وَلْيَدْعُ رَبَّهُ

“..naye amuite Mola Wake Mlezi!”

Yaani, ‘Sijali.’ Huu ni ujeuri uliovuka mipaka.

إِنِّيْٓ اٰخَافُ اَنْ يُبَدِّلَ دِيْنَكُمْ اَوْ اَنْ يُظْهِرَ فِى الْاَرْضِ الْاَفْسَادَ

“Mimi nachelea asije kukubadilishieni dini yenu, au akatangaza uharibifu katika nchi.”

¹ At-Tabari 21:373.

Firauni alihofia kuwa Musa عليه السلام angempotezea watu na kubadili desturi zao, kana kwamba, Firauni alishughulishwa na kile ambacho Musa عليه السلام angewafanyia watu wake! Wengi walifahamu kuwa inamaanisha, 'angedadili dini yenu na kuleta uharibifu ardhini.'

﴿٤٧﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ مِن كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ

“Na Musa akasema: Mimi najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Mola Wenu Mlezi Anilinde na kila mwenye jeuri asiyeiamini Siku ya Hisabu.”

Yaani, aliposikia kuwa Firauni alishasema,

ذُرُونِي أَقْتُلْ مُوسَىٰ

“Niachieni nimuue Musa.”

Musa عليه السلام, alisema, “Ninajikinga kwa Allah تعالى dhidi ya shari zake na za walio kama yeye.” Alisema:

إِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ

“Mimi najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Mola Wenu Mlezi...” Waliokuwa wakiambiwa hapa:

مِن كُلِّ مُتَكَبِّرٍ

“...na kila mwenye jeuri...” Yaani, dhidi ya kila mwovu,

لَا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ

“...asiyeiamini Siku ya Hisabu.”

Imesimuliwa katika Hadithi kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ alipowaogopa baadhi ya watu, alikuwa akisema:

«اللَّهُمَّ إِنَّا نَعُوذُ بِكَ مِنْ شُرُورِهِمْ، وَتَدْرَأُ بِكَ فِي نُحُورِهِمْ»

“Ewe Allah, Hakika sisi tunajikinga Kwako dhidi ya shari zao na tunaomba msaada Wako katika kuwashinda.”¹

¹ An-Nasai katika *Al-Kubra* 5:188.

وَقَالَ رَجُلٌ مُؤْمِنٌ مِّنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَكْتُمُ إِيمَانَهُ أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَنْ يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ
 وَقَدْ جَاءَكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ وَإِنْ يَكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهُ ۗ وَإِنْ يَكُ صَادِقًا
 يُصِيبْكُمْ بِعَظْمِ الَّذِي يَعِدُكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَابٌ ﴿٢٨﴾ يَنْقَوْمَ لَكُمْ
 الْمَلَأُ الْيَوْمَ ظَهْرِيْنَ فِي الْأَرْضِ فَمَنْ يَنْصُرُنَا مِنْ بَأْسِ اللَّهِ إِنْ جَاءَنَا ۗ قَالَ فِرْعَوْنُ مَا
 أُرِيكُمْ إِلَّا مَا أَرَىٰ وَمَا أَهْدِيكُمْ إِلَّا سَبِيلَ الرَّشَادِ ﴿٢٩﴾

28. Na akasema mtu mmoja Muumini, aliyekuwa mmoja katika watu wa Firauni aliyeficha Imani yake: Mtamuwa mtu kwa sababu anasema Mola Wangu Mlezi ni Mwenyezi Mungu? Na hali naye amekujieni na hoja zilizo wazi? Na akiwa yeye mwongo basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe, na akiwa mkweli yatakufikieni baadhi ya hayo anayokuahidini. Hakika Mwenyezi Mungu Hamuongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa.

29. Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika nchi; basi ni nani atakayetusa dia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia? Firauni akasema: Sikupeni shauri ila ile niliyoiona, wala sikuongozeni ila kwenye njia ya uwongofu.

Musa عليه السلام Alisaidiwa na Muumini kutoka Katika Familia ya Firauni

Rai maarufu ni kuwa, muumini huyo alikuwa Mkhufi (Mmisri) kutoka katika familia ya Firauni. As-Suddi alisema, alikuwa binamu, mtoto wa ami yake Firauni. Ilisemekana alikuwa ndiye aliyenusurika pamoja na Musa عليه السلام.¹ Ibn Jurayji alisimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Hakuamini yeyote katika familia ya Firauni zaidi ya mtu huyo, mke wa Firauni, na mmoja ambaye alisema,

يَمُوسَىٰ إِنَّ الْمَلَأَ يَأْتَمِرُونَ بِكَ لِيَقْتُلُوكَ

"Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuu." (28:20)

¹ At-Tabari 21:375.

Hii imesimuliwa na Ibn Abi Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى.¹ Mtu huyo alificha Imani yake dhidi ya watu wake, Wamisri, hakuidhihirisha isipokuwa katika siku hii Firauni aliposema,

ذُرُونِي أَقْتُلْ مُوسَى

“Niachieni nimuue Musa.”

Mtu huyo akakasirika kwa ajili ya Allah تَعَالَى, na Jihad bora zaidi ni kusema neno jema mbele ya mtawala dhalimu, kama ilivyoelezwa katika Hadithi.² Hakuna mfano mkubwa zaidi kuliko maneno ya mtu huyo kumuambia Firauni:

أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَنْ يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ

“Mtamuwa mtu kwa sababu anasema Mola Wangu Mlezi ni Mwenyezi Mungu?”

Al-Bukhari ameandika kisa sawa na hicho katika Sahih yake kutoka kwa 'Urwah bin Az-Zubayr رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, ambaye alisema: “Nilimuambia 'Abdullah bin 'Amr bin Al-' As: 'Niambie, lipi baya zaidi ambalo washirikina walimtendea Mtume ﷺ alisema, 'Mtume ﷺ alipokuwa akisali katika eneo la Ka'bah, 'Uqbah bin Abi Mu'it alikuja na kukamata bega la Mtume ﷺ na kuanza kuviringisha nguo yake ili imkabe. Abubakr رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, alikuja na kukamata bega la 'Uqbah na kumsukuma mbali kumtenganisha na Mtume ﷺ, kisha akasema,

أَتَقْتُلُونَ رَجُلًا أَنْ يَقُولَ رَبِّيَ اللَّهُ وَقَدْ جَاءَكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ رَبِّكُمْ^ط

“Mtamuwa mtu kwa sababu anasema Mola Wangu Mlezi ni Mwenyezi Mungu? Na hali naye amekujieni na hoja zilizo wazi?”

Haya yaliandikwa na Al-Bukhari.³ Kauli ya Allah تَعَالَى:

وَقَدْ جَاءَكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ رَبِّكُمْ^ط

“Na hali naye amekujieni na hoja zilizo wazi?”

¹ Al-Qurtubi 15:306.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:390.

³ Fat'h Al-Bari 8:416.

Yaani, "mtamuua mtu kwa sababu tu anasema, 'Mola Wangu ni Allah تعالیٰ,' na analeta dalili za kuthibitisha." Kisha, ili kutoa hoja, kisha akaendelea kujibizana nao kwa kusema:

وَإِنْ يَكُ كَذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهُ ۖ وَإِنْ يَكُ صَادِقًا يُصِيبْكُمْ بَعْضُ الَّذِي يَعِدُكُمْ ۗ

"Na akiwa yeye mwongo basi uwongo wake ni juu yake mwenyewe, na akiwa mkweli yatakufikieni baadhi ya hayo anayokuahidini."

Yaani, 'kama hamuamini anayosema, basi msimdhuru; kama anaongopa, Allah تعالیٰ Atamuadhibu duniani na Akhera. Kama ni mkweli na mkamdhuru, basi aliyokuonyeeni yatakujieni, kwani anakutishieni adhabu duniani na Akhera kama mtampinga. Inawezekana anakuambieni ukweli, muacheni yeye na watu wake, msimdhuru.' Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa Musa عليه السلام alimuambia Firauni na watu wake wamuache katika amani. Anasema:

وَلَقَدْ فَتَنَّا قَبْلَهُمْ قَوْمَ فِرْعَوْنَ وَجَاءَهُمْ رَسُولٌ كَرِيمٌ ﴿٢١﴾ أَنْ أَدْوَأَ إِلَىٰ عِبَادَ اللَّهِ ۖ إِنِّي لَكُم رَسُولٌ أَمِينٌ ﴿٢٢﴾ وَأَنْ لَا تَعْلُوا عَلَى اللَّهِ ۗ إِنِّي آتِيكُمْ بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٢٣﴾ وَإِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ أَنْ تَزْحَمُونِ ﴿٢٤﴾ وَإِنْ لَمْ تُؤْمِنُوا لِي فَاَعْتَرِلُونِ ﴿٢٥﴾

"Na hakika kabla ya hawa Tuliwafanyia mtihani watu wa Firauni, na aliwafikia Mtume Mtukufu. Akasema: Nipeni waja wa Mwenyezi Mungu; kwa hakika mimi kwenu ni Mtume Muaminifu. Na msimfanyie kiburi Mwenyezi Mungu; hakika mimi nitakuleteeni dalili zilizo wazi. Nami najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Ndiye Mola Wenu Mlezi pia, ili msinipige mawe. Na ikiwa hamniamini, basi jitengeni nami." (44:17-21).

Kadhhalika, Mtume ﷺ aliwaambia Maqurayshi wamuache awaite waja wa Allah تعالیٰ; akawaambia wasimdhuru, na wadumishe undugu uliokuwepo kati yake na wao, kwa kutokumdhuru. Allah تعالیٰ Anasema:

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْآمَوَدَةَ فِي الْغُرُبٰٓءِ ۗ

"Sema: kwa haya (ninayokufundisheni) sikuombeni malipo yoyote; lakini nataka muyapende mambo ya kukusogezeni (kwa Allah)." (42:23),

Yaani, 'msinidhuru, kwani mimi na nyinyi ni ndugu; basi msinidhuru, na niacheni niwalinganie watu.' Huu ulikuwa msingi wa makubaliano ya Siku ya Al-Hudaybiyah, ambao ulikuwa ushindi wa waziwazi.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَّابٌ

"Hakika Mwenyezi Mungu Hamuongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa."

Yaani, 'kama mtu anayedai kuwa ametumwa na Allah تعالى ni muongo, kama mnavyosema, hilo lingekuwa wazi kwa kila mmoja kwa maneno na vitendo vyake, yasingelingana bali yangekanganyana. Lakini tunaweza kuona kuwa mtu huyu ni mnyoofu na anachosema ni kweli. Angekuwa mtenda dhambi na mwongo, Allah تعالى Asingemuahidi na kufanya maneno na vitendo vyake kuwa thabiti kama mnavyoviona.' Kisha muumini huyu aliwaonya watu wake kuwa hawatakosa Neema za Allah تعالى juu yao na kuwa adhabu ya Allah تعالى ingewakuta:

يَنْقُومَ لَكُمْ أَلْمَلِكُ الْيَوْمَ ظَهْرَيْنَ فِي الْأَرْضِ

"Enyi watu wangu! Leo mna ufalme, mmeshinda katika nchi."

Yaani, 'Allah تعالى Amekupeni ufalme, utawala wa ardhini, nguvu na mamlaka, basi zingatieni baraka hizo kwa kumshukuru Allah تعالى na kumuamini Mtume Wake, na ninakutahadharisheni adhabu ya Allah تعالى kama mtamkataa Mtume Wake.'

فَمَنْ يَنْصُرُنَا مِنْ بَأْسِ اللَّهِ إِنْ جَاءَنَا

"...basi ni nani atakayenisaidia kutuokoa na adhabu ya Mwenyezi Mungu kama ikitufikia?"

Yaani, 'wanajeshi hawa hawatakusaidieni chochote wala kuondoa adhabu ya Allah تعالى, kama Ataamua Kutuadhibu.' Firauni aliwaambia watu wake, katika kujibu shauri la mja mwema huyu ambaye alistahiki zaidi ufalme kuliko Firauni:

مَا أُرِيكُمْ إِلَّا مَا أَرَى

"Sikupeni shauri ila ile niliyoiona." Yaani, 'Ninakuambieni na kukupeni rai ya kufanya ninaloona jema hata kwangu, pia.' Lakini Firauni aliongopa, kwa

sababu alijua kuwa Musa عليه السلام alikuwa akisema ukweli kuhusu Ujumbe aliouleta.

قَالَ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا أَنْزَلَ هَتُؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِصَآئِرٍ

“Musa akasema: Wewe unajua bila ya shaka kuwa haya hakuyateremsha ila Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ili kuwa ni ushahidi wa kuonekana.” (17:102)

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنْفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا

“Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo.” (27:14)

مَا أُرِيكُمْ إِلَّا مَا أَرَىٰ

“Sikupeni shauri ila ile niliyo iona.”

Firauni aliongopa na kuzua; alimsaliti Allah تعالى na Mtume Wake, na aliwahadaa watu kwa kutowanasihi kwa unyoofu.

وَمَا أَهْدِيكُمْ إِلَّا سَبِيلَ الرَّشَادِ

“...wala sikuongozeni ila kwenye njia ya uwongofu.”

Yaani, ‘nami nakuiteni tu kwenye njia ya kweli, unyoofu na uongofu.’ Huu pia ulikuwa uongo, lakini watu wake walimtii na walimfuata.

Allah تعالى Anasema:

فَاتَّبِعُوا أَمْرَ فِرْعَوْنَ وَمَا أَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيدٍ ﴿٧٩﴾

“Lakini wao walifuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa yenye uwongofu.” (11:97).

وَأَصْلَ فِرْعَوْنَ قَوْمَهُ وَمَا هَدَىٰ ﴿٧٩﴾

“Na Firauni aliwapoteza watu wake wala hakuwaongoa.” (20:79)

Kwa mujibu wa Hadith:

«مَا مِنْ إِمَامٍ يَمُوتُ يَوْمَ بُمُوتٍ وَهُوَ غَاشٍ لِرَعِيَّتِي، إِلَّا لَمْ يَرَّخْ رَاحَةَ الْجَنَّةِ، وَإِنْ
رِيحَهَا لَيُوجَدُ مِنْ مَسِيرَةِ خَمْسِمِائَةِ عَامٍ»

"Hakuna kiongozi anayekufa huku akiwa amewahadaa watu wake, isipokuwa hatanusa manukato ya Peponi, na manukato yake yanafika umbali wa safari ya miaka mia tano."

Na Allah تعالیٰ Ndiye Mwenye Kuhidi kwenye njia nyoofu.

* * *

¹ Fat'h Al-Bari 13:136.

وَقَالَ الَّذِينَ ءَامَنَ يَنْقُومِ إِلَيْنِ أَخَافُ عَلَيْكُمْ مِثْلَ يَوْمِ
 الْأَحْزَابِ ﴿٣٠﴾ مِثْلَ ذَابِ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ وَالَّذِينَ
 مِنْ بَعْدِهِمْ ؕ وَمَا اللَّهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِّلْعِبَادِ ﴿٣١﴾ وَيَنْقُومِ إِلَيْنِ
 أَخَافُ عَلَيْكُمْ يَوْمَ التَّنَادِ ﴿٣٢﴾ يَوْمَ تُؤَلُّونَ مَدْرِبِينَ مَا لَكُمْ
 مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ ؕ وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ ﴿٣٣﴾
 وَلَقَدْ جَاءَكُمْ يُوسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا زِلْتُمْ فِي
 شَكٍّ مِّمَّا جَاءَكُمْ بِهِ ؕ حَتَّىٰ إِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَبْعَثَ
 اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا ؕ كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ
 مُّرْتَابٌ ﴿٣٤﴾ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي ءَايَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ سُلْطَانٍ
 أَتَتْهُمْ ؕ كَبُرَ مَقَامًا عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ الَّذِينَ ءَامَنُوا ؕ كَذَلِكَ
 يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ قَلْبٍ مُتَكَبِّرٍ جَبَّارٍ ﴿٣٥﴾ وَقَالَ فِرْعَوْنُ
 يَبْهَمُنُّ أَبْنَىٰ لِى صَرِحًا لَعَلِّي أَبْتُلُغُ الْاَسْبَابَ ﴿٣٦﴾ اَسْبَابَ
 السَّمَوَاتِ فَاطَّلَعَ اِلَىٰ اِلٰههٖ مُوسَىٰ وَاِنِى لَاطْنُكُهُ كَذِبًا ؕ
 وَكَذَلِكَ زَيْنَ لِفِرْعَوْنَ سُوءَ عَمَلِهٖ وَصَدَّ عَنِ السَّبِيلِ ؕ
 وَمَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ اِلاَّ فِي تَبَابٍ ﴿٣٧﴾ وَقَالَ الَّذِى
 ءَامَنَ يَنْقُومِ اَنْبِعُوْنِ اَهْدِكُمْ سَبِيْلَ الرِّشَادِ ﴿٣٨﴾
 يَنْقُومِ اِنَّمَا هٰذِهِ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا مَتَّعْ وَاِنَّ الْاٰخِرَةَ هِىَ دَارٌ
 اَلْقَرَارِ ﴿٣٩﴾ مَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَىٰ اِلاَّ مِثْلَهَا ؕ وَمَنْ
 عَمِلَ صٰلِحًا مِّنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْتَىٰ ۗ وَهُوَ مُؤْمِنٌ ۗ فَاُوْتِنٰكَ
 يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ يُرْزَقُوْنَ فِيْهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٠﴾

وَقَالَ الَّذِينَ ءَامَنَ يَنْقُومِ إِلَيْنِ أَخَافُ عَلَيْكُمْ مِثْلَ يَوْمِ
 الْأَحْزَابِ ﴿٣٠﴾ مِثْلَ ذَابِ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ
 وَالَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ ؕ وَمَا اللَّهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِّلْعِبَادِ ﴿٣١﴾
 وَيَنْقُومِ إِلَيْنِ أَخَافُ عَلَيْكُمْ يَوْمَ التَّنَادِ ﴿٣٢﴾ يَوْمَ تُؤَلُّونَ
 مَدْرِبِينَ مَا لَكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ ؕ وَمَنْ يُضْلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ
 مِنْ هَادٍ ﴿٣٣﴾ وَلَقَدْ جَاءَكُمْ يُوسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنَاتِ
 فَمَا زِلْتُمْ فِي شَكٍّ مِّمَّا جَاءَكُمْ بِهِ ؕ حَتَّىٰ إِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ
 لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا ؕ كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ
 مُسْرِفٌ مُّرْتَابٌ ﴿٣٤﴾ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي ءَايَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ
 سُلْطَانٍ أَتَتْهُمْ ؕ كَبُرَ مَقَامًا عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ الَّذِينَ ءَامَنُوا
 ؕ كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ قَلْبٍ مُتَكَبِّرٍ جَبَّارٍ ﴿٣٥﴾
 وَقَالَ الَّذِى ءَامَنَ يَنْقُومِ اَنْبِعُوْنِ اَهْدِكُمْ سَبِيْلَ الرِّشَادِ ﴿٣٨﴾
 يَنْقُومِ اِنَّمَا هٰذِهِ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا مَتَّعْ وَاِنَّ الْاٰخِرَةَ هِىَ
 دَارٌ اَلْقَرَارِ ﴿٣٩﴾ مَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَىٰ اِلاَّ مِثْلَهَا ؕ وَمَنْ
 عَمِلَ صٰلِحًا مِّنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْتَىٰ ۗ وَهُوَ مُؤْمِنٌ ۗ فَاُوْتِنٰكَ
 يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ يُرْزَقُوْنَ فِيْهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٠﴾

**30. Na akasema yule aliye-
 amini: Enyi watu wangu!
 Hakika mimi nakukhofieni
 mfano wa siku za makundi.**

31. Mfano wa hali ya watu wa Nuhu na A'di na Thamudi na wale wa baada yao. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu waja.

32. Na enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni Siku ya mayowe.

33. Siku mtakapogeuka kurudi nyuma. Hamtakuwa na wa kukulindeneni kwa Mwenyezi Mungu. Na mwenye kuhukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi huyo hana wa kumuongoa.

34. Na alikwishawajieni Yusuf zamani kwa dalili zilizo wazi, lakini nyinyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyokuleteeni; mpaka alipokufa mkasema: Mwenyezi Mungu Hataleta kabisa Mtume baada yake. Kama hivyo Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea anayepindukia mipaka katika maasi anayejitia shaka.

35. Hao ambao wanajadiliana katika Aya za Mwenyezi Mungu pasipo ushahidi wowote uliowafikia, ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya walioamini. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa jeuri anayejivuna.

Hapa Allah تعالى Anatuambia kuwa huyu mchamungu, muumini kutoka katika familia ya Firauni, aliwaonya watu wake juu ya adhabu ya Allah تعالى duniani na Akhera, kwa kusema,

يَنْقُومِ رَبِّيَ أَخَافُ عَلَيْكُمْ مِثْلَ يَوْمِ الْأَحْزَابِ

“Enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni mfano wa siku za makundi.”

Maana yake, mataifa yaliyotangulia yaliyowakataa Mitume wa Allah تعالى, kama vile watu wa Nuh, 'Ad, Thamud na mataifa ya kikafiri waliokuja baada yao, namna adhabu ya Allah تعالى ilivyowajia na hawakuwa na wa kuwapa hifadhi au kuwaondolea adhabu hiyo.

وَمَا اللَّهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِّلْعِبَادِ

“Na Mwenyezi Mungu Hataki Kuwadhulumu waja.”

Yaani, Allah تعالى Aliwaangamiza kwa sababu ya madhambi yao na kwa ukafiri

wao na kuwakataa Mitume Wake; hii ilikuwa Amri Yake na Hukumu Yake kwao ambayo ilitimizwa. Kisha akasema:

وَيَقُولُ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ يَوْمَ التَّنَادِ

“Na enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni Siku ya mayowe.”

Maana yake, Siku ya Kiama.

يَوْمَ تُولُونَ مُدْبِرِينَ

“Siku mtakapogeuka kurudi nyuma.”

Yaani, kukimbia.

كَلَّا لَا وَزَرَ ۖ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ۖ

“La! Hapana pa kukimbia! Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola wako Mlezi tu.” (75:11-12)

Allah تعالیٰ Anasema:

مَا لَكُمْ مِّنَ اللَّهِ مِّنْ عَاصِمٍ ۗ

“Hamtakuwa na wa kukulindeni kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake, ‘hamtakuwa na wa kulindeni dhidi ya adhabu na mateso ya Allah تعالیٰ.’

وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ

“Na mwenye kuhukumiwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi huyo hana wa kumuongoa.”

Yaani, yeyote ambaye Allah تعالیٰ Anamuacha apotee hatakuwa na mwingine wa kumuongoa isipokuwa Yeye. Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَلَقَدْ جَاءَكُمْ يُوسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنَاتِ

“Na alikwisha wajieni Yusuf zamani kwa dalili zilizowazi.”

Inakusudia watu wa Misri. Allah تعالیٰ Aliwapelekea Mtume kabla ya wakati wa Musa عليه السلام, ambaye ni Yusuf عليه السلام, ambaye alipata nafasi ya juu

katika serikali ya watu wa Misri. Alikuwa Mtume Aliyewalingania watu wake kwa Allah تعالى kwa uadilifu, lakini hawakumtii katika masuala ya kumuabudu Allah تعالى bali walimtii katika mambo ya kidunia tu yaliyoendana na nafasi yake serikalini. Allah تعالى Anasema:

فَمَا زِلْتُمْ فِي شَكِّ وَمِمَّا جَاءَكُمْ بِهِ^ط حَتَّى إِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا

“...lakini nyinyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyokuleteeni; mpaka alipokufa mkasema: Mwenyezi Mungu Hataleta kabisa Mtume baada yake.”

Yaani, ‘mlikata tamaa, na mlisema kwa tamaa,’

لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا

“Mwenyezi Mungu Hataleta kabisa Mtume baada yake.”

Hayo kwa sababu ya ukafiri wao na kukataa (Mitume).

كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُرْتَابٌ

“Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea anayepindukia mipaka katika maasi anayejitia shaka.”

Yaani, hii ni hali ya yule ambaye Allah تعالى Anamuacha apotee kwa sababu ya vitendo vyake vya dhambi na mashaka moyoni mwake.

الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ سُلْطَانٍ أَتَاهُمْ^ط

“Hao ambao wanajadiliana katika Aya za Mwenyezi Mungu pasipo ushahidi wowote uliowafikia.”

Yaani, waliojaribu kukataa ukweli kwa upotovu na ambao walikataa dalili bila ya ushahidi au dalili kutoka kwa Allah تعالى, Allah تعالى Atawaghadhibikia sana. Allah تعالى Anasema:

كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“...ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya walioamini.”

Maana yake, waumini pia watawadharau wale walio kama hivyo, na yeyote aliye kama hivyo, Allah تعالى Atagonga mhuri moyoni mwa mtu huyo ili baada ya hapo asitambue lolote jema au kukataa shari yoyote. Allah تعالى Anasema:

كَذَلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَى كُلِّ قَلْبٍ مُّتَكَبِّرٍ

“Hivi Ndivyo Mwenyezi Mungu Apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa jeuri...”

Maana yake, ili wasiweze kufuata ukweli.

جَبَّارٍ

“...anayejivuna.” Abuu Imrani Aljawni amesema: Alama na Ishara ya watu makatili ni kuuwa bila ya haki (Allah Ndiye Mjuzi zaidi).

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يَنْهَمْنُنُ ابْنِ لِي صَرَخًا لَعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَ ﴿٣٦﴾ أَسْبَابَ السَّمَوَاتِ فَأَطَّلِعُ إِلَىٰ آلِهِ مُوْسَىٰ وَإِنِّي لِأَظُنُّهُ كَذِبًا ۖ وَكَذَلِكَ نُفِرُّ فِرْعَوْنَ سُوْءَ عَمَلِهِ وَصُدَّ عَنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ إِلَّا فِي تَبَابٍ ﴿٣٧﴾

36. Na Firauni akasema: Ewe Hamana! Nijengee mnara ili nipate kuzifikia njia.

37. Njia za mbinguni ili nikamuone Mungu wa Musa. Na kwa hakika mimi bila ya shaka namjua kuwa ni mwongo tu. Na hivi ndivyo Firauni alivyopambiwa ubaya wa vitendo vyake, na akazuiliwa Njia. Na vitimbi vya Firauni havikuwa ila katika kuangamia tu.

Jinsi Firauni Alivyomfanyia Kejeli Mola Mlezi wa Musa عليه السلام

Allah تعالى Anatuambia kuhusu kiburi na ufidhuli wa Firauni na kumkataa kwake Musa عليه السلام, alipomuamrisha waziri wake Haman kumjengea ngome ndefu, imara na yenye nguvu. Aliijenga kwa matofali ya kuchoma, kama Anavyosema Allah تعالى :

فَأَوْقَدَ لِي يَنْهَمْنُنُ عَلَىٰ آلِطِينٍ فَأَجْعَلَ لِي صَرَخًا

“Niwashie moto unichomee udongo, unijengee mnara...” (28:38).

لَعَلِّي أَبْلُغَ الْأَسْبَابَ ﴿٣٠﴾ أَسْبَابَ السَّمَوَاتِ

“...ili nipate kuzifikia njia, njia za mbinguni...”

Sa'id bin Jubayr na Abu Salih walisema, “Milango ya mbinguni.”¹ Au ilisemekana, njia za mbingu.

فَأَطَّلَعَ إِلَىٰ إِلَهِ مُوسَىٰ وَإِنِّي لِأَظُنُّهُ كَذِبًا ۗ

“...ili nikamuone Mungu wa Musa. Na kwa hakika mimi bila ya shaka namjua kuwa ni mwongo tu.”

Kwa sababu ya ukafiri wake na ufidhuli, hakuamini kuwa Allah تعالى Alimtuma Musa عليه السلام kwake. Allah تعالى Anasema:

وَكَذَلِكَ زَيْنَ لِفِرْعَوْنَ سُوءَ عَمَلِهِ وَصُدَّ عَنِ السَّبِيلِ ۗ

“Na hivi ndivyo Firauni alivyopambiwa ubaya wa vitendo vyake, na akazuliwa Njia.”

Yaani, kitendo hiki cha kujenga jengo refu, kwa namna alivyotaka kuwahadaa watu wake na kuwafanya wadhania kuwa angethibitisha kuwa Musa عليه السلام alikuwa akidanganya. Allah تعالى Anasema:

وَمَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ إِلَّا فِي تَبَابٍ

“Na vitimbi vya Firauni havikuwa ila katika kuangamia tu.”

Ibn 'Abbas na Mujahid amesema, “Maana yake hakuna isipokuwa maangamizi.”¹

وَقَالَ الَّذِي آمَنَ يَنْقَوْمِ اتَّبِعُونِ أَهْدِكُمْ سَبِيلَ الرَّشَادِ ﴿٣١﴾ يَنْقَوْمِ إِنَّمَا هَٰذِهِ

الْحَيَاةُ الدُّنْيَا مَتْنَعٌ وَإِنَّ الْآخِرَةَ هِيَ دَارُ الْقَرَارِ ﴿٣٢﴾ مَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا

مِثْلَهَا ۗ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أَتَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ

يُرزقون فيها بغير حساب ﴿٣٣﴾

¹ Al-Qurtubi 15:314.

² At-Tabari 21:388.

38. Na yule aliyeamini alisema: Enyi watu wangu! Nifuateni mimi, nitakuongozeni njia ya uwongozi mwema.

39. Enyi watu wangu! Hakika haya maisha ya dunia ni starehe ipitayo tu, na hakika Akhera ndiyo nyumba ya daima.

40. Mwenye kutenda uovu hatalipwa ila sawa na huo uwovu wake, na anayetenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila ya hisabu.

Muendelezo wa Maneno ya Aliyemuamini Musa عليه السلام katika Familia ya Firauni

Muumini huyo aliwaambia watu wake waliodumu katika uasi wao na kuruka mipaka, na walipendelea maisha ya kidunia na wakamsahau Mola wao Mtukufu,

يَنْقُومِ اتَّبِعُونَ أَهْدِيكُمْ سَبِيلَ الرَّشَادِ

“Enyi watu wangu! Nifuateni mimi, nitakuongozeni njia ya uwongozi mwema.”

Haya yanapingana na madai ya Firauni:

وَمَا أَهْدِيكُمْ إِلَّا سَبِيلَ الرَّشَادِ

“...nitakuongozeni njia ya uwongozi mwema.” (40:29)

Kisha alitaka kuwafanya waipe mgongo dunia waliyoipenda zaidi kuliko Akhera, na ambayo aliwazuia kumuamini Mtume ﷺ, Musa عليه السلام. alisema:

يَنْقُومِ إِنَّمَا هَذِهِ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا مَتَّعٌ

“Enyi watu wangu! Hakika haya maisha ya dunia ni starehe ipitayo tu,

Yaani, haina umuhimu, ni ya kupita tu, na hivi karibuni itafika mwisho na kuondoka.

وَإِنَّ الْآخِرَةَ هِيَ دَارُ الْقَرَارِ

“...na hakika Akhera ndiyo nyumba ya daima.”

Makazi yasiyo na mwisho na ambapo hakuna kuondoka, ama Peponi au Jahanamu. Allah تعالى Anasema:

مَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا

“Mwenye kutenda uovu hatalipwa ila sawa na huo uovu wake.”

Yaani, kama hayo.

وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أَتَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ يُرْزَقُونَ

فِيهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٠﴾

“...na anayetenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini, basi hao wataingia Peponi, waruzukiwe humo bila ya hisabu.” (40:40)

Yaani, malipo yasiyohesabika, lakini Allah تعالى Atalipa malipo yasiyokoma na Allah تعالى ni Mwenye Kuongoza katika njia iliyonyooka.

* * *

* وَيَقُولُ مَا لِيَ أُدْعُوكُمْ إِلَى النَّجْوَةِ وَتَدْعُونَنِي إِلَى النَّارِ ﴿٤١﴾ تَدْعُونَنِي لِأَكْفُرَ بِاللَّهِ وَأُشْرِكَ بِهِ مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ وَأَنَا أَدْعُوكُمْ إِلَى الْعَزِيزِ الْغَفِيرِ ﴿٤٢﴾ لَا جَرَمَ أَنَّمَا تَدْعُونَنِي إِلَيْهِ لَيْسَ لَهُ دَعْوَةٌ فِي الدُّنْيَا وَلَا فِي الْآخِرَةِ وَأَنْ مَرَدَّنَا إِلَى اللَّهِ وَأَنَّ الْمُسْرِفِينَ هُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٤٣﴾ فَسَتَذَكَّرُونَ مَا أَقُولُ لَكُمْ ۗ وَأُفَوِّضُ أَمْرِي إِلَى اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿٤٤﴾ فَوَقَّهٖ اللَّهُ سَيِّئَاتِ مَا مَكْرُوا ۗ وَحَاقَ بِقَالٍ فِرْعَوْنَ سُوءُ الْعَذَابِ ﴿٤٥﴾ النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۗ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾ وَإِذْ يَتَحَاجُّونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا إِنَّ اللَّهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٨﴾ وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخَزَنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ عَنَّا يَوْمًا مِنَ الْعَذَابِ ﴿٤٩﴾ قَالُوا أَوْلَمْ تَكُنْ تَأْتِيكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ ۗ قَالُوا بَلَىٰ ۗ قَالُوا فَادْعُوا ۗ وَمَا دُعَاؤُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٥٠﴾

* وَيَقُولُ مَا لِيَ أُدْعُوكُمْ إِلَى النَّجْوَةِ وَتَدْعُونَنِي إِلَى النَّارِ ﴿٤١﴾ تَدْعُونَنِي لِأَكْفُرَ بِاللَّهِ وَأُشْرِكَ بِهِ مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ وَأَنَا أَدْعُوكُمْ إِلَى الْعَزِيزِ الْغَفِيرِ ﴿٤٢﴾ لَا جَرَمَ أَنَّمَا تَدْعُونَنِي إِلَيْهِ لَيْسَ لَهُ دَعْوَةٌ فِي الدُّنْيَا وَلَا فِي الْآخِرَةِ وَأَنْ مَرَدَّنَا إِلَى اللَّهِ وَأَنَّ الْمُسْرِفِينَ هُمْ أَصْحَابُ النَّارِ ﴿٤٣﴾ فَسَتَذَكَّرُونَ مَا أَقُولُ لَكُمْ ۗ وَأُفَوِّضُ أَمْرِي إِلَى اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿٤٤﴾ فَوَقَّهٖ اللَّهُ سَيِّئَاتِ مَا مَكْرُوا ۗ وَحَاقَ بِقَالٍ فِرْعَوْنَ سُوءُ الْعَذَابِ ﴿٤٥﴾ النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۗ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

41. Na enyi watu wangu!
Kwa nini mimi nakuiteni

kwenye uwokofu, nanyi mnaniita kwenye Moto?

42. Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na nimshirikishe na yule ambaye simjui, nami nakuiteni kwa Mwenye Nguvu Mwenye Kusamehe?

43. Bila ya shaka mnayeniitia kumuabudu hastahiki wito duniani wala Akhera. Na hakika marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu. Na wanaopindukia mipaka ndio watu wa Motoni!

44. Basi karibuni hivi mtayakumbuka ninayokuambieni. Nami namkabidhi Mwenyezi Mungu mambo yangu. Hakika Mwenyezi Mungu Anawaona waja Wake.

45. Basi Mwenyezi Mungu Akamlinda na maovu ya ubaya wa hila walizozifanya. Na adhabu mbaya itawazunguka watu wa Firauni.

46. Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!

Hitimisho la Maneno ya Muumini, na Mwisho wa Makundi Yote Mawili

Muumini huyo alisema: 'Kwanini ninakulinganieni katika wokovu, ambao ni kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya mwenza au mshirika, na kumuamini Mtume Wake Aliyemtuma,'

وَتَدْعُونِي إِلَى النَّارِ ﴿٤٦﴾ تَدْعُونِي لِأَكْفُرَ بِاللَّهِ وَأُشْرِكَ بِهِ مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ

“...nanyi mnaniita kwenye Moto? Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na nimshirikishe na yule ambaye simjui.”

Yaani, kwa ujinga, bila ya dalili au ushahidi.

وَأَنَا أَدْعُوكُمْ إِلَى الْعَزِيزِ الْغَفَّارِ ﴿٤٧﴾

“...nami nakuiteni kwa Mwenye Nguvu Mwenye Kusamehe?”

Yaani, kwa Uwezo Wake na Kiburi, bado Yeye Husamehe madhambi ya anayetubia Kwake.

لَا جَرَمَ أَنْمَا تَدْعُونَنِي إِلَيْهِ

“Bila ya shaka mnayeniitia kumuabudu...”

Wanasema inamaanisha, “Kiukweli.”

As-Suddi na Ibn Jarir رحمه الله تعالى walisema kuwa Maana ya Kauli Yake:

لَا جَزْمَ

"Bila ya shaka..."

Yaani "Kiukweli." Adh-Dhahhak alisema:

لَا جَزْمَ

"Bila ya shaka..."

Yaani, "Si uongo." Ali bin Abi Talhah na Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema:

لَا جَزْمَ

"Bila ya shaka..."

Yaani, "Kwa hakika, mnayeniitia katika masanamu na miungu potovu."

لَيْسَ لَهُ دَعْوَةٌ فِي الدُّنْيَا وَلَا فِي الآخِرَةِ

"...hastahiki wito duniani wala Akhera."

Mujahid alisema, "Masanamu yasiyo na chochote."¹ Qatadah alisema, "Inamaanisha kuwa masanamu hayakuwa na uwezo wowote, si kunufaisha wala wa kudhuru." As-Suddi alisema, "Hawawajibu waliowaita, si duniani wala Akhera."² Hii inafanana na Aya:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ

دُعَائِهِمْ غَنِيُونَ ﴿٥٦﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٥٧﴾

"Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawajibu mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawawajibu maombi yao. Na ambao watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao." (46:5-6)

¹ At-Tabari 21:392.

² At-Tabari 21:392.

إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا مَا اسْتَجَابُوا لَكُمْ^ط

“Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni.” (35:14).

وَأَنَّ مَرَدَّنَا إِلَى اللَّهِ

“Na hakika marejeo yetu ni kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, katika Akhera, ambapo Atamjazi au Kumuadhibu kila mtu kulingana na amali zake. Anasema:

وَأَنَّ الْمُسْرِفِينَ هُمْ أَصْحَابُ النَّارِ

“Na wanaopindukia mipaka ndio watu wa Motoni!”

Maana yake, wataishi humo milele, kwa sababu ya dhambi zao kubwa, ambayo ni kumshirikisha Allah تعالى katika ibada.

فَسَتَذْكُرُونَ مَا أَقُولُ لَكُمْ^ع

“Basi mtayakumbuka ninayokuambieni.”

Yaani, ‘mtakuja kuujua ukweli wa nilichokuamrisheni na kukukatazeni. Nasaha nilizokupeni na niliyokuelezeni. Mtakuja kujua, na mtajuta pindi ambapo majuto hayatasaidia kitu.’

وَأَفْوِضْ أَمْرِي إِلَى اللَّهِ^ع

“Nami namkabidhi Mwenyezi Mungu mambo yangu.” Yaani, “Ninamtegemea Allah تعالى na ninamuomba msaada, na ninakuacheni.”

إِنَّ اللَّهَ بِصِيرٍ بِالْعِبَادِ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anawaona waja Wake.”

Yaani, Anayajua mambo yao yote, na Anawaongoza waliostahiki kuongoka na Kuwaacha wapotee waliostahiki kupotea; dalili kamilifu ni Zake, Hekima na Uwezo mkubwa.

فَوْقَهُ اللَّهُ سَيِّئَاتِ مَا مَكُرُوا^ط

“Basi Mwenyezi Mungu Akamlinda na ubaya wa hila walizozifanya.”

Yaani, duniani na Akhera; duniani, Allah تعالى Akamuokoa pamoja na Musa عليه السلام, na katika Akhera ataingia Peponi.

Kuthibitika Adhabu ya Kaburi

Allah تعالى Anasema:

وَحَاقَ بِقَالِ فِرْعَوْنَ سُوءُ الْعَذَابِ

“Na adhabu mbaya itawazunguka watu wa Firauni.”

Nayo ni adhabu ya kuzama baharini, kisha kuhamishwa hapo na kwenda Jahanamu, kwani roho zao zilidhihirishwa Motoni asubuhi na jioni mpaka Saa itakapoanza. Siku ya Kiama itakapowadia, roho zao na viwiliwili vitau-nganishwa katika Jahanamu. Allah تعالى Anasema:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ

“Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!”

Maana yake, maumivu na mateso makali. Ayah hii ni mojawapo ya dalil kubwa ambazo hutumiwa na *Ahlu-Sunnah* kuthibitisha kuwa kutakuwa na mateso kaburini katika kipindi cha *Al-Barzakh*; ni Aya:

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا

“Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni.”

Lakini swali linaibuka: Ayah hii bila ya shaka yoyote ilishuka Makkah, lakini waliitumia kama ushahidi kuthibitisha kuwa kutakuwa na mateso kaburini katika kipindi cha *Al-Barzakh*.¹ Imam Ahmad ameandika kutoka kwa ‘A’ishah, رضي الله عنها, kwamba mwanamke wa Kiyahudi aliyekuwa mtumishi wake, na kila mara ‘A’ishah alipomfadhili, mwanamke huyo alikuwa akisema, “Allah تعالى Akuondolee adhabu ya kaburini.” ‘A’ishah رضي الله عنها akasema, “Basi Mtume ﷺ akaingia, na nikamuuliza, ‘Ewe Mtume ﷺ, kutakuwa na adhabu kaburini kabla ya Siku ya Kiama?’ Akajibu,

¹ Maisha ya baada ya mauti, kabla ya Siku ya Kiama.

«لَا، مَنْ زَعَمَ ذَلِكَ؟»

“Hapana, nani kasema hayo.”

Nikasema, ‘Mwanamke huyu wa Kiyahudi, kila nilipomfanyia jema,’ alisema: “Allah تعالی Akunusuru na adhabu ya kaburini.” Mtume ﷺ akasema,

«كَذَّبَتْ يَهُودُ وَهُمْ عَلَى اللَّهِ أَكْذَبُ، لَا عَذَابَ دُونَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Mayahudi wamedanganya, na huwa wanaongopa sana juu ya Allah. Hakuna adhabu isipokuwa Siku ya Kiama.”

Kisha ukapita muda mrefu kadiri ya Alivyopenda Allah تعالی, kisha siku moja (Mtume) alitoka wakati wa jua la utosi, huku amejiviringisha nguo na macho yake yakiwa mekundu, akiita kwa sauti ya juu sana:

«الْقَبْرِ كَفَطَعَ اللَّيْلِ الْمُظْلِمِ، أَيُّهَا النَّاسُ لَوْ تَعْلَمُونَ مَا أَعْلَمُ لَبَكَيْتُمْ كَثِيرًا وَضَجْتُمْ قَلِيلًا، أَيُّهَا النَّاسُ، اسْتَعْبِدُوا بِاللَّهِ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، فَإِنَّ عَذَابَ الْقَبْرِ حَقٌّ»

“Kaburi ni kama viraka vya usiku wenye giza! Enyi watu, kama mngejua ninayoyajua, mngelia sana na kucheka kidogo. Enyi watu, ombeni hifadhi kwa Allah dhidi ya adhabu ya kaburi, kwani adhabu ya kaburi ni kweli.”¹

Njia hii ya riwaya ni Sahih kwa mujibu wa vigezo vya Al-Bukhari na Muslim, ingawa hawakuiandika. Husemwa, ‘riwaya hii inawezaje kuwa na mafungamano na aya, ilhali ukweli ni kuwa Ayah hiyo ilishuka Makkah na huku inaashiria kuwa kutakuwa na adhabu katika kipindi cha *Al-Barzakh*?’ Jibu ni kwamba Ayah inazungumzia roho (ya Firauni na watu wake) kuoneshwa Motoni asubuhi na jioni; haisemi kuwa viwiliwili vyao vitapata maumivu kaburini. Hivyo, inawezekana kuwa hili ni mahususi kwa roho zao. Ama kuhusu viwiliwili vyao kuathirika katika *Al-Barzakh*, na kupata maumivu kwa ajili hiyo, hilo limeoneshwa katika Sunnah, katika baadhi ya Hadithi tutakazozitaja hapa chini. Ilisemekana kuwa Aya hii inaashiria kuadhibiwa makafiri katika *Al-Barzakh*, na kuwa haikutaja muumini ataadhibiwa kaburini kwa madhambi

¹ Ahmad 6:81.

yake. Hayo yamo katika Hadithi iliyoandikwa na Imam Ahmad kutoka kwa 'A'ishah رضي الله عنها, ambapo Mtume ﷺ aliingia kwa 'A'ishah رضي الله عنها wakati akiwa na mwanamke wa Kiyahudi, na (mwanamke Myahudi) kusema, "Niliambiwa mtajaribiwa kaburini." Mtume ﷺ alishikwa na hofu na akasema:

«إِنَّمَا يُفْتَنُ يَهُودُ»

"Hakika Mayahudi wanajaribiwa."

'A'ishah رضي الله عنها, alisema, "Siku kadhaa zikapita, kisha Mjumbe wa Allah ﷻ akasema:

«أَلَا إِنَّكُمْ تُفْتَنُونَ فِي الْقُبُورِ»

"Sikieni Hakika, mtajaribiwa makaburini."

'A'ishah رضي الله عنها, alisema, "Baada ya hapo, Mtume ﷺ alikuwa akiomba kinga ya Allah dhidi ya adhabu ya kaburi."¹ Hayo yameandikwa pia na Muslim.² Inawezekana alisema Ayah hii inaashiria kuwa roho zitaadhibiwa katika *Al-Barzakh*, lakini hii si lazima imaanishe kuwa viwiliwili makaburini mwao vitapatwa na hiyo adhabu. Allah تعالى Alipomshushia Aya za adhabu ya kaburi, Mtume Wake aliomba hifadhi ya Allah dhidi ya hilo. Allah تعالى Anajua zaidi. Hadithi zinazoeleza adhabu ya kaburi ziko nyingi. Qatadah alisema, kuhusu Aya,

غُدُّوْا وَعَشِيًّا

"...asubuhi na jioni."

(Inamaanisha) kila asubuhi na kila jioni, kadiri ya dunia itakavyoendelea kuwepo, wataambiwa kwa kukaripiwa na kudhalilishwa, "Enyi watu wa Firauni, hii ndiyo nafasi yenu."³ Ibn Zayd alisema, "Wapo huko leo, wakioneshwa asubuhi na jioni, mpaka Saa ifike."

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ

"Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!"

¹ Ahmad 6:248.

² Muslim 1:410.

³ At-Tabari 21:396.

Watu wa Firauni ni kama ngamia wapumbavu, wanaojikwaa katika mawe na miti bila ya kufikiri. "Imam Ahmad ameandika kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما, alisema, "Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ أَحَدَكُمْ إِذَا مَاتَ عَرِضَ عَلَيْهِ مَقْعَدُهُ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ، إِنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ فَمِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ، وَإِنْ كَانَ مِنْ أَهْلِ النَّارِ فَمِنْ أَهْلِ النَّارِ، فَيُقَالُ: هَذَا مَقْعَدُكَ حَتَّى يَبْعَثَكَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِلَيْهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*"Mmoja wenu anapofariki, huoneshwa mahali pake Peponi au Jahanamu asubuhi na jioni; kama ni katika watu wa Peponi, basi yeye katika watu wa Peponi, na kama ni katika watu wa Jahanamu, basi yeye ni katika watu wa Jahanamu. Ataambiwa, hapa ni mahali pako mpaka Allah Atakapokufufua kupa endea katika Siku ya Klama."*¹

Pia imesimuliwa katika Sahihi Mbili.²

وَإِذْ يَتَحَاوُونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعْفَتُو لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا إِنَّ اللَّهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٨﴾ وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخَزَنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ عَنَّا يَوْمًا مِنَ الْعَذَابِ ﴿٤٩﴾ قَالُوا أَوْلَمْ تَأْتِيَكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ قَالُوا بَلَىٰ قَالُوا فَأَدْعُوا^ط وَمَا دُعَاؤُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٥٠﴾

47. Na watapohojiana huko Motoni, wanyonge watawaambia waliojitukuza: Hakika sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, hamtuondolei sehemu ya huu Moto?

48. Watasema waliojitukuza: Hakika sote sisi tumo humo humo! Kwani Mwenyezi Mungu keshahukumu baina ya viumbe!

¹ Ahmad 2:1143.

² Fat'h Al-Bari 3:286, Muslim 4:2199.

49. Na walio Motoni watawaambia walinzi wa Jahannamu: Muombeni Mola wenu Mlezi Atupunguzie walau siku moja ya adhabu.

50. Nao watasema: Je! Hawakuwa wakikufikieni Mitume wenu kwa hoja zilizo wazi? Watasema: Kwani? Watasema: Basi ombeni! Na maombi ya makafiri hayawi ila ni ya kupotea bure.

Mabishano ya Watu wa Jahanamu

Allah تعالي Anatuambia jinsi watu wa Jahanamu watakavyobishana na kujadiliana, na Firauni na watu wake - watakuwa miongoni mwao. Watu madhaifu ambao walikuwa wafuasi, watawaambia walio jeuri, ambao ni viongozi na wakuu:

إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا

“Hakika sisi tulikuwa wafuasi wenu.”

Yaani, ‘tulikutiini na kuzingatia wito wenu kwenye ukafiri na upotovu duniani,

فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ

“...basi je, hamtuondolei sehemu ya huu Moto?”

Yaani, ‘je, mtatubebea sehemu ya mizigo yetu.’

قَالَ الَّذِينَ أَسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا

“Watasema waliojitukuza: Hakika sote sisi tumo humo humo!”

Maana yake, ‘hatutakubebeeni mzigo wenu; adhabu yetu wenyewe inatutosha.’

إِنَّ اللَّهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ

“Kwani Mwenyezi Mungu keshahukumu baina ya waja!”

Yaani, ‘Ametupa adhabu baina yetu kulingana na kila mmoja anavyostahiki’.

Hii inafanana na Aya:

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ وَلٰكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

“Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui tu.” (7:38)

وَقَالَ الَّذِينَ فِي النَّارِ لِخَزَنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ عَنَّا يَوْمًا مِّنَ الْعَذَابِ ﴿٧٩﴾

“Na walio Motoni watawaambia walinzi wa Jahannamu: Muombeni Mola wenu Mlezi Atupunguzie walau siku moja ya adhabu.”

Wanajua kuwa Allah تعالى Hatawajibu na hatawasikia dua yao, kwa sababu Alisema,

أَحْسَعُوا فِيهَا وَلَا تَكْلُمُونَ ﴿١٠٨﴾

“Atasema Mwenyezi Mungu: Tokomeeni humo, wala msinisesemeshe.” (23:108),

Hivyo watawaomba walinzi wa Jahanamu, ambao ni askari jela wanao-wachunga watu wa Jahanamu, wamuombe Allah تعالى Awahafifishie Moto angalau kwa siku moja. Lakini walinzi hao wa Jahanamu watakataa, na kuwaambia,

أَوْلَمْ تَأْتِيَكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنَاتِ ۗ

“Je! Hawakuwa wakikufikieni Mitume wenu kwa hoja zilio wazi?”

Maana yake, haikuwa dalili iliyowekwa duniani kwa midomo ya Mitume,

قَالُوا بَلَىٰ ۗ قَالُوا فَأَدْعُوا ۗ

“Watasema: Kwani? Watasema: Basi ombeni!”

Yaani, mko peke yenu. Hatutakuombeeni wala kukusikilizeni; hatutaki muokoke na hatuna la kukufanyieni. Zaidi ya hayo, tunakuambieni kuwa vyovyote ni sawa, mkiomba dua ama la, kwa sababu Allah تعالى Hatajibu na Hatakuhafifishieni adhabu.’ Watasema:

وَمَا دُعَاؤُا الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ

“Na maombi ya makafiri hayawi ila ni kupotea bure.”

Yaani, haitakubaliwa wala kujibiwa.

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ
 يَقُومُ ٱلْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعذِرَتُهُمْ
 وَلَهُمُ ٱللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ ٱلدَّارِ ﴿٥٢﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى
 ٱلْهُدَىٰ وَأَوْرَثْنَا بَنِي إِسْرَءِيلَ ٱلْكِتَآبَ ﴿٥٣﴾ هُدَىٰ
 وَذِكْرَىٰ لِأُولَى ٱلْأَلْبَآبِ ﴿٥٤﴾ فَاصْبِرْ إِن وَعْدَ ٱللَّهِ
 حَقٌّ وَٱسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ بِٱلْعَشِيِّ
 وَٱلْإِبْكَارِ ﴿٥٥﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي ءَايَاتِ ٱللَّهِ
 بِغَيْرِ سُلْطَنٍ أَتَتْهُمْ إِن فِي صُدُورِهِمْ إِلَّا كِبْرٌ مَّا هُمْ
 بِبَٰلِغِيهِ ۗ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ ۗ إِنَّهُ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ﴿٥٦﴾
 لَخَلَقَ ٱلسَّمَوَاتِ ٱلْأَرْضِ أَكْبَرَ مِنْ خَلْقِ ٱلنَّاسِ وَلَٰكِن
 أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٧﴾ وَمَا يَسْتَوِي ٱلْأَعْمَىٰ
 وَٱلْبَصِيرُ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا ٱلصَّٰلِحَاتِ وَلَا ٱلْمُشْرِكُونَ ۗ
 قَلِيلًا مَّا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٨﴾ إِنَّ ٱلسَّاعَةَ لَأْتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا
 وَلَٰكِن أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٩﴾ وَقَالَ رَبُّكُمْ
 ٱدْعُونِيٓ أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَن عِبَادَتِي
 سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَآخِرِينَ ﴿٦٠﴾

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ ٱلْأَشْهَادُ
 ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ
 مَعذِرَتُهُمْ ۗ وَلَهُمُ ٱللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ
 ٱلدَّارِ ﴿٥٢﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى
 ٱلْهُدَىٰ وَأَوْرَثْنَا بَنِي إِسْرَءِيلَ
 ٱلْكِتَآبَ ﴿٥٣﴾ هُدَىٰ وَذِكْرَىٰ
 لِأُولَى ٱلْأَلْبَآبِ ﴿٥٤﴾ فَاصْبِرْ إِن
 وَعْدَ ٱللَّهِ حَقٌّ وَٱسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ
 وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ بِٱلْعَشِيِّ
 وَٱلْإِبْكَارِ ﴿٥٥﴾ إِنَّ ٱلَّذِينَ
 يُجَادِلُونَ فِي ءَايَاتِ ٱللَّهِ بِغَيْرِ
 سُلْطَنٍ أَتَتْهُمْ إِن فِي صُدُورِهِمْ إِلَّا
 كِبْرٌ مَّا هُمْ بِبَٰلِغِيهِ ۗ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ
 ۗ إِنَّهُ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ﴿٥٦﴾

51. Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume

Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi,

52. Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa.

53. Na kwa hakika Tulimpa Musa uwongofu, na Tukawarithisha Wana wa Israeli Kitabu,

54. Ambacho ni Uwongofu na Ukumbusho kwa wenye akili.

55. Basi subiri. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na omba msamaha kwa dhambi zako, na umtakase Mola wako Mlezi kwa kumsifu jioni na asubuhi.

56. Hakika hao wanaobishana katika Aya za Mwenyezi Mungu bila ya dalili yoyote iliyowajia, hawana vifuani mwao ila kutaka ukubwa tu, na wala huo hawaufikili. Basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.

Ushindi wa Mtume ﷺ na Waumini.

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani...”

As-Suddi, “Allah تعالى Hatumi Mtume kwa watu na wao kumuua au baadhi ya waumini wanaowalingania ukweli, kisha kizazi hicho kikaondoka, Huwapelekea wa kusaidia wito wao na kutafuta kisasi kwa ajili ya damu yao kutoka kwa waliowafanyia hayo duniani. Hivyo, Mitume na waumini wanaweza kuuliwa duniani, lakini wito wao utaendelea kuwepo duniani.”¹

Allah تعالى Alimpa ushindi Mtume Wake Muhammad ﷺ na Masahaba Wake juu ya waliompinga, waliomkataa na kumfanyia uadui. Alilifanya neno Lake na dini Yake kuwa juu ya dini zote zingine, Alimuamrisha Mtume Wake ahamie Madinah, ambapo alimpa wasaidizi. Kisha Akampa ushindi juu ya washirikina katika Siku ya Badr, Alipompa ushindi juu yao na Akawadhalilisha, kwa kuwaua viongozi wao na kuwateka wasomi wao, kwa kuwafunga minyororo. Kisha Akawafanyia wema kwa kukubali fidia zao. Punde baada ya hapo, Allah تعالى alimwezesha kuikomboa Makkah, na akafurahi kurejea katika ardhi Tukufu ya

¹ At-Tabari 11:401.

nyumbani, *Al-Haram*. Kupitia kwake, Allah تعالى Akaunusuru mji na ukafiri na Shiriki.

Kisha Allah تعالى Akamuezesha kuikomboa Yemen, na Rasi yote ya Uarabuni kujisalimisha kwake, na watu wakaingia katika Dini ya Allah تعالى kwa makundi. Kisha Allah تعالى Akamchukua (katika mauti), kwa sababu ya daraja yake ya juu, na Aliwaweka Masahaba wake kama Makhalifah. Waliifikisha Dini ya Allah تعالى kutokea kwake, wakiwalingania watu kwa Allah تعالى, walikomboa maeneo mengi, nchi na miji mingi, na walifungua nyoyo za watu, mpaka wito wa Muhammad ﷺ ulienea kote duniani, mashariki na magharibi. Dini hii itaendelea kuwa juu mpaka Saa ifike. Allah تعالى Anasema:

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi.”

Maana yake, katika Siku ya Kiama ushindani utakuwa mkubwa zaidi na kamilifu. Mujahid alisema, “Mashahidi ni Malaika.”¹

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ

“Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao.”

Inakusudia sawa na;

وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ

“...na siku wataposimama Mashahidi.”

Wengine huisoma kwa maana ya;

وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥٢﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ

“...na siku wataposimama Mashahidi, Siku ambayo haitawafaa madhaalimu...”

Na madhaalimu ni washirikina.

¹ At-Tabari 21:402

مَعْدِرَتِهِمْ

“...udhuru wao.”

Yaani, hawatakubaliwa udhuru au kutoa fidia.

وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ

“Nao watapata laana.”

Yaani, watatupwa mbali na Rehema ya Allah تعالى.

وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ

“...na watapata makaazi mabaya kabisa.”

Yaani, moto wa Jahanamu, kama As-Suddi alivyosema, makazi mabaya mno.

Ishara kuwa Mtume ﷺ na Waumini Watapata Ushindi kama Musa عليه السلام na Bani Israel Walivyoshinda.

Allah تعالى Anasema:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْهُدَىٰ

“Na kwa hakika Tulimpa Musa uwongofu.”

Yaani, uongofu na nuru Aliyowapa Allah تعالى.

وَأَوْزَنَّا بَنِي إِسْرَائِيلَ الْكِتَابَ

“...na Tukawarithisha Wana wa Israeli Kitabu.”

Yaani, ‘Tuliwapa ushindi mwishoni na walirithi ardhi na walikusanya mali ya Firauni, kwa sababu ya subira yao katika kumtii Allah تعالى na kumfuata Mtume Wake Musa عليه السلام.’ Kitabu walichorithi, Taurati, kilikuwa,

هُدًى وَذِكْرَىٰ لِأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿٥١﴾

“Ambacho ni Uwongofu na Ukumbusho kwa wenye akili.”

Yaani, mazuri na ya mwenendo mwema.

فَاصْبِرْ

“Basi subiri.” Yaani, ‘Ewe Muhammad’,

إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ

“Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli.”

Yaani, ‘Tumeahidi kuwa neno lako litashinda na kwamba ushindi mkubwa utakuwa wenu na wanaokufuatieni, na Allah تعالى Havunji Ahadi Yake. Tulicho-kuambieni ni kweli na hakuna shaka yoyote ndani yake.’

وَأَسْتَغْفِرُ لَذَنْبِكَ

“Na omba msamaha kwa dhambi zako.”

Hii inausajjiisha ummah kuomba msamaha.

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ بِالْعَشِيِّ

“...na umtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi jioni...”

Maana yake, mwishoni mwa siku na mwanzoni mwa usiku,

وَالْأَبْكَرِ

“...na asubuhi.” Maana yake, mwanzoni mwa siku na mwishoni mwa usiku.

إِنَّ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ بِغَيْرِ سُلْطَانٍ أَتَاهُمْ

“Hakika hao wanaobishana katika Ishara za Mwenyezi Mungu bila ya uthibitisho wowote uliyowajia.”

Yaani, wanajaribu kukataa ukweli kwa kutumia upotovu, na kukataa ushahidi makini kwa hoja zisizo na uhakika, zisizo na dalili au ushahidi kutoka kwa Allah تعالى.

إِنَّ فِي صُدُورِهِمْ إِلَّا كِبْرًا مَا هُمْ بِبَالِغِيهِ

“...hawana vifua ni mwao ila kutaka ukubwa tu, na wala huo hawaufikilii.”

Yaani, wao pia katika vifua vyao mna kiburi cha kukataa kufuata ukweli na kumnyenyekeka Mmoja Aliyeuleta. Lakini jaribio lao kutaka kuuondoa ukweli na kuinua juu batili litashindwa; ukweli utashinda na maneno yao na lengo lao litafeli.

فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ

“Basi jikinge kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, kutokana na hali ya viumbe kama hawa.

إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.”

Au kumuomba hifadhi dhidi ya kuwa kama watu hao wanaobisha Aya za Allah تعالى bila ya kupata mamlaka yoyote.

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥١﴾
 وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَلَا الْمُسِيءُ قَلِيلًا
 مَا تَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٢﴾ إِنَّ السَّاعَةَ لَأْتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا
 يُؤْمِنُونَ ﴿٥٣﴾

57. Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.

58. Na kipofu na mwenye kuona hawalingani; na walioamini na watendao mema hawalingani na muovu. Ni machache mnayoyakumbuka.

59. Hakika Saa (ya Kiyama) itafika, nayo haina shaka. Lakini watu wengi hawaamini.

Uhai Baada ya Mauti

Allah تعالى Anatuambia kuwa Atawarejesha Viumbe Wake katika Siku ya Kiama. Hilo ni jepesi mno Kwake, kwa sababu Aliumba mbingu na ardhi, na hilo ni jambo kubwa zaidi kuliko Kuwaumba wanadamu mara ya kwanza na pale Atakapowaumba tena. Mwenye Uweza wa hilo Anaweza Kufanya chochote chini ya hilo.

Kama Anavyosema Allah تعالى:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْ يَخْلُقْهُنَّ بِقَدْرِ عَلَىٰ أَنْ سُحِّيَ
الْمَوْتِ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٣﴾

“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”
(46:33)

Na Allah تعالى Anasema hapa:

لَخَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٣﴾

“Bila ya shaka Kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko Kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.”

Hivyo, hawafikiri au kutafakari dalili Zake. Kadhalika, Waarabu wengi walitambua kuwa Allah تعالى Aliumba mbingu na ardhi, lakini walipinga na kukataa dhana ya ufufuo; walilikiri jambo lililokuwa kubwa zaidi kuliko walilolikataa. Kisha Allah تعالى Anasema:

وَمَا يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَلَا الْأُمِّيَّةُ قَلِيلًا مَّا
تَتَذَكَّرُونَ ﴿٣٤﴾

“Na kipofu na mwenye kuona hawalingani; na walioamini na watendao mema hawalingani na muovu. Ni machache mnayo yakumbuka.”

Kipofu asiyeona kitu chochote halingani na mtu anayeona kila kitu kadiri ya macho yake yanavyoweza kuona – wanatofautiana sana. Halikadhalika, waumini na makafiri hawalingani.

قَلِيلًا مَّا تَتَذَكَّرُونَ

“Ni machache mnayoyakumbuka.” Yaani, watu wengi hukumbuka machache.

إِنَّ السَّاعَةَ لَأْتِيَةٌ

“Hakika Saa (ya Kiyama) itafika.” Yaani, itakuja kwa hakika.

لَا رَيْبَ فِيهَا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ

“Hakika Saa (ya Kiyama) itafika, nayo haina shaka. Lakini watu wengi hawaamini.”

Yaani, hakika wana mashaka juu ya kuwepo kwake.

وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

60. Na Mola wenu Mlezi Anasema: Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhaliike.

Amri ya Kumuomba Allah تعالیٰ kwa Rehema Zake na Wema,

Allah تعالیٰ Anawashajiisha waja Wake wamuombe Yeye, na Anawahakikishia majibu. Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالیٰ alikuwa akisema: “Ewe Unayewapenda sana wanaokuomba, na Ewe Unayewachukia sana wasiokuomba, na hakuna Mwenye sifa hiyo isipokuwa Wewe, Ewe Mola Wangu Mlezi.” Hayo yaliandikwa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالیٰ. Kadhalika; imekuja katika shairi:

“Allah Hachukii kuombwa, ilhali mwanadamu hapendi kuombwa.”

Qatadah alisema kuwa Ka’b Al-Ahbar alisema, “Ummah huu umepewa mambo matatu ambayo haukupewa umma wowote uliotangulia, isipokuwa Mtume. Allah تعالیٰ Alipomtuma Mtume, alimuambia, ‘Wewe ni shahidi wa umma wako.’ Lakini nyinyi mmefanywa mashahidi juu ya watu; Kila Mtume ﷺ Alimuambia, ‘Allah تعالیٰ Hajakuekea ugumu katika dini,’ lakini aliuambia Ummah huu kwa ujumla:

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

“Wala Hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini.” (22:78)

Na kila Mtume aliambiwa; ‘Niombe Nitakujibu,’ lakini Aliuambia Ummah huu,

¹Al-Qurtubi 15:327.

أَدْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ^١

“Niombeni Nitakuitikieni.”

Haya yalinukuliwa na Ibn Abi Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى.

Imam Ahmad ameandika kuwa Al-Nu'man bin Bashir رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ الدُّعَاءَ هُوَ الْعِبَادَةُ»

“Hakika, Dua ni ibada.” Akasoma,

أَدْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ^٢ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

“Na Mola wenu Mlezi Anasema: Niombeni Nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhallilike.”^١

Haya pia yaliandikwa na wakusanyaji wa Sunan; At - Tirmidhi, An-Nasa'i, Ibn Majah, na Ibn Abi Hatim na Ibn Jarir. At -Tirmidhi alisema, *“Hasan Sahih.”*^٢ Pia yameandikwa na Abu Dawud, At -Tirmidhi, An-Nasa'i, na Ibn Jarir kwa silsila tofauti ya riwaya.^٣ Kauli ya Allah تَعَالَى:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi...”

Yaani, 'pia walijisikia fahari kuniomba na kunipwekesha Mimi,'

سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

“...wataingia Jahannamu wadhallilike.”

Yaani, huku wamefedheheka. Imam Ahmad ameandika kutoka kwa 'Amr bin Shu'ayb kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake kuwa Mtume ﷺ alisema:

¹ Ahmad 4:271.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:308, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:405, Ibn Majah 2:1258, At-Tabari 21:406, 407.

³ Abu Dawud 1:161, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:121, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:450.

⁴ Ahmad 1:179 Uk. 495.

«يُخَشِرُ الْمُتَكَبِّرُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَمْثَالَ الذَّرِّ فِي صُورِ النَّاسِ، يَغْلُوهُمْ كُلُّ شَيْءٍ مِنْ الصَّغَارِ، حَتَّى يَدْخُلُوا سِجْنًا فِي جَهَنَّمَ يُقَالُ لَهُ: بُولَسُ، تَغْلُوهُمْ نَارُ الْأَنْبَارِ، يُسْقَوْنَ مِنْ طِينَةِ الْخَبَالِ، عُصَاةَ أَهْلِ النَّارِ»

“Wenye kiburi watakusanywa katika Siku ya Kiama wakiwa kama sisimizi katika sura za watu, na kila kitu kitawakanyaga, kwa kuwadhalilisha, mpaka waingie katika jela ya Jahanamu inayoitwa Bulas. Watalishwa miale ya moto, na kupewa (twinatil - khabaal) usaha wa watu wa Motoni.”

* * *

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ أَلْيَلٍ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۗ
 إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا
 يَشْكُرُونَ ﴿٦١﴾ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ خَلِيقَ كُلِّ شَيْءٍ لَّا
 إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَأَنَّى تُؤْفَكُونَ ﴿٦٢﴾ كَذَٰلِكَ يُؤْفَكُ الَّذِينَ
 كَانُوا بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴿٦٣﴾ اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ
 الْأَرْضَ قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ
 صُورَكُمْ وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ ۗ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۗ
 فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٤﴾ هُوَ الْحَيُّ لَا إِلَهَ
 إِلَّا هُوَ فَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۗ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ
 الْعَالَمِينَ ﴿٦٥﴾ * قُلْ إِنِّي نُهَيْتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ
 مِنْ دُونِ اللَّهِ لَمَّا جَاءَنِيَ الْآيَاتُ مِنْ رَبِّي وَأُمِرْتُ أَنْ أُسَلِّمَ
 لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٦﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ
 مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ يُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوا
 أَشْدَّكُمْ ثُمَّ لِتَكُونُوا شُيُوخًا ۗ وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَفَّىٰ مِنْ قَبْلُ
 وَلِتَبْلُغُوا أَجَلًا مُّسَمًّى وَلَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ هُوَ
 الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ ۗ فَإِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ
 فَيَكُونُ ﴿٦٨﴾

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ أَلْيَلٍ لِتَسْكُنُوا
 فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَذُو
 فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ
 النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦١﴾
 ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ خَلِيقَ كُلِّ
 شَيْءٍ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَأَنَّى تُؤْفَكُونَ
 ﴿٦٢﴾ كَذَٰلِكَ يُؤْفَكُ الَّذِينَ
 كَانُوا بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴿٦٣﴾
 اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ
 قَرَارًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَصَوَّرَكُمْ
 فَأَحْسَنَ صُورَكُمْ وَرَزَقَكُمْ مِنَ
 الطَّيِّبَاتِ ۗ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ ۗ
 فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٤﴾
 هُوَ الْحَيُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ
 فَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ ۗ
 الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٥﴾

61. Mwenyezi Mungu Aliyekufanyieni usiku ili

mpate kutulia humo, na mchana wa kuonea. Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye Fadhila juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru.

62. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi, Muumba wa kila kitu. Hapana aabudiwaye kwa haki ila Yeye; basi mnageuzwa wapi?

63. Namna hivi ndivyo walivyogeuzwa waliokuwa wakizikataa Aya za Mwenyezi Mungu.

64. Ni Mwenyezi Mungu Aliyekufanyieni ardhi kuwa ni pahala pa kukaa, na mbingu kuwa dari. Na Akakutieni sura, na Akazifanya nzuri sura zenu, na Akakuruzukuni vitu vizuri. Huyu Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.

65. Yeye Ndiye Aliye Hai - hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

Dalili za Allah تعالیٰ Juu ya Uwezo Wake na Tauhidi Yake

Allah تعالیٰ Anatumkumbusha kuhusu Rehema Zake kwa Viumbe Wake ambapo Aliwapa usiku ambao hupumzika, ili waweze kuziendea shughuli zao wakati wa mchana. Anawapa mchana mwangaza, ili waweze kusafiri na kushughulika.

إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ

“Hakika Mwenyezi Mungu bila ya shaka ni Mwenye Fadhila juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru.”

Yaani, hawashukuru kwa neema Alizowapa Allah تعالیٰ. Kisha Allah تعالیٰ Anasema:

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ خَلِقُ كُلِّ شَيْءٍ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi, Muumba wa kila kitu. Hapana mola ila Yeye;”

Yaani, Mmoja Anayefanya yote hayo ni Allah تعالیٰ, Mmoja, wa Pekee, Aliyeumba vyote, hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye.

فَأَنِّي تُؤْفَكُونَ

“...basi mnageuzwa wapi?”

Yaani, ‘kwanini muabudu masanamu yasiyoweza kuumba chochote bali yamechongwa tu kwa mikono.’

كَذَلِكَ يُؤْفِكُ الَّذِينَ كَانُوا بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ ﴿٦١﴾

“Namna hivi ndivyo walivyogeuzwa waliokuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.”

Yaani, kama Maquraysh hawa walivyopotoka kwa kuabudu miungu badala ya Allah تعالى, wale wa kabla yao pia walikufuru na kuabudu Miungu mingine, bila ya dalili au ushahidi, lakini kwa kufuata ujinga na tamaa. Walikataa ishara na dalili za Allah تعالى.

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ قَرَارًا

“Ni Mwenyezi Mungu Aliyekufanyieni ardhi kuwa ni pahala pa kukaa.”

Yaani, ‘Aliifanya imara na Kuitandaza kwa ajili yenu, ili muweze kuishi na kusafiri humo; Aliimarisha kwa milima ili isitingishike pamoja nanyi.’

وَالسَّمَاءُ بِنَاءٍ

“...na mbingu kuwa dari.”

Yaani, ‘paa linaloifunika na kuihifadhi dunia.’

وَصَوَّرَكُمْ فَأَحْسَنَ صُوَرَكُمْ

“Na Akakutieni sura, na Akazifanya nzuri sura zenu.” Yaani, ‘Amekuumbeni katika umbo bora kabisa.’

وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ

“...na Akakuruzukuni vitu vizuri.”

Yaani, vyakula na vinywaji duniani. Allah تعالى Anaeleza kuwa Ameumba mahali pa kuishi na pa wakaazi na pa riziki; Yeye ni Muumbaji na Mpaji, kama Alivyosema katika Surat Al-Baqarah:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٦٢﴾ الَّذِي

جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ

رِزْقًا لَكُمْ ۗ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أُنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٦٣﴾

“Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi Aliyekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka. (Mwenyezi Mungu) Ambaye Amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na Akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo Akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali nyinyi mnajua.” (2:21-22)

Na hapa Allah تعالى Anasema, baada ya Kutaja Uumbaji wa vitu vyote hivyo:

ذَلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَتَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

“Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu Mola wenu Mlezi. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Maana yake, Allah تعالى, Mola Mlezi wa ulimwengu wote.

Kisha Anasema:

هُوَ الْحَيُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Yeye Ndiye Aliye Hai - hapana mola isipokuwa Yeye.”

Yaani, Yeye Yuko Hai Daima, milele na milele, Ambaye Alikuwapo, Atakuwapo, Wa Mwanzo na Wa Mwisho, Aliye Dhahiri, Wa Ghaibu.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“La ilaha illa Huwa.”

Yaani, hakuna wa kufanana au kulingana na Yeye.

فَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

“Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye..”

Yaani, kiri UuMoja Wake kwa kutamka shahada kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipo kuwa Yeye. Kila Sifa Njema ni za Allah تعالى, Mola Mlezi wa Ulimwengu.

Imam Ahmad ameandika kuwa baada ya kukamilisha kila Sala, ‘Abdullah bin Az-Zubayr رضي الله عنه alikuwa akisema:

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْخَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لَا حَزَلٌ وَلَا قُوَّةٌ إِلَّا بِاللَّهِ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَلَا نَعْبُدُ إِلَّا إِيَّاهُ، لَهُ النُّعْمَةُ وَلَهُ الْفَضْلُ وَلَهُ الثَّنَاءُ الْحَسَنُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ»

“Hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Peke Yake, Hana mshirika, ni Wake Ufalme na Sifa, Yeye ni Muweza wa kila kitu, hakuna hila wala nguvu ya kufanya jambo isipokuwa Kwake Allah; hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah na hatumuabudu mwingine isipokuwa Yeye; Kwake Yeye kuna Neema na Fadhila na Sifa Njema; hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Allah, hali ya kumtakasia Yeye Dini, hata kama makafiri watachukia.”

Alisema, “Mtume ﷺ alikuwa akisoma *Tahlil* jinsi hizo baada ya kila Sala.”¹

Riwaya kama hiyo iliandikwa pia na Muslim, Abu Dawud na An-Nasa’i.²

• قُلْ إِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَعْبُدَ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَمَّا جَاءَنِيَ الْبَيِّنَاتُ مِنْ رَبِّي وَأُمِرْتُ أَنْ أُسْلِمَ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٦٦﴾ هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ يُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوا أَشُدَّكُمْ ثُمَّ لِتَكُونُوا شُيُوخًا وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَفَّى مِنْ قَبْلُ وَلِتَبْلُغُوا أَجَلًا مُّسَمًّى وَلَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ هُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ فَإِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٦٨﴾

66. Sema: Mimi nimekatazwa kuwaabudu hao mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, ziliponijia hoja zilizo dhaahiri kutokana na Mola wangu Mlezi. Na nimeamrisha nisilimu kwa Mola wa walimwengu wote.

67. Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha Akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha (Akakuwachen) ili mpate kufikilia wakati wa nguvu zenu kamili, kisha mpate kuwa wazee. Na kati yenu wapo wanaokufa kabla, na ili mfikie muda uliokwishawekwa, na ili mpate kufahamu.

¹ Ahmad 4:4.

² Muslim 1:415-416, Abu Dawud 2:173 - 174, An-Nasai 3:69, 70.

68. Yeye Ndiye Anayehuishia na Anayefisha. Akihukumu jambo liwe, basi Huliambia: Kuwa! Likawa.

Kuharamishwa Ushirikina, Kuamrisha Tawhid, na Ushahidi wa Yote hayo.

Allah تعالى Anasema, 'Ewe Muhammad, waambie hao washirikina, kwamba Allah تعالى Anakataza kumuabudu yeyote, kama vile masanamu na miungu batili.' Allah تعالى Anaeleza kuwa hakuna ghairi Yake anayestahiki kuabudiwa.

Kama Anavyosema:

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ مَخْرَجُكُمْ طِفْلاً ثُمَّ لِتَبْلُغُوا أَشُدَّكُمْ ثُمَّ لِتَكُونُوا شُيُوخًا

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha Akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha (Akakuwachen) ili mpate kufikilia wakati wa nguvu zenu kamili, kisha mpate kuwa wazee.”

Yaani, Yeye ni Mmoja tu, bila ya mwenza au mshirika, Anakupitisheni katika hatua hizi mbalimbali, na hayo hutokea kufuatia Amri Yake, Utashi na Hukumu.

وَمِنْكُمْ مَّنْ يُتَوَفَّىٰ مِنْ قَبْلُ

“Na kati yenu wapo wanaokufa kabla.”

Ya kuumbika kikamilifu na kuja duniani; na mimba inaharibika. Na wapo wanaokufa utotoni au katika ujana, au wanapokuwa wakubwa kabla ya kufikia uzeeni. Kama Allah تعالى Anavyosema:

لَيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيُقَرِّ فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى

“...ili Tukubainishieni. Nasi Tunakiweka katika matumbo ya uzazi Tunachokitaka mpaka muda uliowekwa.” (22:5).

وَلَيَبْلُغُوا أَجْلاً مُّسَمًّى وَلَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“...na ili mfikie muda uliokwisha wekwa, na ili mpate kufahamu.”

Ili muweze kukumbuka ufufuo.

Kisha Allah تعالى Anasema:

هُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ

“Yeye Ndiye Anayehuisha na Anayefisha.”

Maana yake, Yeye Ndiye Pekee Anayeyafanya hayo, na hakuna anayeweza kufanya hivyo isipokuwa Yeye.

فَإِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُن فَيَكُونُ

“Akihukumu jambo liwe, basi Huliambia: Kuwa! Likawa.”

Yaani, Hawezi kupingwa. Chochote Atakacho kitakuwa kwa hakika.

* * *

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ أَنِّي يُضَرِّفُونَ ﴿٦٩﴾
 الَّذِينَ كَذَّبُوا بِالْكِتَابِ وَمَا أَرْسَلْنَا بِهِ رُسُلَنَا^ط
 فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٧٠﴾ إِذِ الْأَغْلُلُ فِي أَعْنَاقِهِمْ
 وَالسَّلْسِلُ يُسْحَبُونَ ﴿٧١﴾ فِي الْحَمِيمِ ثُمَّ فِي النَّارِ
 يُسْجَرُونَ ﴿٧٢﴾ ثُمَّ قِيلَ لَهُمْ آيَاتِ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُونَ
 ﴿٧٣﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ قَالُوا صَلُّوا عَلَيْنَا بَل لَّمْ نَكُنْ نَدْعُوا
 مِنْ قَبْلُ شَيْعًا كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ الْكَافِرِينَ ﴿٧٤﴾ ذَلِكُمْ
 بِمَا كُنْتُمْ تَفْرَحُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَمَا كُنْتُمْ
 تَمْرَحُونَ ﴿٧٥﴾ أَدْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا^ط
 فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٦﴾ فَاصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ
 ﴿٧٧﴾ فَإِذَا نُزِيتُكَ بِعَظْمٍ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيْتُكَ فَإِلَيْنَا
 يُرْجَعُونَ ﴿٧٨﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِنْ قَبْلِكَ مِنْهُمْ مَنْ
 قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَنْ لَمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ وَمَا كَانَ
 لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِآيَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ فَإِذَا جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ
 قُضِيَ بِالْحَقِّ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْمُبْطِلُونَ ﴿٧٩﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِ اللَّهِ أَنِّي يُضَرِّفُونَ ﴿٦٩﴾
 الَّذِينَ كَذَّبُوا بِالْكِتَابِ وَمَا أَرْسَلْنَا بِهِ رُسُلَنَا^ط
 فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٧٠﴾ إِذِ الْأَغْلُلُ فِي أَعْنَاقِهِمْ
 وَالسَّلْسِلُ يُسْحَبُونَ ﴿٧١﴾ فِي الْحَمِيمِ ثُمَّ فِي النَّارِ
 يُسْجَرُونَ ﴿٧٢﴾ ثُمَّ قِيلَ لَهُمْ آيَاتِ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُونَ
 ﴿٧٣﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ قَالُوا صَلُّوا عَلَيْنَا بَل لَّمْ نَكُنْ نَدْعُوا
 مِنْ قَبْلُ شَيْعًا كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ الْكَافِرِينَ ﴿٧٤﴾ ذَلِكُمْ
 بِمَا كُنْتُمْ تَفْرَحُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَمَا كُنْتُمْ
 تَمْرَحُونَ ﴿٧٥﴾ أَدْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا^ط
 فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٦﴾

69. Je! Huwaoni wale wanaobishana katika Aya za Mwenyezi Mungu? Wanageuziwa wapi?

70. Ambao wamekanusha Kitabu na yale Tuliowatuma Mitume Wetu. Basi watakuja jua.

71. Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo, huku wanaburuzwa.

72. Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.

- 73. Tena wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha.**
- 74. Badala ya Mwenyezi Mungu? Watasema: Wametupotea, bali tangu zamani hatukuwa tukiwaomba kitu! Hivyo Ndivyo Mwenyezi Mungu Anawaachia makafiri wapotelee mbali.**
- 75. Haya ni kwa sababu mlikuwa mkijivuna katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mnafanya kiburi na maskhara.**
- 76. Ingieni kwenye milango ya Jahannamu, mdumu humo milele. Basi ni maovu yaliyoje makaazi ya wanaotakabari!**

Mwisho wa Matokeo ya Waliopinga na Kukataa Ishara za Allah تعالى

Allah تعالى Anasema, 'Huwashangai, Ewe Muhammad, waliokataa ishara za Allah تعالى na kupinga ukweli kwa njia batili, jinsi akili zao zilivyouacha ukweli na kupotoka.'

الَّذِينَ كَذَّبُوا بِالْكِتَابِ وَمَا أَرْسَلْنَا بِهِ رُسُلَنَا

"Ambao wamekanusha Kitabu na yale Tuliyouwatumia Mitume Wetu."

Yaani, uongofu na dalili za waziwazi.

فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ

"Basi watakuja jua."

Hili ni onyo kali na kitisho cha wazi kutoka kwa Mola Mlezi kwenda kwa watu hao. Hii inafanana na Aya:

وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ

"Ole wao, siku hiyo hao wanao kanusha!" (77:15)

إِذِ الْأَغْلَالُ فِي أَعْنَاقِهِمْ وَالسَّلْسِلُ

"Zitakapokuwa pingu shingoni mwao na minyororo."

Yaani, minyororo itafungwa katika nguzo za chuma, na walinzi wa Jahanamu watawaburuza juu ya nyuso zao, wakati mwingine kwenda kwenye maji yachemkayo, na wakati mwingine kwenye Moto. Allah تعالى Anasema:

يُسْحَبُونَ ﴿٧٦﴾ فِي الْحَمِيمِ ثُمَّ فِي النَّارِ يُسْجَرُونَ ﴿٧٧﴾

“...huku wanabururwa Katika maji ya moto, kisha wanaunguzwa Motoni.”

Hii inafanana na Aya:

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٤٣﴾ يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءانِ ﴿٤٤﴾

“Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikanusha. Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayo chemka.” (55:43-44).

Baada ya kueleza namna watakavyokula Zaqqum (mti mchungu wa Jahanamu) na kunywa Hamim (maji yanayochemka), Allah تعالى Anasema:

ثُمَّ إِنَّ مَرَجَعَهُمْ لِإِلَى الْجَحِيمِ ﴿٣٨﴾

“Kisha hakika marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannamu.” (37:68),

Na Allah تعالى Anasema:

وَأَصْحَابُ الشِّمَالِ مَآ أَصْحَابُ الشِّمَالِ ﴿٤١﴾ فِي سُمُومٍ وَحَمِيمٍ ﴿٤٢﴾ وَظِلٍّ مِّنْ تَحْتُمُومٍ ﴿٤٣﴾
لَّا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٤٤﴾

“Na watu wa kushotoni; je wana hali gani watu wa Kushotoni? (watakuwa) Katika upepo wa moto, na maji yanayochemka. Na kivuli cha moshi mweusi. Si cha kuburudisha wala kustarehesha.” mpaka,

ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيُّهَا الضَّالُّونَ الْمُكَذِّبُونَ ﴿٤٥﴾ لَأَكُلُونَ مِنْ شَجَرٍ مِّنْ زُقُومٍ ﴿٤٦﴾ فَمَا لِيُونَ مِنهَا
الْبُطُونَ ﴿٤٧﴾ فَشَرِبُونَ عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيمِ ﴿٤٨﴾ فَشَرِبُونَ شُرْبَ أَلْهِيمِ ﴿٤٩﴾ هَذَا نُزُّهُمُ
يَوْمَ الدِّينِ ﴿٥٠﴾

“Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokanusha, Kwa yakini mtakula mti wa Mzaqqumu. Na kwa mti huo mtajaza matumbo. Na juu yake

mtakunywa maji yanayochemka. Tena mtakunywa kama wanavyokunywa ngamia wenye kiu. Hiyo ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.” (56: 41-44, 51-56),

إِنَّ شَجَرَتَ الرَّقُومِ ﴿١٧﴾ طَعَامُ الْأَثِيمِ ﴿١٨﴾ كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ ﴿١٩﴾ كَغَلِي
الْحَمِيمِ ﴿٢٠﴾ خُدُّوهُ فَاعْتَلُوهُ إِلَىٰ سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٢١﴾ ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ
الْحَمِيمِ ﴿٢٢﴾ ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٢٣﴾ إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٢٤﴾

“Hakika Mti wa Mzaqqum. Ni chakula cha mwenye dhambi. Kama shaba iliyoyayushwa, hutokota matumboni kama kutokota kwa maji ya moto. (Itasemwa:) Mkamateni na mtupeni katikati ya Jahannamu! Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayochemka. Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu! Hakika haya ndiyo mliyokuwa mkiyatilia shaka.” (44:43-50)

Yaani, wataambiwa hayo kwa kukaripiwa na kufanyiwa kejeli.

ثُمَّ قِيلَ لَهُمْ أَيُّكُمْ كَفَرٌ ﴿٧٧﴾ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾ مِنْ دُونِ اللَّهِ

“Tena wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha, Badala ya Mwenyezi Mungu?”

Yaani, wataambiwa, ‘yako wapi masanamu mliyokuwa mkiyaabudu badala ya Allah? Yanaweza kukusaidieni leo?’

قَالُوا ضَلُّوا عَنَّا

“Watasema: Wametupotea.”

Yaani, yameondoka na hayawezi kutufanyia chochote.’

بَل لَّمَّا نَكُن نَدْعُوا مِنْ قَبْلُ شِيْعًا

“...bali tangu zamani hatukuwa tukiomba kitu!”

Yaani, watakana kuwa waliyaabudu. Hii inafanana na Aya:

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٦٩﴾

“Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Allah تعالیٰ Anasema:

كَذَلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ الْكَافِرِينَ

“Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anawaachia makafiri wapotelee mbali.”

ذَٰلِكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَفْرَحُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَإِذَا كُنْتُمْ تَمْرَحُونَ ﴿٧٠﴾

“...Haya ni kwa sababu mlikuwa mkijitapa katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mkijiona wajanja na werevu.”

Yaani, Malaika watawa ambia, ‘adhabu mnayopata sasa ni malipo yenu kwa kufurahia duniani bila ya haki yoyote, na kwa kuchupa kwenu mipaka.’

أَدْخَلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا فَبِئْسَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ

“Ingieni kwenye milango ya Jahannamu, mdumu humo milele. Basi ni maovu yaliyoje makaazi ya wanaotakabari!”

Yaani, ni makazi na mwisho mbaya, uliojaa udhalili na adhabu kali kwa waliokuwa jeuri na wakakataa ishara za Allah تعالیٰ na kukataa kupokea dalili Zake na ushahidi. *Allah Aalam.*

فَأَصْبِرْ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ فَإِمَّا نُرَبِّيكَ بِعِضِ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيكَ فَإِلَيْنَا يَرْجِعُونَ

﴿٧١﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ مِنْهُمْ مَنْ قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَّن لَّمْ نَقْضِصْ

عَلَيْكَ ۗ وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِبَيِّنَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ فَإِذَا جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ فُضِيَ بِالْحَقِّ

وَخَيْرَ هُنَالِكَ لِّلْمُتَبَلِّغِينَ ﴿٧٢﴾

77. Basi subiri, hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Na kama Tukikuonesha baadhi ya yale Tuliyoahidi au Tukikufisha, lakini wao watarudishwa Kwetu tu.

78. Na bila ya shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao Tumekusimulia khabari zao, na wengine Hatukukusimulia. Na haiwi Mtume alete Ishara yoyote ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Basi ikija Amri ya Mwenyezi Mungu patahukumiwa kwa Haki, na hapo wapotofu watapata khasara.

Amri ya kuwa na Subira na Habari Njema za Ushindi

Hapa Allah تعالى Anamuamuru Mtume Wake awe na subira kwa kukataliwa na jamaa zake.

‘Allah تعالى Atatimiza Ahadi Yake kwako kuwa utakuwa mshindi na utakuwa juu ya watu wako, na wewe na wafuasi wako, mtafaulu duniani na Akhera.’

فَأِمَّا تَرِينَاكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ

“Na ama Tukikuonesha baadhi ya yale Tuliyo waahidi...”

Yaani, duniani, na hayo ndiyo yaliyotokea, kwani Allah تعالى Aliwapa furaha ya kuwadhalilisha viongozi na wakuu (wa Quraysh), waliouliwa katika Siku ya Badr, kisha Allah تعالى Akawapa ushindi juu ya Makkah na Rasi yote ya Uarabuni wakati wa uhai wa Mtume ﷺ.

أَوْ تَتَوَفَّيْنَاكَ فَأَلَيْنَا يَرْجِعُونَ

“...au Tukikufisha, lakini wao watarudishwa Kwetu tu.”

Yaani, ‘na Tutawapa adhabu kali Akhera.”

Kisha Allah تعالى Anasema, katika kumfariji Mtume Wake:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ مِنْهُمْ مَّن قَصَصْنَا عَلَيْكَ

“Na bila ya shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako. Wengine katika hao Tumekusimulia khabari zao.”

Kama Allah تعالى Alivyosema pia katika Surat An-Nisa (Aya 164)’. Yaani, ‘Tumeeleza visa vya baadhi yao na watu wao walivyowakataa, lakini hatimaye Mitume walishinda.’

وَمِنْهُمْ مَّن لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ

“...na wengine hatukukusimulia.”

Na visa viko vingi zaidi ya vilivyosimuliwa, kama ilivyoelezwa katika *Surat An-Nisa'*. Kila sifa njema Anastahiki Allah تعالى.

وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِبَيِّنَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ

“Na haiwi Mtume alete Ishara yoyote ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hakuna Mtume aliyewafanyia miujiza watu wake isipokuwa baada ya kupewa idhini ya kuwaonesha ishara ya ukweli wa Ujumbe aliowaletea.

فَإِذَا جَاءَ أَمْرُ اللَّهِ

“Basi ikija Amri ya Mwenyezi Mungu...”

Yaani, adhabu na kisasi Chake kitakachowaenea makafiri,

فُضِيَ بِالْحَقِّ

“...huhukumiwa kwa Haki.”

Waumini wataokolewa na makafiri wataangamizwa. Allah تعالى Anasema:

وَحَسْبِرَ هُنَالِكَ الْمُبْطِلُونَ

“...na hapo wapotofu watakhasiri.”

* * *

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَتْعَمَ لِتَرْكَبُوا مِنْهَا وَمِنْهَا
 تَأْكُلُونَ ﴿٧٩﴾ وَلَكُمْ فِيهَا مَنفَعٌ وَلِتَبْلُغُوا عَلَيْهَا حَاجَةً
 فِي صُدُورِكُمْ وَعَلَى الْفُلْكِ تُحْمَلُونَ ﴿٨٠﴾
 وَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ فَأَيَّ آيَاتِ اللَّهِ تُنْكِرُونَ ﴿٨١﴾ أَلَمْ يَسْمُرُوا
 فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ
 كَانُوا أَكْثَرَ مِنْهُمْ وَأَشَدَّ قُوَّةً وَءِثَارًا فِي الْأَرْضِ فَمَا أَعْنَى
 عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾ فَلَمَّا جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم
 بِالْبَيِّنَاتِ فَرِحُوا بِمَا عِنْدَهُمْ مِنَ الْعِلْمِ وَحَاقَ بِهِمْ مَا
 كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٨٣﴾ فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَأَمْنَا
 بِاللَّهِ وَحَدِيثِهِ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٨٤﴾ فَلَمْ
 يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا ۗ سُنَّتَ اللَّهُ الَّتِي قَدْ
 خَلَتْ فِي عِبَادِهِ ۗ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَتْعَمَ
 لِتَرْكَبُوا مِنْهَا وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٩﴾
 وَلَكُمْ فِيهَا مَنفَعٌ وَلِتَبْلُغُوا عَلَيْهَا
 حَاجَةً فِي صُدُورِكُمْ وَعَلَى الْفُلْكِ
 تُحْمَلُونَ ﴿٨٠﴾ وَيُرِيكُمْ
 آيَاتِهِ فَأَيَّ آيَاتِ اللَّهِ تُنْكِرُونَ ﴿٨١﴾

79. Mwenyezi Mungu Aliyekuumbieni wanyama, mifugo, ili muwapande baadhi yao, na muwale baadhi yao.

80. Na katika hao mnayo manufaa kadhaa wa kadhaa, na mnapata kwao haja ziliomo vifuani mwenu; na mnachukuliwa juu yao, na juu ya marikebu.

81. Naye Anakuonesheni Ishara Zake. Basi Ishara gani za Mwenyezi Mungu mnazozikataa?

Mifugo pia ni Neema kutoka kwa Allah تعالی na Ishara Zake

Allah تعالی Anawakumbusha waja kuhusu neema Zake ikiwemo mifugo (Al-An'am) kwa ajili yao, ambao ni ngamia, ng'ombe na mbuzi; baadhi yao ni vipando na wengine chakula. Ngamia wanaweza kuendeshwa au kuliwa; na hutumika katika kubeba mizigo mizito katika safari za mbali. Mifugo ni chakula na maziwa yao ni kinywaji; pia hutumika kulima mashamba. Mbuzi huliwa na maziwa yao ni kinywaji na manyoya ya wanyama yalikuwa yakitumika kujengea mahema, mavazi na samani, kama tulivyoeleza katika Surat Al-An'am na Surat An-Nahl, na zingine. Allah تعالی Anasema hapa:

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَتَعْنَ لِتَرْكَبُوا مِنْهَا وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٩﴾ وَلَكُمْ فِيهَا مَنَفَعٌ
وَلِتَبْتَغُوا عَلَيْهَا حَاجَةً فِي صُدُورِكُمْ وَعَلَى الْفَلَكِ تَحْمَلُونَ ﴿٨٠﴾

“Mwenyezi Mungu Aliyekujaalieni nyama hoa, mifugo, ili muwapande baadhi yao, na muwale baadhi yao. Na katika hao mnayo manufaa kadhaa wa kadhaa, na mnapata kwao haja ziliomo vifuni mwenu; na mnachukuliwa juu yao, na juu ya marikebu.”

وَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ

“Naye Anakuonesheni Ishara Zake.”

Yaani, ‘dalili Zake na ushahidi duniani na katika nafsi zenu.’

فَأَيُّ آيَاتِ اللَّهِ تُنْكِرُونَ

“Basi Ishara gani za Mwenyezi Mungu mnazozikataa?”

Hamuezi kukana ishara Yake yoyote, isipokuwa kwa ukaidi na kiburi.

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا أَكْثَرَ مِنْهُمْ
وَأَشَدَّ قُوَّةً وَءَانَارًا فِي الْأَرْضِ فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨١﴾ فَلَمَّا جَاءَتْهُمْ
رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَرَحُوا بِمَا عِنْدَهُمْ مِنَ الْعِلْمِ وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٨٢﴾
فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدُّهُ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٨٣﴾
فَلَمْ يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا ۗ سُنَّتَ اللَّهُ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ ۗ وَخَيْرٌ
هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ ﴿٨٤﴾

82. Kwani hawakusafiri katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hawa, na wamewashinda kwa nguvu na majengo katika nchi. Wala hayakuwafaa hayo waliyokuwa wakiyachuma.

83. Walipowajia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi walifurahia kwa ilimu waliyokuwa nayo. Basi yakawazunguka waliyokuwa wakiyafanyia maskhara.

84. Walipoiona adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee, na tunaikataa miungu tuliyokuwa tukiishirikisha Naye.

85. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona adhabu Yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja Wake. Na hapo waliokufuru walipata khasara.

Mazingatio kwa Hali za Waliotangulia

Allah تعالیٰ Anatueleza kuhusu mataifa yaliyowakataa Mitume wao hapo zamani. Ameeleza adhabu kali waliyopata licha ya kuwa walikuwa wenye nguvu, Pia Ameeleza kuhusu alama walizoacha ardhini na mali nyingi walizozilimbikiza. Hayo yote hayakuwafaa chochote wala hayakuwazuia hata kidogo kupata adhabu ya Allah تعالیٰ. Hayo ni kwa sababu Mitume walipowafikia huku wakiwa na ishara za wazi na shuhuda zenye nguvu, hawakuwasikiliza. Badala yake, walitosheka na elimu waliyokuwa nayo, au waliyodai kuwa nayo, na walisema kuwa hawakuwa na haja na walicholetewa na Mitume. Mujahid alisema, “Walisema, ‘Sisi tunajua zaidi kuliko wao, hatutafufuliwa na hatutaadhibiwa.”¹ As-Suddi alisema, “Kwa ujinga wao, walifurahia elimu waliyokuwa nayo (ya kidunia). Hivyo Allah تعالیٰ Aliwapelekea adhabu ambayo hawakuweza kuikimbia wala kuizuia.”

وَحَاقَ بِهِم

“Basi yakawazunguka...” Yaani, iliwaenea.

مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ

“...hayo waliyokuwa wakiyafanyia maskhara.”

Yaani, waliyokuwa wakiikataa na kusema isingetokea,

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا

“Walipoiona adhabu Yetu...”

Yaani, walipoiona kwa macho yao adhabu iliyowafikia, walisema,

¹ At-Tabari 21:422.

قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدَّهُدْ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ

“Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee, na tunaikataa miungu tuliyokuwa tukiishirikisha Naye.”

Yaani, walikiri kuwa Allah تعالى ni Mmoja na waliikataa miungu batili, lakini huu ulikuwa wakati ambapo nyudhuru hazikufaa. Hii inafanana na aliyoyasema Firauni alipokuwa akighariki baharini:

ءَامَنْتُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَامَنْتُ بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾

“Naamini kuwa hapana mola ila yule waliyemuamini Wana wa Israeli, na mimi ni miongoni mwa walionyenyekaa!” (10:90)

Lakini Allah تعالى Alisema:

ءَالْقَنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾

“Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi!” (10:91)

Maana yake, Allah تعالى Hakumkubalia hilo, kwa sababu Aliikubali dua ya Mtume Wake Musa عليه السلام, aliposema,

وَأَشَدُّ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ

“Na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.” (10:88).

Allah تعالى Anasema hapa:

فَلَمْ يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا سُنَّتَ اللَّهُ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ

“Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona Adhabu Yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja Wake.”

Maana: Hii ni hukumu ya Allah تعالى kuhusu wote wanaotubu pale tu wanapoona adhabu. Toba yao haitakubaliwa. Kwa mujibu wa Hadithi ifuatayo:-

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَقْبَلُ تَوْبَةَ الْعَبْدِ مَا لَمْ يُغْرِغْهُ»

“Hakika Allah Aliyetukuka Anapokea toba ya Mja Wake muda ambapo roho haijafika kooni.”

Mara tu mauti yanapotoa mlio na roho kufika kooni, na mtu anayekufa kumuona Malaika (wa mauti) kwa hakika, basi hawezi tena kutubu. Allah تَعَالَى Anasema:

وَحَسِرَ هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ

“Na hapo waliokufuru walikhasiri.”

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Surah Ghafir*. Sifa Njema na Shukrani ni kwa Allah تَعَالَى.



Tafsiri ya Suratu Fussilat¹

Sura ya 41

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ فَصَّلَاتٍ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمْدٌ ﴿١﴾ تَنْزِيلٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾ كِتَابٌ فُصِّلَتْ
 ءَايَاتُهُ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣﴾ بَشِيرًا وَنَذِيرًا
 فَأَعْرَضَ أَكْثَرُهُمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿٤﴾ وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي
 أَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَفِي ءَاذَانِنَا
 حِجَابٍ فَأَعْمَلْنَا عَمَلُونَ ﴿٥﴾ قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ
 يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهُ وَاحِدٌ فَاسْتَقِيمُوا إِلَيْهِ
 وَاسْتَغْفِرُوهُ ۗ وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِينَ ﴿٦﴾ الَّذِينَ لَا يُؤْتُونَ
 الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٨﴾

حَمْدٌ ﴿١﴾ تَنْزِيلٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾
 كِتَابٌ فُصِّلَتْ ءَايَاتُهُ قُرْءَانًا
 عَرَبِيًّا لِّقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٣﴾ بَشِيرًا
 وَنَذِيرًا فَأَعْرَضَ أَكْثَرُهُمْ فَهُمْ لَا
 يَسْمَعُونَ ﴿٤﴾ وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي
 أَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَفِي ءَاذَانِنَا
 حِجَابٍ فَأَعْمَلْنَا عَمَلُونَ ﴿٥﴾

1. H'a Mim

2. Uteremsho huu umetoka
 kwa Mwingi wa Rehema,
 Mwenye Kurehemu.

3. Hiki ni Kitabu kilicho
 pambanuliwa Aya zake, cha

kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanaojua.

4. Kitoacho khabari njema, na chenye kuonya. Lakini wengi katika wao wame
 puuza; kwa hivyo hawasikii.

¹ Sura hii pia inaitwa Ha Mim As-Sajdah.

5. Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko kwa hayo unayo tuitia, na masikio yetu yana uziwi, na baina yetu na wewe lipo pazia. Basi wewe tenda, nasi tunatenda.

Sifa ya Qur'an, na Kauli za Wapingaji.

﴿حَمْر﴾ تَنْزِيلٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿٤١﴾

“H’a Mim. Uteremsho huu umetoka kwa Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.”

Yaani, Qur'an imeshuka kutoka kwa Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Hii inafanana na Aya:

قُلْ تَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ مِن رَّبِّكَ بِالْحَقِّ

“Sema: Ameiteremsha hii Roho Mtakatifu kutokana na Mola Wako Mlezi kwa haki.” (16:102).

وَإِنَّهُ لَتَنْزِيلُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٩٢﴾ تَزَلَّ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ ﴿١٩٣﴾ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ ﴿١٩٤﴾

“Na bila ya shaka hii ni Uteremsho wa Mola Mlezi wa walimwengu wote. Ameuteremsha Roho muaminifu, Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji.” (26:192-194).

كِتَابٌ فَصَّلَتْ آيَاتُهُ

“Hiki ni Kitabu kilichopambanuliwa Aya zake.”

Yaani, maana zake ziko dhahiri na hukumu zake ni bora na za hekima.

قُرْءَانًا عَرَبِيًّا

“...cha kusomwa kwa Kiarabu.”

Yaani, kwa sababu ni Qur'an dhahiri ya Kiarabu, maana zake ni sahihi na za kina na maneno yake ni ya waziwazi na hayatatanishi. Hii inafanana na Aya:

كِتَابٌ أَحْكَمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ ﴿١﴾

“Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi, kisha zikapambanuliwa, kilichotoka kwa Mwenye Hikima na Mwenye Khabari.”(11:1).

Yaani, ni ya kimiujiza katika maneno yake na katika maana zake.

لَا يَأْتِيهِ الْبَطُلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

“Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimete-remshwa na Mwenye Hikima, Msifiwa.” (41:42).

لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

“...kwa watu wanaojua.”

Yaani, mtindo huu wa wazi wazi utakuwa uko tayari kufahamika kwa wanazuoni wenye elimu mahiri katika elimu.

بَشِيرًا وَنَذِيرًا

“Kitoacho khabari njema, na chenye kuonya.”

Yaani, wakati mwingine inawapa bishara waumini, na wakati mwingine inawaonya makafiri.

فَأَعْرَضَ عَنْ أَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ

“Lakini wengi katika wao wamepuuza; kwa hivyo hawasikii.”

Yaani, Maquraysh wengi hawakuifahamu hata kidogo, licha ya kuwa iko waziwazi.

وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِيْ أَكِنَّةٍ

“Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko...”

Yaani, zimewekewa kizibo.

مِمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَفِيْ آذَانِنَا وَقْرٌ

“...kwa hayo unayotuitia, na masikio yetu yana uziwi.”

Yaani, 'hatusikii Ujumbe uliotuletea.'

وَمِنْ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ حِجَابٌ

"...na baina yetu na wewe lipo pazia."

'Basi unayoyasema hayatatufikia.'

فَاعْمَلْ إِنَّا عَمِلُونَا

"Basi wewe tenda, nasi tunatenda."

Yaani, endelea na njia yako, nasi tutaenda katika njia yetu, na hatutakufuata.

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ وَاحِدٌ فَاَسْتَقِيمُوا إِلَيْهِ وَاسْتَغْفِرُوهُ
وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِينَ ۖ الَّذِينَ لَا يُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٧﴾ إِنَّ
الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٨﴾

6. Sema: Hakika mimi ni mtu kama nyinyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi nyookeni sawa kumuendea Yeye, na mumtake msamaha, na ole wao wanaomshirikisha.

7. Ambao hawatoi Zaka na wanaikataa Akhera.

8. Hakika wanaoamini na wakatenda mema watakuwa na ujira usio na ukomo.

Wito wa Tawhid

Allah تعالى Anasema,

قُلْ

"Sema..." 'Ewe Muhammad, kuwaambia hao makafiri na washirikina,'

إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ وَاحِدٌ

"Hakika mimi ni mtu kama nyinyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu."

'Si kama haya masanamu na miungu batili mnaowaabudu. Allah تعالی ni Mmoja,'

فَأَسْتَقِيمُوا إِلَيْهِ

"Basi nyookeni sawa kumuendea Yeye."

Yaani, 'kumuabudu Yeye Peke Yake kwa unyoofu, kulingana na Aliyoku-amrisheni kupitia kwa Mitume Wake."

وَأَسْتَغْفِرُوهُ

"...na mumtake msamaha."

'Kwa madhambi yenu yaliyopita.'

وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِينَ

"...na ole wao wanaomshirikisha."

Yaani, wataangamia.

الَّذِينَ لَا يُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

"Ambao hawatoi Zaka ..."

'Ali bin Abi Talhah amesimulia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa inamaanisha ambao hawakushuhudia kuwa hakuna kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالی.¹ Hii ilikuwa pia rai ya 'Ikrimah.² Hii inafanana na Aya:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ﴿٩١﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿٩٢﴾

"Hakika amefanikiwa aliyeitakasa. Na hakika amekhasiri aliyeiviza." (91:9-10) Na;

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّى ﴿٨٧﴾ وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّى ﴿٨٨﴾

"Hakika amekwishafanikiwa aliyejitakasa. Na akakumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akasali." (87:14-15) Na;

¹ At-Tabari 21:430.

² At-Tabari 21:430.

فَقُلْ هَلْ لَكَ إِلَهٌ إِلَّا أَن تَزْكَىٰ ﴿١٨﴾

“Umuambie: Je! Unapenda kujitakasa?” (79:18)

Maana ya Zaka hapa ni kuitakasa nafsi, kwa kuiondolea sifa zote mbaya, na iliyo mbaya zaidi ni Ushirikina. Zaka ya mali imeitwa hivyo kwa sababu inatakasa mali, na pia ni njia ya kuizidisha, kuibariki na kuifanya iwe na manufaa zaidi, na njia ya kumsaidia mtu kuitumia kwenye mema.

Qatadah amesema, “Walizuia Zaka ya mali zao.” Dhahiri ya maelezo ya aya inaonesha hivyo kwa mujibu wa wanazuoni wengi wa *Tafsir*, na hii ni rai aliyoiipendelea Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى¹.

Lakini jambo hilo lina rai nyingi, kwa sababu wajibu wa Zaka ulianza katika mwaka wa pili baada ya Mtume ﷺ kuhama kwenda Madinah, kwa mujibu wa maelezo ya wanazuoni wengi. Si hivyo tu Aya hii ilishuka Makkah. Hata hivyo, haielekei kuwa hili halizuii uwepo wa kanuni ya kutoa sadaka na Zaka, kwani ilishaanza na kuamrisha mwanzoni mwa utume wa Mtume ﷺ, kama Anavyosema Allah تَعَالَى:

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ ۗ

“...na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake.” (6:141).

Ama kuhusu taratibu za Zaka na namna ya kuikokotoa kulingana na viwango vyake “Nusub” zilielezwa baada ya Mtume ﷺ kuhamia Madinah. Hivyo ndivyo tunavyoweza kuweka ulinganifu baina ya rai mbili hizo. Kadhalika, Sala ilifaradhiswa kabla ya mawio na kabla ya machweo mwanzoni mwa utume wa Mtume ﷺ ilikuwa katika usiku wa Isra’a, mwaka mmoja na nusu kabla ya Hijrah, ndipo Allah تَعَالَى Alimfaradhisia Mtume Wake Sala tano kila siku. Masharti na vipengele vya lazima vya Sala vilielezwa baadaye, hatua kwa hatua. *Allah Aalam*. Kisha Allah تَعَالَى Anasema:

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿١٨١﴾

“Hakika wanaoamini na wakatenda mema watakuwa na ujira usio na ukomo.”

¹ At-Tabari 21:431.

Mujahid na wengine walisema, "Hautakatika wala kupungua."

Sawa na Aya:

مُكْتَبِينَ فِيهِ أَبَدًا ﴿١٨﴾

"Wakae humo milele." (18:3)

عَطَاءً غَيْرَ مَجْذُوزٍ ﴿١١٠﴾

"Hicho ni kipawa kisio na ukomo." (11:108)

* * *

* قُلْ أُنِيتُمْ لَتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ
 وَتَجْعَلُونَ لَهُدْ أَنْدَادًا ۚ ذَٰلِكَ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٩﴾ وَجَعَلَ فِيهَا
 رَوَاسِيَ مِنْ فَوْقِهَا وَبَرَكَ فِيهَا وَقَدَّرَ فِيهَا أَقْوَامًا فِي أَرْبَعَةِ
 أَيَّامٍ سَوَاءً لِّلسَّاعِلِينَ ﴿١٠﴾ ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ وَهِيَ
 دُخَانٌ فَقَالَ لَهَا وَلِلْأَرْضِ آئِنْتِنَا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا قَالَتَا أَتَيْنَا
 طَائِعِينَ ﴿١١﴾ فَقَضَيْنَهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ فِي يَوْمَيْنِ وَأَوْحَىٰ
 فِي كُلِّ سَمَاءٍ أَمْرَهَا ۗ وَزَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ
 وَحِفْظًا ۗ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿١٢﴾ فَإِنْ أَعْرَضُوا
 فَقُلْ أُنذَرْتُمْ كَمَا صُعِقْتُمْ مِثْلَ صُعِقَةِ عَادٍ وَتَمُودَ ﴿١٣﴾ إِذْ
 جَاءَهُمُ الرُّسُلُ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا تَعْبُدُوا
 إِلَّا اللَّهَ ۗ قَالُوا لَوْ شَاءَ رَبُّنَا لَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً يَسْقَىٰ
 بِهِ كَافِرُونَ ﴿١٤﴾ فَأَمَّا عَادُ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ
 الْحَقِّ وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً ۗ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي
 خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنهُمْ قُوَّةً ۗ وَكَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿١٥﴾
 فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي أَيَّامٍ نَحْسَاتٍ
 لِنَنْذِرَهُمْ عَذَابَ الْآخِرَةِ ۗ وَكَانُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَكَانُوا
 فِي الْآخِرَةِ أَخْزَىٰ ۗ وَهُمْ لَا يُنصَرُونَ ﴿١٦﴾ وَأَمَّا ثَمُودُ
 فَهَدَيْنَهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَى الْهُدَىٰ ۗ فَأَخَذْتَهُمْ صَاعِقَةً
 الْعَذَابِ آهُونَ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٧﴾ وَجَبْنَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿١٨﴾

* قُلْ أُنِيتُمْ لَتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ
 الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ وَتَجْعَلُونَ لَهُدْ أَنْدَادًا
 ۚ ذَٰلِكَ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٩﴾ وَجَعَلَ فِيهَا
 رَوَاسِيَ مِنْ فَوْقِهَا وَبَرَكَ فِيهَا وَقَدَّرَ
 فِيهَا أَقْوَامًا فِي أَرْبَعَةِ أَيَّامٍ سَوَاءً
 لِّلسَّاعِلِينَ ﴿١٠﴾ ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى
 السَّمَاءِ وَهِيَ دُخَانٌ فَقَالَ لَهَا
 وَلِلْأَرْضِ آئِنْتِنَا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا قَالَتَا
 أَتَيْنَا طَائِعِينَ ﴿١١﴾ فَقَضَيْنَهُنَّ سَبْعَ
 سَمَوَاتٍ فِي يَوْمَيْنِ وَأَوْحَىٰ فِي كُلِّ
 سَمَاءٍ أَمْرَهَا ۗ وَزَيَّنَّا السَّمَاءَ الدُّنْيَا
 بِمَصْبِيحٍ وَحِفْظًا ۗ ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ
 الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿١٢﴾

9. Sema: Hivyo nyinyi
 mnamkataa aliyeumba
 ardhi katika siku mbili, na
 mnamfanyia washirika?
 Huyu Ndiye Mola Mlezi wa
 walimwengu wote.

10. Na Akaweka humo
 milima juu yake, na
 Akakarikia humo chakula
 chake katika siku nne.
 Haya ni sawa kabisa kwa
 wanaotaka kujua.

11. Kisha Akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi, Akaziambia hizo na ardhi: Njooi, kwa khiari au kwa nguvu! Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni watiifu.

12. Basi Akazifanya mbingu saba kwa siku mbili, na Akazipangia kila mbingu mambo yake. Na Tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua.

Baadhi ya Fafanuzi kuhusu Kuumbwa Ulimwengu

Allah تعالى Anawakanushia washirikina wanaoabudu miungu mingine badala ya Allah تعالى ingawa Yeye ni Muumbaji, Mtiishaji na Mdhibiti wa vitu vyote. Anasema:

قُلْ أَنتُمْ لَتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ وَتَجْعَلُونَ لَهُ أُنْدَادًا

“Sema: Hivyo nyinyi mnamkataa Aliyeumba ardhi katika siku mbili, na mnamfanyia washirika?”

Maana yake, ‘miungu batili mnyoishirikisha Kwake.’

ذَٰلِكَ رَبُّ الْعَالَمِينَ

“Huyu Ndiye Mola Mlezi wa walimwengu wote.”

Muumbaji wa vitu vyote ni Mola Mlezi wa viumbe wote. Hapa Aya;

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ

“Mungu Aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita.” (7:54).

Imeelezwa hapa kwa kina; Kuumbwa ardhi na mbingu na maelezo ya Kuumbwa kila kimoja kivyake. Allah تعالى Anasema kuwa kwanza Aliumba ardhi, kwa sababu ni msingi, na msingi lazima utangulie kujengwa, kisha paa. Allah تعالى Anasema katika sehemu nyingine:

هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi. Tena Akazielekea mbingu, na Akazifanya mbingu saba.” (2:29).

Kwa kuzingatia Aya:

ءَأَنْتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَدَهَا ﴿١٧﴾ رَفَعَ سَمَكَهَا فَسَوَّيْنَاهَا ﴿١٨﴾ وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا
وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿١٩﴾ وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحْنَهَا ﴿٢٠﴾ أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَهَا ﴿٢١﴾
وَالْجِبَالَ أَرْسَنَهَا ﴿٢٢﴾ مَتَاعًا لَكُمْ وَلِأَنْعَمِكُمْ ﴿٢٣﴾

“Je! Ni vigumu zaidi Kukuumbeni nyinyi au mbingu? Yeye Ndiye Aliyeijenga! Akainua kimo chake, na Akaitengeneza vizuri. Na Akautia giza usiku wake, na Akautokeza mchana wake. Na juu ya hivyo Ameitandaza ardhi. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake, na milima Akaisimamisha, Kwa ajili ya kukustaharesheni nyinyi.” (79:27-33)

Ayah hii inaeleza kuwa kutandazwa ardhi kulifanyika baada ya Kuumbwa mbingu, lakini ardhi yenyewe iliumbwa kabla ya mbingu kwa mujibu wa baadhi ya maandiko. Hilo lilikuwa jibu la Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, kama alivyoandika Al-Bukhari katika *Tafsir* ya Aya hii katika Sahihi yake. Aliandika kuwa Sa’id bin Jubayr alisema: “Mtu mmoja alimuambia Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: ‘Ninakuta katika Qur’an baadhi ya mambo yanayonitatiza:

فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾

“...hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.” (23:101),

وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٣٧﴾

“Watakabiliana wao kwa wao kuulizana.” (37:27),

وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

“Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.” (4:42),

وَاللَّهُ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٦٣﴾

“Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Lakini katika Aya hii walificha kitu. Allah تعالى Anasema:

﴿١٧﴾ ءَأَنْتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ بَنَاهَا

“Je! Ni vigumu zaidi Kukuumbeni nyinyi au mbingu? Yeye Ndiye Aliyeijenga!” mpaka,

﴿٢٠﴾ وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَلِكَ دَحَاهَا

“Na juu ya hivyo Ameitandaza ardhi.” (79:30)

Hivyo, Alitaja kwanza Kuumbwa mbingu kabla ya ardhi, kisha Akasema:

﴿٢١﴾ قُلْ أَنتُمْ كِتَابٌ لَكُمُ لَتَكْفُرُونَ بِالَّذِي خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ

“Sema: Hivyo nyinyi mnamkataa Aliyeumba ardhi katika siku mbili.” Mpaka Kauli Yake,

﴿٢٢﴾ طَائِعِينَ

“Tumekuja nasi ni watiifu.”

Hapa Alimaanisha Kuumbwa ardhi kabla ya mbingu. Na Anasema:

﴿٢٣﴾ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Maghfira.”

﴿٢٤﴾ عَزِيزًا حَكِيمًا

“Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.” (4:56).

﴿٢٥﴾ سَمِيعًا بَصِيرًا

“Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.” (4:58).

Kana kwamba Alikuwa hivyo na sasa si hivyo?

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, akajibu:

﴿٢٦﴾ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ

“...hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.” (23:101),

Hayo yatatokea litakapopulizwa Parapanda kwa mara ya kwanza.

فَصَبِقَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ

“...wazimie waliomo mbinguni na waliomo katika ardhi, isipokuwa aliyemtaka Mwenyezi Mungu.” (39:68),

Na katika wakati huo hakutakuwa na undugu kati yao, wala hawataulizana. Kisha parapanda itakapopulizwa tena,

وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ

“Watakabiliana wao kwa wao kuulizana.” (37:27).

Ama kuhusu Kauli Yake Allah تعالى،

وَاللَّهُ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ

“Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23) na .

وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا

“...Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.” (4:42),

Allah تعالى Atasamehe madhambi ya waumini wanyoofu, halafu washirikina watasema, ‘Hebu tuseme kuwa hatukumshirikisha Allah تعالى katika ibada.’ Kisha muhuri utapigwa juu ya midomo yao, na mikono yao itazungumza. Kisha itatambulika kuwa hakuna hata jambo moja litakalofichikana kwa Allah تعالى, na wakati huo huo,

يُودُّ الَّذِينَ كَفَرُوا

“...waliokufuru watatamani...” (4:42).

Allah تعالى Aliumba ardhi kwa siku mbili, kisha Aliziumba mbingu, kisha Akalingana sawa mbinguni na Akaipa umbo lake kwa siku mbili zingine. Kisha Akaitandaza ardhi, inamaanisha kuwa Aliiwekea maji na malisho. Na Aliumba milima, mchanga, viumbe visivyo hai, miamba na kila kitu baina yake, kwa siku mbili zingine. Hivyo ndivyo Alivyosema Allah تعالى:

دَحْنَهَا

“...Ameitandaza ardhi.” (79:30)

Na Kauli ya Allah تعالى:

خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ

“...Aliyeumba ardhi katika siku mbili.”

Hivyo, Aliumba ardhi na kila kitu kwa siku nne, na Aliziumba mbingu kwa siku mbili.

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Maghfira.”

Hivyo ndivyo Alivyoeleza Yeye Mwenyewe Sifa Zake, na hivyo ndivyo Alivyo. Chochote Allah تعالى Anachokitaka huwa, basi msipate utata kuhusu Qur’an, kwani yote inatoka kwa Allah تعالى.” Haya yaliandikwa na Al-Bukhari.¹

خَلَقَ الْأَرْضَ فِي يَوْمَيْنِ

“...Aliyeumba ardhi katika siku mbili.”

Yaani, siku ya Jumapili na Jumatatu.

وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ مِنْ فَوْقِهَا وَبَدْرًا فِيهَا

“Na Akaweka humo milima juu yake, na Akabarikia humo...”

Yaani, Aliibariki na Aliipa nishati ya kuweza kupandwa mbegu na kuleta mazao.

وَقَدَّرَ فِيهَا أَقْوَاتَهَا

“...na Akakadiria humo chakula chake...”

Yaani, riziki wanazohitaji watu wake na mahali pa kupanda na kuotesha mmea. Hayo yalikuwa katika siku ya Jumanne na Jumatano, ambazo pamoja na siku mbili zilizotangulia zinakuwa siku nne jumla.

¹ Fat’h Al-Bari 8:418.

فِي أَرْبَعَةِ أَيَّامٍ سَوَاءٍ لِّلسَّائِلِينَ

“...katika siku nne. Haya ni sawa kabisa kwa wanaouliza.”

Maana yake, kwa waliotaka kukuuliza kuhusu hilo, ili wajue. ‘Ikrimah na Mujahid walisema kuhusu Aya:

وَقَدَّرَ فِيهَا أَقْوَابَهَا

“...na Akakadiria humo chakula chake...”

“Aliweka katika kila ardhi ambayo haikufaa kwingine kokote.¹ “Ibn ‘Abbas, Qatadah na As-Suddi walisema, kuhusu Aya,

سَوَاءٍ لِّلسَّائِلِينَ

“Haya ni sawa kabisa kwa wanaouliza.”

Inamaanisha, “Kwa anayetaka kuuliza kuhusu hilo.”² Ibn Zayd alisema:

وَقَدَّرَ فِيهَا أَقْوَابَهَا فِي أَرْبَعَةِ أَيَّامٍ سَوَاءٍ لِّلسَّائِلِينَ

“...na Akabarikia humo na Akakadiria humo chakula chake katika siku nne. Haya ni sawa kabisa kwa wanaouliza.”

“Kwa yeyote anayehitaji riziki, Allah تعالى Humpimia kulingana na haja zake.”³ Hii inafanana na walivyosema kuhusu Aya:

وَأَتَّكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ

“Na Akakupeni kila mlichomuomba.” (14:34). Allahu Aalam.

ثُمَّ أَسْتَوَىٰ إِلَى السَّمَاءِ وَهِيَ دُخَانٌ

“Kisha Akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi.”

Yaani, mvuke unaopanda juu kutokea hapo wakati ilipoumbwa ardhi.

¹ At-Tabari 21:436.

² At-Tabari 21:438.

³ At-Tabari 21:438.

فَقَالَ لَهَا وَلِلْأَرْضِ آتِيَا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا

“...Akaziambia hizo na ardhi: Njoooni, kwa khiari au kwa nguvu!”

Maana yake, ‘itikia Amri Yangu na utiishwe kwenye hilo, kwa hiari au bila hiari.’

فَالْتَأْتَيْنَا طَائِعِينَ

“Tumekuja nasi ni watiifu.”

Yaani, ‘tumekuitikia kwa utiifu na kila unachotaka Kuumba kutokana nasi - malaika, majini na watu – wote watakutii.’

فَقَضَلَهُنَّ سَبْعَ سَمَوَاتٍ فِي يَوْمَيْنِ

“Basi Akazifanya mbingu saba kwa siku mbili.”

Yaani, Alimaliza Kuziumba mbingu saba kwa siku mbili zaidi, ambazo zilikuwa Alhamisi na Ijumaa.

وَأَوْحَىٰ فِي كُلِّ سَمَاءٍ أَمْرَهَا

“...na Akazipangia kila mbingu mambo yake.”

Yaani, Aliweka katika kila mbingu malaika aliyemuhitaji Yeye, na mambo Anayoyajua Yeye Peke Yake.

وَرَيْنَا السَّمَاءَ الدُّنْيَا بِمَصْبِيحٍ

“Na Tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa...”

Yaani, nyota na sayari ambazo watu wa duniani huziona ziking’aa.

وَحِفْظًا

“...na kwa ulinzi.”

Dhidi ya Mashetani, ili wasiwasikie Malaika hao juu.

ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ

“ Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua.”

Yaani, Aliyevitiisha vitu vyote katika Udhibiti Wake, Ajuaye Yote zikiwemo harakati za viumbe wake.

فَإِنْ أَعْرَضُوا فَقُلْ أَنْذَرْتُكُمْ صَاعِقَةً مِثْلَ صَاعِقَةِ عَادٍ وَثُمُودَ ﴿٩﴾ إِذْ جَاءَهُمْ الرُّسُلُ مِنْ
 بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۗ قَالُوا لَوْ شَاءَ رَبُّنَا لَأَنْزَلَ مَلَائِكَةً فَإِنَّا بِمَا
 أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ ﴿١٠﴾ فَأَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا
 قُوَّةً ۗ أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۗ وَكَانُوا بِعَابَتِنَا سَاهُونَ ﴿١١﴾
 فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي أَيَّامٍ نَحْسَاتٍ لِنُنذِرَهُمْ عَذَابَ الْحِزْيِ فِي الْحَيَاةِ
 الدُّنْيَا ۗ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَحْزَىٰ ۗ وَهُمْ لَا يُنصَرُونَ ﴿١٢﴾ وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا
 الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ فَأَخَذَتْهُمُ صَاعِقَةُ الْعَذَابِ آهُونَ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٣﴾ وَجِئْنَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿١٤﴾

13. Basi wakipuuzwa wewe sema: Nakuhadharisheni adhabu mfano wa adhabu ya A'di na Thamudi,

14. Walipowajia Mitume mbele yao na nyuma yao wakawaambia: Msimuabudu ila Mwenyezi Mungu! Wakasema: Angelitaka Mola wetu Mlezi bila ya shaka Angeliwateremsha Malaika. Basi sisi hakika tunayakataa hayo mliyotumwa.

15. Ama kina A'di walijivuna katika nchi bila ya haki, na wakasema: Nani aliyekuwa na nguvu kushinda sisi? Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu Aliyewaumba ni Mwenye Nguvu Kushinda wao? Na wao wakawa wanazikataa Ishara Zetu!

16. Basi Tuliwapelekea upepo wa kimbunga katika siku za ukorofi, ili Tuwaonjeshe adhabu ya Kuwahizi katika uhai wa duniani, na bila ya shaka adhabu ya Akhera ina hizaya zaidi, na wala wao hawatanusuriwa.

17. Na ama Thamudi Tuliwaongoza, lakini walipenda upofu kuliko uwongofu. Basi uliwachukua moto wa adhabu ya kuwafedhehi kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

18. Na Tukawaokoa walio amini na wakawa wanamcha-Mungu.

Onyo kwa Makafiri na Ukumbusho wa Kisa cha 'Ad na Thamud

Anasema: 'Sema, Ewe Muhammad, kuwaambia washirikina hao wanaokataa Ujumbe wa ukweli uliowaletea: kama mtayapa mgongo niliyokuleteeni kutoka kwa Allah تعالى, kisha ninakuonyeni kuhusu adhabu ya Allah تعالى kama yalivyoadhibiwa mataifa yaliyopita kwa kutowaamini Mitume. Kauli ya Allah تعالى,

صَعِقَةً مِّثْلَ صَعِقَةِ عَادٍ وَثَمُودَ

"...adhabu mfano wa adhabu ya A'di na Thamudi."

Na mataifa mengine kama hayo kutokana na vitendo vyao,

إِذْ جَاءَهُمُ الرُّسُلُ مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ

"Walipowajia Mitume mbele yao na nyuma yao."

Hii inafanana na Aya:

وَأَذْكُرُ أَحَا عَادٍ إِذْ أَنْذَرَ قَوْمَهُ بِالْأَحْقَابِ وَقَدْ خَلَّتِ الْيَدُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ

"Na mtaje ndugu wa kina A'di, alipowaonya watu wake kwenye vilima vya mchanga.¹ Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake..." (46:21).

Inamaanisha kuwa katika miji ya karibu, Allah تعالى Aliwatuma Mitume waliowaamrisha watu kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya mshirika, na waliwaletea habari njema na maonyo pia. Waliona adhabu ambayo Allah تعالى Aliwapelekea maadui Zake, na neema Alizowapa marafiki Zake, lakini licha ya hayo yote, hawakuwaamini. Kinyume chake, waliwakataa, na wakasema:

لَوْ شَاءَ رَبُّنَا لَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً طَيِّبًا

"Angelitaka Mola wetu Mlezi bila ya shaka Angeliwateremsha Malaika."

Maana yake, kama Allah تعالى Angewatuma Mitume, wangukuwa Malaika waliotumwa kutoka Kwake.

¹ Tao la vilima vya mchanga vya kusini mwa Rasi ya Uarabuni.

فَإِنَّا بِمَا أَرْسَلْنَا بِهِم كَفِرُونَ

“Basi sisi hakika Tunayakataa hayo mliyotumwa.”

Yaani, ‘kwa sababu nyinyi ni wanadamu tu; hatutakufuateni kwa sababu nyinyi ni watu tu, kama sisi.’

فَأَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوا فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ

“Ama kina A’di walijivuna katika nchi bila ya haki.”

Yaani, walikuwa majeuri, wakaidi na waasi.

وَقَالُوا مَنْ أَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً

“...na wakasema: Nani aliyekuwa na nguvu kushinda sisi?”

Walijifaharishia nguvu zao za kimwili; walidhani kuwa hayo yangewahifadhi dhidi ya adhabu ya Allah تعالى.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً

“Kwani wao hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu Aliyewaumba ni Mwenye Nguvu Kushinda wao?”

Yaani, je, hawatambui, wanapofanya uadui, kuwa Yeye ni Mwenye Uwezo Ambaye Aliumba vitu vyote na Aliwapa nguvu waliyonayo, na kwamba, shambulio Lake litakuwa kubwa mno. Hii inafanana na Aya:

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ

“Na mbingu Tumezifanya kwa Nguvu na Uweza na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye Uweza wa Kuzikunjua.” (51:47)

Walimpinga Allah تعالى waziwazi na walikanusha ishara Zake na wakamwasi Mtume Wake. Allah تعالى Amesema:

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا

“Basi Tuliwapelekea upepo wa kimbunga...”

Baadhi yao walisema kuwa huo ulikuwa upepo mkali; wengine walisema kuwa ulikuwa upepo wa baridi. Pia walisema kuwa ulikuwa upepo uliotoa sauti. Ukweli ni kuwa, ulikuwa na yote hayo, kwani ulikuwa upepo mkali ambao ulikuwa adhabu kali kwa wao kudanganyika na nguvu za kimwili. Pia baridi kali, kama Anavyosema Allah تعالى:

بَرِيحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ۝

“kwa upepo mkali usiozulika.” (69:6),

Yaani upepo wa baridi. Pia ulileta sauti kali. Kwa kuzingatia hilo, kuna mto maarufu huko mashariki ya kati unaoitwa Sarsar kwa sababu ya kuvuma maji yake wakati yanapotembea.

فِي أَيَّامٍ نَحْسَاتٍ

“...katika siku za ukorofi.”

Yaani, siku hizo mfululizo.

سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِينَ أَيَّامٍ حُسُومًا

“Masiku saba, na michana minane, mfululizo bila ya kusita.” (69:7).

Hii inafanana na Aya:

فِي يَوْمٍ نَحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ

“...katika siku korofi mfululizo.” (54:19)

Yaani, adhabu ilianza katika siku ya nuksi kwao, na nuksi hiyo iliendelea kuwapata,

سَبْعَ لَيَالٍ وَثَمَنِينَ أَيَّامٍ حُسُومًا

“Masiku saba, na michana minane, mfululizo bila ya kusita.” (69:7)

Mpaka wakaangamia wote, na udhalili wao duniani uliunganishwa na adhabu yao huko Akhera. Allah تعالى Anasema:

لِنُدَبِقَهُمْ عَذَابَ الْعِزِّي فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَخْزَىٰ

“...ili Tuwaonjeshe adhabu ya kuwafedhehesha katika uhai wa duniani, na bila ya shaka adhabu ya Akhera ina fedheha zaidi.”

Maana yake, kudhalilishwa zaidi.

وَهُمْ لَا يُنصَرُونَ

“...na wala wao hawatanusuriwa.”

Yaani, katika Akhera, kama ambavyo hawakusaidiwa duniani, na hawakuwa na wa kuwahifadhi dhidi ya Allah تعالى au kuwaokoa dhidi ya adhabu Yake.

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ

“Na ama Thamudi Tuliwaongoza.”

Ibn ‘Abbas, Abu Al-Aliyah, Sa’ id bin Jubayr, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd walisema, “Tuliwaeleza.”¹ Ath-Thawri alisema, “Tuliwaita.” Kauli ya Allah تعالى;

فَأَسْتَحِبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ أَهْدَىٰ

“...lakini walipenda upofu kuliko uwongofu.”

Yaani, ‘Tuliwaonesha ukweli na kuwadhihirishia kupitia ndimi za Mtume wao, Salih, lakini walimpinga na wali mkataa, na walimchinja ngamia (jike) wa Allah تعالى ambaye Alimfanya alama ya kuwaonya ukweli wa Mtume wao.’

فَأَخَذْتَهُمْ صَاعِقَةً الْعَذَابِ آهُونَ

“Basi uliwachukua moto wa adhabu ya kuwafedhehi...”

Yaani, Allah تعالى Aliwapelekea ukelele “Sayhah”, tetemeko la ardhi, fedheha, adhabu na mateso.

بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

“...kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.”

Yaani, kwa sababu ya ukafiri wao.

وَنَجَّيْنَا الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Na Tukawaokoa walio amini...” Yaani, ‘Tuliwaokoa hao kutoka miongoni mwao, na hawakudhurika.’ Allah تعالى Aliwaokoa pamoja na Nabii wao Saleh, kwa sababu walimuogopa Allah تعالى.

¹ At-Tabari 21:448.

وَيَوْمَ يُحْشَرُ أَعْدَاءُ اللَّهِ إِلَى النَّارِ فَهُمْ
 يُوزَعُونَ ﴿١٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا مَا جَاءُوهَا
 شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَرُهُمْ
 وَجُلُودُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٠﴾
 وَقَالُوا لِمَ لَجُّودِهِمْ لِمَ شَهِدْتُمْ
 عَلَيْنَا ۗ وَهُوَ خَلَقَكُمْ
 أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢١﴾
 وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَضِئُونَ
 مِنْهُ لِيُصْطَبِرُوا ۗ فإِنَّ
 الْمُعْتَدِينَ ﴿٢٢﴾ * وَقَيْضَنَا هُزُّ قُرْبَاءَ
 فَرَيْنُوا هُمْ مَا بَيْنَ
 أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ
 وَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي
 أَمْرِ قَدْ خَلَتْ
 مِنْ قَبْلِهِمْ مِنَ الْإِنْسِ ۗ
 إِنَّهُمْ كَانُوا خَسِيرِينَ ﴿٢٣﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا
 تَسْمَعُوا هَذَا الْقُرْآنَ
 وَاللَّغْوِ فِيهِ
 لَعَلَّكُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٤﴾
 فَلَنَذِيقَنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا عَذَابًا شَدِيدًا
 وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَشْرَ
 الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٥﴾
 ذَلِكَ جَزَاءُ
 أَعْدَاءِ اللَّهِ النَّارِ ۗ
 هُمْ فِيهَا دَارٌ مُّخَلَّدِينَ
 جَزَاءُ بِمَا كَانُوا
 بِغَايِبَتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٢٦﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ
 كَفَرُوا رَبَّنَا أَرِنَا
 الَّذِينَ أُضْلَلْنَا مِنَ
 الْإِنْسِ لِنَعْمَلَهُمَا
 نَحْتَأْتِدْهُمَا
 لِيَكُونُوا مِنَ
 الْأَسْفَلِينَ ﴿٢٧﴾

وَيَوْمَ يُحْشَرُ أَعْدَاءُ اللَّهِ إِلَى النَّارِ فَهُمْ
 يُوزَعُونَ ﴿١٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا مَا جَاءُوهَا
 شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَرُهُمْ
 وَجُلُودُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٠﴾
 وَقَالُوا لِمَ لَجُّودِهِمْ لِمَ شَهِدْتُمْ
 عَلَيْنَا ۗ وَهُوَ خَلَقَكُمْ
 أَوَّلَ مَرَّةٍ وَإِلَيْهِ
 تُرْجَعُونَ ﴿٢١﴾ وَمَا
 كُنْتُمْ تَسْتَضِئُونَ
 مِنْهُ لِيُصْطَبِرُوا ۗ
 فإِنَّ الْمُعْتَدِينَ ﴿٢٢﴾
 * وَقَيْضَنَا هُزُّ
 قُرْبَاءَ فَرَيْنُوا هُمْ
 مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ
 وَمَا خَلْفَهُمْ وَحَقَّ
 عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي
 أَمْرِ قَدْ خَلَتْ مِنْ
 قَبْلِهِمْ مِنَ الْإِنْسِ ۗ
 إِنَّهُمْ كَانُوا خَسِيرِينَ
 ﴿٢٣﴾ وَقَالَ الَّذِينَ
 كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا
 هَذَا الْقُرْآنَ وَاللَّغْوِ
 فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَعْلَمُونَ
 ﴿٢٤﴾ فَلَنَذِيقَنَّ
 الَّذِينَ كَفَرُوا عَذَابًا
 شَدِيدًا وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ
 أَشْرَ الَّذِي كَانُوا
 يَعْمَلُونَ ﴿٢٥﴾ ذَلِكَ
 جَزَاءُ أَعْدَاءِ اللَّهِ
 النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
 دَارٌ مُّخَلَّدِينَ جَزَاءُ
 بِمَا كَانُوا بِغَايِبَتِنَا
 يَجْحَدُونَ ﴿٢٦﴾ وَقَالَ
 الَّذِينَ كَفَرُوا رَبَّنَا
 أَرِنَا الَّذِينَ أُضْلَلْنَا
 مِنَ الْإِنْسِ لِنَعْمَلَهُمَا
 نَحْتَأْتِدْهُمَا لِيَكُونُوا
 مِنَ الْأَسْفَلِينَ ﴿٢٧﴾

19. Na siku watakapo-
 kusanywa maadui wa
 Mwenyezi Mungu kwenye
 Moto, nao wakagawanywa
 kwa makundi.

20. Hata watakapoufikia Moto yatawashuhudia masikio yao, na macho yao

na ngozi zao kwa waliyokuwa wakiyatenda.

21. Na wao wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmetushuhudilia? Nazo zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu Ambaye Amekitamkisha kila kitu! Na Yeye Ndiye Aliyekuumbeni mara ya kwanza, na Kwake Yeye tu mtarejeshwa.

22. Na hamkuwa wenye kujificha hata masikio yenu, na macho yenu, na ngozi zenu, zisikushuhudilieni. Lakini mlidhani kwamba Mwenyezi Mungu Hayajui mengi katika mliyokuwa mkiyatenda.

23. Basi hiyo dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola wenu Mlezi. Imekuungamizeni; na mmekuwa miongoni mwa waliopata hasara.

24. Basi wakisubiri Moto ndio maskani yao. Na wakiomba radhi hawatokubaliwa.

Siku ya Kukusanywa, Viungo vya Wakosaji Vitashuhudia Dhidi Yao

وَيَوْمَ يُحْشَرُ أَعْدَاءُ اللَّهِ إِلَى النَّارِ فَهُمْ يُوزَعُونَ ﴿٨٦﴾

“Na siku watakapokusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu kwenye Moto, nao wakagawanywa kwa makundi.”

Yaani, wakumbushe washirikina kuhusu watakapokusanywa kwenda Motoni watasukumwa. Walinzi wa Jahanamu watawakusanya kuanzia wa kwanza wao mpaka wa mwisho wao.

Kama Anavyosema Allah تعالیٰ sehemu nyingine:

وَنَسُوقُ الْمُجْرِمِينَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ وِرْدًا ﴿٨٧﴾

“Na Tukawachunga waovu kuwapeleka Jahannamu hali ya kuwa wana kiu.” (19:86).

حَتَّىٰ إِذَا مَا جَاءُوهَا

“Hata watakapoufikia Moto...”

Yaani, watakaposimama ukingoni mwake,

شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَأَبْصَرُهُمْ وَجُلُودُهُمْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“...yatawashuhudilia masikio yao, na macho yao na ngozi zao kwa waliyokuwa wakiyatenda.”

Yaani, amali zao zote, za mwanzo na za mwisho; hakuna hata moja itakayofichwa.

وَقَالُوا لَجُلُودِهِمْ لِمَ شَهِدْتُمْ عَلَيْنَا

“Na wao wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmetushuhudilia?”

Watailaumu mikono na miguu yao na ngozi zao zitakapotoa ushahidi dhidi yao, ambapo mikono na miguu itajibu:

قَالُوا أَنْطَقَنَا اللَّهُ الَّذِي أَنْطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَهُوَ خَلَقَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

“Nazo zitasema: Ametutamkisha Mwenyezi Mungu Ambaye Ametamkisha kila kitu! Na Yeye Ndiye Aliyekuumbeni mara ya kwanza.”

Yaani, na Hawezi kupingwa au kuzuiwa, na Kwake Yeye mtarejea. Al-Hafidh Abubakr Al-Bazzar رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alicheka na kutabasamu siku moja, na akasema:

«أَلَا تَسْأَلُونِي عَنْ أَيِّ شَيْءٍ صَحَّحْتُ؟»

“Hamniulizi kuhusu kwanini nimecheka?”

Walisema, “Ewe Mjumbe wa Allah, kwanini umecheka?” Akasema:

«عَجِبْتُ مِنْ مُجَادَلَةِ الْعَبِيدِ رَبَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَقُولُ: أَيُّ رَبِّي أَلَيْسَ وَعَدْتَنِي أَنْ لَا تَظْلِمَنِي، قَالَ: بَلَى، يَقُولُ: فَإِنِّي لَا أَقْبَلُ عَلَيَّ شَاهِدًا إِلَّا مِنْ نَفْسِي، يَقُولُ اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى: أَوْلَيْسَ كَفَىٰ بِي شَهِيدًا وَبِالْمَلَائِكَةِ الْكِرَامِ الْكَاتِبِينَ - قَالَ -: فَيَرُدُّ هَذَا الْكَلَامَ مِرَازًا - قَالَ -: فَيُخْتَمُ عَلَيَّ فِيهِ وَتَتَكَلَّمُ أَرْحَانُهُ بِمَا كَانَ يَعْمَلُ، يَقُولُ: بَعْدًا لَكَرَّ وَسُخْفًا، عَنْكَرْتُ كُنْتُ أَجَادِلُ»

“Nilistaajabishwa na mja anaweza kujadiliana na Mola wake Mlezi Siku ya Kiama. Atasema, “Ewe Mola wangu Mlezi, je, hukunyahidi

kuwa hutanidhulumu?" Allah Atasema, "Ndiyo." Mtu huyo atasema, "Sitakubali shahidi yeyote dhidi yangu isipokuwa kutokana na nafsi yangu." Allah Atasema, "Je haitoshi kwamba Mimi na Malaika, waandishi watukufu, kuwa mashahidi?" Atarudia maneno hayo mara nyingi, kwa hiyo tutafungwa midomo, muhuri utapigwa juu ya mdomo wake na viungo vyake vitasema aliyoyafanya. Atasema: "Poteleeni mbali na kuchukiwa! Nilikuwa najadiliana kwa ajili yenu!"¹

Haya yameandikwa na yeye na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى.² Pia yameandikwa na Muslim na An-Nasa'i.³ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى ameandika kuwa Abu Burdah alisema kuwa Abu Musa alisema, "Kafiri au mnafiki ataitwa kwenye hesabu na Mola wake Mlezi Atamuonesha amali zake, lakini atazikana na kusema, 'Ewe Mola Mlezi, ninaapa kwa Utukufu Wako, malaika huyu ameniandikia jambo ambalo sikulifanya.' Malaika atamuambia, 'Kwani wewe hukufanya kadha wa kadha katika siku kadha na mahali kadha?' Atasema, 'Hapana, ninaapa kwa Utukufu Wako, ewe Mola Mlezi, Sikufanya hayo.' Baada ya hapo muhuri utapigwa juu ya mdomo wake." Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema, "Nadhani kiungo cha kwanza mwilini kitakachosema ni paja lake la upande wa kulia..." Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا كُنْتُمْ تَشْتَرُونَ أَنْ يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلَا أَبْصَارُكُمْ وَلَا جُلُودُكُمْ

"Na hamkuwa wenye kujificha hata masikio yenu, na macho yenu, na ngozi zenu, zisikushuhudilieni."

Yaani, viungo na ngozi zao vitawaambia, watakapovilaumu kwa kutoa ushahidi dhidi yao, 'hamkujificha mbali nasi mlipokuwa mkitenda, badala yake, mlifikufu na kufanya madhambi waziwazi, na mlidai kuwa hamkujali, kwa sababu hamkuamini kuwa Allah تعالى Alizijua amali zenu zote.' Allah تعالى Anasema:

وَلَيْكِن ظَنَنْتُمْ أَنَّ اللَّهَ لَا يَعْلَمُ كَثِيرًا مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾ وَذَلِكُمْ ظَنُّكُمُ الَّذِي ظَنَنْتُمْ بِرَبِّكُمْ

أُرْدَكُمْ

"...Lakini mlidhani kwamba Mwenyezi Mungu Hayajui mengi katika mliyokuwa mkiyatenda. Basi hiyo dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola wenu Mlezi. Imekuangamizeni."

¹ Al-Hakim 4:601. ² At-Tabari 21:452. ³ Muslim 4:2280, An-Nasai katika Al-Kubra 6:508.

Maana yake, 'Fikra hii mbaya, yaani, kuamini kwenu kuwa Allah تعالی Hakujuu mliyokuwa mkiyafanya, ndicho kilichokusababisheni kuangamia na kukupeni hasara mbele ya Mola wenu Mlezi.'

فَأَصْبَحْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ

“...na mmekuwa miongoni mwa waliokhasiri.”

Yaani, 'mahali pa Ufufuo, mmejipoteza nyinyi na familia zenu.' Imam Ahmad ameandika kuwa 'Abdullah رضي الله عنه, alisema, "Nilikuwa nimejificha chini ya pazia wakaja watu watatu – mmoja katika Quraysh na wawili mashemeji zake wa kabila la Thaqif, au mtu mmoja kutoka kabila la Thaqif na mashemeji zake wawili katika Quraysh. Matumbo yao yalikuwa makubwa sana, na hawakuwa na ufahamu sana. Walisema maneno ambayo sikuyasikia, kisha mmoja wao akasema, 'Msidhani kuwa Allah تعالی Anaweza kutusikia tunayoyasema sasa.' Mwingine akasema, 'Tukupaza sauti zetu, Atatusikia, lakini tusipopaza, Hatasikia.' Mwingine akasema, 'Kama Atatusikia jambo moja tu, Atasikia kila kitu.' Nikamueleza hayo Mtume, kisha Allah تعالی Akashusha:

وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَشِيرُونَ أَنْ يَشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلَا أَبْصَارُكُمْ وَلَا جُلُودُكُمْ

“Na hamkuwa wenye kujificha hata masikio yenu, na macho yenu, na ngozi zenu, zisikushuhudilieni.”Mpaka;

مِنَ الْخَاسِرِينَ

“...miongoni mwa waliokhasiri.”¹

Hivyo ndivyo alivyoandika At-Tirmidhi.² Riwaya sawa na hiyo ilisimuliwa na Ahmad (kwa riwaya nyingine), Muslim na At-Tirmidhi,³ na Al-Bukhari na Muslim pia wameandika (riwaya nyingine).⁴

فَإِنْ يَصْبِرُوا فَالنَّارُ مَثْوًى لَهُمْ وَإِنْ يَسْتَعْتِبُوا فَمَا هُمْ مِنَ الْمُعْتَبِينَ

“Basi wakisubiri Moto ndio maskani yao. Na wakiomba radhi hawakubaliwi.”

¹ Ahmad 1:381.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 9:123.

³ Ahmad 1:408, Muslim 4:2142, Tuhfat Al-Ahwadhi 9:124.

⁴ Fat'h Al-Bari 8:424, Muslim 4:2141, 2142.

Yaani, kama watasubiri laa, wataingia Motoni na hawatatoroka au kuwa na njia ya kuuepuka, na hata kama watajaribu kumsihi Allah تعالى na kutoa nyudhuru, hawatakubaliwa. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Maana ya Aya,

وَأِنْ يَسْتَعْتَبُوا

“Na wakiomba radhi...”

Wataomba kurejea duniani, lakini ombi hili halitajibiwa. Hii inafanana na Aya:

قَالُوا رَبَّنَا غَلَبَتْ عَلَيْنَا شِقْوَتُنَا وَكُنَّا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٧﴾ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِنْ
عُدْنَا فَإِنَّا ظَلِمُونَ ﴿١٨﴾ قَالَ أَحْسَعُوا فِيهَا وَلَا تَكْلِمُونَ ﴿١٩﴾

“Mola wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tuliopotea. Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi ni wenye kudhulumu. Atasema Mwenyezi Mungu: Tokomeeni humo, wala msinisemeze.” (23:106-108).¹

* وَقَيِّضْنَا لَهُمْ قُرَنَاءَ فَزَيَّنُوا لَهُمْ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أُمِّ
قَدِ خَلَّتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنَ آلِجِنِّ وَالْإِنْسِ إِنَّهُمْ كَانُوا خَسِرِينَ ﴿٢٠﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا
تَسْمَعُوا لِهَذَا الْقُرْآنِ وَالْغَوْا فِيهِ لَعَلَّكُمْ تَعْلَبُونَ ﴿٢١﴾ فَلَنُذِيقَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا عَذَابًا
شَدِيدًا وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَشْوَأَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٢﴾ ذَلِكَ جَزَاءُ أَعْدَاءِ اللَّهِ النَّارُ هُمْ فِيهَا
دَارُ الْآخِلَةِ جَزَاءُ مَا كَانُوا بِغَايَتِنَا سَاجِدُونَ ﴿٢٣﴾ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا رَبَّنَا أَرِنَا الَّذِينَ
أَضَلَّانَا مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ لِنَجْعَلَهُمَا تَحْتَ أَقْدَامِنَا لِيَكُونَا مِنَ الْأَسْفَلِينَ ﴿٢٤﴾

25. Na Tukawawekea marafiki, na wakawapambia yaliyo mbele yao na nyuma yao. Basi ikawathibitikia kauli wawe pamoja na mataifa yaliyopita kabla yao, miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamekuwa ni wenye kukhasirika.

26. Na waliokufuru walisema: Msiisikilize Qur’ani hii, ipotosheni na kubatilisha kisomo chake, huenda mkashinda.

¹ At-Tabari 21:458.

27. Basi hapana shaka Tutawaonjesha hao waliokufuru adhabu kali, na hapana shaka Tutawalipa malipo mabaya ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

28. Hayo ndiyo malipo ya Maadui wa Mwenyezi Mungu - Moto! Humo watakuwa na maskani ya kudumu, ndiyo malipo yao kwa sababu walikuwa wakizipinga Aya Zetu.

29. Na waliokufuru watasema: Mola wetu Mlezi! Tuoneshe waliotupoteza miongoni mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni mwa walio chini kabisa.

Marafiki wa Washirikina Wanawapambia Vitendo Viovu

Allah تعالی Anatuambia kuwa Yeye ni Mmoja Anayewaacha washirikina wapotee, na kuwa hayo hutokea kwa Utashi na Hukumu Yake.

Yeye ni Mwingi wa Hekima katika Matendo Yake, Anapowateulia marafiki kutoka katika mashetani ya kibinadamu na majini.

فَزَيَّنُوا لَهُمْ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ

“...na wakawapambia yaliyo mbele yao na nyuma yao.”

Yaani, walifanya amali zao ziwavutie hapo zamani. Kadiri ya mustakbali ulivyo, wao hujiona kama wanatenda wema, kama Anavyosema Allah تعالی:

وَمَنْ يَعْشُ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقَيِّضْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٣٦﴾ وَإِنَّهُمْ لَيَصُدُّوهُمْ عَنْ

السَّبِيلِ وَهُمْ مُهْتَدُونَ ﴿٣٧﴾

“Anayeyafanyia upofu maneno ya Mwingi wa Rehema Tunamuekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake. Na hakika wao wanawazuilia Njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka.”

(43:36-37)

وَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ

“Basi ikawathibitikia kauli...”

Yaani, Neno la adhabu, kama ilivyofanyika dhidi ya mataifa ya waliotangulia waliofanya vitendo vyao, watu na majini.

إِنَّهُمْ كَانُوا خَسِرِينَ

“Hakika hao wamekuwa ni wenye kukhasirika.”

Wote wakalingana sawa katika hasara na kuangamia.

Makafiri Walikatazana Kusikiliza Qur’an, na Matokeo ya Hilo.

Allah تعالى Anasema:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَسْمَعُوا لِهَذَا الْقُرْآنِ

“Na waliokufuru walisema: Msiisikilize Qur’ani hii.”

Yaani, waliambizana kuwa wasiizingatie Qur’an au kutii amri zake.

وَالْعَوَّا فِيهِ

“...na ipotosheni na kubatilisha kisomo chake.”

Yaani, inaposomwa, msiisikilize. Hii ilikuwa rai ya Mujahid. “Na mpige kelele katikati yake (inaposomwa).” Yaani, kupiga miluzi na kujaribu kumvuruga Mtume ﷺ wakati aliposoma Qur’an, ambacho ndicho walichofanya Quraysh.

لَعَلَّكُمْ تَغْلِبُونَ

“...huenda mkashinda.”

Yaani, haya ni matendo ya makafiri wajinga na waliofuata njia zao, waliposikia Qur’an. Allah تعالى Ametuamrisha tuwe kinyume na hali hiyo Akasema:

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٢٠٤﴾

“Na isomwapo Qur’ani isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa.” (7:204).

Kisha Allah تعالى Akasema:

فَلَنْذِيقَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا عَذَابًا شَدِيدًا

“Basi hapana shaka Tutawaonjesha hao waliokufuru adhabu kali.”

Maana yake, kutokana na wanayoyafanya wanapoisikia Qur’an.

وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَسْوَأَ الَّذِي كَانُوا يَعْمَلُونَ

“..na hapana shaka Tutawalipa malipo mabaya ya yale waliyokuwa wakiyafanya.”

Yaani, kutokana na matendo yao maovu.

ذَٰلِكَ جَزَاءُ أَعْدَاءِ اللَّهِ النَّارُ هُمْ فِيهَا دَارُ الْخُلْدِ ۗ جَزَاءُ ۙ بِمَا كَانُوا بِآيَاتِنَا يَجْحَدُونَ ﴿٦٦﴾
 وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا رَبَّنَا أَرِنَا الَّذِينَ أُضْلَلْنَا مِنَّا مِنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ جَعَلَهُمَا نَحْتًا وَقَدَامِنَا
 لِيَكُونَا مِنَ الْأَسْفَلِينَ ﴿٦٧﴾

Hayo ndiyo malipo ya Maadui wa Mwenyezi Mungu - Moto! Humo watakuwa na maskani ya kudumu, ndiyo malipo yao kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara Zetu. Na waliokufuru watasema: Mola wetu Mlezi! Tuoneshe waliotupoteza miongoni mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni wa walio chini kabisa.”

Imesimuliwa kuwa ‘Ali رضي الله عنه, alisema, kuhusu maneno,

الَّذِينَ أُضْلَلْنَا

“...waliotupoteza...”

Iblis na mwana wa Adam ambaye alimuua ndugu yake.¹ As-Suddi alisimulia kuwa ‘Ali رضي الله عنه, amesema; “Iblis humlingania kila anayefanya ushirikina na mwana wa Adam humlingania kila anayefanya dhambi kubwa. Hivyo Iblis ndiye anayewaita watu kwenye uovu, kama vile *Ushirikina* na dhambi ndogo ndogo.”² Ama kuhusu mtoto wa kwanza wa Adam عليه السلام, ni kama ilivyo-thibitishwa na Hadithi:

«مَا قُتِلَتْ نَفْسٌ ظَلَمْنَا إِلَّا كَانَ عَلَى ابْنِ آدَمَ الْأَوَّلِ بِغُلٍّ مِنْ دَمِهَا، لِأَنَّهُ أَوَّلُ مَنْ سَنَّ الْقَتْلَ،

“Hakuna nafsi iliyouliwa kwa dhuluma, isipokuwa sehemu ya dhambi hiyo itamuendea mtoto wa kwanza wa Adam, kwa sababu alikuwa wa kwanza kufanya mauaji.”³

¹ At-Tabari 21:462.

² At-Tabari 21:462.

³ Fat’h Al-Bari 6:419.

تَجْعَلُهُمَا نَحْتًا أَقْدَامِنَا

"...ili tuwaweke chini ya miguu yetu."

Yaani, 'waweke chini yetu katika adhabu, ili waadhibiwe vikali zaidi kuliko sisi.'

لِيَكُونَا مِنَ الْأَسْفَلِينَ

"...wapate kuwa miongoni wa walio chini kabisa."

Yaani, katika sehemu ya chini kabisa katika Jahanamu, kama tulivyotaja katika *Surat Al-A'raf*, kuhusu wafuasi kumuomba Allah تعالى Awazidishie adhabu viongozi wao:

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ وَلٰكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

"Atasema: Itakuwa kwenu nyote maradufu, lakini nyinyi hamjui tu." (7:38)

Yaani, Allah تعالى Atamuadhibu anayestahiki kwa mujibu wa amali zake. Hii inafanana na:

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَاهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا

يُفْسِدُونَ ﴿٣٨﴾

"Wale waliokufuru na kuzu ilia njia ya Mwenyezi Mungu Tutawazidishia Adhabu juu ya adhabu, kwa walivyokuwa wakifisidi." (16:88).

* * *

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَفْتَمُوا تَنْزِيلَ عَلَيْهِمْ
 الْمَلَائِكَةَ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشُرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ
 تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ نَحْنُ أَوْلِيَآؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي
 الْآخِرَةِ ۗ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهَى أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا
 تَدْعُونَ ﴿٣١﴾ ثُلَاثًا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ ﴿٣٢﴾ وَمَنْ أَحْسَنُ
 قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ
 الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٣﴾ وَلَا تَسْتَعِزَّيْ أَحْسَنَهُ وَلَا السَّيِّئَةَ ۗ أَدْفَعُ
 بِأَلْتِي هِيَ أَحْسَنُ فِإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ
 وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٤﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا
 إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٥﴾ وَإِنَّمَا يَنْزَعُكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْعٌ
 فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ ۗ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٦﴾ وَمِنْ آيَاتِهِ
 اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۗ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا
 لِلْقَمَرِ ۗ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ ۚ إِن كُنْتُمْ إِيَّاهُ
 تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ فَإِنِ اسْتَكْبَرُوا فَالَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ
 يُسْتَعْتَبُونَ لَهُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُمْ لَا يَسْأَمُونَ ﴿٣٨﴾ وَمِنْ
 آيَاتِهِ أَنْ تَرَى الْآرْضَ خَشِيعَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ
 اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ۗ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيِي الْمَوْتِ ۗ إِنَّهُ عَلَى
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ
 اسْتَفْتَمُوا تَنْزِيلَ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ
 أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَبْشُرُوا بِالْجَنَّةِ
 الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ نَحْنُ
 أَوْلِيَآؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي
 الْآخِرَةِ ۗ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهَى
 أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدْعُونَ ﴿٣١﴾
 ثُلَاثًا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ ﴿٣٢﴾

30. Hakika waliosema:
*Mola wetu Mlezi ni Mwe-
 nyezi Mungu! Kisha
 wakanyooka sawa, hao
 huwateremkia Malaika
 wakawaambia: Msiogope,
 wala msihuzunike; nanyi
 furahini kwa Pepo mliyo-
 kuwa mkiahidiwa.*

**31. Sisi ni vipenzi vyenu
 katika maisha ya dunia na
 katika Akhera, na humo
 mtapata kinachotamaniwa
 na nafsi zenu, na humo
 mtapata mtakavyovitaka.**

32. Ni takrima itokayo kwa Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.

Bishara kwa Waliomuamini Allah تعالی Peke Yake na Kuwa Imara

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا

“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa.”

Yaani, wanafanya kwa ajili Allah تعالی amali njema kwa unyoofu, na wanamtii Allah تعالی, kwa kufanya Aliyowafaradhishia Allah تعالی. Ibn Jarir رحمه الله تعالی ameandika kuwa Sa' id bin 'Imran alisema, “Nilimsomea Aya hii Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا

“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa.”

Alisema, ‘wale waliomshirikisha Allah تعالی.’¹ Kisha imesimuliwa masimulizi ya Al-Aswad bin Hilal, ambaye alisema, “Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه alisema, ‘Unasemaje kuhusu Aya hii:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا

“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa.”

Walisema:

رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا

“Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa.”

‘Wanakwepa dhambi.’ Alisema, ‘Hukuitafsiri vyema.’ Wanasema: ‘Mola wetu ni Allah, kisha wanakuwa imara na hawamgeukii mola mwingine asiyekuwa Yeye.’² Hii ilikuwa pia rai ya Mujahid, ‘Ikrimah, As-Suddi na wengine.’³

Ahmad ameandika kuwa Sufyan bin ‘Abdullah Ath-Thaqafi alisema, “Nilisema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, niambie jambo nitakaloshikamana nalo.’ Akasema:

¹ At-Tabari 21:464.

² At-Tabari 21:464.

³ At-Tabari 21:465.

«قُلْ: رَبِّيَ اللهُ، ثُمَّ اسْتَقِيمْ»

“Sema, ‘Mola wangu Mlezi ni Allah,’ kisha nyooka sawa.”

Nikasema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, ni nini unachohofia zaidi kwangu.’ Mtume ﷺ akakamata ncha ya ulimi wake na akasema,

«هُذَا»

“Huu.”¹

Hayo yaliandikwa na At -Tirmidhi na Ibn Maj ah; At -Tirmidhi alisema, *“Hasan Sahih.”²*

Muslim pia ameandika katika Sahih yake, na An-Nasa’i ameandika kuwa Sufyan bin ‘Abdullah Ath-Thaqafi رضى الله عنه alisema, “Nilisema, ‘Ewe Mtume, niambie jambo la Uisilamu ambalo sitamuuliza yeyote kuhusu hilo baada yako.’ Akasema:

«قُلْ: آمَنْتُ بِاللهِ ثُمَّ اسْتَقِيمْ»

“Sema, Nimemuamini Allah, halafu nyooka.”

Kisha akamalizia Hadithi.³

تَنْزَلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ

“...hao huwateremkia Malaika...”

Mujahid, As-Suddi, Zayd bin Aslam na mwanaye Zayd walisema, “Inamaanisha, wakati wa mauti.” Na watasema,

أَلَّا تَخَافُوا

“Msiogope.”⁴

Mujahid, ‘Ikrimah na Zayd bin Aslam alisema, “Yaani kutokuogopa mtakayokabiliana nayo huko Akhera.”⁵

¹ Ahmad 4:413.

² *Tuhfatul Al-Ahwadhi* 7:91, Ibn Majah 2:1314.

³ Muslim 21:466.

⁴ At-Tabari 21:466, Al-Qurtubi 15:358.

⁵ At-Tabari 21:467.

وَلَا تَحْزَنُوا

“...wala msihuzunike.”

Mambo ya kidunia uliyoyaacha, watoto, familia, mali na madeni, kwani tutayashughulikia kwa ajili yako.

وَأَبَشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ

“...nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa.”

Basi wanatoa bishara kuhusu kumalizika mambo mabaya na kufika mema. Hii inafanana na kilichosemwa katika Hadithi iliyosimuliwa na Al-Bara' رضي الله عنه:

«إِنَّ الْمَلَائِكَةَ تَقُولُ لِرُوحِ الْمُؤْمِنِينَ: أَخْرِجِي أَجْتِهَا الرُّوحُ الطَّيِّبَةُ فِي الْجَسَدِ الطَّيِّبِ
كُنْتَ تَعْمُرُهُ، أَخْرِجِي إِلَى رَوْحٍ وَرَبْحَانٍ وَرَبِّ غَيْرِ غَضَبَانَ»

“Hakika Malaika huiambia roho ya Muumini, “Toka, Ewe roho mwema kutoka katika mwili mzuri ulimokuwa ukiishi twende kwenye pumziko na mirehani na Mola Mlezi Ambaye Hajaghadhibika.”¹

Ilisemekana kuwa Malaika watawateremkia katika siku watakapofufuliwa makaburini. Zayd bin Aslam alisema, “Watampa bishara wakati wa kufariki, kaburini kwake, na atakapofufuliwa.” Haya yaliandikwa na Ibn Abi Hatim, na rai hii inapatana na rai zote; ni rai njema na pia ni kweli.

فَخُنْ أَوْلِيَاءَكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

“Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera.”

Yaani, Malaika watawaambia waumini pindi mauti yatakapowakaribia: “Tulikuwa marafiki zenu, yaani, wandani wenu, duniani, kwa kukulideni na kukusaidieni kwa Amri ya Allah تعالى, na tutakuwa pamoja nanyi Akhera, kwa kukuondoleeni kujihisi upweke makaburini mwenu na pindi Parapanda litakapopulizwa; tutakuondoleeni mashaka katika Siku ya Kiama na kukupitisheni katika *Sirat* na kukupelekeni katika bustani zenye furaha.”

¹ Ahmad 4:287.

وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهَى أَنْفُسُكُمْ

“...na humo mtapata kinachotamaniwa na nafsi zenu.”

Yaani, ‘Peponi mtapata yote mtakayotamani na yenye kukufurahisheni.’

وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدْعُونَ

“...na humo mtapata mtakavyovitaka.”

Yaani, ‘chochote mtakachoomba, kitakuwepo mbele yenu kama mtakavyotaka.’

تُزَلَّأُ مِنَ غَفُورٍ رَحِيمٍ ﴿٣٠﴾

“Ni takrima itokayo kwa Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.”

Yaani, mapokezi ya mgeni kukaribishwa, kipawa na kuneemeshwa, kutoka kwa Msamehevu wa madhambi yenu, Aliyekusameheni, Amesitiri makosa yenu, Mkarimu na Mwingi wa Rehema.’

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣١﴾ وَلَا تَسْتَوِ الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ۚ ادْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٢﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حِظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٣﴾ وَإِنَّمَا يَنْزَعَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْعٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ ۚ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٤﴾

33. Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?

34. Mema na maovu hayalingani. Ondosha uovu kwa lililo jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.

35. Lakini hawapewi wema huu ila wanaosubiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.

36. Na Shetani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua.

Fadhila za Kulingania kwa Allah تعالی.

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّن دَعَا إِلَى اللَّهِ

“Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu...”

Yaani, anawalingania waja wa Allah تعالی Kwake.

وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ

“...na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?”

Yaani, yeye mwenyewe anafuata anayoyasema, hivyo ananufaika yeye pia na wengine. Na wala yeye si katika wenye kuamrisha mema lakini hawayatendi, au wanakataza maovu na huku wao wanayatenda. Anatenda mema na kuepuka maovu, na anawaita watu kwenda kwa Muumba wao تعالی. Hii ni kanuni ya jumla na inatumika kwa kila anayewalingania watu kwenye heri na yeye mwenyewe anaongozwa na anachosema. Mtume ﷺ ni wa mwanzo kabisa katika hilo, kama Muhammad bin Sirin, As-Suddi na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam walivyosema.¹ Pia alisema kuwa kilichokusudiwa hapa ni waadhini wema, kama ilivyoelezwa katika Sahih Muslim:

«الْمُؤَدَّبُونَ أَطْوَلُ النَّاسِ أَعْنَاقًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Waadhini watakuwa watu wenye shingo ndefu zaidi Siku ya Kiama.”²

Katika As-Sunan kumesimuliwa kuwa Mtume ﷺ alisema:

«الْإِمَامُ ضَامِرٌ، وَالْمُؤَدَّبُ مُؤْتَمِنٌ، فَأَرْشَدَ اللَّهُ الْأَيْمَةَ وَعَفَّرَ لِلْمُؤَدَّبِينَ»

“Imamu ni mdhamini na Mwadhini yupo katika nafasi ya amana. Allah Awape uongofu Maimamu na awasamehe Waadhini.”³

¹ Al-Qurtubi 15:360.

² Muslim 1:290.

³ Abu Dawud 1:356, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 1:614. Maana yake ni kwamba, watu wanapaswa kumfuata Imamu katika Sala na yanayohusiana nayo ni katika majukumu yake, kadhalika *Muadhdhinin*, watu wanatakiwa wategemee adhana yake.

Rai sahihi ni kwamba maana ya Ayah inajumuisha watu wote waadhini na wengine. Ayah hii iliposhuka, *Adhana* haikuwa imeamriwa. Aya hii ilishuka Makkah, na *Adhana* iliamriwa Madinah baada ya Hijrah, alipooteshwa 'Abdullah bin 'Abd Rabbihi Al-Ansari رَضِيَ اللهُ عَنْهُ ndotoni. Alimsimulia Mtume ﷺ, na akamuambia amfundishe Bilal رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, ambaye alikuwa na sauti nzuri zaidi, kama tulivyoeleza katika sehemu nyingine. Hivyo rai sahihi ni kwamba, maana ya aya inawahusu watu wote, kama 'Abdur-Razzaq alivyosema, akisimulia kutoka kwa Ma'mar, kutoka kwa Al-Hasan Al-Basri رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, ambaye alisoma Aya hii:

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٠﴾

“Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?”

Na akasema, “Huyo ni kipenzi cha Allah تَعَالَى, huyo ni rafiki sana wa Allah تَعَالَى, huyo ni mteule wa Allah تَعَالَى, huyo ni mpendwa zaidi kuliko wote kwa Allah تَعَالَى. Anaitikia wito wa Allah تَعَالَى na anawaita watu kwenye hilo aliloitikia. Amefanya amali njema katika kuitikia na akasema, ‘Mimi ni katika Waislamu.’ Huyo ni Khalifah wa Allah تَعَالَى.”¹

Hekima katika Ulinganiaji (Da’wah) na Mambo Mengine.

Allah تَعَالَى Anasema:

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا أَلْسِيَّةٌ ﴿٣١﴾

“Mema na maovu hayalingani.”

Yaani, kuna tofauti kubwa baina yao.

أَدْفَعِ بِأَيْدِي هِيَ أَحْسَنُ ﴿٣٢﴾

“Ondosha uovu kwa lilio jema zaidi.” Yaani, ‘mtu anapokufanyia kosa, mrudishie kwa kumtendea wema,’ kama ‘Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, alivyosema, “Hakuna adhabu nzuri kwa mwenye kumuasi Allah تَعَالَى kuhusu wewe, kuliko wewe kumtii Allah تَعَالَى kwa ajili ya yeye.”

¹Abdur-Razzaq 2:187.

فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ

“Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.”

Yaani, ‘mkiwatendea wema waliokufanyieni uovu, amali njema hizo zitapelekea kwenye mapatano, mapenzi na hisia, na watakuwa kama rafiki mwandani kwenu na watakuhurumieni na kukufanyieni wema.’ Kisha Allah تعالى Anasema:

وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا

“Lakini hawapewi wema huu ila wanaosubiri.”

Maana yake, hakuna anayepokea ushauri huu na kuutumia, isipokuwa wenye subira katika kuyafanya, kwani ni nzito kwa watu.

وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ

“...wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.”

Yaani, Mwenye kumiliki sehemu kubwa ya furaha duniani na Akhera. ‘Ali bin Abi Talhah alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliitafsiri Aya hii: “Allah تعالى Anawaamrisha waumini wawe na subira wanapokasirika, wawe wastahamilivu wanapo- kabiliana na ujinga, na wasamehe wanapotendewa ubaya. Kama watafanya hivyo, Allah تعالى Atawaokoa dhidi ya *Shaytan* na Kuwadhalilisha maadui zao kwao mpaka wanakuwa marafiki wa ndani.”¹

وَأِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ

“Na Shetani akikuchochea kwa uchochezi wewe jikinge kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, mashetani miongoni mwa watu wanaweza kuhadaika mnapowatendea wema, lakini mashetani ya kijini, wanapopenyeza uovu wao, hauwezi kuondolewa isipokuwa kwa kuomba Hifadhi ya Muumbaji Mwenye Kuwapa nguvu juu yenu. Mkiomba Hifadhi ya Allah تعالى na kugeukia Kwake, Atazuia madhara na juhudi zao. Mtume ﷺ aliposimama ili kusali, alikuwa akisema:

¹ Fat’h Al-Bari 8:418.

«أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ، مِنْ هَمَزِهِ وَنَفْخِهِ وَنَفْثِهِ»

“Ninajikinga kwa Allah Msikivu, Mjuzi, dhidi ya Shetani Mlaaniwa na shari ya ushawishi wake, pumzi yake na kupulizia kwake.”¹

Tumeshaeleza kuwa hakuna kitu kama hicho katika Qur’an, mbali ya ibara katika Surat Al-A’raf, ambapo Allah تعالى Anasema:

خُذِ الْعَفْوَ وَأْمُرْ بِالْعُرْفِ وَأَعْرِضْ عَنِ الْجَاهِلِينَ ﴿٣٠﴾ وَإِنَّمَا يَنزَعَنَّكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْعٌ
فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٣١﴾

“Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili. Na uchochezi wa Shetani ukikuchochea basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi.” (7:199-200)

Na katika Surat Al-Mu’minun ambapo Allah تعالى Anasema:

أَدْفَعْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةِ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٣٦﴾ وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ
هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٣٧﴾ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ تَحْضُرُونَ ﴿٣٨﴾

“Kinga maovu kwa kutenda yaliyo mema zaidi. Sisi tunajua wayasemayo. Na sema: Mola wangu Mlezi! Najikinga Kwako na wasi wasi wa mashetani. Na najikinga Kwako, Mola wangu Mlezi, wasinikaribie.” (23:96-98)

وَمِنْ ءَايَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ
الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾ فَإِنِ اسْتَكْبَرُوا فَالَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ
يُسَبِّحُونَ لَهُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُمْ لَا يَسْأَمُونَ ﴿٣٨﴾ وَمِنْ ءَايَاتِهِ أَنْ تَرَى الْأَرْضَ
خَشَعَةً فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ ﴿٣٩﴾ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيِ الْمَوْتِ إِنَّهُ
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٠﴾

¹ Ahmad 8:253.

37. Na katika alama Zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu Aliyeviumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu.

38. Na ikiwa watafanya jeuri, basi hao walioko kwa Mola wako Mlezi wanamtakasa Yeye usiku na mchana, na wao hawachoki.

39. Na katika Ishara Zake ni kwamba unaiona ardhi nyonge, lakini Tunapoiteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka. Bila ya shaka Aliyehuishia ardhi Ndiye Atakayehuishia wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

Katika Alama za Allah تعالى

Hapa Allah تعالى Anawakumbusha viumbe Wake kuhusu Uweza Wake, na kuwa Yeye ni Mmoja Asiyeye na wa kulingana Naye, na Yeye ni Mwenye Uweza wa Kufanya vitu vyote. Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ

“Na katika alama Zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi.”

Yaani, Aliumba usiku pamoja na giza lake na mchana pamoja na mwangaza wake, na hivyo viwili vinapishana bila ya kukoma. Na Aliumba Jua a nuru yake ing’aaayo, na Mwezi pamoja na nuru yake iliyoakisiwa. Na Alipanga hatua zao na Kuzipanga njia tofauti mbinguni, ili kwa kubadilika nyendo zao, mtu anaweza kujua hatua za mchana na usiku, za wiki, miezi na miaka, na vipindi vyenye kuhusiana na haki za watu, mambo ya ibada na miamala mingine. Zaidi ya hayo, kwa kuwa Jua na Mwezi ndivyo vyenye nguvu zaidi katika vitu vya angani vinavyoweza kuonekana kutokea ulimwengu wa juu na wa chini, Allah تعالى Anaonesha kuwa viumbe hivyo ni kama viumbe Vyake vingine, vilivyo chini ya Mamlaka na Udhibiti Wake. Hivyo Anasema:

لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنْتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ

“Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu Aliyeviumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu.”

Maana yake, ‘msimshirikishe na chochote katika kumuabudu, kwani kumuabudu kwenu hakutakuwa na faida yoyote kama mtamshirikisha, kwa sababu Hasamehe dhambi ya kumshirikisha.’ Anasema:

فَإِنْ أَسْتَكْبَرُوا

“Na ikiwa watafanya jeuri.”

Yaani, kumuabudu Yeye Peke Yake, na wakaendelea kumshirikisha,

فَالَّذِينَ عِنْدَ رَبِّكَ

“...basi hao walioko kwa Mola wako Mlezi...” Yaani, Malaika,

يُسَبِّحُونَ لَهُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُمْ لَا يَسْأَمُونَ

“... wanamtakasa Yeye usiku na mchana, na wao hawachoki.”

Hii inafanana na Aya ifuatayo:

فَإِنْ يَكْفُرْ بِهَا هَتُّوْلاً فَقَدْ وَكَّلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا بِهَا بِكَافِرِينَ ﴿٤١﴾

“Ikiwa hawa watayakataa hayo, basi Tumekwisha yawakilisha kwa watu wasioyakataa.” (6:89).

وَمِنْ آيَاتِهِمْ

“Na katika Alama Zake...” Yaani, Ishara za Uweza Wake wa Kufufua wafu.

أَنْتَ تَرَى الْأَرْضَ خَادِحَةً

“...unaiona ardhi nyonge.” Yaani, isiyo hai, bila ya kumea kitu; imekufa.

فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ

“...lakini Tunapoiteremshia maji mara unaiona inataharaki na kuumuka.”

Yaani, inaleta aina zote za mazao na matunda.

إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيٍ الْمَوْتَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Bila ya shaka Aliyehiusha ardhi Ndiye Atakayehiusha wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”

إِنَّ الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي آيَاتِنَا لَا
 مَخْفُونَ عَلَيْنَا ۗ أَفَمَنْ يُلْقَى فِي النَّارِ
 خَيْرٌ أَمْ مَنْ يَأْتِي ءَامِنًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ
 أَعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ ۗ إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ
 بَصِيرٌ ﴿٤٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالذِّكْرِ
 لَمَّا جَاءَهُمْ ۗ وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ ﴿٤١﴾
 لَا يَأْتِيهِ الْبَطِلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا
 مِنْ خَلْفِهِ ۗ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ
 ﴿٤٢﴾ مَا يُقَالُ لَكَ إِلَّا مَا قَدْ قِيلَ لِلرُّسُلِ
 مِنْ قَبْلِكَ ۗ إِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ
 وَذُو عِقَابٍ أَلِيمٍ ﴿٤٣﴾
 40. Hakika wale wanao-
 upotoa ukweli uliomo
 katika Aya Zetu hawatu-
 fichikii Sisi. Je! Atakaye-
 tupwa Motoni ni bora au
 atakaye kuja kwa amani
 Siku ya Kiyama? Tendeni
 mpendavyo, kwa hakika
 Yeye Anayaona mnayo-
 yatenda.

41. Kwa hakika wanayo-
 yakataa mawaidha haya

وَظَنُوا مَا هُمْ مِنْ مُّحِيسٍ ﴿٤٤﴾

yanapowajia (wataa- ngamia), na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu.

42. Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Mwenye kusifiwa.

43. Huambiwi ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako. Hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ni Mwenye Msamaha, na ni Mwenye Adhabu Chungu.

Adhabu ya Wakanushaji na Wasifu wa Qur'an

إِنَّ الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي آيَاتِنَا

“Hakika wale wanaoupotoa ukweli uliomo katika Ishara Zetu...”

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maana ya *Al-Ilhad* yaani ni kutokuweka vyema maneno.”¹ Qatadah na wengine walisema, “Inamaanisha ukaidi.”

لَا يَخْفَوْنَ عَلَيْنَا

“...hawatufichikii Sisi.”

Hili ni onyo na kitisho kikubwa, kwa kueleza kuwa Yeye تعالى, Anajua anayekataa Ishara Zake, Majina na Sifa Zake, na Atawaadhibu kwa hilo. Anasema:

أَفَمَنْ يُلْفَىٰ فِي النَّارِ خَيْرٌ أَمْ مَن يَأْتِي ءَامِنًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Je! Atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja kwa amani Siku ya Kiyama?”

Yaani, je, hao wawili wanalingana? Kisha Allah تعالى Anawaonya makafiri:

اعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ

“Tendeni mpendavyo.” Mujahid, Adh-Dhahhak na 'Ata' Al-Khurasani walisema kuwa,

اعْمَلُوا مَا شِئْتُمْ

“Tendeni mpendavyo.” Ni kitisho.² Maana yake, fanya unavyotaka katika wema au uovu, kwani Anajua na Anayaona mnayoyafanya.' Anasema:

¹ At-Tabari 21:478.

² At-Tabari 21:478.

إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

“...kwa hakika Yeye Anayaona mnayoyatenda.”

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِالذِّكْرِ لَمَّا جَاءَهُمْ

“Kwa hakika wanayoyakataa mawaidha haya yanapowajia (wataangamia).”

Adh-Dhahhak, As-Suddi na Qatadah alisema, “Hiyo ni Qur’an.”¹

وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ

“...na haya bila ya shaka ni Kitabu chenye nguvu na utukufu.”

Yaani, kimehifadhiwa na kulindwa, hakuna anayeweza kuleta kama hicho.

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ

“Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake.”

Yaani, hakuna njia ya kukipotosha, kwa sababu kimeshushwa na Mola Mlezi wa ulimwengu. Allah تعالى Anasema:

تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ

“Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Msifiwa.”

Maana yake, Yeye ni Mwingi wa Hekima katika yote Anayosema na Kufanya, Mwenye Sifa Njema katika yote Anayoamrisha na Anayokataza; kila Anachokifanya ni kwa ajili ya Sifa Njema na matokeo yake yatakuwa mema.

مَا يُقَالُ لَكَ إِلَّا مَا قَدْ قِيلَ لِلرُّسُلِ مِنْ قَبْلِكَ

“Huambiwi ila yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako.”

Qatadah, As-Suddi na wengine walisema, “Hakuna aliyekuambieni kwa kukupingeni na ukafiri, ambayo hawakuambiwa Mitume waliokuja kabla yako. Kama ulivyokataliwa, wao pia walikataliwa. Kama walivyovumilia matusi ya watu wao kwa subira, hivyo pia vumilia matusi ya watu wako kwa subira.”²

¹ At-Tabari 21:479.

² At-Tabari 21:481.

إِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ

“Hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka ni Mwenye Msamaha.

Yaani, kwa waliogeukia Kwake kwa toba.

وَذُو عِقَابٍ أَلِيمٍ

“...na ni Mwenye Adhabu Chungu.”

Yaani, kwa walioendelea na ukafiri, warukaji mipaka na wakaidi.

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ قُرْءَانًا أَعْجَمِيًّا لَقَالُوا لَوْلَا فُضِّلَتْ آيَاتُهُمْ أَءِتَيْنَاهُمْ أَءِتَانِيًّا وَعَرَبِيًّا قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ
 ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى
 أُولَئِكَ يُنَادَوْنَ مِنْ مَكَّانٍ بَعِيدٍ ﴿٤٤﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَآخْتَلَفَ فِيهِ
 وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ وَإِنَّهُمْ لَفِي شَكٍّ مِنْهُ مُرِيبٍ ﴿٤٥﴾

44. Na lau Tungeliifanya Qur’ani kwa lugha ya kigeni wangelisema: Kwanini Aya zake hazikupambanuliwa? Yawaje lugha ya kigeni na Mtume Mwaarabu? Sema: Hii Qur’ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali.

45. Na hakika Tulimpa Musa Kitabu, lakini pakatokea khitilafu kati yake. Na lau kuwa halikwisha tangulia neno la Mola wako Mlezi wangelihukumiwa. Na hakika wao wamo katika shaka yenye kuwatia wasiwasi.

Washirikina na Athari ya Ulinganiaji Kwao

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa Qur’an ni fasaha sana katika maneno na maana zake, lakini licha ya hayo, washirikina hawaiamini. Anatuambia kuwa ukafiri wao ni ukafiri wa kikaidi. Kama Anavyosema katika sehemu nyingine:

وَلَوْ نَزَّلْنَاهُ عَلَىٰ بَعْضِ الْأَعْجَمِينَ ﴿٤٦﴾ فَقَرَأَهُ عَلَيْهِمْ مَا كَانُوا بِهِ مُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾

“Na lau kuwa Tungeliiteremsha juu ya mmoja wa wasiokuwa

***Waarabu, Na akawasomea, wasingelikuwa wenye kuamini.”
(26:198-199).***

Kama Qur’an ingeteremshwa kwa lugha isiyo ya Kiarabu, wangesema, kwa sababu ya ukaidi wao:

لَوْلَا فَضَّلْتَ آيَاتُنَا ۖ أَعْجَمِي وَعَرَبِي ۖ

“Kwanini Aya zake hazikupambanuliwa? Yawaje lugha ya kigeni na Mtume Mwaarabu?”

Yaani, kwanini Qur’ani isingeliteremshwa kwa Kiarabu na kwa njia ya shutuma wangesema, “Vipi, si Kiarabu wala kutoka kwa Mwarabu - yaani, maneno ya kigeni yanawezaje kushushiwa Mwarabu asiyeyafahamu.” Tafsiri hii ilisimuliwa kutoka kwa Ibn ‘Abbas, Mujahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, As-Suddi na wengine.¹

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ۖ

“Sema: Hii Qur’ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini.”

Yaani, ‘sema Ewe Muhammad: Qur’an hii, kwa mwenye kuiamini, ni uwongofu moyoni mwake na tiba kwa mashaka na utata uliomo moyoni mwa watu.’

وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ

“Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao.”

Yaani, hawafahamu yaliyomo humo.

وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى ۖ

“Nayo kwao imezibwa hawaioni.”

Yaani, hawakuongozwa kwenye maelezo yaliyomo humo. Hii ni kama Aya:

وَنُزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ۚ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

***“Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara.”
(17:82).***

¹ At-Tabari 21:482.

أُولَئِكَ يُنَادُونَ مِنْ مَكَانٍ بَعِيدٍ

“Hao wanaitwa nao wako pahala mbali.”

Mujahid alisema, “Mbali kabisa na nyoyo zao.”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Ni kama vile anayewahutubia na kuwaita kutokea sehemu ya mbali, na hawataweza kufahamu anayoyasema.”² Hii inafanana na Aya:

وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً صُمُّ بِكُمْ عُمَى
فَهُمْ لَا يَعْقلُونَ ﴿١٧١﴾

“Na mfano wa waliokufuru ni kama mfano wa anayempigia kelele asiyesikia ila wito na sauti tu - ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawaelewi.” (2:171)

Kumfanya Mtume Musa عليه السلام kuwa Mfano Katika Kuliwazika

Allah تعالى Anasema:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَأَخْتَلَفَ فِيهِ

“Na hakika Tulimpa Musa Kitabu, lakini pakatokea khitilafu kati yake.”

Yaani, walimkufuru na hawakumheshimu.

فَأَصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ

“Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye ustahamilivu mkubwa.” (46:35).

وَأُولَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ

“Na lau kuwa halikwisha tangulia neno la Mola wako Mlezi...”

Yaani, kuchelewesha hesabu mpaka Siku ya Kiama,

¹ At-Tabari 21:485.

² At-Tabari 21:484.

لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ^ع

"...wangelihukumiwa."

Yaani, wangeharakishiwa adhabu. Lakini wana muda uliopangwa, ambapo ukifika hawataweza kukimbia.

وَأَنَّهُمْ لِيَئِي شَاكٍ مِّنْهُ مَرِيْبٍ

"Na hakika wao wamo katika shaka yenye kuwatia wasiwasi."

Yaani, maneno yao ya kufuru hayana hekima yoyote au uoni kwa upande wao; bali walizungumza bila ya kujaribu kuchunguza kikamilifu. Hii ilikuwa pia tafsiri ya Ibn Jarir رحمه الله تعالى, nayo inakubalika. *Allahu Aalam.*

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ^ط وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا^ث وَمَا رَبُّكَ بِظَلَمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٤٦﴾ * إِلَيْهِ يُرْدُ
 عِلْمُ السَّاعَةِ^ع وَمَا تَخْرُجُ مِنْ ثَمَرَاتٍ مِّنْ أَكْمَامِهَا وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أَثْقَالٍ وَلَا تَضَعُ إِلَّا
 بِعِلْمِهِ^ع وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ أَيْنَ شُرَكَآئِي قَالُوا ءَاذَنَّا مَا مِنَّا مِنْ شَيْءٍ ﴿٤٧﴾ وَصَلَّ عَنْهُمْ
 مَا كَانُوا يَدْعُونَ مِن قَبْلُ^ط وَطَنُوا مَا هُمْ مِنْ مَّحِيصٍ ﴿٤٨﴾

46. Anayetenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake, na Mwenye kutenda uovu basi ni juu ya nafsi yake vile vile; wala Mola wako Mlezi si Mwenye Kuwadhulumu waja.

47. Ujuzi wa kujua Saa ya Kiyama unarudishwa Kwake tu Mwenyezi Mungu. Na matunda hayatoki katika mafumba yake, wala mwanamke hachukui mimba, wala hazai, ila kwa Ujuzi wake. Na siku Atakayowaita, Akawaambia: Wako wapi washirika wangu? Hapo watasema: Tunakiri Kwako ya kwamba hapana miongoni mwetu anayeshuhudia hayo.

48. Na wakawapotea wale waliokuwa wakiwaomba hapo kwanza, na wakawa na yakini kuwa hawana pa kukimbilia.

Kila Mmoja Atalipwa kwa Mujibu wa Amali Zake

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ^ط

“Anayetenda mema basi anajitendea mwenyewe nafsi yake.”

Yaani, atanufaika yeye mwenyewe.

وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا^ط

“Na mwenye kujitendea uovu basi ni juu ya nafsi yake vilevile.”

Yaani, hakika si vingine hurejea ubaya huo juu yake

وَمَا رُبُّكَ يَظْلَمُ لِلْعَبِيدِ

“...wala Mola wako Mlezi si Mwenye Kuwadhulumu waja.”

Yaani, Kwa kuwasukumiza watu kwenye madhambi yao, na Yeye Hamwadhibu yeyote isipokuwa baada ya Kudhihirisha dalili dhidi yake na Kumpelekea Mtume.

Elimu ya Saa Iko kwa Allah تعالی

Halafu Allah تعالی Anasema:

إِلَيْهِ يُرَدُّ عِلْمُ السَّاعَةِ^ع

“Ujuzi wa kujua saa ya Kiyama unarudishwa Kwake tu...”

Maana yake, hakuna anayejua hayo isipokuwa Yeye. Kama ambavyo Mtume Muhammad ﷺ, kiongozi wa wanadamu, alivyomuambia Jibril عليه السلام, ambaye ni mmoja wa Malaika wakuu, alipomuuliza kuhusu saa:

«مَا الْمَسْئُورُ عَنْهَا بِأَعْلَمَ مِنَ السَّائِلِ»

“Aliyeulizwa hana elimu kuliko muulizaji.”¹

Na Allah تعالی Anasema:

¹ Fat'h Al-Bari 1:140.

إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَىٰ ﴿٤١﴾

“Kwa Mola wako Mlezi ndio mwisho wake.” (79:44)

لَا تُجَلِّبُهَا لِوَقْتِهَا إِلَّا هُوَ ۗ

“Haidhirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye.” (7:187).

وَمَا تَخْرُجُ مِنْ ثَمَرَاتٍ مِّنْ أَكْمَامِهَا وَمَا تَحْمِلُ مِنْ أَثْقَالٍ وَلَا تَتَضَعُ إِلَّا بِعِلْمِهِ ۗ

“Na matunda hayatoki katika mafumba yake, wala mwanamke hachukui mimba, wala hazai, ila kwa kujua Kwake.”

Yaani, Anayajua yote hayo, na hakuna kilichofichikana kwa Mola wenu Mlezi hata kwa uzito wa punje ya vumbi ardhini au mbinguni. Allah تعالى Anasema:

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا

“Na halidondoki jani ila Analijua.” (6:59).

اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنْثَىٰ وَمَا تَغِيصُ الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ ۗ وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ

“Mwenyezi Mungu Anajua mimba abebayo kila mwanamke, na kinachopunguka na kuzidi matumboni. Na kila kitu Kwake ni kwa kipimo.” (13:8).

وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُّعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ ۗ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٤١﴾

“Na wala hapewi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu. Hakika hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu.” (35:11)

وَيَوْمَ يُنَادِيهِمْ أَيْنَ شُرَكَآئِي

“Na siku Atakayowaita, Akawaambia: Wako wapi washirika Wangu?”

Yaani, katika siku ya Kiama, Allah تعالى Atawaita washirikina mbele ya viumbe wote na kusema, “Wako wapi wenza Wangu mliokuwa mkinishirikisha nao?”

قَالُوا ءَاذَنَّاكَ

“Hapo watasema: Tunakiri Kwako...”

Yaani, ‘tunakuambia,’

مَا مِنَّا مِن شَهِيدٍ

“...ya kwamba hapana miongoni mwetu anayeshuhudia hayo.”

Yaani, ‘hakuna katika sisi atakayetoa ushahidi leo kuwa Wewe una mwenza yeyote.’

وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوا يَدْعُونَ مِن قَبْلُ

“Na wakawapotea wale waliokuwa wakiwaomba hapo kwanza.”

Yaani, wataondoka, na hawatawasaidia.

وَوَظَنُوا مَا هُمْ مِن مُّحِيصٍ

“...na wakawa na yakini kuwa hawana pa kukimbilia.”

Yaani, hawatakuwa na njia ya kuikimbia Adhabu ya Allah تعالى. Inafanana na Aya:

وَرَاءَ الْمُجْرِمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُم مُّوَافِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿٥٣﴾

“Na wakhalifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.” (18:53)

* * *

لَا يَسْتَعْمُ الْإِنْسَانُ مِنْ دُعَاءِ الْخَيْرِ وَإِنْ مَسَّهُ الشَّرُّ فَيُتَوَسَّسُ
 قَنُوطًا ﴿٤٩﴾ وَلَئِنْ أَذَقْنَاهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ مَسَّتْهُ
 لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَئِنْ رُجِعْتُ إِلَىٰ
 رَبِّي إِنَّ لِي عِنْدَهُ لَلْحَسَنَىٰ فَلَنُنَبِّئَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِمَا عَمِلُوا
 وَلَنُذِيقَنَّهُمْ مِنَ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٠﴾ وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَىٰ
 الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَسَا بِجَانِبِهِ وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ فَذُو دُعَاءٍ
 عَرِيضٍ ﴿٥١﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنْ عِندِ اللَّهِ ثَمَرٌ
 كَفَرْتُمْ بِهِ مِنْ أَضَلِّ مِمَّنْ هُوَ فِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿٥٢﴾
 سَتُرِيهِمْ عَائِنَاتِنَا فِي الْأَفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ
 الْحَقُّ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِدٌ ﴿٥٣﴾ أَلَا
 إِنَّهُمْ فِي مِرْيَةٍ مِنْ لِقَاءِ رَبِّهِمْ أَلَا إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُحِيطٌ ﴿٥٤﴾

لَا يَسْتَعْمُ الْإِنْسَانُ مِنْ دُعَاءِ الْخَيْرِ
 وَإِنْ مَسَّهُ الشَّرُّ فَيُتَوَسَّسُ قَنُوطًا ﴿٤٩﴾
 وَلَئِنْ أَذَقْنَاهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ
 مَسَّتْهُ لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي وَمَا أَظُنُّ
 السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَئِنْ رُجِعْتُ إِلَىٰ رَبِّي
 إِنَّ لِي عِنْدَهُ لَلْحَسَنَىٰ فَلَنُنَبِّئَنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا بِمَا عَمِلُوا وَلَنُذِيقَنَّهُمْ مِنَ
 عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٠﴾ وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَىٰ
 الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَسَا بِجَانِبِهِ وَإِذَا
 مَسَّهُ الشَّرُّ فَذُو دُعَاءٍ عَرِيضٍ ﴿٥١﴾

49. Mwanaadamu hachoki kuomba dua za kheri, na

inapompata shari, mara huvunjika moyo akakata tamaa.

50. Na pindi Tukimuonjesha rehema itokayo Kwetu baada ya kumgusa dhara, bila ya shaka husema: Haya nayastahiki mimi, wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. Na hata nikirudishwa kwa Mola wangu Mlezi bila ya shaka nina mema yangu Kwake! Basi kwa yakini Tutawaelezea waliokufuru hayo waliyoyatenda, na kwa yakini Tutawaonjesha adhabu ngumu.

51. Na Tukimneemesha mwanaadamu hugeuka na kujitenga upande, na inapomgusa shari, huwa anaomba madua marefu marefu.

Mwanadamu Kubadilika Anapopata Raha Baada ya Shida

Allah تعالى Anatuambia kuwa mwanadamu kamwe hachoki kumuomba Mola wake Mlezi Ampe mazuri, kama vile mali, afya, n.k., lakini anapopatwa na baya - yaani, mitihani na shida au njaa,

فَيُؤَسِّسُ فَنُوطٌ

“...mara huvunjika moyo akakata tamaa.”

Yaani, anadhani kuwa hatapata tena faraja yoyote.

وَلَيْنَ أَذَقْتَهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ مَسَّتْهُ لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي

“Na pindi Tukimuonjeshia rehema itokayo Kwetu baada ya kumgusa dhara, bila ya shaka husema: Haya nayastahiki mimi.”

Yaani, kama jambo jema litamfikia au kupata riziki baada ya kipindi cha shida, anasema, ‘haya ni kwa kuwa ninayastahiki kutoka kwa Mola wangu Mlezi.’

وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً

“...wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. ”

Yaani, haamini kuwa Saa itafika. Hivyo anapobarikiwa, anazembea, na kuwa mjeuri asiye na shukrani, kama Anavyosema Allah تعالى:

كَلَّا إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٦٧﴾ أَنْ رَأَاهُ اسْتَغْفِي ﴿٦٨﴾

“Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri. Akijiona katajirika.”

(96:6-7)

وَلَيْنَ رُجِعْتُ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّ لِي عِنْدَهُ لَلْحُسْنَىٰ

“Na hata nikirudishwa kwa Mola wangu Mlezi bila ya shaka nina mema yangu Kwake!”

Yaani, ‘kama kuna Akhera baada ya yote, basi Mola wangu Mlezi Atanifanyia ukarimu kama Alivyonifanyia duniani.’

Hivyo anatarajia kuwa Allah تعالى Atamfadhili licha ya amali zake mbaya na kutokuwa na imani.”

Allah تعالى Anasema:

فَلَنَنْبِتَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِمَا عَمِلُوا وَلَنُذِيقَنَّهُمْ مِنَ عَذَابٍ غَلِيظٍ

“Basi kwa yakini Tutawaelezea waliokufuru hayo waliyoyatenda, na kwa yakini Tutawaonjesha adhabu ngumu.”

Basi Allah تعالى Anawatishia adhabu na kisasi wale wenye tabia na imani kama hiyo.

وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَى الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَسَا حُجَّتَيْنَاهُ

“Na Tukimneemesha mwanaadamu hugeuka na kujitenga upande.”

Yaani, anaacha kuwa mtiifu na anakuwa mjeuri katika kutii amri za Allah تعالى. Hii inafanana na Aya:

فَتَوَلَّى بِرُكْبَتِهِ

“Lakini alipuuzwa kwa sababu ya nguvu zake...” (51:39).

وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ

“...na inapomgusa shari.” Yaani, shida,

فَدُودُ دُعَائِهِ عَرِيضٍ

“...huwa na madua marefu marefu.”

Yaani, anaomba kitu kimoja kwa muda mrefu. Dua ndefu ni zile ambazo ni ndefu kwa maneno na maana yake ni fupi. Kinyume chake ni maneno mafupi lakini yaliyojaa maana.

Na Allah تعالى Anasema:

وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبَيْهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ

كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَى ضُرِّ مَسَّهُ

“Na mtu akiguswa na shida hutuomba anapolala ubavu, au kaka, au kasimama. Lakini Tukimuondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba Tumuondoshee shida iliyompata.”

(10:12)

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ثُمَّ كَفَرْتُمْ بِهِ مَنْ أَضَلُّ مِمَّنْ هُوَ فِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ
 ﴿٥٢﴾ سُنُّرِهِمْ ءَايَاتِنَا فِي الْأَفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَّبِعِنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ
 أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٥٣﴾ أَلَا إِنَّهُمْ فِي مَرِيبٍ مِّنْ لِّقَاءِ رَبِّهِمْ ۗ أَلَا إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ
 مُّحِيطٌ ﴿٥٤﴾

52. Sema: Mnaonaje! Ikiwa haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi ikawa ndio mmeyakataa, ni nani aliyepotea zaidi kuliko aliye katika upinzani wa mbali?

53. Tutawaonesha Ishara Zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?

54. Ama wao wamo katika shaka ya kukutana na Mola wao Mlezi! Ama hakika Yeye Amekizunguka kila kitu.

Qur'an na Dalili za Ukweli Wake

Allah تعالیٰ Anasema:

قُلْ

“Sema...” - ‘Ewe Muhammad, kuwaambia washirikina hao wasioamini Qur’an’-

أَرَأَيْتُمْ إِنْ كَانَ

“Mnaonaje! Ikiwa haya...” Yaani, hii Qur’an -

مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ثُمَّ كَفَرْتُمْ بِهِ

“...yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi ikawa ndio mmeyakataa.”

Yaani, ‘munaonaje hali zenu mbele ya yule Aliyeteremsha Mtume Wake.’ Allah تعالیٰ Anasema:

مَنْ أَضَلُّ مِمَّنْ هُوَ فِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ

“...ni nani aliyepotea zaidi kuliko aliye katika upinzani wa mbali?”

Yaani, yupo katika kukataa, kukaidi na kupinga ukweli, na anafuata njia inayoacha uongofu. Kisha Allah تعالى Anasema:

سُنُّرِهِمْ ءَايَاتِنَا فِي الْآفَاقِ وَفِي أَنْفُسِهِمْ

“Tutawaonesha Ishara Zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe...”

Maana yake, ‘Tutawaonesha ushahidi Wetu na dalili kuwa Qur’an ni ya kweli na kwa hakika imeshuka kutoka kwa Allah kwenda kwa Mtume ﷺ, kwa kutumia ishara za nje,

فِي الْآفَاقِ

“...katika upeo wa mbali...”

Kama ukombozi na kuingia Uislamu katika maeneo mengi na juu ya dini zote zingine. Mujahid, Al-Hasan na As-Suddi walisema, “Na dalili za ndani mwao wenyewe yaani, vita vya Badr, ukombozi wa Makka, na matukio mengine yaliyowakumba, ambapo Allah تعالى Alimpa ushindi Mtume Muhammad ﷺ na Masahaba wake, na Akapeleka udhalili na kushindwa kwa batili na wafuasi wake.” Pia huenda kilichokusudiwa ni mtu na alivyo kimaumbile. Kama ilivyoelezwa kirefu katika elimu ya maumbo, inayoashiria hekima ya Muumbaji - تعالى - na matakwa tofauti ya watu, mema au mabaya, n.k., na Hukumu (ya kiungu) aliyotiishwa navyo mtu huyo, bila ya kuwa na uwezo wa kubadili au kuikwepa.

حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“...mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?”

Yaani, Allah تعالى Anatosha kuwa Shahidi juu ya maneno na amali za waja Wake, na Anashuhudia kuwa Mtume Muhammad ﷺ anasema kweli, kama Anavyosema Allah تعالى:

لَٰكِنَ اللَّهُ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ ۗ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ

“Lakini Mwenyezi Mungu Anayashuhudia Aliyokuteremshia wewe. Ameyeremsha kwa Kujua Kwake.” (4:166).

أَلَا إِنَّهُمْ فِي مَرِيضٍ مِّن لِّقَاءِ رَبِّهِمْ

“Ama wao wamo katika shaka ya kukutana na Mola wao Mlezi! ”

Yaani, walikuwa na shaka kama Saa itakuja, hawaidhani au kujishughulisha nayo au kuizingatia; badala yake, wanaifanya kama haiwahusu na hawaijali. Lakini bila ya shaka itakuja. Kisha Allah تعالى Anaeleza kuwa Ana Uweza wa Kufanya vitu vyote na Amekienea kila kitu, na Kwake ni rahisi sana Kuileta Saa:

أَلَا إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطٌ

“Ama hakika Yeye Amekizunguka kila kitu.”

Yaani, viumbe wote wako chini ya Udhhibiti na Ujuzi Wake; Anadhhibiti vitu vyote kwa Nguvu Zake, basi Atakacho Huwa, na Asichotaka hakiwi, na hakuna wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye.

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Suratu Fussilat*. Kila Sifa Njema pamoja na Shukurani ni stahiki Yake Allah تعالى.

* * *

Tafsiri ya Suratu Ash-Shura

Sura ya 42

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الشُّرَىٰ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمَّ ۝ عَسَقَ ۝ كَذَلِكَ يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ
 قَبْلِكَ اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ۝ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي
 الْأَرْضِ ۝ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ۝ تَكَادُ السَّمَوَاتُ
 يَتَفَطَّرْنَ مِنْ فَوْقِهِنَّ ۝ وَالْمَلَائِكَةُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ
 وَيَسْتَغْفِرُونَ لِمَنْ فِي الْأَرْضِ ۝ أَلَا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَفُورُ
 الرَّحِيمُ ۝ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ اللَّهُ حَفِيفٌ
 عَلَيْهِمْ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ۝ وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ
 قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنذِرَ يَوْمَ
 الْجَمْعِ لَا رَبَّ فِيهِ ۝ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ۝
 وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَهُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي
 رَحْمَتِهِ ۝ وَالظَّالِمُونَ مَا لَهُمْ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ۝

حَمَّ ۝ عَسَقَ ۝ كَذَلِكَ يُوحَىٰ
 إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكَ اللَّهُ الْعَزِيزُ
 الْحَكِيمُ ۝ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ
 وَمَا فِي الْأَرْضِ ۝ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ
 ۝ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ
 مِنْ فَوْقِهِنَّ ۝ وَالْمَلَائِكَةُ يُسَبِّحُونَ
 بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِمَنْ فِي
 الْأَرْضِ ۝ أَلَا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَفُورُ
 الرَّحِيمُ ۝ وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ
 دُونِهِ أَوْلِيَاءَ اللَّهُ حَفِيفٌ عَلَيْهِمْ وَمَا
 أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ ۝

1. H'a Mim

2. A'yn Sin Qaf

3. Hivi ndivyo Mwenyezi -

Mungu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima Anavyokuletea Wahyi wewe na walio kabla yako.

4. Ni vyake viliomo mbinguni, na viliomo katika ardhi. Na Yeye Ndiye Mtukufu, Mkuu.

5. Zinakaribia mbingu kupasuka juu huko, na Malaika wakimtakasa Mola wao Mlezi na kumshukuru, na wakiwaombea msamaha waliomo kwenye ardhi. Ama hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Kurehemu.

6. Na wale waliowafanya walinzi wengine badala Yake, Mwenyezi Mungu ni Muangalizi juu yao. Wala wewe si wakili juu yao.

Wahyi na Nguvu za Allah تعالى.

Tumeshaeleza kuhusu herufi mkato. Na Kauli Yake Allah تعالى:

كَذَلِكَ يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ اللَّهُ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٢٠﴾

“Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima Anavyokuletea Wahyi wewe na walio kabla yako.”

Yaani, ‘kama Qur’an hii ilivyoteremshwa kwako, ndivyo pia Vitabu na Maandiko yalivyoshushwa kwa Mitume wa kabla yako.’

اللَّهُ الْعَزِيزُ

“Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu...” Yaani, katika kisasi Chake.

الْحَكِيمُ

“Mwenye Hikima.” Yaani, katika yote Anayosema na Anayofanya. Imam Malik رحمه الله تعالى amesimulia kuwa mama A’ishah رضي الله عنها alisema, “Al-Harith bin Hisham alimuuliza Mtume ﷺ, ‘Ewe Mjumbe wa Allah, Wahyi unakufikiaje.’ Mtume ﷺ akasema:

«أَخْبَانَا يَا بُنَيَّ مِثْلَ صَلْصَلَةِ الْجَرَسِ، وَهُوَ أَشَدُّ عَلَيَّ فَيَقْصِمُ عَنِّي وَقَدْ وَعَيْتُ مَا قَالَ، وَأَخْبَانَا يَا بُنَيَّ الْمَلِكُ رَجُلًا فَيَكَلِّمُنِي فَأَعِي مَا يَقُولُ»

“Wakati mwingine hunijia kama mlio wa kengele, ambao ni shida sana kwangu; halafu huisha, nami hufahamu yaliyosemwa. Wakati mwingine Malaika hunijia katika taswira ya kibinadamu, naye huzungumza nami na mimi hufahamu anachosema.”

Mama A'ishah رضي الله عنها, alisema, "Nilimuona alipokuwa akipokea Wahyi katika siku ya baridi kali, na wakati huo, paji la uso wake lilikuwa na vitone vya jasho."¹ Pia ilisimuliwa katika Sahihi Mbili, na riwaya iliyonukuliwa hapa iliandikwa na Al-Bukhari.²

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ^ط

"Ni Vyake viliomo mbinguni, na viliomo katika ardhi."

Yaani, kila kitu kimetiishwa chini ya miliki na udhibiti Wake.

وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

"Na Yeye Ndiye Mtukufu, Mkuu."

Hii inafanana na Aya:

الْكَبِيرُ الْمُتَعَالِ

"Mkuu Aliyetukuka." (13:9), na

هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

"...na hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyejuu na Ndiye Mkubwa." (22:62).

Na kuna Aya nyingi kama hizo.

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْ فَوْقِهِنَّ^ع

"Zinakaribia mbingu kupasuka juu huko."

Ibn 'Abbas, Adh-Dhahhak, Qatadah, As-Suddi na Ka'b Al-Ahbar walisema, vipande vipande, "Kwa kuhofia Nguvu Zake."³

وَالْمَلَائِكَةُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِمَنْ فِي الْأَرْضِ^د

"...na Malaika wakimtakasa Mola wao Mlezi na kumhimidi, na wakiwaomba maghfira waliomo kwenye ardhi."

Hii inafanana na Aya:

¹ Muwatta' 1:202.

² Fat'h Al-Bari 1:25, Muslim 4:1816.

³ At-Tabari 21:501.

الَّذِينَ تَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلُهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ
ءَامَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَعِلْمًا

“Wale wanaobeba A'rshi, na wanaoizunguka, wanamtukuza na kumsifu Mola wao Mlezi, na wanamuamini, na wanawaombea msamaha walioamini kwa kusema: Mola Wetu Mlezi! Umekienea kila kitu kwa Rehema na Ujuzi.” (40:7)

أَلَا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

“Ama hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.”

Huu ni ukumbusho, ili kuzingatia jambo hili.

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ

“Na wale waliowafanya walinzi wengine badala Yake Yeye.”

Hii inawakusudia washirikina,

اللَّهُ حَفِيظٌ عَلَيْهِمْ

“Mwenyezi Mungu ni Mwangalizi juu yao.” Maana yake, Anashuhudia amali zao, Kuziandika na Kuzihesabu kwa umakini, na Atawalipa kikamilifu.

وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ

“Wala wewe si wakili juu yao.” Maana yake, ‘wewe ni mwonyaji tu, na Allah ni Mdhamini wa mambo yote.”

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَى وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنذِرَ يَوْمَ الْجُمُعِ لَا
رَيْبَ فِيهِ ۚ فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ﴿٥١﴾ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَهُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ
يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ ۗ وَالظَّالِمُونَ مَا لَهُمْ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٥٢﴾

7. Na namna hivi Tumekufunulia Qur’ani kwa Kiarabu ili uwaonye watu wa Mama wa Miji na walio pembezoni mwake. Na uwaonye Siku ya Mkutano, haina shaka hiyo. Kundi moja litakuwa Peponi, na kundi jengine Motoni.

8. Na Mwenyezi Mungu Angelipenda Angewafanya wote umma mmoja, lakini Anamuingiza katika Rehema Yake Amtakaye. Na wenye kudhulumu hawana mlinzi wala msaidizi.

Qur'an Iliteremshwa ili Kuonya.

Allah تعالى Anasema, 'kama Tulivyopeleka wahyi kwa Mitume wa kabla yako,'

أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا

"Na namna hivi Tumekufunulia Qur'ani kwa Kiarabu..."

Maana yake, dhahiri, waziwazi,

لِتُنذِرَ أُمَّ الْقُرَىٰ

"...ili uwaonye watu wa Mama wa Miji.." Yaani, Makka,

وَمَنْ حَوْلَهَا

"...na walio pembezoni mwake." Yaani, ardhi yote, mashariki na magharibi. Makka inaitwa *Umm Al-Qura* (Mama wa Miji) kwani ni mtukufu kuliko ardhi nyingine, kama ilivyo katika shuhuda nyingi zilizoenezwa katika sehemu nyingine. Muhtasari mmojawapo wa dalili dhahiri aliandika Imam Ahmad kutoka kwa 'Abdullah bin 'Adi bin Al-Hamra' Az-Zuhri رضي الله عنه, kuwa alimsikia Mtume ﷺ alipokuwa amesimama katika sehemu ya soko la Makka, akisema,

«وَاللَّهِ إِنَّكَ لَخَيْرُ أَرْضِ اللَّهِ وَأَحَبُّ أَرْضِ اللَّهِ إِلَيَّ اللَّهُ، وَلَوْلَا أَنِّي أَخْرَجْتُ مِنْكَ مَا خَرَجْتُ»

"Naapa kwa Allah, wewe ni ardhi bora kabisa ya Allah, ardhi Anayoipenda zaidi Allah; isingekuwa nimetolewa kutoka kwako, nisingetoka."¹

Hii iliandikwa pia na At-Tirmidhi, An-Nasa'i na Ibn Majah; At -Tirmidhi alisema, **"Hasan Sahih."**²

وَتُنذِرَ يَوْمَ الْجَمْعِ

"Na uhadharishe na Siku ya Mkutano".

¹ Ahmad 4:305.

² *Tuhfatul Al-Ahwadhi* 10:426, An-Nasai katika *Al-Kubra* 2:249, Ibn Majah 1:1037.

Yaani, Siku ya Kiyama, Allah تعالى Atakapowakusanya wa mwanzo na wa mwisho katika uwanja mmoja.

لَا رَيْبَ فِيهِ^٤

“...haina shaka hiyo.” Yaani, hakuna shaka kuwa itafika na hayo ni hakika.

فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ

“Kundi moja litakuwa Peponi, na kundi jingine Motoni.”

Hii inafanana na Aya:

يَوْمَ نَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ^٥ ذَلِكَ يَوْمُ التَّنَائِينِ^٦

“Siku Atakayokukusanyeni kwa ajili ya Siku ya Mkusanyiko.” (64:9).

Inamaanisha kuwa watu wa Peponi na wa Jahanamu watapata faida na hasara, mtawalia. Ni kama Aya:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّمَن خَافَ عَذَابَ الْآخِرَةِ^٧ ذَلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَهُ النَّاسُ وَذَلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ^٨ وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مَّعْدُودٍ^٩ يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ^{١٠} فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ^{١١}

“Hakika katika haya yapo mazingatio kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa. Na Sisi hatucheleweshi ila kwa muda unaohisabiwa. Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa Idhini Yake Mwenyezi Mungu. Kati yao watakuwamo waliomo waovu na wema.” (11:103-105)

Imam Ahmad ameandika kuwa ‘Abdullah bin ‘Amr رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ alitujia, huku ameshika vitabu viwili mkononi.” Akasema,

«أَتَدْرُونَ مَا هَذَانِ الْكِتَابَانِ؟»

“Je, mnajua nini vitabu hivi viwili?”

“Tukasema, “Hatujui, isipokuwa mpaka utuambie, Ewe Mjumbe wa Allah.” Kuhusu kitabu kilichokuwa mkono wake wa kulia, alisema:

«هَذَا كِتَابٌ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ بِأَسْمَاءِ أَهْلِ الْجَنَّةِ وَأَسْمَاءِ آبَائِهِمْ وَقَبَائِلِهِمْ، ثُمَّ أُجْمِلَ عَلَى آخِرِهِمْ، لَا يُزَادُ فِيهِمْ وَلَا يُنْقَصُ مِنْهُمْ أَبَدًا»

“Hiki ni kitabu kutoka kwa Mola Mlezi wa ulimwengu, kina majina ya watu wa Peponi na ya mababa zao na makabila yao; wote wameorodheshwa, mpaka wa mwisho wao, na hakuna atakayeongezwa au kuondolewa kutoka humo abadan.”

Kisha kuhusu kitabu cha mkono wake wa kushoto, alisema:

«هَذَا كِتَابُ أَهْلِ النَّارِ بِأَسْمَائِهِمْ وَأَسْمَاءِ آبَائِهِمْ وَقَبَائِلِهِمْ، ثُمَّ أُجْمِلَ عَلَى آخِرِهِمْ، لَا يُزَادُ فِيهِمْ وَلَا يُنْقَصُ مِنْهُمْ أَبَدًا»

“Hiki ni Kitabu cha watu wa Jahanamu, kina majina yao na ya baba zao na makabila yao, yameorodheshwa mpaka wa mwisho wao, na hakuna wa kuongezwa wala wa kuondolewa kutoka humo abadan.”

Masahaba wa Mtume ﷺ wakasema, “Kwa nini tujitahidi ikiwa ni jambo ambalo tayari lishamalizika.” Mtume ﷺ alisema:

«سَدُّوْا وَقَادِرُوْا فَإِنَّ صَاحِبَ الْجَنَّةِ يُخْتَمُ لَهُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ، وَإِنْ عَمِلَ أَيُّ عَمَلٍ، وَإِنْ صَاحِبَ النَّارِ يُخْتَمُ لَهُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ، وَإِنْ عَمِلَ أَيُّ عَمَلٍ»

“Fanyeni vizuri na karibianeni, kwani mtu wa Peponi atahitimishiwa kwa amali za watu wa Peponi, na hata akifanya amali yoyote; na mtu wa Jahanamu atahitimishiwa huku akifanya amali za watu wa Jahanamu, na hata akifanya amali yoyote.”

Kisha akaashiria kwa ngumi yake na akasema,

«فَرَعَّ رَبُّكُمْ عَزَّ وَجَلَّ مِنَ الْعِبَادِ»

“Mola wenu Mlezi Ameshaamua suala la waja Wake.”

Na akafunua mkono wake wa kulia kama anatupa kitu;

«فَرِيضٌ فِي الْجَنَّةِ»

“Kundi la Peponi.” Na akaashiria vivyo hivyo kwa mkono wake wa kushoto;

«فَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ»

“Na kundi lingine litakuwa motoni.”¹

Hayo pia yameandikwa na At-Tirmidhi, na An-Nasa’i; At - Tirmidhi alisema, “*Hasan Sahih Gharib.*”

Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Nadrah alisema, “Sahaba wa Mtume, Abu Abdullah رضي الله عنه, alitembelewa na marafiki zake, na wakamkuta akilia. Wakamuuliza, ‘Nini kinachokuliza? Kwani Mtume ﷺ hakusema,

«خُذْ مِنْ شَارِبِكَ نَمًّا أَفْرَهُ حَتَّى تَلْقَانِي»

“Punguza sharubu na uendelee hivyo mpaka utakapokutana nami?”

Akasema, ‘Ndiyo, lakini nilimsikia Mtume ﷺ akisema;

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَبَضَ بِيَمِينِهِ قُبْضَةً وَأُخْرَى بِالْيَدِ الْأُخْرَى، قَالَ: هَذِهِ لَهُدْيٌ، وَهَذِهِ لَهُدْيٌ، وَلَا أُبَالِي»

“Allah Alichukua kiasi katika Mkono Wake wa Kulia na kingine katika Mkono Wake Mwingine, na akasema, “Hii ni kwa ajili ya huku, na hii ya huku. Na wala Sijali.”

‘Sijui mimi ni wa upande upi.’”³ Kuna Hadithi nyingi kuhusu *Al-Qadr* (Qadari) katika vitabu vya *Sahih*, *Sunan* na *Musnad*. Ni pamoja na yaliyosimuliwa na ‘Ali, Ibn Mas‘ud, Mama A’ishah na Masahaba wengi رضي الله عنهم.

«وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَهُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً»

“***Na Mwenyezi Mungu Angelipenda Angewafanya wote umma mmoja.***”

¹ Ahmad 2:167. (Angalia tanbihi inayofuata).

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:350, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:452, (Silsila ya Hadithi hii ina msimulaji ambaye uhakika wake umegawanyika katika rai mbalimbali. Wengi huichukulia kuwa ni Hadithi Sahihi).

³ Ahmad 4:176.

Yaani, ama wote kuongoka au wote kuwa wapotovu, lakini Amewafanya tofauti, na Yeye Anamhidi Amtakaye kwenye ukweli na Anamuacha apotee Amtakaye, na Amekamilisha Hekima na Dalili kamilifu. Allah تعالى Anasema:

وَلٰكِنْ يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمُونَ مَا لَهُمْ مِنْ وٰلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ

“Lakini Anamuingiza katika Rehema Yake Amtakaye. Na wenye kudhulumu hawana mlinzi wala msaidizi.”

* * *

أَمْرٍ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ فَأَلَّهُ هُوَ الْوَلِيُّ وَهُوَ يُحْيِي
 الْمَوْتَى وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٩﴾ وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ
 شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ ۗ ذَلِكُمْ اللَّهُ رَبِّي عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ
 وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿١٠﴾ فَاطِرُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ
 أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَمِنَ الْأَنْعَامِ أَزْوَاجًا ۗ يَذُرُّكُمْ فِيهِ لَيْسَ
 كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١١﴾ لَهُ مَقَالِيدُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّهُ
 بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٢﴾ * سَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ
 نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى
 وَعِيسَى ۗ أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ ۗ كَبُرَ عَلَى
 الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ ۗ اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَنْ يَشَاءُ
 وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ يُنِيبُ ﴿١٣﴾ وَمَا تَفَرَّقُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا
 جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَعِيًّا ۗ بَيْنَهُمْ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ
 أَجَلٍ مُسَمًّى لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ ۗ وَإِنَّ الَّذِينَ أُورِثُوا الْكِتَابَ مِنْ
 بَعْدِهِمْ لَفِي شَكٍّ مِمَّنْهُ مُرِيبٍ ﴿١٤﴾ فَلِذَلِكَ فَادْعُ ۗ
 وَاسْتَقِمْ كَمَا أُمِرْتَ ۗ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ ۗ وَقُلْ ءَامَنْتُ
 بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ كِتَابٍ ۗ وَأُمِرْتُ لِأَعْدِلَ بَيْنَكُمُ ۗ اللَّهُ
 رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ ۗ لَنَا أَعْمَلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ ۗ لَا حُجَّةَ بَيْنَنَا
 وَبَيْنَكُمُ ۗ اللَّهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا ۗ وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿١٥﴾

أَمْرٍ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ فَأَلَّهُ هُوَ الْوَلِيُّ وَهُوَ يُحْيِي
 الْمَوْتَى وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٩﴾ وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ
 مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ ۗ ذَلِكُمْ اللَّهُ رَبِّي عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ
 وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿١٠﴾ فَاطِرُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ
 أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَمِنَ الْأَنْعَامِ أَزْوَاجًا ۗ يَذُرُّكُمْ فِيهِ لَيْسَ
 كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١١﴾ لَهُ مَقَالِيدُ
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ
 وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٢﴾

9. Au wamechukua walinzi
 wengine badala Yake!
 Lakini Mwenyezi Mungu
 Ndiye Mlinzi khasa. Na
 Yeye Ndiye Anayehuisa
 wafu. Na Yeye Ndiye
 Muweza wa kila kitu.

10. Na mkikhitalifiana
 katika jambo lolote, basi
 hukumu yake iko kwa
 Mwenyezi Mungu. Huyo

Mwenyezi Mungu Ndiye Mola Wangu Mlezi, ninayemtegemea na Kwake Yeye narejea.

11. Yeye Ndiye Muumba mbingu na ardhi, Amekujaalieni mke na mume katika nafsi zenu, na katika wanyama hoa, wake kwa waume, Anakuzidishieni namna hii. Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.

12. Yeye Ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi. Humkunjulia riziki Amtakaye, na Humkadiria Amtakaye. Hakika Yeye ni Mjuzi wa kila kitu.

Allah تعالیٰ ni Mlinzi, Mtawala na Muumbaji

Hapa Allah تعالیٰ Anawakanusha washirikina kwa kuiabudu miungu mingine badala ya Allah تعالیٰ, na Anatangaza kuwa Yeye ni Mungu wa kweli, na si haki kumuabudu yeyote isipokuwa Yeye Peke Yake. Yeye ni Mmoja Mwenye Uwezo wa Kufufua wafu na Ndiye Mwenye uwezo wa kila kitu. Kisha Anasema:

وَمَا آخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

“Na mkikhitalifiana katika jambo lolote, basi hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, katika lolote mnalotofautiana. Hiyo ina maana ya ujumla na inatumika kwa vitu vyote.

فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

“...basi hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, Yeye ni Hakimu wa hayo, kwa mujibu wa Kitabu Chake na Sunnah ya Mtume Wake.

Hii inafanana na Aya:

فَإِنْ تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ

“Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume.” (4:59).

ذَٰلِكُمْ أَلَّفَهُ بَيْنِي

“Yeye Mwenyezi Mungu Ndiye Mola Wangu Mlezi.”

Yaani, (Yeye ni) Hakimu wa vitu vyote.

عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ

“...ninayemtegemea na Kwake Yeye narejea.”

Yaani, ‘mambo yote ninayarejesha Kwake.’

فَاطِرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

“Yeye Ndiye Muumba mbingu na ardhi.”

Yaani, Aliyeziumba na vilivyo baina ya hivyo viwili.

جَعَلَ لَكُم مِّنْ اَنْفُسِكُمْ اَزْوَاجًا

“...Amekujaalieni mke na mume katika nafsi zenu.”

Yaani, wa mfano wenu. Kama Neema na Fadhila Zake, Amefanya namna yenu, mwanamume na mwanamke.

وَمِنَ الْاَنْعَامِ اَزْوَاجًا

“...na katika wanyama, hoa dume na jike.”

Yaani, na Amekuumbieni jozi nane za mifugo.

يَذَرُوكُمْ فِيْهِ

“...Anakuzidishieni namna hii.”

Yaani, kwa namna hiyo, Amekuumbeni, mwanamume na mwanamke, kizazi baada ya kizazi cha watu na mifugo.

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ

“Hapana kitu kama mfano wake.” Yaani, hakuna aliye kama Muumbaji wa jozi hizo, kwani Yeye ni wa Kipekee, Bwana Anayejitosheliza, Asiye na mwenzi wala wa kulingana.

وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

“Naye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.”

لَهُ مَقَالِيدُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ^ط

“Yeye Ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi.”

Tumeshaeleza tafsiri ya maneno hayo katika Surat Az-Zumar (39:63), kwa ujumla ni kwamba Yeye ni Mmoja Anayejitosheleza na Kukidhibiti kila kitu katika mbingu na ardhi.

يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ^ط

“Humkunjulia riziki Amtakaye, na Humpimia...”

Yaani, Anamkunjulia riziki Amtakaye na Anaipunguza kwa Amtakaye, na Yeye ni Mwingi wa Hekima na Mwadilifu.

إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“Hakika Yeye ni Mjuzi wa kila kitu.”

* شَرَعَ لَكُم مِّنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَى وَعِيسَى^ط أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ^ط كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ^ط اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَن يُنِيبُ ﴿١٣﴾ وَمَا تَفَرَّقُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ^ط وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى لَّفُضِيَ بَيْنَهُمْ^ط وَإِنَّ الدِّينَ أَوْرَثُوا الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِهِمْ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيبٍ ﴿١٤﴾

13. Amekuamrisheni Dini ile ile aliyomuusia Nuhu na Tuliyo-kufunulia wewe, na Tuliyouwasia Ibrahim na Musa na Isa, kwamba simamisheni Dini wala msifarikiane kwayo. Ni ngumu kwa washirikina hayo unayowaitia. Mwenyezi Mungu humchagua Kwake amtakaye, na humuongoa Kwake aelekeaye.

14. Na hawakutengana ila baada ya kuwajia ilimu kwa sababu ya husuda iliyo kuwa baina yao. Na lau kuwa haikwisha tangulia kauli kutoka kwa Mola wako Mlezi ya kuakhirisha mpaka muda maalumu, basi bila ya shaka palingelihukumiwa baina yao. Na hakika waliorithishwa Kitabu baada yao wanakitilia shaka inayowahangaisha.

Dini ya Mitume ni Moja

Allah تعالی Anauambia Umati huu:

شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّى بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ

“Amekuamrishi Dini ile ile Aliyomuusia Nuhu na Tuliyokufunulia wewe,”

Allah تعالی Anamtaja Mtume wa kwanza kutumwa baada ya Adam عليه السلام, ambaye ni, Nabii Nuh عليه السلام, na wa mwisho ni Mtume Muhammad . Kisha Anataja waliokuja baina yao Mitume waliopata matatizo na shida kubwa ambao ni Nabii Nuhu عليه السلام, Nabii Ibrahim عليه السلام, Nabii Musa عليه السلام, Nabii Isa bin Maryam عليه السلام na Mtume Muhammad ﷺ. Aya hii inawataja wote watano, kama walivyotajwa pia katika Aya ndani ya Surat Al-Ahzab, ambapo Allah تعالی Anasema:

وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنْكَ وَمِنْ نُوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ ابْنِ مَرْيَمَ

“Na Tulipochukua ahadi kwa Manabii na kwako wewe, na Nuhu na Ibrahim na Isa mwana wa Mariamu.” (33:7).

Ujumbe walioleta Mitume wote ulikuwa kumuabudu Allah تعالی Peke Yake, bila ya mwenza au mshirika, kama Anavyosema Allah تعالی:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana Mola isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.” (21:25).

Na kwa mujibu wa Hadithi (Mtume ﷺ amesema):

«نَحْنُ مَعَشَرَ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عَالَمَاتٍ، وَبَيْنَنَا وَاجِدُهُ»

“Sisi Mitume ni ndugu na Dini yetu ni moja.”

Kwa maana mfungamano uliopo kwa wote hao ni kuwa, Allah تعالى Peke Yake Ndiye Anayestahiki kuabudiwa, bila ya mwenza au mshirika, ingawa sheria zao zinaweza kutofautiana. Kama Anavyosema Allah تعالى.

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شَرْعَةً وَمِنْهَا جَاءَ

“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuekea sharia yake na njia yake.”
(5:48).

Allah تعالى Anasema hapa:

أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ

“...kwamba shikeni Dini wala msifarikiane kwayo.”

Maana yake, Allah تعالى Aliwaamrisha Mitume wote wawe kitu kimoja na Aliwakataza kutofautiana na kugawanyika.

كَبُرَ عَلَى الْمُشْرِكِينَ مَا تَدْعُوهُمْ إِلَيْهِ

“Ni magumu kwa washirikina hayo unayowaitia.”

Yaani, ‘hawawezi kustahamili, na wanachukia unalowaitia, Ewe Muhammad, yaani, *Tawhid*.’

اللَّهُ يَجْتَبِي إِلَيْهِ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ يُنِيبُ

“Mwenyezi Mungu Humteua Kwake Amtakaye, na Humuongoa Kwake aelekeaye.”

Yaani, Yeye ni Mmoja Anayewapa uongofu wenye kustahiki, na Kuwaacha kwenye upotovu wenye kuuchagua huo badala ya njia iliyonyooka.

Allah تعالى Anasema hapa:

وَمَا تَفَرَّقُوا إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ

“Na hawakufarikiana ila baada ya kuwajia ilimu...”

Yaani, kupinga kwao ukweli kulikuja baada ya ukweli huo kuwafikia na baada ya kuthibitishiwa. Hakuna kilichowafanya wawe hivyo isipokuwa madhambi yao na ukaidi.

وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى

“Na lau kuwa haikwishatangulia kauli kutoka kwa Mola wako Mlezi ya kuakhirisha mpaka muda maalumu.”

Yaani, kama isingekuwa ukweli kuwa Allah تعالى tayari Alishahukumu kuwa Angechelewesha hesabu ya waja Wake mpaka Siku ya Kiama, wangeharakishiwa adhabu duniani.

وَإِنَّ الَّذِينَ أُورِثُوا الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِهِمْ

“... Na hakika waliorithiwa Kitabu baada yao...”

Yaani, kizazi kilichokuja baada ya cha mwanzo kilichokataa ukweli.

لَفِي شَكٍّ مِنْهُ مُرِيبٍ

“...wanakitilia shaka inayowahangaisha.”

Yaani, hawana usadikishaji imara katika mambo ya dini; wao wanawaiga wahenga wao tu, bila ya ushahidi au dalili yoyote. Hivyo wana kiwewe na mashaka.

فَلَذَلِكَ فَادَعُ ۖ وَاسْتَقِمْ ۖ كَمَا أُمِرْتَ ۖ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ ۖ وَقُلْ ءَامَنْتُ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ

مِنْ كِتَابٍ ۖ وَأُمِرْتُ لِأَعْدِلَ بَيْنَكُمُ ۖ اللَّهُ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ ۖ لَنَا أَعْمَلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَالُكُمْ ۖ لَا

حُجَّةَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ ۖ اللَّهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا ۖ وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ ﴿٤٥﴾

15. Basi kwa haya waite! Nawe simama sawa sawa kama ulivyoamrisha, wala usiyafuate matamano yao. Na sema: Naamini aliyoteremsha Mwenyezi Mungu katika Vitabu. Na nimeamrisha nifanye uadilifu baina yenu. Mwenyezi Mungu ni Mola wetu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Sisi tuna jukumu kwa vitendo vyetu, na nyinyi mna jukumu kwa vitendo vyenu. Hapana kuhojiana baina yetu na nyinyi. Na Mwenyezi Mungu Atatukusanya pamoja, na marejeo ni Kwake.

Aya hii Ina mambo kumi tofauti, kila moja ni hukumu inayojitegemea.

(Wanazuoni) walisema kuwa katika Qur'an hakuna aya nyingine yenye kufanana na aya hii, isipokuwa *Ayat Al-Kursi* 2:255, ambayo pia ina habari kumi.

فَلْيَذْكِفَكَ فَأَدْعُ

"Basi kwa haya waite!"

Yaani, 'basi waite watu kwenye haya Tuli yokuteremshia na Tuli yowaagiza Mitume wa kabla yako,' Mitume wa mfumo mkuu wa Shari'ah uliofuatwa na wengi, kama vile Mitume waliopata tabu na shida kubwa, na wengine.

وَأَسْتَقِمَّ كَمَا أَمَرْتُ

"Nawe simama sawa sawa kama ulivyoamrisha."

Yaani, 'shikamana na wanaokufuata, katika kumuabudu Allah تعالى kama Alivyokuamrisha."

وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ

"...wala usiyafuate matamaniao yao."

Yaani, matakwa ya washirikina, katika mambo waliyozusha kwa kuabudu masanamu.

وَقُلْ ءَامَنْتُ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ مِنْ كِتَابٍ

"Na sema: Naamini aliyoteremsha Mwenyezi Mungu katika Vitabu."

Yaani, 'Ninaamini vitabu vyote walivyoteremshiwa Mitume kutoka mbinguni; hatumtofautishi yeyote kati yao.'

وَأُورِثُ لِعَدِلٍ بَيْنَكُمْ

"Na nimeamrisha nifanye uadilifu baina yenu."

Yaani, wakati wa kuhukumu kwa kufuata Amri za Allah تعالى.

اللَّهُ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ

"Mwenyezi Mungu ni Mola wetu Mlezi, na Mola wenu Mlezi."

Yaani, 'Yeye ni Mmoja Anayestahiki kuabudiwa, na hakuna Mungu wa kweli isipokuwa Yeye. Tunasadikisha hilo kwa hiari, na hata kama hamfanyi hivyo kwa hiari, kila mmoja ulimwenguni anamsujudia kwa utii. Yaani kwa kutaka au kwa kutokutaka, yaani kwa kanuni za kimaumbile.'

لَنَّا أَعْمَلْنَا وَلَكُمْ أَعْمَالُكُمْ^ط

“Sisi tuna jukumu kwa vitendo vyetu, na nyinyi mna jukumu kwa vitendo vyenu.”

Yaani, 'hatuna cha kukufanyieni.' Hii inafanana na Aya:

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ أَعْمَالُكُمْ^ط أَنتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

“Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina a’ mali yangu, na nyinyi mna a’ mali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo.” (10:41)

لَا حُجَّةَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ^ط

“Hapana kuhojiana baina yetu na nyinyi.”

Mujahid alisema, “Inamaanisha, hakuna hoja.”¹ As-Suddi alisema, “Hayo yalikuwa kabla ya kuteremshwa Ayah kuhusu kupigana kwa upanga katika vita.” Hii inaendana na mazingira, kwa sababu Ayah hii iliteremshwa Makkah, na Aya kuhusu amri ya kupigana 22:39-40 iliteremshwa baada ya Hijrah.

اللَّهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا^ط

“Na Mwenyezi Mungu Atatokusanya pamoja.”

Yaani, katika Siku ya Kiama. Hii inafanana na Aya:

قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيمُ ﴿٢٦﴾

“Sema: Mola wetu Mlezi Atatokusanya, kisha Atatuhukumu kwa haki; na Yeye Ndiye Hakimu Mwenye kujua.” (34:26).

¹ At-Tabari 21:518.

وَالِيهِ الْمَصِيرُ

"...na marejeo ni Kwake."

Yaani, marejeo ya mwisho katika Siku ya Hesabu.

* * *

وَالَّذِينَ يُحَاجُّونَ فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا اسْتُجِيبَ لَهُمْ حُجَّتُهُمْ دَاحِضَةً عِنْدَ رَبِّهِمْ وَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ وَلَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ﴿١٦﴾
 اللَّهُ الَّذِي أَنْزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَالْمِيزَانَ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ قَرِيبٌ ﴿١٧﴾ يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا آتِيَةٌ أَلَّا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارُونَ فِي السَّاعَةِ لِيَفِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿١٨﴾
 اللَّهُ لَطِيفٌ بِعِبَادِهِ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ﴿١٩﴾ مَنْ كَانَتْ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ وَمَنْ كَانَتْ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ ﴿٢٠﴾ أَمْ لَهُمْ شُرَكَاتُ شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢١﴾
 تَرَى الظَّالِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا كَسَبُوا وَهُوَ وَاقِعٌ بِهِمْ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي رَوْضَاتٍ الْجَنَّاتِ هُمْ مَّا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ذَلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ﴿٢٢﴾

وَالَّذِينَ يُحَاجُّونَ فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا اسْتُجِيبَ لَهُمْ حُجَّتُهُمْ دَاحِضَةً عِنْدَ رَبِّهِمْ وَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ وَلَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ﴿١٦﴾
 اللَّهُ الَّذِي أَنْزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ وَالْمِيزَانَ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ قَرِيبٌ ﴿١٧﴾ يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا آتِيَةٌ أَلَّا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارُونَ فِي السَّاعَةِ لِيَفِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿١٨﴾

16. Na wanaohojiana juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kukubaliwa, hoja za hawa ni baat'ili mbele ya Mola wao Mlezi, na juu yao ipo ghadhabu, na itakuwa kwao adhabu kali.

17. Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeteremsha Kitabu kwa Haki, na Mizani. Na nini kitakachokujuulisha ya kwamba pengine Saa ya Kiyama ipo karibu?

18. Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli. Ama kwa hakika hao wanaobishana katika khabari za hiyo Saa wamo katika upotofu wa mbali kabisa.

Onyo kwa Waliopinga Masuala ya Kidini

Hapa Allah تعالى Anawaonya waliojaribu kuwakwaza waliomuamini Allah تعالى ili wasiifuate njia Yake.

وَالَّذِينَ يُخَاجِرُونَ فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا اسْتُجِيبَ لَهُمْ

“Na wanaohojiana juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kukubaliwa.”

Yaani, walioshindana na waumini waliomuitikia Allah تعالى na Mtume Wake, na kujaribu kuwazuia wasiifuate njia ya uongofu.

مَجْتَمِعَةً دَاخِضَةً عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Hoja za hawa ni baat’ili mbele ya Mola wao Mlezi.”

Yaani, hazina mashiko yoyote mbele ya Allah تعالى.

وَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ

“...na juu yao ipo ghadhabu.” Yaani, kutoka Kwake.

وَلَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ

“...na itakuwa kwao adhabu kali.”

Yaani, katika Siku ya Kiama. Ibn ‘Abbas, na Mujahid walisema, “Walibishana na waumini baada ya kumuitikia Allah تعالى na Mtume Wake, na wakajaribu kuwazuia kufuata njia ya uongofu, kwa matumaini kuwa wangerejea katika *Jahiliyyah*.”¹ Qatadah alisema, “Hao walikuwa Mayahudi na Wakristo waliowaambia, ‘Dini yetu ni bora kuliko dini yenu, Mtume wetu alikuja kabla ya Mtume wenu, na sisi ni bora kuliko nyinyi na karibu zaidi kwa Allah kuliko nyinyi.’”² Hayo ni uongo tu. Kisha Allah تعالى Akasema:

اللَّهُ الَّذِي أَنْزَلَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeteremsha Kitabu kwa Haki.”

Kwa maana, vitabu vilivyoteremshwa kutoka Kwake kwenda kwa Mitume Wake.

¹ At-Tabari 21:518, 519.

² At-Tabari 21:519.

³ At-Tabari 21:520.

وَالْمِيزَانَ

"...na Mizani."

Yaani, haki na uadilifu. Hii ilikuwa rai ya Mujahid na Qatadah. Hii inafanana na Aya:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنْزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

"Kwa hakika Tuliwatuma Mitume Wetu kwa dalili waziwazi, na Tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu." (57:25).

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ ﴿٥٥﴾ أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ﴿٥٦﴾ وَأَقِيمُوا الزُّنْبَانَ ﴿٥٧﴾ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ﴿٥٨﴾

"Na mbingu Ameziinua, na Ameweka mizani, Ili msidhulumu katika mizani. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani." (55:7-9)

وَمَا يَذْرُوكُ لَعَلَّ السَّاعَةَ قَرِيبٌ

"Na nini kitakacho kujuulisha ya kwamba pengine Saa ya Kiyama ipo karibu?"

Hoja hii ni himizo (la kujitahidi) kwa ajili Yake, onyo lenye kutisha, na ni nasaha kuhusu kutokuitanguliza dunia.

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا

"Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi."

Yaani, wanasema, 'ahadi hii itatimizwa lini, kama mnasema kweli,' lakini wao husema haya kwa ukafiri na ukaidi, wakidhania kuwa haiyumkiniki kutokea.

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا

"...lakini wanaoamini wanaiogopa."

Yaani, wanahofu kutokea kwake.

وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا الْحَقُّ

“...na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli.”

Yaani, ambao bila ya shaka yoyote itafika, hivyo wanajiandaa na wanajitahidi kwa ajili yake. Imesimuliwa kupitia riwaya kadhaa, idadi inayofikia kiwango cha *Mutawatir*, katika masimulizi *Sahih* na *Hasan*, katika vitabu vya *Sunan* na *Musnad*. Kwa mujibu wa baadhi ya riwaya, mtu mmoja alimuambia Mtume ﷺ kwa sauti ya juu, alipokuwa katika mojawapo ya safari zake, alimuita, “Ewe Muhammad!” Mtume ﷺ aliitika kwa namna hiyo hiyo, “Niko hapa!” Mtu huyo akasema, “Saa itafika lini.” Mtume ﷺ akasema,

«وَيَنحَكُ إِنَّهَا كَانَتْهُمَا فَمَا أَغْدَدْتَ لَهَا؟»

“Ole wako! Kwa hakika itafika. Umeiandalia nini?”

Akasema, “Kumpenda Allah تعالى na Mtume Wake.” Akasema:

«أَنْتَ مَعَ مَنْ أَحْبَبْتَ»

“Utakuwa pamoja na unaowapenda.”

Kwa mujibu wa Hadithi nyingine:

«الْمَرْءُ مَعَ مَنْ أَحَبَّ»

“Mtu atakuwa pamoja na anaowapenda.”

Hii bila ya shaka ni *Mutawatir*. Cha kuzingatia ni kuwa, hakujiibu swali lake kuhusu Saa itakuwa lini, bali alimuamrisha ajiandae kwa ajili yake.

أَلَا إِنَّ الَّذِينَ يُمَارُونَكَ فِي السَّاعَةِ

“Ama kwa hakika hao wanaobishana...” Yaani, wanaobisha kuja kwake na wanadhani haiyumkiniki kamwe kutokea.

لَيْفَى ضَلَّلِ بِعَيْدٍ

“...wamo katika upotofu wa mbali kabisa.” Yaani, hao ni wajinga kabisa, kwa sababu Aliyeumba mbingu na ardhi Ana uwezo wa Kufufua wafu, kama Anavyosema Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ۗ

“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha viumbe, kisha Atavirudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27).

اللَّهُ لَطِيفٌ بِعِبَادِهِ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ﴿١٦﴾ مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ
 الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ ۗ وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ
 مِنْ نَصِيبٍ ﴿١٧﴾ أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ وَلَوْلَا
 كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨﴾ تَرَى الظَّالِمِينَ
 مُشْفِقِينَ مِمَّا كَسَبُوا وَهُوَ وَاقِعٌ بِهِمْ ۗ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي رَوْضَاتِ
 الْجَنَّاتِ ۗ هُمْ مَّا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ ذَلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ ﴿١٩﴾

19. Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja Wake. Humruzuku Amtakaye. Naye ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.

20. Mwenye kutaka mavuno ya Akhera Tutamzidishia katika mavuno yake, na mwenye kutaka mavuno ya duniani Tutampa katika hayo, lakini katika Akhera hana fungu.

21. Au hao wana washirika wa kishirikina waliowawekea dini asiyoitolea Idhini Mwenyezi Mungu? Na lau lisingekuwako neno la kupambanua basi ingelikatwa hukumu baina yao. Na hakika wenye kudhulumu watapata adhabu chungu.

22. Utawaona hao madhaalimu wanavyokuwa na khofu kwa sababu ya waliyoyachuma, nayo yatawafika tu. Na walioamini na wakatenda mema watakuwamo katika bustani za Peponi. Humo watapata wayatakayo kwa Mola wao Mlezi. Hiyo ndiyo Fadhila kubwa.

Riziki ya Allah تعالى na Ugawaji wake Duniani na Akhera

Hapa Allah تعالى Anazungumzia wema Wake kwa Viumbe Wake, kwa Kumpa kila mmoja wao bila kumsahau yeyote katika riziki Yake, Huwagaiya basi hupata wema na waovu. Allah تعالى Anasema:

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابٍ

مُتَّبِعِينَ

“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6)

Na kuna Aya nyingi kama hiyo.

يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ

“Humruzuku ampendaye.” Yaani, Anampa kwa ukarimu yeyote Amtakaye.

وَهُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ

“Naye ni Mwenye Nguvu, Mtukufu.”

Yaani, hakuna wa kumshinda. Kisha Allah Anasema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ

“Mwenye kutaka mavuno ya Akhera...”

Yaani, anayetenda kwa ajili ya Akhera,

نَزَدَ لَهُ فِي حَرْثِهِ

“...Tutamzidishia katika mavuno yake.”

Maana yake, ‘Tutampa nguvu na Kumsaidia afanye anachotaka, na Tutamzidishia. Hivyo kwa kila jema, Tutamzidishia na kumpa baina ya malipo mema kumi na mia saba,’ kadiri ya Anavyotaka Allah تعالى.

وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ

“...na mwenye kutaka mavuno ya duniani Tutampa katika hayo, lakini katika Akhera hana fungu.”

Yaani, anayejitahidi kwa ajili ya kupata manufaa ya kidunia tu, na wala hana habari kabisa na Akhera, Allah تعالی Atamnyima Akhera na duniani. Kama Allah تعالی Akitaka Atampa, na kama Hataki hatapata kitu. Hivyo anayejitahidi kwa lengo hilo, atapata hasara duniani na Akhera. Ushahidi wa hayo ni kuwa Aya hii maelezo yake yamekuja kuhusishwa kwa kuwekewa mpaka na aya iliyopo katika sura ya *Subhan* (yaani, *Surat Al-Isra*) ambamo Allah تعالی Anasema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصَلِّيهَا
 مَذْمُومًا مَدْحُورًا ﴿١٦﴾ وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ
 سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٧﴾ كُلًّا نُمِدُّ هُنُوًا وَهَنُورًا ۖ وَمِنْ عَطَايَ رَبِّكَ ۗ وَمَا كَانَ عَطَايَ
 رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿١٨﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۗ وَلَلْآخِرَةُ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ
 تَفْضِيلًا ﴿١٩﴾

“Anayetaka yapitayo upesi upesi, Tutafanya haraka kumletea hapa hapa Tunayoyataka kwa Tumtakaye. Kisha Tumemuekea Jahannamu; ataingia humo hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa na kufurushwa. Na anayeitaka Akhera, na akazifanyia juhudi a’ mali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa. Wote hao Tunawakunjulia - hawa na hao - katika neema za Mola wako Mlezi. Wala neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki. Angalia vipi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wengine. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na Fadhila kubwa zaidi.” (17:18-21)

Imesimuliwa kuwa Ubayy bin Ka’b رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«بَشِّرْ هَذِهِ الْأُمَّةَ بِالسَّعَاءِ وَالرَّفْعَةِ وَالنُّصْرِ وَالتَّمْكِينِ فِي الْأَرْضِ، فَمَنْ عَمِلَ مِنْهُمْ
 عَمَلَ الْآخِرَةِ لِلدُّنْيَا، لَمْ يَكُنْ لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ»

“Ubashirie Ummah huu utukufu, hadhi ya juu, ushindi na uthabiti katika ardh. Lakini yeyote miongoni mwao afanyae amali za Akhera kwa ajili ya manufaa ya kidunia, hatakuwa na fungu Akhera.”¹

¹ Ahmad 5:134.

Kuwatungia Sheria Viumbe ni katika Kumshirikisha Allah تعالى

Allah تعالى Anasema:

أَمْ لَهُمْ شُرَكَتُؤُا شَرَعُوا لَهُمْ مِنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَنْ بِهِ اللَّهُ

“Au hao wana miungu ya kishirikina waliowatungia dini asiyoitolea Idhini Mwenyezi Mungu?”

Yaani, hawafuati dini iliyonyooka aliyokuamrisha Allah تعالى; badala yake, wanafuata waliyoagizwa na mashetani, watu na majini. Wamejiharamishia wao wenyewe kwa kuzusha miiko, kama vile *Bahirah*. *Bahirah* ni Ngamia ambaye katika kipindi cha Ujahili, anapozaa watoto watano humpasua sikio lake, na hujizuia kunufaika na Ngamia huyo, na wala hawamkatazi katika kulisha kwake au kunywa maji. Uislamu ulivyokuja ulibatilisha mila hizi.¹

Pia wamehalalisha ulaji wa nyama na damu za wanyama wasiochinjwa kwa ajili ya kula, kamari na aina nyingine za upotovu, ujinga na upotovu. Hayo ni mambo waliyoyazua katika enzi za *Jahiliyyah*, walipoleta kila namna ya hukumu potovu juu ya halali na haramu, ibada potovu na fikra zingine mbaya. Imeandikwa katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema:

«رَأَيْتُ عَمْرَو بْنَ لُحَيِّ بْنِ قَمَعَةَ يَجْرُ قُضْبَهُ فِي النَّارِ»

*“Nilimuona ‘Amr bin Luhayy bin Qama’ah akiburuza matumbo yake katika Jahanamu.”*²

Kwa sababu alianzisha fikra ya *Sa’ibah*. Mtu huyo alikuwa mfalme wa kabila la Khuza’ah, na alikuwa wa kwanza kufanya hayo. Ndiye aliyewafanya Quraysh waabudu masanamu, Allah Amlaani. Allah تعالى Alisema:

وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ

“Na lau lisingekuwako neno la kupambanua basi wangelikatiwa hukumu baina yao.”

¹ Ili kupata maelezo ya jambo hilo, angalia juzuu ya tatu, *Tafsir ya Surat Al-Maidah* 5:103.

² *Fat’h Al-Bari* 6:633.

Yaani, wangeharakishiwa adhabu, kama isingelikuwa hayo yaliyotangulia katika maonyo, mpaka Siku ya Kiama.

وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Na hakika wenye kudhulumu watapata adhabu chungu.”

Yaani, adhabu iumizayo katika Jahanamu, nayo ni makazi mabaya mno.

Mfazaiko wa Washirikina katika Kiwanja cha Kukusanywa Watu

Allah تعالى Anasema:

تَرَى الظَّالِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا كَسَبُوا

“Utawaona hao madhaalimu wanavyokuwa na khofu kwa sababu ya waliyo yachuma.”

Yaani, katika uwanja wa Ufufuo.

وَهُوَ وَاقِعٌ بِهِمْ

“...nayo yatawafika tu.”

Yaani, wanayoyaogopa yatawafikia kwa hakika. Hivyo ndivyo watakavyokuwa katika Siku ya Kiama; watakuwa na hofu kubwa.

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي رَوْضَاتِ الْجَنَّاتِ هُمْ مَا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Na walioamini na wakatenda mema watakuwamo katika bustani za Peponi. Humo watapata wayatakayo kwa Mola wao Mlezi.”

Hakuna mshabihiano hapa baina ya watu wa Motoni na wa Peponi. Vipi aliye katika hali ya udhalili mkubwa na hofu katika eneo la Ufufuo, kwa sababu ya maovu yake, ashabihiane na yule ataka yekuwa katika bustani za Peponi, akifurahia vyakula, vinywaji, mavazi, mandhari, wanawake na raha katika ambavyo macho hayajaona, hakuna sikio lililosikia, na halijapita akilini mwa watu.

¹ Fat'h Al-Bari 6:633.

Allah تعالى Anasema:

ذَلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيرُ

“Hiyo ndiyo Fadhila kubwa.”

Yaani, ushindi mkubwa na neema kamili.

* * *

ذَلِكَ الَّذِي يُبَشِّرُ اللَّهَ عِبَادَهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۗ قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ۗ وَمَن يَقْتَرِفْ حَسَنَةً نَّزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْنًا ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٢٣﴾ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۗ فَإِن يَشَأِ اللَّهُ يَخْتِمْ عَلَىٰ قَلْبِكَ ۗ وَيَمْحُ اللَّهُ الْبَاطِلَ وَيُخَيِّطُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢٤﴾ وَهُوَ الَّذِي يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَن عِبَادِهِ وَيَعْفُو عَنِ السَّيِّئَاتِ وَيَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٢٥﴾ وَتَسْتَجِيبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَيَزِيدُهُم مِّن فَضْلِهِ ۗ وَالْكَافِرُونَ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ﴿٢٦﴾ * وَلَوْ بَسَطَ اللَّهُ الرِّزْقَ لِعِبَادِهِ لَبَغَوْا فِي الْأَرْضِ وَلَٰكِن يُنَزِّلُ بِقَدَرٍ مَّا يَشَاءُ ۗ إِنَّهُ بِعِبَادِهِ خَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٢٧﴾ وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِن بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنشُرُ رَحْمَتَهُ ۗ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٨﴾ وَمِن ءَايَاتِهِ خَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا مِن دَابَّةٍ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ جَمْعِهِمْ إِذَا يَشَاءُ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾ وَمَا أَصْبَحُكُمْ مِّن مُّصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَن كَثِيرٍ ﴿٣٠﴾ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ ۗ وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِن وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٣١﴾

ذَلِكَ الَّذِي يُبَشِّرُ اللَّهَ عِبَادَهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ ۗ قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ۗ وَمَن يَقْتَرِفْ حَسَنَةً نَّزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْنًا ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ ﴿٢٣﴾ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۗ فَإِن يَشَأِ اللَّهُ يَخْتِمْ عَلَىٰ قَلْبِكَ ۗ وَيَمْحُ اللَّهُ الْبَاطِلَ وَيُخَيِّطُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٢٤﴾

23. Hayo ndiyo aliyowabashiria Allah waja wake walioamini na wakatenda mema. Sema: "Kwa haya (ninayokufundisheni) Sikuombeni malipo yoyote; lakini (nataka) muyapende mambo ya kukusogezeni (kwa Allah)." Na anayefanya wema Tutamzidishia wema. Hakika Allah ni Msamehevu Mwenye Shukrani.

24. Ati wanasema: Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Mwenyezi Mungu Akipenda Atapiga muhuri juu

ya moyo wako. Na Mwenyezi Mungu Anaufuta upotofu na Anaithibitisha Haki kwa maneno Yake. Hakika Yeye Anayajua yaliomo vifuni.

Habari njema za Neema za Peponi kwa Ajili ya Wenye Imani

Baada ya kutaja bustani za Peponi, Allah تعالى Kisha Anawaambia waja Wake wenye kuamini na kutenda mema:

ذَٰلِكَ الَّذِي يُبَشِّرُ اللَّهَ عِبَادَهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ¹

“Hayo ndiyo aliyowabashiria Mwenyezi Mungu waja wake walioamini na wakatenda mema.”

Maana yake, bila ya shaka hayo yatawakuta, kwa sababu ni bishara kutoka kwa Allah تعالى.

قُلْ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ²

“Sema: “Kwa haya (ninayokufundisheni) Sikuombeni malipo yoyote; lakini (nataka) muyapende mambo ya kukusogezeni (kwa Allah).”

Yaani, ‘sema, Ewe Muhammad, kuwaambia washirikina hao miongoni mwa makafiri wa Quraysh: Sikuombeni chochote kama malipo kwa ajili ya Ujumbe huu na ushauri wa dhati. Ninachokuombeni ni kwamba muache kunifanyia uovu na mniache nifikishe Ujumbe wa Mola wangu Mlezi. Kama hamtanisaidia, basi msinisumbue, kwa ajili ya udugu uliopo kati ya nyinyi na mimi.’ Al-Bukhari ameandika kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, aliulizwa kuhusu Aya hii:

إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ

“...lakini (nataka) muyapende mambo ya kukusogezeni (kwa Allah).”

Sa’ id bin Jubayr alisema, “Kuifanyia wema familia ya Mtume Muhammad.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Hapana, umeharakisha jibu. Koo zote za Quraysh zilikuwa na udugu kwa Mtume ﷺ.” Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Bali ni kwamba, mshikilie udugu uliopo kati yangu na nyinyi.” Haya yaliandikwa na Al-Bukhari.¹

Pia yameandikwa na Imam Ahmad kwa riwaya tofauti.²

¹ Fat’h Al-Bari 8:326.

² Ahmad 1:229.

وَمَنْ يَقْتَرِفْ حَسَنَةً نَّزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْنًا

“Na anayefanya wema Tutamzidishia wema.”

Yaani, ‘anayefanya mema, Tutamzidishia malipo.’ Hii inafanana na Aya:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۗ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُّضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha na Hutoa kutoka Kwake malipo makubwa.” (4:40)

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye shukrani.”

Yaani, Anasamehe amali nyingi mbaya; Anasitiri na Kusamehe madhambi na Anazidisha malipo ya amali njema.

Madai kuwa Mtume ﷺ Amezua Qur’an - na Majibu ya Madai hayo.

Kauli ya Allah تعالى:

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۗ فَإِنْ يَشَأِ اللَّهُ يَخْتِمْ عَلَى قَلْبِكَ ۗ

“Ati wanasema: Amemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Mwenyezi Mungu Akipenda Atapiga muhuri juu ya moyo wako.”

Kwa maana, lau ungemzulia Allah تعالى uwongo kama wanavyodai hawa wajinga;

يَخْتِمْ عَلَى قَلْبِكَ ۗ

“...Atapiga muhuri juu ya moyo wako.”

Yaani, Angeliuziba moyo wako, na kisingekujia tena chochote katika Qur’an. Ni sawa na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿٤١﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿٤٢﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِينَ

﴿٤٣﴾ فَمَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ عَنْهُ حَاجِزِينَ ﴿٤٤﴾

“Na lau kama angelituzulia baadhi ya Maneno tu. Bila ya shaka Tungelimshika kwa mkono wa kulia. Kisha kwa hakika Tungeli mkata mshipa mkubwa wa moyo! Na hapana yeyote katika nyinyi ambaye angeliweza Kutuzuia.” (69:44-47)

Yaani, ‘Tungelimuadhibu vikali na hakuna mwanadamu wa kumhifadhi.’

وَيُحِقُّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ

“...na Anaithibitisha Haki kwa Maneno Yake.”

Yaani, Anauthibitisha na Kuuimarisha na Kudhihirisha kwa Maneno Yake. Yaani, Ushahidi na Ishara Zake.

إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ

“Hakika Yeye Anayajua yaliomo vifuani.”

Yaani, yote yaliyofichikana nyoyoni mwa watu.

وَهُوَ الَّذِي يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَعْفُو عَنِ السَّيِّئَاتِ وَيَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٢٥﴾
 وَيَسْتَجِيبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَيَزِيدُهُمْ مِنْ فَضْلِهِ ؕ وَالْكَافِرُونَ هُمْ عَذَابٌ
 شَدِيدٌ ﴿٢٦﴾ * وَلَوْ بَسَطَ اللَّهُ الرِّزْقَ لِعِبَادِهِ لَبَغَوْا فِي الْأَرْضِ وَلَكِنْ يُنَزِّلُ بِقَدَرٍ مَّا يَشَاءُ
 ؕ إِنَّهُ بِعِبَادِهِ خَبِيرٌ بَصِيرٌ ﴿٢٧﴾ وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنْشُرُ
 رَحْمَتَهُ ؕ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٨﴾

25. Naye Ndiye Anayepokea toba kutoka kwa waja wake, na Anasamehe makosa, na Anayajua mnayoyatenda.

26. Na Anawaitikia wanaoamini na wakatenda mema, na Anawazidishia Fadhila Zake. Na makafiri watakuwa na adhabu chungu.

27. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwakunjulia riziki waja Wake, basi bila ya shaka wangelipanda kiburi katika dunia. Lakini Anaiteremsha kwa kipimo Akitakacho. Hakika Yeye Anawajua vyema waja Wake na Anawaona.

28. Naye Ndiye Anayeiteremsha mvua baada ya wao kwisha kata tamaa, na Hueneza Rehema Yake. Naye Ndiye Mlinzi Mwenye Kushukuriwa.

Allah تعالیٰ Anakubali Toba na Anapokea Dua

Hapa Allah تعالیٰ Anawakumbusha waja Wake kuwa Anapokea toba. Kama wanamgeukia na kurejea Kwake, basi kwa Wema na Ukirimu Wake Anasamehe, na Kusitiri (madhambi yao). Kama Anavyosema:

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٤١﴾

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwenye Kurehemu.” (4:110)

Imesimuliwa katika Sahih Muslim kwamba Anas bin Malik رضي الله عنه, alisema, “Mtume ﷺ amesema:

«اللَّهُ تَعَالَىٰ أَشَدُّ فَرَحًا بِتَوْبَةِ عَبْدِهِ - جِبْنَ يَتُوبُ إِلَيْهِ - مِنْ أَحَدِكُمْ كَمَا نَتَّ رَاحِلَتُهُ بِأَرْضِ فَلَاةٍ، فَأَنْقَلَتُ مِنْهُ، وَعَلَيْهَا طَعَامُهُ وَسُرَابُهُ، فَأَيْسَ مِنْهَا فَأَتَى شَجْرَةً فَأَضْطَجَعَ فِي ظِلِّهَا، فَذُ أَيَسَ مِنْ رَاحِلَتِهِ، فَبَيْنَمَا هُوَ كَذَلِكَ إِذَا هُوَ بِهَا، فَأَيْمَةً عِنْدَهُ، فَأَخَذَ بِخَطَامِهَا، ثُمَّ قَالَ مِنْ شِدَّةِ الْفَرَحِ: اللَّهُمَّ أَنْتَ عَبْدِي وَأَنَا رَبُّكَ، أَخْطَأُ مِنْ شِدَّةِ الْفَرَحِ»

“Allah Anafurahishwa sana na toba ya mja Wake kuliko yeyote katika nyinyi aliyempoteza mnyama wake wa kuendesha katika jangwa, mwenye kubeba chakula na kinywaji chake; anakata tamaa ya kumpata, basi anaenda kwenye mti na kulala katika kivuli chake, bila matumaini yoyote ya kumpata mnyama na kipando chake hapo katika hali hiyo, ghafla anamuona amesimama karibu yake, basi anakamata hatamu zake na kutokana na kufurahi sana, anasema, “Ewe Allah, Wewe ni mja na mimi ni Mola wako Mlezi!”- yaani anakosea kwa sababu ya kufurahi sana.”¹

¹ Muslim 4:2104.

Riwaya kama hiyo pia imesimuliwa katika Sahih kutoka kwa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه.¹

وَهُوَ الَّذِي يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

“Naye Ndiye Anayepokea toba kutoka kwa waja Wake.”

Imesimuliwa kuwa Az-Zuhri رحمه الله تعالى alisema, kuhusu Aya hii, kwamba Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«اللَّهُ أَشَدُّ فَرَحًا بِتَوْبَةِ عَبْدِهِ مِنْ أَحَدِكُمْ يَجِدُ ضَالَّتَهُ فِي الْمَكَانِ الَّذِي يَخَافُ أَنْ يَقْتُلَهُ فِيهِ الْعَطَشُ»

“Allah Anafurahia zaidi toba ya mja Wake kuliko mtu anavyohisi anapompata ngamia wake aliyepotea mahali alipohofia kuwa angekufa kwa kiu.”²

Hammam bin Al-Harith alisema, “Ibn Mas'ud رضي الله عنه aliulizwa kuhusu mtu aliyetenda madhambi mabaya na mwanamke halafu akamuoa. Alisema, ‘Hakuna ubaya katika hilo,’ na akasoma:

وَهُوَ الَّذِي يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

“...Naye Ndiye Anayepokea toba kwa waja Wake.”³

وَيَعْفُوا عَنِ السَّيِّئَاتِ

“...na Anasamehe makosa.”

Yaani, Atakubali toba baadaye, na Anasamehe madhambi yaliyopita.

وَيَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ

“...na Anayajua mnayoyatenda.”

Yaani, anajua amali zenu zote na vitendo na maneno, lakini Anapokea toba ya waliotubia Kwake.

¹ Muslim 4:2105.

² 'Abdur-Razzaq 3:191.

³ At-Tabari 21:533.

وَيَسْتَجِيبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Na Anawaitikia wanaoamini na wakatenda mema.”

As-Suddi alisema, “Inamaanisha, Anawajibu.” Hii ilikuwa pia rai ya Ibn Jarir: “Maana yake, Anajibu dua zao kwa ajili yao wenyewe, na rafiki zao na ndugu.”¹

وَيَزِيدُهُمْ مِّنْ فَضْلِهِ^٢

“...na Anawazidishia Fadhila Zake.”

Yaani, Anajibu dua na Anawazidishia. Qatadah alisema, akisimulia kutoka kwa Ibrahim An-Nakha'i Al-Lakhmi kuhusu Aya:

وَيَسْتَجِيبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Na Anawaitikia wanaoamini na wakatenda mema,”

(Inamaanisha) wanawaombea ndugu zao.

وَيَزِيدُهُمْ مِّنْ فَضْلِهِ^٢

“...na Anawazidishia Fadhila Zake.”

(Inamaanisha) wanawaombea ndugu wa ndugu zao.²

وَالْكَافِرُونَ هُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ

“Na makafiri watakuwa na adhabu chungu.”

Baada ya kuwataja waumini na jaza yao kubwa, halafu Allah تعالى Anawataja makafiri na adhabu yao kali, yenye kuumiza, watakaoipata Kwake katika Siku ya Kiama, watakapohesabiwa.

¹ At-Tabari 21:534.

² At-Tabari 21:534.

Sababu ya Kutokuongezewa Kipato.

Allah تعالى Anasema:

وَلَوْ بَسَطَ اللَّهُ الرِّزْقَ لِعِبَادِهِ لَبَغَوْا فِي الْأَرْضِ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwakunjulia riziki waja Wake, basi bila ya shaka wangelipanda kiburi katika dunia.”

Yaani, ‘Tungewaruzuku zaidi ya haja zao, wangeasi na kuruka mipaka baina yao kwa kiburi na ufidhuli.’

وَلَكِنْ يُنَزَّلُ بِقَدَرٍ مَّا يَشَاءُ ۚ إِنَّهُ بِعِبَادِهِ خَبِيرٌ بَصِيرٌ

“Lakini Anaiteremsha kwa kipimo Akitakacho. Hakika Yeye Anawajua vyema waja Wake na Anawaona.”

Yaani, lakini Huwapa riziki kulingana na mahitaji yao bora zaidi, na Allah تعالى Anajua zaidi hayo. Hivyo Anamtajirisha anayestahiki kutajirika, na Anamfanya maskini anayestahiki hivyo.

وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَتَلُوا

“Naye Ndiye Anayeteremsha mvua baada ya wao kwisha kata tamaa.”

Yaani, baada ya watu kukata tamaa ya kunyeshwa mvua, Anawapelekea wakati inapohitajika kwao. Hii inafanana na Aya:

وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلِ أَنْ يُنَزَّلَ عَلَيْهِمْ مِنْ قَبْلِهِ لَمُبْلِسِينَ ﴿٤٩﴾

“Na ingawa kabla ya kuteremshiwa walikuwa wenye kukata tamaa.” (30:49)

وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهُ

“...na Hueneza Rehema Yake.”

Yaani, Anawaneemesha nayo watu wote wanaoishi katika eneo hilo. Qatadah alisema, “Tuliambiwa kuwa mtu mmoja alimuambia ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, ‘Ewe Amiri wa Waumini, mvua hainyeshi na watu wamekata tamaa.’ ‘Umar رضي الله عنه, alisema, ‘Mvua itanyesha kwenu,’ na akasoma:

وَهُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْ بَعْدِ مَا قَنَطُوا وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهُ ۗ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْأَحْمَدُ ﴿٢٩﴾

“Naye Ndiye Anayeiteremsha mvua baada ya wao kwisha kata tamaa, na Hueneza Rehema Yake. Naye Ndiye Mlinzi Mwenye Kuhimidiwa.”¹

Maana yake, Yeye ni Mmoja Anayewadhibiti Viumbe Wake, kwa Kuwapa yenye Kuwafaa duniani na Akhera, na matokeo ya Hukumu Zake na Matendo Yake ni mema, ambapo Yeye Ndiye Anayestahiki sifa zote njema.

وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا مِنْ دَابَّةٍ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ جَمْعِهِمْ إِذَا

يَشَاءُ قَدِيرٌ ﴿٣٠﴾ وَمَا أَصَابَكُمْ مِنْ مُصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبْتُمْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ ﴿٣١﴾

وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ ۗ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٣٢﴾

29. Na katika Ishara Zake ni Kuumba mbingu na ardhi, na viumbe vyenye uhai Alivyovieneza humo. Naye ni Mwenye Uweza wa Kuwakusanya apendapo.

30. Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu. Naye Anasamehe mengi.

31. Na nyinyi hamuezi kumshinda katika ardhi. Na wala nyinyi hamna mlinzi wala msaidizi badala ya Mwenyezi Mungu.

Miongoni mwa ishara za Allah تعالیٰ ni Kuumbwa Mbingu na Ardhi.

Allah تعالیٰ Anasema:

وَمِنْ آيَاتِهِ

“Na katika Ishara Zake...”

Ishara zenye kuonesha Uweza Wake Mkubwa,

خَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا

“...ni Kuumba mbingu na ardhi, na viumbe vyenye uhai Alivyo-vieneza humo.”

¹ At-Tabari 21:537

Yaani, vyote Alivyumba baina yake, yaani, mbinguni na ardhini.

مِن دَابَّةٍ

“...na viumbe vyenye uhai...”

Wakiwemo Malaika, wanadamu, majini na wanyama wote wa maumbo mbalimbali, rangi, lugha, tabia, sampuli na aina zao. Amewaeneza kote mbinguni na ardhini.

وَهُوَ

“Naye...”

Yaani, lakini licha ya hayo yote,

عَلَىٰ جَمْعِهِمْ إِذَا يَشَاءُ قَدِيرٌ

“Naye ni Mwenye Uweza wa Kuwakusanya Apendapo.”

Yaani, katika Siku ya Kiama, Atawakusanya wa mwanzo na wa mwisho wao, na Kuwakusanya viumbe Wake wote katika sehemu moja ambapo wote watasikia sauti ya anayenadi na wote wataonekana waziwazi; Kisha Atahukumu baina yao kwa haki na ukweli.

Mabalaa Huletwa na Dhambi.

Allah تعالى Anasema:

وَمَا أَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فِيمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ

“Na misiba inayokusibuni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu.”

Yaani, ‘balaa lolote lenye kukupateni, enyi wanadamu, husababishwa na madhambi mliyofanya katika siku za nyuma.’

وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ

“Naye Anasamehe mengi.”

Yaani, madhambi; ‘Hakuadhibuni, bali Anakusameheni.’

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهَرِهَا مِنْ دَابَّةٍ

“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwaadhibu watu kwa waliyoyachuma, basi Asingelimuacha juu ya ardhi hata kiumbe mmoja.” (35:45).

Kwa mujibu wa Hadithi Sahihi:

«وَالَّذِي تَفْسِي بِيَدِهِ مَا يُصِيبُ الْمُؤْمِنِينَ مِنْ نَصَبٍ وَلَا وَصْبٍ وَلَا هَمٍّ وَلَا حَزَنِ إِلَّا كَفَّرَ اللَّهُ عَنْهُ بِهَا مِنْ خَطَايَاهُ، حَتَّى الشُّوْكَةِ يُشَاكُهَا»

“Naapa kwa Ambaye Mkononi Mwake ipo roho yangu, hakuna Muumini anayepatwa na uchovu, maradhi, woga au huzuni, isipokuwa Allah Atamsamehe baadhi ya dhambi zake, hata mwiba unaomchoma.”¹

Imam Ahmad ameandika kuwa Mu'awiyah bin Abi Sufyan رضي الله عنه, alisema, “Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَا مِنْ شَيْءٍ يُصِيبُ الْمُؤْمِنِينَ فِي جَسَدِهِ يُؤْذِيهِ إِلَّا كَفَّرَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ بِهِ مِنْ سَيِّئَاتِهِ»

“Hakuna chochote kinachomsibu Muumini katika mwili wake lenye kumuudhi, isipokuwa Allah Atamfutia baadhi ya dhambi zake kwa sababu hiyo.”²

Imam Ahmad pia ameandika kuwa Mama A'ishah رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا كَثُرَتْ ذُنُوبُ الْعَبْدِ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ مَا يُكْفِرُهَا، ابْتَلَاهُ اللَّهُ تَعَالَى بِالْحَزَنِ لِيَكْفِرَهَا»

“Mtu akitenda dhambi nyingi na hana cha kuyafutia, Allah Atamtahini kwa baadhi ya huzuni zitakazomfutia.”³

* * *

¹ Ahmad 2:303.

² Ahmad 4:98.

³ At-Tabari 21:541.

وَمِنْ آيَاتِهِ الْجَوَارِ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَمِ ﴿٣٢﴾ إِنْ يَشَأْ يُسْكِنِ
 الرِّيحَ فَيَظْلَلْنَ رَوَاكِدَ عَلَى ظَهْرِهِ ؕ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣٣﴾ أَوْ يُوقِنُ بِمَا كَسَبُوا وَيَعْفُ عَن
 كَثِيرٍ ﴿٣٤﴾ وَيَعْلَمَ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِنَا مَا هُمْ مِنْ
 حَيْصٍ ﴿٣٥﴾ فَمَا أُوتِيتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا
 وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْغَىٰ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ
 ﴿٣٦﴾ وَالَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا
 غَضِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا
 الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾
 وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾ وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ
 سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّهُ لَا
 يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٠﴾ وَلَمَنْ آتَنَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَٰئِكَ
 مَا عَلَيْهِمْ مِنْ سَبِيلٍ ﴿٤١﴾ إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ
 يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ أُولَٰئِكَ
 لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٢﴾ وَلَمَنْ صَبَرَ وَعَفَرَ ۗ إِنَّ ذَلِكَ لَمِنْ
 عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿٤٣﴾

وَمِنْ آيَاتِهِ الْجَوَارِ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَمِ ﴿٣٢﴾ إِنْ يَشَأْ يُسْكِنِ
 الرِّيحَ فَيَظْلَلْنَ رَوَاكِدَ عَلَى ظَهْرِهِ ؕ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ
 لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٣٣﴾ أَوْ يُوقِنُ بِمَا كَسَبُوا وَيَعْفُ عَن
 كَثِيرٍ ﴿٣٤﴾ وَيَعْلَمَ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِنَا مَا هُمْ مِنْ
 حَيْصٍ ﴿٣٥﴾

32. Na katika Ishara Zake ni vyombo vinavyokwenda na kurejea baharini kama vilima.

33. Akitaka, Huutuliza upepo navyo hivyo vyombo husimama tutwe juu ya bahari. Hakika katika hayo zipo Aya kwa kila mwenye kusubiri akashu- kuru.

34. Au Huviangamiza hivyo vyombo kwa sababu ya waliyoyatenda hao watu. Naye Husamehe mengi.

35. Na ili wajue wanaojadiliana katika Aya Zetu kwamba hawana pahala pa kukimbilia.

Meli pia ni Katika Ishara za Allah تعالیٰ

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa alama nyingine ya Nguvu Zake kubwa na Mamlaka Yake ni ukweli kuwa Ametiisha bahari ili meli zipite kwa Amri Yake, ili zipite baharini kama milima. Hii ilikuwa rai ya Mujahid, Al-Hasan, As-Suddi na Adh-Dhahhak. Kwa maneno mengine, meli hizo baharini ni kama milima ardhini.

إِنْ يَشَأْ يُسْكِنِ الرِّيحَ

“Akitaka, Huutuliza upepo...”

Yaani, upepo wenye kuzifanya meli zisafiri baharini. Angetaka, Angefanya upepo usimame, kisha meli zisingeenda na zingesimama, bila kwenda wala kuja, zikabakia pale pale zilipo katika usawa wa maji.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ

“Hakika katika hayo zipo Ishara kwa kila mwenye kusubiri...”

Yaani, mwenye subira katika kukabili matatizo.

شُكْرٍ

“...akashukuru.”

Yaani, katika ukweli kuwa Allah تعالیٰ Ameitiisha bahari na Anapeleka upepo mwingi kadiri inavyohitajika ili kusafiri. Kuna ishara za Neema Zake kwa viumbe Wake kwa kila mwenye subira, yaani, wakati wa shida, na mweye kushukuru, wakati wa faraja.

أَوْ يُوبِقَهُنَّ بِمَا كَسَبُوا

“Au Huviangamiza hivyo vyombo kwa sababu ya waliyoyatenda hao watu.”

Yaani, kama Atakavyo, Anaweza Kuangamiza meli na Kuzizamisha, kwa sababu ya madhambi watu walioyatenda.

وَيَعْفُ عَنْ كَثِيرٍ

“Naye Husamehe mengi.” Yaani, katika madhambi yao; kama Angetaka Kuwaadhibu kwa madhambi yao yote, Angewaangamiza wote wanaosafiri baharini. Baadhi ya wanazuoni walitafsiri Aya,

أَوْ يُوقَهُنَّ بِمَا كَسَبُوا

“Au Huviangamiza hivyo vyombo kwa sababu ya waliyoyatenda hao watu.”

Kuwa inamaanisha, Angetaka, Angetuma upepo uvume vikali ili kuzitoa meli katika njia zao, kuzipeleka kulia au kushoto, ili zipotee na kushindwa kufuata njia zao zilizokusudiwa. Tafsiri hii inajumuisha dhana ya kuangamizwa. Hii pia inaendana na maana ya kwanza, ambayo ni kwamba, Allah تعالى Angetaka, Angeufanya upepo utulie, na katika hali hiyo, meli zisingetembea, au Angeufanya upepo uwe mkali, ambapo meli zingepotea na kuangamia. Lakini kwa Rehema na Neema Zake, Anautuma upepo kulingana na haja zao kama Anavyopeleka mvua ya kutosha. Angepeleka mvua nyingi mno, ingeamaliza nyumba zao, na Angepeleka chache, basi mazao na matunda yao yasingemea. Kwa mfano kama katika ardhi ya nchi ya Misri, Anapeleka maji kutoka katika ardhi nyingine, kwa sababu hawahitaji mvua; kwani mvua ingewanyeshea, ingeharibu nyumba zao na kuangusha kuta.

وَيَعْلَمُ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِي آيَاتِنَا مَا هُمْ مِنْ حَيْصٍ ﴿٣٦﴾

“Na ili wajue wanaojadiliana katika Ishara Zetu kwamba hawana pahala pa kukimbilia.”

Yaani, hawana namna ya kukwepa Adhabu Yetu na Kisasi, kwani wametiishwa kwa Nguvu Zetu.

فَمَا أُوتِيتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۗ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَى لِلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٣٦﴾ وَالَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبِيرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَإِذَا مَا غَضِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَمْرُهُمْ شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾ وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٣٩﴾

36. Basi vyote mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora, na cha kudumu kwa ajili ya walioamini, na wakawa wanamtegemea Mola wao Mlezi.

37. Na wanaojiepusha na madhambi makubwa na mambo machafu, na wanapo kasirika wao husamehe,

38. Na wanaomuitikia Mola wao Mlezi, na wakasimamisha Sala, na mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao, na kutokana na Tulichowaruzuku wakawa wanatoa.

39. Na ambao wanapofanyiwa jeuri hujitetea.

Sifa za Wanaostahiki Yaliyoko kwa Allah تعالی.

Hapa Allah تعالی Anaonesha udhalili wa maisha ya kidunia na starehe zake na mapambo ya mpito.

فَمَا أُوْتِيتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَمَتَّعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا

“Basi vyote mlivyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu.”

Yaani, haijalishi unachokipata na kukusanya, usihadaike nayo, kwa kuwa ni furaha ya kidunia tu, ambayo ni ya ulimwengu wa chini, wa mpito ambao bila ya shaka yoyote utafikia mwisho.

وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ وَأَبْقٰى

“...lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora, na cha kudumu...”

Yaani, malipo ya Allah تعالی ni bora kuliko dunia, na ya milele, hivyo msiyatangulize ya mpito juu ya yale ya milele. Allah تعالی Anasema:

لِّلَّذِيْنَ ءَامَنُوْا

“...kwa ajili ya walioamini.”

Yaani, kwa waliokuwa na subira juu ya furaha zinazoendelea za kidunia,

وَعَلٰى رَبِّهٖمۡ يَتَوَكَّلُوْنَ

“...na wakawa wanamtegemea Mola wao Mlezi.”

Yaani, ili iwasaidie kuwa na subira katika kufanya yaliyo faradhi na kuepuka yaliyokatazwa.

Kisha Allah تعالى Anasema:

وَالَّذِينَ يَحْتَبُونَ كِبْرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ

“Na wanaoyaepuka madhambi makubwa...”

Tumeshaeleza madhambi na machafu (*Al-Fawahish*) katika *Surat Al-A'raf*.¹

وَإِذَا مَا غَضِبُوا هُمْ يَغْفِرُونَ

“...na wanapokasirika wao husamehe.”

Yaani, mwenendo wao unaashiria kuwa wanapaswa kuwasamehe watu na kustahamili. Kisasi si mwenendo wao. Imesimuliwa katika Sahihi kuwa Mtume ﷺ hakulipiza kisasi kwa ajili yake mwenyewe, isipokuwa pale zilipokiukwa Sheria Tukufu za Allah تعالى.²

وَالَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ

“Na wanaomitikia Mola wao Mlezi.”

Yaani, walimfuata Mtume Wake na kutii amri Zake na kuepuka Aliyoyakataza.

وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ

“...na wakashika Sala.”

Ambalo ni tendo kubwa la kumuabudu Allah تعالى.

وَأْمُرُهُمْ سُورَىٰ بَيْنَهُمْ

“...na mambo yao yakawa ni kwa kushauriana baina yao.”

Yaani, hawafanyi maamuzi bila ya kushauriana jambo husika ili wasaidiane kwa kupeana fikra zao katika masuala kama ya vita na mengine. Hii inafanana na Aya:

وَشَاوَرَهُمْ فِي الْأَمْرِ

“...na shauriana nao katika mambo.” (3:159).

¹ Angalia *Surat Al-A'raaf* 7:33.

² *Fat'h Al-Bari* 10:541.

Mtume ﷺ alikuwa akiwataka ushauri kuhusu vita na mambo mengine, ili waweze kujiamini. ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه, alipokuwa akifariki, baada ya kuchomwa kisu aliwakabidhi watu sita ili washauriane kuhusu kuchagua *Khalifah* aliyefuatia. Walikuwa ‘Uthman, ‘Ali, Talhah, Az-Zubayr, Sa‘ad na ‘Abdur-Rahman bin ‘Awf رضي الله عنهم. Kisha Masahaba wote, waliafikiana kumteua ‘Uthman رضي الله عنه kuwa kiongozi wao.

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ

“...na kutokana na Tulichowaruzuku wakawa wanatoa.”

Inamaanisha kuwatendea wema viumbe wa Allah, kwa kuanza na wa karibu zaidi, kisha wanaofuatia, na kuendelea.

وَالَّذِينَ إِذَا أَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُونَ ﴿٩٢﴾

“Na ambao wanapofanyiwa jeuri hujitetea.”

Yaani, wana nguvu za kulipiza kisasi juu ya waliowadhulumu na kuwafanyia uadui. Hawana ajizi ya kufanya hayo na si kwamba hawajiwezi; wanaweza kulipiza kisasi dhidi ya waliowakosea, lakini wanaamua kusamehe, kama Yusuf عليه السلام, alipowaambia ndugu zake:

قَالَ لَا تَثْرِبَ عَلَيَّ الْيَوْمَ يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ

“Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu Atakusameheni.”
(12:92).

Ingawa alikuwa katika nafasi ya kulipiza kisasi juu yao kwa waliyomfanyia. Mtume ﷺ aliwasamehe watu themanini waliotaka kumdhuru katika mwaka wa Hudaybiyah, alipopiga kambi karibu na Mlima wa At-Tan'im. Alipowazidi nguvu, aliwaachilia huru, ingawa alikuwa katika nafasi nzuri ya kulipiza kisasi juu yao. Pia alimsamehe Ghawrath bin Harith ambaye alitaka kumuua na alishachomoa panga lake alipokuwa usingizini. Mtume ﷺ aliamka na kumkuta akimuelekezea panga. Alimkaripia kwa hasira na panga likamdondoka. Mtume ﷺ aliliokota panga na kuwaita Masahaba wake, akawaeleza kilichotokea, na akamsamehe mtu huyo. Kuna Hadithi na riwaya nyingi kama hiyo. Allah تعالى ndiye Mjuzi zaidi

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾
 وَلَمَنِ اتَّصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِّن سَبِيلٍ ﴿٤٥﴾ إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ
 يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٦﴾ وَلَمَن
 صَبَرَ وَغَفَرَ إِنَّ ذَلِكَ لَمِنَ عِزِّ الْأُمُورِ ﴿٤٧﴾

40. Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo. Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye Hawapendi wenye kudhulumu.

41. Na wanaojitetea baada ya kudhulumiwa, hao hapana njia ya kuwalaumu.

42. Bali lawama ipo kwa wale wanaowadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.

43. Na anayesubiri, na akasamehe, hakika hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.

Fadhila ya Kusamehe na Ubora wa Kujinusuru Kutokana na Dhuluma

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ

“Na malipo ya uovu ni uovu mfano wa huo.”

Hii inafanana na Aya:

فَمَنْ آعَتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَآعَتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا آعَتَدَىٰ عَلَيْكُمْ ۗ

“Anayekushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadiri alivyokushambulieni.” (2:194), na

وَإِن عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ ۗ

“Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa.” (16:126).

Haki imefaradhihwa, katika sheria ya usawa katika adhabu (Al-Qisas), lakini njia bora zaidi ni kusamehe, kama Anavyosema Allah تعالى:

وَالْجُرُوحَ قِصَاصٌ ۖ فَمَن تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَّهُ ۗ

“...na kwa majeraha kisasi. Lakini atakayesamehe basi itakuwa ni kafara kwake.” (5:45).

Allah تعالی Anasema hapa:

فَمَن عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ

“Lakini mwenye kusamehe, na akasuluhisha, basi huyo malipo yake yapo kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hayatapotea kwa Allah تعالی. Kama inavyoeleza Hadithi Sahihi:

﴿وَمَا زَادَ اللَّهُ تَعَالَى عَبْدًا بِعَفْوٍ إِلَّا عِزًّا﴾

“Allah Hamzidishii mtu anayesamehe isipokuwa utukufu.”¹

إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ

“Hakika Yeye Hawapendi wenye kudhulumu.”

Yaani, Walipizaji visasi, yaani, wenye kuanzisha vitendo viovu.

وَلَمَن آتَنَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَئِكَ مَا عَلَيْهِم مِّن سَبِيلٍ ﴿٥١﴾

“Na wanaojitetea baada ya kudhumiwa, hao hapana njia ya kuwalaumu.”

Yaani, hana dhambi kwa kulipiza kisasi kwa mtu aliyemkosea.

إِنَّمَا السَّبِيلُ

“Bali lawama...” Yaani, mzigo wa dhambi.

عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۗ

“...ipo kwa wale wanaowadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki.”

¹ Muslim 4:2001.

Yaani, wenye kuanzisha matendo maovu dhidi ya wengine, kama inavyosema Hadithi Sahihi:

«الْمُسْتَبَانَ مَا قَالَا فَعَلَى الْبَادِي، مَا لَمْ يَغْتَدِ الْمَظْلُومُ»

“Watu wawili wakitukanana, yule aliyeanza ndiye mkosefu, kama aliyetukanwa akivuka mpaka.”¹

أَوْلَيْتِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Hao watapata adhabu iliyochungu.”

Yaani, kali na ya kuumiza. Imesimuliwa kuwa Muhammad bin Wasi’ alisema, “Nilikuja Makka na kulikuwa na ulinzi katika handaki ambapo walinzi wake walinipeleka kwa Marwan bin Al-Muhallab, ambaye alikuwa gavana wa Basrah. Alisema, ‘Una haja gani, Ewe Abu ‘Abdullah?’ Nikasema, ‘kama utakubali, ninakutaka uwe kama ndugu wa Banu ‘Adiy.’ Akasema, ‘Ni nani ndugu wa Banu ‘Adiy.’ Akasema, ‘Al-’ Ala’ bin Ziyad; aliwahi kumteua rafiki yake katika nafasi ya mamlaka, na alimuandikia: ukiweza, usiwe unalala isipokuwa baada ya kuhakikisha kuwa hakuna kitu mgongoni mwako, yaani hudaiwi na yeyote, tumbo lako halina kitu na mikono yako isiwe na damu na mali ya Waislamu. Kama utafanya hivyo, basi hutalaumiwa.’

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ أَوْلَيْتِكَ لَهُمْ

عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٧﴾

“Bali lawama ipo kwa wale wanaowadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika nchi bila ya haki. Hao watapata adhabu iliyo chungu.”

Marwan alisema, ‘Allah تعالی Amesema kweli, Wallahi, na Ametoa ushauri wa kweli.’ Halafu akasema, ‘Una haja gani, Ewe Abu ‘Abdullah.’ Nikasema, ‘Nina haja kuwa uniruhusu niungane na familia yangu.’ Akasema, ‘Ndiyo, nitafanya hivyo.’²

¹ Muslim 4:2000.

² Angalia Abi Shaybah 7:245.

Haya yaliandikwa na Ibn Abi Hatim رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Allah تَعَالَى Aliposhutumu dhuluma na wenye kudhu lumu, na kuamuru *Al-Qisas*, Alihimiza msamaha:

وَلَمَن صَبَرَ وَغَفَرَ

“...Na anayesubiri, na akasamehe.”

Inamaanisha, anayevumilia matusi kwa subira na kusitiri maovu,

إِنَّ ذَلِكَ لَمِنَ عَزْمِ الْأُمُورِ

“...hakika hayo ni katika mambo ya kuazimiwa.”

Sa'id bin Jubayr alisema, “Maana yake, moja katika mambo Aliyofaradhisha Allah تَعَالَى.” Yaani, matendo mema yatakayokuwa na malipo makubwa zaidi na sifa nyingi.

* * *

وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ وَدِيِّ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَتَرَى
 الظَّالِمِينَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ يَقُولُونَ هَلْ إِلَىٰ مَرَدٍّ مِنْ
 سَبِيلٍ ﴿٤٤﴾ وَتَرْتَهُمْ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا حَشِيعَاتٍ مِنْ
 الذُّلِّ يَنْظُرُونَ مِنْ طَرْفٍ خَفِيٍّ ۗ وَقَالَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ
 الْحَسِرَاتِ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ
 أَلَا إِنَّ الظَّالِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّقِيمٍ ﴿٤٥﴾ وَمَا كَانَ لَهُمْ
 مِنْ أَوْلِيَاءَ يَنْصُرُونَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا
 لَهُ مِنْ سَبِيلٍ ﴿٤٦﴾ أَسْتَجِيبُوا لِرَبِّكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ
 يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ ۗ مَا لَكُمْ مِنْ مَلْجَأٍ يَوْمَئِذٍ وَمَا
 لَكُمْ مِنْ نَكِيرٍ ﴿٤٧﴾ فَإِنْ أَعْرَضُوا فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ
 حَفِيفًا ۗ إِنَّ عَلَيْكَ إِلَّا الْبَلْغُ ۗ وَإِنَّا إِذَا أَذَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنَّا
 رَحْمَةً فَرَحَّ بِهَا ۗ وَإِنْ نَصَبْنَاهُمْ سِيقَةً إِذَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ
 فَإِنَّ الْإِنْسَانَ كَفُورٌ ﴿٤٨﴾

وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ وَدِيِّ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَتَرَى
 الظَّالِمِينَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ يَقُولُونَ هَلْ إِلَىٰ مَرَدٍّ مِنْ
 سَبِيلٍ ﴿٤٤﴾ وَتَرْتَهُمْ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا
 حَشِيعَاتٍ مِنْ الذُّلِّ يَنْظُرُونَ مِنْ
 طَرْفٍ خَفِيٍّ ۗ وَقَالَ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ
 الْحَسِرَاتِ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ
 وَأَهْلِيهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ أَلَا إِنَّ
 الظَّالِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّقِيمٍ ﴿٤٥﴾ وَمَا
 كَانَ لَهُمْ مِنْ أَوْلِيَاءَ يَنْصُرُونَهُمْ مِنْ
 دُونِ اللَّهِ ۗ وَمَنْ يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ
 مِنْ سَبِيلٍ ﴿٤٦﴾

44. Na Ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha kupotea, hana mlinzi baada Yake. Na utawaona wenye kudhulumu watakapoiona

adhabu wanasema: Je! Ipo njia ya kurudi?

45. Na utawaona wanapelekwa kwenye Moto, nao wamekuwa wanyonge kutokana na udhalili, wanatazama kwa mtazamo wa kificho. Na walioamini watasema: Hakika wapatao khasara ni hao walioziletea hasara nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama. Ama hakika wenye kudhulumu watakuwa katika adhabu ya daima.

46. Wala hawatakuwa na marafiki wa kuwanusuru mbele ya Mwenyezi Mungu. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemuacha kupotea, hana njia yoyote.

Hali ya Madhalimu Siku ya Kiyama

Allah تعالى Anatuambia kuwa Akitakacho huwa na Asichokitaka hakiwi, na hakuna wa kukifanya kiwe. Aliyemuongoa Yeye, hakuna wa kumpotosha, na Anayemuacha apotee, hakuna wa kumuongoa.

Kama Alivyosema:

وَمَنْ يُضِلِّ فَلَنْ نَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرْشِدًا

“Na Anayemuacha kupotea basi hutampatia mlinzi wala mwongozi.” (18:17).

Kisha Allah تعالى Anatuambia kuhusu madhalimu, yaani, washirikina wanao-mshirikisha Allah تعالى katika ibada:

لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ

“...watakapoiona adhabu...”

Yaani, katika Siku ya Kiyama, watatamani wangerejea duniani.

يَقُولُونَ هَلْ إِلَىٰ مَرَدٍّ مِّن سَائِلٍ

“...wanasema: Je! Ipo njia ya kurudi?”

Hii inafanana na Aya:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وَقَفُوا عَلَىٰ النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِعَايِنَتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٧﴾ بَلْ بَدَا لَهُمْ مَا كَانُوا يُخْفُونَ مِن قَبْلُ ﴿٦٨﴾ وَلَوْ رُدُّوا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ
 لَكَاذِبُونَ ﴿٦٩﴾

“Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Aya za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini. Bali yamewadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeparejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo.” (6:27-28)

وَتَرْتَهُمْ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا

“Na utawaona wanapelekwa kwenye Moto.”

Yaani, Motoni.

خَشِيعِينَ مِنَ الْذُلِّ

“...nao wamenyenyekea kwa unyonge.”

Yaani, katika hali ya udhalili, kwa sababu ya kumuasi Allah تعالى hapa duniani.

يَنْظُرُونَ مِنْ طَرْفٍ خَفِيٍّ

“...wanatazama kwa mtazamo wa kificho.”

Mujahid alisema, “Katika namna ya kudhalilisha.” Yaani, watatazana kwa siri, kwa sababu wanauogopa. Lakini watawachokiogopa kitawafikia kwa hakika, na kibaya zaidi ya hicho - Allah تعالى Atunusuru.

وَقَالَ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Na walioamini watasema...”

Yaani, katika Siku ya Kiyama watasema:

إِنَّ الْخَسِرِينَ

“hakika wapatao khasara...” Yaani, wenye hasara kubwa.

الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَأَهْلِيَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Ni hao waliokhasirika nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama.”

Yaani, watapelekwa Motoni na kunyimwa furaha yoyote ya Akhera. Watapotezana na kutenganishwa na wapenzi wao, marafiki, familia na ndugu na jamaa watawapoteza.

أَلَّا إِنَّ الظَّالِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّقِيمٍ

“Ama hakika wenye kudhulumu watakuwa katika adhabu ya daima.”

Yaani, milele, bila kutoka wala kutoroka.

وَمَا كَانَتْ هُمْ مِّنْ أَوْلِيَاءَ يَنْصُرُونَهُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ ۗ

“Wala hawatakuwa na walinzi wa kuwanusuru mbele ya Mwenyezi Mungu.”

Yaani, hakuna wa kuwaokoa dhidi ya adhabu na mateso wanayoteseka Kwayo.

وَمَنْ يُضَلِّلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ سَبِيلٍ

“Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha kupotea, hana njia yoyote.”

Yaani, bila ya wokovu.

أَسْتَجِيبُوا لِرَبِّكُمْ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ مَا لَكُمْ مِّنْ مَّلْجَأٍ يَوْمَئِذٍ وَمَا لَكُمْ مِّنْ نَّكِيرٍ ﴿٤٧﴾ فَإِنْ أَعْرَضُوا فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ۗ إِنَّ عَلَيْكَ إِلَّا الْبَلْغُ ۗ وَإِنَّا إِذَا أَذَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً فَرِحَ بِهَا ۗ وَإِنْ تُصِيبَهُمْ سَيِّئَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ فَإِنَّ الْإِنْسَانَ كَفُورٌ ﴿٤٨﴾

47. Mwitikieni Mola wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyoepekika itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Siku hiyo hamtakuwa na pa kukimbilia wala hamtakuwa na njia ya kukataa.

48. Na wakipuuza, basi Sisi hatukukupeleka ili uwe mwangalizi wao. Si juu yako ila kufikisha Ujumbe tu. Na hakika Sisi Tukimuonjesha mtu rehema kutoka Kwetu, huifurahia. Na akisibiwa na ovu kwa sababu ya iliyoyatanguliza mikono yao, basi hakika mtu huyu anakufuru.

Himizo la kumtii Allah تعالی kabla ya Siku ya Kiyama

Allah تعالی Anapotuambia kuhusu mambo ya kutisha na kuogofya ya Siku ya Kiyama, Anatuonya hayo na Anatuamuru tujandae kwa ajili hiyo:

أَسْتَجِيبُوا لِرَبِّكُمْ مِّنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّهِ ۗ

“Mwitikieni Mola wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyoepekika itokayo kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, Atakapoamuru tu, itapita kama kupepesa jicho tu, na hakuna atakayeweza kuiondoa au kuizuia.

مَا لَكُمْ مِّن مَّلْجٍ يَوْمَئِذٍ وَمَا لَكُمْ مِّن نَّكِيرٍ

“Siku hiyo hamtakuwa na pa kukimbilia wala hamtakuwa na cha kukingia.”

Yaani, hamtakuwa na ngome ya kukimbilia, hakuna mahali pa kujificha, kwani Allah تعالى Atakuzungukeni kwa Ujuzi Wake na Nguvu Zake, na hamtakuwa na mahali pa kujihifadhi dhidi Yake isipokuwa Kwake Yeye.

يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُجُ ﴿١٠﴾ كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿١١﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿١٢﴾

“Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio? La! Hapana pa kukimbilia! Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola wako Mlezi tu.”
(75:10-12)

فَإِن أَعْرَضُوا

“Na wakipuuza.” inawahusu washirikina,

فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا

“...basi Sisi Hatukukupeleka ili uwe mwangalizi wao.”

Yaani, ‘huna nguvu juu yao.’ Na Allah تعالى Anasema katika sehemu nyingine,

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ

“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye.” (2:272).

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

“...juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu.” (13:40).

Na Allah تعالى Anasema hapa:

إِنَّ عَلَيْكَ إِلَّا الْبَلْغُ

“Si juu yako ila kufikisha Ujumbe tu.”

Maana yake, ‘Tunachokutaka wewe ni kuwafikishia Ujumbe wa Allah.’

وَأِنَّا إِذَا أَذَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً فَرِحَ بِهَا ط

“Na hakika Sisi Tukimuonjesha mtu rehema kutoka Kwetu, huifurahia.”

Yaani, wakati wa faraja unapomfikia, yeye hufurahia.

وَإِن تُصِيبِهِمْ

“Na akisibiwa...” Yaani akipatwa na jambo baya.

سَيِّئَةً

“...na ovu...” Yaani, ukame, adhabu, mtihani au taabu,

فَإِنَّ الْإِنْسَانَ كَفُورٌ

“...basi hakika mtu huyu anakufuru.”

Yaani, anasahau nyakati zilizopita za faraja na neema na hatambui chochote isipokuwa kipindi kilichopo. Kama wakati wa faraja unamfikia, anakuwa jeuri na kuruka mipaka, lakini kama mtihani utamfika, yeye hukata tamaa na hupoteza matumaini. Hii inafanana na kile Mtume ﷺ alichowaambia wanawake:

«يَا مَعْشَرَ النِّسَاءِ، تَصَدَّقْنَ، فَإِنِّي رَأَيْتُكُنَّ أَكْثَرَ أَهْلِ النَّارِ»

“Enyi wanawake, toeni sadaka, kwa kuwa nimeona idadi kubwa ya watu wa Jahanamu ni wanawake.”

Mwanamke mmoja akamuuliza, “Kwa nini hivyo, ewe Mtume ﷺ.” Akasema:

«لِأَنَّكُنَّ تُكْذِبْنَ الشُّكَايَةَ وَتَكْفُرْنَ الْعَمِيرَ، لَوْ أَحْسَنْتَ إِلَى إِخْدَاهُنَّ اللَّذَّهْرَ ثُمَّ تَرَكْتِ يَوْمًا، قَالَتْ: مَا رَأَيْتُ مِنْكَ خَيْرًا قَطُّ»

“Kwa sababu nyinyi mnalalamika mno, na hamna shukrani kwa waume (wenu). Kama mmoja wenu atafanyiwa wema katika muda wote wa uhai wake, halafu siku moja ukakosekana wema huo, atasema, ‘Sijapata kuona lolote jema kutoka kwako (katika maisha yangu!)’¹

¹ Muslim 1:86.

Hii ni hali ya wanawake wengi, isipokuwa wale Aliowaongoza Allah تعالى na wale waliyo miongoni mwa watu wanaoamini na kutenda mema.

Sawa na alivyosema Mtume ﷺ, muumini ni yule ambaye:

«إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَّاءٌ شُكِرَ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَّاءٌ صَبِرَ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ،
وَلَيْسَ ذَلِكَ لِأَحَدٍ إِلَّا لِلْمُؤْمِنِ»

*"... kama jambo jema litamtokea, yeye hushukuru, na hiyo ni heri kwake. Akipatwa na jambo baya, atakuwa na subira, na hiyo ni heri kwake. Hayo hayamtokei yeyote isipokuwa muumini."*¹

* * *

¹ Muslim 4:2295.

اللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ تَخْلُقُ مَا يَشَاءُ يَهَبُ لِمَنْ
 يَشَاءُ إِنْتًا وَيَهَبُ لِمَنْ يَشَاءُ الذُّكُورَ ﴿٤٩﴾ أَوْ يُزَوِّجُهُمْ
 ذُكْرَانًا وَإِنْتًا ط وَيَجْعَلُ مَنْ يَشَاءُ عَقِيمًا إِنَّهُ عَلِيمٌ قَدِيرٌ
 ﴿٥٠﴾ * وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَكْلِمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِنْ
 وَرَائِ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولًا فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِ مَا يَشَاءُ
 إِنَّهُ عَلَىٰ حَكِيمٍ ﴿٥١﴾ وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا
 مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ
 وَلَكِنْ جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا
 وَإِنَّكَ لَتَهْدَىٰ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٢﴾ صِرَاطِ اللَّهِ
 الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ أَلَا إِلَى اللَّهِ
 نَصِيرُ الْأُمُورِ ﴿٥٣﴾

اللَّهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ تَخْلُقُ
 مَا يَشَاءُ يَهَبُ لِمَنْ يَشَاءُ إِنْتًا وَيَهَبُ
 لِمَنْ يَشَاءُ الذُّكُورَ ﴿٤٩﴾ أَوْ يُزَوِّجُهُمْ
 ذُكْرَانًا وَإِنْتًا ط وَيَجْعَلُ مَنْ يَشَاءُ
 عَقِيمًا إِنَّهُ عَلِيمٌ قَدِيرٌ ﴿٥٠﴾

**49. Ufalme wa mbingu na
 ardhi ni wa Mwenyezi
 Mungu; Anaumba Ape-
 ndavyo, Anamtunukia
 Amtakaye watoto wa kike,
 na Anamtunukia Amtakaye
 watoto wa kiume.**

**50. Au Huwachanganya
 wanaume na wanawake,
 na Akamfanya Amtakaye
 tasa. Hakika Yeye ni Mjuzi
 Mwenye Uweza.**

Allah تعالی Anatuambia kuwa Yeye ni Muumbaji, Mwenye Mamlaka na Mdhibili wa Mbingu na Ardhi.

Akitakacho Huwa, na Asichokitaka Hakiwi. Humpa Amtakaye na Humnyima Amtakaye; hakuna wa kuzuia Atoacho, na hakuna wa kutoa Akizuiacho, na Huumba Akitakacho.

يَهَبُ لِمَنْ يَشَاءُ إِنْتًا

“...Anamtunukia amtakaye watoto wa kike.”

Yaani, huwapa watoto wa kike tu. Al-Baghawi رحمه الله تعالی alisema, “Na miongoni mwao (waliopewa watoto wa kike peke yao) alikuwa Lut عليه السلام.”¹

¹ Al-Baghawi 4:132.

وَيَهَبُ لِمَن يَشَاءُ أَلذُّكُورَ

“...na Anamtunukia amtakaye watoto wa kiume.”

Yaani, Huwapa watoto wa kiume tu. Al-Baghawi رحمه الله تعالى alisema, “Kama Ibrahim Al-Khalil عليه السلام, ambaye hakuwa na mabinti.”¹

أَوْ يَزُوجَهُمْ ذُرِّيَّاتَنَا وَإِنشَاءً

“Au huwachanganya wanaume na wanawake.”

Yaani, Humpa yeyote Amtakaye, watoto wa kike na wa kiume. Al-Baghawi رحمه الله تعالى alisema, “Mithili ya Mtume Muhammad ﷺ.”²

وَيَجْعَلُ مَن يَشَاءُ عَقِيمًا

“...na Akamfanya Amtakaye tasa.”

Yaani, asiye na watoto kabisa. Al-Baghawi رحمه الله تعالى alisema, “Kama Yahya na ‘Isa, (ziwafikie amani).”³ Hivyo, watu wamegawanyika katika makundi manne: Wengine hupewa watoto wa kike, baadhi yao hupewa watoto wa kiume, wengine hupewa watoto wa kiume na wa kike na baadhi yao hawapewi watoto wa kiume wala wa kike, bali huwa hawana kabisa watoto.

إِنَّهُ عَلِيمٌ

“Hakika Yeye ni Mjuzi...”

Yaani, Anamjua kila mmoja anastahiki kuwa katika kundi lipi.

قَدِيرٌ

“Mwenye Uweza.”

Yaani, ili kufanya chochote Anachokitaka na kutofautisha baina ya watu katika namna hii. Hii inafanana na yaliyo katika Aya ambapo Allah تعالى Anasema kuhusu ‘Isa عليه السلام:

¹ Al-Baghawi 4:132.

² Al-Baghawi 4:132.

³ Al-Baghawi 4:132.

وَلِتَجْعَلَهُدَىٰ آيَةً لِلنَّاسِ

"Na ili Tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu." (19:21)

Yaani, dalili juu ya Uweza Wake, kwani Aliwaumba watu katika namna nne tofauti. Adam عليه السلام, aliumbwa kutokana na udongo, si kutokana na mwanamume na mwanamke. Hawa, aliumbwa kutokana na mwanamume bila ya mwanamke. Watu wengine wote, isipokuwa 'Isa عليه السلام, waliumbwa kutokana na mwanamume na mwanamke, na dalili hii ya Allah تعالى ilikamilika kwa kuumbwa 'Isa bin Maryam عليه السلام, ambaye aliumbwa kutokana na mwanamke bila ya mwanamume. Allah Anasema:

وَلِتَجْعَلَهُدَىٰ آيَةً لِلنَّاسِ

"Na ili Tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu." (19:21)

Aya hii inawahusu wazazi, ilhali ile iliyotangulia inawahusu watoto, na katika hali zote kuna makundi manne. Utukufu ni wa Mwenye Kujua yote Mwenye Uweza wa yote.

• وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْيًا أَوْ مِنْ وَرَآئِ حِجَابٍ أَوْ يُرْسِلَ رَسُولًا فَيُوحِيَ
بِإِذْنِهِ مَا يَشَاءُ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥١﴾ وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا ۗ مَا
كُنْتَ تَدْرِي مَا آتَيْنَاكَ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِنْ عِبَادِنَا
ۗ وَإِنَّكَ لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٢﴾ صِرَاطِ اللَّهِ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي
الْأَرْضِ ۗ أَلَا إِلَى اللَّهِ تَصِيرُ الْأُمُورُ ﴿٥٣﴾

51. Na haikuwa kwa mwanaadamu kwamba Mwenyezi Mungu Amsemeze ila kwa Wahyi (Ufunuo), au kwa nyuma ya pazia, au kumtuma Mjumbe. Naye Humfunulia Ayatakayo kwa Idhini Yake. Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye Hikima.

52. Na namna hivi Tumekufunulia Qur'ani kwa Amri Yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani. Lakini Tumekifanya kitabu hiki kuwa ni Nuru ambayo kwayo Tunamuongoza Tumtakaye katika waja Wetu. Na hakika wewe Unaongoza kwenye njia iliyo nyooka.

53. Njia ya Mwenyezi Mungu Ambaye ni Vyake Yeye tu vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.

Jinsi Wahyi Unavyoteremshwa

Hii inahusu jinsi Allah تعالى Anavyotuma Wahyi. Wakati mwingine Yeye Hutia jambo katika moyo wa Mtume Muhammad ﷺ, na hana shaka yoyote kuwa ni kutoka kwa Allah تعالى, kama ilivyosimuliwa katika Sahih Ibn Hibban kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ رُوحَ الْقُدْسِ نَفَثَ فِي رُوعِي أَنَّ نَفْسًا لَنْ تَمُوتَ حَتَّى تَسْتَكْمِلَ رِزْقَهَا وَأَجَلَهَا،
فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَجْمِلُوا فِي الطَّلَبِ»

“Kwa hakika Ar-Ruh Al-Qudus (yaani, Jibril) alinipulizia moyoni mwangu kuwa hakuna nafsi itakayokufa isipokuwa mpaka riziki yake na muda wake uliotengwa uishe, basi mcheni Allah na mdumu katika kutafuta heri.”¹

أَوْ مِنْ وَرَائِي حِجَابٍ

“...au kwa nyuma ya pazia,”

Kama alivyozungumza na Musa عليه السلام. Na yeye aliomba kumuona Yeye baada ya kuzungumza Naye, lakini hakuruhusiwa hilo. Katika Sahih, kumeandikwa kuwa Mtume ﷺ alimuambia Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنهما:

«مَا كَلَّمَ اللَّهُ أَحَدًا إِلَّا مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ، وَإِنَّهُ كَلَّمَ أَبَاكَ كَيْفَاحًا»

“Allah Hakuzungumza na yeyote isipokuwa kutoka nyuma ya pazia, lakini Alizungumza na baba yako moja kwa moja.”²

Hivi ndivyo ilivyoelezwa katika Hadithi. Baba yake Jabir رضي الله عنه aliuliwa katika Siku ya Uhud. Hili linahusu ulimwengu wa maisha ya Al-Barzakh. Aya inazungumzia ulimwengu huu wa kidunia.

¹ Musnad Ash-Shihab 2:185.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:360.

أَوْ يُرْسِلَ رَسُولًا فَيُوحِيَ بِإِذْنِهِ مَا يَشَاءُ^ع

“...au kumtuma Mjumbe. Naye Humfunulia Ayatakayo kwa idhini Yake.”

Kama Jibril عليه السلام, na Malaika wengine walivyoteremka kwa Mitume.

إِنَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥١﴾

“Hakika Yeye ni Mtukufu, Mwenye Hikima.”

Yeye ni تعالیٰ, Ajuaye Yote, Mwingi wa Hekima.

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا^ع

“Na namna hivi Tumekufunulia Qur’ani kwa amri Yetu.”

مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ

“Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani.”

Yaani, ‘maelezo mliyopewa katika Qur’an.’

وَلَكِن جَعَلْنَاهُ

“Lakini Tumekifanya...” Yaani, Qur’an,

نُورًا يَهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِّنْ عِبَادِنَا^ع

“...kuwa ni Nuru ambayo kwayo Tunamuongoa Tumtakaye katika waja wetu.”

Hii inafanana na Aya:

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً^ط وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَادَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى^ع

“Sema: Hii Qur’ani ni uwongofu na pozo kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni.” (41:44).

وَإِنَّكَ

“Na hakika wewe...”

Yaani, Mtume Muhammad ﷺ;

لَتَهْدِي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

“...unaongoa kwenye njia iliyonyooka.”

Yaani, mwenendo sahihi. Kisha Allah تعالى Anaeleza hili zaidi kwa kusema:

صِرَاطِ اللَّهِ

“Njia ya Mwenyezi Mungu...”

Maana yake, Sheria Zake Anazoamuru.

الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“...ambaye ni Vyake Yeye tu vilivyomo mbinguni na katika ardhi.”

Yaani, Mola wao Mlezi na Mwenye Mamlaka, Mmoja Anayedhibiti na Kuzitawala, Ambaye Hukumu Yake haiwezi kubadilishwa.

أَلَا إِلَى اللَّهِ تَصِيرُ الْأُمُورُ

“Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Mwenyezi Mungu.”

Yaani, mambo yote hurejea Kwake na Anayahukumu. Ametakasika dhidi ya wanayosema waovu na makafiri.

Huu ni mwisho wa *Tafsiri ya Suratu Ash-Shura*.

* * *

Tafsiri ya Suratu Az-Zukhruf

Sura ya 43

Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الزُّكْرُوفِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمِّ ۝ وَالْكِتَابِ الْمُمِينِ ۝ إِنَّا جَعَلْنَاهُ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا
لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ۝ وَإِنهٗ فِي أَمْرِ الْكِتَابِ لَدَيْنَا لَعَلٌّ
حَكِيمٌ ۝ أَفَنَضْرِبُ عَنْكُمُ الذِّكْرَ صَفْحًا أَنْ كُنْتُمْ
قَوْمًا مُّسْرِفِينَ ۝ وَكَمْ أَرْسَلْنَا مِنْ نَبِيِّ فِي الْأَوَّلِينَ ۝
وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ۝ فَأَهْلَكْنَا
أَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا وَمَضَىٰ مَثَلُ الْأَوَّلِينَ ۝

حَمِّ ۝ وَالْكِتَابِ الْمُمِينِ ۝ إِنَّا
جَعَلْنَاهُ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ
تَعْقِلُونَ ۝ وَإِنهٗ فِي أَمْرِ الْكِتَابِ
لَدَيْنَا لَعَلٌّ حَكِيمٌ ۝ أَفَنَضْرِبُ
عَنْكُمُ الذِّكْرَ صَفْحًا أَنْ كُنْتُمْ
قَوْمًا مُّسْرِفِينَ ۝ وَكَمْ أَرْسَلْنَا
مِنْ نَبِيِّ فِي الْأَوَّلِينَ ۝ وَمَا يَأْتِيهِمْ
مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ۝
فَأَهْلَكْنَا أَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا وَمَضَىٰ
مَثَلُ الْأَوَّلِينَ ۝

1. "H'a Mim."

2. "Naapa kwa Kitabu kinachobainisha."

3. "Hakika Sisi Tumeifanya Qur'ani kwa Kiarabu ili mfahamu."

4. "Na hakika hiyo imo katika Asili ya Maandiko yalioko Kwetu, ni tukufu na yenye hekima."

5. "Je! Tuache kukukumbusheni kabisa kwa kuwa nyinyi ni watu mliopita kiasi mipaka ya ubaya?"

6. **“Na Manabii wangapi Tuliwapeleka kwa watu wa zamani!”**

7. **“Na hawajii Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli.”**

8. **“Na Tuliwaangamiza waliokuwa na nguvu kushinda wao. Na mfano wa watu wa zamani umekwishapita.**

حَمِّمٌ وَالْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿٤٣﴾

“H’a Mim. Naapa kwa Kitabu kinachobainisha.”

Yaani: kilicho bayana, chenye ufafanuzi, maana za wazi na matamshi dhahiri. Kwa kuwa Allah تعالى Amekiteremsha kwa lugha ya Kiarabu ambayo ndiyo fasaha zaidi kwa mazungumzo baina ya watu. Allah تعالى Amesema:

إِنَّا جَعَلْنَاهُ

“Hakika Sisi Tumeifanya...”

Yaani, Tumeiteremsha,

قُرْآنًا عَرَبِيًّا

“... Qur’ani kwa Kiarabu...”

Yaani: Tumeifikisha kwa lugha ya kiarabu iliyo fasaha na wazi,

لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ

“...ili mfahamu.”

Muielewe na muizingatie.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُّبِينٍ ﴿٤٤﴾

“Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi.” (26:195)

Kauli ya Allah تعالى:

وَإِنَّهُ فِي أُمْرِ الْكِتَابِ لَدَيْنَا لَعَلٌّ حَكِيمٌ ﴿٤٥﴾

“Na hakika hiyo imo katika Asili ya Maandiko yalioko Kwetu, ni tukufu na yenye hikima.”

Aya hii inaeleza Utukufu wa juu kabisa wa Qur'an kwa wakazi wa huko juu (Malaika), ili watu wa duniani waitukuze na kuitii.

Allah تعالى Anasema:

وَإِنَّهُ

“Na hakika hiyo...” Yaani Qur'an,

فِي أُمْرِ الْكِتَابِ

“...imo katika Asili ya Maandiko...”

Yaani: *Al-Lawh Al-Mahfudh* (Ubao uliohifadhiwa). Haya yalisemwa na Ibn 'Abbas na Mujahid.¹

لَدَيْنَا

“...yalioko Kwetu...”

Maana yake, Kwetu. Ni kauli ya Qatadah na wengine.²

لَعَلِّي

“...ni tukufu...”

Maana yake, ikishika mahali pa heshima na fadhila. Hiyo ilikuwa rai ya Qatadah.¹

حَكِيمٌ

“...na yenye hikima.”

Iliyo mbali na utata na upotevu. Yote haya ni katika kutanabahisha Utukufu Wake na Fadhila Zake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّهُ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾ فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٨﴾ لَا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ ﴿٧٩﴾ تَنْزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾

“Hakika hii bila ya shaka ni Qur'ani Tukufu. Katika Kitabu kilichohifadhiwa. Hapana akigusaye ila waliotakaswa. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote.”
(56:77-80)

¹ Ar-Razi 27:167.

² Al-Baghawi 4:33.

كَلَّا إِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ﴿١١﴾ فَمَنْ شَاءَ ذَكَرْهُ ﴿١٢﴾ فِي صُحُفٍ مُّكَرَّمَةٍ ﴿١٣﴾ مَّرْفُوعَةٍ مُّطَهَّرَةٍ ﴿١٤﴾
بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ﴿١٥﴾ كِرَامٍ بَرَرَةٍ ﴿١٦﴾

“Sivyo hivyo! Huu ni ukumbusho. Basi anayependa akumbuke. Yamo katika kurasa zilizohishimiwa. Zilizoinuliwa, zilizotakaswa. Zimo mikononi mwa Malaika waandishi. watukufu, wema.”(80:11-16)

Kauli ya Allah تعالى:

أَفَنْصُرُبْ عَنْكُمْ آلذِّكْرَ صَفْحًا أَنْ كُنْتُمْ قَوْمًا مُّسْرِفِينَ ﴿١٦﴾

“Je! Tuache kukukumbusheni kabisa kwa kuwa nyinyi ni watu mliopita mipaka kwa ukafiri?”

Maana yake, ‘Mnadhani tutakusameheni na hatutakuadhibuni pindi msipoyatekeleza mliyoamrisha?’ Haya yalisemwa na Ibn ‘Abbas, Abu Salih, Mujahid na As-Suddi. Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliyakhitari maelezo haya.² Qatadah aliizungumzia kauli ya Allah تعالى,

أَفَنْصُرُبْ عَنْكُمْ آلذِّكْرَ صَفْحًا

“Je! Tuache kukukumbusheni kabisa...”

“Wallahi! Qur’an hii ingeliondolewa baada ya kizazi cha kwanza cha umati huu kuikataa, wangeliangamia, lakini, Allah تعالى, kwa Rehema Zake, Aliendelea Kuwapelekea kwa muda wa miaka ishirini, na Kuwalingania ili waifuate au kwa muda mrefu kadiri Alivyotaka.”¹

Kauli ya Qatadah ni nzuri sana, kwa sababu ya ulatifu na Rehema za Allah تعالى kwa waja Wake, Allah تعالى Hakuacha Kuwalingania katika kheri na Kuwapelekea ukumbusho wenye hikima, yaani, Qur’an, ingawa waliziba masikio. Hakuwapa mgongo, bali Aliwaamuru wafuate mwongozo Wake kwa mwenye kuufuata, ili ushahidi usimame dhidi ya wale ambao hukumu yao imeshapitishwa.

¹ At-Tabari 21:567.

² At-Tabari 21:567, 568.

³ At-Tabari 21:568.

Kuliwazwa Mtume ﷺ kwa Kupingwa na Makureishi

Katika kumliwaza Mtume Wake kuhusu baadhi ya watu katika kaumu yake ambao wanamkadhibisha, pamoja na kumuamuru awe na subira. Allah تعالى Amesema,

وَكَمْ أَرْسَلْنَا مِنْ نَبِيِّ فِي الْأَوَّلِينَ ﴿٤١﴾

“Na Manabii wangapi Tuliwatuma kwa watu wa zamani!”

Yaani: miongoni mwa jamii za hapo zamani,

وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ نَبِيِّ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٤٢﴾

“Na hawajii Nabii yeyote ila walikuwa wakimkejeli.”

Yaani, wakimkataa na kumdhihaki. Kauli ya Allah تعالى:

فَأَهْلَكْنَا أَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا

“Na Tuliwaangamiza waliokuwa na nguvu kushinda wao.”

Maana yake: ‘Tukawahilikisha waliowakadhibisha Mitume, nao walikuwa na nguvu kuliko hao wanaokukanusha, ewe Muhammad’. Sawa na Kauli ya Allah

تعالى:

أَفَلَمْ يَسْمُرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ كَانُوا أَكْثَرَ مِنْهُمْ وَأَشَدَّ قُوَّةً

“Kwani hawatembe katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hawa, na wame washinda kwa nguvu...” (40:82)

Aya zinazolizungumzia hilo ni nyingi sana.

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَضَىٰ مَثَلُ الْأَوَّلِينَ

“Na mfano wa watu wa zamani umekwishapita.”

¹ At-Tabari 21:568.

Mujahid alisema, “Mwenendo wao.”¹ Qatadah alisema, “Ni adhabu yao.”² Wengine wali sema, “Fundisho kwao.” Yaani, ‘Tuliwafanya wawe fundisho kwa wakadhibishaji wa baada yao kuwa yatawapata yaliyo wasibu hao.”

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى mwishoni mwa Sura hii,

فَجَعَلْنَهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِلْآخِرِينَ

“Kisha Tukawafanya kuwa watangulizi na mfano kwa wa baadaye.”
(43:56)

Na Kauli nyingine,

سُنَّتَ اللَّهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ

“Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja Wake.” (40:85)

وَلَنْ نَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّهِ تَبْدِيلًا

“Wala hutapata mabadiliko katika ada ya Mwenyezi Mungu.”
(33:62)

* * *

¹ At-Tabari 21:571.

² At-Tabari 21:571.

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مِّنْ خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَيَقُولُنَّ
 خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ ﴿٩﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ
 مَهْدًا وَجَعَلَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا لَّعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٠﴾
 وَالَّذِي نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ فَأَنْشَرْنَا بِهِ بَلْدَةً
 مَّيْتًا ۚ كَذَلِكَ نُخْرِجُوهَا ﴿١١﴾ وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا
 وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿١٢﴾ لِيَسْتَوُوا
 عَلَىٰ ظُهُورِهِ ثُمَّ تَذْكُرُوا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ إِذَا اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ
 وَتَقُولُوا سُبْحَانَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ
 مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾ وَإِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿١٤﴾ وَجَعَلُوا لَهُ
 مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا ۚ إِنَّ الْإِنسَانَ لَكَفُورٌ مُّبِينٌ ﴿١٥﴾ أَمِ
 اتَّخَذَ مِمَّا يَخْلُقُ بَنَاتٍ وَأَصْفَنَكُمْ بِالْبَيْنِ ﴿١٦﴾ وَإِذَا بُرِّئَ
 أَحَدُهُمْ بِمَا صَرَبَ لِلرَّحْمَنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهَهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ
 كَظِيمٌ ﴿١٧﴾ أَوْ مَن يَنْشَأُ فِي الْحُلِيِّهِ وَهُوَ فِي الْخِصَامِ
 غَيْرُ مُبِينٍ ﴿١٨﴾ وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبْدُ الرَّحْمَنِ
 إِنثًا ۚ أَشْهَدُوا خَلْقَهُمْ ۖ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ وَيُسْأَلُونَ ﴿١٩﴾
 وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَنُ مَا عَبَدْنَاهُمْ ۗ مَا لَهُمْ بِذَلِكَ مِنْ
 عِلْمٍ ۗ إِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٢٠﴾

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مِّنْ خَلْقِ السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ لَيَقُولُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ
 الْعَلِيمُ ﴿٩﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ
 الْأَرْضَ مَهْدًا وَجَعَلَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا
 لَّعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٠﴾ وَالَّذِي نَزَّلَ
 مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ فَأَنْشَرْنَا
 بِهِ بَلْدَةً مَّيْتًا ۚ كَذَلِكَ نُخْرِجُوهَا
 ﴿١١﴾ وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا
 وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا
 تَرْكَبُونَ ﴿١٢﴾ لِيَسْتَوُوا
 عَلَىٰ ظُهُورِهِ ثُمَّ تَذْكُرُوا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ إِذَا
 اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحَانَ الَّذِي
 سَخَّرَ لَنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ ﴿١٣﴾
 وَإِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿١٤﴾

9. "Na ukiwauliza: Nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye Nguvu, Mjuzi."

10. "Ambaye Amekufanyieni ardhi kama tandiko, na Akakufanyieni ndani yake njia ili mpate kuongoka."

11. "Na Ambaye Ndiye Aliyeteremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi, na kwa hayo Tukaifufua nchi iliyokufa. Na namna hivi ndivyo mtakavyotolewa."

12. “Na Ambaye Ndiye Aliyeumba katika kila kitu jike na dume, na Akakufanyieni marikebu na wanyama mnaowapanda.”

13. “Ili mkae vizuri migongoni mwao, kisha mkumbuke neema za Mola Wenu Mlezi mnapokaa sawa sawa juu yao na msembe: Ametakasika Aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe.”

14. “Na hakika sisi tutarudi kwa Mola Wetu Mlezi.”

Kukiri kwa Washirikina Kwamba Allah تعالى Peke Yake Ndiye Muumba, na Ishara Nyingi juu ya Uthibitisho wa hilo.

Kauli ya Allah تعالى: ‘Na kama utawasaili ewe Muhammad, hao wamshirikishao Allah, wenye kumuabudu ghairi Yake’.

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيزُ الْعَلِيمُ

“Nani Aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila ya shaka watasema: Kaziumba Mwenye Nguvu, Mjuzi.”

Yaani: watakiri kwamba Muumbaji wa vyote hivyo ni Allah تعالى Peke Yake, Hana mshirika, lakini wao, licha ya hali hii, humuabudu kwa kumshirikisha na masanamu, na miungu ya uongo.

الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ مَهْدًا

“Ambaye Amekufanyieni ardhi kama tandiko...”

Yaani: Tulivu, imara ili muweze kusafiri juu yake, mnasimama, mnalala na kwenda huku na huko, licha ya kwamba imetandikwa juu ya maji, lakini, Allah تعالى Aliipa nguvu kwa milima ili isiyumbe.

وَجَعَلَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا

“...na Akakufanyieni ndani yake njia...”

Yaani: njia kati ya milima na mabonde,

لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

“...mpate kuongoka.”

Yaani, katika safari zenu kutoka mji mmoja hadi mwingine, eneo moja hadi jingine na ardhi moja hadi ardhi nyingine,

وَالَّذِي نَزَّلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ

“Na Ambaye Ndiye Aliyeteremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi...”

Maana yake, cha kuitosheleza mimea yenu, matunda, na kinywaji, chenu na mifugo yenu,

فَأَنْشَرْنَا بِهِ بَلْدَةً مَّيْتًا

“...na kwa hayo Tukaifufua nchi iliyokufa.”

Yaani, kwa ukame.

Maana: Ardhi kavu, maji yanapoifikia hutaharaki na kulowana na kuotesha kila jozi nzuri. Kisha, Allah تعالى Alilishabihisha jambo la Kuhuisha ardhi na Kuhuisha miili katika Siku ya marejeo baada ya kufa kwake. Allah تعالى Alisema,

كَذَلِكَ نُخْرِجُكَوْبَ

“Na namna hivi ndivyo mtakavyotolewa.”

Kisha, Allah تعالى Akasema:

وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا

“Na Ambaye Ndiye Aliyeumba katika kila kitu jike na dume...”

Yaani: katika vinavyoota ardhini, kama vile aina kwa aina za mimea, mazao, matunda, maua na vingine. Pia katika namna mbalimbali za wanyama.

وَجَعَلَ لِكُلِّ مِّنَ الْفُلْكِ

“...na Akakufanyieni marikebu...” Maana yake, meli na vyombo vingine vya baharini.

وَالْأَنْعَامِ مَا تَرَكَبُونَ

“...na wanyama mnaowapanda.”

Yaani: Amedhalilisha kwa ajili yenu, Akawatiisha na Kuwafanya wapole ili muweze kula nyama zao, mnywe maziwa yao, na mpande juu ya migongo yao.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

لِتَسْتَوُوا عَلَى ظُهُورِهِ

“Ili mkae vizuri migongoni mwao...”

Yaani, ili mkae vyema na kwa salama,

عَلَى ظُهُورِهِ

“...migongoni mwao...”

Yaani: migongoni mwa wanyama wa namna hii,

ثُمَّ تَذْكُرُوا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ

“...kisha mkumbuke neema za Mola wenu Mlezi...”

Yaani: katika Alivyokutiishieni,

إِذَا أَسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحَانَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ

“...mnapokaa sawa sawa juu yao na msemi: Ametakasika Aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe.”

Maana yake, Kumudu, kama Allah تعالى Asingevitiisha vitu hivi kwetu, basi tusingeweza kuyafanya haya kwa nguvu zetu.’

Ibn ‘Abbas, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd wamesema: “Maana ya *Wamaa Kunnaa Muqriniin*, Tusingeweza kuyafanya haya sisi wenyewe.”¹

¹ At-Tabari 21:576, 577.

وَإِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿٤٣﴾

“Na hakika sisi tutarudi kwa Mola Wetu Mlezi.”

Tutarejea Kwake baada ya kufa na mwishowe yote tutaenda Kwake. Kutajwa kwa safari za kidunia ni njia ya kutanabahisha juu ya safari ya Akhera. Ni sawa na Alivyoeleza masurufu ya kidunia juu ya yale ya Akhera katika Kauli Yake nyingine,

وَتَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ ۗ

“Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu.”
(2:197)

Kadhaliika mavazi ya kidunia juu ya yale ya Akhera katika Kauli Yake,

وَرِدْشًا ۗ وَلِبَاسُ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۗ

“...nguo za pambo. Na nguo za uchamungu ndio bora.” (7:26)

وَجَعَلُوا لَهُ مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ مُّبِينٌ ﴿٤٤﴾ أَمْ آتَّخَذَ مِنْ مِمَّا يَخْلُقُ بَنَاتٍ وَأَصْفَنَكُمْ بِالْبَنِينَ ﴿٤٥﴾ وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِمَا صَرَبَ لِلرَّحْمَنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهَهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٤٦﴾ أَوْ مَن يُنَشِّئُوا فِي الْحِلْيَةِ وَهُوَ فِي الْخِصَامِ غَيْرُ مُبِينٍ ﴿٤٧﴾ وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبْدُ الرَّحْمَنِ إِنثًا ۗ أَشْهَدُوا خَلْقَهُمْ ۗ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ وَيُسْأَلُونَ ﴿٤٨﴾ وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَنُ مَا عَبَدْنَاهُمْ ۗ مَا لَهُمْ بِذَٰلِكَ مِنْ عِلْمٍ ۗ إِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٤٩﴾

15. “Na wanamfanyia katika waja Wake fungu. Kwa hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila aliyedhaahiri.”

16. “Au amejichukulia watoto wanawake katika vile Alivyoviumba, na Akakuteulieni nyinyi watoto wanaume?”

17. “Na anapobashiriwa mmoja wao kwa yale aliyompigia mfano Mwenyezi Mungu, uso wake husawijika na hujaa hasira.”

18. “Ati aliyelewa katika mapambo, na katika mabishano hawezi kusema kwa bayana...?”

19. “Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake! Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wao watahojiwa!”

20. “Nao husema: Angelipenda Mwingi wa Rehema tusingeli waabudu sisi. Hawana ujuzi wowote wa hayo! Hawana ila kusema uwongo tu!”

Kukanushwa Washirikina Juu ya Kumjaalia Allah Kuwa na Mtoto

Allah تعالی Anauzungumzia uzushi na uongo walioueneza washirikina kwa kuhusisha baadhi ya wanyama kwa miungu yao batili na wengine kwa Allah. Ni sawa na Alivyoeleza Allah تعالی juu yao katika *Surat Al-A'aam*, katika Kauli Yake:

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا فَقَالُوا هَذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا فَمَا كَانَ لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى اللَّهِ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَى شُرَكَائِهِمْ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿١٣٦﴾

“Na wamemuekea sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea na wanyama Aliumba, nao husema: Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu - kwa madai yao - na hii ni ya miungu tunaowashirikisha. Basi vile walivyowakusudia miungu yao havimfikii Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia miungu yao. Ni uovu kabisa hayo wanayoyahukumu.” (6:136)

Kadhalika, wamefanya katika namna mbili za watoto, wa kiume na wa kike, kwa kumjaalia Allah تعالی Jinsia iliyo mbaya na hakiri machoni mwao, ambayo ni Jinsia ya watoto wa kike. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

أَلَكُمُ الذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَى ﴿٥٣﴾ تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَى ﴿٥٤﴾

“Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio Awe na wanawake? Huo ni mgawanyo wa dhulma!” (53:21-22)

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

وَجَعَلُوا لَهُ مِنْ عِبَادِهِ جُزْءًا إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ مُّبِينٌ ﴿٤٣﴾

“Na wanamfanyia katika waja wake fungu. Kwa hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila aliyedhahiri.”

Kisha, Allah تعالى Akasema:

أَمْ آتَّخَذَ مِمَّا يَخْلُقُ بَنَاتٍ وَأَصْفَنَكُمْ بِالْبَيْنِ ﴿٤٤﴾

“Au amejichukulia watoto wanawake katika vile Alivyoviumba, na Akakuteulieni nyinyi watoto wanaume?”

Huku ni kukanusha ghaya ya kuwakanushia wao, Allah تعالى Akasema,

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِمَا ضَرَبَ لِلرَّحْمَنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهَهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٤٥﴾

“Na anapobashiriwa mmoja wao kwa yale aliyompigia mfano Mwenyezi Mungu, uso wake husawijika na hujaa hasira.”

Yaani, pindi anapobashiriwa mmoja wao kwamba amezaliwa mmojawapo katika mabinti hao anaowafanya kuwa ni fungu la Allah تعالى, basi huichukia habari hiyo upeo wa chuki, tena humzidishia sana huzuni, na kujitenga na watu kwa sababu ya kujisikia aibu kutokana na hayo. Allah تعالى Anasema, ni kwa nini mnayachukia hayo na badala yake mnamnasibishia Allah hayo hayo.

Kisha, Allah تعالى Akasema,

أَوْ مَن يُنَشِّؤُا فِي الْحَلِيَّةِ وَهُوَ فِي الْخِصَامِ غَيْرُ مُبِينٍ ﴿٤٦﴾

“Ati aliyelelewa katika mapambo, na katika mabishano hawezi kusema kwa bayana...?”

Maana yake: Ni kuwa, mwanamke huchukuliwa kwamba ni mpungufu hukamilika kwa kuvaa mapambo tangu utotoni, na anapokhasimiana huwa hawezi kujieleza vyema na kujitetea. Kwa hivyo, ni kwa nini huyu anasibishwe kwa Allah تعالى, Ambaye Yeye Ndiye Mtukufu? Mwanamke ni mwenye upungufu wa dhahiri na wa ndani kwa hali halisi na kimaana. Yeye huukamilisha upungufu wake wa dhahiri na kuurekebisha kwa kuvaa mapambo na vilivyo katika maana hiyo ili auzibe upungufu wake. Maana ya upungufu wake, ni kwamba, yeye ni

dhaifu na hawezi kujinusuru pindi haja hiyo inapotokea kwa kutokuwa na njia wala hima.

وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبَادُ الرَّحْمَنِ إِنْتًا

“Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake!”

Yaani, itikadi yao ilikuwa hiyo. Allah تعالی Akawakanushia kauli yao hiyo kwa Kusema,

أَشْهَدُوا خَلْقَهُمْ

“Kwani wameshuhudia kuumbwa kwao?”

Inamaanisha, walishuhudia kwamba Allah تعالی Aliwaumba hali ya kuwa ni wanawake?

سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ

“Ushahidi wao utaandikwa...” Yaani: kuhusu hayo,

وَيُسْأَلُونَ

“...na wao watahojiwa!”

Juu ya hayo katika Siku ya Kiyama. Hili ni tishio kali na ahadi yenye nguvu kabisa.

وَقَالُوا لَوْ شَاءَ الرَّحْمَنُ مَا عَبَدْنَاهُمْ

“Nao husema: Angelipenda Mwingi wa Rehema tusingeliwaabudu sisi.”

Maana yake, walisema kuwa, ‘Lau Allah تعالی Angetaka, Angetuzuia sisi kuabudu masanamu haya ambayo yamefanywa katika maumbo ya Malaika ambao ni mabinti wa Allah تعالی, na Yeye Anayajua haya na Kutuacha tufanye hivyo.’ Kwa kuyasema haya, wakawa wamejumuisha namna nyingi za makosa. Kwanza: Kumnasibishia Allah تعالی watoto. Allah تعالی ni, Mwenye Utakasifu Mkubwa.

Pili: Madai yao kwamba Allah تعالی Aliwateua wana wa kike badala ya wa kiume, na wakawafanya kuwa Malaika, ambao ni waja wa *Ar-Rahman*, kuwa ni wanawake.

Tatu: Ibada yao kwao hao, bila ya dalili wala ushahidi au Idhini ya Allah تعالى, bali ni kutokana na uzushi tu, matamanio na kuwaiga waliowatangulia, viongozi wao, wakubwa na mababa, na kuingia katika ujahili.

Nne: Kuhoji kwao kwa kulipa dai hilo hadhi ya juu, na katika kuhoji huku wamefanya ujahili mkubwa. Allah تعالى Aliwakanushia vikali, kwani tangu Ampeleke Mtume na Kuteremsha Vitabu, Amri Yake ni kumuabudu Yeye tu Peke Yake, Asiye na mshirika, na Akawakataza waja Wake ku muabudu yoyote isipokuwa Yeye. Allah تعالى Akasema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ۗ فَمِنْهُمْ مَن هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ ۚ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكذِبِينَ ﴿٣٦﴾

“Na kwa hakika kwa kila umati Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo Aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao uliowathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanaokanusha.” (16:36)

وَسَأَلَ مَن أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رُّسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِن دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾

“Na waulize Mitume wetu Tuliowatuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah’mani?” (43:45)

Katika Aya hii, na baada ya kuitaja hoja yao, Allah تعالى Akasema:

مَا لَهُمْ بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ

“Hawana ujuzi wowote wa hayo!”

Yaani: kuhusu usahihi wa waliyoyasema na kuyafanyia hoja,

إِنَّ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ

“Hawana ila kusema uwongo tu!” Ina maana, wanaongopa na kuzusha uwongo. Mujahid alisema kuhusu kauli ya Allah تعالى,

مَا لَهُمْ بِذَلِكَ مِنْ عِلْمٍ إِنْ هُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ

“Hawana ujuzi wowote wa hayo! Hawana ila kusema uwongo tu!”

Mujahid alisema, “Hawaijui Kudura ya Allah تعالى juu ya hayo.”¹

* * *

¹ At-Tabari 21:583.

أَمْ آتَيْنَهُمْ كِتَابًا مِّن قَبْلِهِمْ فَهُمْ بِهِ مُسْتَمْسِكُونَ ﴿٢١﴾
 بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ
 مُّهْتَدُونَ ﴿٢٢﴾ وَكَذَٰلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّن
 نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا
 عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّهْتَدُونَ ﴿٢٣﴾ وَكَذَٰلِكَ مَا
 أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ
 إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا
 عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ
 مُّقْتَدُونَ ﴿٢٤﴾ * قُلْ أُولُو
 جِحْتِكُمْ بِأَهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ
 آبَاءَكُمُ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ
 كَافِرُونَ ﴿٢٥﴾ فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَنْظَرُ
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٦﴾
 مِمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢٧﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيِّدِي ﴿٢٨﴾
 وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٩﴾ بَلْ
 مَتَّعْتُ هَٰؤُلَاءِ وَآبَاءَهُمْ حَتَّىٰ جَاءَهُمُ الْحَقُّ وَرَسُولٌ مُّبِينٌ ﴿٣٠﴾
 وَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ قَالُوا هٰذَا سِحْرٌ وَإِنَّا بِهِ كَافِرُونَ ﴿٣١﴾
 وَقَالُوا لَوْلَا نَزَلَ هٰذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّن
 آلِ فِرْعَوْنَ لَكُنَّا بِآيَاتِهِ لَمُحْسِنِينَ ﴿٣٢﴾ أَهْمٌ يَقْسُمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ ۗ خُنْ
 فَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَّعِيشتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ
 فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُم بَعْضًا سُخْرِيًّا ۗ وَرَحْمَتُ
 رَبِّكَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٣٣﴾ وَلَوْلَا أَن يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةً
 وَاحِدَةً لَّجَعَلْنَا لِمَن يَكْفُرُ بِالرَّحْمٰنِ لِيُؤْتِيَهُم سُقْفًا مِّن
 فِضَّةٍ وَمَعَارِجَ عَلَيَّهَا يَظْهَرُونَ ﴿٣٤﴾ وَلِيُؤْتِيَهُم آتُونَآ وَسُرْرًا
 عَلَيَّآ يَتَّكُونَ ﴿٣٥﴾ وَزُخْرَفًا ۗ وَإِن كُلُّ ذَٰلِكَ لَمَّا
 مَتَّعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَالْآخِرَةُ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٣٦﴾

أَمْ آتَيْنَهُمْ كِتَابًا مِّن قَبْلِهِمْ فَهُمْ بِهِ مُسْتَمْسِكُونَ ﴿٢١﴾
 بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ
 مُّهْتَدُونَ ﴿٢٢﴾ وَكَذَٰلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مَا
 أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ
 إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا
 عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ
 مُّقْتَدُونَ ﴿٢٤﴾ * قُلْ أُولُو
 جِحْتِكُمْ بِأَهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ
 آبَاءَكُمُ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ
 كَافِرُونَ ﴿٢٥﴾ فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَنْظَرُ
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿٢٦﴾

21. "Kwani Tuliwapa Kitabu kabla ya hichi, na ikawa wao wanakishikilia hicho?"

22. "Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, basi na sisi tunaongoka juu ya nyayo zao."

23. "Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake walioneemeka walisema:

Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao."

24. "Akasema (Mwonyaji): Hata nikikuleteeni Dini yenye uwongofu bora kuliko mliowakuta nao baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyotumwa."

25. "Basi Tukawalipizia. Angalia ulikuwaje mwisho wa waliokadhibisha!"

Ubainisho Kuwa Washirikina Hawana Hoja

Allah تعالى Anawakanushia makafiri kutokana na ibada zao kwa asiyekuwa Allah تعالى, pasi na ushahidi, dalili, wala hoja,

أَمْ آتَيْنَهُمْ كِتَابًا مِّن قَبْلِهِ

"Kwani Tuliwapa Kitabu kabla yake..."

Yaani: kabla ya ushirikina wao,

فَهُمْ بِهِ مُسْتَمْسِكُونَ

"...na ikawa wao wanakishikilia hicho?"

Maana yake, katika ambayo wao wamo ndani yake, yaani, jambo lenyewe haliko hivyo.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

أَمْ أَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا فَهُوَ يَتَكَلَّمُ بِمَا كَانُوا بِهِ يُشْرِكُونَ ﴿٣٥﴾

"Au Tumewateremshia hoja ambayo kwayo ndio wanafanya ushirikina?" (30:35)

Yaani: haikuwa kama hivyo. Kisha, Allah تعالى Akasema:

بَلْ قَالُوا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّهْتَدُونَ ﴿٣٦﴾

"Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, basi na sisi tunaongoka juu ya nyayo zao."

Yaani: hawana ushahidi wa kutegemea, katika ambayo wamo ndani yake, miongoni mwa mambo ya ushirikina, bali ni kuwaiga mababa na mababu wao, kwani wao walikuwa ni katika umma mmoja, kusudio lake ni Dini moja. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنَّ هِنْدِيَمَ أُمَّتِكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja...” (23:52),

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنَا عَلَىٰ عَآئِرِهِمْ

“...basi na sisi kwa kufuata nyayo zao.”

Yaani, nyuma yao,

مُهْتَدُونَ

“...tunajiongoza...”

Hili ndio dai lao bila ya dalili. Halafu, Allah تعالى Alibainisha kwamba kauli yao hiyo ilikwishatangulia kusemwa na walioshabihiana nao na walio mithili yao katika nyumati zilizopita waliowakadhibisha Mitume. Nyoyo zao zimefanana kama yalivyo maneno yao.

كَذَلِكَ مَا آتَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْتَوٍ ۗ أَتَوَاصَوْا بِهِ ۗ

بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَآغُونَ ۗ

“Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu. Je! Wameambizana kwa haya? Bali hawa ni watu waasi.” (51:52-53)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema katika Aya hii,

وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ

أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ عَآئِرِهِمْ مُقْتَدُونَ ۗ

“Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake waliodeka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao.”

Kisha, Allah تعالى Akasema:

قَلَّ

“Akasema (Mwonyaji)...”

Yaani, Ewe Muhammad! Waambie hao washirikina,

أُولُو جُنَّتِكُمْ بِأَهْدَىٰ مِمَّا وَجَدْتُمْ عَلَيْهِ ءَابَاءُكُمْ قَالُوا إِنَّا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ كَافِرُونَ

“...Hata nikikuleteeni yenye uwongofu bora kuliko mliowakuta nayo baba zenu? Wakasema: Sisi tunayakataa tu hayo mliyotumwa.”

Yaani, lau wangejua na kuyakinisha usahihi wa uliyowaletea, wasingeliongoka kwayo, kwa sababu ya nia zao mbaya na kuifanyia kiburi haki na watenda haki. Allah تعالى Alisema,

فَأَتَقَمْنَا مِنْهُمْ

“Basi Tukawalipizia.”

Yaani, miongoni mwa nyumati zilizokataa Mitume, kwa adhabu za namna kwa namna, sawa na Alivyoeleza Allah تعالى katika habari zao, Kauli ya Allah تعالى,

فَأَنْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكْذِبِينَ

“Angalia ulikuwaje mwisho wa waliokadhibisha!”

Yaani, jinsi walivyohilikishwa na namna Allah تعالى Alivyowa nusuru Waumini.

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٦٦﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ

سَيَّبِدِينَ ﴿٦٧﴾ وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦٨﴾ بَلْ مَتَّعْتُ هَؤُلَاءِ

وَأَبَاءَهُمْ حَتَّىٰ جَاءَهُمُ الْحَقُّ وَرَسُولٌ مُّبِينٌ ﴿٦٩﴾ وَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ وَإِنَّا

بِهِ كَافِرُونَ ﴿٧٠﴾ وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ الْفَرِيقَيْنِ عَظِيمٍ ﴿٧١﴾

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ ۗ لَنْ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَّعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَرَفَعْنَا

بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَاتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سُخْرِيًّا ۗ وَرَحِمْتُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِّمَّا

تَجْمَعُونَ ﴿٢١﴾ وَلَوْلَا أَنْ يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً لَجَعَلْنَا لِمَنْ يَكْفُرُ بِالرَّحْمَنِ لِبُيُوتِهِمْ
 سُقُفًا مِّنْ فِضَّةٍ وَمَعَارِجَ عَلَيْهَا يَظْهَرُونَ ﴿٢٢﴾ وَلِبُيُوتِهِمْ أَبْوَابًا وَسُرُرًا عَلَيْهَا يَتَكَبَّرُونَ ﴿٢٣﴾
 وَزُخْرَفًا وَإِنْ كُلُّ ذَلِكَ لَمَّا مَتَّعَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةَ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٢٤﴾

26. "Na pale Ibrahim alipomuambia baba yake na kaumu yake: Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu,"

27. "Isipokuwa yule aliyeniumba, kwani Yeye Ataniongoa."

28. "Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee."

29. "Bali Niliwastarehesha hawa na baba zao mpaka ikawafikia Haki na Mtume aliyebainisha."

30. "Na ilipowafikia Haki wakasema: Huu ni uchawi, na sisi hakika tunaukataa."

31. "Na walisema: Kwa nini Qur'ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?"

32. "Kwani wao ndio wanaogawa rehema za Mola wako Mlezi? Sisi Tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani, na Tukawanyanyua baadhi yao juu ya wengine kwa daraja nyingi; kwa hivyo baadhi yao wanawafanya wengine wawatumikie. Na Rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya."

33. "Na lau isingekuwa watu watakuwa kundi moja Tungeliwajaalia wanaomkufuru Rahmani wana nyumba zao zina dari ya fedha, na ngazi zao pia wanazopandia."

34. "Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyoegemea juu yake."

35. "Na mapambo. Lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu, na Akhera iliyoko kwa Mola wako Mlezi ni ya wenye kumchamungu."

Nabii Ibrahim عليه السلام Kutangaza Kujitenga na Shiriki na Watu Wake

Allah تعالى Anatufahamisha kuhusu Mja Wake, Mtume Wake na Rafiki Yake, Kiongozi wa waongofu na baba wa Mitume wote waliokuja baada yake, ambaye nasaba na dini ya Makuraishi inanasibiana na yeye. Alijitenga mbali na baba yake na kaumu yake katika ibada yao ya masanamu, akasema:

إِنِّي وَإِذْ بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ ﴿٢١﴾ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيِّدِي ﴿٢٢﴾ وَجَعَلَهَا كَلِمَةً
بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ

“Hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu. Isipokuwa yule Aliyeniumba, kwani Yeye Ataniongoa. Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake.”

Yaani, kalima hii, ambayo ni kumuabudu Allah تعالى tu Peke Yake, asiye na mshirika, na kuyakana masanamu yote, isipokuwa Yeye. Nayo ni kalima ya *Laa ilaaha illallah* ambaye imeifanya iwe ya kudumu kwa dhuriya ya Ibrahim عليه السلام ambayo wanaifuata walio katika dhuriya yake, ambao Allah تعالى Amewaongoa.

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

“...ili warejee.”

Maana yake, kwenye neno hili.

‘Ikrimah, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, As-Suddi na wengine wamesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ

“Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake...”

“Inamaanisha Tamko la, *“Laa ilaaha illallah”* haliachi kuwa miongoni mwa wanaolisema katika dhuriya Zake.”¹

Rai sawa na hii ilisemwa na Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Ibn Zayd alisema, “Ni neno la Uislamu.”² Mtazamo wake huu unarejea katika yale yale yaliyoelezwa na walio wengi.

¹ At-Tabari 21:589.

² Al-Qurtubi 21:77.

Namna Watu wa Makkah Walivyopinga Kuwa Allah تعالی Hakuteremsha Qur'an na Jibu Lake

Kisha, Allah تعالی Alisema:

بَلْ مَتَّعْتُ هَتُولَاءِ

"Bali Tuliwastarehesha hawa..."

Yaani, washirikina,

وَأَبَاءَهُمْ

"...na baba zao..."

Umri wao ukawa mrefu katika upotevu wao,

حَتَّىٰ جَاءَهُمُ الْحَقُّ وَرَسُولٌ مُّبِينٌ

"...mpaka ikawafikia Haki na Mtume aliyebainisha."

Maana yake, baina ya Ujumbe na maonyo,

وَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ قَالُوا هَذَا سِحْرٌ وَإِنَّا بِهِ كَافِرُونَ ﴿٤٦﴾

"Na ilipowafikia Haki wakasema: Huu ni uchawi, na sisi hakika tunaukataa."

Kwamba walimfanyia kiburi na ukaidi, wakamuondosha Mtume ﷺ kutokana na ukafiri wao, husuda na kuruka mipaka.

وَقَالُوا

"Na walisema..."

Kama kupinga kile Alichoteremsha Allah تعالی na kutukuzwa,

لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ الْقَرَبَاتِ عَظِيمٍ

"...Kwa nini Qur'ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?"

Yaani: kwa nini Qur'an hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa ambaye ni mashuhuri machoni mwao, kutoka katika miji miwili, wakimaanisha, Makka

na At-Taif. Hili amelisema Ibn 'Abbas, Ikrimah, Muhammad bin Ka'ab, Al-Quradhi, As-Suddi na Ibn Zayd رضي الله عنهم¹.

Maulamaa wengi wa *Tafsir* walitaja kuwa kauli hiyo ilimkusudia Al-Walid bin Al-Mughirah na 'Urwah bin Mas'ud Ath-Thaqafi. Lililo dhahiri ni kwamba, lengo lao lilikuwa mtu mkubwa kutoka mojawapo kati ya miji hiyo miwili mikubwa.

Allah تعالى Akawajibu kuhusu huku kukengeuka kwao,

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ^٢

“Kwani wao ndio wanaogawa rehema za Mola wako Mlezi?”

Yaani, jambo hilo halijarudishwa kwao, bali ni la Allah تعالى, Naye Ndiye Ajuae zaidi namna ya Kujaalia Ujumbe Wake, kwani Hauteremshi, isipokuwa kwa kiumbe msafi zaidi wa nafsi na mtukufu wao zaidi, wa kaya na msafi wao zaidi wa asili.

Kisha, Allah تعالى Akabainisha kwamba Yeye Ametofautisha baina ya viumbe Wake vitu Alivyowapa miongoni mwa mali, riziki, akili, fahamu zao na nguvu za dhahiri na za ndani. Allah تعالى Amesema:

فَخُنَّ قَسَمَنَا بَيْنَهُمْ مَعِيشَتَهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا^٣

“Sisi Tumewagawanyia baina yao maisha yao katika uhai wa duniani...”

Kauli ya Allah تعالى:

لِيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سُخْرِيًّا^٤

“...baadhi yao wanawafanya wengine wawatumikie.”

Ilisemwa kuwa hii inamaanisha kuwa baadhi yao wanawahudumia wengine katika kazi zao, kwa sababu kila mmoja anamhitaji mwingine. Hii ni rai ya As-Suddi na wengine.¹ Kisha Allah تعالى Alisema,

¹ At-Tabari 21:592, 593.

² At-Tabari 21:595.

وَرَحْمَتُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ

“Na rehema za Mwenyezi Mungu ni bora kuliko hayo wanayo-yakusanya.”

Yaani, Rehema ya Allah تعالى kwa viumbe Wake ni kheri kwao kuliko mali waliyonayo na samani za maisha ya kidunia.

Mali Si Alama au Dalili ya Kuridhiwa na Allah تعالى

Halafu, Allah تعالى Akasema,

وَلَوْلَا أَنْ يَكُونَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Na lau isingekuwa watu watakuwa kundi moja...”

Maana yake, ‘kama si watu wengi kuamini kuwa kutoa mali ni alama ya mahaba Yetu kwa Tuliyempa, na kwa hivyo wangelikubali ukafiri kwa ajili ya mali.’ Hii ndio maana ya kauli ya Ibn ‘Abbas, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم.¹

لَجَعَلْنَا لِمَنْ يَكْفُرُ بِالرَّحْمَنِ لِبُيُوتِهِمْ سُقْفًا مِّنْ فِضَّةٍ وَمَعَارِجَ

“...Tungeliwajaalia wanaomkufuru Rahmani wana nyumba zao zina dari ya fedha, na ngazi zao...”

Yaani, ngazi na vidaraja vya fedha. Hili amelisema Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, As-Suddi, Ibn Zayd na wengine رضي الله عنهم.²

عَلَيْهَا يَطَّهَّرُونَ

“...pia wanazopandia.” Yaani, wanakwea.

وَلِبُيُوتِهِمْ أَبْوَابًا

“Na milango ya nyumba zao.” Na milango ya nyumba ina makomeo,

¹ At-Tabari 21:597.

² At-Tabari 21:600.

وَسُرُّرًا عَلَيَّهَا يَتَّكُونَ ﴿٢١﴾

“...na vitanda wanavyoegemea juu yake.”

Maana yake, vyote hivyo vinatokana na fedha,

وَزُخْرَفًا

“Na mapambo.”

Yaani, na dhahabu. Haya ameyasema Ibn ‘Abbas, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd رضي الله عنهم¹. Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَإِنْ كُلُّ دَٰلِكَ لَمَّا مَتَّعِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا

“Lakini hayo si chochote ila ni starehe ya maisha ya dunia tu...”

Yaani, hivyo ni katika vyenye kuisha, kuondoka na duni mbele ya Allah تعالى. Yeye Huwaharakishia malipo ya amali zao njema wanazofanya duniani, vyakula na vinywaji ili Akhera wasilipwe, watakuwa hawana jema lolote kwa Allah تعالى watakalolipwa. Ni sawa na ilivyosimuliwa katika Hadithi Sahih.² Pia ilielezwa katika Hadithi nyingine:

«لَوْ أَنَّ الدُّنْيَا تَرَبُّنُ عِنْدَ اللَّهِ جَنَاحَ بَعُوضَةٍ مَا سَمَىٰ مِنْهَا كَافِرًا شَرِبَةَ مَاءٍ»

“Lau kama dunia ingelingana kufikia uzani wa ubawa wa mbu mbele ya Allah, basi Asingelimnyweshwa humo kafiri tone la maji.”³

Al-Baghawi رحمه الله تعالى alieleza isnadi yake.⁴ Kisha Allah تعالى Akasema:

وَالْآخِرَةُ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِينَ

“...na Akhera iliyoko kwa Mola Wako Mlezi ni ya wenye kumchamungu.”

¹ At-Tabari 21:601, 602.

² Muslim 4:2162.

³ At-Tirmidhi 6:611.

⁴ Al-Baghawi 4:38. Riwaya sawa na hiyo ilinukuliwa na At-Tirmidhi na wengine.

Yaani: hiyo ni yao peke yao, wala hawashirikiani na yeyote asiyekuwa katika wao. Kwa ajili hii, pindi ‘Umar رضي الله عنه alipomtembelea Mtume ﷺ wakati akiwa katika kujitenga na wakeze, akamuona akiwa na alama za mkeka mbavuni mwake, macho yake yalibubujikwa na machozi kwa kulia na akasema: “Ewe Mjumbe wa Allah! Angalia Kisra na Kaisar na vile walivyo navyo, ilhali wewe ndiye bora zaidi katika viumbe Wake.” Wakati huo, Mtume ﷺ alikuwa amejjegemeza, akakaa na kusema,

«أَوْ فِي شَكِّ أَنْتَ يَا ابْنَ الْخَطَّابِ؟»

“Una mashaka ewe Ibn Al-Khattab?”

Halafu akasema:

«أَوْلَيْكَ قَوْمٌ عَجَلَتْ لَهُمْ طَيِّبَاتُهُمْ فِي حَيَاتِهِمُ الدُّنْيَا»

“Hao ni watu ambao mazuri yao yameharakishwa katika uhai wao wa duniani.”¹

Na katika masimulizi mengine,

«أَمَّا تَرْضَى أَنْ تَكُونَ لَهُمُ الدُّنْيَا وَلَنَا الْآخِرَةُ»

“Je hamridhii kwamba wao wawe na dunia na sisi tuwe na Akhera?”²

Pia, katika *Sahih* Mbili na nyingine, kumeandikwa kuwa, Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَشْرَبُوا فِي آيَةِ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ، وَلَا تَأْكُلُوا فِي صِحَافِهَا، فَإِنَّهَا لَهُمْ فِي الدُّنْيَا
وَلَنَا فِي الْآخِرَةِ»

“Msinywe katika vyombo vya dhahabu na fedha, wala msile katika sahani zake, kwani vitu hivyo ni kwa ajili yao duniani, na ni kwa ajili yetu huko Akhera.”³

¹ Muslim 2:113.

² Muslim 1:110.

³ *Fat’h Al-Bari* 9:465, Muslim 3:1637

Allah تعالى Amewapa vitu hivi duniani kwa sababu ya uduni wake, sawa na alivyopokea At-Tirmidhi na Ibn Majah kupitia njia ya Abu Hazim kutoka kwa Sahl bin Sa'd رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَوْ كَانَتِ الدُّنْيَا تَرْدُنُ عِنْدَ اللَّهِ جَنَاحَ بُعُوضَةٍ مَا سَمَى مِنْهَا كَافِرًا شَرِبَ مَاءَ أَبَدًا»

"Lau kama dunia ingelingana kufikia uzani wa ubawa wa mbu mbele ya Allah, basi Asingelimnyweshwa humo kafiri tone la maji."

At-Tirmidhi alisema: "Ni *Hasan Sahih*."



وَمَنْ يَعِشْ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقِضْ لَهُ
 لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٣٦﴾
 وَإِنَّهُمْ لَيَصُدُّوهُمْ عَنِ السَّبِيلِ
 مُهْتَدُونَ ﴿٣٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَنَا قَالَ يَلَيْتَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ
 بَعْدَ الْمَشْرِقَيْنِ فَبِئْسَ الْقَرِينُ ﴿٣٨﴾ وَلَنْ يَنْفَعَكُمُ الْيَوْمَ
 إِذْ ظَلَمْتُمْ أَنْتُمْ فِي الْعَذَابِ مُشْتَرِكُونَ ﴿٣٩﴾ أَفَأَنْتَ تُسْمِعُ
 الصُّمَّ أَوْ تَهْدِي الْأَعْمَىٰ وَمَنْ كَانَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٤٠﴾
 فَإِنَّمَا نَذَرْهُنَّ بِكَ فَإِنَّا مِنْهُم مُّنتَقِمُونَ ﴿٤١﴾ أَوْ تُرِيكَ
 الَّذِي وَعَدْنَاهُمْ فَإِنَّا عَلَيْهِم مُّقْتَدِرُونَ ﴿٤٢﴾ فَاسْتَمْسِكَ
 بِالَّذِي أُوحِيَ إِلَيْكَ ۗ إِنَّكَ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٤٣﴾ وَإِنَّهُ
 لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ ۗ وَسَوْفَ تُسْأَلُونَ ﴿٤٤﴾ وَسْأَلَ مَنْ
 أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ آلِهَةً
 يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ
 وَمَلَائِكِهِ فَقَالَ إِنِّي رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٤٦﴾ فَأَمَّا جَاءَهُمْ
 بِآيَاتِنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَضْحَكُونَ ﴿٤٧﴾ وَمَا نُرِيهِمْ مِنْ آيَةٍ
 إِلَّا هِيَ أَكْبَرُ مِنْ أُخْتِهَا ۗ وَأَخَذْنَاهُمْ بِالْعَذَابِ لَعَلَّهُمْ
 يَرْجِعُونَ ﴿٤٨﴾ وَقَالُوا يَا أَيُّهُ السَّاحِرُ الْوَدَّاعُ لَنَا رَبُّكَ بِمَا
 عَهِدَ عِنْدَكَ إِنَّا لَمُهْتَدُونَ ﴿٤٩﴾ فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ
 الْعَذَابَ إِذَا هُمْ يَنْكُتُونَ ﴿٥٠﴾

ءَالِهَةً يُعْبَدُونَ ﴿٥٠﴾

36. "Anayeyafanyia upofu maneno ya Rahmani Tunamuekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake."

37. *"Na hakika wao wanawazuilia njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka."*

38. *"Hata atakapotujia atasema: Laiti ungelikuwako baina yangu na wewe kama umbali baina ya mashariki na magharibi. Rafiki mwovu mno wewe!"*

39. *"Na kwa kuwa mlidhulumu, haitakufaeni kitu leo kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu."*

40. *"Je! Unaweza kuwasikilizisha viziwi, au unaweza kuwaongoa vipofu na waliomo katika upotofu uliowazi?"*

41. *"Na hata Tukikuondoa, Sisi Tatalipiza kisasi chetu kwao."*

42. *"Au Tutakuonesha Tuliowaahidi. Nasi bila ya shaka Tuna uweza juu yao."*

43. *"Basi wewe yashike yaliyofunuliwa kwako. Hakika wewe uko kwenye njia Iliyonyooka."*

44. *"Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako. Na mtakuja ulizwa."*

45. *"Na waulize Mitume Wetu Tuliowatuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah'mani?"*

Shetani Ndiye Rafiki wa Mtu Anayempinga Allah تعالی

Allah تعالی Amesema:

وَمَنْ يَعْشُ

"Anayeyafanyia upofu..."

Yaani, kwa makusudi, anajifanya kipofu na kuyapa mgongo,

عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ

"...maneno ya Rahmani..."

Neno Al-'Ashaa (asili ya neno Ya'sh) lina maana ya udhaifu katika jicho, na makusudio katika Aya hii ni udhaifu wa busara, na maarifa. Kauli ya Allah تعالی,

نُقِيضَ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ

“...Tunamuekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَمَنْ يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ

“Na anayempinga Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu...”
(4:115),

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ

“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke.”
(61:5) na,

وَقِيضْنَا لَهُمْ قُرَنَاءَ فَزَيَّنُوا لَهُمْ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ

“Na Tukawawekea marafiki, na wakawapambia yaliyo mbele yao na nyuma yao.” (41:25)

Allah تعالى Akasema katika Aya hii:

وَالَّذِينَ لَيُصَدُّونَهُمْ عَنِ السَّبِيلِ وَهُمْ مُحْسِنُونَ ۖ أَهْمُ مَهْتَدُونَ ﴿٤٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَنَا

“Na hakika wao wanawazuilia njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka. Hata atakapotujia...”

Yaani: Aliyeghafilisha na uongofu, Sisi Humpelekea mashetani wa kumpoteza na Humuelekeza njia ya Jahanamu. Pindi atakapokuja mbele ya Allah تعالى, katika Siku ya Kiyama, atalalamika kuhusu shetani aliyeteuliwa kuwa pamoja naye,

قَالَ يَنْلَيْتَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ بَعْدَ الْمَشْرِقَيْنِ فَبِئْسَ الْقَرِينُ

“...atasema: Laiti ungelikuwako baina yangu na wewe kama umbali baina ya mashariki na magharibi. Rafiki muovu mno wewe!”

Baadhi ya wasomaji husoma,

(حَتَّىٰ إِذَا جَاءَنَا)

(na wengine husoma hivi, *jaa-anaa*),

Ikiwa na maana ya mja wa Allah تعالى na shetani aliyepelikewa, wote wawili watatujia. Kisha, Allah تعالى Akasema,

وَلَنْ يَنْفَعَكُمْ أَلْيَوْمَ إِذْ ظَلَمْتُمْ أَنْتُمْ فِي آعْدَابٍ مُّشْتَرِكُونَ ﴿٣٦﴾

“Na kwa kuwa mlidhulumu, haitakufaeni kitu leo kwamba nyinyi mnashirikiana katika adhabu.”

Yaani, kujumuika kwenu Motoni wala kushirikiana kwenu katika adhabu ya uchungu hakutakusaidieni hata kidogo. Kauli ya Allah تعالى,

أَفَأَنْتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ أَوْ تَهْدِي الْعُمْىَ وَمَنْ كَانَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٧﴾

“Je! Unaweza kuwasikilizisha viziwi, au unaweza kuwaongoa vipofu na waliomo katika upotofu ulio wazi?”

Yaani, hilo si juu yako, bali, jukumu lako ni kufikisha tu, wala si kuongoka kwao, Allah تعالى Ndiye Humpa uongofu Amtakaye na Kumuacha apotee Amtakaye. Na Yeye, katika hayo, ni Mwenye Hekima na Uadilifu.

Lipizo la Allah تعالى kwa Maadui wa Mtume ni Lenye Kutokea

Kisha, Allah تعالى Alisema,

فَأِمَّا تَذْهَبَنَّ بِكَ فَإِنَّا مِنْهُمْ مُّنتَقِمُونَ ﴿٣٨﴾

“Na hata Tukikuondoa, Sisi Tutalipiza kisasi Chetu kwao.”

Kwamba hapana budi Tutawalipizia kisasi na Kuwaadhibu, hata kama wewe utaondoka,

أَوْ نُرِيَنَّكَ الَّذِي وَعَدْنَاهُمْ فَإِنَّا عَلَيْهِمْ مُّقْتَدِرُونَ ﴿٣٩﴾

“Au Tutakuonesha Tuliyo waahidi. Nasi bila ya shaka Tuna Uweza juu yao.”

Yaani, 'Tunaweza kuyafanya hayo yote mawili,' lakini, Allah تعالی Hatamfisha Mjumbe Wake mpaka Alitulize jicho lake kwa kuona maadui zake wamedhalilika na Kumpa umiliki na mamlaka juu yao na yanayodhamini. Hii ndio maana ya kauli ya As-Suddi na ndiyo aliyoihitari Ibn Jarir رحمه الله تعالى.¹

Kuhimizwa Kushikamana na Qur'an

Kisha, Allah تعالی Akasema,

فَأَسْتَمِسْكَ بِالذِّئْبِ أَوْحَىٰ إِلَيْكَ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٤٤﴾

“Basi wewe yashike yaliyofunuliwa kwako. Hakika wewe uko kwenye njia iliyonyooka.”

Yaani: shikamana na Qur'an inayoteremshwa moyoni mwako, kwani ni ya kweli, na yale inayoyaelekeza ya kweli ambayo hupelekea kwenye njia iliyonyooka yenye kufikisha kwenye Bustani zenye neema na kheri ya daima milele.

وَإِنَّهُ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ ۗ

“Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako.”

Ilisemwa kwamba hii inamaanisha kuwa, 'ni kwa ajili ya heshima yako na kwa kaumu yako.' Ni rai ya Ibn Abbas, Mujahid, Qatadah, As-Suddi na Ibn Zayd رضي الله عنهم.²

Maana yake ni kwamba, hiyo ni heshima kwao, kwa sababu iliteremshwa kwa lugha yao, basi wao ndio wenye kuifahamu zaidi, na kwa hivyo, inatakikana wawe ndio wenye kuitilia nguvu zaidi na wawe wajuzi zaidi kuliko watu wengine na wawe wenye kushikamana zaidi na amri zake. Hivi ndivyo wabora wao walivyokuwa, miongoni mwa Muhajirina wa mwanzo waliotangulia na walioshabihiana nao na waliowafuata. Imesemwa pia, kuwa maana ya Aya,

وَإِنَّهُ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ ۗ

“Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako.”

¹ At-Tabari 21:609.

² At-Tabari 21:610, 611.

Ni, kwa ajili ya kukukumbusha wewe na kaumu yako. Na kuainishwa wao kutajwa hapa, hakufanyi kukawatoa wengine katika hili.

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٣﴾

“Na hakika Tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo makumbusho yenu. Je! Hamzingatii?” (21:10)

وَأَنْذِرْ عَشِيرَتَكَ الْأَقْرَبِينَ ﴿٢٦﴾

“Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe.” (26:214)

وَسَوْفَ تَسْتَظُنُّونَ

“Na mtakuja ulizwa.”

Kuhusu hii Qur’an, na namna mlivyokuwa mkiitumia na namna mlivyoipokea.

وَسَأَلْنَا مَنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿١٦﴾

“Na waulize Mitume wetu Tuliowatuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah’mani?”

Yaani: Mitume wote walilingania katika hayo uliyowalingania watu, kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiye na mshirika, na walikataza kuabudiwa masanamu washirika wengine.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْبِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

“Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na mue pukeni Shetani.” (16:36)

Mujahid anasema, usomaji wa ‘Abdallah bin Mas’ud رضي الله عنه ni,

(وَاسْأَلِ الَّذِينَ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا)

“Was-alil-Ladhina Arsalnaa ilayhim qablaka (min) rusulina.”¹

Na hivi ndivyo alivyoisimulia Qatadah, Adh-Dhahhak na As-Suddi, kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه.²

Hii inaonekana kama namna nyingine ya *Tafsiri* na si kisomo. *Allahu Aalam.*

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَقَالَ إِنِّي رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٦﴾
 فَلَمَّا جَاءَهُمْ بِآيَاتِنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَضْحَكُونَ ﴿٣٧﴾ وَمَا نُرِيهِمْ مِنْ آيَةٍ إِلَّا هِيَ أَكْبَرُ
 مِنْ أُخْتِهَا ۗ وَأَخَذْنَاهُمْ بِالْعَذَابِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٣٨﴾ وَقَالُوا يَا أَيُّهُ السَّاحِرُ الْوَدَّاعُ لَنَا
 رَبُّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ إِنَّا لَمُهْتَدُونَ ﴿٣٩﴾ فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ الْعَذَابَ إِذَا هُمْ
 يَنْكُتُونَ ﴿٤٠﴾

46. “Na bila ya shaka Tulimtuma Musa kwa Ishara Zetu ende kwa Firauni na waheshimiwa wake, na akasema: Hakika mimi ni Mtume wa Mola Mlezi wa walimwengu wote!”

47. “Lakini alipowajia na Ishara Zetu wakaingia kuzicheka.”

48. “Na hatukuwaonesha Ishara yoyote ila hiyo ilikuwa kubwa zaidi kuliko nyenginewe. Na Tukawakamata kwa adhabu ili warejee.”

49. “Na wakasema: Ewe mchawi! Tuombe kwa Mola wako Mlezi kwa ile ahadi aliyokuahidi; hakika sisi tutakuwa wenye kuongoka.”

50. “Basi Tulipowaondolea adhabu hiyo, mara wakaingia kuvunja ahadi.”

¹ At-Tabari 21:611.

² At-Tabari 21:611, 612.

Ishara za Nabii Musa عليه السلام na Kuchekwa na Watu wa Firauni na Kutengua Kwao Ahadi

Allah تعالى Anaeleza kuhusu mja na Mjumbe Wake, Musa عليه السلام kwamba Alimtuma kwa Firauni na wakuu wake, kama vile maamiri, mawaziri, makada, wafuasi na raia waliotokana na makhofti na Wana wa Israel, akiwalingania katika kumuabudu Allah تعالى tu, Peke Yake, Asiye na mshirika, na Akawakanya dhidi ya kumuabudu mwingine, asiyekuwa Yeye, na kwamba amepewa ishara kubwa za kumpa nguvu kama vile mkono wake na fimbo yake. Pamoja na ishara nyingine, kama vile tufani, nzige, chawa,¹ vyura, damu, kupungua kwa mazao, watu na matunda. Licha ya haya yote, walifanya kiburi dhidi ya kuufuata ujumbe na kumfuata yeye. Wakayakataa, wakayakejeli, na wakayacheka aliyowaletea,

وَمَا تُرِيهِمْ مِّنْ آيَةٍ إِلَّا هِيَ أَكْبَرُ مِنْ أُخْتِهَا^ط

“Na hatukuwaonesha Ishara yoyote ila hiyo ilikuwa kubwa zaidi kuliko nyenginewe.”

Pamoja na haya, hawakurejea kutoka katika uasi na upotevu, ujahili na kuchanganyikiwa, na kila ilipowajia ishara mojawapo katika hizo, walinyenyekwa kwa Nabii Musa عليه السلام na walimbembeleza katika mazungumzo, kwa kusema:

يَتَأَيَّهَ السَّاحِرُ

“Ewe mchawi!...” Yaani: mtaalamu hili amelisema Ibn Jarir رحمه الله تعالى¹. Wataalamu wa zama zao walikuwa wachawi, wala uchawi katika zama zao, haukuwa jambo la kulaumiwa kwao. Kwa hivyo, kauli yao hiyo, haikuwa kama njia yao ya kumkosa, kwa sababu walikuwa katika hali ya dharura, kwa hivyo wasingelikuwa na fursa ya kumsema vibaya. Hii ilikuwa njia ya kumpa heshima, katika madai yao, na kila mara, walikuwa wakimuahidi Musa عليه السلام, kwamba wakiondoshewa tatizo hili, wangemuamini na kuwaacha Wana wa Israil waondoke pamoja naye, lakini, kila mara waliyavunja waliyoyaahidi. Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

¹ Angalia maelezo ya matukio hayo katika juzuu ya nne, *Tafsir ya Surat Al-A'raaf* (7:133).

² At-Tabari 21:615.

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجُرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالْأَدَمَ ۚ آيَاتٍ مُّفَصَّلَاتٍ فَاسْتَكْبَرُوا
وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿٣٦﴾ وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوا يَا مُوسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا
عَهِدَ عِنْدَكَ لَئِن كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٣٧﴾
فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمْ الرِّجْزَ إِلَىٰ أَجَلٍ هُمْ بَلِغُوهُ إِذَا هُمْ يَنْكُتُونَ ﴿٣٨﴾

“Basi Tukawapelekea tufani, na nzige, na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu. Na ilipowaangukia adhabu wakasema: Ewe Musa! Tuombe kwa Mola Wako Mlezi kwa Aliyokuahidi. Ukituondolea adhabu hii hapana shaka tutakuamini, na tutawaachilia Wana wa Israeli wende nawe. Lakini tukiwaondolea adhabu mpaka muda fulani wao waufikie, mara wakivunja ahadi yao.” (7:133-135)

* * *

وَنَادَى فِرْعَوْنُ فِي قَوْمِهِ قَالَ يَا قَوْمِ أَلَيْسَ لِي مُلْكُ مِصْرَ
 وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٥١﴾ أَمْ
 أَنَا خَيْرٌ مِّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ وَلَا يَكَادُ يُبِينُ ﴿٥٢﴾
 فَلَوْلَا أَلْفَىٰ عَلَيْهِ آسُورَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَأِكَةُ
 مُقْتَرِبِينَ ﴿٥٣﴾ فَاسْتَخَفَّ قَوْمَهُ فَاطَاعُوهُ إِنَّهُمْ كَانُوا
 قَوْمًا فٰسِقِينَ ﴿٥٤﴾ فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اٰنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ
 فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾ فَجَعَلْنَاهُمْ سَلْفًا وَمَثَلًا
 لِّلْآخِرِينَ ﴿٥٦﴾ * وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا
 قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٥٧﴾ وَقَالُوا ءَأَلْهَيْتَنَا خَيْرٌ أَمْ هُوَ
 مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا بَلْ هُمْ قَوْمٌ خٰصِمُونَ ﴿٥٨﴾ إِنَّ
 هُوَ إِلَّا عَبْدٌ اٰتَعَمَّنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرٰءِيلَ
 ﴿٥٩﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْاَرْضِ يَخْلُقُونَ
 ﴿٦٠﴾ وَإِنَّهُمْ لَعِلْمٌ لِّلسَاعَةِ فَلَا تَمْتَرْنَ بِهَا وَاَتَّبِعُونَ ؕ
 هَذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾ وَلَا يَصُدُّكُمْ الشَّيْطٰنُ إِنَّهُ
 لَكُمُ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٢﴾ وَلَمَّا جَاءَ عِيسَىٰ بِالْبَيِّنٰتِ قَالَ قَدْ
 جِئْتُكُمْ بِالْحِكْمَةِ وَلِأُبَيِّنَ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي تَخْتَلِفُونَ فِيهِ
 ؕ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ هُوَ رَبُّكُمْ
 فَاعْبُدُوهُ ؕ هَذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦٣﴾ فَاخْتَلَفَ
 الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ ؕ قَوْلٌ لِّلَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ عَدَابِ
 يَوْمِ أَلِيمٍ ﴿٦٤﴾

وَنَادَى فِرْعَوْنُ فِي قَوْمِهِ قَالَ يَا قَوْمِ أَلَيْسَ لِي مُلْكُ مِصْرَ وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٥١﴾ أَمْ أَنَا خَيْرٌ مِّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ وَلَا يَكَادُ يُبِينُ ﴿٥٢﴾ فَلَوْلَا أَلْفَىٰ عَلَيْهِ آسُورَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَأِكَةُ مُقْتَرِبِينَ ﴿٥٣﴾ فَاسْتَخَفَّ قَوْمَهُ فَاطَاعُوهُ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فٰسِقِينَ ﴿٥٤﴾ فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اٰنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾ فَجَعَلْنَاهُمْ سَلْفًا وَمَثَلًا لِّلْآخِرِينَ ﴿٥٦﴾

51. "Na Firauni alitangaza kwa watu wake, akisema: Enyi watu wangu! Sikuwa mimi mwenye ufalme wa Misri, na hii mito inapita chini yangu? Je! Hamuoni?"

52. "Au mimi si bora kuliko huyu aliye mnyonge, wala hawezi kusema waziwazi?"

53. "Basi mbona hakuvikwa vikuku vya dhahabu, au hawakuja Malaika pamoja naye wakamwandama?"

54. *“Basi aliwachezea watu wake, na wakamtii. Kwa hakika hao walikuwa watu wapotovu.”*

55. *“Walipotukasirisha Tuliwapatiliza Tukawazamisha wote!”*

56. *“Kisha Tukawafanya kuwa watangulizi na mfano kwa watu wa baadaye.”*

Hotuba ya Firauni kwa Watu Wake na Namna Allah تعالی Alivyomuangamiza

Allah تعالی Anatoa habari juu ya Firauni, kuhusu ukaidi, ufidhuli, ukafiri na ujeuri wake, kwamba alikusanya kaumu yake na kuwakhutubia kwa majivuno na ufakhari juu ya dola ya Misri na mamlaka yake humo,

أَلَيْسَ لِي مُلْكُ مِصْرَ وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي^ط

“Kwani mimi sinao huu ufalme wa Misri, na hii mito inapita chini yangu?”

Qatadah amesema, “Walikuwa na bustani na mito ya maji.”¹

أَفَلَا تُبْصِرُونَ

“Je! Hamuoni?”

Yaani: Je, hamuoni ukuu na ufalme nilio nao, akimaanisha kuwa Musa عليه السلام na wafuasi wake ni mafukara na dhaifu. Hii ni sawa na Kauli Yake nyingine:

فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٢٣﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَى ﴿٢٤﴾ فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَى ﴿٢٥﴾

“Akusanya watu akanadi. Akasema: mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu kabisa. Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa tamko la mwisho na la mwanzo.” (79:23-25)

أَمْرًا أَنَا خَيْرٌ مِّنْ هَذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ

“Au mimi si bora kuliko huyu aliyeponyongea...”

¹ At-Tabari 21:616.

As-Suddi alisema, "Alikuwa akisema, 'kwa ukweli, mimi ni mbora kuliko huyu, wa kudharaulika.'"¹ Hivi ndivyo pia walivyosema baadhi ya wanasarufi wa Basrah,² kuwa, maana ya neno *Am* (ama, au) hapa ni *bal* (bali). Hili linatiliwa nguvu na aliyoyasimulia Al-Fura-a kutoka kwa baadhi ya wasomaji Qur'ani kwamba walisoma, "*Amaa ana khayrun min haadhaal-Ladhiy huwa mahiyn.*"³ Ibn Jarir alisema, "Lau kisomo hiki kingelikuwa sahihi, basi maana yake nayo ingelikuwa sahihi na wazi, lakini kisomo hiki kimetofautiana na kisomo cha watu wa miji mingine ambao waliisoma, "*Am ana khayrun min haadhal-Ladhiy huwa mahiyn,*" kwa kuuliza.⁴

Ibn Kathir رحمه الله تعالى anasema, kwa kuikadiria, vyovyote vile, Firauni, laana ya Allah تعالى imshukie, anamaanisha kuwa yeye ni mbora kuliko Musa عليه السلام, na katika kauli yake hii, alidanganya dhahiri shahiri, laana za Allah تعالى zimshukie mfululizo mpaka Siku ya Kiyama. Amekusudia kwa kauli yake, "...aliye mnyonge." Ni sawa na alivyosema Sufyan: "Duni." Qatadah na As-Suddi wamesema, "Yaani, dhaifu." Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema: "Yaani, hana ufalme wala utawala wala mali."

وَلَا يَكَادُ يُبِينُ

"...wala hawezi kusema waziwazi?"

Yaani, hana ufasaha katika mazungumzo yake, hawezi kusema vyema.

Kauli ya Firauni, "aliye mnyonge," ni uongo, bali yeye (Firauni) ndiye dhaifu, hakiri kwa umbo, tabia na dini. Musa عليه السلام ndiye sharifu kwa kuwa mkweli, mwema na mwongofu.

وَلَا يَكَادُ يُبِينُ

"...wala hawezi kusema waziwazi?"

Pia ni uzushi, kwani, ingawa Musa عليه السلام alipatwa na tatizo katika ulimi wake utotoni kwa kuunguzwa na kaa la moto, alikwisha muomba Allah تعالى Akifungue kifundo katika ulimi wake ili wayaelewe maneno yake. Allah تعالى Alimtakabalia dua yake hiyo katika Kauli Yake nyingine,

¹ At-Tabari 21:616.

² At-Tabari 21:617.

³ At-Tabari 21:618.

⁴ At-Tabari 21:618.

قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَىٰ

“Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa!” (20:36)

Inawezekana kuwa vitu ambavyo hakuomba kuondoshewa vilikuwa vimebakia, kama alivyosema Al-Hasan Al-Basri رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, na kwa hakika, aliomba kuondoshewa kilichozuia katika jambo lake la kubalighisha na kuelewika. Kwa hivyo, mambo ya kimaumbile, ambayo hayakutendwa kwa makusudi na mja, hayamtii aibu wala lawama. Ingawa Firauni alikuwa na ufahamu na akili, alikuwa akiyajua haya, lakini alitaka kuwavuruga na kuwapoteza raia wake, kwani wao walikuwa majahili na mazuzu, na ndio maana ya Kauli Yake,

فَلَوْلَا أَلْقَىٰ عَلَيْهِ آسُورَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ

“Basi mbona hakuvikwa vikuku vya dhahabu...”

Yaani, mapambo ya mikononi. Hii rai ya Ibn ‘Abbas, Qatadah na wengine رضي الله عنهم.¹

أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَائِكَةُ مُقْتَرِنِينَ

“...au hawakuja Malaika pamoja naye wakamuandama?”

Yaani: wa kumtumikia na kumtolea ushahidi kuhusu ukweli wake. Aliangalia sura ya nje, na hakuifahamu siri ya ndani ambayo ndiyo iliyo wazi zaidi kuliko aliyoitizama, lau kama angelikuwa mwerevu.

Kwa ajili hii, Allah تَعَالَى Amesema:

فَأَسْتَخَفَّ قَوْمَهُ، فَطَاعُوهُ

“Basi aliwachezea watu wake na wakamtii.”

Yaani, alizikhafifisha akili zao na akawaitia katika upotevu, nao wakamuitikia,

إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ

“Kwa hakika hao walikuwa watu wapotovu.”

Allah تَعَالَى Alisema:

¹ At-Tabari 21:619.

فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اَنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ اَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

“Walipotukasirisha Tuliwapatiliza Tukawazamisha wote!”

‘Ali bin Abi Twalhah amesema toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: “Wametukasirisha, maana yake wametughadhishisha.”¹ Adh-Dhahhak amesema: “Wametughadhishisha, Hii pia ni rai ya Ibn ‘Abbas, Mujahid, Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi, Qatadah, As-Suddi na wafasiri wengine رضي الله عنهم.”² Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa ‘Uqbah bin ‘Amir رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا رَأَيْتَ اللهَ تَبَارَكَ وَتَعَالَى يُعْطِي الْعَبْدَ مَا يَشَاءُ، وَهُوَ مُقِيمٌ عَلَى مَعَايِيبِهِ، فَإِنَّمَا ذَلِكَ اسْتِذْرَاجٌ مِنْهُ لَهُ»

“Pindi utakapoona Allah Anampa mja akitakacho, ilhali anaendelea katika maasi, basi huko ni kuvutwa Kwake.” Kisha akasoma,

فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اَنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ اَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

“Walipotukasirisha Tuliwapatiliza Tukawazamisha wote!”³

Twariq bin Shihaab amesema, “Nilikuwa pamoja na ‘Abdullah akatajiwa mauti ya ghafla, akasema, ‘Hiyo ni nafuu kwa Muumini na majuto kwa kafiri.’ Halafu akasoma,

فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اَنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ اَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

“Walipotukasirisha Tuliwapatiliza Tukawazamisha wote!”⁴

‘Umar bin ‘Abdul-‘Aziz رحمه الله تعالى amesema, “Nimekuta adhabu huja pamoja na mghafala.” Anamaanisha Kauli ya Allah تعالى,

فَلَمَّا ءَاسَفُونَا اَنْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ اَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

“Walipotukasirisha Tuliwapatiliza Tukawazamisha wote!”

¹ At-Tabari 21:622.

² At-Tabari 21:622, Ad-Dur Al-Manthur 7:383.

³ Ahmad 4:145, kuna tofauti ndogo.

⁴ Ad-Dur Al-Manthur 7:384.

فَجَعَلْنَهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِّلَّآخِرِينَ ﴿٥١﴾

“Kisha Tukawafanya kuwa watangulizi na mfano kwa wa baadaye.”

Abu Mijlaz alisema, “Ni mithili ya wale wanaofanya sawa na walivyofanya wao.”¹ Yeye na Mujahid walisema, “Mfano” yaani, fundisho kwa wanaokuja baada yao.²

Allah تعالى, Ndiye Mwenye Kuwaongoza waja katika njia nyoofu, na Kwake Yeye Ndiko marejeo ya mwisho.

* وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٥٢﴾ وَقَالُوا ءَأَلِهَتُنَا خَيْرٌ أَمْرٌ هُوَ مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴿٥٣﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٤﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾ وَإِنَّهُمْ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا وَاتَّبِعُونِ ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٥٦﴾ وَلَا يَصُدُّكُمْ الشَّيْطَانُ ۗ إِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٥٧﴾ وَلَمَّا جَاءَ عِيسَى بِالْبَيِّنَاتِ قَالَ قَدْ جِئْتُكُمْ بِالْحِكْمَةِ وَلِأُبَيِّنَ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي تَخْتَلِفُونَ فِيهِ ۗ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ هُوَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٥٨﴾ فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ ۗ فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ عَذَابِ يَوْمِ أَلِيمٍ ﴿٥٩﴾

57. “Na alipopigiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele.”

58. “Wakasema: Miungu yetu kwani si bora kuliko huyu? Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu. Bali hao ni watu wagomvi!”

59. “Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliyeemnesha na Tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israeli.”

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:384.

² Al-Qurtubi 16:102.

60. "Na Tungelipenda Tungeliwafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi badala yenu."

61. "Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama. Basi usiitilie shaka, na nifuatani. Hii ndiyo Njia Iliyonyooka."

62. "Wala asikuzuilieni Shetani. Hakika yeye ni adui yenu wa dhaahiri."

63. "Na alipokuja Isa na dalili zilizo wazi, alisema: Nimekujieni na hikima, na ili nikuelezeni baadhi ya yale mliyokhitalifiana. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, na mnitii mimi."

64. "Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mola Wangu Mlezi, na ni Mola Wenu Mlezi. Basi Muabuduni Yeye tu. Hii ndiyo Njia Iliyonyooka."

65. "Lakini makundi kwa makundi yao yalikhitalifiana wao kwa wao. Ole wao waliodhulumu kwa adhabu ya siku iumizayo"

Dharau ya Makuraishi kwa Mwana wa Maryam عليه السلام na Hadhi yake Mbele ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza kuhusu ukaidi wa Makuraishi katika ukafiri wao,

وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٥١﴾

"Na alipopigiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele."

Wengine kadha walisimulia kwamba Ibn 'Abbas , Mujahid, 'Ikrimah, As-Suddi na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم walisema, "Walicheka, yaani, walipendezwa nalo."¹ Qatadah alisema, "Wanatishika na kucheka."² Ibrahim An-Nakha'i alisema, "Waliupa mgongo."³ Sababu ya hayo, ni kama aliyotaja Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى katika Sira, pale aliposema, "Ilinifikia habari, kwamba,

¹Al-Qurtubi 16:103.

²At-Tabari 21:627.

³Al-Qurtubi 16:103.

siku moja Mtume ﷺ aliketi pamoja na Al-Walid bin Al-Mughirah msikitini. Akaja An-Nadhr bin Al-Harith na kukaa pamoja nao. Katika kikao hicho, walikuwepo watu wengine wa kabila la Kikuraishi. Mtume ﷺ akazungumza, kisha An-Nadhr bin Al-Harith akamjia, Mtume ﷺ akazungumza naye mpaka [Mtume] akamshinda kwa hoja, Kisha akamsomea yeye na wao:

إِنكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصْبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرِدُونَ ﴿٥١﴾

“Hakika nyinyi na hao mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu; huko mtaingia tu.” (21:98)

Kisha Mtume ﷺ akasimama, akamuelekea ‘Abdullah bin Az-Zab’ari At-Tamimi. Al-Walid bin Al-Mughirah akamuambia: “Wallahi! An-Nadhr bin Al-Harith hakusimama kwa mwana wa ‘Abdul-Muttwalib, wala hakuketi (alishindwa kwa hoja), na Muhammad amedai kuwa mimi na miungu yetu hii tunayoiabudu ni kuni za Jahanamu.”

‘Abdullah bin Az-Zab’ari, alisema: “Wallahi! Ikiwa nitakutana naye, nitamshinda kwa hoja. Muulizeni Muhammad, iwapo kila anayeabudiwa ghairi ya Allah ﷻ ataingia Jahanamu pamoja na hao waliomuabudu, kwani sisi huwaabudu Malaika, Mayahudi humuabudu ‘Uzayr na Wakristo humuabudu ‘Isa bin Maryam.” Al-Walid na waliokuwa naye katika baraza hilo, wakafurahishwa sana na kauli ya ‘Abdullah bin Az-Zab’ari. Wakaona kwamba ameleta hoja nzuri ya kuweza kushinda. Akayasema hayo kwa Mtume ﷺ, ambaye alisema,

«كُلُّ مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُعْبَدَ مِنْ دُونِ اللَّهِ فَهُوَ مَعَ مَنْ عَبَدَهُ، فَإِنَّهُمْ إِنَّمَا يَعْْبُدُونَ الشَّيْطَانَ وَمَنْ أَمَرَهُمْ بِعِبَادَتِهِ»

“Kila mwenye kupenda kuabudiwa kinyume cha Allah, basi yeye yu pamoja na anayemuabudu, kwa hakika, wao wanamuabudu Shetani na aliyewaamuru kumuabudu.”

Allah ﷻ Akateremsha Aya,

إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنَّا مُبْعَدُونَ ﴿١٠١﴾

“Ama wale ambao wema Wetu umewatangulia, hao watatenganishwa na hayo.” (21:101)

Yaani: 'Isa, 'Uzayr, watawa na wanazuoni wachamungu walioabudiwa kinyume na matakwa yao, ambao waliishi katika kumtii Allah تعالى. Wapotevu waliokuja baada yao, ndio waliwafanya wao kuwa miungu badala ya Allah تعالى. Allah تعالى Aliteremsha pia, Aya inayohusu wao kuwaabudu Malaika na kudai kuwa hao ni mabinti wa Allah,

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ﴿٥١﴾

“Na wanasema: Arrahman, Mwingi wa Rehema, ana mwana! Subhanahu, Ametakasika na hayo! Bali hao (wanaowaita wana) ni watumwa waliotukuzwa.” (21:26)

Aliteremsha pia, Aya zinazotaja jambo la 'Isa bin Maryam عليه السلام, kuabudiwa badala ya Allah تعالى, akastaajabu Al-Walid na wengine waliokuwepo katika mjadala, Aya ifuatayo iliteremshwa:

وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٥٢﴾

“Na alipopigiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele.”

Yaani: wanatumia kama hoja ya kuukataa ujumbe wako. Kisha Allah تعالى Alimtaja Nabii Isa عليه السلام kwa Kusema,

إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٣﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَجْعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِنَّهُ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliye neemesha na Tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israeli. Na Tungelipenda Tungeliwafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi wakifuatana. Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama.”

Maana yake, ishara alizowekewa mkononi mwake, kama vile kuhuisha maiti na kuponya maradhi, zinatoshwa kuwa ni dalili za kukurubia Saa ya Mwisho. Allah تعالى Anasema:

فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا وَاتَّبِعُونِ ۗ هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ

“Basi usiitilie shaka, na nifuatani. Hii ndiyo njia iliyo nyooka.”

Ibn Jarir رضي الله عنهما Alitaja katika riwaya ya Al-'Awfi kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

﴿وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ﴾

“Na Alipopiwa mfano Mwana wa Mariamu, watu wako waliupiga ukelele.”

Kuwa, Maana yake ni Makuraishi, pindi walipoambiwa,

﴿إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرِدُونَ﴾

“Hakika nyinyi na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu; huko mtaingia tu.” (21:98)

Mpaka mwisho wa Aya hizi. Makuraishi wakamuuliza, ‘Ni vipi kuhusu Mwana wa Maryam?’ Yeye akawajibu,

﴿ذَٰكَ عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ﴾

“Huyo ni Mja na Mjumbe wa Allah.”

Wakasema, ‘Wallahi! Anakusudia sisi tumfanye yeye awe mola mlezi, sawa na Wakristo walivyomfanya Nabii Isa bin Maryam عليه السلام kuwa bwana.’ Allah تعالى Akasema,

﴿مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ﴾

“Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu. Bali hao ni watu wagomvi!”

﴿إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَتَعَمَّنَا عَلَيْهِ﴾

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliemneemesha...”

Qatadah alieleza, “Walikuwa wakisema, ‘Miungu yetu ni bora zaidi kuliko Yeye.’” Qatadah alisema tena, kuwa Ibn Mas‘ud رضي الله عنه alisoma,

¹ At-Tabari 21:625. Zipo riwaya nyingine kama hiyo: *Mushkil Al-Athar* 1:431 na Al-Hakim 2:385.

(أَلَيْهِنَّ خَيْرٌ أَمْ هَذَا)

(Je, miungu yetu ni bora au (mtu) huyu?) Wakimdhania Muhammad ﷺ.

مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا

“Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu.”

Maana yake, kwa ajili ya ubishi tu lakini, walikuwa wakijua kwamba ‘Isa hakujumuishwa katika Aya (21:98), kwa sababu isingelingia akilini. Nalo ni Neno la Allah تعالى:

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

“Hakika nyinyi na hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu...” (21:98)

Kisha, hayo wanaambiwa Makuraishi, kwamba wao walikuwa wakiyaabudu masanamu na vyenye kushirikishwa na Allah تعالى, wala hawakuwa wakimuabudu Masihi, kwa hivyo, kwa nini aingizwe katika Aya? Hii inaoneshwa wazi kuwa maneno yao hayo yalikuwa ni ubishi wao, hawakuwa wakiamani kuwa ni sahihi. Imamu Ahmad, alisimulia kuwa Abu Umamah رضي الله عنه alieleza kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا ضَلَّ قَوْمٌ بَعْدَ هُدًى كَانُوا عَلَيْهِ، إِلَّا أُزِرُوا الْجَدَلَ»

“Hapana watu wanaopotea baada ya uongofu waliokuwa nao, isipokuwa hurithishwa katika malumbano (yasiyo na maana).”

Kisha, Mtume ﷺ, akasoma Aya hii:

مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴿٥١﴾

“Hawakukupigia mfano huo ila kwa ubishi tu. Bali hao ni watu wagomvi!”¹

Pia ilinukuliwa na At-Tirmidhi, Ibn Majah na Ibn Jarir. At-Tirmidhi alisema “Hadithi hii ni *Hasan Sahih*, hatuijui, isipokuwa kutokana na Hadithi ya Hajjaj bin Dinar...”²

¹ Ahmad 5:256.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:130, Ibn Majah 1:19, At-Tabari 21:629.

إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliye mneemesha...”

Yaani, ‘Isa عليه السلام, si namna nyingine, bali ni mmojawapo kati ya waja wa Allah تعالى, Amemneemesha kwa Kumpatia Unabii na Utume,

وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥١﴾

“...na Tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israili.”

Yaani, ni dalili, hoja na ushahidi juu ya Uweza Wetu kwa yale Tuyatakayo. Kauli ya Allah تعالى:

وَلَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ مَلَائِكَةً فِي الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ

“Na Tungelipenda Tungeliwafanyia miongoni mwenu Malaika katika ardhi wakifuatana.”

As-Suddi alisema, “Waliichukua sehemu yenu (duniani).”¹ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na Qatadah walisema, “Wangelifuatana kama mnavyofuatana nyinyi kwa nyinyi.”² Rai hii inalingana na iliyotangulia. Mujahid alisema, “wanaimarisha ardhi badala yenu.”³ Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنَّهُ لَعَلَّمَ لِّلسَّاعَةِ

“Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama.”

Lililo sahihi katika hilo, ni kwamba, makusudio yake ni kule kuja kuteremka kwake kabla ya Siku ya Kiyama. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَإِن مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ^ط

“Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake.” (4:159)

Yaani, kabla ya mauti ya ‘Isa عليه السلام,

¹ At-Tabari 21:631.

² At-Tabari 21:630.

³ At-Tabari 21:630.

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا

“Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.” (4:159)

Maana hii inatiliwa nguvu na kisomo cha awali katika Aya,

(وَإِنَّهُ لَعَلَّمَ لِّلسَّاعَةِ)

(Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama)

Inamaanisha kuja kwake kwa mara ya pili kuwa ishara na dalili za kukaribia kwa Saa. Mujahid alisema,

وَإِنَّهُ لَعَلَّمَ لِّلسَّاعَةِ

“Na kwa hakika yeye ni alama ya Saa ya Kiyama.”

Maana yake, “Mojawapo ya ishara na dalili za Kiyama ni kuja tena kwa Nabii Isa mwana wa Maryam عليه السلام, kabla ya Siku ya Kiyama.”¹

Hivi ndivyo alivyosimulia Abu Hurayrah, Ibn ‘Abbas, Abu Al-‘Aliyah, Abu Malik, ‘Ikrimah, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine رضي الله عنهم.²

Hadithi nyingi *Mutawaatir* zimekuja kutoka kwa Mtume ﷺ zikieleza kwamba yeye alieleza juu ya kuteremka kwa ‘Isa عليه السلام kabla ya Siku ya Kiyama, akiwa kiongozi na hakimumuadilifu. Kauli ya Allah تعالى,

فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا

“Basi usiitilie shaka...”

Yaani: msiitilie mashaka juu ya kutukia kwake, kwani kipo na hakina budi.

وَأَتَّبِعُونَ

“...na nifuateni.”

Yaani, katika niliyokujulisheni,

¹ At-Tabari 21:632.

² At-Tabari 21:632; Al-Qurtubi 16:106.

هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٥﴾ وَلَا يَصُدُّكُمْ الشَّيْطَانُ ط

“Hii ndiyo Njia Iliyonyooka. Wala asikuzuilieni Shetani.”

Inamaanisha, dhidi ya kuufuata ukweli,

إِنَّهُ لَكُمُّرٌ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٤﴾ وَلَمَّا جَاءَ عِيسَى بِالْبَيِّنَاتِ قَالَ قَدْ جِئْتُكُمْ بِالْحِكْمَةِ

“Hakika yeye ni adui yenu wa dhaahiri. Na alipokuja Isa na dalili zilizowazi, alisema: Nimekujieni na hikima...”

Maana yake, Utume,

وَلَا بُيِّنَ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي تَخْتَلِفُونَ فِيهِ ط

“...na ili nikuelezeni baadhi ya yale mliyokhitalifiana.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Maana yake, katika mambo ya dini, si ya dunia.”¹ Maneno haya aliyoyasema ni mazuri sana.

فَاتَّقُوا اللَّهَ

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu...”

Katika Aliyokuamrisheni,

وَأَطِيعُوا

“...na mnitii mimi.”

Katika niliyokuleteeni,

إِنَّ اللَّهَ هُوَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٦﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mola Wangu Mlezi, na ni Mola Wenu Mlezi. Basi Muabuduni Yeye tu. Hii ndiyo njia iliyonyooka.”

Maana yake, mimi na nyinyi ni waja Wake, tuna haja Kwake, tunashirikiana katika kumuabudu Yeye, Asiye na mshirika,

¹ At-Tabari 21:635.

هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ

Hii ndiyo Njia Iliyonyooka.

Yaani, niliyokuleteeni ndiyo njia iliyonyooka, nayo ni kumwabudu Allah تعالیٰ Peke Yake. Kauli ya Allah تعالیٰ:

فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ

“Lakini makundi kwa makundi yao yalikhitalifiana wao kwa wao.”

Yaani, makundi yaligawanyika na kuwa vikundi vikundi. Baadhi yao husema kwamba yeye ni mja na Mjumbe wa Allah – ambao ndio ukweli – baadhi yao wanadai kuwa ni mwana wa Allah, na baadhi yao wanasema kuwa yeye ndiye Allah – Allah تعالیٰ ni, Mwenye Utukufu Mkubwa sana Ameepukana na haya. Kwa ajili hii, Allah تعالیٰ Amesema:

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ عَذَابِ يَوْمِ أَلِيمٍ

“Ole wao waliodhulumu kwa adhabu ya siku chungu.”

* * *

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا
 يَشْعُرُونَ ﴿٦٦﴾ إِلَّا خَلَاءَ يَوْمٍ مِنْ بَعْضِهِمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ
 إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿٦٧﴾ يَعْجَادُ لَا خَوْفَ عَلَيْكُمْ الْيَوْمَ وَلَا
 أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٦٨﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا
 مُسْلِمِينَ ﴿٦٩﴾ أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ أَنتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ تُخْبَرُونَ
 يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِصِحَافٍ مِنْ ذَهَبٍ وَأَكْوَابٍ ۗ وَفِيهَا مَا
 تَشْتَهُ مِنَ الْأَنْفُسِ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ۗ وَأَنتُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٧٠﴾
 وَتِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾
 لَكُمْ فِيهَا فَاكِهَةٌ كَثِيرَةٌ مِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾ إِنَّ
 الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿٧٣﴾ لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ
 وَهُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٧٤﴾ وَمَا ظَلَمْتَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا هُمْ
 الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾ وَنَادُوا يَمْلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رَبُّكَ قَالَ
 إِنَّكُمْ مُنْكَرُونَ ﴿٧٦﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ بِالْحَقِّ وَلَكِنْ أَكْثَرْتُمْ
 لِلْحَقِّ كِبْرَهُونَ ﴿٧٧﴾ أَمْ أَبْرَمُوا أَمْرًا فَإِنَّا مُبْرِمُونَ ﴿٧٨﴾ أَمْ
 يَحْسَبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ ۗ بَلَىٰ وَرُسُلْنَا لَدَيْهِمْ
 يَكْتُبُونَ ﴿٧٩﴾

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٦﴾
 إِلَّا خَلَاءَ يَوْمٍ مِنْ بَعْضِهِمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿٦٧﴾
 يَعْجَادُ لَا خَوْفَ عَلَيْكُمْ الْيَوْمَ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٦٨﴾
 الَّذِينَ ءَامَنُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿٦٩﴾
 أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ أَنتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ تُخْبَرُونَ يُطَافُ عَلَيْهِمْ
 بِصِحَافٍ مِنْ ذَهَبٍ وَأَكْوَابٍ ۗ وَفِيهَا مَا تَشْتَهُ مِنَ الْأَنْفُسِ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ۗ
 وَأَنتُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٧٠﴾ وَتِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنتُمْ
 تَعْمَلُونَ ﴿٧١﴾ لَكُمْ فِيهَا فَاكِهَةٌ كَثِيرَةٌ مِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾
 إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿٧٣﴾ لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ
 وَهُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٧٤﴾ وَمَا ظَلَمْتَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا هُمْ
 الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾ وَنَادُوا يَمْلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رَبُّكَ قَالَ إِنَّكُمْ مُنْكَرُونَ ﴿٧٦﴾
 لَقَدْ جِئْتُمْ بِالْحَقِّ وَلَكِنْ أَكْثَرْتُمْ لِلْحَقِّ كِبْرَهُونَ ﴿٧٧﴾ أَمْ أَبْرَمُوا أَمْرًا
 فَإِنَّا مُبْرِمُونَ ﴿٧٨﴾ أَمْ يَحْسَبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ ۗ بَلَىٰ
 وَرُسُلْنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ ﴿٧٩﴾

66. "Je! Nini wanangojea ila

Kiama kiwajie kwa ghafla na wala wao hawatambui?"

67. "Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipo kuwa wachamungu."

68. "Enyi waja Wangu! Hamtakuwa na khofu siku hiyo, wala hamtahuzunika."

69. "Ambao waliziamini Aya Zetu na walikuwa Waislamu."

70. *"Ingieni Peponi, nyinyi na wake zenu; mtafurahishwa humo."*

71. *"Watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu na vikombe; na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele."*

72. *"Na hiyo ni Pepo mliyorthishwa kwa hayo mliyokuwa mkiyafanya."*

73. *"Mnayo humo matunda mengi mtakayoyala."*

Kiyama Kitakuja Ghafla, na Kutatokea Uadui Baina ya Marafiki Vipenzi Miongoni mwa Makafiri:

Allah تعالیٰ Anasema, Je hao washirikina wakadhibishaji wanangojea Mitume?

إِلَّا السَّاعَةَ أَنْ تَأْتِيَهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ

"...ila Saa iwajie kwa ghafla na wala wao hawatambui?"

Yaani, itatukia bila ya shaka yoyote, na hao watakuwa wameghafilika nayo, pasi na kujiandaa. Itakapokuja, itawafikia wakiwa hawatambui, na watajuta wakati huo lakini majuto hayatawafaa wala kuwakinga dhidi yake.

الْأَخْلَاءَ يَوْمَئِذٍ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ

"Siku hiyo marafiki watakuwa ni maadui, wao kwa wao, isipokuwa wachamungu."

Maana yake, kila urafiki na ushuba kwa ajili ya asiyekuwa Allah تعالیٰ, siku hiyo utageuka kuwa uadui, isipokuwa uliokuwa kwa ajili ya Allah تعالیٰ, utaendelea milele. Haya ni kama Ibrahim عليه السلام alivyowaambia watu wake,

إِنَّمَا أَخَذْتُم مِّن دُونِ اللَّهِ أَوْلِيَانًا مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُم بِبَعْضٍ وَبَلَغَ بَعْضُكُم بَعْضًا وَمَأْوَأَتُكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُم مِّن نَّاصِرِينَ

"Hakika nyinyi mmeyafanya masanamu miungu badala ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yaliyo baina yenu katika uhai wa duniani. Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na

mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi. Na makaazi yenu ni Motoni. Wala hamtapata wa kukunusuruni.” (29:25)

Bishara kwa Wachamungu Siku ya Kiyama, na Kuingia kwao Peponi

Kauli ya Allah تعالى:

يَعْبَادِ لَا خَوْفَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ

“Enyi waja wangu! Hamtakuwa na khofu siku hiyo, wala hamtahuzunika.”

Kisha akawapa bishara kwa kusema:

الَّذِينَ ءَامَنُوا بِقَايَتِنَا وَكَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿٦٦﴾

“Ambao waliziamini Ishara Zetu na walikuwa Waislamu.”

Yaani, nyoyo zao ziliamini na viungo vyao vikafuata sheria ya Allah تعالى. Al-Mu'tamar bin Sulayman alisema kuwa baba yake alieleza: “Itakapofika Siku ya Kiyama, pindi watakapofufuliwa, hatasalia yeyote, bali ataingiwa na khofu.” Kisha mwenye kunadi atanadi:

يَعْبَادِ لَا خَوْفَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ وَلَا أَنتُمْ تَحْزَنُونَ ﴿٦٧﴾

“Enyi waja Wangu! Hamtakuwa na khofu siku hiyo, wala hamtahuzunika.”

Kwa hivyo, watu wote watakuwa na matumaini. Haya yatafuatiwa na maneno mengine,

الَّذِينَ ءَامَنُوا بِقَايَتِنَا وَكَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿٦٨﴾

“Ambao waliziamini Ishara Zangu na walikuwa Waislamu.”

“Hapo watu kwa kauli hiyo watakata tamaa, isipokuwa Waumini.”¹

أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ

“Ingieni Peponi...” Wataambiwa,

¹ At-Tabari 21:639.

أَنْتُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ

“...nyinyi na wake zenu...”

Maana yake, wenzenu,

تُخْبِرُونَ

“...mtafurahishwa humo.”

Yaani, mnastarehe na kuneemeka.

Tafsiri yake imetangulia katika Surat Ar-Rum.

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِصِحَافٍ مِّنْ ذَهَبٍ وَأَكْوَابٍ

“Watakuwa wanapitishiwa sahani za dhahabu...”

Maana yake, zaidi ya hayo, kuna vyombo vya chakula vya dhahabu visivyokuwa na kamba wala vishikio,

(وَفِيهَا مَا تَشْتَهِي الْأَنْفُسُ)

(na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda)

Baadhi yao walisoma,

مَا تَشْتَهِيهِ الْأَنْفُسُ

“...ambavyo nafsi zinavipenda...”

وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ

“...na macho yanavifurahia ...”

Yaani, chakula kizuri, harufu na mandhari nzuri.

وَأَنْتُمْ فِيهَا

“...nanyi humo...” Yaani, Peponi,

خَالِدُونَ

“...mtakaa milele...” Inamaanisha hamtatoka wala kutaka kubadilishiwa.

Halafu wataambiwa kwa namna ya kufadhilishwa neema na kuzingatiwa: Kauli ya Allah تعالى،

وَتِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾

“Na hiyo ni Pepo mliyarithishwa kwa hayo mliyokuwa mkiyafanya.”

Yaani, amali zenu njema zimekuwa sababu ya kukusanyiwa kwenu Rehema za Allah تعالى، kwani hapana atakayeingia Peponi kutokana na amali zake, bali ni kwa rehema na Fadhila za Allah تعالى. Lakini, daraja hupatikana na kutofautiana kulingana na amali njema.

لَكُمْ فِيهَا فَاكِهَةٌ كَثِيرَةٌ

“Mnayo humo matunda mengi...”

Yaani, ya namna mbali mbali،

مِنْهَا تَأْكُلُونَ

“...mtakayo yala.”

Inamaanisha, pindi watakapoyahitaji. Baada ya kutaja chakula na vinywaji, Amefuatishia matunda ili neema na furaha itimie. Allah ni Mjuzi Zaidi

إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ مُّهِينٍ ﴿٦٧﴾ لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ وَهُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٦٨﴾
 وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا هُمُ الظَّالِمِينَ ﴿٦٩﴾ وَنَادَوْا بِمَمْلِكٍ لِّيَقْضِيَ عَلَيْنَا رَبُّكَ ۗ قَالَ
 إِنَّكُمْ مُّكْتَبُونَ ﴿٧٠﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ بِالْحَقِّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَكُمْ لِلْحَقِّ كَرِهُونَ ﴿٧١﴾ أَمْ
 أَبْرَمُوا أَمْرًا فَإِنَّا مُبْرِمُونَ ﴿٧٢﴾ أَمْ يَحْسَبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ ۗ بَلَىٰ وَرُسُلْنَا
 لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ ﴿٧٣﴾

74. “Kwa hakika waovu watakaa katika adhabu ya Jahannamu.”

75. “Hawatapumzishwa nayo na humo watakata tamaa.”

76. “Wala Sisi hatukuwadhulumu, bali wao ndio waliokuwa madhaalimu.”

77. ***“Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik! Na Atufishe Mola Wako Mlezi! Naye aseme: Hakika nyinyi mtakaa humo humo!”***

78. ***“Kwa yakini Tulikuleteeni Haki, lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia Haki.”***

79. ***“Au waliweza kupitisha amri yao? Bali ni Sisi ndio Tunaopitisha.”***

80. ***“Au wanadhani kwamba hatusikii siri zao na minong’ono yao? Wapi! Na wajumbe Wetu wapo karibu nao, wanayaandika.”***

Mwisho Mbaya wa Waovu

Baada ya kutaja hali za waja wema, Allah تعالى Alifuatishia kwa kuwataja wakosefu. Alisema:

إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي عَذَابٍ جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿٧٦﴾ لَا يُفْتَرُ عَنْهُمْ

“Kwa hakika wakosefu watakaa katika adhabu ya Jahannamu. Hawatapumzishwa nayo...”

Hata kwa saa moja,

وَهُمْ فِيهِ مُتَبَسِّئُونَ

“...na humo watakata tamaa.”

Dhidi ya kheri zote,

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا هُمُ الظَّالِمِينَ ﴿٧٧﴾

“Wala Sisi Hatukuwadhulumu, bali wao ndio waliokuwa madhaalimu.”

Kwa amali zao mbaya baada ya kusimamishiwa hoja dhidi yao, na kuwapelekea Mitume, wakakadhibisha na wakakosa utii. Kutokana na hayo wanalipwa jaza inayoendana sawa kabisa na hayo,

وَنَادَوْا يٰمَلِكُ

“Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik!”

Yaani, Mlinzi wa Moto.

Al-Bukhari aliandika: “Swatan bin Ya’alaa amehadithia kutoka kwa baba yake alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisoma juu ya mimbari,

وَنَادُوا يَمْلِكُ لِيَقْضَ عَلَيْنَا رُبُّكَ^ط

“Nao watapiga kelele waseme: Ewe Malik! Na Atufishe Mola Wako Mlezi!”¹

Yaani, Azitoe roho zetu ili tupumzike dhidi ya haya tuliyomo. Kwani, wao ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِّنْ عَذَابِهَا^ع

“...hawatahukumiwa kufa, wala hawatapunguziwa adhabu yake.”
(35:36)

وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى^{١١} الَّذِي يَصْلَى النَّارَ الْكُبْرَى^{١٢} ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَى^{١٣}

“Na atajitenga mbali nayo mpotovu, ambaye atauingia Moto mkubwa. Tena humo hatakufa wala hawi hai.” (87:11-13)

Baada ya kumuomba awafishe, Malaika aliwajibu:

قَالَ إِنَّكُمْ مِّنْ كٰثِرُونَ

“Naye aseme: Hakika nyinyi mtakaa humo humo!”

Yaani, humo hamtatoka, wala hapana wa kukukingeni nyinyi dhidi yake. Halafu akataja sababu ya kuadhibiwa kwao. Nayo ni kule kuukhalifu kwao ukweli na kuupinga. Kwa hivyo Amesema:

لَقَدْ جِئْتَكُمْ بِالْحَقِّ

“Kwa yakini Tulikuleteeni Haki...”

Kwamba, Tuliibainisha, Tukaitafsiri na Kuifafanua,

¹ Fat'h Al-Bari 8:431.

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرُكُمْ لِلْحَقِّ كَرَهُونَ

“...lakini wengi katika nyinyi mlikuwa mnaichukia Haki.”

Maana yake, lakini desturi yenu ilikuwa ni kutokuikubali na kutoifuata, mkaufuata ubatilifu na kuutukuza, mnazuia haki na kuikataa, na mnawachukia wenye kuifuata. Kwa hivyo jilaumuni nyinyi wenyewe, na mjute majuto yasiyokunufaisheni. Halafu, Allah تعالى Alisema:

أَمْ أُبْرِمُوا أَمْرًا فَإِنَّا مُبْرِمُونَ ﴿٦٦﴾

“Au waliweza kupitisha amri yao? Bali ni Sisi ndio Tunaopitisha.”

Mujahid alisema, “Walitaka kupanga njama, lakini Sisi pia Tunapanga.”¹ Kauli hii ya Mujahid ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَمَكْرُؤًا مَكَرًا وَمَكْرَتَنَا مَكَرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٧﴾

“Basi wakapanga mipango yao, na Sisi Tukapanga mipango Yetu, na wao hawatambui.” (27:50)

Hayo, ni kwa sababu washirikina walikuwa wakifanya njama za kuukataa ukweli, lakini Allah تعالى Naye, Alipanga ili waliyoyapanga yawarudie wao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

أَمْ نَحْسَبُونَ أَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ^٤

“Au wanadhani kwamba hatusikii siri zao na minong’ono yao?”

Yaani, Yale wanayofanya siri na yale wanayodhihirisha.

بَلَىٰ وَرُسُلْنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُونَ

“Wapi! Na wajumbe Wetu wapo karibu nao, wanayaandika.”

Yaani, Sisi Tunayajua yale waliyomo wao na Malaika nao wanaziandika amali zao zote, ndogo na kubwa.

* * *

¹ At-Tabari 21:146.

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِينَ ﴿٨١﴾ سُبْحَانَ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٨٢﴾ فَذَرَهُمْ مَخْضُوضًا وَيَلْعَبُوا حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٨٣﴾ وَهُوَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ إِلَهٌُ وَفِي الْأَرْضِ إِلَهٌُ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٨٤﴾ وَتَبَارَكَ الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَعِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٥﴾ وَلَا يَمْلِكُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ الشَّفَعَةَ إِلَّا مَنْ شَهِدَ بِالْحَقِّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٨٦﴾ وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۗ فَأَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٨٧﴾ وَقِيلَ لَهُمْ يَرْبِّ إِنَّ هَؤُلَاءِ قَوْمٌ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾ فَاصْفَحْ عَنْهُمْ وَقُلْ سَلِّمْ ۖ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٨٩﴾

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِينَ ﴿٨١﴾ سُبْحَانَ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٨٢﴾ فَذَرَهُمْ مَخْضُوضًا وَيَلْعَبُوا حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٨٣﴾ وَهُوَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ إِلَهٌُ وَفِي الْأَرْضِ إِلَهٌُ وَهُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٨٤﴾ وَتَبَارَكَ الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَعِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٥﴾ وَلَا يَمْلِكُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ

الشَّفَعَةَ إِلَّا مَنْ شَهِدَ بِالْحَقِّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٨٦﴾ وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۗ فَأَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٨٧﴾ وَقِيلَ لَهُمْ يَرْبِّ إِنَّ هَؤُلَاءِ قَوْمٌ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٨٨﴾ فَاصْفَحْ عَنْهُمْ وَقُلْ سَلِّمْ ۖ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٨٩﴾

81. "Sema: Ingelikuwa Mwingi wa Rehema Ana mwana, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu."

82. "Ametakasika Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, Mola Mlezi wa Arshi, na hayo wanayomsifia."

83. "Basi waache wapige porojo wakicheza mpaka wakutwe na hiyo siku yao waliyoahidiwa."

84. "Na Yeye Ndiye Mungu mbinguni, na Ndiye Mungu katika ardhi. Naye Ndiye Mwenye Hikima, Mwenye Ujuzi."

85. *“Na Ametukuka Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo ndani yake. Na uko Kwake Ujuzi wa Saa ya Kiyama, na Kwake Yeye mtarudishwa.”*

86. *“Wala hao mnaowaomba badala yake Yeye hawana uweza wa kumuomba mtu, isipokuwa anayeshuhudia kwa haki, na wao wanajua.”*

87. *“Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu! Basi ni wapi wanakogeuziwa?”*

88. *“Na usemi wake (Mtume) ni: Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasioamini.”*

89. *“Basi wasamehe, na uwambie maneno ya salama. Watakuja jua.”*

Allah تعالیٰ Hana Mtoto

Allah تعالیٰ Anasema:

قُلْ

“Sema...” Ewe Muhammad!

إِنْ كَانَ لِلرَّحْمَنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعَبِيدِ

“Ingeli kuwa Rahmani Ana mwana, basi mimi ningelikuwa wa kwanza kumuabudu.”

Yaani, lau haya yangelifaradhihwa, mimi ningelimuabudu juu ya hilo, kwani mimi ni mmojawapo katika waja Wake, ninayatii yote Anayoniamuru. Mimi sina kiburi wala majivuno ya kukataa ibada Yake. Lau Angelimuru hayo, ningeliyafuata, lakini hili limezuilika katika haki ya Allah تعالیٰ. Hata hivyo, kuwepo kwa sharti hakulazimishi kutukia wala kujuzu kwake. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالیٰ:

لَوْ أَرَادَ اللَّهُ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا لَأَصْطَفَىٰ مِمَّا خَلَقَ مَا يَشَاءُ ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٤﴾

“Lau kuwa Mwenyezi Mungu Angelitaka kuwa na mwana, basi bila ya shaka Angelimchagua Amtakaye katika Aliowaumba. Subhanahu, Ametakasika na hayo! Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtenda Atakalo.” (39:4)

Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

سُبْحَانَ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٨٦﴾

“Ametakasika Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, Mola Mlezi wa Arshi, na hayo wanayo msifia.”

Yaani, Mtukufu, Mtakatifu na Ameepukana Muumbaji dhidi ya kuwa na mwana. Yeye ni Peke Yake, Mmoja, Mkusudiwa, Hana aliye mfano Wake wala mwenye kulingana Naye. Hivyo, Hana mwana. Kauli ya Allah تعالى:

فَذَرَهُمْ خَوْضًا

“Basi waache wapige porojo...” Katika ujinga na upotevu wao,

وَيَلْعَبُوا

“...wakicheza...” Katika dunia hii,

حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي يُوعَدُونَ

“...mpaka wakutwe na hiyo siku yao waliyohidiwa.”

Hiyo ni Siku ya Kiyama, yaani, hivi karibuni watajua utakavyokuwa mwisho wao, makazi yao na hali zao.

Ubainifu wa Upekee wa Mola Mlezi

Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي فِي السَّمَاءِ إِلَهٌُ وَفِي الْأَرْضِ إِلَهٌُ ۗ

“Na Yeye Ndiye Mungu mbinguni, na Ndiye Mungu katika ardhi.”

Yaani, Yeye ni Mola Mlezi wa walio mbinguni na Mola Mlezi wa walio ardhini, wakazi wa sehemu hizo mbili wanamuabudu Yeye, na wote ni wanyenyekevu Kwake, tena ni dhalili mbele Yake,

وَهُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ

“Naye Ndiye Mwenye Hikima, Mwenye Ujuzi.” Aya hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

وَهُوَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَفِي الْأَرْضِ يَعْلَمُ سِرِّكُمْ وَجَهْرَكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُونَ ﴿٨١﴾

“Na Yeye Ndiye Mwenyezi Mungu mbinguni na ardhini. Anajua ya ndani yenu na ya nje yenu. Na Anajua mnayoyachuma.” (6:3)

Maana yake, Yeye Ndiye Anayelitwa Allah تعالى huko mbinguni na ardhini,

وَتَبَارَكَ الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا

“Na Ametukuka Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na viliomo ndani yake.”

Yaani, Yeye Ndiye Muumbaji na Mmiliki wa hivyo, pia ni Mwenye Kuvidhibiti pasi na wa kumpinga wala kumzuia. Utakasifu na Utukufu ni Wake kwa kutokuwa na mwana, na Ametakasika dhidi ya mambo ya aibu na nuksani, kwa sababu Yeye ni Mola Mlezi, Mtukufu, Adhimu, Mmiliki wa vitu vyote, ambaye, Mkononi Mwake kuna udhibiti wa mambo yote, kwa Kubatilisha na Kuidhinisha.

وَعِنْدَهُ عِلْمُ السَّاعَةِ

“Na uko Kwake ujuzi wa Saa ya Kiyama...”

Yaani, hapana ajuaye kitasimama lini, isipokuwa Yeye tu Peke Yake,

وَالِيهِ تُرْجَعُونَ

“...na Kwake Yeye mtarudishwa.”

Na kila mmoja atalipwa kulingana na amali zake, ikiwa ni njema, basi ni kheri kwake, na kama ni mbaya, basi ni hasara kwake.

Masanamu Hayana Uwezo wa Nguvu ya Maombezi

Kisha, Allah تعالى Alisema:

وَلَا يَمْلِكُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ

“Wala hao mnaowaomba badala Yake Yeye hawana uweza...”

Yaani, hayo masanamu na miungu hiyo ya bandia,

الشَّفَعَةَ

“...wa kumuomba mtu...”

Maana yake, hawawezi kuwaomba,

إِلَّا مَنْ شَهِدَ بِالْحَقِّ وَهُمْ يَعْلَمُونَ

“...isipokuwa anayeshuhudia kwa haki, na wao wanajua.”

Inamaanisha, lakini mwenye kuushuhudia ukweli ana uoni na ujuzi, kwa hivyo, uombezi wake utafanyika kwa ruhusa Yake.

Washirikina Wanakiri Upweke wa Allah تعالی katika Uumbaji.

Allah تعالی Anasema:

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَن خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ فَأَنَّى يُؤْفَكُونَ

“Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu! Basi ni wapi wanakogeziwa?”

Yaani, na kama utawauliza hawa wamshirikishao Allah تعالی, na wanamuabudu pamoja na wasiokuwa Yeye,

مَن خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

“Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu!”

Maana yake, wanakiri kwamba Yeye Ndiye Muumba wa vitu vyote, Yu Mpweke hana mshirika. Pamoja na haya, wanaviabudu pamoja Naye vingine ambavyo havimiliki chochote, wala havina uwezo wa chochote. Wao katika hayo, wako katika upeo wa ujinga, upumbavu na ukosefu wa busara.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

فَأَنَّى يُؤْفَكُونَ

“Basi ni wapi wanakogeziwa?”

Malalamiko ya Mtume ﷺ kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Anasema:

وَقِيلَ يَا رَبِّ إِنَّ هَذَا قَوْمٌ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٨١﴾

“Na usemi wake (Mtume) ni: Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasioamini.”

Yaani, Mtume Muhammad ﷺ alitoa kauli yake, maana yake, alishitakia kwa Mola Wake juu ya watu waliomkanusha katika kaumu yake. Alisema:

وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا ﴿٨٢﴾

“Na Mtume alikuwa akisema: Ee Mola Wangu Mlezi! Hakika watu wangu wameifanya Qur’ani hii ni kitu kilichohamwa.” (25:30)

Hili tulilolisema ni kauli ya Ibn Mas’ud, Mujahid na Qatadah رضي الله عنهم, na hivi ndivyo Ibn Jarir رحمه الله تعالى alivyoitafsiri.¹

Al-Bukhari alisema: “’Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisoma, (Aya ya 88 katika Surat Az-Zukhruf):

(وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ)

(Na Mtume alikuwa akisema: Ee Mola Wangu)²

Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَقِيلَ يَا رَبِّ إِنَّ هَذَا قَوْمٌ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٨١﴾

“Na usemi wake (Mtume) ni: Ewe Mola Wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasioamini.”

Allah تعالى Anaeleza aliyoyasema Muhammad ﷺ.³ Qatadah alisema: “Haya ni maneno ya Mtume wenu anawashitaki watu kwa Mola Wake Mlezi.”⁴

¹ At-Tabari 21:656.

² At-Tabari 21:656.

³ Fat’h Al-Bari 8:431.

⁴ At-Tabari 21:656.

Kauli ya Allah تعالى:

فَأَصْفَحْ عَنْهُمْ

“Basi wasamehe...” Washirikina,

وَقُلْ سَلَامٌ

“...na uwambie maneno ya salama.”

Yaani, usijibizane nao kama wanavyokuambia maneno mabaya, bali lainisha nyoyo zao na uwasamehe kwa vitendo na kauli.

فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ

“Watakuja jua.”

Hili ni tishio la Allah تعالى kwao. Kwa ajili hii, Allah تعالى Aliihalalisha Adhabu Yake kwao, ambayo haiwezi kuondolewa, na Akainyayua Dini na Neno Lake. Baada ya hapo Akaifaradhisha Jihadi na uvumilivu, mpaka watu wakaingia katika Dini ya Allah تعالى kwa makundi, na Uislamu ukaenea mpaka Mashariki na Magharibi. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Az-Zukhruf*.

* * *

Tafsiri ya Suratu Ad-Dukhan

Sura ya 44

Iliteremshwa Makkah

Fadhila za Suratu Ad-Dukhan

Katika *Musnad* wa *Al-Bazzar*, kutokana na masi mulizi ya Abu Tufail 'Amir Bin Waathilah, toka kwa Zaydu bin Haarithah, Mtume ﷺ alimuambia Ibn Swayyaad,

«إِنِّي قَدْ خَبَأْتُ خَبَاءً فَمَا هُوَ؟»

“Mimi Nimeficha kitu, ni kitu gani?”

Mtume ﷺ alimfichia Surat Ad-Dukhan.

Akajibu: “Ni *Ad-Dukh*.” Mtume ﷺ akasema:

«اِخْسَاءَ مَا شَاءَ اللهُ [كَانَ]»

“Acha! Chochote Allah Akitakacho huwa.”¹

* * *

¹ At-Tabarani 5:88, kuna udhaifu katika masimulizi haya.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الدُّخَانِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

حَمِّ ۝ وَالْكِتَابِ الْمُمِينِ ۝ إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ مُبَرَّكَةٍ ۝ إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ ۝ فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ ۝ أَمْرًا مِّنْ عِنْدِنَا ۝ إِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ ۝ رَحْمَةً مِّنْ رَبِّكَ ۝ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۝ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۝ إِن كُنْتُمْ مُوقِنِينَ ۝ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ۝ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ يَلْعَبُونَ ۝ فَارْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُحَانٍ مُّبِينٍ ۝ يَغْشى النَّاسُ هَذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ۝ رَبَّنَا اكْشِفْ عَنَّا الْعَذَابَ إِنَّا مُؤْمِنُونَ ۝ أَنَّى لَهُمُ الذِّكْرَى وَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مُّبِينٌ ۝ ثُمَّ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوا مُعَلَّمٌ مَّجْنُونٌ ۝ إِنَّا كَاشِفُو الْعَذَابِ قَلِيلًا ۝ إِنَّكُمْ عَائِدُونَ ۝ يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَى ۝ إِنَّا مُنْتَقِمُونَ ۝

حَمِّ ۝ وَالْكِتَابِ الْمُمِينِ ۝ إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ مُبَرَّكَةٍ ۝ إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ ۝ فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ ۝ أَمْرًا مِّنْ عِنْدِنَا ۝ إِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ ۝ رَحْمَةً مِّنْ رَبِّكَ ۝ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۝ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۝ إِن كُنْتُمْ مُوقِنِينَ ۝ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأُولِينَ ۝ بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ يَلْعَبُونَ ۝

1. "H'a Mim."

2. "Naapa kwa Kitabu kina-chobainisha,"

3. "Hakika Tumekite-remsha katika usiku uliobari-rikiwa. Hakika Sisi ni Waonyaji."

4. "Katika usiku huu hubainishwa kila jambo la hikima,"

5. "Jambo litokalo Kwetu. Hakika Sisi ndio wenye kutuma."

6. ***“Ni rehema itokayo kwa Mola Wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.”***

7. ***“Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao, ikiwa nyinyi mna yakini.”***

8. ***“Hakuna mungu ila Yeye; Anahuisha na Anafisha - Mola Mlezi Wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa mwanzo.”***

9. ***“Lakini wao wanacheza katika shaka.”***

Qur’an Iliteremshwa katika Usiku Wenye Cheo

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa Aliiteremsha Qur’an Tukufu katika usiku uliobarikiwa, Laylatul-Qadr. Ni sawa na Kauli Yake nyingine:

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ﴿٩٧﴾

“Hakika Sisi Tumeiteremsha Qur’ani katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu.” (97:1)

Hilo lilikuwa ni katika mwezi wa Ramadhani. Ni sawa na Kauli nyingine,,

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ

“Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur’ani...” (2:185)

Tumekwisha taja Hadithi juu ya jambo hilo katika Surat Al-Baqarah, kiasi cha kutosha, hivyo hakuna haja ya kurudia tena. Kauli ya Allah تعالیٰ:

إِنَّا كُنَّا مُنذِرِينَ

“Hakika Sisi ni Waonyaji.”

Yaani, wenye kuwajulisha watu kuhusu yanayowanufaisha na yanayowadhuru, kisheria, ili hoja isimame juu ya waja Wake.

فِيهَا يُفْرَقُ كُلُّ أَمْرٍ حَكِيمٍ ﴿٩٨﴾

“Katika usiku huu hubainishwa kila jambo la hikima.”

Yaani, katika *Laylatul-Qadr*, Kudura huhamishwa kutoka katika *Al-Lawh Al-Mahfudh* (Ubao uliohifadhiwa) kwenda kwa (Malaika) waandishi ambao huandika Kudura (zizazo) pamoja na umri, riziki na matukio ya mwaka mzima yatakayojiri. Hivi ndivyo pia, alivyosimulia Ibn 'Umar, Mujahid, Abu Malik, Adh-Dhahhak na *Salaf* wengine zaidi ya mmoja رضي الله عنهم.¹

حَكِيمٍ

“...la hikima.”

Maana yake, limezatitiwa, halitabadilishwa wala kugeuzwa. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

أَمْرًا مِّنْ عِنْدِنَا

“Jambo litokalo Kwetu.”

Yaani, yote yanayotukia ni kwa Kudura ya Allah تعالى na Anayoyafunulia Wahyi, ni kutokana na Amri, Idhini na Ilimu Yake.

إِنَّا كُنَّا مُرْسِلِينَ

“Hakika Sisi Ndio Wenye Kutuma.”

Yaani, wajumbe kwenda kwa watu, wanaowasomea Aya za Allah تعالى zenye kubainisha. Haja ya kufanya hivyo ilikuwa kubwa. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٠﴾ رَبِّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ط

“Ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilio baina yao...”

Yaani, Aliyeiteremsha Qur'an Ndiye Mola, Muumbaji na Mmiliki wa mbingu na ardhi na vilivyo baina ya hivyo viwili,

إِن كُنْتُمْ مُّوقِنِينَ

“...ikiwa nyinyi mna yakini.”

¹ At-Tabari 22:9.

Kisha, Allah تعالى Akasema:

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦﴾

“Hakuna mungu ila Yeye; Anahuisha na Anafisha - Mola Mlezi Wenu na Mola Mlezi wa baba zenu wa mwanzo.”

Aya hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قُلْ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mungu ila Yeye Anayehuisha na Anayefisha.”
(7:158)

بَلْ هُمْ فِي شَكٍّ يَلْعَبُونَ ﴿١٧﴾ فَأَرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُحَانٍ مُّبِينٍ ﴿١٨﴾
يَغْشَى النَّاسَ هَذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٩﴾ رَبَّنَا اكْشِفْ عَنَّا الْعَذَابَ إِنَّا مُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾
أَنِي لَهُمُ الدِّكْرَىٰ وَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مُّبِينٌ ﴿٢١﴾ ثُمَّ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوا مُعَلِّمٌ مِّثْلُ نَحْنُونَ ﴿٢٢﴾
﴿٢٣﴾ إِنَّا كَاشِفُو الْعَذَابِ قَلِيلًا ۖ إِنَّكُمْ عَائِدُونَ ﴿٢٤﴾ يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَىٰ
﴿٢٥﴾ إِنَّا مُنْتَقِمُونَ ﴿٢٦﴾

9. ***“Lakini wao wamo katika shaka wanacheza tu.”***

10. ***“Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhaahiri,”***

11. ***“Utakaowafunika watu: Hii ni adhabu chungu!”***

12. ***“Mola Wetu Mlezi! Tuondolee adhabu hii. Hakika tutaamini.”***

13. ***“Nini faida ya kukumbuka kwao? Na alikwishawafikia Mtume mwenye kubainisha.”***

14. *“Na wao wakamgeuzia uso, na wakasema: Huyu amefunzwa, naye ni mwendawazimu.”*

15. *“Hakika sisi Tutaiondoa adhabu kidogo, lakini nyinyi kwa yakini mtarejea vile vile!”*

16. *“Siku Tutayoyashambulia mashambulio makubwa, bila ya shaka Sisi ni wenye kutesa.”*

Kuwakhofisha Washirikina Kwa Siku Ambayo Mbingu Zitaleta Moshi

Allah تعالى Anasema: Bali hawa washirikina, “wanacheza katika shaka.” Yaani, ukweli wa uhakika umewafikia, lakini wanautilia shaka na wanashindana wala hawausadiki. Kisha, Allah تعالى Aliwapa ahadi na Kuwatishia kwa Kusema:

فَأَرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ

“Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhaahiri.”

Masruq alieleza: “Tuliingia msikiti wa Kufa kupitia milango ya Kindah, tukamkuta mtu mmoja akiwasomea wenzake,

يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ

“...siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhaahiri...”

Akawauliza, ‘Mnaujua moshi? Moshi huo utakuja Siku ya Kiyama na kuondosha usikivu na uonaji wa washirikina, na Waumini watapatwa na mfano wa mafua.’ Tukamjia Ibnu Mas’ud رضي الله عنه, tukamtajia hayo. Wakati huo alikuwa amelala kibavu, akagutuka na kukaa. Akasema: ‘Allah تعالى Alimuambia Mtume wenu ﷺ:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ ﴿٨٦﴾

“Sema (Ewe Mtume) : Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.” (38:86)

Pia ni sehemu ya elimu ambayo pindi mwanaadamu anapokuwa hafahamu jambo, aseme, ‘Allah A`alam.’ Nitakutajieni nyinyi Hadithi inayozungumzia jambo hilo. Wakati Makureishi walipoukataa Uislamu na kuwa wakaidi, Mtume ﷺ aliwaapiza kwa ukame kama ule wa kipindi cha Nabii Yusuf عليه السلام.

Wakapata taabu na njaa kali mpaka wakala mifupa na mizoga. Wakawa wanatazama juu angani na hawakuona chochote zaidi ya moshi."¹

Katika masimulizi mengine: "Mtu aliweza kuangalia angani na hakuweza kuona kitu baina yake na anga isipokuwa ukungu, kwa sababu ya taabu."

فَأَرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ ﴿٤٤﴾ يَغْشَى النَّاسَ هَذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٥﴾

"Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhaahiri. Utakaowafunika watu: Hii ni adhabu chungu!"

Mtume ﷺ akajiwa na kuambiwa: "Ewe Mjumbe wa Allah! Waombe Mvua wa Mwenyezi Mungu inyeshe kwani wamepatwa na maafa." Mtume ﷺ akawaombea mvua, na wakanyeshewa mvua. Ikashuka Aya:

إِنَّا كَاشِفُوكَ الْعَذَابِ قَلِيلًا إِنَّكُمْ عَائِدُونَ ﴿٤٦﴾

"Hakika sisi Tutaiondoa adhabu kidogo, lakini nyinyi kwa yakini mtarejea vile vile!"

Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema: "Unaonaje, wataondolewa adhabu Siku ya Kiyama? Walipopewa faraja, walirejea kwenye hali yao." Allah تعالى Akateremsha Aya:

يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَىٰ إِنَّا مُنتَقِمُونَ ﴿٤٧﴾

"Siku Tutayoyashambulia mashambulio makubwa, bila ya shaka Sisi ni Wenye Kutesa."

Alisema, "Inamaanisha siku ya Badr."² Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasema: "Mambo matano yameshapita: moshi, Warumi (kushindwa), mwezi (kupasuka), adhabu na mauti." Hadithi hii ilinukuliwa ndani ya *Sahih* Mbili.³ Pia ilinukuliwa na Imam Ahmad katika *Musnad* wake, pia na At-Tirmidhi na An-Nasai katika (Vitabu vyao vya) Tafsiri, pia na Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى na idadi kubwa ya isnadi.⁴

¹ Muslim 4:2155

² *Fat'h Al-Bari* 8:434

³ *Fat'h Al-Bari* 8:434. "Adhabu" hapa inakusudia Aya ya mwisho ya SuratAl-Furqan. Angalia maelezo yake katika juzu ya saba, na. 4767 katika Bukhari, na imetajwa tena kwa kifupi.

⁴ Ahmad 1:380 *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:133 An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:455 At-Tabari 22:13, 14.

Maulamaa kadha wa *Salaf*, kama vile Mujahid, Abu Al-'Aliyah, Ibrahim An-Nakha'i, Adh-Dhahhak na 'Atiyyah na Al-'Awfi waliwafikiana na tafsiri ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه juu ya Aya hii na rai yake kwamba moshi tayari umeshatokea.¹ Na huu ni uchaguzi wa Ibn Jarir رحمه الله تعالى.

Mtazamo wa pili wa ufafanuzi kuhusu Moshi (*Ad-Dukhan*), ni kwamba Moshi huo bado haujatokea, kwani Moshi huo ni katika alama ya Qiyama kujiri kwake.

Katika Hadithi ya Abu Sariyah, Hudhaifah bin Asiyad Al-Ghifaari رضي الله عنه alisema: "Mtume ﷺ alituangalia kutoka chumbani, sisi tulipokuwa tukiizungumzia Saa. Mtume ﷺ akasema:

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى تَرَوْا عَشْرَ آيَاتٍ: طُلُوعَ الشَّمْسِ مِنْ مَغْرِبِهَا، وَالذُّخَانَ، وَالذَّابَّةَ، وَخُرُوجَ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ، وَخُرُوجَ عِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَالذِّجَالَ، وَثَلَاثَةَ خُسُوفٍ: خَسْفٍ بِالشَّرْقِ، وَخَسْفٍ بِالمَغْرِبِ، وَخَسْفٍ بِجَزِيرَةِ العَرَبِ، وَنَارًا تَخْرُجُ مِنْ قَعْرِ عَدْنٍ تَسُوقُ النَّاسَ - أَوْ تَحُشِّرُ النَّاسَ - تَبِيثٌ مَعَهُمْ حَيْثُ بَاتُوا، وَتَقْبِيلٌ مَعَهُمْ حَيْثُ قَالُوا»

"Kiyama hakitasimama mpaka muone ishara kumi. Jua kuchomoza kutoka upande wa magharibi yake; moshi; mnyama; kutokea kwa Yajuj na Majuj; kutokea kwa Isa bin Maryam; Ad-Dajjaal; mwezi kupatwa mara tatu; moja upande wa mashariki; mwingine upande wa magharibi; na katika Rasi ya Uarabuni; moto utakaotokea katika sehemu za chini za Aden ambao utawaswaga watu – au utawakusanya – utatulia pamoja nao mahali watakapolala usiku na kupumzika nao, katika nyakati za mchana."

Hii ilinukuliwa na Muslim peke yake, katika *Sahih* yake.²

Katika *Sahih* Mbili kuna Hadithi iliyonukuliwa kwamba Mtume ﷺ alimuambia Ibn Swayyaad:

«إِنِّي خَبَأْتُ لَكَ خَبَاءً»

"Nimekufichia wewe jambo, ni jambo gani?." Akasema: "Ni Ad-Dukh." Mtume ﷺ akasema:

¹ At-Tabari 22:16.

² Muslim 4:2225.

«اِحْسَا فَلَئِنْ تَعُدُّوْا قَدْرَكَ»

“Acha! Hutavuka uwezo wako.” Mtume ﷺ alimficha Aya hii,

فَاَرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُحَانٍ مُّبِينٍ ﴿٤٤﴾

“Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhaahiri.”¹

Hii inaashiria kwamba moshi ni katika alama zinazongojewa kutokea. Ibn Swayyad alikuwa mtabiri ambaye alikuwa akisikia vitu kupitia majini, ambao hawana ufasaha wa maneno. Kwa hivyo alisema *Ad-Dukh*, akimaanisha *Ad-Dukhaan* (moshi). Baada ya Mtume ﷺ kung’amua kuwa chanzo cha maelezo hayo kilikuwa Shetani, alimuambia,

«اِحْسَا فَلَئِنْ تَعُدُّوْا قَدْرَكَ»

“Acha! Hutaweza kwenda zaidi ya kiwango chako.”

Imenukuliwa kutoka kwa Abuu Malik Al-Ash’ari رضى الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema “Hakika Mola wenu Mlezi amewaonya vitu vitatu: Moshi utakaosababisha kwa Muumini mfano wa Mafua, ama kwa Kafiri utaleta madhara makubwa atakamua Pua yake hadi utaondoka usikivu wake. Pili, Mnyama. Tatu, Dajjali. Kadhalika Hadithi hii ameiandika Twabarani, na Isnadi yake ni nzuri. Nakupitia masimulizi kutoka kwa bin Umar رضى الله عنه: “Na Moto huo utapenya katika usikivu wa Kafiri na mnafiki na kukifanya Kichwa kama kilichobanikwa katika moto.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Abdillahi Bin Abuu Mulaika amesema “Nilimuendea bin Abbasi رضى الله عنهما siku moja wakati wa asubuhi, sikupata usingizi usiku wote hadi kumekucha: Nikamuambia, “kwa nini?” “Akasema: “wamesema nyota (sayari) imejitokeza. Hivyo, nikahofia isije ikawa Moshi uliosema umewadia. Hivyo, sikupata usingizi hadi asubuhi.”

Bin Abuu Hatim naye amepokea kama hivyo kutoka kwa baba yake, naye amesimulia kutoka kwa bin Umar رضى الله عنهما, Kutoka kwa Sufiani, kutoka kwa Abdillahi bin Abuu Yazidi, kutoka kwa Abdillahi bin Abii Mulaika, kutoka kwa Bin Abbasi رضى الله عنهما, kisha naye akaitaja Hadithi hiyo. Na Isnadi - njia hii ni sahihi. Hadi kwa bin Abbas رضى الله عنهما mbobezi wa Umma katika elimu na

¹ *Fat’h Al-Bari* 3:258, *Muslim* 4:2240.

mfasiri wa Qur'an. Kadhalika hii pia ni kauli iliyokubaliwa na Masahaba wengi na Taabiina wote.

Ilinukuliwa pia, katika Hadithi *Marfu'* na *Mawquf* zilizo *Sahih* na *Hasan* na nyingine zilizo na uthibitisho na dalili dhahiri kwamba moshi ni miongoni mwa alama zinazongojewa, licha ya kwamba ndiyo maana ya dhahiri ya Aya ndani ya Qur'an. Allah تعالى Amesema:

فَأَرْتَقِبْ يَوْمَ تَأْتِي السَّمَاءُ بِدُخَانٍ مُّبِينٍ ﴿٤٤﴾

"Basi ingoje siku ambayo mbingu zitakapoleta moshi uliodhahiri."

Yaani, ulio bayana ambao kila mmoja atauona. Kwa mujibu wa tafsiri ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه, hayo ni mazingira waliyoyaona machoni mwao, kutokana na ukali wa kiu na taabu. Na hii ndiyo Kauli ya Allah تعالى:

يَغْشَى النَّاسَ ط

"Utakaowafunika watu..." Maana yake, utawafunika na kuwaenea. Lakini kama ingelikuwa ni jambo la ndoto tu lililowatokea washirikina wa Makkah, isingelisemwa, ***"Utakaowafunika watu..."*** Kauli ya Allah تعالى:

هَذَا عَذَابٌ أَلِيمٌ

"...Hii ni adhabu chungu!" Waambiwa hayo, kwa ajili ya Kuwakaripia na kuwafedhehesha. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَوْمَ يُدْعَوْنَ إِلَىٰ نَارِ جَهَنَّمَ دَعَاً ﴿٤٥﴾ هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٤٦﴾

"Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu, (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha!" (52:13-14)

Au baadhi yao watawaambia hayo wenzao. Kauli ya Allah تعالى:

رَبَّنَا اكْشِفْ عَنَّا الْعَذَابَ إِنَّا مُؤْمِنُونَ ﴿٤٧﴾

"Mola wetu Mlezi! Tuondolee adhabu hii. Hakika tutaamini."

Yaani, baada ya kuona adhabu ya Allah تعالى, makafiri wataomba iondolewe mbali nao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يُوقَفُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَّا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِعَايَتِ رَبِّنَا وَنَكُونُ مِنَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿٤٧﴾

“Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini.” (6:27)

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخْرَجْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ مِنْ
 دَعْوَتِكَ وَتَتَّبِعِ الرَّسُولَ ۖ أُولَٰئِكَ تَكُونُونَ أَقْسَمْتُمْ مِنْ قَبْلُ مَا لَكُمْ مِنَ زَوَالٍ ﴿٤٨﴾

“Na waonye watu siku itapowajia adhabu, na waliodhulumu waseme: Ewe Mola wetu Mlezi! Tuakhirishe muda kidogo tuitikie wito Wako na tuwafuate Mitume. Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondolewa?” (14:44)

Hivi ndivyo Alivyosema Allah تعالی katika Aya hii,

أَنَّىٰ لَهُمُ الذِّكْرَىٰ وَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مُّبِينٌ ﴿٤٩﴾ ثُمَّ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوا مُعَلَّمٌ مَجْنُونٌ ﴿٥٠﴾

“Nini faida ya kukumbuka kwao? Na alikwishawafikia Mtume mwenye kubainisha. Na wao wakamgeuzia uso, na wakasema: Huyu amefunzwa, naye ni mwendawazimu.”

Anasema, wanataka ukumbusho gani zaidi, ilhali Tumewapelekea Mtume aliyebainisha Ujumbe na maonyo. Pamoja na haya, walimpa mgongo, wala hawakukubaliana naye, bali walimkanusha, na wakasema: “Huyu amefunzwa, naye ni mwendawazimu.” Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ وَأَنَّىٰ لَهُ الذِّكْرَىٰ ﴿٥١﴾

“...siku hiyo mtu atakumbuka! Lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?” (89:23)

Pia, ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ فَرَعُوا فَلَا قَوَّةَ وَأَخَذُوا مِنْ مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٥٢﴾ وَقَالُوا ءَأَمْنَا بِهِمْ وَأَنَّىٰ لَهُمُ
 التَّنَاوُسُ مِنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٥٣﴾

“Na lau ungeliona watapobabaika, basi hapana pa kukimbilia! Na watakamatwa mahala pa karibu. Na watasema: Tunaiamini! Lakini wataipata wapi kutoka huko mahala mbali?” (34:51-52)

Mpaka mwishoni mwa Sura. Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّا كَاشِفُو الْعَذَابِ قَلِيلًا إِنَّكُمْ عَائِدُونَ ﴿٥٢﴾

“Hakika sisi Tutaiondoa adhabu kidogo, lakini nyinyi kwa yakini mtarejea vile vile!”

Maana yake, kama Sisi Tungewaondolea adhabu na Kukurejesheni duniani, mngelayarejelea yale mliyokuwa nayo, miongoni mwa kufuru na kukanusha. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَلَوْ رَجَعْنَاهُمْ وَكَشَفْنَا مَا بِهِمْ مِنْ ضُرٍّ لَلْجُودِ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٥﴾

“Na lau Tungeliwarehemu na Tukawaondolea shida waliyo nayo bila ya shaka wangeliendelea katika upotofu wao vile vile, wakitangatanga.” (23:75)

وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوْا لِمَا نُهُوْا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُوْنَ ﴿٢٨﴾

“Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangeyarejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo.” (6:28)

Tafsiri ya “Batwshah” (Kisasi) Kubwa

Allah تعالى Anasema:

يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرَىٰ إِنَّا مُنْتَقِمُونَ ﴿١١﴾

“Siku Tutayoyashambulia Batwshah kubwa, bila ya shaka Sisi ni wenye kutesa.”

Ibn Mas‘ud رضي الله عنه aliitafsiri hii kumaanisha siku ya Badr.¹ Hii ilikuwa pia rai ya maulamaa walioafikiana na Ibn Mas‘ud رضي الله عنه kuhusu maana ya moshi,

¹ At-Tabari 22:22.

kama ilivyoielezwa hapo juu. Pia ilisimuliwa na Ibn 'Abbas رضي الله عنهما katika mapokezi ya Al-'Awfi¹ na kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه.² Hii yawezekana dhahiri kwamba inakusudia katika Siku ya Kiyama, ingawa siku ya Badr ilikuwa pia siku ya kisasi. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema alieleza kuwa 'Ikrimah alisema: Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa habari kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alieleza: "Al-Batwshah Al-Kubrah (Kisasi kikubwa) ni siku ya Badr." Mimi nasema ni Siku ya Kiyama. Hii ndio isnadi sahihi, na ndio rai ya Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى na 'Ikrimah رحمه الله تعالى katika masimulizi yaliyo sahihi zaidi kati ya mawili, *Allah A'alam*.



¹ At-Tabari 22:22.

² At-Tabari 22:23.

* وَلَقَدْ فَتَنَّا قَبْلَهُمْ قَوْمَ فِرْعَوْنَ وَجَاءَهُمْ رَسُولٌ كَرِيمٌ
 أَنْ أَدْوَأَ إِلَىٰ عِبَادِ اللَّهِ إِنِّي لَكَرُمٌ رَسُولٌ أَمِينٌ
 وَأَنْ لَا تَعْلُوا عَلَى اللَّهِ إِنِّي ءَاتِيكُمْ بِسُلْطَنِ مُبِينٍ
 وَإِنِّي عَذْتُ بربِّي وَرَبِّكُمْ أَنْ تَرْجُمُونِ ۚ وَإِنْ لَمْ
 تُؤْمِنُوا لِي فَاعْتَرِلُونِ ۚ فَدَعَا رَبَّهُ أَنْ هتُوْلَاءِ قَوْمٌ
 مُّجْرِمُونَ ۚ فَأَسْرَبِ عِبَادِي لَيْلًا إِنَّكُمْ مُّتَّبِعُونَ ۚ
 وَأَتْرِكِ الْبَحْرَ رَهْوًا ۚ إِنَّهُمْ جُنْدٌ مُّغْرَقُونَ ۚ كَذَرَكُوا
 مِنْ جَنَّتِ وَعُيُونٍ ۚ وَزُرُوعٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ۚ
 وَنَعْمَةً كَانُوا فِيهَا فَكَيْهِنَ ۚ كَذَلِكَ ۚ وَأَوْرَثْنَاهَا قَوْمًا
 ءآخِرِينَ ۚ فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ وَمَا
 كَانُوا مُنظَرِينَ ۚ وَلَقَدْ حَجَّيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنْ
 الْعَذَابِ الْمُهِينِ ۚ مِنْ فِرْعَوْنَ ۚ إِنَّهُ كَانَ عَلِيًّا مِّنَ
 الْمُسْرِفِينَ ۚ وَلَقَدْ أَخْتَرْنَاهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ عَلَى الْعَالَمِينَ
 ۚ وَءَاتَيْنَاهُمْ مِّنَ الْآيَاتِ مَا فِيهِ بَلْتُوْا مُبِينٌ ۚ
 إِنَّ هتُوْلَاءِ لَيَقُولُونَ ۚ إِنَّ هِيَ إِلَّا مَوْتُنَا الْأُوْلَىٰ وَمَا
 نَحْنُ بِمُنشَرِينَ ۚ فَآتُوا بِقَابِلٍ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ
 ۚ أَهْمُ خَيْرٌ أَمْ قَوْمُ تُبَعِّ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ أَهْلَكْنَاهُمْ
 ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا مُّجْرِمِينَ ۚ

* وَلَقَدْ فَتَنَّا قَبْلَهُمْ قَوْمَ فِرْعَوْنَ
 وَجَاءَهُمْ رَسُولٌ كَرِيمٌ ۚ أَنْ
 أَدْوَأَ إِلَىٰ عِبَادِ اللَّهِ إِنِّي لَكَرُمٌ رَسُولٌ
 أَمِينٌ ۚ وَأَنْ لَا تَعْلُوا عَلَى اللَّهِ
 إِنِّي ءَاتِيكُمْ بِسُلْطَنِ مُبِينٍ ۚ وَإِنِّي
 عَذْتُ بربِّي وَرَبِّكُمْ أَنْ تَرْجُمُونِ ۚ
 وَإِنْ لَمْ تُؤْمِنُوا لِي فَاعْتَرِلُونِ ۚ
 فَدَعَا رَبَّهُ أَنْ هتُوْلَاءِ قَوْمٌ
 مُّجْرِمُونَ ۚ فَأَسْرَبِ عِبَادِي لَيْلًا إِنَّكُمْ
 مُّتَّبِعُونَ ۚ وَأَتْرِكِ الْبَحْرَ رَهْوًا ۚ
 إِنَّهُمْ جُنْدٌ مُّغْرَقُونَ ۚ كَذَرَكُوا
 مِنْ جَنَّتِ وَعُيُونٍ ۚ وَزُرُوعٍ
 وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ۚ وَنَعْمَةً كَانُوا فِيهَا
 فَكَيْهِنَ ۚ كَذَلِكَ ۚ وَأَوْرَثْنَاهَا
 قَوْمًا ءآخِرِينَ ۚ فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ
 السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ وَمَا كَانُوا مُنظَرِينَ
 ۚ وَلَقَدْ حَجَّيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنْ
 الْعَذَابِ الْمُهِينِ ۚ مِنْ فِرْعَوْنَ ۚ إِنَّهُ
 كَانَ عَلِيًّا مِّنَ الْمُسْرِفِينَ ۚ وَلَقَدْ
 أَخْتَرْنَاهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ عَلَى
 الْعَالَمِينَ ۚ وَءَاتَيْنَاهُمْ مِّنَ الْآيَاتِ
 مَا فِيهِ بَلْتُوْا مُبِينٌ ۚ

17. *"Na hakika kabla ya hawa Tuliwafanyia mtihani watu wa Firauni, na aliwafikia Mtume Mtukufu."*
18. *"Akasema: Nipeni waja wa Mwenyezi Mungu; kwa hakika mimi kwenu ni Mtume Muaminifu."*
19. *"Na msimfanyie kiburi Mwenyezi Mungu; hakika mimi nitakuleteeni dalili zilizo wazi."*
20. *"Nami najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Ndiye Mola Wenu Mlezi pia, ili msinipige mawe."*
21. *"Na ikiwa hamniamini, basi jitengeni nami."*
22. *"Ndipo akamuomba Mola Wake Mlezi: Hakika watu hawa ni waovu."*
23. *"Mwenyezi Mungu Akasema: Basi nenda na waja Wangu usiku. Kwa yakini mtafuatwa."*
24. *"Na iache bahari vivyo hivyo imeachana, hakika wao hao ni jeshi litakalozamishwa."*
25. *"Bustani ngapi, na chemchem ngapi waliziacha!"*
26. *"Na mimea na vyeo vitukufu!"*
27. *"Na neema walizokuwa wakijistareheshea!"*
28. *"Ndio hivyo! Na Tukawarithisha haya watu wenginewe."*
29. *"La mbingu wala ardhi hazikuwalilia, wala hawakupewa muhula."*
30. *"Na bila ya shaka Tuliwaokoa Wana wa Israeli katika adhabu ya kuwadhalilisha."*
31. *"Ya Firaun. Hakika yeye alikuwa jeuri katika wenye kupindukia mipaka."*
32. *"Na tukawachagua kwa Ujuzi Wetu kuliko walimwengu wenginewe."*
33. *"Na Tukawapa katika ishara zenye majaribio yaliyo wazi."*

Kisa cha Nabii Musa عليه السلام na Firauni, na Vipi Wana wa Israel Walivyookolewa

Allah تعالى Amesema: Kabla ya washirikina hawa, Tulikwishaijaribu kaumu ya Firauni, ambao ni Waqibti wa Misri,

وَجَاءَهُمْ رَسُولٌ كَرِيمٌ

“...na aliwafikia Mtume Mtukufu.”

Yaani, Nabii Musa عليه السلام ambaye alizungumza na Allah تعالى.

أَنْ أَدُورًا إِلَيَّ عِبَادَ اللَّهِ

“Nipeni waja wa Mwenyezi Mungu..” Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَأَرْسَلْنَا مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَا نُعَذِّبُهُمْ قَدْ جَعَلْنَاكَ بِرَأْيِكَ مِنَ رَحْمَتِ اللَّهِ وَأَلْسَلْنَا عَلَىٰ مَنْ اتَّبَعَ أَهْدَىٰ

“Basi waache Wana wa Israeli watoke nasi, wala usiwaadhibu. Sisi Tumekuletea ishara itokayo kwa Mola Wako Mlezi. Na amani itakuwa juu ya aliyefuata uwongofu.” (20:47)

إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ

“...kwa hakika mimi kwenu ni Mtume Muaminifu.”

Yaani, ni mwenye kuaminiwa kwa yale ninayokufikishieni. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَنْ لَا تَعْلُوا عَلَى اللَّهِ

“Na msimfanyie kiburi Mwenyezi Mungu...” Yaani, msilete kiburi katika kufuata Aya Zake na kuzikubali hoja Zake na kuamini ushahidi Wake.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.” (40:60)

إِنِّي آتِيكُمْ بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ

“...hakika mimi nitakuleteeni uthibitisho ulio wazi.”

Maana yake, kwa ushahidi ulio wazi, nazo ni Aya na dalili zenye nguvu,

وَأِنِّي عُذْتُ بِرَبِّي وَرَبِّكُمْ أَن تَرْجُمُونِ ﴿١٧﴾

“Nami najikinga kwa Mola Wangu Mlezi na Ndiye Mola Wenu Mlezi pia, ili msinipige mawe.”

Ibn ‘Abbas na Abu Swalih رضي الله عنهما walisema: “Hayo ni mashambulizi ya ulimi, yaani matusi.”¹

Qatadah alisema, “Kurujumiwa kwa mawe.” Yaani, ‘Najikinga kwa Allah تعالى, Aliyeniumba mimi na nyinyi, dhidi ya kunifikia madhara ya maneno na vitendo vyenu vibaya.”²

وَإِن لَّمْ تُوْمِنُوا لِي فَاَعْتَرِلُونِ ﴿١٨﴾

“Na ikiwa hamniamini, basi jitengeni nami.”

Yaani, msinipinge, na jambo hili mliache baina yangu na nyinyi, kwa amani, hadi Allah تعالى Atakapohukumu kati yetu. Baada ya Nabii Musa عليه السلام kuwa nao kwa kipindi kirefu na kusimamisha hoja za Allah تعالى kwao katika yote hayo, hayakuwazidishia isipokuwa ukafiri na ukaidi. Akamuomba Mola Wake dhidi yao na akajibiwa. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَقَالَ مُوسَىٰ رَبَّنَا إِنَّكَ آتَيْتَ فِرْعَوْنَ وَمَلَأَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا رَبَّنَا

لِيُضِلُّوهُ عَنِ سَبِيلِكَ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلَيَّ أَمْوَالِهِمْ وَاشْدُدْ عَلَيَّ قُلُوبَهُمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ

يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١٩﴾ قَالَ قَدْ أُجِيبَت دَعْوَتُكُمْ مَا فَاسْتَقِيمَا وَلَا تَتَّبِعَانَّ سَبِيلَ

الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٠﴾

“Na Musa akasema: Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe Umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia. Hivyo wanapoteza watu na njia Yako. Mola Wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu. Mwenyezi Mungu Akasema: Maombi yenu yamekubaliwa. Basi simameni sawa sawa, wala msifuate njia za wale wasio jua.” (10:88-89)

¹ At-Tabari 22:26.

² At-Tabari 22:27.

Sawa na hivyo, Allah تعالی Anasema katika Aya hii,

فَدَعَا رَبَّهُ أَنْ هَتُوْا لَآءِ قَوْمٍ مُّجْرِمُوْنَ ﴿١٧﴾

“Ndipo Akamuomba Mola Wake Mlezi: Hakika watu hawa ni wakosefu.”

Wakati huo, Allah تعالی Alimuamuru aondoke pamoja na Wana wa Israel kutoka katika maeneo yao, bila ya amri wala idhini ya Firauni na washauri wake. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema:

فَأَسْرِ بِعِبَادِي لَيْلًا إِنَّكُمْ مُّتَّبِعُونَ ﴿١٨﴾

“Basi nenda na waja Wangu usiku. Kwa yakini mtafuatwa.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَلَقَدْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِي فَاصْرَبْ لَهُمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَفُ
دَرْكًا وَلَا تَخَفْ ﴿١٩﴾

“Na Tulimfunulia Musa: Toka usiku na waja Wangu, na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa, wala usiogope.” (20:77)

Kauli ya Allah تعالی katika Aya hii:

وَأَتْرَكَ الْبَحْرَ رَهْوًا ۗ إِنَّهُمْ جُنْدٌ مُّغْرَقُونَ ﴿٢٠﴾

“Na iache bahari vivyo hivyo imeachana, hakika wao hao ni jeshi litakalozamishwa.”

Hilo ni kuwa, baada ya Musa عليه السلام na Wana wa Israel kuvuka bahari, Musa عليه السلام alitaka kuipiga kwa fimbo yake ili irejee katika hali iliyokuwa hapo kabla ili iwe kizuizi baina yao na Firauni, apate kushindwa kuwafikia. Allah تعالی Akamuamuru aiache ikiwa tulivu katika hali yake hiyo. Na Akampa bishara kwamba hao, “ni jeshi litakalozamishwa ndani yake.” Na kwamba asihofu kukutwa na Firauni wala asiogope.

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما Alisema, Allah تعالی Alisema:

وَأَتْرَكَ الْبَحْرَ رَهْوًا ۗ

“Na iache bahari vivyo hivyo imeachana...”

Maana yake, iache kama ilivyo na uendeleo.¹ Mujahid alisema:

رَهَوًا ط

“...imeachana...” Maana yake, njia kavu, kama ilivyo. ‘Usiilamuru kurejea; iache mpaka wa mwisho wao awe ameiingia.² Kama hivi alisema ‘Ikrimah, Ar-Rabi’ bin Anas, Adh-Dhahhak, Qatadah, Ibn Zayd, Ka’b Al-Ahbar, Simaak bin Harb na wengine.³ Halafu, Allah تعالى Alisema:

كَمْ تَرَكُوا مِنْ جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٤٤﴾ وَزُرُوعٍ

“Bustani ngapi, na chemchem waliziacha. Na mimea...”

Inakusudia mito na visima,

وَمَقَامٍ كَرِيمٍ

“...na vyeo vitukufu!”

Ambapo ni mahali pasafi na mahali pazuri. Qatadah na Sa’id bin Jubayr walisema:

وَمَقَامٍ كَرِيمٍ

“...na vyeo vitukufu!” Maana yake, ni mimbari nyingi.⁴

وَنَعْمَةً كَانُوا فِيهَا فَنكِهِينَ ﴿٤٥﴾

“Na neema walizokuwa wakijistareheshea!”

Yaani, maisha waliyokuwa wakiyafurahia, wakawa wanakula chakula walichokitaka, wakavaa mavazi waliyoyapenda, pamoja na mali kadha wa kadha, jaha na ukuu katika ardhi. Yote hayo yakachukuliwa katika asubuhi moja tu, wakaiacha dunia, wakaenda Jahanamu, ambapo ni mwisho mbaya kabisa.

كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا قَوْمًا آخَرِينَ ط

“Ndio hivyo! Na Tukawarithisha haya watu wenginewe.”

Nao ni Wana wa Israel. Kauli ya Allah تعالى:

¹ Ad-Dur Al-Manthur 7:410.

² At-Tabari 22:30.

³ At-Tabari 22:30.

⁴ At-Tabari 22:32.

فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ

“La mbingu wala ardhi hazikuwalilia...”

Yaani, hawakuwa na amali njema zilizopanda milango ya mbinguni ili ziweze kulia kwa kukosekana kwao, wala hapana sehemu ya ardhini walikofanya ibada, nayo ikawakosa. Kwa ajili hii, wamestahiki kutokutazamwa, wala kuakhirishwa, kwa sababu ya kufuru, uovu, ufidhuli na ukaidi wao. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Sa'id bin Jubayr alisema, “Mtu mmoja alikuja kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما na akasema, ‘Ewe Ibn 'Abbas! Unaonaje Kauli ya Allah تعالى,

فَمَا بَكَتْ عَلَيْهِمُ السَّمَاءُ وَالْأَرْضُ وَمَا كَانُوا مُنظَرِينَ ﴿٤٤﴾

“La mbingu wala ardhi hazikuwalilia, wala hawakupewa muhula.”

‘Je, mbingu na ardhi humlilia mtu?’ Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema,: ‘Naam, kila kiumbe ana mlango mbinguni, humo hushuka riziki yake na humo hupanda amali yake. Pindi Muumini anapofariki, basi lango hilo hufungwa, basi kwa kumkosa kwake humlilia, na mahali pa kusalia duniani ambapo alikuwa akisali na kumd hukuru Allah تعالى na humo basi humlilia. Kwa hakika kaumu ya Firauni haikuwa na athari njema duniani, na hawakuwa na amali njema zilizopanda kwa Allah تعالى, kwa hivyo, mbingu na ardhi hazikuwalilia.’”¹ Al-'Awfi alisimulia maelezo kama haya kutoka kwa Ibnu 'Abbas رضي الله عنهما.²

وَلَقَدْ حَجَّيْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مِنَ الْعَذَابِ الْمُهِينِ ﴿٤٥﴾ مِنْ فِرْعَوْنَ إِنَّهُ كَانَ عَلِيًّا مِّنَ الْمُسْرِفِينَ ﴿٤٦﴾

“Na bila ya shaka Tuliwaokoa Wana wa Israeli katika adhabu ya kuwadhalilisha. Ya Firauni. Hakika yeye alikuwa jeuri katika wenye kupindukia mipaka.”

Allah تعالى Anawakumbusha namna Alivyowaokoa kutoka katika waliyokuwamo, miongoni mwa ukandamizaji wa Firauni na udhalilishaji wake kwao kwa kushurutishwa kufanya kazi ngumu zenye kudhalilisha,

¹ At-Tabari 22:34.

² At-Tabari 22:35.

مِن فِرْعَوْنَ إِنَّهُ كَانَ عَلِيًّا

“Ya Firauni. Hakika yeye alikuwa jeuri...” Yaani, mwenye kiburi, mkorofi na mkaidi. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْأَرْضِ

“Hakika Firauni alitakabari katika nchi...” (28:4)

فَأَسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا عَالِينَ

“Lakini walijivuna, nao walikuwa watu majeuri.” (23:46)

Katika wafujaji, yaani mwenye kufanya israfu katika mambo yake, mwenye rai ya kipumbavu nafsini mwake.

وَلَقَدْ آخَرْتَهُمْ عَلَىٰ عِلْمٍ عَلَىٰ الْأَعْيُنِ ﴿١٧﴾

“Na Tuliwakhiri kwa ujuzi wetu kuliko walimwengu wenginewe.”

Mujahid alisema, “Waliteuliwa kuwa juu ya wengine wanaoishi nao.” Qatadah amesema, “Waliteuliwa juu ya watu wa zama zao hizo.” Na ilikuwa ikisemwa kuwa kwa kila zama kuna mwanachuoni. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قَالَ يَمُوسَىٰ إِنِّي أُصْطَفَيْتُكَ عَلَىٰ النَّاسِ

“Mwenyezi Mungu Akasema: Ewe Musa! Mimi Nimekuteuwa wende kwa watu...” (7:144)

Yaani, watu wa zama zake hizo. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَأُصْطَفَيْنِكَ عَلَىٰ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ﴿١١﴾

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amekuteuwa, na Akakutakasa, na Akakutukuza kuliko wanawake wote.” (3:42)

Yaani, Bibi Maryam رضي الله عنها aliteuliwa katika zama zake. Kwani mama Khadijah رضي الله عنها, ama anaweza kuwa bora zaidi yake au kulingana naye kwa fadhila. Kadhalika Bibi Asiyah bint Muzaahim رضي الله عنها, mke wa Firauni, na ubora wa mama Aishah رضي الله عنها juu ya wanawake wengine ni kama ubora wa Thariyd (mkate wa maziwa) kwa vyakula vingine.

وَأَتَيْنَهُم مِّنَ الْأَيْتِ

“Na Tukawapa katika ishara...” Yaani, ushahidi, dalili na miujiza isiyo ya kawaida,

مَا فِيهِ بَلَلُوا مُبِينٌ

“...zenye majaribio yaliyo wazi.” Maana yake, jaribio dhahiri kwa ajili ya watakaongozwa nalo.

إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَيَقُولُونَ ﴿١٧﴾ إِنَّ هِيَ إِلَّا مَوْتَتُنَا الْأُولَىٰ وَمَا نَحْنُ بِمُنشَرِينَ ﴿١٨﴾ فَاتُّوا بِعَابِئِنَّا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٩﴾ أَهُمْ خَيْرٌ أَمْ قَوْمُ تَبَعِ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ أَهْلَكْنَاهُمْ إِنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿٢٠﴾

34. **“Hakika hawa wanasema:**

35. **“Hapana ila kufa kwetu mara ya kwanza tu, wala sisi hatufufuliwi.”**

36. **“Basi warudisheni baba zetu, ikiwa nyinyi mnasema kweli.”**

37. **“Je! wao ni bora au watu wa Tubbaa’ na waliokuwa kabla yao? Tuliwaangamiza. Hakika hao walikuwa wakosefu.”**

Majibu kwa Wanaopinga Kiyama

Allah تعالیٰ Anaeleza habari za washirikina kuhusu kukanusha kwao jambo la kufufuliwa na marejeo, na kwamba hakuna kingine zaidi, isipokuwa maisha haya ya dunia, wala hakutakuwa na uhai tena baada ya umauti, wala kufufuliwa. Na hoja yao ni kuwa baba zao waliotangulia waliondoka bila ya kurejea, basi ikiwa kufufuliwa ni jambo la kweli,

فَاتُّوا بِعَابِئِنَّا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٢٠﴾

“Basi warudisheni baba zetu, ikiwa nyinyi mnasema kweli.”

Hoja hii ni batili na ina utatanishi mbaya, kwani marejeo ni Siku ya Kiyama, si duniani, bali ni baada ya dunia kuondoka kwake na kumalizika, Allah Atawarejesha upya viumbe, na kuwafanya madhalimu kuni za moto wa Jahanamu. Siku ambayo mtakuwa mashahidi juu ya watu, na Mtume anakuwa

shahidi juu yenu. Halafu, Allah تعالی Alizungumza kwa Kuwaogopesha, Kuwakemea na Kuwaonya kuhusu adhabu Yake isiyozuilika. Kama yaliyowasibu mfano wao miongoni mwa washirikina waliopinga kufufuliwa, kama vile kaumu ya *Tubba'*, ambao ni Sabai (Sheba), ambao Allah تعالی Aliwahiliki, Akaiharibu nchi yao na Akawafukuza katika miji na Akawatenganisha makundi makundi. Kama ilivyokwishatangulia, katika *Surat Sabai*.¹ Chanzo ni washirikina kukataa marejeo. Katika Aya hii, Allah تعالی Amewashabihisha nao. Hao *Tubba'* walikuwa ni Waarabu waliotokana na Qahtwaan, kama walivyo hawa (Makuraishi) ni Waarabu waliotokana na 'Adnaan. Miongoni mwa wa-Himyar, ambao ndio Wasabai, waliwaita wafalme wao *Tubba'i*, kama lilivyo jina la Kisra, kwa wafalme wa Uajemi, Kaisari, kwa wafalme wa Roma; Firauni, kwa watawala wa kikafiri wa Misri; An-Najjashi, kwa watawala wa Al-Habashah (Ethiopia) na himaya nyingine za watawala.

Lakini imeafikiwa kuwa mmojawapo wa wafalme-*Tubbai'* aliondoka Yemen kupita miji mbalimbali mpaka akafika Samarqand Himaya yake ikawa kubwa na yenye nguvu pamoja na jeshi lake. Mamlaka yake yakapanuka na raia wake wakaongezeka. Yeye ndiye aliyeasisi Al-Hiyrah. Imefikiwa kwamba alipita Madinah katika zama za ujahili. Akataka kupigana na wakazi wake, lakini wakamzuia. Wakawa wanapigana naye mchana, usiku wanampatia chakula. Akaona haya akaacha kupigana nao. Alikuwa akiambatana na wanachuoni wawili wa kiyahudi waliomshauri na kumuambia asingeweza kupata ushindi katika mji huu, kwani utahamiwa na Mtume wa zama za mwisho, Kwa hivyo, akarejea na kuwachukua Wayahudi hao wawili kuelekea Yemen.

Alipopita Makkah, akataka kuivunja Al-Ka'bah, wakamkataza hilo pia, wakamueleza utukufu wa Nyumba hii, na kuwa alijenga Nabii Ibrahim, *Al-Khalil* عليه السلام, na kuwa kutakuwa na jambo kubwa, kwa Mtume huyo atakayetumwa mwisho wa zama. Akaiheshimu, akatufu, kisha akaifunika shuka za *Mulaa-a*, *Wasaa-il* na *Hibar*. Akarejea Yemen, akawa anawalingania wakazi wake kufuata dini ya Kiyahudi pamoja naye. Kwa wakati huo, dini ya Nabii Musa عليه السلام, ndio iliokuwa ya watu waliokuwa katika uongofu, kabla ya kutumwa Masih. Kwa hivyo, watu wengi wa Yemen wakaingia dini ya kiyahudi pamoja naye.

¹ Angalia Tafsiri ya *Surat Sabai* (34:15-19).

'Abdur-Razzaq amepokea toka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«مَا أَدْرِي تَبِعَ نَبِيًّا كَانَ، أَمْ غَيْرَ نَبِيٍّ»

*"Sijui kama Tubba' alikuwa ni Nabii au hakuwa Nabii."*¹

Ilisimuliwa pia, kuwa Tamim bin 'Abdur-Rahman alisema: "'Ata bin-Rabaah alisema, 'Msimtukane Tubba', kwani Mtume ﷺ alikataza kumtukana.'"² *Allahu Aalam.*

* * *

¹ Al-Baghawi 4:154, ina udhaifu katika namna ya usimulizi na mpangilio wa maneno. Hata hivyo, kuna riwaya nyingi sahihi zenye kuunga mkono maana yake ya kiumjama. Angalia As-Sahihah 5:251.

²'Abdur-Razzaq 3:209.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لِعِبَادٍ ﴿٣٨﴾
 مَا خَلَقْنَاهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾
 إِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ مِيقَتُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٠﴾ يَوْمَ لَا يُغْنِي
 مَوْلَىٰ عَن مَّوْلَىٰ شَيْئًا وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤١﴾ إِلَّا مَن
 رَّحِمَ اللَّهُ ۗ إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٤٢﴾ إِنَّ شَجَرَتَ
 الزُّقُومِ ﴿٤٣﴾ طَعَامُ الْأَيْمِ ﴿٤٤﴾ كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ
 ﴿٤٥﴾ كغَلِي الْحَمِيمِ ﴿٤٦﴾ خَذُوهُ فَأَعْيَلُوهُ إِلَىٰ سَوَاءِ
 الْجَحِيمِ ﴿٤٧﴾ ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِن عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٤٨﴾
 ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٤٩﴾ إِنَّ هَذَا مَا
 كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٥٠﴾ إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي مَقَامٍ أَمِينٍ ﴿٥١﴾
 فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٢﴾ يَلْبَسُونَ مِن سُندُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ
 مُتَقَابِلِينَ ﴿٥٣﴾ كَذَلِكَ وَزَوَّجْنَاهُم بِحُورٍ عِينٍ ﴿٥٤﴾
 يَدْعُونَ فِيهَا بِكُلِّ فَاكِهَةٍ ءَامِنِينَ ﴿٥٥﴾ لَا يَدْخُلُونَ
 فِيهَا الْمَوْتَ إِلَّا الْمَوْتَةَ الْأُولَىٰ ۗ وَوَقَّعْنَا لَهُمُ عَذَابَ الْجَحِيمِ
 ﴿٥٦﴾ فَضَلًّا مِّن رَّبِّكَ ۗ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٥٧﴾
 فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٨﴾ فَأَرْتَقِبْ
 إِنَّهُمْ مُّرْتَقِبُونَ ﴿٥٩﴾

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا
 بَيْنَهُمَا لِعِبَادٍ ﴿٣٨﴾ مَا خَلَقْنَاهُمَا
 إِلَّا بِالْحَقِّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا
 يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾ إِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ
 مِيقَتُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٠﴾ يَوْمَ لَا
 يُغْنِي مَوْلَىٰ عَن مَّوْلَىٰ شَيْئًا وَلَا هُمْ
 يُنصَرُونَ ﴿٤١﴾ إِلَّا مَن رَّحِمَ اللَّهُ ۗ
 إِنَّهُ هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ ﴿٤٢﴾

38. "Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo."

39. "Hatukuviumba hivyo ila kwa Haki, lakini wengi wao hawajui."

40. "Hakika siku ya Upambanuzi ni wakati uliowekwa kwa wao wote."

41. "Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki yake kwa

chochote, wala hawatanusuriwa."

42. "Isipokuwa atakayepata Rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu."

Dunia Imeumbwa kwa Hekima

Allah تعالى Anatueleza kuhusu Uadilifu Wake, na kwamba Amejitenga mbali na mchezo, upuuzi na batili. Ni sawa na Kauli Yake nyingine:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطِيلاً ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۖ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا
مِنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾

“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya waliokufuru. Ole wao waliokufuru kwa Moto utaowapata.” (38:27)

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿٤٨﴾ فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۚ
لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿٤٩﴾

“Je! Mlidhani ya kwamba Tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.” (23:115-116)

Kisha, Allah تعالى Akasema:

إِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ مِيقَتُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٠﴾

“Hakika siku ya Uamuzi ni wakati uliowekwa kwa wao wote.”

Hiyo ni Siku ya Kiyama ambapo Allah Atawahukumu viumbe Wake, na Atawaadhibu makafiri na Kuwapa jaza Waumini.

مِيقَتُهُمْ أَجْمَعِينَ

“...ni wakati uliowekwa kwa wao wote.” Yaani, Atawakusanya wote, wa kwanza na wa mwisho wao,

يَوْمَ لَا يُغْنِي مَوْلَىٰ عَنْ مَوْلَىٰ شَيْئًا

“Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki yake kwa chochote.”

Inamaanisha, jamaa hatomsaidia mwenzake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿٣٨﴾

“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.” (23:101)

وَلَا يَسْتَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿٣٩﴾ يُبْصَرُونَ ﴿٤٠﴾

“Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake. Ijapokuwa wataoneshwa waonane.” (70:10-11)

Maana yake, ndugu hatamuuliza hali yake, ilhali anamuona kwa macho yake. Allah تعالى Anasema:

وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ

“...wala hawatanusuriwa.” Jamaa hatamnusuru jamaa yake, wala hakuna msaada kutoka nje utakaomsaidia. Kisha, Allah تعالى Akasema:

إِلَّا مَنْ رَحِمَ اللَّهُ

“Isipokuwa atakayepata Rehema ya Mwenyezi Mungu.” Yaani, hakitanufaisha kitu chochote, isipokuwa Rehema ya Allah تعالى kwa viumbe Wake,

هُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ

“Hakika Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Kurehemu.”

Maana yake, Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwingi Mno wa Huruma.

إِنَّ شَجَرَتَ الرَّقُومِ ﴿٤١﴾ طَعَامُ الْأَثِيمِ ﴿٤٢﴾ كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ ﴿٤٣﴾ كَغَلِي الْحَمِيمِ ﴿٤٤﴾ خُدُوهُ فَأَعْتَلُوهُ إِلَىٰ سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٤٥﴾ ثُمَّ صُبُوءًا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٤٦﴾ ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٤٧﴾ إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٤٨﴾

43. **“Hakika Mti wa Zaqqum,”**

44. **“Ni chakula cha mwenye dhambi.”**

45. **“Kama shaba iliyoyayushwa, hutokota matumboni.”**

46. **“Kama kutokota kwa maji ya moto.”**

47. **“(Itasemwa:) Mkamateni na mtupeni katikati ya Jahannamu!”**

48. *“Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayochemka.”*

49. *“Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu!”*

50. *“Hakika haya ndiyo mliyokuwa mkiyatilia shaka.”*

Hali ya Washirikina na Adhabu yao Siku ya Kiyama

Allah تعالی Anaeleza adhabu Atakayowaadhibu makafiri wanaopinga kukutana Naye,

إِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّومِ ﴿٤٨﴾ طَعَامُ الْآثِمِينَ ﴿٤٩﴾

“Hakika Mti wa Zaqqum, ni chakula cha mwenye dhambi.”

Mwenye madhambi, yaani katika kauli na matendo yake, huyu ni kafiri. zaidi ya mmoja. Wamesema kuwa huyu ni Abu Jahli, wala hapana shaka yeye kuhusika katika Aya hii, lakini si makhususi kwake. Ibnu Jarir رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Abu Dardaai رضي الله عنه alikuwa akimsomea mtu mmoja:

إِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّومِ ﴿٤٨﴾ طَعَامُ الْآثِمِينَ ﴿٤٩﴾

“Hakika Mti wa Zaqqum. Ni chakula cha mwenye dhambi.”

Mtu huyo akasema, “Chakula cha yatima.” Abu Dardaai رضي الله عنه akasema, “Sema, mti wa Zaqqum ni chakula cha muovu.”¹ Yaani, hatakuwa na chakula kingine zaidi ya hicho. Mujahid amesema, “Ikiwa tone lake moja lingedondoka ardhini, lingewaharibia watu wa duniani maisha yao.”² Masimulizi kama haya yametangulia.

كَالْمُهْلِ

“Kama shaba iliyoyayushwa...”

Walisema: “Kama makapi ya mafuta.”

يَغْلَى فِي الْبُطُونِ ﴿٥٠﴾ كَغَلَى الْحَمِيمِ ﴿٥١﴾

“...hutokota matumboni. Kama kutokota kwa maji ya moto.”

Kwa sababu ya joto lake na uozo wake. Kauli ya Allah تعالی:

¹ At-Tabari 22:43.

² At-Tabari 22:43.

خُدُوهُ

“Mkamateni...” Kafiri. Imesimuliwa kuwa Allah تعالی Atakapowaambia Zabaania yaani wale (Malaika walinzi wa Jahanamu), “Mkamateni...” basi watamkimbilia Malaika elfu sabini kumkamata. Kauli ya Allah تعالی:

فَاعْتَلُوهُ

“...na mtupeni...” Yaani, mswageni kwa kumkokota mgongoni mwake. Mujahid amesema kuwa maana ya:

خُدُوهُ فَاعْتَلُوهُ

“Mkamateni na mtupeni...” Mchukueni na mumrushe,

إِلَى سَوَاءٍ الْجَحِيمِ

“...katikati ya Jahannamu!” Sehemu ya kati yake,

ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٤٤﴾

“Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayo chemka.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يُصَبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوسِهِمُ الْحَمِيمُ ﴿٢١﴾ يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴿٢٢﴾

“...na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka. Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia.” (22:19-20)

Yaani, Malaika atampiga kwa mtaimbo wa chuma utafunua ubongo wake. Kisha maji ya moto yatamiminiwa juu ya kichwa chake na kuteremka mwilini mwake, na kukatika vilivyomo tumboni mwake miongoni mwa matumbo yake, mpaka yatiririke kwenye visigino vyake. Tunamuomba Allah تعالی Atukinge nayo.

ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿١٥﴾

“Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu!”

Yaani, muambieni hivyo, kwa kumkebehi na kumfedhehesha. Adh-Dhahhak alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa, “Maana yake, hakuwa mwenye nguvu wala hakuwa mtukufu.”

إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٣٨﴾

“Hakika haya ndiyo mliyokuwa mkiyatilia shaka.”

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَوْمَ يَدْعُونَ إِلَى نَارٍ جَهَنَّمَ دَعَاً ﴿٣٩﴾ هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تَكْذِبُونَ ﴿٤٠﴾ أَفَسِحْرُهُ
هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٤١﴾

“Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu. (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha! Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu?” (52:13-15)

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema katika Aya hii,

إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٤٢﴾

“Hakika haya ndiyo mliyokuwa mkiyatilia shaka.”

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي مَقَامٍ أَمِينٍ ﴿٤٣﴾ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٤٤﴾ يَلْبَسُونَ مِنْ سُنْدُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ
مُتَقَابِلِينَ ﴿٤٥﴾ كَذَلِكَ وَرَوَّجْنَاهُمْ بِحُورٍ عِينٍ ﴿٤٦﴾ يَدْعُونَ فِيهَا بِكُلِّ فَنَكْحَةٍ
ءَامِينِينَ ﴿٤٧﴾ لَا يَدُوقُونَ فِيهَا الْمَوْتَ إِلَّا الْمَوْتَةَ الْأُولَىٰ ط وَوَقْنَاهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ
﴿٤٨﴾ فَضلاً مِّن رَّبِّكَ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٤٩﴾ فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لَعَلَّهُمْ
يَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٠﴾ فَأَرْتَقِبْ إِنَّهُمْ مُّرْتَقِبُونَ ﴿٥١﴾

51. Hakika wachamungu watakuwa katika mahali pa amani.

52. Katika bustani na chemchem.

53. Watavaa hariri nyepesi na hariri nzito wakikabiliana.

54. Hivi ndivyo itakavyokuwa, na Tutawaoza mahurilaini.

55. Humo watataka kila aina ya matunda, na wakae kwa amani.

56. Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza, na (Mwenyezi Mungu) Atawalinda na adhabu ya Jahannamu.

57. Kuwa ni Fadhila zitokazo kwa Mola Wako Mlezi. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

58. "Basi Tumeifanya nyepesi hii Qur'ani kwa ulimi wako, ili wapate kukumbuka."

59. "Ngoja tu, na wao wangoje pia."

Hali ya Wachamungu na Neema Zao Peponi

Baada ya Allah تعالى kutaja hali za waovu, Alifuatisha kwa Kuwataja wema, kwa ajili hii, Qur'an iliitwa *Al-Mathaani* (yaani, yenye kutaja vitu viwili visivyolingana). Allah تعالى Amesema:

إِنَّ الْمُتَّقِينَ

"Hakika wachamungu..." Wanaomuogopa Allah تعالى humu duniani,

فِي مَقَامٍ أَمِينٍ

"...watakuwa katika mahali pa amani." Huko Akhera, nako ni Peponi. Wamepata amani humo, dhidi ya mauti na hofu ya kutoka Peponi, na kila namna ya woga, huzuni, taabu, uchovu na dhidi ya shetani na vitimbi vyake, shida na maafa mengine,

فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٤٤﴾

"Katika bustani na chemchem." Hii ni kinyume na hali ya waovu, ambao watapewa mti wa *Zaqqum* na kinywaji kichemkacho. Kauli ya Allah تعالى:

يَلْبَسُونَ مِنْ سُندُسٍ

"Watavaa hariri nyepesi..." Hiyo ni hariri nyepesi zaidi, kama vile kanzu na mfano wake,

وَإِسْتَبْرَقٍ

"...na hariri nzito..." Maana yake, hariri ambayo hufumwa kwa nyuzi zing'azoo na huwa kama manyoya ya ndege, na huvaliwa juu ya nguo nyingine za kawaida,

مُتَقَابِلِينَ

"...wakikabiliana," Yaani, wakiwa wamekaa juu ya vitanda hapana yeyote katika wao akaaye kwa kumpa mgongo mwingine. Kauli ya Allah تعالى,

كَذَٰلِكَ وَرَوَّجْنَهُمْ يُحْوِرُ عَيْنٍ ﴿٥٦﴾

“Hivi ndivyo itakavyo kuwa, na Tutawaoza mahurilaini.”

Maana yake, hii ni zawadi, pamoja na Tuliyowatunuku miongoni mwa wake wazuri, mahurilaini, ambao,

لَمْ يَطْمِئِنَّ ۤإِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌ ﴿٥٧﴾

“...hajawagusa mtu kabla yao wala jini.” (55:56)

كَأَنَّهُنَّ ٱلْيَاقُوتُ وَٱلْمَرْجَانُ ﴿٥٨﴾

“Kama kwamba wao ni yakuti na marijani.” (55:58)

هَلْ جَزَاءُ ٱلْإِحْسَنِ إِلَّا ٱلْإِحْسَنُ ﴿٥٩﴾

“Ati yaweza kuwa malipo ya ihsani ila ihsani?” (55:60)

يَدْعُونَ فِيهَا بِكُلِّ فِكْهَةٍ ءَامِينٍ ﴿٦٠﴾

“Humo watataka kila aina ya matunda, na wakae kwa amani.”

Yaani, kila watakapohitaji aina yoyote ya matunda, wataletewa, hali ya kuwa wao wameaminika na kutokukatika wala kuzuilika kwake, bali wataletewa kila wanapoyahitaji.

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا ٱلْمَوْتَ إِلَّا ٱلْمَوْتَ ٱلْأُولَىٰ ۗ

“Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza...”

Huku ni kusesitiza ukanusho. Maana yake, humo hawataonja mauti milele. Kama ilivyoandikwa ndani ya *Sahih Mbili*, kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يُزْتَمَىٰ بِٱلْمَوْتِ فِي صُورَةِ كَنْبَسٍ أَمْلَحَ فَيُرَقَفُ بَيْنَ ٱلْجَنَّةِ وَٱلنَّارِ، ثُمَّ يُذْبَحُ، ثُمَّ يُقَالُ: يَا أَهْلَ ٱلْجَنَّةِ خُلُودٌ فَلَا مَوْتَ، وَيَا أَهْلَ ٱلنَّارِ خُلُودٌ فَلَا مَوْتَ»

“Mauti yataletwa katika sura ya kondoo mzuri na kusimamishwa kati ya Pepo na Moto. Kisha yatachinjwa. Patasemwa, ‘Enyi watu wa Peponi, ni milele, hakuna mauti, na enyi wa Motoni! Ni milele hakuna mauti.’”¹

¹ *Fat’h Al-Bari* 8:282; *Muslim* 4:2188.

Hadithi hii ilishaelezwa katika *Surat Maryam*. 'Abdur-Razzaq aliwanukuu Abu Sa'id na Abu Hurayrah رضي الله عنهما kuwa walisema: Mtume ﷺ amesema:

«يُقَالُ لِأَهْلِ الْجَنَّةِ: إِنَّ لَكُمْ أَنْ تَصِيحُوا فَلَا تَسْمَعُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَعِيشُوا فَلَا تَمُوتُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَتَّعَمُوا فَلَا تَبْأَسُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تُشَبُّوا فَلَا نَهْرَمُوا أَبَدًا»

“Watu wa Peponi wataambiwa: ‘Nyinyi mtakuwa wenye afya na hamtaugua abadani, na hakika nyinyi mtaishi, wala hamtafariki abadani, nanyi mtaneemeka, wala hamtapata tabu abadani, nanyi mtaendelea kuwa vijana, wala hamtazeeka abadani.”¹

Muslim aliandika Hadithi hii.² Abu Hurayrah رضي الله عنه alieleza kuwa, Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ اتَّقَى اللَّهَ دَخَلَ الْجَنَّةَ، يَنْعَمُ فِيهَا وَلَا يَبْأَسُ، وَيَعِيشُ فِيهَا فَلَا يَمُوتُ، لَا تَبْلَى ثِيَابُهُ، وَلَا يَفْنَى شَبَابُهُ»

“Mwenye kumcha Allah ataingia Peponi, ataneemeka humo bila kupata tabu, atakuwa hai humo, wala hatakufa, nguo zake hazitachakaa, wala ujana wake hautaisha.”²

وَوَقَدَهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ

“...Atawalinda na adhabu ya Jahannamu.”

Yaani, pamoja na neema hizi kubwa za kudumu, Allah تعالى Amewalinda, Kawapa salama, Amewanusuru na Amewaepusha adhabu iumizayo katika vina vya Jahanamu, kwa hivyo watakuwa wamepata matilaba yao, na Amewaepusha mbali na walivyovihofu. Kwa ajili hii, Allah تعالى Amesema:

فَضْلًا مِّن رَّبِّكَ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٥٧﴾

“Kuwa ni Fadhila zitokazo kwa Mola Wako Mlezi. Huko ndiko kufuzu kukubwa.”

Yaani, haya yametokana na Fadhila Zake na Ihsani Yake kwao. Ni sawa na ilivyothibiti katika *Sahih Mbili*, kwamba Mtume ﷺ amesema:

¹Muslim 4:2182.

²At-Tabari katika *Al-Awsat* 4895.

«اغْمَلُوا وَسَدُّوا وَقَارِبُوا، وَاعْلَمُوا أَنَّ أَحَدًا لَنْ يُدْخِلَهُ عَمَلُهُ الْجَنَّةَ»

“Tendeni na mfanye bidii na mtambue kwamba hapana yeyote ambaye matendo yake pekee yatamuingiza Peponi.”

Wakauliza, “Hata wewe ewe Mjumbe wa Allah?” Mtume ﷺ akawajibu:

«وَلَا أَنَا، إِلَّا أَنْ يَتَّعَمَدَنِي اللَّهُ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَفَضْلٍ»

“Hata mimi, isipokuwa Allah Akinifunika kwa Rehema na Fadhila kutoka Kwake.”¹

فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ بِلِسَانِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٥٧﴾

“Basi Tumeifanya nyepesi Qur’ani hii kwa ulimi wako, ili wapate kukumbuka.”

Maana yake, kwa hakika, Tumeirahisisha Qur’an hii Tuliyoiteremsha kuwa sahali, wazi, bainifu, na dhahiri katika lugha yako ambayo ndiyo fasaha zaidi, iko waziwazi na nzuri zaidi ya lugha nyingine,

لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ

“...ili wapate kukumbuka.”

Yaani, watajifahamisha na kujua. Kisha, pamoja na kuwa kwake wazi na ubainifu huu, kuna watu wanaokufuru, wanaokhalifu na wanaokaidi. Allah تعالی Akamuambia Mjumbe Wake Akimfariji na Kumuahidi ushindi, ilhali Akiwaonya wanaomkanusha kwa lawama na maangamivu:

فَأَرْتَقِبْ إِنَّهُمْ مُرْتَقِبُونَ

“Ngoja tu, na wao wangoje pia.”

Yaani, hivi karibuni, watajua ni nani atakayepata ushindi na watakaokuwa na neno la juu duniani na Akhera. Ushindi ni wako, ewe Muhammad na nduguzo, miongoni mwa Manabii na Wajumbe, na Waumini watakaokufuata. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

¹ Fat’h Al-Bari 11:33, Muslim 4:2170.

كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَيْنَا أَنَا وَرُسُلِي ۗ

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda.” (58:21)

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ۖ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٥٢﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi. Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa.” (40:51-52)

Mwisho wa tafsiri ya *Suratu Ad-Dukhan*. Kuhimidiwa na Shukurani ni kwa Allah تعالیٰ, na Kwake Ndiko Kwenye Tawfiki na Hifadhi.

* * *